# DA'WAT-UL-AMIR

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.**

Kurasa zifuatazo zina maelezo ya itikadi na mafundisho ya Mwendeleo wa Ahmadiyya katika Uislamu, kifafanuzi cha madai ya Mwanzilishi wake Mtakatifu na hoja za msingi wa madai yake.

Makusudio yangu katika kuandika kurasa hizi, msomaji mpenzi, ni kukufikishia wewe na wengine, Ujumbe ambao Mwenyezi Mungu Ameuleta kwa wanadamu siku hizi ili kuwakusanya kwenye Uislamu na Mtume Wake Mtakatifu (s.a.w.). Kama uchukue taabu ya kuzisoma kurasa hizo zote, sio tu kwamba utapata shukurani zangu nyingi, bali vilevile utajipatia radhi ya Mwenyezi Mungu.

## Uahmadiyya Si Dini Mpya

Kwanza ningependa kubainisha suala moja kwamba majina Mwahmadiyya, Uahmadiyya n.k., hayaashirii kwenye dini mpya. Waahmadiyya ni Waislamu na dini yao ni Islam. Kuutoka Uislamu hatua moja tu wanaamini kuwa ni haramu na kukosa bahati. Naam, Waahmadiyya wametwaa majina, Uahmadiyya, Mwendeleo wa Ahmadiyya na kadhalika. Lakini kutwaa jina sio maana yake kuwa ni dini mpya. Majina Mwahmadiyya, Uahmadiyya n.k., yanakusudiwa tu kuwapambanua Waislamu Waahmadiyya na Waislamu wengine.

## Uislamu Ulitabiriwa

Jina Islam, ni jina zuri ambalo Mwenyezi Mungu mwenyewe amewapa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. na ambalo miaka mingi kabla yake lilipata nafasi ya heshima katika bishara za Manabii wa zamani. Quran Tukufu inasema:

> "Yeye aliwaiteni Waislamu tangu zamani na katika (Quran) hii pia" (22:79).
>
> Na katika Biblia imeandikwa:
>
> "Nawe utaitwa jina jipya litakalotajwa kwa kinywa cha Bwana" (Isaya 62:2).

Hakuna jina jingine linaloweza kuwa na baraka zaidi na takatifu kuliko lile ambalo Mwenyezi Mungu amelivisha heshima kwa kuwafanya Manabii wengine walitabiri. Nani ataliacha jina hili?

Jina hili ni penzi kwetu kuliko maisha yetu. Na dini inayoungana na jina hili ndicho chanzo cha pekee cha uhai wa kiroho.

Lakini kama ilivyo katika wakati wetu huu, firka (makundi) mbalimbali za Waislamu, kwa sababu ya hitilafu ya itikadi zao na mwendo, wamejitwalia majina mbalimbali, imetuwia lazima nasi pia tuwe na jina maalum ili tujipambanuwe katika Waislamu wengine. Jina bora tuliloweza kutwaa ni jina Mwahmadiyya au Uahmadiyya. Jina hili linalingana na wakati huu. Huu ndio wakati ulioteuliwa kwa ajili ya kutangazwa dunia nzima ule Ujumbe wa Kiulimwengu wa Mtukufu Mtume s.a.w. Ndio wakati wa kuenezwa sifa za Mwenyezi Mungu na kuenezwa Elimu ya Fadhili na Uzuri Wake, ndio wakati wa kudhihirishwa sifa ya Ahmadiyyat baada ya kudhihirishwa sifa ya Muhammadiyyat. Hakuna jina zuri lenye kutambulisha siku hizi zaidi ya hili tuliloweza kutwaa.

Tu Waislamu kwa moyo na roho. Tunashika itikadi ambazo Mwislamu wa kweli inamlazimu kuzishika na tunakana itikadi ambazo Mwislamu wa kweli inamlazimu kuzikana. Kama licha ya kushiriki kwetu kwa moyo kwenye kweli za Uislamu na kufuata kwetu amri za Mwenyezi Mungu, mtu yeyote atupe sifa ya ukafiri

na atueleze kama waghushi au waaminio wa dini mpya, ni mtu katili sana. Atahukumiwa na Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza kulaumiwa kwa yale anayoyatangaza kwa mdomo wake, sio kwa yale yaliyo moyoni mwake. Kwani, nani awezaye kusema yaliyomo moyoni mwa mwingine? Kama mtu anamshutumu mwenzake kwa kusema jambo moja na kuamini jingine, anajiinua mwenyewe kwenye cheo cha Mwenyezi Mungu. Ni Mwenyezi Mungu tu ndiye ajuaye yaliyomo mioyoni mwa watu. Yeye peke yake anaweza kusema yale afikiriayo mtu na yale anayoamini. Mtukufu Mtume s.a.w. anakubali ukomo huu wa kibinadamu. Na tena ni nani angeweza kujua moyo wa mtu zaidi kuliko yeye? Anasema juu yake mwenyewe:

> "Miongoni mwenu kuna wanaonileteea mabishano yao. Mimi ni mtu kama ninyi. Inawezekana baadhi yenu wakawa watetezi hodari kuliko wengine. Hivyo, kama nikimpa mmoja haki ya mwingine, nitakuwa ninampa sehemu ya moto. Ni juu yake kukataa." *(Sahihi Bukhari, Kitabul-Ah'kaam Babu Mauizatul-Imam lilikhusuum).*

Tunasoma katika Hadithi kwamba Usama bin Zaid aliteuliwa na Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa Amir wa kikosi fulani. Usama alipambana na kafiri mmoja na kumshambulia. Kafiri huyu alipokaribia kuuawa, alitamka Kalima, akithibitisha kuamini ukweli wa Dini ya Islam. Hata hivyo Usama alimwua. Mtukufu Mtume s.a.w. kusikia hivi, akamkaripia Usama. Akijitetea Usama alisema: "Oo Mtume wa Mwenyezi Mungu, alifanya vile kwa woga." Mtukufu Mtume s.a.w. akamjibu, "Kwa nini? Je, ulipasua moyo wake ukauona? (*Masnud*, Imam Ahmad bin Hambal).
Elimu ya yale yapitayo mioyoni mwa watu haikupewa wanadamu. Haikumpasa Usama kudhani kama Kalima aliyotamka mtu huyu ilikuwa ni matokeo ya woga au la.

Kwahiyo, tunaweza kulaumiwa kwa yale tuyatamkayo, sio kwa yale yanayoweza kudhaniwa kuwa yamo mioyoni mwetu. Yaliyomo mioyoni mwetu anayajua Mwenyezi Mungu tu. Anayedai kumlaumu mwenzake kwa yaliyomo moyoni mwake ni mwongo. Yeye anakiuka mipaka yake na atahukumiwa na Mwenyezi Mungu.

Hivyo, sisi wa Jumuiya ya Ahmadiyya tunapotangaza kuwa tu Waislamu, hapana mwenye haki kusema kwamba Uislamu wetu ni wa kujisingizia; ya kwamba mioyoni tunakana Uislamu au tunamkana Mtume Mtukufu s.a.w.; na ya kwamba tuna Kalima mpya au kuelekea Kibla kipya tunaposali. Kama inaweza kuwa haki kwa wengine kutupa sifa hizi, basi inaweza kuwa haki kwetu kutoa sifa hizi kwa watu wengine. Tungeweza kusema kuwa tangazo lao la Uislamu ni kisingizio, kwamba Mungu apishe mbali, wanaukana Uislamu na kumtukana Mtukufu Mtume s.a.w. wanaporudi majumbani kwao. Lakini hatuwezi kupotezwa na upinzani. Hatutasema juu ya yeyote kwamba anasema jambo moja na kuamini jingine; ya kwamba ana jambo moja midomoni mwake na jingine moyoni mwake. Kwa amri ya Sheria, uamuzi wetu juu ya wengine utafuata yale waliyonayo na wanayoyatangaza waziwazi.

## Itikadi za Waahmadiyya

Sasa ninaendelea kueleza itikadi zinazoshikwa na Jumuiya yetu ili uone kama kuna yoyote iliyo kinyume na Uislamu:-

(1) Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu yupo; kushiriki katika kuamini kuwapo Kwake ni kutangaza ukweli wa maana sana; sio kufuata mawazo au dhana.

(2) Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Mmoja. Hana mshirika hapa wala mbinguni. Kila kitu kingine ni kiumbe Chake na kinategemea msaada Wake. Hana mwana wala binti. Hana baba wala mama. Hana mke wala ndugu. Ni wa pekee katika Umoja Wake na katika Nafsi Yake.

(3) Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Mtakatifu, ameepukana na kila upungufu na ni mwenye kila ukamilifu. Hakuna upungufu unaoweza kuonekana ndani Yake, na hakuna ukamilifu

usioweza kupatikana ndani Yake.

Uwezo Wake hauna ukomo. Na ndivyo ilivyo Elimu Yake. Amekizunguka kila kitu na hakuna kinachomzunguka Yeye. Ni wa Mwanzo na wa Mwisho, Yu Dhahiri na Amejificha pia. Ndiye Mwumbaji na Mola wa viumbe vyote. Utawala Wake haujapata kushindwa, haushindwi, na hautashindwa kamwe. Ameepukana na kufa. Ni Mwenye uhai wa milele. Hapati upungufu wowote. Matendo yake ni ya hiyari Yake, halazimishwi. Anautawala ulimwengu wote hivi sasa kama alivyokuwa akiutawala zamani. Sifa Zake ni za milele, Uwezo Wake u dhahiri siku zote.

(4) Tunaamini kwamba Malaika ni sehemu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Wanafuata kanuni iliyoelezwa na Quran Tukufu -"Wanafanya wanayoamrishwa" (16:51). Kwa Hekima Yake wameumbwa ili wafanye kazi fulani fulani maalum. Kuwapo kwao ni hakika na kutajwa kwao ndani ya Kitabu Kitakatifu si kwa methali. Wanamtegemea Mwenyezi Mungu kama wamtegemeavyo wanadamu au viumbe Vyake vingine. Hawategemei wao kwa kudhihirisha Uwezo Wake. Laiti Angetaka, Angeumba ulimwengu bila Malaika, lakini Hekima Yake kamilifu ilitaka kuumbwa kwao. Kwa hivi Malaika wakawapo. Mwenyezi Mungu aliumba nuru kwa ajili ya macho na mkate kwa ajili ya njaa. Aliumba nuru na mkate siyo kwa sababu alikuwa na haja navyo, la; kadhalika Hakuwaumba Malaika kwa sababu Anawategemea, bali Malaika wanadhihirisha tu matakwa na Hekima ya Mwenyezi Mungu.

(5) Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu Anasema na watumishi Wake wateule na kuwafunulia makusudio Yake. Ufunuo wa Mungu hushuka kwa maneno. Mpokeaji wa ufunuo hatoi maana wala maneno ya ufunuo. Vyote hutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ufunuo unatoa haja hasa ya mtu. Mtu anaishi kwa huo na kwa njia ya huo mtu anapata kuungana na Mwenyezi Mungu. Maneno ya ufunuo ni ya pekee katika nguvu na utukufu. Hakuna mtu awezaye kuyatunga maneno hayo. Yanabeba hazina ya elimu na hekima. Yako kama mgodi ambao unakunufaisha zaidi ukiendelea kuchimba. Kwa kweli, mgodi si kitu mbele ya ufunuo. Mgodi unaweza kwisha, lakini sio hekima ya ufunuo. Ufunuo uko kama bahari yenye ambari kwa juu yake na chini yake kuna lulu za thamani sana. Wale

wanaoelekea bahari wanaburudishwa na manukato, na wale wanaozama wanakuta lulu chini yake. Ufunuo ni wa namna nyingi. Baadhi ya wakati unaleta amri na Sheria, pengine maonyo na mawaidha. Baadhi ya wakati unaleta elimu ya ghaibu, pengine hazina za elimu za kiroho. Baadhi ya wakati unaleta furaha na radhi ya Mwenyezi Mungu, pengine wajulisha makasiriko Yake, pengine wadhihirisha mapenzi Yake, na pengine humwelekeza mtu kwenye wajibu wake kwa kumkaripia . Baadhi ya wakati unafundisha tabia njema za ndani na pengine unaleta elimu Yake juu ya mwendo m'baya uliojificha wa mtu. Kwa ufupi, itikadi yetu ni kwamba Mwenyezi Mungu anaeleza matakwa Yake kwa watumishi Wake. Maneno haya ni mbalimbali kwa watu wa vyeo na hali mbalimbali na huwa ya namna nyingi. Katika maneno yote ya Kiungu, yaliyokamilika zaidi na bora zaidi ni maneno ya Quran Tukufu. Sheria iliyoelezwa na Quran Tukufu na mwongozo wa kiroho uliomo ndani yake ni wa milele. Hautabatilishwa na ufunuo wowote mwingine wa Mwenyezi Mungu.

(6) Tunaamini kwamba giza linapoenea ulimwenguni na wanadamu kuzama kwenye madhambi, zama ambazo bila msaada wa Mungu inawawia shida kujifungua kamba za Shetani, kwa huruma Yake nyingi na Rehema isiyokadirika, Mwenyezi Mungu Huteua kutokana na watumishi Wake wapenzi na watiifu, wale ambao anawapa kazi ya kuuongoza ulimwengu. Mwenyezi Mungu anasema katika Quran:

"Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji (Sura 35:25).

Ina maana kwamba Mwenyezi Mungu alituma Wajumbe Wake kwa watu wote ulimwenguni. Maisha yao safi na mfano wao mkamilifu ukafanya kazi daima kama mwongozo kwa wanadamu wengine. Wale wanaowapa migongo, wanajishusha. Wale wanaowaelekea wanajipatia radhi ya Mwenyezi Mungu. Wanafunguliwa milango ya baraka Zake. Rehema Yake inawafunika. Wanakuwa waalimu wa kiroho kwa vizazi na vizazi na wanafikia ukuu katika Akhera na dunia.

Tunaamini pia kwamba Mitume wa Mwenyezi Mungu ambao toka zamani wamewasaidia wanadamu kuwatoa kwenye giza la

madhambi, walikuwa wa daraja mbalimbali za ukuu wa kiroho na walitimiza kwa kadiri mbalimbali makusudio ya kutumwa kwao. Mkuu wa hao wote alikuwa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Mwenyezi Mungu alimwita mfalme wa wanadamu naye ni "Mjumbe kwa wanadamu wote" (34:29). Mwenyezi Mungu alimfunulia elimu ya mema na mabaya na akambariki kwa msaada Wake. Wafalme wenye nguvu sana ardhini waligwaya kwa kumwogopa. Ardhi yote ikawa mahali pa kuabudia kwa ajili yake (*Sahihi Bukhari: mlango wa Tayammum*). Wakati ulifika ambao wafuasi wake walionekana dunia nzima; kila sehemu ya dunia kulikuwa waaminio walioinama na kumsujudia Mwenyezi Mungu Mmoja, Mungu asiye kifani. Uadilifu ukaanza kutawala mahala pa batili, huruma mahala pa ukatili. Kama Manabii wa zamani wangeishi wakati wa Mtume s.a.w., wangelazimika kumtii na kumfuata Nabii huyu mkamilifu. Quran Tukufu imesema kweli:

> "Na (Kumbukeni) Aliposhika Mwenyezi Mungu ahadi kwa Manabii: Nikiisha wapeni Kitabu na hekima, kisha awafikieni Mtume msadikishaji wa yale yaliyo pamoja nanyi, ni juu yenu kumwamini na kumsaidia" (3:82).

Mtume s.a.w. mwenyewe amesema:

> "Lau kama Musa na Isa wangekuwa hai wasingekuwa na njia ila kunifuata" (Tafsir *Ibn Kathir*, Kitabu cha 2, uk. 246).

(7) Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu anasikia maombi ya watumishi Wake wanaomwomba. Anawaondolea shida zao. Ni Mungu aliye Hai, na Uhai Wake u dhahiri katika mambo yote wakati wote. Mwenyezi Mungu si kama jengo tujengalo tunapochimba kisima ambalo hubomolewa baada ya kuchimbwa kisima. Bali Yeye ni kama nuru na pasipo Yeye hatuoni chochote; ni kama roho ambaye akiondoka kila kitu kitakufa. Akiondolewa Yeye na tuwe mara kama makundi yasiyo na uhai. Sio kweli ya kwamba Mwenyezi Mungu

aliumba ulimwengu kishapo akaenda kukaa pembeni. Anaendelea kutoa ukarimu Wake na kufungamana na viumbe Vyake. Wanapojiona wanyonge na wadhaifu, anawageukia kwa msaada Wake. Kama wakimsahau, anawakumbusha juu ya dhati Yake. Ndipo kwa njia ya Mtume Wake anawathibitishia:

"Basi hakika Mimi Nipo karibu. Nayaitikia maombi ya mwombaji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka" (2:187).

Yaani, Mwenyezi Mungu anasikia maombi ya watu Wake. Ni juu yao kumwamini na kumwomba Yeye. Kama wakifanya hivi, bila shaka atawaongoza.

(8) Tunaamini kwamba kwa zama mbalimbali Mwenyezi Mungu hupanga kutokea kwa matukio kwa njia maalum. Matukio ya duniani hayafanyiki kwa kanuni za asili peke yake. Bali, mbali na kanuni hizi kuna kanuni maalumu ambayo kwayo Mwenyezi Mungu hudhihirisha Uwezo Wake, Utukufu Wake na Kudra Yake. Ndiyo Kudra ya Mwenyezi Mungu ambayo baadhi ya watu kwa ujinga wao wanaikana. Watu kama hao hawaamini chochote ghairi ya kanuni za asili. Naam, kanuni za asili ni za asili tu lakini sio kanuni za Kudra ya Mwenyezi Mungu. Kanuni za Kudra ya Mwenyezi Mungu ni kanuni ambazo kwazo Mwenyezi Mungu huwasaidia wateule Wake, wale anaowapenda; kwa hizo anahilikisha na kufedhehesha maadui wa rafiki Zake. Kama hakungekuwa kanuni hizi, Musa, aliyekuwa dhaifu na mnyonge angewezaje kumshinda Firauni aliyekuwa mfalme jabari na katili? Ingewezekanaje Musa kushinda na Firauni kushindwa ambapo Musa alikuwa dhaifu na Firauni alikuwa mwenye nguvu? Kama hakuna kanuni ghairi ya kanuni za asili, ni kwa vipi Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. angeweza kuishinda Bara Arabu iliyoamua kumwua na kufuta kabisa kazi yake. Katika kila pambano, Mwenyezi Mungu alimsaidia Mtukufu Mtume s.a.w. na kumpa ushindi juu ya maadui zake. Kila shambulio walilofanya maadui

liliishia kwa kushindwa kwao, na hatimaye, baada ya miaka kumi ya kuuhama mji wa Makka alipokuwa na Sahaba mmoja tu aliyejitoa maisha yake kwa kumlinda Mtume, aliuingia tena mji wa Makka akiwa na Watakatifu elfu kumi. Je, kanuni za asili zinaweza kutoa matukio hayo? Je, zinaweza kuruhusu mambo hayo? Kanuni za asili zinadhamini tu ushindi wa mwenye nguvu dhidi ya dhaifu; na kushindwa kwa dhaifu mbele ya mwenye nguvu.

(9) Tunaamini kwamba mauti sio mwisho wa kuwapo kote kwa wanadamu. Mwanadamu anaishi baada ya mauti na kulipwa matendo yake katika Akhera. Wale watendao matendo mema wanapata malipo ya ukarimu. Wale wanaoasi mafundisho Yake na amri Zake wanakutana na adhabu iliyo ni haki yao. Hakuna kinachoweza kuzuia hesabu hii. Wanadamu lazima waishi na kukutana nayo. Mtu anaweza kuchomwa mpaka akawa majivu na majivu yapeperushwe hewani; anaweza kuliwa na mnyama au ndege au wadudu au ageuke kuwa mavumbi na mavumbi yageuke kitu kingine hata hivyo ataishi tu baada ya mauti na kukutana na Mwumba wake na kutoa maelezo ya matendo yake. Uwezo wa Mwenyezi Mungu unadhamini jambo hili. Sio lazima kwamba mwili huu uwepo ndipo roho iwe hai. Mwenyezi Mungu anao uwezo wa kuhuisha mwanadamu kutokana na chembe chembe ndogo sana za mwili wake au sehemu nyembamba ya roho yake. Hivi ndivyo itakavyokuwa. Mwili unaweza kugeuka kuwa majivu lakini si lazima yawe si chochote na kutoweka. Hata roho haiwi hivyo bila idhini ya Mwenyezi Mungu.

(10) Tunaamini kwamba makafiri na maadui wa Mwenyezi Mungu, mpaka wasamehewe na Mwenyezi Mungu kwa Rehema Yake kubwa, wataishi mahala paitwapo Jahannamu. Joto kali na baridi kali vitakuwa ndiyo adhabu za mahala hapo, lakini makusudio hayatakuwa kuwaumiza wadhalimu, bali kuwasuluhisha. Huko Motoni, makafiri na maadui wa Mwenyezi Mungu watatumia siku zao kwa mayowe na maombolezo, wakijutia siku walizotumia kwa kufanya maasi. Wataendelea hivi, mpaka Rehema ya Mwenyezi Mungu, ambayo imevizunguka vitu vyote, itakapowazunguka waasi na maasi yao. Hapo ndipo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyotangazwa na Mtukufu Mtume s.a.w. itakapotimia:

"Zama zitaifikia Jahanamu ambapo hamtakuwa yeyote ndani yake; pepo zitavuma na madirisha yatapiga kelele nyingi" (Tafsir *Ma'alim-ut-Tanziil* chini ya Aya 107, Sura Hud).

(11) Tumaamini kwamba wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, Malaika Wake na Vitabu Vyake; ambao wanafuata, kwa mioyo yao na roho zao, mwongozo utokao Kwake; ambao wanatembea kwa unyenyekevu na wanajinyenyekeza mbele Yake; wale ambao wanaishi kama maskini ijapokuwa wawe matajiri; ambao wanawatumikia wanadamu na kujinyima starehe yao kwa ajili ya wengine; ambao wanaacha kila namna za dhuluma, ukatili na uhaini; ambao ni mifano ya wema kwa wanadamu na kujitenga na tabia mbaya; watu hawa watakwenda mahala paitwapo Jannah. Amani na furaha zitaenea mahala hapo. Hakutakuwa na maumivu. Kila mtu atajipatia furaha na radhi ya Mwenyezi Mungu. Mungu atakuwapo mbele ya wote, fadhili Zake zitamzunguka kila mmoja. Watakuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu hivi kwamba kila mmoja atakuwa kama kioo akiangaza kwa Mwenyezi Mungu na sifa Zake kamilifu. Matamanio yote ya ovyo ya mtu yatatoweka. Matamanio ya watu yatakuwa matamanio ya Mwenyezi Mungu. Watakuwa wamefikia uzima wa Milele, kila mmoja akiwa mdhihirishaji wa Mwumba Wake.

Hizi ndizo itikadi zetu. Kama kuna itikadi zingine zozote ambazo mtu lazima awe nazo kabla ya kusemwa kuwa ni Mwislamu, sisi hatuzijui. Maimamu wa Kiislamu hawaelezi itikadi zaidi ya hizi. Tunaamini itikadi zote za Kiislamu na kuzishika kuwa itikadi zetu.

## Tofauti na Waislamu Wengine

Sasa, msomaji mpenzi, unaweza kuanza kustaajabu kwa nini tunafikiriwa kuwa tofauti, tunapoamini kwa moyo wote itikadi zote zinazojulikana za Uislamu? Kwa nini Maulamaa wanatutukana? Kwa nini wanatuita makafiri?

Kwa kujibu, ninaweza tu kutaja mambo ambayo kwayo Maulamaa wanasema tumeutoka Uislamu. Mwenyezi Mungu Akulinde na maoni ya kosa na Akufungulie milango ya Rehema Zake!

## Nabii Isa Alikufa Kama Kawaida

Jambo la kwanza na kubwa kabisa ambalo maadui zetu wanatupinza kwalo ni kwamba sisi tunasadiki kwamba Nabii Isa (a.s.) wa Nazareti alikufa kifo cha asili. Kusadiki kwamba Nabii Isa alikufa kifo cha asili kunasemwa ni kumtusi Nabii Isa, ni kuiacha Quran Tukufu na fundisho la Mtukufu Mtume s.a.w. Ni kweli kuwa tunasadiki kufa kwa Nabii Isa. Lakini si kweli kwamba kusadiki kuwa amekufa ni kumtusi au kuacha Quran Tukufu au kuwa mbali na fundisho la Mtukufu Mtume s.a.w. Mtu akifikiri zaidi juu ya jambo hili mara moja atagunduwa kwamba lawama tunazolaumiwa sisi hazitokani na itikadi yetu juu ya kifo cha Nabii Isa. Bali zinatokana na itikadi yao kwamba Nabii Isa hakufa bali yu mzima mbinguni.

Tu Waislamu, na tukiwa Waislamu wajibu wetu wa kwanza ni kuthibitisha Ukuu wa Mwenyezi Mungu na heshima ya Mtukufu Mtume s.a.w. Naam, tunawaamini Manabii wote wa Mwenyezi Mungu. Lakini mapenzi yetu na heshima yetu kwa Mtukufu Mtume s.a.w. ni ya juu sana, kwa sababu yeye alijitolea kwa ajili yetu; alijikaribishia mauti kwa kutuokoa na kifo cha kiroho; alihuzunika sana kwa ajili yetu. Aliacha starehe yake kwa ajili yetu. Alijishusha ili sisi tusimame juu. Alipanga namna za manufaa yetu na kutuombea starehe za daima. Aliacha miguu yake ivimbe kwa kusimama ibadani. Akiwa mtakatifu, aliomba tutibiwe madhambi yetu, kutuokoa katika Moto; alisali mpaka msala ukaloa kwa machozi. Alilia mpaka kifua chake kilitoa sauti kama birika la maji yanayochemka.

Kwa ajili yetu alisogeza Huruma ya Mwenyezi Mungu; alitaabika kwa kumpendeza Yeye na kutusaidia sisi pia. Alitufanya tufunikwe na shuka ya Rehema Yake, kawa la Huruma Yake.

Alijitahidi na akapata njia ambazo kwazo tuweze kumridhisha Mwenyezi Mungu; njia ambazo kwazo tuweze pia kuungana naye. Aliyoyafanya kwa ajili yetu hayajapata kufanywa kabla na Nabii yeyote kwa ajili ya kaumu yake.

Basi, fatwa za ukafiri zinatupendeza sisi. Tungependa kuitwa makafiri kuliko kumfahamu Nabii Isa kuwa sawa na Mungu Mwumba wetu, Mruzuku wetu na Mlinzi wetu, ambaye anatupa mkate wetu wa kila siku na elimu na mwongozo tunaotegemea kwa starehe yetu ya kiroho. Fatwa za ukafiri zinakaribishwa mno nasi kuliko kusadiki kwamba Nabii Isa yuko hai mbinguni bila ya kula wala kunywa. Tunamheshimu Nabii Isa. Lakini kwa nini? Kwa sababu ni Nabii wa Mungu wetu. Twampenda Masihi. Lakini kwa nini? Kwa sababu Mungu alimpenda naye alimpenda Mungu. Kumheshimu kwetu ni kwa sababu ya kumheshimu Mwenyezi Mungu. Tunawezaje kumweka juu ya Mwenyezi Mungu na kumdharau Mungu kwa sababu yake? Je, tuwape nguvu wahubiri wa Kikristo ambao kazi yao kila siku ni kutafuta makosa katika Uislamu na Quran Tukufu? Je, tuwafanye wafikiri kwamba Nabii Isa alikuwa Mungu? Kwani, kama hakuwa Mungu, anawezaje kuwa hai mbinguni? Tunawezaje kwa vinywa vyetu wenyewe, kusema jambo livunjalo heshima ya Umoja wa Mwenyezi Mungu? Tunawezaje kuiharibu na kuangamiza dini Yake? Maulamaa wako huru kufanya watakalo; wanaweza kuwachochea watu dhidi yetu, watupige mawe au watuue. Hatuwezi kumwacha Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Nabii Isa. Tungekubali mauti kama tungelazimishwa kusema kwamba Nabii Isa yuko hai mbinguni kama Mungu - Nabii Isa ambaye Wakristo wanaamini kuwa ni mwana wa Mungu na ambaye kwa ajili yake wanautupa Umoja na Kujitegemea kwa Mwenyezi Mungu. Laiti tungebakia ujingani, ingelikuwa vingine. Lakini tangu macho yetu yafumbuliwe na Mtume wa Mwenyezi Mungu, ambaye ametuonesha Umoja wa Mwenyezi Mungu, na Utukufu Wake, na Uwezo Wake, na Ukuu Wake na ukarimu Wake hatuwezi kufanya hivyo. Na litokee lolote, hatuwezi kumwacha Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kiumbe mwanadamu. Kama tufanye hivi, hatujui tutakuwa wapi. Heshima ni ya Mwenyezi Mungu na vyeo vyote vinatoka Kwake. Tunapoona waziwazi kwa

kusadiki kuwa Nabii Isa yuko mbinguni ni kumtusi Mwenyezi Mungu, hatuwezi kusema ya kuwa itikadi hii ni kweli. Sisi hatuwezi kuelewa kwa nini kusadiki kifo cha Nabii Isa ni kumtusi Isa. Mitume wakubwa wakubwa kuliko Nabii Isa wamekufa na vifo vyao havikuleta fedheha kwa ajili yao. Vilevile kifo cha Isa hakiwezi Kuwa fedheha kwake. Lakini kama, kudhania yasiyowezekana, tukutanishwe na mawili - Mungu au Isa - na kama tutakiwe kufanya uchaguzi, bila shaka tutamchagua Mwenyezi Mungu. Tuna hakika kuwa Nabii Isa mwenyewe, ambaye alimpenda sana Mwenyezi Mungu, asingekubali kamwe cheo kinachomheshimisha Isa na kumdharaulisha Mwenyezi Mungu na Umoja Wake. Quran Tukufu inatufundisha hivihivi:

"Masihi hatebeua kuwa mtumishi wa Mwenyezi Mungu wala Malaika waliokurubishwa" (4:173).

## Quran na Hadithi Vinasema Nabii Isa Kafa

Tunafungwa hapa na Neno la Mwenyezi Mungu. Tunaposoma katika Quran Tukufu:

"Na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao, na Wewe ni Shahidi juu ya kila kitu" (5:118).

Mwenyezi Mungu katika jina la Nabii Isa anatangaza kwamba Wakristo walipotea baada ya kifo cha Isa. Alipokuwa hai, walishika imani safi. Kwa kusoma haya ndani Ya Quran, tunawezaje kufikiri kuwa Isa si mfu bali yu mzima mbinguni? Pia tunasoma ndani ya Quran Tukufu:

"Ewe Isa, kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama" (3:56).

Nabii Isa aliinuliwa kwa Mwenyezi Mungu baada ya kifo chake. Maneno "Nitakuinua" au "Nitakunyanyua" yanakuja baada ya maneno "Nitakufisha". Ni lazima tufuate kanuni za lugha. Linalotajwa mwanzo, lazima litendeke kwanza. Lakini pengine Maulamaa wanajua kanuni hizi vizuri zaidi kuliko Mwenyezi Mungu. Huenda wanafikiri kuwa ijapokuwa "Nitakuinua" imetajwa mwisho katika aya hii, lakini ingetajwa mwanzo. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye hekima kinyume na maarifa yetu. Anajua vizuri mno namna gani mawazo yanatakiwa yaelezwe. Katika usemi Wake hakuwezi kuwa na kosa, wala kupotoka neno moja katika mpango wa maneno Yake. Ni Mwumba wetu nasi ni viumbe Vyake. Tutathubutuje kuona kosa katika usemi Wake? Lakini Maulamaa wanaonekana kufikiri kwamba kunaweza kuwa na kosa katika usemi wa Mwenyezi Mungu na sio katika wao kuelewa usemi huo. Sisi hatuwezi kusema hivi; kwani, tunaona ni maangamio matupu fikara hii. Hali tuna macho, hatuwezi kutumbukia shimoni. Hali tunajua, hatuwezi kunywa kikombe cha sumu.

Baada ya Mwenyezi Mungu, tunampenda Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. tu. Ni Mkuu wa Manabii wote. Hakuna mwanadamu mwingine, awe nabii au la, ambaye amefanya hata sehemu ndogo sana ya yale aliyoyafanya Mtukufu Mtume s.a.w. kwa ajili yetu. Hatuwezi kumheshimu zaidi mtu mwingine. Haiwezekani kwetu kufikiri kwamba Isa, Masihi, yu hai mbinguni hali Muhammad, Mtume wetu Mtukufu, amezikwa chini ya ardhi. Hatuwezi kufikiri hivyo. Tunasadiki kwamba kwa daraja ya kiroho, Mtukufu Mtume s.a.w. amesimama juu sana kuliko Isa. Inawezekana kweli Mwenyezi Mungu ampandishe Isa mbinguni kwa sababu ya

alama ndogo sana ya hatari kwa maisha yake, lakini asimpandishe Mtukufu Mtume s.a.w. walau karibu ya nyota alipokuwa akifukuzwa na maadui zake huku na huko? Hatuwezi kusadiki kwamba bwana wetu yu mfu ardhini lakini Isa yu hai mbinguni. Tunaona kifo ni afadhali kuliko imani hii ambayo ni fedheha mbele ya Wakristo. Lakini, mshukuru Mwenyezi Mungu, mambo hayako hivyo. Mwenyezi Mungu hangeweza, na kwa kweli, hajapata kumfanyia Mtukufu Mtume s.a.w. namna kama hii. Mwenyezi Mungu Ndiye Bwana wa mahakimu wote. Yeye Mwenyewe alimwita Mtukufu Mtume s.a.w. kama Mfalme wa wanadamu, hangeweza kumjali zaidi Isa. Kwa ajili ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu aliutikisa ulimwengu wote. Yeyote aliyefikiri kumfedhehesha, alifedheheka mwenyewe. Je, angeweza kumfedhehi Mtukufu Mtume s.a.w. na kuwapa maadui nafasi ya kuchekelea fedheha yake? Kufikiri kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. yu mfu ardhini na Isa wa Nazareti yu hai mbinguni, kunanisisimua nywele. Ninaona ni kiroja na fedheha pia, kwa hiyo ninajiona nikitangaza "La, Mungu hawezi kufanya hivi". Anampenda Mtukufu Mtume s.a.w. kuliko yeyote mwingine. Hangeweza kumwacha afe na kuzikwa lakini ampandishe Isa mbinguni. Laiti mtu yeyote angestahiki kuwa hai na kupanda mbinguni huyo angekuwa Mtukufu Mtume s.a.w. Kama amekufa kama kawaida, basi Manabii wengine wamekufa kama kawaida. Hali ya kujua cheo kikubwa sana alichonacho Mtukufu Mtume s.a.w. mbele ya Mwenyezi Mungu, hatuwezi hata kidogo kufikiri kwamba angefanyiwa na Mungu Mwenyezi duni ya yale aliyofanyiwa Isa. Hatuwezi kufikiri kwamba zama za Hijra, Mtukufu Mtume s.a.w. alipojificha ndani ya pango la Thaur, ambalo ili alifikie ilimbidi abebwe na Seyidna Abubakar r.a., Mwenyezi Mungu hakupeleka Malaika wowote kumwokoa; lakini Mayahudi walipotaka kumkamata Isa, Mungu akamnyanyua mpaka mbingu ya nne ili kumwokoa na mpango wa Mayahudi wa kumwua. Katika vita ya Uhud, Mtukufu Mtume s.a.w. alibakiwa na Waislamu wachache tu waliomzunguka alipokuwa akishambuliwa na maadui. Mungu hakupeleka Malaika wowote, wala hakuumba pale zingaombwe ili maadui walishambulie badala ya kumshambulia Mtukufu Mtume s.a.w., na kuvunja meno ya zingaombwe hilo badala ya meno ya

Mtukufu Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu aliwaacha maadui wamshambulie Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe na mpaka alipoanguka kama aliyekufa, maadui wakapiga kelele za shangwe na hoihoi kwamba (Mungu apishe mbali). wamemwua Muhammad, Mtume wa Mungu. Lakini kwa kumhusu Isa, Mungu hakuacha hata maumivu kidogo tu yamsumbue. Mara tu Mayahudi walipoamua kumkamata, Mungu akamnyanyua mbinguni, na mahala pake, wakamkamata mmoja wa maadui zake ambaye Mungu alimfanya awe na sura ya Isa, na hivyo wakamwamba msalabani huyu badala ya kumwamba Isa!

Tunastaajabu juu ya matokeo ya watu hawa. Upande mmoja wanadai kumpenda sana Mtukufu Mtume s.a.w.; na upande mwingine, wenyewe wanaelekea kumdhararu na kumfedhehesha. Na hawakomei hapo. Wanaendelea mbele na kutoa Fatwa za ukafiri kwa wale ambao kwa sababu ya kumpenda Mtume s.a.w. wanakataa kushiriki kwenye zile itikadi zinazomweka mtu mwingine juu ya Mtukufu Mtume s.a.w. Tunashangaa wana muradi gani kwa ukafiri? Je, kufikiri kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. ana daraja ya juu zaidi ya Manabii wengine na kumtolea heshima inayomstahiki ni ukafiri? Kama huu ni ukafiri, basi Wallahi ukafiri wetu una thamani mara nyingi zaidi kuliko imani ya wale wanaotupa ukafiri huo. Seyidna Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa, alisema sawa:

> "Baada ya Mwenyezi Mungu, nimelevywa na mapenzi ya Muhammad. Kama hii ni kufuru, Wallahi, mimi ndiye kafiri mkubwa wa makafiri wote".

Ni lazima sote tufe siku moja na kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu na kujibu tutakayoulizwa. Kwa nini tumwogope mwanadamu yeyote? Wanadamu wanaweza kutupa dhara gani? Tunamwogopa Mwenyezi Mungu tu na tunampenda Yeye tu. Baada Yake, tunampenda na kumheshimu Mtukufu Mtume s.a.w. zaidi. Kama kwa ajili ya Mtukufu Mtume s.a.w. italazimu kutoa heshima yetu, manufaa na vitu vya dunia hii, tutaona rahisi sana. Lakini kumdharau Mtukufu Mtume s.a.w. hatuwezi kuvumilia hata kidogo. Hali ya kujua utakatifu aliokuwa nao, elimu ya kiroho aliyokuwa

nayo na ukaribu aliokuwa nao na Mwenyezi Mungu hatuwezi kufikiri kwamba Mwenyezi Mungu alimpenda mtu mwingine yeyote zaidi kuliko alivyompenda Mtukufu Mtume s.a.w. Kama sisi tuchukue fikara hii, tutastahiki adhabu zaidi kuliko wengine wote. Tunajua vizuri sana kwamba waliomkataa Mtukufu Mtume s.a.w. walimwambia wakimtaka aoneshe mwujiza wa kupanda mbinguni. Walisema:

"Au upande mbinguni; na hatutaamini kupanda kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome" (17:94).

Kwa kujibu ombi lao hili, Mwenyezi Mungu hakumpa Mtume s.a.w. uwezo wa kuonesha mwujiza aliotakiwa kuuonesha. Badala yake, Mwenyezi Mungu alimwambia Mtukufu Mtume s.a.w.:

Sema: Mola wangu ni Mtakatifu! mimi siye ila ni mtu tu, Mtume" (17:94).

Lakini, Maulamaa wanavyofundisha, Nabii Isa, Mwenyezi Mungu alimpandisha mbinguni. Mtukufu Mtume s.a.w. anapoombwa kupanda mbinguni, kupanda mbinguni kunasemwa na Mwenyezi Mungu kuwa hakuwezekani na mwanadamu. Lakini Isa anapandishwa mbinguni bila haja hata kidogo. Kama hili ni kweli, je, haitakuwa kwamba Isa hakuwa mwanadamu bali Mungu? Mungu atulinde na mawazo haya. Je, haitaleta maana kwamba Isa alikuwa na daraja ya juu zaidi na alipendwa na Mungu zaidi kuliko Mtukufu Mtume s.a.w.? Lakini tunajua, na ni dhahiri kama jua, kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. ni m'bora na mkuu wa manabii wote. Hali ya kujua hivi, tunawezaje kufikiri kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. hakupanda mbinguni, bali alikufa na kuzikwa ardhini kama kawaida, lakini Isa apae mbinguni na kuwa huko hai kwa miaka mamia na mamia?

Sio tu kwamba ni jambo la ghera juu Ya Mtume s.a.w. Bali ni jambo la ukweli wake pia, ukweli wa madai yake. Je, hakusema Mtume s.a.w. kwamba "Lau kama Musa na Isa wangalikuwa hai,

wasingekuwa na njia ila kunifuata?" (*Zurqani,* Kitabu cha 6 uk. 54).

Kama Isa yu hai, basi madai haya ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni lazima yasemwe kuwa ni ya uongo. Maneno ya Mtukufu Mtume s.a.w. yana maana sana na yako dhahiri. Anasema, "Lau kama" Musa na Isa wangalikuwa hai. Hii "Lau kama" inawaweka Musa na Isa pamoja na ina maana kwamba hawa wawili ni wafu. Musa si mzima wala Isa si hai. Hili ni tangazo la maana sana la Mtukufu Mtume s.a.w. Baada ya kusikia tangazo hili, hakuna mfuasi wa kweli wa Mtukufu Mtume s.a.w. anayeweza kufikiri kwamba Isa yu hai mbinguni. Maana kama Isa yu hai mbinguni, tangazo la Mtukufu Mtume s.a.w. linageuka kuwa la uwongo; pia elimu yake juu ya jambo lenyewe.

Kuna tamko jingine la maana sana la Mtukufu Mtume s.a.w. Wakati wa ugonjwa wake wa mwisho, alimwambia binti yake Fatima:

> "Hakika Jibrili alikuwa akinisomea Quran mara moja kila mwaka. Na mwaka huu amenisomea mara mbili. Na akaniambia kuwa kila Nabii aliishi nusu ya umri wa Nabii aliyemtangulia. Akaniambia pia ya kuwa Isa bin Mariamu aliishi miaka 120. Kwa hiyo, nafikiri ninaweza kuishi mpaka miaka 60" (*Mawaahib-ul-ladunniyyah,* kilichoandikwa na Qastalani, Kitabu cha I uk. 42).

Tamko hili ni la ufunuo. Mtukufu Mtume s.a.w. hakusema lolote kwa kujikinai, bali alieleza aliyoambiwa na Jibrili, Malaika wa Wahyi. Sehemu ya maana sana ya tamko hili ni kwamba Isa aliishi miaka 120. Kwa maelezo ya Agano Jipya, Isa alikuwa yapata miaka 32 au 33 hivi alipowambwa msalabani na "akapaa mbinguni." Kama Isa kweli "alipaa" basi umri wake mpaka wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. unakuwa karibu miaka 600, sio 120. Kama aliyoyapokea Mtukufu Mtume s.a.w. kutoka kwa Jibrili ni ya kweli, Mtume s.a.w.

angeishi mpaka karibu miaka 300. Lakini aliishi miaka 63 tu. Na kwa maelezo ya Jibrili, Isa aliishi miaka 120. Tamko hili la Mtukufu Mtume s.a.w. linathibitisha kuwa kufikiri kuwa Isa yu hai mbinguni ni kinyume na fundisho la Mtukufu Mtume s.a.w., kinyume na yale aliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu. Hali ya kujua yote haya, tunawezaje kusadiki kuwa Isa yu hai? Tunawezaje kukana chochote alichofundisha Mtukufu Mtume s.a.w. waziwazi?

## Masahaba Wanakubali Nabii Isa Kafa

Ilisemwa kwamba mnamo miaka 1300 hakuna yeyote bali sisi ndio tunaeleza ukweli juu ya kifo cha Nabii Isa. Maulamaa wote na Masheikh wa Kiislamu hawakujua jambo hili. Fikara ni kwamba makubaliano ya Waislamu wa nyuma hayawafiki yale tunayofundisha sisi juu ya suala hili. Lakini wale wanaofikiri hivi wanasahau kwamba mufasirina wa kwanza wa Uislamu walikuwa ni Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. Masahaba ndio walioanza kueleza itikadi ya mafundisho ya Uislamu kwa wengine. Halafu hawa wengine wakawa waalimu, wakaeneza itikadi hizo na mafundisho ulimwenguni. Sasa basi, kuhusu Masahaba, wao wako pamoja nasi kwa yale tunayofundisha sisi leo juu ya Isa. Tena, wangewezaje kufundisha kinyume na hivi? Wangeweza kufundisha itikadi inayomshusha chini Mtukufu Mtume s.a.w.? Sio tu kwamba Masahaba wako pamoja nasi; bali tangazo la kwanza ambalo Masahaba waliamua kwa pamoja lilikuwa ni ukweli juu ya kifo cha Nabii Isa. Ijma'i (makubaliano) ya kwanza ya Masahaba ilipiga muhuri juu ya jambo hili. Kwani ndani ya Hadithi na vitabu vya historia tunaona kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alipofariki, Masahaba waliingiwa na butwaa kwa huzuni. Hawakuweza hata kutamka neno. Baadhi yao waliathirika sana na kifo hivi kwamba siku chache tu baadaye walifariki, kwa kushindwa kuvumilia mtengano huu. Umar r.a. miongoni mwa watu wote, aliathirika sana hivi kwamba aliamua asisadiki kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa amekufa. Alikamata upanga na kutangaza kwamba yeyote ambaye angesema kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. amefariki,

angepoteza kichwa chake. Akaanza kusema kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa ametoweka tu pale kwa muda, kama vile Musa alivyojitenga na watu wake alipoitwa na Mwenyezi Mungu. Musa alirejea kwa watu wake baada ya siku arobaini, hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Atakaporejea Mtume s.a.w. atawauliza wale wote waliosema mabaya juu yake na walioonesha unafiki. Hata anaweza kuwaua au kuamuru watundikwe mtini. Umar alikuwa akisema hivi kwa dhati. Hapakuwa hata mmoja wa Masahaba aliyethubutu kukana na kumpinga kwa kauli hii, wengine walikuwa wameukubali usemi wa Umar. Walianza kufikiri kwamba Mtume s.a.w. hakuwa amekufa. Kwa sababu hii huzuni yao ikabadilika. Alama yake ikaonekana nyusoni mwao. Wale waliokuwa wamejiinamia kwa huzuni, waliinua nyuso zao. Wengine ambao hawakushindwa na huzuni, ambao waliweza kuona mbali, walimtuma mmoja wao akamwite Seyidna Abubakar. Abubakar hakuwepo mjini Madina alipofariki Mtume s.a.w., alikuwa amemruhusu aende, kwa sababu wakati ule hali yake ilionekana kuwa njema. Kabla sahaba huyu hajautoka mji alimwona Abubakar akija. Kumwona tu, sahaba huyu hakuweza kujizuia. Machozi yakamtoka. Haikuwa lazima atamke neno. Abubakar akaelewa nini kilikuwa kimetokea. Alimwuliza Sahaba huyo, "Mtume amefariki?" Sahaba huyo alipojibu, siyo tu kwamba alithibitisha habari hii ya huzuni, bali pia alimwambia Abubakar yale aliyokuwa akisema Umar kwamba "Yeyote atakayesema kuwa Mtume s.a.w. amekufa atapoteza kichwa chake"!!! Abubakar alisikia hayo na mara moja akaenda kule kulikolazwa maiti ya Mtukufu Mtume s.a.w. Alifunua shuka aliyokuwa amefunikwa maiti na akatambua mara moja kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa amekufa. Uchungu wa kutengana na rafiki yake mpenzi na kiongozi wake ukamfanya atokwe na machozi. Aliinama na kuubusu uso wa Mtukufu Mtume s.a.w. na kusema:

> "Wallahi hutakufa mara mbili. Hasara waliyopata wanadamu kwa kifo chako ni kubwa zaidi ya hasara waliyopata kwa kifo cha Nabii mwingine yeyote. Huna haja ya sifa na kilio hakiwezi kupunguza uchungu wa kutengana. Kama tungeliweza kuzuia mauti yako, tungefanya hivi kwa maisha yetu yote."

Abubkar alisema haya na kufunika uso wa Mtukufu Mtume s.a.w.; kisha akaenda pale Umar alipokuwa akizungumza na Masahaba. Umar alikuwa akiwaambia kwamba Mtume s.a.w. hakuwa amekufa; bali alikuwa amejitenga nao kwa muda. Abubakar akamwomba Umar anyamaze kidogo ili naye awaeleze yake. Umar hakunyamaza, akaendelea tu kusema. Abubakar akawageukia baadhi ya Masahaba na kuanza kuwaambia, Mtume s.a.w. hakika amekufa. Masahaba wengine wakamgeukia Abubakar na kuanza kumsikiliza. Umar pia akalazimika kusikiliza. Abu Bakar akasoma aya za Quran Tukufu:

> "Na siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu?" (3:145).

> "Kwa yakini wewe utakufa na hakika wao pia watakufa" (39:31).
> Baada ya kusoma aya hizi aliendelea kusema:

> "Enyi watu, yeyote miongoni mwenu aliyekuwa akimwabudu Muhammad, na ajue kuwa Muhammad amekufa, na aliyekuwa miongoni mwenu akimwabudu Allah, na ajue kuwa Allah yu Hai, Hatakufa" (*Bukhari,* Kitabu cha 2, mlango Manaaqibi Abubakar).

Abubakar aliposoma aya za Quran Tukufu na kuashiria maana zake, Masahaba walitambua nini kilikuwa kimetokea. Mtume s.a.w. alikuwa amekufa. Walianza kulia. Inaelezwa ya kuwa Umar alisimulia kwamba Abubakar alipokuwa akizisoma aya hizi, na maana zake zikiwa zimemwingia ghafla, aliona kana kwamba aya zile zilikuwa zimeshuka wakati ule. Miguu yake haikukaza. Alipepesuka na kuanguka chini kwa kulemewa na huzuni.

Maelezo haya juu ya yaliyotokea kati ya Masahaba alipofariki Mtukufu Mtume s.a.w. yanathibitisha mambo matatu ya maana sana:

Kwanza, yanathibitisha ya kuwa maoni ya Masahaba waliyoamua wote baada ya kifo cha Mtukufu Mtume s.a.w. yalikuwa kwamba Mitume wote kabla ya Mtume s.a.w. walikuwa wamekufa. Hakukuwa na ubaguzi. Laiti Masahaba waliokuwapo kwenye mkusanyiko wa siku ile walifikiri kwamba baadhi ya Mitume wa zamani walikuwa wazima, hawajafa, wangesimama na kuwataja. Wangesema kwa akali Nabii Isa alikuwa hai kwa miaka 600 huko mbinguni. Ya kwamba ilikuwa ni kosa kusema kwamba Mitume wote wa zamani walikuwa wamekufa. Wangeendelea kusema kwamba ikiwa Mtume fulani na fulani ni hai, kwa nini asiwe Mtukufu Mtume s.a.w.?

Pili, yanathibitisha ya kuwa itikadi ya Masahaba kwamba Mitume waliopita kabla ya Mtume s.a.w. walikuwa wamekufa haikuwa ni maoni kati ya Masahaba wenyewe. Ilikuwa ni ukweli uliohifadhiwa ndani ya Quran Tukufu na ukafundishwa wazi na Kitabu Kitakatifu. Zama Abubakar aliposoma aya hizi, Masahaba walizipokea bila taabu. Kama ukweli wa kufariki kwa Mitume wa zamani haukuwamo ndani ya aya hizi, wangesema kwamba ijapokuwa Mitume wa zamani kweli wamekufa, lakini aya alizosoma Abubakar hazikuwa zimehusu kufariki kwao. Hivyo, Abubakar kusoma aya inayotaja Mitume wa kabla yake, kuthibitisha kufariki kwa Mitume wa zamani, na kule kunyamaza kwa Masahaba iliposomwa aya hii, la, bali kufurahi kwao juu ya aya hii na kuetembea kwao mjini wakiisoma, wao ambao walimsikia Abubakar akitoa hoja yake kwa aya hii, kunathibitisha bila shaka kwamba Masahaba walikubali moja kwa moja tafsiri ya aya hii alivyoitoa Abubakar.

Tatu, yanathibitisha ya kuwa Masahaba, wawe walisadiki au la juu ya vifo vya Mitume wa zamani, hawakuwa na wazo kwamba Nabii Isa alikuwa hai mbinguni. Maelezo yote ya tukio hili la maana sana na hotuba muhimu zilizotolewa kwenye mkusanyiko huo yanaonesha kwamba hata Umar, katika hali ya ghadhabu kali, akiogofya kuwaua wale ambao wangesema kwamba Mtume s.a.w. alikuwa amekufa, aliweza kutaja mfano wa Musa tu ambaye

alitoweka kwa siku arobaini kati ya kaumu yake. Hata hakutaja mfano wa Isa. Kama Masahaba walikuwa na wazo kuwa Isa alikuwa hai mbinguni, je, Umar au Masahaba waliofikiri kama yeye wasingeweza kutaja mfano wa Isa? Kule kutaja kwao mfano wa Musa tu kunathibitisha ya kwamba hawakuwa na wazo hata dogo sana kwamba Nabii Isa alikuwa hai, au kwamba alipata hali iliyofikiwa na Musa.

## Jamaa Ya Mtume inakubali Nabii Isa Kafa.

Mbali na maoni ya pamoja ya Masahaba, maoni ya jamaa ya Mtume s.a.w. pia yasaidia itikadi kwamba Nabii Isa s.a. alikufa kama kawaida. Akieleza tukio la kufariki kwa Hadhrat Ali, Imam Hasan alisema:

> "Mtu aliyefariki leo hana kufu yake kwa hali nyingi. Hana wa mfano wake miongoni mwa waliomtangulia wala watakaomfuata. Mtume s.a.w alipomtuma vitani, alikuwa na Jibrili kuumeni kwake na Mikaili kushotoni kwake wakimsaidia. Hakurudi vitani ila alikuwa mshindi. Aliacha nyumbani wasia wa dirham mia saba. Alikuwa ameziweka hizi kwa ajili ya kununulia uhuru wa watumwa. Alikufa mnamo usiku wa tarehe 27 ya mwezi wa Ramadhani, usiku kama ule ambao roho ya Isa ilipaishwa mbinguni" ( *Tabaqaat* cha Ibn Sa'ad Kitabu cha 3).

Kutokana na maelezo haya ya Imam Hasan inadhihirika kwamba kwa maoni ya jamaa ya Mtume s.a.w., Nabii Isa alikufa kama

kawaida. Mpaka iwe walisadiki hivyo, Imam Hasan asingesema kuwa Hadhrat Ali alifariki usiku kama uleule ambao roho ya Isa ilipaishwa mbinguni.

Mbali na Masahaba wa Mtume s.a.w. na jamaa yake, wanazuoni wa Kiislamu waliofika baadaye walithibitisha kifo cha Nabii Isa. Walizamia Quran Tukufu, waliyazamia maneno ya Mtume s.a.w., pia maoni ya Masahaba na familia yake. Inaonekana kwamba swali la ama Isa alikufa au la halikuwagonga kama swali la maana sana. Hivyo hawakutamka hivi juu ya swali hili. Wala maoni yao hayakuhifadhiwa juu ya madhumuni hii. Lakini maoni ya wanazuoni hawa vilevile yanaonesha bila shaka kwamba hata wao walisadiki kwamba Nabii Isa alikuwa amekufa. Ndani ya *Majm'a-ul-Bihaar* mmeandikwa maoni ya Imam Malik kwamba Nabii Isa alikufa kifo cha kawaida.

Kwa ufupi, Quran Tukufu, Hadithi, kupatana kwa maoni ya Masahaba na jamaa ya Mtume s.a.w. na maoni ya wanazuoni wa baadaye wa Kiislamu, yote yanasaidia itikadi yetu juu ya kifo cha Nabii Isa. Yote yanafundisha ya kwamba Nabii Isa alikufa kama watu wote. Kwa hiyo ni kosa kusema kwamba kusadiki kuwa Isa alikufa ni kumdharau Isa, na kwamba ni kukana Quran Tukufu na Hadithi za Mtume s.a.w. Hatumdharau Nabii Isa. Badala ya kumdharau Isa sisi tunashika wazo la maana sana juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na kuonesha cheo kikubwa cha Mtume s.a.w. Tunamtumikia Isa, kwa sababu Isa mwenyewe asingeshika itikadi inayodhalilisha Umoja wa Mwenyezi Mungu; inayosaidia ushirikina, inayoondoa hadhi ya kiroho ya Mtume s.a.w.

Msomaji mpenzi, sasa unaweza kuona mwenyewe ni wapi walio katika haki. Sisi au wapinzani wetu? Je, ni wao wanaostahiki lawama au sisi? Wanamweka mwanadamu kuwa kufu ya Mwenyezi Mungu. Wanashika itikadi inayomdhalilisha Mtume s.a.w.; wanasaidia maadui za Uislamu na kuudhoofisha Uislamu.

## Kuja Kwa Masihi Ni Kuja kwa Mfuasi Wa Mtume s.a.w.

Jambo la pili tunalopinzwa ni kwamba eti kinyume na itikadi inayokubaliwa ya Kiislamu, tunaamini kwamba mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. amedhihiri miongoni mwetu akiwa Masihi Aliyeahidiwa . Kuamini hivi, tunaambiwa, ni kinyume na Hadithi za Mtume s.a.w., eti sawa na hadithi hizo, Masihi ni Isa, mwana wa Mariamu, ambaye atashuka kutoka mbinguni katika wakati wake hasa.

Naam, ni kweli kabisa kwamba tunamwamini Mwanzilishi wa Mwendeleo wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, (Gurdaspur, Punjab, India), kuwa ndiye Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa. Kwa nini isiwe hivi? Ndani ya Quran Tukufu, Hadithi na akili ya kawaida, mnatangazwa ya kuwa Masihi wa kwanza alikufa kama kawaida, hivyo imani yetu kwamba Masihi Aliyeahidiwa ni wa kutokana na wafuasi wa Mtume s.a.w. haiwezi kuwa kinyume cha Quran Tukufu na Hadithi. Quran Tukufu inatangaza kwamba Isa amekufa. Hadithi zinasema hivyohivyo. Kama hadithi bado inaahidi kudhihiri kwa Mjumbe aliyetajwa kama mwana wa Mariamu, huyu aliyeahidiwa anaweza tu kuwa mfuasi wa Mtume s.a.w., siyo Masihi wa Nazareti aliyekufa kama kawaida. Inasemwa ya kwamba hata kama Quran Tukufu na Hadithi vitangaze kifo cha Nabii Isa, mwana wa Mariamu, sisi tuendelee tu kutazamia kufika kwa yuleyule mwana wa Mariamu binafsi. Eti kwani Mwenyezi Mungu si Mwenye uwezo? Eti je, hawezi kumfufua Masihi mfu na kumleta tena duniani? Kwamba kama tusiwe na fikara na tumaini la namna hii tutakuwa tunaukana uwezo wa Mwenyezi Mungu. Lakini hali yetu ni tofauti sana na hii. Hatukani uwezo wa Mwenyezi Mungu. Tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Mweza wa yote. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mweza wa yote, hana haja ya kumfufua Masihi wa Nazareti. Anaweza kuinua mwalimu miongoni mwa wafuasi wa Mtume s.a.w., amfanye kuwa Masihi Aliyeahidiwa na kumpa kazi ya kuuhuisha ulimwengu. Tunashindwa kuona ni kwa vipi mtu ambaye anafikiri kwa makini sana jambo hili, anaweza kusisitiza kwamba uwezo wa Mwenyezi Mungu unamtaka Mwenyezi Mungu amlete hai tena duniani Masihi

wa kwanza. Jambo hili ni kinyume na kanuni zote zinazokubalika. Ni mazoea ya kila siku kwamba mtu anayeweza kuwa na koti jipya, anachukia kuendelea kutumia koti la zamani. Kama ana haja ya koti jipya, analitupa lile la zamani na kuchukua jingine jipya. Ni mtu asiye na uwezo tu ndiye anayetengeneza koti lilelile la zamani kulitumia tena. Mtu maskini tu ndiye anayejali kupita kiasi vitu vya zamani. Mwenyezi Mungu si maskini. Yu Mwenye Uwezo. Kama anaona kwamba waja wake wanahitaji wa kuwaongoza hana haja kumfufua Nabii mfu. Anaweza kumwinua mmoja kati ya waja wake walio hai kuhuisha na kuongoza wengine wote. Tokea Adam hadi Mtume s.a.w., Mwenyezi Mungu hakumfufua hata mara moja Nabii mfu kwa ajili ya kuongoza waja wake. Njia hii si ya lazima kabisa. Ingalikuwa ni ya lazima kama tu kutakasa na kuhuisha kwa taifa fulani kulikiuka uwezo wa Mwenyezi Mungu; kama ufalme wa Mwenyezi Mungu haukuenea kwa watu wa zama zote. Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo na utawala wake unawaenea watu wa zama zote. Si jambo la akili kusema kwamba kwa ajili ya kuongoza watu wa zama fulani, alazimike kumfufua mmoja wa Manabii wafu na kumtoa nje ya pepo ili kumleta hapa duniani mara nyingine. Uwezo wa Mwenyezi Mungu hauna mpaka. Aliweza kuinua Nabii kama vile Mtukufu Mtume s.a.w. kutokana na Waarabu. Haikiuki uwezo wake kuinua mtu mmoja wa zama hizi kuwa mfano wa Nabii Isa au hata mkuu kuliko Isa miongoni mwa Waislamu.

Hivyo, ukweli ni kwamba tunakataa kudhihiri kimwili mara ya pili kwa Masihi wa kwanza, kwa sababu tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Mweza na anaweza kumwinua yeyote kwenye daraja ya kiongozi na Nabii, zama zozote na miongoni mwa watu wowote. Wanakosea sana wale wanaofikiri kwamba Mwenyezi Mungu hawezi kufanya hivi, ya kwamba badala ya kuinua mmoja miongoni mwetu, alazimike kufufua Nabii mfu. Kweli hawa watu hawajapima uwezo wa Allah kama anavyoustahiki.

Kwa hiyo kufika mara nyingine kwa Masihi wa kwanza kunashusha uwezo na hekima ya Mwenyezi Mungu. Kadhalika ni kudhoofisha nguvu ya kiroho ya Mtume s.a.w. Kusema kwamba kudhihiri tena kwa Masihi wa kwanza hakuna budi ni kusema jambo moja la kiroja sana. Tokea azali wakati wowote watu walipopotea

na kuhitaji mwongozo wa mbingu, alikuwa mmoja miongoni mwao wenyewe ndiye ambaye Mwenyezi Mungu alimwinua kwa kazi hii. Je, zama hizi ambapo wafuasi wa Mtume s.a.w. walipopotea na kuhitaji mwongozo wa mbingu, kawaida hii ya kiungu itupwe? Je, Umma huu uhuishwe na Manabii wa zamani, na wafuasi wa Mtume s.a.w. wenyewe washindwe kumpata mhuishaji miongoni mwao? Maana yake ni kwamba Waislamu wawafuate Mayahudi na Wakristo ambao wanapinga uwezo wa kiroho wa Mtukufu Mtume s.a.w. Ni ajabu Waislamu wasitegemee nguvu ya kuhuisha ya Mtukufu Mtume s.a.w. Kama tunafikiri kwamba mfuasi wa Mtume s.a.w. hawezi kuongoza Umma huu wakati wa haja, basi tunawaunga mkono wale wanaokataa mvuto wa kiroho wa Mtukufu Mtume s.a.w. Taa moja yenye nuru kali sana inaweza kuzing'arisha taa zingine nyingi. Taa iliyokufa tu ndiyo haiwezi kufanya hivi. Kama wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. ilikuwa wapotee kiasi hiki hivi kwamba asiweze yeyote yule miongoni mwao kuwahuisha wengine wote, ni lazima ikubaliwe kwamba wakati huo fadhila na hazina ya mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. na mfano wake utakuwa umekoma. Tokeo hili haliwezi kukubaliwa na Mwislamu yeyote wa kweli. Kila Mwislamu wa kweli anajua kwamba wafuasi wa Nabii Musa a.s. walihitaji kuhuishwa wakati hata wakati, na kuhuishwa huku kulifanywa na waalimu walioinuliwa miongoni mwao wenyewe. Alikuwa mfuasi wa Musa aliyewahuisha wafuasi wa Musa. Silsila ya Musa ilidumu mpaka muda aliopenda Mwenyezi Mungu. Hatimaye ulipofika wakati wa kukoma kwa silsila hiyo, Mwenyezi Mungu aliwaachia wafuasi wa Musa na kuelekea dhuria wa Ismail kuinua Nabii kwa ajili ya kuwaongoza wanadamu. Kama sasa, aje Nabii wa silsila ya Musa kuwaongoza wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w., itakuwa na maana (Mungu apishe mbali) kwamba Mwenyezi Mungu ameamua kuikomesha silsila ya Mtukufu Mtume s.a.w. kama alivyokomesha silsila ya Musa, na ya kwamba mahala pake anaanzisha silsila mpya. Itakuwa na maana (Mungu apishe mbali tena) ya kwamba nguvu ya kiroho ya Mtume Mtukufu s.a.w. haina athari tena hivi kwamba inashindwa kumpatia hata mfuasi mmoja nuru iliyo muhimu kwa kuhuishia na kuongozea wafuasi wake tokana na mafundisho na mfano wake.

Ole wao! juu ya kosa dogo sana linalotaka kushusha hadhi yao wenyewe hawawezi kuvumilia; hawakubali dosari yoyote au upungufu ndani yao. Lakini hawachelei kuingiza dosari na udhaifu kwa Mtukufu Mtume s.a.w., na bado wanadai kuwa wapenzi wa Mtume s.a.w. Mtukufu. Yana faida gani mapenzi ya kubwata kwa midomo tu lakini hayapatikani moyoni? Imani isiyofuatana na vitendo ina maana gani? Kama Waislamu walimpenda kweli Mtukufu Mtume s.a.w. wasingechekelea kufika kwa Nabii wa Kiyahudi kuja kuhuisha wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Ni nani anayeomba kwa jirani yake haja anayoweza kuikidhi nyumbani mwake mwenyewe? Ni nani anayemwomba msaada mwenzake ambapo anaweza kujisaidia mwenyewe? Masheikh wanaofikiri na kufundisha wafuasi wa Mtume s.a.w. kwamba Masihi wa Nazareti atafika mara ya pili wakati wa haja, wenyewe wanapita kiasi katika kulinda uluwa wao hivi kwamba katika majadiliano ya dini wangependa kuanguka kuliko kukubali msaada kwa mwingine yeyote. Kama kuna msaada wowote, hawawi na furaha: wanaumwa na kusema: "Je, tumeishiwa elimu sisi hivi kwamba tuhitaji msaada wa wengine?" Lakini inapofika kwa Mtukufu Mtume s.a.w. wanakuwa wepesi mara moja! Wanakuwa chapu sana kuamini na kufundisha ya kuwa zama wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. wanapohitaji kuhuishwa, hawatapata uhuishaji huo kutokana na wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe, sio kutokana na mvuto wa kiroho wa mwenyewe Mtume s.a.w., bali kutokana na ukarimu wa Nabii wa silsila ya zamani, ambaye hakupata chochote katika mafundisho ya Mtume s.a.w. Je, watu wamekuwa wafu na masugu kiasi hiki? Je, wamepotewa na uwezo wote wa kufikiri na kuhisi? Wanahifadhi heshima yao na uluwa wao wenyewe, lakini siyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. Wanaweza kuonesha ghadhabu na makasiriko kwa maadui zao binafsi, lakini siyo kwa wale wanaomkosea Mungu na Mtume Wake?

Tunaulizwa kwa nini tunakataa kufika mara ya pili kwa Nabii wa Kiisraeli. Lakini tunaweza tufanyeje? Hatuwezi kubadili mioyo yetu. Hatuwezi kuonesha mahaba yetu kwa Mtukufu Mtume s.a.w. isipokuwa katika njia za kiasili. Heshima ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni penzi mno kwetu. Hatuwezi kufikiri kwamba kwa ajili ya kuhuisha

wafuasi wake, Mtume s.a.w. ahitaji msaada wa Nabii aliye mbali na yeye na kuwa mdeni wake. Hatuwezi kufikiri hata kidogo kwamba siku ya Kiyama, wanadamu tokea wa mwanzo mpaka wa mwisho kabisa watakapokusanyika mbele ya Mwenyezi Mungu, na matendo na mafanikio yao yote yatatangazwa, Mtume s.a.w. atasimama na mzigo wa deni la Masihi Mwisraeli, Malaika wakitangaza mbele ya wanadamu wote ya kwamba wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. walipopotea, mfano wa kiroho wa Mtukufu huyu mwenyewe ulishindwa kuwahuisha kwenye nguvu ya kiroho, kwa kumhurumia Mtukufu Mtume s.a.w., Masihi wa Kiisraeli akajitupa kutoka peponi na kurudi ulimwenguni kuwahuisha. Hatuwezi kuingiza fikara kama hii. Tungependa ndimi zetu zikatwe kuliko kumkashifu Mtume s.a.w. kwa udhalilifu namna hii. Tungependa mikono yetu ife ganzi kabisa kuliko kuandika jambo la namna hii kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Mtukufu Mtume s.a.w. ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Nguvu yake ya kiroho haiwezi kamwe kufutika. Yu Muhuri wa Manabii. Fadhili na baraka zake za kiroho hazimaliziki kabisa. Hana haja kupata deni kwa Manabii wengine wowote na kudaiwa nao. Manabii wengine ndio wanaodaiwa naye. Hakuna Nabii hata mmoja ambaye Mtukufu Mtume s.a.w. hakutangaza ukweli wake mbele ya waliomkataa. Yalikuwa mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. yaliyowaingiza mamilioni ya wanadamu katika imani juu ya Manabii ambao walikuwa hawana habari nao. Kuna Waislamu milioni 80 katika India*. Wachache miongoni mwao walitoka nchi za nje. Wengine ni wazawa hasa wa nchi hii na walikuwa hawajapata kusikia juu ya Nabii yeyote yule. Lakini tangu walipomwamini Mtukufu Mtume Muhammad, walianza kumwamini Ibrahimu, Musa, Isa na wengine (amani ya Mungu iwe juu yao). Kama wasingelikuwa Waislamu, wangeendelea kuwadharau Manabii hawa, hata kuwatukana pia. wangeendelea kuwafahamu kuwa walikuwa waongo kama vile Wahindu katika India wanavyoendelea kuamini hivyo mpaka leo. Kadhalika Afghanistan, China na Iran. Wenyeji wa nchi hizi hawakuwa na habari, hivyo hawakumkubali Musa na Isa kuwa Manabii. Ujumbe wa Mtume s.a.w. ukaenea katika

*Wakati kitabu hiki kilipoandikwa.

nchi hizi, na watu wake wakamwamini Mtume s.a.w. na kila alichofundisha. Walianza kuwajua Manabii wengine na kuwaheshimu kama Manabii wa kweli. Hivyo Mtukufu Mtume s.a.w. amewatwika mzigo wa deni Manabii waliomtangulia wote. Ukweli wao ulikuwa haujulikani, Mtukufu Mtume s.a.w. akaujulisha kwa watu. Mtukufu Mtume s.a.w. hana deni la mtu yeyote. Fadhili na baraka za mafundisho yake lazima ziendelee milele. Kwa ajili ya kuhuisha wafuasi wake hana haja ya msaada wa Nabii mwingine. Wakati wowote haja ya namna hii inapotokea, Mwenyezi Mungu atainua mmoja wa wafuasi wake (Mtume s.a.w.) awaongoze wafuasi wengine na kutengeneza kilichoharibika. Huyo atapata kila kitu kutoka kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Atajifunza kila kitu kutoka kwake. Chochote awezacho kufanya, katika kuhuisha na kujenga upya, kitakuwa ni cha Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe. Chochote apatacho mwanafunzi kutoka kwa mwalimu, hakika ni cha mwalimu. Mfuasi hawezi kutengwa mbali na Imam wake, na hivihivi mwanafunzi hawezi kutengwa mbali na mwalimu wake. Mfuasi anayewaongoza wafuasi wenzake atawiwa na Mtukufu Mtume s.a.w. na moyo wake na ubongo wake utakuwa umejaa mapenzi yake.

Kwa ufupi, kuja kwa Nabii wa zamani kwa ajili ya kuhuisha wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. ni matusi kwa Mtukufu Mtume s.a.w.. Tukio kama hili linaweza kudhuru ukuu wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kadhalika litakadhibisha fundisho la Quran Tukufu lisemalo:

> "Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao" (13:12).

Hali ya kuona fundisho hili la Quran, hatuna budi kukubali ama ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. (Mungu apishe mbali), amekuwa hastahiki ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa kubadilika hali yake, au ya kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe amekhalifu ahadi yake. Kwa wengine wote, mwendo wa Mwenyezi Mungu haukuwa kunyang'anya zawadi aliyokwisha itoa; lakini kwa Mtukufu Mtume s.a.w. afanye vingine! Kuingiza fikira kama hii kunafanya ukafiri. Kunafanya ama kumkataa Mwenyezi Mungu au kumkataa Mtume s.a.w. Kwa sababu ya matokeo haya ya hatari tumechoka na itikadi

kama hizi. Tunaamini kwamba Masihi, ambaye kufika kwake kulitabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni wa kutokana na wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu ana hiyari kumpa cheo hiki mtu yeyote.

## Masihi na Mahdi ni Mtu Mmoja.

Katika Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w. inadhihirika pia ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa ilikuwa awe ni mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Hadithi moja inatuambia kuwa

"Mahdi siye ila ni Isa". (*Ibni Majah* - Kitabul Fitan, Baab Shiddatuz -zaman)

Hadithi nyingine inasema

Mtakuwaje atakapowafikieni mwana wa Mariam na kiongozi wenu atakuwa miongoni mwenu?" (*Bukhari,* Kitabul-Anbiya, mlango Nuzuul Isa bin Maryam).

Hadithi hizi mbili zinatoa shaka kabisa kwamba Masihi mwenyewe atakuwa Mahdi. Atawaongoza wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. atatokana miongoni mwao, hatakuwa mtu wa nje. Kufikiri kuwa Masihi na Mahdi ni watu wawili mbalimbali ni kosa. Ni kinyume na Ishara ya wazi iliyomo ndani ya Hadithi: "Mahdi siye ila ni Isa." Inafaa waaminio wema kufikiri kwa makini matamshi ya Bwana wao. Kama matamshi haya yanaonekana yanahitilafiana, ni juu yetu kujaribu kuondoa hitilafu hiyo. Kama Mtukufu Mtume s.a.w. alisema upande mmoja, kwamba Mahdi atadhihiri kabla ya Masihi, na kisha Masihi atajiunga na Mahdi na kumfuata katika ibada; na upande mwingine, kwamba Masihi mwenyewe ndiye Mahdi, tutafanyaje? Je, tukubali tamko moja na kukataa jingine? Au je, siyo wajibu wetu kwamba tufikirie matamshi haya mawili kwa makini sana na kujaribu kupatanisha moja na jingine? Matamshi

mawili haya yanaweza kupatana kama tulitumie moja kulitafsiri jingine. Inaonekana ya kwamba ahadi ya kudhihiri kwa Mahdi ilibebwa ndani ya maneno yaliyodhanisha kwamba Masihi na Mahdi ni watu wawili mbalimbali. Maoni haya yanasahihishwa na Hadithi isemayo kwamba "Mahdi siye ila ni Isa". Hadithi hii inabainisha ya kuwa hiyo Hadithi nyingine ni ya methali. Ina maana kwamba mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. atatokea kwa ajili ya kuuhuisha ulimwengu, lakini hatakuwa na cheo cha Nabii. Halafu ile ahadi ya kufika mara ya pili kwa Nabii Isa itatimia katika nafsi yake na atajitangaza kuwa Masihi Aliyeahidiwa. Kwa hiyo, Hadithi inatuambia ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa ataanzia na kazi ya Mujaddid wa Kiislamu ambaye atakuja pewa kazi ya Masihi. Vyeo viwili vitafuatana kwa mtu huyohuyo mmoja. Bishara za kiungu mara nyingi hutumia methali. Ni mara chache sana zinapotumia vingine.

Kama tafsiri yetu ya Hadithi hizi si sahihi, basi kumebakia njia mbili tu kwa ajili ya atafutaye ukweli: nazo zote ni za upuuzi na za hatari pia. Ama, tukubali ya kuwa ile Hadithi inayoeleza kuwa Masihi na Mahdi ni mtu mmoja siyo Hadithi ya kweli, au, tukubali ya kuwa Masihi na Mahdi ni watu wawili mbalimbali na ya kwamba dhamiri ya Hadithi ni kuashiria hitilafu ya fadhila ya kiroho ya watu wawili hao. Inaweza kuwa na maana ya kwamba Mahdi wa kweli atakuwa Masihi. Maana nyingine, ni kwamba Mahdi atakuwa duni ya Masihi. Itakuwa kama kusema: "Hakuna mwanachuoni ila fulani." Tusemapo hivyo, hatuna maana hasa kwamba hakuna mwingine ajuaye. Bali tuna maana kwamba huyu fulani anajua sana. Kwa vyovyote tafsiri hizi mbili ni za hatari. Moja inatutaka tuifanye kuwa ni ya uwongo Hadithi ya Mtukufu Mtume s.a.w. iliyo ya kweli kwa kila mizani. Nyingine inafahamisha kuwa Mahdi atakuwa si chochote mbele ya Masihi. Fikara hii itakuwa kinyume na Hadithi zinazofundisha ya kuwa Mahdi atakuwa Imam na Masihi atakuwa mfuasi anayesimama nyuma ya Imam katika sala ya jamaa. Hivyo njia zote mbili ni za kipuuzi. Tafsiri zilizo bora ambazo tunaweza kuzitolea Hadithi hizi ni hizi tu ya kuwa zinatabiri kuja kwa Mjumbe tokana miongoni mwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Mjumbe huyu kwanza atadhihiri akiwa Mujaddid na baadaye atajitangaza

kuwa Masihi wa bishara. Mtu huyo huyo atakuwa Mahdi na Masihi pia. Hakutakuwa na tafsiri yenye maana ya Hadithi hizi isipokuwa tafsiri hii.

## Nuzuul Sio Maana Yake Kushuka Kutoka Mbinguni

Sababu ya mgogoro huu ni kwamba kila mtu amepotezwa na neno *nuzuul* lililomo ndani ya Hadithi. Maana yake halisi ni *kushuka.* Kwa hiyo watu wengi wamepotezwa na fikara kwamba kwa vile Masihi imesemwa atashuka ni budi awe yule Masihi wa kwanza. Sasa basi, ni kosa kufikiri ya kwamba neno *nuzuul* siku zote lina maana ya kushuka kutoka juu. Neno *nuzuul* linaashiria tu ni ubora ulioje wa kitu kinachosemwa kuwa kitashuka. Linatuambia kuwa kitu hicho cha kushuka kitakuwa chombo cha utukufu na uwezo wa Mwenyezi Mungu. Vitu kama hivi vinasemwa kuwa huwashukia wanadamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hii maana ya kushuka ni sawa na matumizi ya neno hili ndani ya Quran Tukufu mahala pengi Inasema:

"Kisha Mwenyezi Mungu Akateremsha utulivu Wake juu ya Mtume Wake" (9:26).
"Kisha baada ya huzuni Aliwateremshieni utulivu - usingizi ambao ulifunika kundi moja katika ninyi" (3:155).
"Na Akawateremshieni wanyama wanne kwa jozi" (39:7).
"Hakika Tumekuteremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo; na nguo za utawa ndizo bora. Hayo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu ili wapate kushika mauidha" (7:27).

"Na Tukawateremshieni Manna na Salwa" (2:58).
"Na tukakiteremsha chuma, chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu; na ili Mwenyezi Mungu Ajulishe anayemsaidia Yeye na Mitume wake kwa siri. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Hodari, Mwenye nguvu" (57:26).
"Na kama Mwenyezi Mungu Angetoa riziki nyingi kwa watumishi wake bila shaka wangaliasi ardhini, lakini Huiteremsha kwa kipimo akipendacho. Hakika Yeye kwa watumishi Wake ni Mwenye habari, Mwenye kuona" (42:28).

Kila mtu anajua ya kuwa utulivu ni sifa ya akili ya mwanadamu na usingizi ni kazi ya ubongo wake. Wanyama, nguo, mashamba, salwa, chuma na vitu vingine vinakuwa ardhini au baadhi vinatoka ndani ya ardhi. Havishuki au kudondoka kutoka mbinguni. Wala kushuka kwao kutoka mbinguni sio maelezo yaliyotumiwa na Quran Tukufu. Maelezo ya Quran Tukufu yako wazi kabisa. Inasema:

"Na Akaweka humo milima juu ya uso wake, na Akabarikia humo na Akapima humo chakula chake katika nyakati nne, ni sawa kwa waulizao" (41:11).

Katika aya hii, Mwenyezi Mungu anaashiria kwamba maumbile yote ya kiasili na kuumbwa kwa mali za namna mbalimbali kunahitaji elimu ya namna nyingi ili kufahamike. Elimu hii Mwenyezi Mungu Huifunua sehemu sehemu. Sehemu imekwisha funuliwa, na sehemu itafunuliwa wakati ujao. Kila swali jipya litatolewa na yote yatapata majibu yake. Lakini, anasema Mwenyezi Mungu tumeeleza kuumbwa kwa maumbile ya kiasili na kuumbwa kwa mali ya asili kwa njia ambayo watu wa nyakati zote (sawa na uwezo wao) watapata ndani yake maelezo ya kweli na ya kutosheleza.

Hivyo, kutokana na Quran Tukufu, inadhihirika kwamba vitu vyote vya kiasili hutoka kwa Mwenyezi Mungu - vinatolewa na Mwenyezi Mungu - na tena havidondoki kutoka mbinguni.

Kuumbwa kwao kunafanyika ndani na juu ya hii ardhi. Vinakua juu yake au kuchipuka kutoka chini yake. Hivyo, neno *nuzuul* (kushuka), linapotumiwa kwa kuja kwa Masihi haliwezi kuwa na maana nyingine. Linaweza tu kuashiria ubora, ubarikiwa na adhama ya kiroho ya Masihi Aliyeahidiwa. Hata kidogo halikusudii kueleza kwamba atadondoka kimwili kutoka mbinguni mpaka ardhini. Watu wengi wanasahau kwamba neno *kushuka* limetumiwa ndani ya Quran Tukufu kwa ajili ya Mtukufu Mtume s.a.w. pia. Mufasirina wote wa Kitabu hiki Kitukufu wanachukua tamshi hili kuashiria ukuu na ubora wa kudhihiri kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Na hawakosei; kwani, kama ulimwengu mzima unavyojua, Mtukufu Mtume s.a.w. alizaliwa na wazazi walioheshimika wa Kikuraishi. Jina la baba yake lilikuwa Abdullah na jina na mama yake ni Amina.

Aya inayoeleza kudhihiri kwa Mtukufu Mtume s.a.w. kama *kushuka* ni hii:

> "Hakika Mwenyezi Mungu Amewateremshieni Ukumbusho - Mtume anayewasomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha, ili kuwatoa wale walioamini na watendao mema katika giza kuwapeleka kwenye nuru" (65:11,12).

Sasa inastaajabisha kwamba neno hilihili *nuzuul* limetumiwa kuhusu Mtukufu Mtume s.a.w. na Masihi. Na bado, neno hilihili linatafsiriwa namna moja kwa Mtukufu Mtume s.a.w. na namna nyingine kabisa kwa ajili ya Masihi. Mtukufu Mtume s.a.w. alizaliwa kama mwanadamu mwingine yeyote juu ya ardhi na akakua mpaka kuwa Nabii. Tukio hili lilielezwa kuwa ni *nuzuul* (maana yake halisi ni kushuka). Kwa nini lisiwe na maana ileile wakati neno lilelile linapotumiwa kwa kumhusu Masihi! Kwa nini hata Masihi *asishuke* kwa njia ya kawaida, yaani, azaliwe juu ya ardhi na kukua mpaka kufikia unabii?

## Kwa Nini Masihi Ameitwa Isa Ibn Maryam?

Taabu ya tatu inatokea kuhusu bishara hii ya kufika mara ya pili kwa Masihi. Katika Hadithi, Aliyeahidiwa anaitwa Isa ibn Maryam. Kwa hivi bishara hii inamhusu Masihi wa kwanza hasa, Isa wa zamani. Kama itimizwe, ni budi iwe kwa kufika kwa Isa kimwili. Inasahauliwa ya kuwa methali zinatumiwa katika lugha zote. Jina Isa linatumiwa huria kwa watu wengine wasio Isa wa zamani. Hakuzuki shida yoyote. Lakini kama katika usemi wa Mwenyezi Mungu mtu fulani anapewa jina la Isa, watu wanaanza kushangaa juu ya maana yake. Je, wanasahau ya kuwa mtu aliye mkarimu mno, kwa methali anaitwa Haatim wa Tai, na mtu mwenye hekima sana anaitwa Tusi, na mtu aliye hojaji sana anaitwa Razi? Kwa nini tena kuwe na shida juu ya jina Ibn Maryam? Kama jina Ibn Maryam ni jina la mtu fulani ajulikanaye, je, majina Haatim, Tusi na Razi siyo ya watu wanaojulikana? Kama kwa kuwapa majina haya watu wengine, hakuna anayepotezwa na fikara kwamba watu hao ni walewale. Haatim, Tusi au Razi hasa wa zamani, je, kuna haja mtu yeyote afikiri kwamba Aliyeahidiwa anapoitwa Isa ibn Maryam, ni lazima iwe na maana ya yuleyule Isa mwana wa Maryam aliyedhihiri duniani miaka 1900 iliyopita? Na bado, kuna tofauti kati ya majina Haatim, Tusi na Razi na jina "Mwana wa Maryam." Majina hayo yana maana moja tu, lakini jina Maryam limetumiwa na Quran Tukufu kueleza hali ya kiroho:

"Na tena Mwenyezi Mungu Amepiga mfano wa walioamini kwa mkewe Firauni, aliposema: Ee Mola wangu, Unijengee nyumba Peponi karibu Yako, na Uniokoe na Firauni na matendo yake, na Uniokoe katika watu wadhalimu." (66:12).

"Na (mfano wa) Mariamu binti Imrani aliyejilinda uchi wake, na Tukampulizia humo roho Yetu na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na Vitabu Vyake; na alikuwa miongoni wa wanyenyekevu" (66:13).

Katika maneno haya waaminio wanafananishwa na mke wa Firauni wa Misri aliyemtesa Nabii Musa. Alijitafutia maisha ya Peponi, ukaribu na Mwenyezi Mungu, na akaomba aepushwe na Firauni na matendo yake ya kikatili. Vilevile waaminio wanamithilishwa na Maryam bint Imran. Alijilinda uchi wake na alipokea ufunuo wa Mwenyezi Mungu na kusadikisha ukweli wa mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Vitabu Vyake. Alijithibitisha kuwa mmoja wa watumishi watii sana wa Mwenyezi Mungu. Hapa waaminio wanaelezwa kuwa ni wa namna mbili: Aina iliyo mfano wa mke wa Firauni, na aina iliyo mfano wa Maryam. Ni dhahiri ya kuwa kwa akali aina moja ya waaminio ni ya mfano wa Maryam. Hivyo, kama Aliyeahidiwa anaitwa mwana wa Maryam, inaweza kuwa na maana kuwa huyo Aliyeahidiwa, ataanzia na hali ya mfano wa Maryam, na kwa kukua katika hali hii, atafikia hali ya mfano wa Isa. Inaweza kuwa na maana ya kuwa maisha ya awali ya Aliyeahidiwa yatakuwa matakatifu na yasiyo na ila kama vile Maryam alivyokuwa mtakatifu na asiye na ila, halafu maisha yake ya baadaye yawe sawa na ya Isa. Isa alipata msaada kwa Roho Takatifu, hivi ndivyo atakavyokuwa huyo Aliyeahidiwa. Maisha yake yote yatapita katika kuthibitisha ukweli na kuleta islahi duniani.

Inasikitisha ya kuwa Maulamaa wa wakati wetu hawafikiri kwa makini sana maneno ya Quran Tukufu. Wamejipigia marufuku kuzamia maana yake. Ndiyo sababu, wanakosa ule uzuri na fadhila iliyo chini ya uso wa Maneno Matakatifu. Lakini kama Masheikh wetu wangesoma maandishi ya Masufi wa zamani wa Kiislamu, (maandishi yenye msingi wa Quran Tukufu na Sunna za Manabii wa zamani), wangeliona ukweli. Sheikh Shahaab-ud-Din Suhrawardi, kutaja mfano mmoja wa walii wa Kiislamu aliyeandika yanayohusiana na madhumuni hii, anasema katika kitabu chake *'Awarif-ul-Ma'aarif* ya kuwa uzazi ni wa namna mbili: Uzazi wa kimwili na wa methali. Akisaidia maelezo haya walii mkubwa huyu anaendelea kumtaja sio mtu mwingine bali Isa mwenyewe. Sheikh

anaandika:-

> "Murid ni sehemu ya Sheikh, kama vile katika uzazi wa kimwili, mtoto ni sehemu ya baba. Murid anazaliwa kimethali katika maana aliyoieleza Isa aliposema kuwa hakuna mtu atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni mpaka azaliwe mara ya pili. Uzazi wa kwanza unamfungamanisha mtu na dunia hii, na uzazi wa pili unamfungamanisha na ulimwengu wa kiroho. Fundisho hili limo katika Quran pia:

> "Na hivyo, Tukamwonesha Ibrahimu ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini" (6:76).

Hivyo, kwa maoni ya Sheikh Shahaab Suhrawardi, kila mwanadamu anapata uzazi wa kiroho. Kwa kusaidia maoni haya anataja aya ya Quran Tukufu na maneno ya Nabii Isa aliyeonelea kwamba uzazi wa kiroho ni wa lazima kwa ajili ya maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Kwa nini uzazi huu wa kiroho usiwezekane au uwe shida kwa Masihi Aliyeahidiwa ambaye ndiye mfano wa Nabii Isa?

Basi kwa ufupi? fikara kwamba Masihi wa kwanza afufuke, na kudhihiri leo kuwaongoza wanadamu, ni kinyume na Ukuu wa Fundisho la Mwenyezi Mungu; na ni kinyume pia na daraja ya juu sana ya Mtukufu Mtume s.a.w. Fikara hii si safi, bali ni matokeo ya kutokufikiri kwa mapana. Ukweli ni kwamba kuja kwa mara ya pili kwa Masihi ilikuwa kufanyike kwa njia ya mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Mfuasi huyu ilikuwa adhihiri katika roho na tabia ya Masihi wa kwanza. Imani yetu ni kwamba Masihi wa pili amekwisha kuja. Mafundisho yake yamewaongoza watu wengi. Wengi waliomtoka Mwenyezi Mungu, wamemwona tena.

## Wahyi na Unabii Unaendelea

Upinzani wa nne mkubwa ulioletwa juu yetu ni kwamba tunaamini ya kuwa desturi ya kushuka kwa wahyi na kufika kwa manabii inaendelea baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Upinzani huu vilevile unatokea kwa sababu ya kutofikiri sana, au kwa sababu ya chuki na kujipendelea. Ukweli ni kwamba sisi hatujali sana maneno kama tunavyojali maana yake. Tunapendelea kuamini chochote kinachosaidia kumtukuza Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hata kidogo hatuwezi kuamini kuja kwa mtu ambaye kuja kwake kunafuta silsila ya Mtukufu Mtume s.a.w., ambaye ataupa ulimwengu Kalima mpya na Kibla kipya na kuupa sheria mpya ya dini au kubadilisha sehemu yoyote ya sheria ya Quran Tukufu; au ambaye atawakataza watu kumtii Mtume s.a.w. na kuwataka wamtii yeye badala ya Mtukufu Mtume s.a.w. au ambaye atapata hata sehemu ndogo sana ya cheo chake cha kiroho bila kukiwiacho kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Kwa maoni yetu kuja kwa mtu kama huyu kutakuwa ndio mwisho wa Uislamu. Itakuwa na maana kwamba zile ahadi ambazo Mwenyezi Mungu alimfanyia Mtukufu Mtume s.a.w. ni za uongo. Jambo kama hili haliwezekani na tunachukia hata kulifikiria. Hapohapo tunafikiri ni kosa kuamini ya kwamba kwa kufika Mtukufu Mtume s.a.w., fadhili zote na baraka ambazo hapo kabla wanadamu walikuwa wakizipokea, zimekoma. Hatufikiri ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alikuja kufunga milango maarufu ya maendeleo ya kiroho. Bali tunafikiri kwamba kufika kwa Mtume s.a.w. kumeleta na kupanua njia za maendeleo ya kiroho. Hatufikiri ya kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. alikuja kuwazuia watu kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu. Kama tunavyochukia kufikiri kwamba Nabii yeyote anaweza kumkiuka Mtume s.a.w., tunachukia vilevile kufikiri ya kuwa kufika kwa Mtukufu Mtume s.a.w. ndio mwisho wa wahyi na baraka zinazoletwa na ufunuo. Itikadi zote mbili ni fedheha kwa Mtukufu Mtume s.a.w. na zinaharibu mafundisho yake. Hatukubali moja wala nyingine. Tuna hakika ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa ni baraka kwa ajili ya wanadamu. Tunajua ya kuwa baraka na fadhili za Mtukufu Mtume s.a.w. zinaendelea. Kuja kwake hakukuzuia kamwe wanadamu

kujipatia manufaa ya kiroho. Badala ya hivyo, manufaa ya kiroho na fadhili ambazo Mwenyezi Mungu amepata kuwajaalia wanadamu, zimeanza kutiririka kwa wingi zaidi kuliko hapo zamani. Ikiwa hapo kabla zilikuwa kijito, sasa zimekuwa jito kubwa kabisa. Kabla ya Mtukufu Mtume s.a.w. elimu ya mambo ya kiroho haikuwa imeendelea mbali sana. Lakini kwa kufika Mtukufu Mtume s.a.w. elimu hii imefikia ukamilifu, na ni elimu ya kiroho tu ndiyo iwezayo kuleta hekima ya kiroho.

Quran Tukufu inafundisha yasiyopata kufundishwa na Kitabu cha Kimbinguni chochote. Hivyo, Mtukufu Mtume s.a.w. alizawadiwa elimu ya ndani sana ya kiroho kuliko aliyopata kujaaliwa mwingine yeyote kabla yake. Mwongezeko wa elimu ya kiroho unawawezesha waaminio leo kufikia daraja za kiroho ambazo hazikuweza kufikiwa zamani. Isipokuwa kwa baraka hizi, ni fadhila gani anayoweza kuwa nayo Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya Manabii wengine? *Kufikia unabii bila kumtegemea Mtukufu Mtume s.a.w. hakuwezekani sasa.* Ndiyo sababu tunakataa kuwa Masihi wa Nazareti hawezi kurudi kuja kuwaongoza wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kuja kwake kutakuwa bila ulezi wa kiroho wa Mtukufu Mtume s.a.w. Lakini hatukani ule unabii unaopatikana kwa kumfuata Mtukufu Mtume s.a.w. ambao ni wa kumtukuza.

Mwenyezi Mungu aung'arishe moyo wako, msomaji, na akupanulie akili yako. Nabii anayempita nabii aliyemtangulia ni yule anayeleta sheria mpya na ambaye anafikia cheo chake bila ufuasi wa nabii aliyemtangulia. Lakini nabii anayefikia cheo chake kwa kumtegemea nabii aliyemtangulia kwa njia ya fadhili na mvuto wa mfano na mafundisho yake, na kwa njia ya kumtii, nabii huyu hampiti na wala hawezi kumpita nabii aliyemtangulia. Mbali na kumshusha, unabii huu unamtukuza nabii aliyemtangulia, kadhalika mafundisho yake na mfano wake. Katika Quran Tukufu inadhihirika ya kuwa njia ya kufikia unabii wa namna hii iko wazi kwa ajili ya wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Akili ya kawaida tu pia inakubali wazo hili. Maana kama wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. hawawezi kufikia unabii kama huu, hawawezi kuwa na fadhila juu ya wafuasi wa Manabii wengine.

Mtukufu Mtume s.a.w. alisema ya kuwa miongoni mwa wafuasi

wa Nabii Musa kulikuwako watu wengi waliofikia daraja ya *Muhaddath,* cheo cha kiroho chini ya unabii. Kwa hiyo kama mfano wa kiroho na mvuto wa Mtukufu Mtume s.a.w. hauwezi kuwapandisha watu kwenye daraja ya juu zaidi kuliko *Muhaddath,* basi Mtukufu Mtume s.a.w. hawezi kuwa na fadhili juu ya manabii wengine, licha ya kuwa ni "Mbora wa watu" na "Mbora wa Manabii." Kuwa "Mbora wa Manabii", ni lazima kwa Mtukufu Mtume s.a.w. awe na sifa wasizokuwa nazo manabii wa zamani. Kwa maoni yetu, sifa hii ya pekee ni kwamba wafuasi wa manabii wa zamani walifikia, sana sana, daraja ya *Muhaddath.* Nguvu ya kiroho ya manabii wa zamani haikupata zaidi ya hapo. Lakini wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. wanaweza kufikia daraja ya manabii, na hii ni kwa sababu ya ubora wa mvuto wa mfano wa kiroho na mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. Kwa sababu ya itikadi hii, mwumini anajawa na mapenzi ya Mtukufu Mtume s.a.w. moyoni mwake na anajitolea kwa ajili yake. Kama kufika kwa Mtukufu Mtume s.a.w. kumekomesha kufikiwa kwa unabii wa namna hii, basi kufika kwake ni budi kuhesabiwe kama siyo baraka bali mkosi. Quran Tukufu itabidi itupiliwe mbali kama kitabu kisicho na maana. Kwani, kama wafuasi wa Mtume huyu na Kitabu hiki hawawezi kufikia daraja ya manabii, hatuna budi tukubali ya kuwa kabla ya kufika kwake iliwezekana waaminio kufikia kituo hiki cha kiroho, lakini imekuwa haiwezekani baada ya kufika kwake. Vitabu vilivyofunuliwa kabla ya kudhihiri Mtume s.a.w. vilikuwa na nguvu ya kuwainua wasomaji na wafuasi wake kwenye daraja ya manabii, (yaani kuwawezesha kufikia ile hatua ya baraka ya kimbinguni ambayo nyuma yake wanapata unabii); lakini Quran Tukufu haina nguvu hii! Ikiwa hii ni kweli hasa, mioyo ya waaminio wa kweli itaanza kutoka damu na roho zao kupooza. Kuja kwa Mtukufu Mtume s.a.w., "Rehema kwa ajili ya wanadamu" aliyekuwa, "Mkuu wa Manabii", ilikuwa kufungue njia mpya za maendeleo ya kiroho; kwa kumfuata yeye watu ilikuwa wasogee karibu sana na Mola wao kuliko hapo zamani. Lakini, badala yake, hata milango iliyokuwa wazi zamani sasa ifungwe kwa sababu yake. Hakuna mwumini wa kweli anayeweza kuingiza wazo hili hata kwa dakika moja juu ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hakuna mpenzi

wa Mtukufu Mtume s.a.w. anayeweza kuamini hivi walau kwa nukta moja. Wallahi, Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa ni bahari ya baraka za kiroho. Yeye alikuwa ni mbingu ya kiroho ambayo hakuna mwanadamu anayeweza kuupima upana wake. Milango ya baraka za kiroho na maendeleo ya kiroho haikufungwa naye. Bali imefunguliwa zaidi kwa sababu yake. Ndiyo tofauti baina yake na Manabii wa zamani. Wafuasi wa manabii wa zamani waliweza kufikia cheo cha *Muhaddath* (uwalii). Ili kufikia cheo cha *Nubuwwat* (unabii), ilibidi wapate mafunzo zaidi. Ni tofauti na wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kumtii na kuiga mfano wake kunaweza kumpandisha mtu kwenye cheo cha unabii; hata anapokuwa nabii, mfuasi anabakia kuwa mfuasi. Kiwe juu vilioje cheo chake, hawezi kuenda nje ya duara. Anabakia kuwa mtumwa na mtumishi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Anaweza kufikia daraja ya juu lakini urefu wa daraja yake hauwezi kubadilisha sifa yake ya kuwa mfuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kwani, kwa kweli, kila kilivyo cha juu zaidi cheo chake, ndivyo anavyowiwa zaidi na Mtukufu Mtume s.a.w. Kuhusu ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu Mtume s.a.w. alifikia mahala ambapo hapajafikiwa na mwanadamu yeyote. Amefikia daraja ambayo wengine hawawezi kufikiri kuifikia. Wakati huo huo, ukuu wa daraja yake unaendelea kuongezeka upesi zaidi kuliko fikara ya mwanadamu. Lakini, anavyoendelea Mtukufu Mtume s.a.w., ndivyo walivyo wafuasi wake. Mtukufu Mtume s.a.w. anaposogea hatua fulani mbele, huku nyuma yake wafuasi wake wanafanya kadhalika.

Hili wazo la cheo cha Mtukufu Mtume s.a.w. lina maana kwamba zawadi ya unabii iwe wazi kwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kama zawadi hii iwazi kwa wafuasi, itaongezea utukufu na ukuu wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kama zawadi hii ipigwe marufuku, ni upungufu na kushindwa kwake. Nani asiyejua ya kuwa mwalimu hodari ambaye uhodari wake unatakiwa kuthibitishwa, ni lazima awe na mwanafunzi hodari. Mfalme mkuu ni lazima awe na wafalme wengine chini yake. Kama mwalimu hatoi wanafunzi hodari, hawezi mwenyewe kuitwa hodari sana. Mfalme mkuu ambaye hana wafalme chini yake, hawezi kuwa mkuu sana. Mfalme mkuu ni mfalme wa wafalme. Kuwa mfalme wa wafalme ni heshima kubwa zaidi kuliko

kuwa mfalme wa watu raia tu. Hivi hivi, nabii ambaye wafuasi wake wanaweza kuwa manabii, ni nabii mkuu mno kuliko manabii ambao wafuasi wao wanabakia wafuasi, lakini hawawezi kuwa manabii.

Ni suala la maana sana kujua ni kwa vipi wazo la kosa sana juu ya unabii limeenea miongoni mwa Waislamu wa leo. Ninasema 'Waislamu wa leo' kwa sababu Maulamaa wa mwanzo wa Dini hii wana maoni kinyume kabisa na wazo linalokubaliwa na Waislamu wa leo. Mawalii wa wanazuoni kama Muhyi Din Ibn Arabi, Mulla Ali Qari, Ibn Qayyim, Maulana Rumi, Hadhrat Sheikh Ahmad wa Sarhand, wanaweza kutajwa miongoni mwa Maulamaa wakubwa wa Dini ya Islam ambao wameeleza juu ya madhumuni hii maoni kinyume na maoni yanayoshikwa na Waislamu wa leo. Wazo hili la kosa lilitokea kwa sababu Waislamu walianza kulitafsiri neno *Nubuwwat* vibaya. Kwa namna fulani walianza kufikiri ya kuwa nabii ni lazima awe mletaji wa sheria pia. Ni lazima, ama alete sheria mpya. au lazima atengue sehemu za sheria ya zamani. Ukweli ni kwamba sharti hizi si za lazima kwa mtu kuwa nabii. Nabii anaweza kutimiza sharti hizi au la. Mtu anaweza asitimize yoyote ya sharti hizi na bado awe nabii. Anaweza asilete sheria mpya, anaweza asitengue sehemu yoyote ya sheria ya zamani, au anaweza awe na lazima ya kumfuata nabii wa zamani. Bado mtu huyu anaweza kuwa nabii. Kwani, unabii ni hali ya kiroho, daraja ya ukaribu na Mwenyezi Mungu. Mtu anayefikia hali hii, anayefikia daraja hii ya ukaribu, anateuliwa kuwaongoza wanadamu kwa Mwenyezi Mungu. Anapewa kazi ya kuhuisha wafu wa kiroho na kuloanisha mioyo iliyokauka kwa kiu ya kiroho. Ni wajibu wake kuwaambia wanadamu ufunuo aliopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu, awakusanye pamoja wale wanaomwamini yeye na ufunuo wake, na kuwafanyia jumuiya iliyo tayari kujitolea maisha yao kwa ajili ya kutangaza ukweli. Mfano wake uwe na athari ya kutakasa mioyo ya watu na kuinua sifa na hali ya matendo yao ya kila siku.

Kwa ufupi, watu wameanza kukataa au kutilia shaka kuendelea kwa zawadi ya unabii, kwa sababu wameshindwa kuelewa maana ya hali hii ya kiroho. Hali zingine za unabii ni za namna ambayo kuendelea kwake miongoni mwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. kunapandisha zaidi cheo chake badala ya kukishusha.

## Maana ya Khaatamannabiyyin

Inasemwa ya kuwa Quran Tukufu inafundisha kutokuendelea kufika kwa manabii wa namna zote, kwa sababu inasema

"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Khaatamannabiyyin" (33:41).

Katika tafsiri ya aya hii tumelinakili vilevile neno *Khaatamannabiyyin*, kwa sababu ndani yake ndimo imo maana ya aya yenyewe. Inahojiwa hapa ya kwamba, kwa mujibu wa Quran Tukufu, sasa hakuwezi kuwa na manabii hata kutoka miongoni mwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Lakini wengi wanaonekana wamesahau kuwa katika tamko la kiungu hili, neno *khaatam* limetumiwa na Mwenyezi Mungu kwa fat'ha juu ya 'te' sio kwa kasra. *Khaatam* maana yake ni muhuri. *Khaatim* ingekuwa na maana ya "mtu wa mwisho" au "wa mwisho." Sasa basi, muhuri una kazi ya kuthibitisha. Kwa hiyo aya hii itakuwa na maana kwamba Muhammad, Mtukufu Mtume s.a.w., ni "Muhuri wa Manabii." Katika kueleza aya hii Imam Bukhari ametaja Hadith zinazosema juu ya athari fulani kwenye mwili mtakatifu wa Mtukufu Mtume s.a.w. ambayo imeitwa na muhaddithina kuwa ni muhuri wa utume.

Lo! watu hawafikiri sana juu ya Kitabu Kitakatifu hivyo wanakosa maana yake ya kweli. Laiti kwanza wangefikiria umbile la maneno, halafu aya na maneno, wasingeikosa maana ya aya hii. Kwani pasipo kufahamu umbile la maneno, hakuna anayeweza kuelewa maana ya aya. Sasa, umbile lenyewe la maneno linaanza kwa kusema kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. si baba wa mwanamume yeyote; yaani, hana mwana wa kimwili. Halafu aya inaendelea kusema kwamba ijapokuwa Mtukufu Mtume s.a.w. hana mtoto wa kiume, lakini ni nabii; na si nabii tu bali yu Muhuri wa Manabii wote. Idhihirike ya kuwa linalosemwa katika sehemu ya pili ya aya hii limo katika kudhoofisha lile linalokubaliwa mwanzo. Sehemu ya kwanza inakubali kushindwa kwa dhahiri, na sehemu

ya pili inasema jambo linalodhoofisha kushindwa huko. Kwa vyovyote, Waislamu wanaosoma Kitabu Kitakatifu wanajua ya kuwa kukubali ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. hakuwa na mtoto wa kiume ni kupinga linalosemwa katika aya nyingine maarufu sana ya Quran Tukufu:

"Hakika adui yako atakuwa mkiwa" (108:4).

Kukubali kunakopinga tamko la mbele kunalazimu ufafanuzi. Aya moja (yaani aya 4, Sura 108) inamtaja adui wa Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa bila mtoto, nyingine (yaani aya 41, Sura 33) inamtaja Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa hana mwana. Kwa kuondoa upinzani huu, Mwenyezi Mungu anatoa dai la maana kwa niaba ya Mtukufu Mtume s.a.w. katika aya 41, Sura 33. Dai hili ni kuondoa shaka au shida ambayo kukubali kwa upinzani huu kunaweza kuileta kwa urahisi. Dai lenyewe ni hili: Naam, Mtukufu Mtume hana mwana wa kimwili. Lakini hii siyo fedheha. Haina maana ya kwamba hana hasa kizazi. Kwa nini? Kwa sababu ni Nabii wa Mwenyezi Mungu. Kama Nabii wa Mwenyezi Mungu, atakuwa na wafuasi wake; dhuria wake wa kiroho watafidia utovu wowote wa dhuria wa kimwili. Bali yu zaidi kuliko nabii. Yu Muhuri wa Manabii. Maneno *Muhuri wa Manabii* yanaeleza jambo fulani zaidi. Yanaeleza ya kuwa siyo tu kwamba Mtume huyu atakuwa na wafuasi na waaminio wa taratibu ya kawaida. Kama Muhuri wa Manabii, atakuwa na nguvu zaidi kuwanyanyua wengine kwenye cheo cha kiroho cha unabii. Atakuwa baba siyo wa waaminio wa kawaida tu, bali hata wa manabii. Katika aya iliyotajwa dhidi ya kuendelea unabii, kwa hakika tuna uthibitisho wa kuendelea unabii; kuendelea kwa desturi ya unabii uliokwisha tajwa na kufafanuliwa tayari, unabii usio wa kuleta sheria mpya, au kujitenga na sheria ya zamani. Kuendelea kwa unabii wa sheria mpya, au hata kutengua sehemu ya sheria ya zamani, au wa kujitegemea, ni kosa kwa ubaba wa kiroho wa Mtukufu Mtume s.a.w. Unabii wa namna hii tu ndiwo unaokataliwa katika aya ya 41, Sura 33.

## "Mimi ni Mwisho wa Manabii na Msitiki Wangu ni Mwisho wa Misikiti"

Vilevile inasemwa kwamba Hadithi fulani za Mtukufu Mtume s.a.w. zinapinga itikadi ya kuendelea unabii. Mathalan alisema: "Mimi ni mwisho wa manabii," na tena "hapana nabii baada yangu." Inafuata ya kwamba kwa hadithi hizi, hakuwezi kuwa nabii wa namna yoyote baada ya Mtukufu Mtume s.a.w.! Inasikitisha ya kwamba hao wanaotaja Hadithi hizi za Mtukufu Mtume s.a.w., wanasahau ya kuwa maneno "Mimi ni mwisho wa manabii" yanafuatwa na maneno ya maana sana "na msikiti wangu ni mwisho wa misikiti" (*Muslim* jalada la kwanza). Kwa hiyo kama Mtukufu Mtume ni mwisho wa manabii hasa, basi msikiti alioujenga Madina ni mwisho wa misikiti hasa. Itakuwa kosa kujenga msikiti wowote baada ya msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. wa Madina. Lakini hakuna anayeona upinzani katika maana iliyowekwa juu ya sehemu ya kwanza ya Hadithi hii na maana iliyowekwa juu ya sehemu ya pili ya Hadithi hii hii. Sehemu ya kwanza inasemwa ina maana ya kukomesha unabii wa kila aina baada ya kufika Mtume s.a.w. Lakini sehemu ya pili haisemwi kama hivi kuwa na maana ya kukomesha ujenzi wa misikiti. Watu haohao wanaosadiki kukoma kwa unabii, hawaoni ubaya wowote kwa kujenga misikiti zaidi. Kwa kweli ari yao ya kujenga misikiti imepita kiasi. Kuna miji yenye misikiti zaidi kuliko inayohitajiwa hasa; hivyo mingi inabaki mitupu. Katika miji mingi misikiti inapatikana hatua chache mmoja baada ya mwingine, hivi kwamba wingi wao uko dhahiri. Kama maneno "mwisho wa manabii" yanaleta maana ya kukomeshwa kwa unabii, basi maneno, "Mwisho wa misikiti" ni lazima yalete maana ya kukomeshwa kujengwa kwa misikiti baada ya msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w.

Ili kuwa na hakika, kunajaribiwa kutafutwa vitatuzi vya taabu hii. Inasemwa ya kuwa misikiti inayojengwa na Waislamu baada ya wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. ni misikiti inayojitolea kwa ajili ya ibada iliyofundishwa na Mtume s.a.w. Inajengwa kwa makusudio yaleyale ambayo kwayo Mtukufu Mtume s.a.w. alijenga msikiti wa kwanza. Kwa hiyo, misikiti inayojengwa na Waislamu ni misikiti ya Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe. Haiwezi kutengwa

mbali na mfano inayouiga. Misikiti haiwezi na haipingi umwisho wa msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. Tatuzi hili ni la kufaa sana. Lakini vilevile inafaa kusema kwamba maneno "nabii wa mwisho" hayakatazi kufika kwa manabii wanaoiga maisha ya mfano wa mtukufu Mtume s.a.w., ambao hawafundishi chochote kipya, ambao wanamfuata yeye tu na mafundisho yake; ambao wanapewa kazi ya kueneza mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w., ambao wananasibisha neema za kiroho walizopata pamoja na unabii kwa mfano wa kiroho wa mvuto wa mwalimu wao na bwana wao, Mtukufu Mtume s.a.w. Kuja kwa manabii hawa hakuendi kinyume dhidi ya haki ya Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa "nabii wa mwisho"; kwa njia ileile na kwa sababu ileile ambayo kwayo kujengwa kwa misikiti leo hakuendi dhidi ya daraja ya msikiti wa Mtume s.a.w. kuwa "Msikiti wa Mwisho".

Sasa, hebu tuirudie Hadithi ile isemayo "hapana nabii baada yangu." Hadithi hii haiwezi kuwa na maana hasa kwamba hakuwezi kuwa nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hadithi hii vilevile ina maana hii tu: Kwamba hakuna nabii anayeweza kuja sasa ambaye atatengua mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hadithi hii ya Mtume s.a.w. inaelekea kwenye neno *baada*. Jambo fulani linakuja *baada* ya jingine hapo tu jambo la kwanza linapokwisha na la pili linashika mahala pake. Nabii anayefika kwa ajili ya kutangaza, na kwa kila njia, kusaidia na kukuza unabii wa Mtukufu Mtume s.a.w., hawezi kusemwa amefika *baada* ya Mtukufu Mtume s.a.w. Unabii wa Mtukufu Mtume s.a.w. utakuwa palepale. Nabii anayekuja kuutumikia unabii huu ni sehemu ya silsila ya Mtukufu Mtume s.a.w. Nabii angeweza kusemwa amefika *baada* ya Mtukufu Mtume s.a.w., kama angeleta kutenguliwa kwa sehemu yoyote ya mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mtu mwenye busara hujaribu kufikiria kwa makini kila madhumuni yenye maana na kupata undani wa maana ya hilo kila neno lililomo ndani yake. Si la ajabu, Bibi Aisha r.a., mke wa Mtukufu Mtume s.a.w., akihofia Waislamu watakaofika baadaye wasije wakaikosa maana ya Hadithi ya Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya unabii aliwaonya watu akisema:

"Semeni yeye (Mtume s.a.w) ni Khaatamannabiyyin wala msiseme hakuna nabii baada yake" (Takmila Majma'-ul-Bihaar, uk. 85).

Kama katika maoni ya Bibi Aisha, kama katika ujuzi wake, kuja kwa manabii kulikwisha hasa kwa nini aliwaonya watu dhidi ya kusema kuwa hakuna nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w.? Kama alipotoa onyo hili, alikosea, na aliyosema yalikuwa kinyume cha mafundisho ya Mtukufu s.a.w., kwa nini Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. hawakumpinga? Onyo lake dhidi ya Hadithi "hapana nabii baada yangu" linaonesha waziwazi ya kuwa kwa maoni yake, kuja kwa nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. kunawezekana. Ila tu, nabii kama huyo hawezi kuwa mletaji wa sheria, au nabii asiyemtegemea Mtukufu Mtume s.a.w. Kule kupokea kwa Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. onyo hili la bibi Aisha bila ya hoja au kupinga, kunaonesha kwamba Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. walifahamu aliyoyasema na kuamini aliyoamini.

## Quran Inafundisha nini Juu ya Unabii?

Ole wao wale wasiofikiria kwa makini maneno ya Kitabu Kitakatifu: Hali wamepotea, wanatafuta kuwapoteza wengine. Ole wao wale wanaotughadhibikia sisi tunaokataa kupotezwa. Wanatuita sisi *makafiri.* Lakini aaminiye haogopi vitisho vya watu wengine. Anamwogopa Mwenyezi Mungu tu. Ni dhara gani anayoweza mtu mmoja kumtia mwingine? Sana sana, kuua? Lakini mwenye imani haogopi kuuawa. Kwa ajili yake, kifo kinamfungulia mlango wa kumwona Mwenyezi Mungu. Laiti mahasidi wetu wangejua Quran Tukufu ni hazina iliyoje. Ni hazina isiyoweza kumalizwa; ni ya kukidhi haja za wanadamu nyakati zote. Ina mafundisho juu ya maendeleo ya kiroho ya wanadamu ambayo vitabu vingine havina hata sehemu yake ndogo. Laiti watu wangelikuwa na habari yoyote juu ya thamani ya Quran Tukufu, wasingelitosheka na elimu ndogo waliyookota. Wangelizama chini sana ya maana na kutafuta njia za kumridhisha Mwenyezi Mungu zaidi na zaidi, na kupata ukaribu naye. Laiti wangelijua thamani ya usafi wa moyo dhidi ya kufuata

kwa dhahiri, laiti wangelijali zaidi roho na siyo tu kujali maandishi ya mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w., wangelijaribu kujua njia wanazokaribishwa na Quran Tukufu kwa ajili ya maendeleo yao ya kiroho. Laiti wangelifanya hivi, wangeligundua kwamba wanajali zaidi ganda kuliko kiini, kwamba wanatumaini kufaidi kinywaji kwa kuweka midomoni mwao vikombe vitupu. Je, hawasomi Surat Faatiha, sura ya kwanza ya Quran Tukufu? Je, dua iliyomo ndani ya sura hii haiwafundishi waaminio kumwomba Mwenyezi Mungu neema za kiroho? Je, hawatamki karibu mara hamsini kila siku dua hii "Utuongoze njia ya wale Uliowaneemesha?" Kama wanafanya hivi, je, wanafikiria kwa makini maana ya *neema* wanazoomba waaminio katika Surat Faatifa katika Sala zao kila siku? Laiti wangeliomba kwa jicho lionalo sana maana ya dua hii, walau mara moja, wangelijiuliza tena na tena: "Ni ipi hii njia iliyonyoka? Ni zipi hizi neema zinazoletwa na kufuata njia iliyonyoka?" Na laiti wangeuliza haya, jawabu lao wangelilipata katika aya ya maana sana ya sura ya 4 isemayo:

"Na kama wangalifanya waliyoagizwa ingalikuwa bora kwao na inayoimarisha zaidi. Na ndipo Tungewapa malipo makubwa kutoka Kwetu. Na hakika Tungewaongoza njia iliyonyooka. Na Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao ni miongoni mwa wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu -- Manabii na Masidiki na Mashahidi na Masalih; na hao ndio marafiki wema. Hiyo ni fadhili itokayo kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mjuzi" (Sura 4:67-71).

Kutokana na aya hizi inadhihirika ya kuwa mwumini anapoomba

njia ya wale waliozawadiwa baraka za Mwenyezi Mungu, anaomba awe pamoja na manabii, masidiki, mashahidi na masalih. Kwa hiyo, kama alivyotufundisha Mwenyezi Mungu dua hii kwa njia ya Mtume Wake, dua tunayoikariri mara hamsini kila siku, na kama ilivyokwisha elezwa na Mungu Mwenyewe hiyo njia iliyonyoka tunayoiomba kuwa ni njia ambayo mwisho wake waaminio wanajikuta pamoja na manabii, masidiki, mashahidi na masalih, nani anayeweza kusema na inawezekanaje ya kwamba kwa ajili ya wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w., mlango wa kila aina za unabii uwe umefungwa? Je, wazo kama hili haliwi la kipumbavu? Je, Mwenyezi Mungu anaweza kufundisha chochote cha kipumbavu? Je, inawezekana upande mmoja atutake sisi tuombe kuwa miongoni mwa manabii, masidiki, mashahidi na masalih, na upande mwingine atuambie kuwa neema ya unabii imepigwa marufuku kwa ajili ya wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w., tena marufuku ya milele. Mwenyezi Mungu apishe mbali matokeo haya. Mwenyezi Mungu ni Mtakatifu na Msafi, ameepukana na kila udhaifu na upungufu. Kama kwa sababu fulani, amepiga kweli marufuku neema ya "unabii," basi hangetufundisha sisi kuomba njia inayoongoza kwa wale walioneemeshwa na Mwenyezi Mungu. Wala asingetangaza wazi namna hii kwamba kumtii Mtukufu Mtume s.a.w. kunamfanya mfuasi awe mwenye kubarikiwa, na kubarikiwa kwa juu kabisa ni kuwa nabii.

Inasemwa ya kuwa aya yenye mgogoro huu ina neno *Ma'a* (pamoja) na sio *Min* (miongoni mwa au mmoja wa). Kwa hiyo inasemwa, dua hii inatoa uwezekano wa waaminio kujiunga na jamii ya manabii, uwezekano wa kuwa *pamoja* nao; sio mmoja wao. Lakini wale wanaosema hivi, wanasahau kwamba aya hii haisemi juu ya manabii tu. Inasema pia juu ya masidiki, mashahidi na masalih. Kama *ma'a* katika aya hii ina maana kwamba mwumini amezuiwa kufikia cheo cha nabii, basi ni lazima tukubali ya kuwa atazuiwa kufikia cheo cha masidiki au mashahidi au masalih. Sio kukoma kwa manabii tu bali lazima tukubali kukoma kwa wabarikiwa wa daraja za chini vilevile. Anayeomba kuchanganywa na walioneemeshwa atosheke na kujiunga na jamii yao tu. Hawezi kuwa mmoja wao. Mwumini anaweza kujiunga na jamii ya masidiki,

lakini asiwe mmoja wa masidiki. Anaweza kuingia jamii ya mashahidi lakini asiwe shahidi. Anaweza kuingia jamii ya masalih, lakini asiwe mmoja wa masalih. Ina maana kwamba neema zote za kiroho na vyeo vimepigwa marufuku kwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kwa kukubaliwa dua yao, sana, wanaweza kutazamia kuingia jamii moja ya kiroho au nyingine. Hawawezi kutazamia kupata cheo sawa na wengine katika yoyote ya jamii hizo. Kila jamii iwe ya wafuasi wa manabii wa zamani. Wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. watamani tu kuungana nao kama watazamaji, sio sawa nao. Hakuna Mwislamu wa kweli anayeweza kuingiza fikara hii. Fikara kama hii inashusha hadhi ya dini ya Islam, Quran Tukufu na Mtukufu Mtume s.a.w. Inaleta maana kwamba wafuasi wa Mtume s.a.w. hawawezi kutumainia hata kupata cheo cha waaminio wema. Wanaweza kutumaini kupata haki ya kuwa pamoja nao. Kwa hiyo neno *ma'a* au *pamoja* haliwezi kuchukuliwa katika maana yake ya nje. Katika maana hii, aya haileti maana yoyote. Inaweza tu kusaidia nia ya Maulamaa kwa kupiga marufuku zawadi ya unabii kwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Lakini kama *ma'a* itafsiriwe hivi, sio unabii tu utakaopigwa marufuku, bali vilevile usidiki, ushahidi na usalih.

Kwa vyovyote, ukweli ni kwamba neno *ma'a* (pamoja) halitumiwi kwa maana ya kutokea kwa wakati mmoja au mahala pamoja tu. Halina maana kwamba vitu viwili au watu wawili wanaonekana pamoja. Bali vilevile mara nyingi lina maana ya usawa wa daraja. Tunao mfano wake katika katika Quran Tukufu:

> "Bila shaka wanafiki wako katika daraja ya chini ya Moto, wala hutakuta kwa ajili yao msaidizi yeyote. Isipokuwa wale wanaotubu na kujisahihisha na kumshika Mwenyezi Mungu, na kuuhalisisha utii wao kwa Mwenyezi Mungu, basi hao wako pamoja na

waaminio. Na Mwenyezi Mungu karibuni Atawapa waaminio ujira mkuu" (4:146-147).

Katika aya hizi wale wanaotubu na wakajitupa kwa Mwenyezi Mungu, wameelezwa kuwa ndio watakaokuwa pamoja na waaminio. Kama "kuwa pamoja na waaminio" kutafsiriwe kwa tafsiri yake hasa, itakuwa na maana kwamba juu ya kuwa wenye kutubu, wenye kutenda vitendo vizuri, wenye kujihalisisha kwa Mwenyezi Mungu, na watiifu wakweli, wale watendao wema huu, hawatafikia daraja za waaminio, bali watakuwa tu pamoja na waaminio. Watapata haki ya kuwa pamoja nao, lakini sio kuwa sawa nao na kuwa miongoni mwao. Tokeo la namna hii ni la kipumbavu kupita kiasi. Kwa hiyo, yatupasa tukubali kuwa *Ma'a* (pamoja) mara kwa mara maana yake ni kufanana au usawa wa daraja. Ni kufanana kwa daraja ndiko kunakotajwa katika maneno "wako pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu" katika aya hii.

Kutoka sehemu nyingine ya Quran Tukufu pia inaonekana kuwa mlango wa aina moja ya unabii bado uko wazi kwa ajili ya wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Huu ni unabii ulio mfano wa unabii wa Mtukufu Mtume s.a.w., na ambao una makusudio ya kuinua na kueneza mafundisho yake. Unabii wa aina hii utapatikana kwa kumtii na kumfuata Mtukufu Mtume s.a.w. Hivi katika Sura Al-A'raaf, Mwenyezi Mungu anasema juu ya Mtukufu Mtume s.a.w. na wafuasi wake:

"Sema: Hakika Mola wangu Ameharimisha mambo ya aibu, yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi na uasi pasipo haki,

na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambacho Hakukiteremshia dalili, na kusema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua. Na kila umati una muda. Basi utakapowafikia muda wao hawatakawia hata saa moja wala hawatatangulia. Enyi wanadamu, bila shaka watawafikieni Mitume kutoka miongoni mwenu, watawaelezeni Aya Zangu. Basi atakayeogopa na kufanya wema, haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika" (Sura 7:34-36).

Kwa aya hizi ni wazi kuwa Mitume watatokea kutoka miongoni mwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Maneno haya yanahusiana na wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. na ni kwa kuwahusu wao ndio Mwenyezi Mungu anaeleza kufika kwa Mitume na kuwakumbusha wajibu wao kuwakubali Mitume hao. Kama hawakukubali watapata taabu. Kama mtu yeyote anataka kudhani kuwa kuna "kama" katika maandishi ya Quran, na kwa hiyo hii "kama" inafanya kuja kwa Mitume kuwe na masharti na kusiko na hakika, hili halitatimiza makusudi yake; kwa sababu neno kama hilo limetumiwa katika Quran Tukufu katika kueleza kutoka kwa Adamu Bustanini (2:39). Lakini hata kama tuchukue "kama" katika aya hii kuonyesha sharti, ni wazi kuwa kwa maoni ya Mwenyezi Mungu, Wahyi na unabii haujafikia kikomo. Tamasha linalokubaliwa ambalo halitaonekana tena, haliwezi kutajwa na Mwenyezi Mungu hata kwa hali ya sharti. Kulitaja jambo lisilowezekana kwa njia kama hii ni kinyume na Heshima ya Mwenyezi Mungu.

Mbali na dalili zilizomo ndani ya Quran Tukufu, Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w. pia zinakubali kuwa wahyi na unabii haukukoma. Haukupigwa marufuku kabisa. Mtukufu Mtume s.a.w. amemtaja Masihi Aliyeahidiwa kwa jina la nabii. Kama, kwa maoni ya Mtukufu Mtume s.a.w., hapana nabii wa aina yoyote anayeweza kutokea baada yake, kwa nini alimtaja Masihi Aliyeahidiwa kwa jina la nabii? (*Muslim*).

## Imani ya Waahmadiyya Juu ya Jihadi.

Hoja ya nne kubwa iliyotolewa dhidi yetu ni kwamba tunakana kanuni ya Jihad. Kila siku nimekuwa nikishangazwa ni kwa vipi lawama hii ya uongo inatolewa dhidi yetu. Kwani kusema kuwa tunakana Jihadi ni uongo. Bila ya Jihad, kwa maoni yetu, imani haiwezi kufanywa kamilifu. Udhaifu wa Uislamu na Waislamu, uoza, au kutoweka kwa imani kunakoonekana leo kila mahala ni matokeo ya kupuuzwa Jihad. Kwa hiyo kusema kuwa tunakana Jihad ni uzushi. Fundisho la Jihad linatokea katika sehemu nyingi ndani ya Quran Tukufu, nasi, tukiwa Waislamu na tuliojitoa kwa ajili ya Kitabu Kitakatifu, tunawezaje kulikana? Tunayokataa na kujiepusha nayo ni fikara ambayo inaruhusu kumwaga damu, kueneza magomvi na uasi, na kuondoa amani ya watu na kuwanyang'anya kwa jina la Islam. Hatuwezi kukubali ya kuwa mafundisho matakatifu ya Islam yanaweza kupotolewa muradi tu tutimize matengenezo na matamanio yetu. Hatuipingi Jihad. Tunachopinga ni maelekeo ya kueneza dhulma na ujeuri na kukuita kuwa ndio Jihad.

Na sasa, msomaji mpenzi, unaweza kufahamu vizuri sana kuwa kama jaribio lifanywe kutafuta kosa kwa mtu mpendwa, ni kubwa kiasi gani kosa litakaloletwa na jaribio hilo kwa mpendaji. Ni ghadhabu ya kadri gani atakayopata kwa mtafutaji wa kosa. Hivyo, sisi tuna ghadhabu kubwa kwa wale wanaosingizia Dini ya Islam kwa maneno yao na vitendo. Watu wengi wanaidhania Islam kuwa Dini ya kikatili sana na Mtukufu Mtume s.a.w., Mtume wa Islam, anadhaniwa kuwa mfalme mshenzi wa kivita. Je, wanaona chochote katika maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w. kinachokubali sifa hii? Kitu chochote kinyume na kanuni za wema na utawa? La, bali Waislamu wenyewe kwa vitendo vyao wameuzuia ulimwengu usikubali Uislamu, hivi kwamba si rahisi sana kuupindua kwenye wazo jingine. Miongoni mwa makosa yaliyofanywa dhidi ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni kosa walilofanya Waislamu wenyewe kwa kumsingizia jambo hili. Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa mfano wa huruma na msamaha. Hakutaka kukidhuru kilicho kidogo sana cha viumbe vya Mwenyezi Mungu. Na bado anaelezwa mbele ya watu kwa namna ambayo nyoyo zao zinamchukia na bongo zao zinakataa

kumwelekea.

Kilio cha Jihad kinasikika tena na tena kutoka pande nyingi mbalimbali. Lakini ni ipi hiyo Jihadi ambayo kwayo Mungu na Mtume Wake waliita? Ni ipi Jihadi ambayo kwayo leo sisi tunaitwa? Jihad ambayo kwayo Mwenyezi Mungu anatuita katika Quran inaelezwa katika aya hii:

> "Basi usiwatii makafiri na ushindane nao kwa (Quran) hii mashindano makubwa" (25:53).

Hivyo, Jihad kubwa kabisa ni Jihad kwa msaada wa Quran, Je, ndiyo Jihad ambayo kwayo Waislamu wanaitwa leo? Ni wangapi wanaotaka kupigana na makafiri, wakiwa na Quran tu mikononi? Je, Islam na Quran vimekuwa visivyostahili sifa na mvuto? Kama Islam na Quran haviwezi kuwavuta watu leo kwa uzuri uliomo ndani yake, tunayo dalili gani ya ukweli wa Islam? Maneno ya wanadamu yanaweza kubadili mioyo. Maneno ya Mwenyezi Mungu yasibadili mioyo yoyote? Hayawezi kuleta mabadiliko yoyote duniani isipokuwa kwa msaada wa upanga? Mazoea ya wanadamu yanaonesha kuwa upanga hauwezi kubadili mioyo, na kwa mujibu wa Islam, ni laana kusilimu kwa sababu ya hofu au kwa ajili ya tamaa. Mwenyezi Mungu amesema waziwazi katika Quran Tukufu kuwa:

> "Wanapokujia wanafiki, husema: Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Anajua kwa hakika wewe ni Mtume Wake; na Mwenyezi Mungu Anashuhudia ya kuwa kwa hakika wanafiki ni waongo hasa" (63:2).

Hapa pana alama ya waaminio - wanafiki. Kama ingekuwa ni sawa kueneza Uislamu kwa upanga, basi kulikuwa na haja gani kuwataja hivi wale waliokubali Uislamu kinje-nje tu lakini ndani

yao walikuwa bado makafiri? Kama ilikuwa ni sawa kuwasilimisha watu kwa nguvu, basi hata waaminio wa aina hii ambao hawakuamini mioyoni mwao wangekuwa Waislamu wa kweli kwa mujibu wa Quran Tukufu. Hakuna awezaye kutumaini kupata waaminio wa kweli kwa njia ya upanga. Hivyo ni kosa kufikiri kuwa Islam inafundisha kutumia upanga kwa kuwasilimisha wasio Waislamu. Kinyume na hayo Islam ni Dini ya kwanza inayoweka kanuni ya hiari katika mambo ya dini kwa maneno yaliyo waziwazi. Fundisho la Islam ni hili:

> "Hakuna karaha katika dini; hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu" (2:257).

Kwa mujibu wa Quran kila mtu anayo hiari kuamini au kukataa. Ana hiari kufuata mwongozo wa akili. Kadhalika Islam inafundisha:

> "Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msiruke mipaka. Kwa yakini Mwenyezi Mungu Hawapendi warukao mipaka" (2:191).

Hapa sheria ya vita za kidini imeelezwa waziwazi. Vita ya kidini ipiganwe kwa wale tu wanaowapiga Waislamu kwa sababu ya dini; ambao wanatafuta kuwaingiza Waislamu katika dini zao kwa maguvu. Hata katika vita za namna hii Islam inakataza kupita mipaka. Kama wasio Waislamu wanatafuta kuwaingiza Waislamu kwa nguvu kwenye dini zao, basi Waislamu wafanye vita nao. Wao wakiacha, vita lazima ikomeshwe; maana kupita kiasi kumekatazwa. Kwa fundisho kama hili, hapana mmoja awezaye kusema kuwa Uislamu unafundisha vita kwa kuueneza. Kama Islam iruhusu vita, si kwa ajili ya kuifuta au kuidhuru dini yoyote. Ni kwa ajili ya kuzidisha hiari ya dini na kulinda mwahala mwa ibada. Imeelezwa wazi ndani ya Quran Tukufu:

"Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia; Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu. Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia Yeye; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mshindi; (22:40-41).

Sehemu hii ya Quran Tukufu inaondoa mashaka kabisa kwamba vita ya kidini hairuhusiwi na Dini ya Islam mpaka iwe ni kwa ajili ya watu wale wanaowalazimisha watu wengine waikane dini yao; mpaka mathalan, Waislamu walazimishwe kuikana Islam. Vita ya kidini inaweza kuruhusiwa pale tu inapotokea kuingiliana katika dini. Lakini hata kama iruhusiwe, vita ya kidini haikusudiwi kuwalazimisha watu waiache imani yao, wala sio makusudio yake kuaibisha au kuzifuta sehemu za ibada, wala kuua. Makusudio ya vita za kidini ni kulinda dini, na kusalimisha kila sehemu za ibada, bila ya kujali ni za dini gani. Ni vita ya kidini ya namna hii tu ndiyo inayoruhusiwa na Islam. Islam ni shahidi na mlinzi wa dini zingine. Islam si sehemu katika jeuri au ukatili au utovu wa uhuru.

Kwa ufupi, Jihad ya Islam ni kufanya vita kwa wale tu wanaowazuia watu kwa nguvu wasikubali Islam, au wanataka kuwalazimisha watu waikane Islam. Inaweza kufanywa kwa watu wale wanaowauwa wengine kwa sababu ya Islam. Ni kwa watu wa namna hii tu ndio kufanya vita kumeruhusiwa na Islam. Kwa watu

wengine wowote kufanya Jihad ya vita ni kosa na ni kinyume na Islam. Vita isiyo na sharti hizi inaweza kuwa vita ya kisiasa, vita baina ya nchi na nchi nyingine, au baina ya watu na watu wengine. Inaweza kuwa vita baina ya Waislamu wa pande mbili. Lakini haiwezi kuwa vita ya kidini.

Jihadi ambayo siyo ila ukatili na uasi, imechukuliwa na Waislamu kutoka kwa watu wengine. Hairuhusiwi na Islam. Hata haijulikani kabisa katika Islam. Ajabu, kama inavyoweza kuonekana, kazi ya kueneza wazo hili kwa Waislamu imefanywa na Wakristo, watu wanaopiga kelele nyingi wakiulaumu Uislamu kwa fundisho lake linalodhaniwa kuwa Jihad. Katika siku za kati, vita za kidini zilikuwa ndio mtindo wa siku hizo. Ulaya yote iliingia katika vita hizo. Waogofyaji wa Kikristo na wapiganaji wao walishambulia mipaka ya nchi za Kiislamu katika njia ileile ambayo makabila fulani yaliyokuwa huru yalishambulia mipaka ya India. Kwa wakati huohuo walishambulia makabila ya Ulaya wale waliokuwa hawajauingia Ukristo. Wakristo waliopigana vita hizi walifanya hivi kwa kutaka kumpendeza Mwenyezi Mungu ati! Inaonekana Waislamu waliotaabishwa katika ukatili huu na mashambulio ya Wakristo walipoteza haiba yao. Wakifuata mfano wa Wakristo, walianza wao pia kushambulia mipaka na nchi za watu wengine. Wakasahu kabisa mafundisho ya dini yao. Wanaonekana dhahiri kuwa wameigiza mtindo wa Wakristo ambao kwao Wakristo wenyewe wameanza kutoa hoja. Licha ya kuwa hoja sasa zinatoka kwa Wakristo, Waislamu wanashindwa kuona mchezo huu wa Wakristo. Katika dunia nzima leo hoja hii inatolewa dhidi ya Islam. Kila mahala inatumiwa kama silaha dhidi ya Uislam; lakini Waislamu hawatambui. Bila ya kukusudia wanaendelea kuwapa maadui wa Islam vitabu na hoja kuishambulia Islam. Adui anakuwa na uwezo wa kuishambulia Islam kwa silaha zilizotengenezwa na Waislamu. Vita, amabazo wanaziita Jihad, hazikuufaa Uislam chochote. Bali zimeudhuru Uislamu. Waislamu wamepoteza kabisa njia za ushindi. Ushindi hauji kwa silaha au idadi. Bali unakuja kwa ustadi, taratibu, elimu, kujiaandaa, tabia njema na kutakia wema mataifa mengine. Taifa dogo sana wakati mwingine linaweza kulishinda taifa kubwa. Hii ni kwa sababu taifa hili dogo lina sharti

za tabia ya ushindi upande wake. Pasipo sharti hizi, watu wawe wengi namna gani hawawezi kuambua kitu. Ingekuwa bora sana, kama Waislamu wangetafuta ufaulu wao sio kwa Jihad yoyote ya batili, bali kwa utawa na ustadi unaoleta ufaulu wa taifa. Kwa kushiriki kwenye Jihad ya kosa wanausingizia Uislamu na kuudhuru. Kama taifa fulani liendekeze vita ya siasa kwa sura ya dini, taifa kama hilo linawaongoza tu watu wa mataifa mengine kuungana na kulishambulia. Mataifa mengine yataanza kujiona si salama. Zama vita za kitaifa zinapoamshwa kwa sura ya tofauti za dini, serikali yenye dhana njema sana kwa wengine haitaepuka shambulio la adui wa nje. Zama serikali zinapogawanywa kwa tofauti za dini, kila moja huziogopa zingine. Tabia njema na dhana njema hapo hazina maana. Wema huu unaweza tu kukinga vita za siasa lakini sio za kidini.

Kwa kifupi hatupingi bali tunathibitisha umuhimu wa Jihad. Tunakana tu maana yake mbaya, ambayo imeleta madhara yasiyohesabika katika Uislamu. Maisha ya Waislamu, kwa maoni yetu, yanategemea ni kwa kadri gani wanaendelea kuelewa maana hasa ya Jihad. Laiti wangeliweza kutambua ya kuwa Jihad hasa ni Jihad ya Quran (25:53), na sio Jihad ya upanga, kama watambue kuwa tofauti za dini hazileti fundisho lolote la vita juu ya maisha na haki au heshima ya wengine (4:91; 2:191 na 60:9), akili zao na hali zao zitapata mabadiliko makubwa; mabadiliko yatakayowapeleka karibu sana na njia ya haki. Halafu basi watakuwa wanafanya sawa na aya ya Quran Tukufu isemayo:

> "Si wema kwenu kuingia majumba kwa nyuma yao, bali wema hasa ni wa yule anayemcha. Na fikeni majumbani kwa milangoni mwao, na Mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu (2:190). Na halafu wataendelea toka ufaulu hata ufaulu.

Nimeeleza kwa kifupi itikadi za Jumuiya Ahmadiyya. Vilevile nimeeleza hoja za upinzani zinazotolewa na majibu yetu juu ya hoja hizo. Sasa nitaendelea kutoa muhtasari wa madai ya Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya na msingi juu ya hoja za madai yake.

Ninafanya hivi ili nisimame nisiye na lawama mbele ya Mwenyezi Mungu; ili ije isemwe kuwa nimefikisha ujumbe, na ya kwamba wewe, msomaji mpenzi, upate makusudio ya Mwenyezi Mungu, na kufanya bidii kutenda sawa na makusudio haya, na urithi rehema za Mwenyezi Mungu na upokee zawadi ya Mapenzi Yake.

## MADAI YA HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD

Madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., ni kwamba Mwenyezi Mungu amemwinua yeye kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu; yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa katika Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w. na Mahdi Aliyebashiriwa na Hadithi zake; ya kwamba bishara zilizomo ndani ya vitabu vya dini mbalimbali juu ya kufika kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika siku za mwisho pia zimetimia katika nafsi yake; na ya kwamba Mwenyezi Mungu amemwinua yeye kwa kuwakilisha na kutangaza Uislamu katika wakati wetu; Mwenyezi Mungu amemjaalia elimu ya Quran Tukufu, na amemfunulia maana zake za ndani sana na kweli; na ya kwamba amemfunulia siri za maisha ya utawa. Amekabidhiwa kazi ya kumtukuza Mtukufu Mtume s.a.w. na kuonesha ubora wa Islam juu ya dini zingine. Makusudio ya kuja kwake ni kwamba mapenzi ya Mwenyezi Mungu yadhihirike kwa ajili ya Islam na Mtukufu Mtume s.a.w. na ionekane ya kuwa watu kukaa mbali na Uislamu na Mtukufu Mtume s.a.w. kunamchukiza Mwenyezi Mungu. Kadhalika amedai ya kuwa kuja kwake kulitabiriwa na karibu manabii wote na waanzilishi wa kila dini wa hapo kale. Hii ni kwa sababu Mtume wa Islam alitumwa kuwa Mwalimu kwa wanadamu wote. Ilikuwa awakusanye wanadamu katika fundo moja, kuwaunganisha katika imani moja. Kama kazi hii ilikuwa itimizwe, ilikuwa ni lazima kwamba tofauti za kitaifa na mila na chuki ziondolewe kabisa, ili kwamba Mtume wa Islam aweze kukubaliwa kama Muhuri wa Manabii na watu wote duniani. Kwa hiyo, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, manabii na waalimu wa dini wa zamani kila mmoja alitabiri kufika kwa nabii mmoja wa dini hiyohiyo katika siku za mwisho. Bishara hizi zilimhusu mfuasi wa Mtukufu Mtume

s.a.w., ambaye ilikuwa aamriwe na Mwenyezi Mungu kuthibitisha na kutangaza ukweli wa Mtukufu Mtume s.a.w., na ilikuwa awaunganishe wafuasi wa dini mbalimbali katika dini ya Islam. Bishara zilizomo katika vitabu vya dini zingine zinazotabiri kufika kwa mwalimu ajaye - zote zimetimia katika nafsi yake. Alikuwa Masihi kwa Wakristo na Wayahudi, alikuwa Masiodarbahmi kwa Wazartashti, na alikuwa Krishna kwa Mabaniani. Kuja kwake na kutimia bishara zilizomo katika vitabu vya zamani ni dalili ya ukweli wake. Kama alivyo yeye mwenyewe ni mfuasi wa dini ya Islam, kuja kwake ni wito kwa wafuasi wa dini zingine wasilimu na kuingia katika kundi la Mtukufu Mtume s.a.w.

## HOJA ZINAZOSAIDIA MADAI YAKE.

Baada ya kueleza kwa ufupi madai ya Masihi Aliyeahidiwa, Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, ningependa kueleza mizani ambayo kwayo ukweli wa mdai kama huyo unaweza kupimwa. Inapoonekana kuwa mtu fulani ametumwa kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu huwa hapana budi kila mtu kukubali madai yake. Kama mtu amechaguliwa na Mwenyezi Mungu kuwa kiongozi, ni vigumu kwamba anaweza kujaribu kupotosha watu. Kama kiongozi aliyetumwa na Mwenyezi Mungu anaweza kupotosha, itakuwa na maana (Mungu apishe mbali) ya kwamba Mwenyezi Mungu amefanya kosa katika uteuzi wake, hivi kwamba amemtuma kuwa Mjumbe wake mtu ambaye si msafi wa roho, ambaye anatafuta heshima kwa ajili yake, lakini sio kueneza ukweli, hata anajiweka juu kuliko Mwenyezi Mungu.

Sio tu kwamba fikra kama hii ni kinyume na akili; bali Quran Tukufu waziwazi inaikana fikira hii. Anasema Mwenyezi Mungu katika Quran Tukufu:

"Haimpasi mtu kwamba Mwenyezi Mungu Ampe Kitabu na hukumu na Unabii kisha aseme kwa watu: Muwe watumishi wangu badala ya Mwenyezi Mungu; bali (yeye atawaambia), kuweni wenye kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa sababu mlikuwa mkifundisha Kitabu, na kwa sababu mlikuwa mkisoma. Wala yeye hatawaamuruni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa waungu; je, atawaamuruni ninyi kufuru baada ya ninyi kuwa Waislamu? (3:80-81).

Haiwezekani, yaani, kwamba Mwenyezi Mungu ampe mtu Kitabu, hekima na cheo cha unabii, na tena mtu kama huyo awafundishe watu kumwacha Mwenyezi Mungu na kuwataka wamtii yeye badala ya Mwenyezi Mungu. Mtu kama huyu hawezi ila kuwafunza watu wamtii Mwenyezi Mungu, maana wanasoma maneno Yake na kuwasomea hayo wengine. Wala mtu kama huyu hawezi kuwafundisha watu kuwafanya Malaika na Mitume kuwa waungu. Haiwezekani kwa yeyote kuwashawishi watu waamini na tena awafanye wasioamini.

Kwa hiyo, swali kubwa tunapokabiliwa na ukweli wa mdai wa uongozi wa mbingu ni kwamba je, kiongozi huyo ni mkweli? Kama madai yake ni ya kweli mafundisho yake ni ya kweli. Kama madai yake hayaonekani kuwa ya kweli, basi ni bure kujaribu kupima mafundisho yake. Kwa kufuata kanuni hii ing'aayo, ninapenda kuyapima madai ya Mwanzilishi wa Jamia ya Ahmadiyya, ili wasomaji wangu wapate habari kamili juu ya msingi wa madai yake, ambao kwao mamia ya maelfu ya watu wamekwisha mkubali.

## HOJA YA KWANZA - HAJA YA WAKATI

Hoja ya kwanza inayoshuhudia ukweli au uwongo wa mdai wa unabii iko juu ya msingi wa haja ya wakati. Kanuni maarufu ya Mwenyezi Mungu inatwambia kuwa tendo la Mwenyezi Mungu halijiri mahala pasipo pake wala wakati usio wake. Wazo jipya

halishuki kutoka kwa Mwenyezi Mungu mpaka ulimwengu uwe na haja nalo. Kwa upande mwingine wakati haja ya wazo imedhihirika, haliwezi kuchelewa zaidi. Kanuni inakuwa yenye kuifaa dunia. hakuna hata haja moja ya kidunia ambayo Mwenyezi Mungu hakuikidhi. Haja hata ndogo sana imo katika kanuni ya Mwenyezi Mungu. Kilicho cha kweli katika haja za kimwili za mwanadamu, ni lazima kiwe kweli vilevile katika haja zake za kiroho. Ingekuwa kinyume na upaji na ukarimu wa Mwenyezi Mungu kama isingekuwa hivyo. Ni ajabu ya kwamba atimize haja za mwili wa mtu, lakini sio za roho yake. Mwili ni udongo tu. Haja zake ni za muda mfupi. Kanuni zake na makusudio vina kikomo. Kinyume cha hayo roho imekusudiwa kuishi milele. Tamaa za roho hazina kikomo. Haja zinazotafutwa na roho na njia zake za kuzikidhi haziwezi kwisha.

## KUONGOZA WANADAMU NI WAJIBU WA MWENYEZI MUNGU

Kama mtu asome kwa fikira juu ya sifa za Mwenyezi Mungu katika nuru ya Quran Tukufu, hawezi hata kwa dakika moja kufikiri kuwa zama hali ya kiroho ya wanadamu inapolilia kuhuishwa, Mwenyezi Mungu asimwinue mhuishaji. Kama ingekuwa hivyo, kungekuwa hakuna maana yoyote katika maisha ya mwanadamu; na isitoshe Mwenyezi Mungu anafundisha katika Quran Tukufu kuwa mbingu na ardhi na kila kilichomo ndani yake havikuumbwa kwa mchezo; bali kwa haki:

> "Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo katika yao kwa mchezo. Hatukuviumba ila kwa haki, lakini wengi wao hawajui" (44:39-40).

Kwa hiyo, inafuata hivi ya kwamba wanadamu wanapoanza kupata taabu kwa maanguko ya kiroho na kuhitaji mhuishaji wa

kiroho, hawana budi wampate mmoja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mhuishaji huyu awarudishe wanadamu tena kwenye njia ya haki na kuwaondoa katika udhalilifu, na kuwaweka mara nyingine katika barabara ya ukweli.

Kwa hivi, sifa za Mwenyezi Mungu zinakataa kabisa kufikiri kuwa Mwenyezi Mungu asifanye lolote wakati waja wake wanapohitaji msaada wake na mwongozo. Lakini pamoja na hayo, tunalo thibitisho la dhahiri katika Quran Tukufu la msaada wa Mwenyezi Mungu kila unapohitajiwa. Amesema Mwenyezi Mungu:

> "Na hakuna kitu chochote ila tunayo hazina yake, wala Hatukiteremshi isipokuwa kwa kipimo maalumu" (15:22).

Chanzo cha kila kitu ni mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Mtu huvipokea kama zawadi; bali kwa kipimo maalum. Zawadi hizi zinaambatanishwa na haja za mwanadamu. Hazishuki ila zinapohitajiwa. Wala hazikawizwi wakati haja imedhihirika. Asema tena Mwenyezi Mungu:

> "Na Amewapeni kila mlichomwomba; na kama mkihesabu neema za Mwenyezi Mungu, hamtaweza kuzihesabu" (14:35).

Mwenyezi Mungu humpa mtu kila anachohitaji. Anampa kama zawadi. Hizi haziwezi kuhesabika. Akiombacho mtu ni kile hasa ahitajicho. Mtu huomba vitu vingi, lakini hapati kila anachokiomba. Kwa hiyo, aya hii ina maana kuwa haja hasa za mtu, haja zile ambazo mtu kwa asili anazihitaji, ambazo zinahusiana na uzima wake wa milele, zinaahidiwa kutimizwa na Mwenyezi Mungu.

Hivyo, tunalo thibitisho kuwa haja za mwanadamu, za kimwili na za kiroho, haziwezi kukosa kukidhiwa. Juu ya suala la mwongozo, kwa hali yoyote, tunalo thibitisho halisi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wanadamu wanapohitaji mwongozo, Mwenyezi Mungu hana budi kuuleta mwongozo huo. Kwa kweli, kutoa mwongozo ni wajibu wa Mwenyezi Mungu, wajibu asio nao mshirika. Anasema

Mwenyezi Mungu katika Quran:

"Hakika kuongoza ni juu Yetu" (92:13).

Katika Quran Tukufu tunaambiwa kuwa kutolewa kwa mwongozo wa mbingu wakati hata wakati sio tu kunatamaniwa, bali ni lazima. Laiti Mwenyezi Mungu asingekidhi haja hii, siku ya Kiyama, wanadamu wangemjibu wakisema, "Kwa sababu hatukuwa na viongozi kutoka kwako, huna haki kutuhukumu kwa kutotenda au kutenda kwetu, wala huna haki kutuadhibu" Tunasoma ndani ya Quran Tukufu:

"Na lau kama Tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla yake (Mtume) wangesema: Ee Mola wetu, mbona hukutuletea mtume tukazifuata Aya Zako kabla sisi kudhilika na kufedheheka? (20:135).

Ndiyo kusema kuwa kama Mwenyezi Mungu Akipeleka adhabu yake kabla hajamtuma Mtume wake kwa watu, wangemhoji na kusema: Kwa nini Mungu hakutuongoza tulipohitaji mwongozo wake? Kwa nini hakututumia Mjumbe ambaye tungemkubali na kumfuata kabla ya kudhilisha nafsi zetu? Mwenyezi Mungu hakani hoja hii. Bali anaikubali. Wajibu wa Mwenyezi Mungu kuongoza umetiliwa mkazo katika sehemu zingine ndani ya Quran Tukufu.

Quran inaendelea. Inafikiria kuwa si haki kupeleka adhabu, mpaka katika wakati wa haja, watu walimpata wa kuwaongoza. Inasema Quran Tukufu:

"Enyi makundi ya majinni na wanadamu! Je hawakuwafikieni Mitume toka miongoni mwenu kuwabainishieni Aya Zangu na kuwaonyeni juu ya mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako Hakuwa wa kuiangamiza miji kwa dhuluma, hali wenyeji wake wameghafilika" (6:131-132).

Akiwaambia majinni na watu, Mwenyezi Mungu anauliza kama hawakuwapokea wajumbe Wake na kama hawakuonywa juu ya siku yao hiyo. Kwa kumjibu majinni na watu wanakubali kuwa walimpata mwonyaji. Ila tu, walidanganywa na maisha ya dunia. Wanathibitisha ukafiri wao wenyewe. Hivyo basi, Mwenyezi Mungu huonya kabla hajahilikisha; kwani, kuhilikisha bila ya kuonya kwanza itakuwa ni ukatili, dhuluma na mbali na sifa ya Mwenyezi Mungu.

Aya hizi za Quran Tukufu zinadhihirisha kuwa kuwahukumu watu kuwa wapasao kuadhibiwa na kuwafanyia hivyo kana kwamba kweli na batili vilipambanuliwa kwao, ambapo hawakuonywa hata kidogo, ni ukatili ulioruka mipaka. Kwa upande mwingine, kama watu wanahitaji mwongozo, lakini hawapati mwongozo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kama licha ya hivi, Mwenyezi Mungu awaadhibu siku ya Kiyama, itakuwa ni ukatili mkubwa sana usio kifani. Lakini Mwenyezi Mungu si katili. Kwa hiyo, ni vigumu ya kwamba watu wahitaji msaada Wake lakini asikidhi haja yao.

## QURAN IMEAHIDI MWONGOZO KWA WAISLAMU

Hivyo, inaonekana kuwa kwa mujibu wa Islam, zama watu wanapohitaji mwongozo, mwongozo huo hutolewa. Pamoja na hayo, ndani ya Quran inaonekana kuwa mbali na kanuni ya mwongozo katika wakati wa haja, wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w., Ummati Muhammadiyya, wamepata ahadi mahsusi ya mwongozo wa

mbingu. Ahadi hii imo katika aya hii:

"Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao" (15:10).

Ndiyo kusema kuwa Mwenyezi Mungu ni Mfunuaji na pia Mhifadhi wa Quran Tukufu.

Sasa basi, hifadhi ni za namna mbili. Hifadhi moja ni ya nje, - hifadhi ya maandishi ya Quran. Na nyingine ni ya ndani, - hifadhi ya maana na ujumbe. Mpaka vyote viwili herufi na maana vimelindwa makusudio ya hifadhi hayatatimizwa. Kama tuhifadhi ngozi, mdomo na miguu ya ndege, na tuijaze ngozi ile majani, tutakuwa tumesalimisha hali ya nje ya ndege, lakini sio ndege. Ndege hataishi tena. Kadhalika, kama ndege yule ahasiri mdomo wake na miguu yake, kama apoteze manyoya yake, hawezi kusemwa amesalimika. Kitabu kinachoingizwa maneno mengine zaidi yasiyo ya asili yake na kupunguzwa ambacho lugha yake imekufa hivi kwamba hakuna awezaye kuelewa, kitabu ambacho hakitimizi tena makusudio yake ambayo kwayo kilifunuliwa, ni kitabu kilichokufa. Hakikuhifadhiwa. Yawezekana maneno yake yawe salama. Lakini maana yake ikatoweka. Na maana ndiyo kitabu. Kama maneno ya kitabu yanahitaji kuhifadhiwa, ni kwa sababu ya maana yake. Kwa hiyo hifadhi ya Quran Tukufu ni hifadhi ya vyote viwili maneno na maana yake.

Njia mbalimbali ambazo kwazo Mwenyezi Mungu ameihifadhi Quran Tukufu na hivyo akatimiza sehemu moja ya ahadi ya hifadhi inastaajabisha. Mpaka wakati wa ufunuo wa Quran Tukufu, lugha ya Kiarabu ilikuwa haijapangwa kwa mpango maalum, nahau yake, maneno yake na fasaha yake vilikuwa havijawekwa. Namna za msemo, na jinsi zingine za lugha zilikuwa hazijakusanywa. Hata ufundi wa kuandika ulikuwa bado mchanga sana. Mara Quran Tukufu ilipofunuliwa tu, Mwenyezi Mungu aliwachangamsha waaminio kupanga elimu hizi. Ili kuitumikia Quran na kuilinda katika mabadiliko ya nyakati, Waislamu wa zamani walivumbua elimu nyingi za sarufi na nahau ya lugha ya Kiarabu; Tajwid,

ufasaha, ma'aani, bayaan, taarikh na fiqh. Elimu zote hizi zilizidisha faida yao wenyewe katika kuilinda Quran Tukufu. Katika hizi, elimu ya nahau na sarufi na lugha ilikuwa ndiyo yenye maana sana kwa kuilinda Quran Tukufu. Inastaajabisha kwamba elimu hizi ni za juu sana miongoni mwa elimu za Kiislamu. Hata kwa maoni ya wanazuoni wa Ulaya, Nahau ya Kiarabu na Kamusi zake zimepangwa vizuri zaidi kuliko nahau na kamusi zote za lugha zingine.

Sio tu kwamba tunazo elimu hizi za lugha; bali pamoja na hayo tuna mamia ya maelfu ya watu walioweza kuikumbuka Quran Tukufu yote kwa ghaibu. Kwa upande mwingine, maandishi ya Quran Tukufu si kama utenzi au mashairi, lakini kama kitu fulani kati ya hivi, kukumbukwa kwake kwa ghaibu kukawa rahisi sana. Wale waliojaaliwa kukumbuka sehemu fulani, wanajua kuwa maandishi yaliyo rahisi sana kukumbukwa kwa ghaibu ni Quran Tukufu. Sio tu kwamba Quran ni rahisi kukumbukwa bali pia tunao mamia ya maelfu ya Waislamu walioona shauku ya kuikumbuka kwa ghaibu. Mbali na hayo, kila Mwislamu inampasa kusoma sehemu za Quran Tukufu katika sala zake kila siku, hivi kwamba hata Waislamu wa kawaida tu wanajua sehemu za Quran Tukufu kwa ghaibu. Kama, (Mungu apishe mbali), nakala zote zilizopo za Quran Tukufu zitoweke, bado haitaleta kutoweka kwa Quran Tukufu. Quran Tukufu itasalimika ikiwa ndani ya vichwa vya Waislamu.

Hivyo, inaonekana kuwa Mwenyezi Mungu ametoa njia za kutosha kwa kuihifadhi Quran Tukufu kwa nje yake. Mbele ya njia hizi zote, ni jambo lisilowezekana ya kwamba tunaweza kupoteza sehemu yoyote ya Maandishi Matakatifu.

Kwa hali yoyote, shabaha hasa ni kwamba kulindwa kwa maneno si hata nusu ya umuhimu wa kulindwa kwa maana ya maneno. Maneno yako kwa ajili ya maana, sio maana kwa ajili ya maneno. Kama Mwenyezi Mungu amefanya kiasi hiki kwa kulinda maneno ya Quran Tukufu, hawezi kuwa amefanya kiasi chini ya hiki kwa kulinda maana yake. Kila mtu, awezaye kupima na kuelewa, atakubali kuwa haiwezekani kwamba Mwenyezi Mungu asilinde maana ya Quran Tukufu ambapo ameweza kulinda maneno yake.

Kama Mwenyezi Mungu amefanya hivi kwa kulinda Quran kwa nje, ni lazima awe amefanya zaidi kwa ajili ya kulinda maana yake. Ukweli ulio wazi ni kwamba katika aya hii:

"Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao" (15:10), tunayo ahadi ya zote hifadhi ya nje na ya ndani pia. Hifadhi ya ndani ya Quran Tukufu maana yake ni kuwa zama wafuasi wa Kitabu Kitakatifu wamepotoka kabisa mbali na Quran Tukufu, hivi kwamba Kitabu kinapungua thamani na kubakia maneno matupu, na mioyo na akili za watu vinafunga kabisa, Mwenyezi Mungu ahuishe nguvu ile ya zamani na mvuto wa Kitabu Kitukufu, aifanye maana yake wazi mara nyingine, na kuhuisha uzuri wote uliokufa wa Kitabu hiki. Ahadi hii ya Mwenyezi Mungu inashuhudiwa na Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w., - moja imepokelewa na Abu Huraira aliyesimulia kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alisema:

"Hakika Mwenyezi Mungu atainua kwa ajili ya Ummati huu katika mwanzo wa kila karne moja, mtu atakayejadidisha dini yao" (Abu Daud, Kitabul-Fitan).*

Hadithi hii ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni hashia ya aya ya 10 ya sura ya 15 ya Quran Tukufu. Inawakilisha kwa urahisi zaidi maana ya aya hii tukufu. Inawezekana kuwa wale wanaochukua maana ya kijuu juu ya kila kitu na kuambatanisha imani yao kwenye herufi tu na kupuuza roho yake na maana, wafikiri kuwa aya hii ya Quran Tukufu inaahidi hifadhi ya maneno yake tu. Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya kufika kwa Mujaddid katika mwanzo wa kila karne, amewaonya Waislamu wasisahau maana hasa ya kuhifadhi. Ni shauri yao sasa wasijipotoshe wala wasipotoshe wengine.

*Wachunguzi wa Hadithi wameafikiana juu ya usafi wa Hadithi hii. Miongoni mwao ni Imam Hakim na Imam Baihaki (Hujajul-Karamah, uk. 233).

## KUHIFADHIWA KWA QURAN NI KUHIFADHIWA UISLAMU.

Kwa hali yoyote, Hadithi inaleta shabaha nyingine. Mujaddidina walioahidiwa katika Hadithi iliyotajwa, ilikuwa watokee katika mwanzo wa kila karne. Makosa ambayo wangepigana nayo - ni makosa yanayotokea kwa kukosa kufahamu maana ya Quran Tukufu - ambayo yangetokea katika mwanzo wa kila karne. Mujaddid, kila miaka mia, ni dhamana ya ulinzi wa kimbinguni. Uislamu ilikuwa ulindwe kwa kufika Mujaddid kila miaka mia moja. Uislamu ilikuwa utumikiwe na Mujaddidina hawa na wafuasi wao. Ilikuwa ulindwe katika hatari ya tafsiri za kosa.

Kwa ufupi fundisho la Quran ni kama hivi:-

(1) Zote, haja za kimwili na za kiroho za mwanadamu zimeahidiwa kukidhiwa, hususa haja za kiroho kwa sababu upeo wake ni mpana zaidi na ubora wake ni mkubwa sana. Isipokuwa kwa ahadi hii, kazi yote ya uumbaji itakuwa isiyo na maana yoyote.

(2) Kuna ahadi mahususi ya mwongozo wa mbingu kila utakapohitajiwa mwongozo huo na mwanadamu.

(3) Kama mwongozo huo usije, mwanadamu atakuwa na haki kumtoa makosa Mwenyezi Mungu.

(4) Kama mwongozo haukuja katika wakati wa haja, wale wanaohangaika kuutafuta mwongozo hawataadhibiwa; kuwaadhibu kutakuwa ni tendo la ukatili, na Mwenyezi Mungu si katili.

(5) Kuna ahadi iliyo wazi ya kuinuliwa Mujaddidina kufasiri upya maana ya Quran Tukufu.

(6) Mujaddidina hao watatokea kila miaka mia moja.

## HALI YA WAISLAMU

Sasa, msomaji mpenzi, Mwenyezi Mungu afungue moyo wako uukubali ukweli Wake! Ni juu yako kufikiri kama uliopo sio wakati wa kufika Mujaddid. Inaonekana katika Hadithi kuwa haja ya

Mujaddid itatokea kila miaka mia. Kila miaka mia tupate Mujaddid wa kuifasiri Quran Tukufu kwa watu wote. Lakini sasa sio mwanzo bali katikati ya karne. (Wakati wa tafsiri ya Kiswahili kutolewa, karne hii imekaribia kwisha. *Mfasiri*). Hata kama tuipuuze Hadithi hii ya Mtukufu Mtume s.a.w., hatuwezi kupuuza kweli kama tunavyoziona. Kwa kutazama kweli hizi, mara moja tunakubali kuwa Mujaddid anahitajiwa hasa kwa wakati huu. Kama Waislamu na watu wengine wangekuwa hai katika mambo ya kiroho, kama wangeweza kuaminiwa kuendelea wenyewe tu bila ya kuongozwa, hatuna haja ya kumjali mdai yeyote wa Ujaddid. Lakini kama hali ya kiroho ya Waislamu inahitaji Mujadid na kama maadui wa Uislamu wameruka mipaka yote ya uadui, yatupasa tukubali kuwa uliopo ndio wakati wa kuja Mujaddid, kufundisha Uislamu tena, kushambulia maadui zake, kuwarudisha Waislamu kwenye Uislamu wa kweli, kuumba tena katika mioyo yao mapenzi yaliyokuwako zamani juu ya dini; kwa ufupi kuonesha mara nyingine nguvu iliyo hai ya Dini ya Islam.

Kwa hali ya ujumla ya Waislam leo na shabaha ya maadui za Uislamu, hakuwezi kuwa na maoni ya namna mbili. Kila mmoja, asiye na tabia ya kuficha ukweli, kila mmoja awezaye kupambanua wema na ubaya, atakubali kuwa kwa akili na kwa roho, kwa imani na kwa vitendo, Waislamu wamekwenda mbali kabisa na Uislamu. Aya ya Quran inasema:

> "Na Mtume atasema; Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Quran hii kitu kilichoachwa" (25:31).

Huu ni ukweli mkavu kabisa juu ya Waislamu leo. Suala tena sio, "Ni mambo mangapi ya Uislamu wameyaacha?" Bali hasa suala ni "Mangapi hawajayaacha?" Kweli ni leo hii kwamba "Utawakuta Waislamu makaburini na Islam katika kitabu chake"! Islam leo inaweza kukutwa ndani ya kurasa za Quran Tukufu, vitabu vya Hadithi, na vitabu vya Maimamu, lakini sio katika maisha ya Waislamu. Kwanza Waislamu hawana hata habari ya mafundisho ya Islam. Kama wanatafuta kujua hayo, mara moja wanaona kuwa

imekuwa vigumu kujua maana na roho ya Islam. Kila kinachohusiana na Islam kimepotolewa. Imani juu ya Mwenyezi Mungu inavyowakilishwa leo kwa jina la Islam imekuwa ya ajabu hivi kwamba shauku ya kumhimidia Mwenyezi Mungu haiwezi kupatikana kwa mtu mwaminifu. Itikadi juu ya Malaika pia ni mbaya ajabu. Juu ya Malaika, Mwenyezi Mungu alifundisha kuwa: "Wanafanya wanayoamriwa" (16:51). Na bado mufasirina wa Quran wanawaeleza kuwa wapinzani wa Mwenyezi Mungu, kuwa ni viumbe dhaifu walio katika sura za kibinadamu wakiwa na tamaa za wanawake wabaya. Manabii wa Mwenyezi Mungu wanaelezwa kama wahadaa na wenye dhambi, hivi kwamba mapenzi na heshima, ambayo wangepokea wakiwa wapendwa wa Mwenyezi Mungu hayawezi kupewa kwao tena. Kadhalika tunaambiwa kuwa wahyi wa Mwenyezi Mungu haukusalimika na mvuto wa shetani; hivyo chanzo cha pekee cha usalama kinaondolewa. Mifano ya divai, pepo na Jahannam, inasukumwa mbali sana, hivi kwamba kinachowakilishwa kwa jina la Islam kinaonekana aidha upuuzi au kichekesho.

Wachilia mbali manabii wengine, mufasirina wa Islam hawakumwacha hata Mtukufu Mtume s.a.w. Kwa uongo kabisa wamemsingizia kuwa na mambo mengine mengi yasiyo ya kweli. Kwa njia hii wamepunguza uzuri usio kifani wa tabia ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa ni taswira ya Quran Tukufu, alisema Hadhrat Aisha ambaye alimjua vizuri zaidi. Na bado mufasirina wamemchorea sura ya namna nyingine kabisa. Fundisho la kutenguliwa kwa Quran limevumbuliwa na Kitabu kikamilifu kimeingizwa katika shaka. Bila kuweza kuelewa sehemu za Quran Tukufu, mufasirina wameziita zilizotenguliwa. Wamefanya hivyo bila ya ruhusa ya Quran Tukufu au ya Mtukufu Mtume s.a.w. Wanasahu kwamba kwa kufanya hivyo wanaleta shaka sio katika sehemu za Quran Tukufu tu bali katika Quran yote.

Halafu inafundishwa kuwa aliyekufa, mwenyewe akiwa mfuasi wa Nabii Musa, atakuja na kuhuisha Uislamu katika zama hizi; wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. na mvuto wake ukiwa ulioshindwa kufanya hivyo.

Ni mengi kuhusu itikadi za Waislamu. Maisha yao yanasikitisha

sana. Kiasi cha 75 katika mia hawasimamishi sala tano au kufunga saumu za Ramadhan. Hapana mtu alipaye zaka au sadaka zilizolazimishwa. Katika hao wanaolipa, wachache sana, vigumu kupata wawili katika mia wanaotoa kwa shauku ya mioyo yao. Wachache miongoni mwa wale ambao lazima yao ya kwenda kuhiji wanaifikiria, mbali kuitimiza. Wale ambao kwa ajili yao hija sio kwamba haikulazimika tu, bali imekatazwa kwa sababu ya hali fulani, wanakwenda kuhiji. Basi tu kuleta dharau katika Islam. Wachache, wanaosimamisha amri za Islam, wanafanya hivyo kwa namna ambayo makusudio ya amri hizo yanapotezwa kabisa. Maana ya maneno ya Kiarabu yanayotumiwa katika sala ni shida sana kufahamika nchi za nje ya Bara Arabu. Wale wanaosali pasipo kufahamu maana yake hawasali kwa shauku, bali kana kwamba ni mzigo uchukizao. Sijda zinapelekwa, kwa haraka sana hivi kwamba anayesali hawezi kupambanua katika ya rukuu na sijda. Kuomba dua katika lugha ya mtu mwenyewe baina ya dua zilizoelezwa inasemwa kuwa ni kufuru. Saumu, badala ya kuleta manufaa ya kiroho, imekuwa sababu ya adhabu ya mbingu. Watu wanasema uwongo na kusengenyana hali wamefunga.

Sheria ya Islam juu ya mirathi pia imepuuzwa. Kula riba, kulivyoelezwa na Quran kama ni kupingana na Mwenyezi Mungu, ndio kumekuwa sasa desturi ya ulimwengu mzima. Ahsante sana Maulamaa na Masheikh! Tafsiri nyingi za kosa na mambo mengi waliyozidisha yanawawezesha Waislamu wa leo kupokea riba katika mali zao bila ya kufikiri kuwa ni dhambi; na licha ya haya yote, Waislamu bado ni maskini, wako mbali kabisa nyuma ya wengine katika mambo ya maendeleo.

Tabia njema ambayo kwanza ilikuwa ndio asili ya Waislamu wote, sasa inaonekana kuwa mbali nao kama ilivyo kufuru mbali na Uislamu. Wakati ulikuwako ambao neno la mdomoni mwake lilipokelewa kama ahadi iliyofanywa kwa kuandika. Lakini leo hakuna kisichoaminika zaidi kama neno la Mwislamu. Uaminifu umetoweka kabisa. Kauli ya kweli imekuwa ghali, tumaini limekuwa jambo lililopita. Uasi, uongo, uhaini, ulaghai, woga na upumbavu vimewazinga Waislamu. Matokeo ya upungufu wa tabia njema ni kwamba ulimwengu mzima unawaandama Waislamu. Ujasiri wao katika mambo ya uchumi umekoma. Jina lao tukufu limeondoka.

Elimu na hekima ambayo kwanza vilikuwa vijakazi vyao na visahibu vyao vya daima, leo vinaonekana vigeni mbele ya macho yao. Masufi pia wameharibika. Wameifanya dini kuwa dunia na wamezipuuza sheria za dini. Wakubwa wa Waislamu wanazidisha chuki na uadui. Wanadhamini maoni yao wenyewe kuwa mafundisho ya Mungu na Mtume Wake. Hivyo wanaupiga mzizi wa Islam na nguvu ya Waislamu. Walio matajiri miongoni mwa Waislamu si chochote ukilinganisha na matajiri wa mataifa mengine, bado wanajivuna sana hivi kwamba kujishirikisha katika dini inaonekana ni fedheha kwa ajili yao. Wachilia mbali wao kushiriki katika kazi za dini, wana fikara ndogo sana juu yake mioyoni mwao. Tunaweza kuwaona wahubiri miongoni mwa matajiri wa mataifa ya Ulaya, lakini kati ya matajiri wa Kiislamu itakuwa taabu sana kupata wengi wenye elimu, walau kidogo tu, ya dini. Falme za Kiislamu zimefutika. Kuwalia vyao maskini na wajinga ndiyo shughuli ya kila siku ya watawala wao. Fursa ya kutawala, kwao, sio fursa ya kutumika, bali fursa ya kutoa amri za ukatili. Wafalme wa Kiislamu wanajifurahisha na anasa za dunia. Mawaziri wao wanaweka mipango ya uasi na uhaini. Waislamu raia wamekuwa wabaya kuliko washenzi. Mamia ya maelfu miongoni mwao hawawezi hata kutamka Kalima, wachilia mbali kusema wanaweza kueleza maana yake. Islam, kwanza ilikuwa tisho kwa dini zingine, leo imekuwa mzoga, ikiliwa na mbwa na tai. Kwa ajili ya haja zao zote, Waislamu wanaweza kupata njia na fedha, lakini sio kwa ajili ya kuulinda na kuueneza Uislamu. Wakati unaweza kupatikana kwa kukashifu, kwa kupiga soga, na kwa kuzungumza na marafiki, lakini sio kwa kujifunza na kufundisha Kitabu Kitakatifu cha Quran. Kila mtu anajua ni ubora gani wa sala tano ulikuwa machoni pa Mtukufu Mtume s.a.w. Sio mlegevu au mkosekanaji wa kawaida, bali mkosekanaji katika sala za Alfajiri na Ishaa, alilaumiwa na Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa ni mnafiki. Mtukufu Mtume s.a.w. alitangaza:

Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, wakati watu wamejumuika kwa ajili ya Sala, ninapenda kuwa na kuni za kutosha, halafu nimchague mtu mmoja awe Imam nami nitoke nje nikawachome pamoja na nyumba zao wale watu ambao hawakufika kwenye sala ya jamaa" (Tajridul Bukhari, Kitabu cha kwanza uk. 72).

Leo kujumuika katika sala ni jambo gumu sana. Isipokuwa 'Iddi mbili, mamilioni za Waislamu hawawezi kupata dakika chache zinazohitajiwa kwa ajili ya sala za kila siku. Wale wanaojumuika kwenye sala za kila siku hata hivyo hawatimizi sharti na kanuni zake. Mara nyingi wanajumuika kwa kujionesha tu. Hata hawajui kanuni za kutawadha.

Kwa neno zima, Islam leo iko pweke kabisa. Kila mtu ana rafiki lakini sio Dini ya Islam. Hali hii ya Islam imeelezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya katika beti alizoandika katika shairi la Kifarsi (Kiajemi):

Mazuri hasa ya hamu; haya machozi ya damu,
yamiminikayo humu, kuililia imani.
Hii imani ya kweli, aliyoleta Rasuli,
imedidimizwa kweli, na kufuru imewini.
Hao majitu dhalili, wasio imani kweli,
wamuumbua Rasuli, mcha Mungu wa yakini.
Watu ambao ni wafu, wenye madhambi sufufu,
waushusha utukufu, wa Muhammad Amini.
Huyu Bwana apitile, kuliko yeyote yule,
wamemlenga mishale, kama vua la uzani.
Enyi mloghafilika, dini yadharaulika,
kinga gani mtashika, mbele ya wenu Manani.
Kufuru ilivyozidi, kamithili ya Yazidi,
pamwe na yake junudi, kuhilikisha imani.
Dini ya Mungu Manani, Mwingi mno wa hisani,
naye wanamuamini, Kazainu Abidini.
Wako wapi waumini, waje kuihami dini,
wote wamo furahani, na wanawake nyumbani.
Wako wapi Maulama, na wenye fikira pana,
dini habari hawana, yashambuliwa na nini.
Maadui wanaranda, waje dini kuiponda,
kwa kutoona wapenda, wenye kuipenda dini.
Kila mtu mpumbavu, ajitutumua mbavu,
ati aje kuharibu, dini ya Mola Manani.

Milioni za unasi, wote dini wameasi,
hata wapita kiasi, kwa uongo na uhuni.
Misiba imewangia, kwenye zote zao njia,
haiba yao na haya, vyote vimesha wahuni.
Iwapo yote dunia, imbeuwe Rasua,
hawatashika hatua, kuingia utamboni.
Dunia wameipenda, hata hadi ya kupenda,
mali zao waziponda, kwa furaha za nyumbani.
Mikutano ya uasi, wameishika kwa kasi,
na wameipamba jinsi, imekuwa rasumini.
Wamekuwa mashuhuri, vilabuni mwa khamri,
wala hawana habari, ya wamchao Manani.
Nifanyeje Ahmadi, naona huzuni hadi,
adui kupiga hodi, na marafiki kuhuni.
Ya Rabbi Mola Manani, Usiye Chako kifani,
nakuomba niauni, niwe mbali na Motoni.
Ya Rabbi Mola Muweza, Nuru yondoayo giza,
mulika macho ya giza, yakuone Rahmani.
Rabbi ninakuarifu, kuwa mimi sina hofu,
naamini tatawafu, nishindile utamboni.
Sisi takutumikia, mimi na yangu Jamia,
kwa msadao Jalia, Utupao ufichoni.

Kwa hiyo inaonekana kuwa hali ya ujumla iliyopo leo ni ya namna ambayo ni yumkini tuwe na sio Mujaddid tu, bali zaidi kuliko Mujaddid kutoka kwa Mwenyezi Mungu; mmoja ambaye auweke tena Uislamu kwenye mwendo wake, apambane na ukafiri kila upande, na autwishe tena hoja zisizojibika, silaha za dalili. Mwanzo wa karne yetu (1835-1908), mtu mmoja tu amekuja mbele na madai ya kwamba ameteuliwa na Mwenyezi Mungu kuulinda Uislamu, naye ndiye Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Inamwajibikia kila mwenye busara na akili, akiwa mwanamume au mwanamke, kufikiria vizuri madai haya, siyo kuyakataa bila ya kufikiri vya kutosha. Kama wayakatae madai haya, wanaukataa wajibu ulio mkubwa sana. Na kwa huo wataulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

## SHAKA IMEONDOLEWA

Mwenyezi Mungu akusaidie, msomaji mpenzi, kwa msaada wake maalum! Wengi katika hatua hii wataanza mnong'ono wa shaka. Wataanza kusema kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa Mtume mkamilifu. Baada ya Mtume mkamilifu hatuna haja ya Mujaddid au Mhuishaji. Quran Tukufu ndio mhuishaji wetu na nguvu ya kiroho ya Quran Tukufu itaturudisha tena kwenye imani na hekima. Wazo hili linapendeza. Lakini linapochunguzwa sana, linaonekana linapingana na mafundisho ya Quran Tukufu na Hadithi na pia akili na ujuzi wa tangu zamani.

Wazo hili liko kinyume na Quran na Hadithi kwa vipi?

Kwa sababu mote humo tunayo ahadi iliyo dhahiri shahiri ya kufika kwa Mujaddidina na viongozi wa kiroho. Kama kufika kwa Mujaddid au Imam kulikuwa ni idhilali kwa ukamilifu wa Mtukufu Mtume s.a.w., kwa nini Mwenyezi Mungu aliahidi kufika kwa Mujaddidina na Maimam hao, baada ya kumfanya Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa Mkuu na Mbora wa Mitume wote na Mkamilifu wa watu wote? Je, Mungu alijikadhibisha mwenyewe? Je, aliweza kufanya na hapohapo tena asifanye jambo Yeye Mwenyewe? Kwa nini basi Mtukufu mtume s.a.w. alitabiri kufika kwa Mujaddidina na Maimamu? Je, tunajua zaidi kuliko alivyojua yeye? Ni nini basi ilikuwa maana ya ukamilifu wake katika utu na utume? Je, sio ajabu hii, ya kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. atuambie juu ya kuja kwa Mujaddidina na halafu tuanze kufikiri ni kinyume cha Utukufu wake?

Wazo hili ni kinyume na akili pia. Kwa sababu, kama baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. ilikuwa kusiwe na Mujaddidina wala viongozi walioteuliwa na Mwenyezi Mungu, hali ya kiroho ya Waislamu isingeharibika kiasi hiki. Waislamu wangejitosha wenyewe katika utawa na utakatifu. Lakini kwa hakika wako kinyume cha hivi. Akili tu peke yake haiwezi kujiongoza kufikiri kuwa Waislamu waanguke na kuwa wabaya zaidi na zaidi, lakini asije Mujaddid yeyote kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuwahuisha. Kama Uislamu uachwe hivihivi tu bila kutupiwa jicho, haitaonesha kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa mkamilifu zaidi katika watu

wote na manabii. Bali itaonesha kuwa Mwenyezi Mungu anataka kukomesha Uislamu. Kama Mujaddidina na Maimamu wa kiroho wakome kufika, kikomo hicho kitafuatana na thibitisho dhahiri la kupotea kwa Waislamu. Leo Waislamu ndio wangekuwa wenye nguvu ya kiroho na wenye afya kama walivyokuwa mwanzoni mwa Uislamu, katika wakati wa masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kama kuna uoza wa kiroho hivi, ni lazima tuwe na njia ya kuuondoa.

Uchunguzi mwingine unalifanya wazo hili liwe kinyume na akili. Ni kwamba kama ukamilifu wa Mtukufu Mtume s.a.w. maana yake ni kukoma kwa Maimamu wa kiroho, ambao wanamwakilisha Mtukufu Mtume s.a.w. na kuiga tabia yake na mwendo, basi kwa nini tunao duniani makhalifa wa Mwenyezi Mungu, aliye ni chanzo cha kila Ukamilifu, Qayyum na wa milele? Ukweli unaonekana kuwa zama jambo fulani linafichikana katika mawazo ya kibinadamu, tunahitaji kitu cha kutukumbusha na kutuwezesha kujifaidisha na mvuto ulioweza kuletwa na jambo hilo. Basi Mtukufu Mtume s.a.w. ni mkamilifu zaidi katika wanadamu wote na manabii. Pamoja na hayo baada yake, tunahitaji watu wa kufafanua thamani yake, waige utawa wake na kuutoa tena mwendo wake. Watu hawa watukumbushe juu yake na kuweka nguvu yake mara nyingine ulimwenguni.

Wazo hili ni kinyume na mazoea pia. Katika muda wa miaka 1300 iliyopita baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mujadddina wengi wametokea miongoni mwa Waislamu. Walipokea zawadi ya wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na wakadai kuwa waliinuliwa kwa kuuhuisha Uislamu. Mujaddidina hawa walikuwa ni mifano ya pekee katika Uislamu, na wakafanya vya kutosha katika kuueneza na kuuimarisha Uislamu. Watu hao ni Hadhrat Junaid wa Baghdad, Seyid Abdul Qadir Jilani, Sheikh Shahab-ud-Din Suhrawardi, Hadhrat Muhy-ud-Din Ibn Arabi, Hadhrat Baha-ud-Din Naqshbandi, Sheikh Ahmad wa Sirhind, Khawaja Muin-ud-Din Chisti, Hadhrat Shah WaliUllah wa Delhi na wengine (r.a.). Kwa kuwakumbuka hao wote, bila kusahau walichofanya kwa ajili ya Usialmu na Waislamu, tunawezaje kuamini kuwa baada ya Mtume s.a.w. tusiwe na Mujaddid au Imam aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu kuuhuisha Uislamu? Kwahiyo, ni wazi kuwa hata baada ya Mtukufu Mtume

s.a.w. yumkini tuwe na Mujaddidina. Tuliwapata siku zilizopita na ni budi tuwapate siku zijazo vilevile. Hali iliyopo leo ya Waislamu inalia kwa kumhitaji mmoja aliye mkuu. Kama ilivyo, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ni peke yake leo, aliyedai kuwa Mujaddid. Hii dalili inatoa hoja yenye nguvu sana kuthibitisha ukweli wake.

## HOJA YA PILI
## USHUHUDA WA MTUKUFU MTUME S.A.W.

Hoja iliyopita ilikuwa ya kwamba uliopo ndiyo wakati wa kufika Mujaddid, na kama ilivyo hakuna mwingine aliyedai kuwa ameteuliwa na Mwenyezi Mungu kwa kazi hii, yatupasa tufikiri kwa makini madai ya mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya ambaye peke yake ndiye aliyedai kuteuliwa kwa kazi hii. Kwa hali yoyote, madai ya Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya siyo tu kwamba yeye ni Mujaddid Aliyeahidiwa kwa Waislamu tangu zamani sana. Yeye ndiye Masihi na Mahdi wa bishara za zamani. Kwa kuthibitisha madai yake nitaeleza ushuhuda wenye nguvu sana wa Mtukufu Mtume s.a.w., Mfalme wa wanadamu, Mteule wa Mwenyezi Mungu. Na hakuna ushuhuda mkuu zaidi ya huu.

Itikadi juu ya kufika mara ya pili kwa Masihi imekuwa ikishikwa tangu kabla ya Uislamu. Ilikuwako karne nyingi kabla ya kudhihiri Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., kama moja wapo ya Hadithi za nabii Musa. Lakini katika Uislamu kufika mara ya pili kwa Masihi kumefundishwa kwa namna ambayo tunalazimika kukufahamu kama mojawapo ya itikadi ya maana sana katika itikadi za Kiislamu. Dalili, ambazo zimeipa nguvu itikadi hii ya Islam, ni hizi zifuatazo:

1. Masihi Aliyeahidiwa, kwa mujibu wa fundisho la Islam ilikuwa aje katika wakati uleule ambao ulielezwa kuwa wa kufika kwa Mahdi. Naam, katika Hadithi zingine, tunaambiwa kuwa Mahdi siye ila ni Masihi. Bali kuamini kwa wakati wa kudhihiri kwa Mahdi na Masihi kumewaongoza Waislamu wawe watu wa kukufahamu kuja

kwa Masihi kama kuja kwa mmoja wa umati huu, siyo kuja kwa mtu mgeni.

2. Kufika kwa Masihi kumeelezwa katika Hadithi za Kiislamu kama kufika kwa zama mpya ya maendeleo ya Islam. Ushindi wa Islam juu ya dini zingine ulitazamiwa katika wakati wa kuja kwa Masihi. Ushindi huu ulikuwa uletwe na Masihi.
3. Masihi na Mahdi kuwa mtu mmoja, kuja kwa Masihi kumeonekana kama kuja kwa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. mwenyewe, na Masahaba wa Masihi kuwa kama Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. Hali za namna hii zimejenga katika mioyo ya wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya kufika mara ya pili kwa Masihi Aliyeahidiwa.
4. Masihi Aliyeahidiwa ilikuwa afanye kazi kubwa kwa ajili ya Islam katika wakati wa shida kubwa. Wakati huo umeelezwa katika maneno ya kutisha sana ndani ya Hadithi. Wakati wa hatari isiyoepukika, ulikuwa utikise Uislamu na misingi yake; hapo ndipo Masihi aje na kuulinda Uislamu katika mashambulio ya maadui. Hali hizi zimewaongoza Waislamu kuungojea wakati wa kufika Masihi kama kufika kwa Malaika wa rehema. Je, Mtukufu Mtume s.a.w. hakusema, "Hakuna kitakachoteteresha Jamia ambayo ina mimi upande mmoja na Masihi upande wa pili"? Maneno yenye adhama kama haya yameupamba wakati wa kufika Masihi kwa ubora maalum na yamewatumainisha Waislamu matumaini makubwa. Kuja kwa Masihi ilikuwa kuupa nguvu Uislamu pande zote na kuuondoa katika mashambulio.

Dalili hizi zimekusanyika kufanya kuja kwa Masihi kuwa tukio kubwa sana katika taarikh ya Kiislamu. Tukio hili ilikuwa liwasaidie Waislamu kushuhudia tena, mfano wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. mwenyewe. Pia lilete suluhu katika Uislamu. Isingewezekana kuahidi tukio hili, na bado kusitajwe alama zitakazopatikana wakati wa kutokea kwake.

Mara kwa mara kufika kwa wasuluhishi na Wajumbe huelezwa ndani ya vitabu vya dini. Maelezo yake mara nyingi huwa katika lugha ya mfano, maelezo ya hasa huwa hayaleti kupata mtu malipo ya mbinguni. Kama alama za wakati zielezwe kwa dakika na kila

hali yake hasa, kutakuwa hakuna tofauti baina ya mwumini na kafiri. Kwa alama kama hizo, suala juu ya ama mdai fulani ni mkweli au siyo halitakuwa na maana ya kutosha. Alama za kuja kwa wahuishaji ni budi zijifiche ili kuwainua watu katika imani na shauku juu ya uchunguzi wa uaminifu. Watu wanazichungua alama na wanaweza kuufikia ukweli. Majeuri na wenye nia mbaya wanakuwa na uwezo kuona udhuru wa kutoamini kwao. Zama jua linaonekana mbinguni hakuna anayefikiri kupata thawabu kwa kuamini kuwapo kwake. Imani kama hii haina thawabu. Juu ya wahuishaji na wajumbe wa Mwenyezi Mungu makusudio ni kuongoza lakini siyo zaidi ya shabaha. Kitu cha uficho kimo ndani ya alama zao hivi kwamba ukweli wao unakanwa kwa urahisi kama unavyoweza kuthibitishwa.

Tunapofikiri juu ya bishara za wakati wa Masihi Aliyeahidiwa ni lazima tuiweke kanuni hii akilini. Bishara hizi zimo katika lugha ambazo kwazo bishara za kufika kwa wahuishaji na wajumbe zimehifadhiwa ndani ya vitabu vya dini. Kwa njia yoyote, hii haipunguzi thamani ya bishara hizo kwa watafutao ukweli. Ishara zilizotajwa katika vitabu vyenye bishara bado ni zenye kung'aa. Yule, anayeamini nabii mmoja kwa msingi wa akili, na ambaye imani yake kwa nabii huyo siyo matokeo ya kutokana na ukoo wa waaminio, anaweza kupata mwongozo wote atakao ndani ya alama hizi. Wale ambao kijuu juu tu wanaamini mamia ya manabii, lakini hawamwamini hata mmoja wao kwa njia ya akili, wataona shida kumwamini mjumbe yeyote mkweli wa Mwenyezi Mungu ijapokuwa atokee na ishara zisizo kikomo. Watu kama hawa hawana imani yao wenyewe. Imani yao wanapewa na Maulamaa, wazazi au akina babu. Tangu hawajapata kumwona nabii kimwili na hawajapata kumwamini yeyote kwa msingi wa akili, wanaona shida sana kumtambua nabii na kumwamini kwa njia ya kufikiri na kuyapima madai yake. Watu kama hao hawawezi kuona ukweli wa nabii, mpaka kwanza wasugue mboni za macho yao. Ni lazima wapanguse vumbi lililomo machoni mwao na kuacha itikadi zilizotengenezwa na watu na za upendeleo, kama wanataka kuona ukweli wa nabii mkweli.

## ISHARA ZA MASIHI NA MAHDI ALIYEAHIDIWA

Baada ya melezo hayo, ninaendelea kutoa maelezo ya Ishara za Masihi Aliyeahidiwa kama zilivyosimuliwa na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Mtu yeyote mwenye nia safi, kwa ishara hizi, hatakuwa na shida kuutambua wakati ulioteuliwa kwa kufika Masihi Aliyeahidiwa. Hata hivyo, inafaa sana tujikumbushe wenyewe kwamba zama dini ilipogawanywa katika madhehebu, watu wengi walianza kuzusha Hadithi za uongo ili kutimiza mapendekezo yao. Uzushi huu ulifanywa kwa ajili ya kuzipa nguvu itikadi za kimadhehebu. Tunasoma Hadithi; nyingi za namna hii zinazoeleza kufika kwa Mahdi na kueleza ishara za kufika kwake. Lakini maneno yaliyotumiwa ndani ya Hadithi hizi yanaonesha waziwazi kuwa yametengenezwa ili yatimize baadhi ya itikadi za kimadhehebu. Baadhi ya Hadithi hizi zinaweza kuwa za kweli au zinaweza kuwa na maneno fulani ya asili. Hata hivyo, mwenye kutafuta ukweli hana budi aangalie sana katika kuzitumia. Hadithi kama hizi zisiruhusiwe kutumiwa kama aumuzi katika kuchungua ukweli. Mathalan, Hadithi nyingi zilizokusanywa wakati wa utawala wa Bani Abbas, kijuu juu zinaeleza juu ya Mahdi na wakati wake. Lakini sababu yake hasa ni kutaka ifahamike kwa watu kuwa maasi ya nyuma yaliyotokea kwa kuwaunga mkono Waabbasi katika Khurasan yaliidhiniwa na Mwenyezi Mungu. Kusema ya kwamba Hadithi hizi zilizushwa imehakikishwa na taarikh ya baadaye. Miaka elfu moja imepita tangu Hadithi hizi zilipotimia, lakini Mahdi wa kutimiza ishara za hadithi hizo hajatokea bado ulimwenguni. Hivyohivyo kuna hadithi ambazo ishara zilizotajwa za wakati wa Mahdi zimechanganywa na maelezo ya matukio ya kale. Mpaka vyote viwili vipambanuliwe, moja na nyingine; mpaka matukio ya zamani yanayosemwa kuwa ishara za baadaye yamepambanuka na ishara za kweli za baadaye, hatuwezi kuufikia ukweli. Wale waliokuwa hawajui matukio makuu ya taarikh ya Kiislamu wamepotezwa na hadithi hizi za uzushi. Wamezifanya hadithi hizi kama ishara za baadaye na kukaa kungojea matukio yaliyokwisha tokea hata kabla ya hadithi hizi kubuniwa. Uzushi, kama nilivyosema, ulitengenezwa kwa kusaidia makusudio ya kimadhehebu. Hivyo basi, tukiwa katika kufikiri ishara za Mahdi,

ni lazima tutenge mbali kutokana na ishara za hadithi zile ambazo haziashirii kwenye matukio yaliyodhihirika. Ni kwa njia hii tu tunaweza kujiepusha mbali na shimo lililochimbwa na watu kwa ajili ya kuyapa nguvu mapendekezo yao.

Mtukufu Mtume s.a.w. aliangalia sana katika kusimulia ishara za kufika kwa Masihi na Mahdi. Alizieleza kama mnyororo mrefu uendeleao. Kama tukumbuke hivi, tunaweza kujiepusha na makosa mengi yaliyozushwa na watu. Mnyororo wa ishara hauna budi uning'inie pamoja. Chochote kilichoongezwa, kisichopatana na mnyororo, kinaweza kuonekana upesi kama kitu kigeni na cha uwongo. Mathalan, kama Mtukufu Mtume alisema kuwa Aliyeahidiwa atakuwa na jina fulani, babu yake ataitwa fulani na kadhalika, watu wengi wangeweza kuchukua majina haya na kudai kuwa katika wao ishara alizosema Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya kufika kwa Aliyeahidiwa zimetimia. Hapana shaka, Mtume s.a.w. alijiepusha na alama za aina hii; ilikuwa rahisi kwa watu wapendekezao kuzishika na kuzitimiza. Kinyume cha hayo Mtukufu Mtume s.a.w. alitaja alama ambazo haikuwezekana alama moja idhihirike pamoja na nyingine hapo kabla. Ni ishara za kungojea katika mabadiliko mbalimbali ya ulimwengu kwa mamia ya miaka. Ishara hizi, hakuna wanadamu, au makundi ya wanadamu wanaofanya kazi pamoja tangu vizazi hata vizazi, wanaoweza kuzitengeneza. Hadhari moja aliyoishika Mtume s.a.w. katika kusimulia ishara za Mahdi ni kwamba nyingine katika ishara hizi zimetajwa kuwa ishara za pekee kabisa katika wakati wa Mahdi. Zilikuwa ni ishara ambazo si za kutokea wakati wowote kabla ya kufika kwa Mahdi. Yatupasa tuongozwe na shabaha hizi zenye maana. Kama katika kufikiria ishara ambazo zimesimuliwa katika Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w., tunaona matukio mbalimbali ya dunia ambayo si katika uwezo wa mtu kuyafanya, na mabadiliko hayo na matukio yanasemwa kudhihiri wakati Mahdi, basi hatuwezi ila kufikiri kuwa wakati uliowekwa kwa kufika Masihi na Mahdi umefika. Kama, katika wakati huo, tunaambiwa ishara zingine za Mahdi ambazo hazijatokea bado, itatupasa tukubali kuwa ama ishara hizo ni uzushi uliochanganywa na watu wasiwo na unyofu wa roho; au kwamba maana ya ishara hizo imejificha; na ya kwamba ni mifano inayotakiwa kufasiriwa.

Pamoja na haya, ninapenda kusisitiza kuwa ishara zilizosimuliwa na Mtukufu Mtume s.a.w za kufika kwa Masihi na Mahdi ni lazima zichukuliwe pamoja. Haziwezi kuchukuliwa mojamoja. Ni sura ya pande nyingi, ambayo ndiyo ya kufanywa sura ya wakati wa Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa. Mathalan, inasemwa katika Hadithi kuwa ishara moja ya Mahdi ni kutoweka kwa uaminifu, na nyingine kutoweka kwa elimu. Sasa, kama ishara hizi zichukuliwe mbalimbali na kila moja ifanywe ndiyo ishara ya kufika kwa Masihi na Mahdi, tunaweza kufikiri kuwa zama uaminifu umetoweka duniani, tumtazamie Mahdi na Masihi, na zama elimu imetoweka na ujinga umejenga, tumtazamie tena Mahdi na Masihi. Huu ungekuwa upuuzi. Katika miaka 1300 iliyopita Waislamu wamekutana na mabadiliko mengi katika taarikh yao. Wakati mwingine walipoteza elimu, wakati mwingine uaminifu, lakini Mahdi au Masihi hakutokea. Hivyo, inaonekana kwamba ishara hizi si za kuchukuliwa mojamoja. Tunachopaswa kufanya ni kuzikusanya pamoja ishara zote zilizotajwa na Mtukufu Mtume s.a.w., na kuifanya sura yote kuwa sura ya wakati uliochaguliwa wa kufika Masihi. Kwa kuchukua mojamoja, ishara hizi zinaweza kuuhusu wakati mwingine, lakini kama zichukuliwe pamoja, haziwezi kuuhusu wakati mwingine ila wakati wa Masihi na Mahdi.

Ili kujua wakati, yatupasa tutumie njia zilezile tutumiazo kuwajua wanadamu. Tunapotaka kumweleza mtu asiyejulikana, ambaye hajaonwa na wengine, tunafanyaje? Tunaeleza uso wake, kimo chake, rangi yake, tabia yake, rafiki zake, ndugu na mengine. Hata tunaweza kueleza nyumba anamokaa. Tunaweza kusema mtu huyo ni mrefu, mzuri, mwenye unene wa wastani, mwenye uso mpana, pua ndefu, macho makubwa, midomo mikubwa na kidevu kikubwa. Zaidi tunaweza kusema kuwa anajua Kiarabu, kwa dini ni Mwislamu, ya kwamba jamaa zake wanamchukia na ya kwamba ni mtu mwenye tabia njema sana. Hata tunaweza kuieleza nyumba yake na nyumba zilizo jirani yake. Mtu anayeelezwa kwa ukamilifu namna hii anaweza kujulikana na kila mtu. Hapana yeyote amsakaye mtu wa namna hii anayeweza kumkosa hata kama juhudi ifanywe kuzuia msako wake. Sasa ni ishara zipi zinazoweza kutumiwa kama ishara za wakati fulani. Kama tunaweza kuashiria kwenye mambo

ya kimbinguni, mabadiliko ya ardhini, hali za siasa na ujamaa, hali ya dini, elimu, tabia; kama tunaweza kuongeza zaidi, hali ya uhusiano baina ya mataifa, hali ya uchumi, njia za uchukuzi na usafiri, basi kila atakayeziona ishara hizi, ataweza kutambua wakati unaohusiana na ishara hizo. Mara atakapouingia wakati huo, ataweza kusema kuwa wakati (uliotabiriwa), umefika. Hatakuwa na taabu yoyote. Ishara zote alizoambiwa zitamwondolea kabisa shaka juu ya wakati huo.

Hii ndiyo sababu Mtukufu Mtume s.a.w . ametoa ishara zote juu ya wakati wa Masihi na Mahdi. Alifanya hivyo ili kuzuia ushindani wa kimadhehebu usiingie katika Hadithi na kuleta mgogoro katika kujulikana wakati wa Masihi na Mahdi. Hapana shaka kwamba kumekuwako uzushi katika Hadithi lakini wazushi hao walikuwa na mawazo mafupi sana juu ya ishara zilizoelezwa na Mtukufu Mtume s.a.w. Kwahiyo uzushi wao haukuleta taabu yoyote. Mtu yeyote leo, anayezifikiri kwa makini ishara zote, hatokuwa na mashaka kwamba uliopo ndiyo wakati wa Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa.

Sasa nitaendelea kuhadithia ishara zilizosemwa na Mtukufu Mtume s.a.w. Itaonekana wazi, hivi nikiendelea, ya kwamba Masihi hangeweza kufika katika wakati mwingine ghairi ya huu.

## HALI YA DINI KWA UJUMLA.

Ishara ya kwanza ninayopenda kueleza ni juu ya hali ya dini. Hali ya dini kwa wakati wowote inaweza kuelezwa ama kwa hali ya uwiano. (Ni watu wangapi wako dini moja au nyingine?) Au, inaweza kuelezwa kwa kutaja nguvu ya mafundisho ya dini kwa wafuasi wake. Mtukufu Mtume s.a.w. alitumia njia zote mbili katika kueleza hali ya dini wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Sehemu ya uwiano ya maelezo ya Mtukufu Mtume s.a.w. iko wazi sana. Mtume s.a.w. alisema ya kuwa katika wakati huo wa kuja mara ya pili kwa Masihi, Ukristo utakuwa na nguvu. Katika Kitabu cha Hadithi

kiitwacho Muslim, inasemwa kwamba siku ya Kiyama watu wengi watakuwa Warumi, ambao katika mwito wa Kiislamu maana yake ni Wakristo. Katika wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w., Warumi walikuwa ndio watazwa (alama) wa Ukristo, na chombo cha maendeleo yake. Ishara hii imejaa maana kubwa. Mtume s.a.w. alisema pia:

"Anapokufa Kisra, hakuna Kisra baada yake.Hivyohivyo anapokufa Kaisar, hakuna Kaisar baada yake. Halafu mtatumia hazina zao katika njia ya Mwenyezi Mungu" (Tirmidh - Abwabul Fitan).

Hapa Mtukufu Mtume s.a.w. alitabiri juu ya kuanguka kwa dola ya Warumi, na kutoweka kwa laqabu za wafalme wao. Kama baada ya maanguko ya dola ya Warumi, Wakristo ilikuwa wainuke tena na kuwa wenye nguvu wa dunia, ni lazima yawe maendeleo yasiyo ya kawaida katika taarikh. Na bado ndiyo maendeleo yaliyotajwa kama ishara ya wakati ulioahidiwa. Utawala wa Ukristo baada ya kuanguka kwake, kusikodhaniwa kama ilivyokuwa, unaonekana uliotabiriwa zamani. Bishara hii ilitimia barabara. Utawala wa Kaisar ulitoweka sawa na bishara. Kwa muda fulani laqabu ya 'Kaisar' iliendelea. Wafalme wa mwisho wa Constantinople walijiita Makaisar. Kwa kuanguka Constantinople laqabu hii pia ilitoweka. Islam ikashika nafasi ya Ukristo katika sehemu zote za dunia iliyojulikana wakati huo. Karne kumi baada ya Hijra mwanguko wa Islam ukaanza. Ukristo ukaanza kusimama tena katika nchi ambazo ulikuwa haujulikani kabisa wakati wa bishara ya Mtukufu Mtume s.a.w. Sasa kwa miaka 100 iliyopita mataifa ya Ukristo yametawala dunia ili kwamba bishara ya Mtukufu Mtume s.a.w. "ardhi itakuwa chini ya Warumi" iweze kusemwa imetimia barabara.

Bishara hii ina maana kwa sababu nyingine. Baadhi wa Maulamaa wa Kiislamu wamesema kuwa - kuinuka kwa Ukristo - itakuwa ya mwisho kutokea miongoni mwa ishara za wakati uliochaguliwa. Hivyo, Nawab Siddiq Hassan Khan, katika kitabu chake Hujajul Karaamah, akitaja maneno ya kitabu kingine, Risala-i-Hashriyya, ameandika:

"Zama ishara zote zitakapokwisha kutokea, hapo Wakristo watainuka na kusimamisha utawala wao katika sehemu karibu zote za dunia'. (Hujajul Karaamah uk. 344).

Kwahiyo, inaonekana kuwa bishara ya utawala wa Ukristo siyo ishara tu miongoni mwa ishara bali ishara ya maana maalumu. Ni ishara ambayo, kwa maoni ya baadhi ya Maulamaa wa Kiislamu, ilikuwa ya kumaliza sura yote ya wakati wa Masihi Aliyeahidiwa.

## HALI YA WAISLAMU KWA UJUMLA

Ni gani ilikuwa iwe hali ya Waislamu? Kwa maneno ya Mtukufu Mtume s.a.w., "Wakati huo Islam itakuwa dhaifu sana na maskini" (Ibn Maajah). Ilikuwa ije kuwa dini ya maskini. Katika bishara inayomhusu Dajjal, Mtume s.a.w., amesema kuwa Waislamu watakuwa wafuasi wa Dajjal (mataifa ya Kikristo). Sehemu hii ya bishara (iliyomo katika Tirmidh) imetimia sawasawa. Waislamu walikuwa na siku zao za utukufu. Kulikuwako wakati ambao walikuwa peke yao wenye nguvu duniani. Leo wako kama mayatima. Mpaka nguvu nyingine miongoni mwa Wakristo ije kuwasaidia, Waislamu hawawezi kujisaidia. Mamia ya maelfu ya Waislamu wameingia Ukristo. Na mnyororo huu unaendela.

Hali ya ndani ya dini imeelezwa wazi katika bishara za Mtukufu Mtume s.a.w. Hali ya Waislamu walioshika imani ya Uislamu, imeelezwa kwa ukamilifu. Mathalan, imesemwa, ya kuwa Waislamu, wakati huo, hawataamini tena Kadri ya Mwenyezi Mungu. Kwa maelezo ya Hadhrat Ali, Mtukufu Mtume s.a.w. alisema ya kuwa siku ya Kiyama itaoneshwa kwa ishara ya watu kutoamini Kadri ya Mungu. Kutoamini huku kwa Kadri, kwa hakika maana yake ni kutoamini kwa Waislamu. Wafuasi wa dini zingine walikwisha kuwa wakanaji wa Kadri ya Mungu toka zamani. Ukanaji wa Kadri sasa umeenea sana kwa Waislamu. Mvuto wa elimu za kisasa umekuwa na nguvu sana katika ukanaji wa Kadri. Hata

waandishi duni sana wa Ulaya wanaweza kuwaogofya wasomaji wa Kiislamu ambao wanaonekana tayari kukana ubora wa Kadri. Waislamu wamevurugika kabisa juu ya suala hili. Ubora wake umepotea kabisa kwao.

Ishara ya pili ya hali ya dini ni Waislamu kutojali amri ya Zaka. Sehemu hii ya bishara imesimuliwa na Hadhrat Ali na imepokelewa na Albazzar, nayo imetimia barabra. Wakati huu Waislamu wako mashakani. Wamekuwa wapokeaji wa kila namna ya taabu. Katika wakati kama huu ni wajibu wao kutoa sadaka za kujitolea kwa kuinua jamia. Lakini wachilia mbali sadaka za kujitolea, wamekuwa mabahili wa kutoa Zaka ambayo kwa Waislamu ni sadaka ya lazima. Katika nchi nyingine za Kiislamu Zaka inajulikana chini ya sheria za serikali. Waislamu wengi katika nchi hizo wanalipa zaka, lakini siyo kwa hiyari. Mahali ambapo Zaka haikutiwa katika sheria za serikali, Waislamu wachache sana wanalipa. Makundi mengine ya Waislamu wanalipa kwa hiyari, lakini siyo katika njia iliyo sawa. Wanalipa Zaka kana kwamba ni kazi ya watu fulani kwa ajili ya wengine.

Badiliko la maana katika hali ya tabia ya Waislamu ambalo Mtume s.a.w. ametaja ni mapenzi yao ya dunia. Watu ambao waliweza kutoa wakfu vitu vilivyo vipenzi sana kwao, ambao machoni pao vitu vya dunia hii vilikuwa si chochote zaidi ya mzoga ilikuwa wabadilike hata wawe tayari kuiuza dini yao kwa ajili ya dunia. Badiliko hili ambalo Mtume s.a.w. alitabiri liko wazi, hivi kwamba wale waliobakiwa na mapenzi yoyote ya Islam, hawawezi kulitazama kwa utulivu. Badiliko hili linaonekana limewasoza Waislamu wa aina zote, Masheikh, Waalimu, matajiri na maskini. Wote wanaonekana kuitanguliza dunia juu ya dini yao. Kwa ajili ya manufaa ya kidunia, wanakuwa tayari kutupilia mbali maslahi ya dini na taifa lao.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w., ambalo limepokelewa na Ibn Abbas kwa maelezo ya Ibn Mardwaih, ni kutoweka kwa Sala tano. Badiliko hili sasa liko wazi vilevile. Kama uchunguzi ufanywe, mtu anaweza kusema kuwa kwa shida sana mtu mmoja katika mia moja ya Waislamu anasimamisha Sala tano kila siku, na hali sala tano ndiyo ya kwanza katika faradhi za

Islam. Kwa rai ya baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu, wale wasiosali Sala tano kila siku, ni makafiri. Leo misikiti imejaa tele, lakini Waislamu wachache tu wanafika humu kwa ajili ya Sala tano. Misikiti imetumiwa kama mazizi. Kwa ujumla Waislamu wameacha kabisa kuitumia misikiti kama nyumba za ibada.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni haraka watakayotumia wataabadi katika Sala zao. Kwa maelezo ya Ibn Masud, Mtume s.a.w. (kama ilivyopokelewa na Abu Shaikh katika Ishaat) alisema, ya kwamba wakati utafika ambao watu hamsini watasali pamoja na hata mmoja wao hatakubaliwa Sala yake na Mwenyezi Mungu. Watasali kwa sura ya nje tu na kwa haraka sana. Ama Sala fulani inakubaliwa au la, hakuna ajuaye. Alama moja ya nje, kwa hali yoyote, inayofanya Sala isikubaliwe ni haraka iliyopita kiasi. Mtu fulani alisali kwa haraka sana. Mtukufu Mtume s.a.w. alimwona, akamwambia asali tena. Waislamu wanaosali sala tano, wanasali kwa haraka ajabu. Sijdah zinazofuatana haraka, zinaonekana kama mdono wa kuku. Baada ya sala, wanakaa kwa muda mrefu wakiimba dua fulani fulani na kuvuta nyiradi zilizobuniwa.

Ishara nyingine iliyotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni "kutoweka" kwa Quran Tukufu. Ilikuwa itoweke roho yake. Maneno ya Kitabu Kitukufu yalikuwa yabakie salama. Alama hii iko dhahiri leo. Quran Tukufu inaweza kuonwa katika kila nyumba. Hata inasomwa pia, lakini wachache wanaosoma kwa kuelewa maana yake. Ni ajabu na ni kweli pia, ya kwamba isipokuwa miongoni mwa wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Quran Tukufu haisomwi kwa makusudio haya na Waislamu. Masheikh, Mafuqahaa na wataalamu wa Hadithi, hawana shauku ya kusoma na kujifunza tafsiri wa Quran Tukufu. Wanadhani ni marufuku kuchimbua maana ya Kitabu Kitakatifu na wanafikiri ni kosa kujaribu kupatanisha mafundisho yake na hali mpya. Katika mawazo yao, neno la mwisho limekwisha semwa na mufasirina hao. Inastaajabisha. Kwani, tafsiri ya Quran Tukufu imekuwa ikitolewa hata baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hakuna sababu kwa nini isitolewe sasa pia.

Ishara nyingine iliyotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w.(Ibn Mardwaih kwa upokezi wa Ibn Abbas), ni kwamba katika wakati

wa Masihi Aliyeahidiwa heshima ya nje itayooneshwa kwa Quran Tukufu itakiuka heshima ya maana yake na mafundisho. Kitabu Kitukufu kitakafiniwa kwa dhahabu na fedha. Ishara hii iko wazi sana siku hizi. Waislamu hawaifuati Quran. Ni taabu hata kuifunuwa na kuisoma, lakini wanajali sana kuitilia majalada ya dhahabu na atlasi na kuitunza vizuri sana katika rafu. Heshima ya nje juu ya Quran Tukufu iliyooneshwa na Waislamu wa zamani haiko wazi sana, na hali Waislamu wa zamani walikuwa na fadhila kwa utawa na utajiri juu ya Waislamu wa leo.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni mapambo ya nje yaliyopita kiasi juu ya misikiti. Tena, alama hii i wazi. Kwa kuwaiga watu wengine, hususan Wakristo, Waislamu wanachukua taklifu kubwa kwa kuiremba misikiti yao. Wanatoa maua na mapambo kadha wa kadha kwa ajili ya kuta na kuweka thurea na vifaa chungu nzima vya gharama kubwa kubwa kwa ajili ya dari. Kadhalika wanaweka pazia. Vyote hivi vinafanya misikiti ya Waislamu ionekane zaidi kama mahekalu ya ibada za masanamu, kuliko kama nyumba za ibada ya Kiislamu.

Badiliko lingine linahusiana na watu wa Bara Arabu. Kwa mujibu wa bishara Waarabu ilikuwa wawe mbali na Uislamu wa kweli, na hii inaweza kuonekana ajabu sana. Naam, Dini ya Islam ilishuka kwa Waarabu. Wafuasi wake wa kwanza walikuwa Waarabu. Ilienezwa nje ya Bara Arabu na Waarabu. Kitabu cha Islam kilishuka katika lugha ya Waarabu. Mpaka sasa kinasomwa na kuandikwa katika lugha hiyohiyo ya Kiarabu, na lugha ile i hai kwa sababu ni lugha ya Kitabu cha Islam. Nani aliweza kufikiri ya kuwa katika mataifa yote, Waarabu wangeachilia mbali Uislamu, na licha ya elimu yao ya lugha ya Kiarabu wangekuja kuwa wasiojua Kiarabu cha Quran kama vile watu wasio Waarabu ambao hawawezi kusoma Kiarabu cha Quran? Kwa maelezo ya Dailami, Hadhrat Ali amesimulia ya kuwa Mtume s.a.w. alisema kuwa katika Akhir Zaman, Waarabu watasema Kiarabu lakini akili yao na roho vitakuwa kama vya watu wasio Waarabu. Dini ya Islam haitakuwa mioyoni mwao. Badiliko hili liko dhahiri, Waarabu leo ni wageni wa Uislamu kwa kadiri ileile walivyo wasio Waarabu ambao hawawezi kusoma na kuelewa Kiarabu cha Quran.

Badiliko kubwa alililotabiri Mtume s.a.w. juu ya hali ya Waislamu linahusu uhuru wa dini katika Bara Arabu. Kwa mujibu wa bishara hii, Bara Arabu ilikuwa ije kuwa nchi ya udhia sana kwa mtu yeyote mjuzi wa maana kuinuka na kufanya kazi kwa ajili ya kutia nguvu dini. Kama ilivyopokelewa na Dailami, Hadhrat Ali anasimulia kuwa Mtume s.a.w. alisema kuwa katika Bara Arabu watu wenye makusudio mema na dhana njema watajificha na watajirudisha nyuma. Badiliko hili la mastaajabu linaweza kuonekana leo katika Bara Arabu. Utii wa dini umetoweka katika nchi hizi. Mapenzi ya itikadi zao za kipagani na mila yamekuwa na nguvu tena. Wale ambao wanamwamini Mwenyezi Mungu na wanapenda kufasiri mafundisho yao wao wenyewe, hawako salama. Ugonjwa huu umeenea katika nchi zingine pia za Waislamu, lakini wa mastaajabu zaidi ni wa Bara Arabu kwani Bara Arabu ni Markaz ya Islam. Haj ya kila mwaka iliyolazimishwa kwa Waislamu ni lazima itimizwe kwa kwenda Bara Arabu. Kutojali huku katika Bara Arabu kunaathiri Waislamu wa nchi nyingine. Inaelekea kwa sababu ya kuzuia mahaba ya kweli ya dini. Waislamu wa madhehebu mbalimbali bado wanakwenda Bara Arabu kutimiza faradhi ya Hija, lakini kama wamo katika itikadi ya wachache au isiyokubalika na Waarabu, hawana budi wahiji kwa kimya na kurudi. Laiti watu wa Bara Arabu wangetambua madaraka yao haya ya pekee! Laiti wangeushika Uislamu kwa juu sana kama walivyofanya zaidi ya miaka 1300 iliyopita!

## HALI YA TABIA

Baada ya hali ya dini ninaendelea kueleza hali ya tabia kama ilivyotabiriwa na Mtukufu mtume s.a.w. Ishara moja inayohusu hali ya tabia katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa ni kuongezeka zinaa. Zinaa ilikuwa ije kuwa kwa wingi hivi kwamba badala ya kuona soni watu watajivuna kwa kuwa wazinzi. Kwa maelezo ya Ibn Abi Shaiba, moja wapo ya ishara ya siku ya Kiyama ni mwongezeko wa zinaa (Hujajul-Karaamah). Hivyohivyo, kwa maelezo ya Anas Ibn Malik, kama ilivyopokelewa katika Muslim,

mojawapo ya ishara za Akhir Zaman ni mwongezeko wa zinaa. Abu Huraira kwa upokezi wa Ibn Mardwaih anasimulia kuwa mojawapo ya bishara alizotoa Mtume s.a.w. kuhusu Akhir zaman ni kuongezeka kwa watoto wa haramu (Hujajul Karaamah). Zinaa leo iko dhahiri shahiri. Madhambi ya zinaa yamejaa tele. Vitendo ambavyo Uislamu unavilaani kuwa ni vitendo vichafu, sasa vinaonekana kama tabia njema. Densi, kusifia uzuri wa wanawake, kutumia siku za mapumziko na wanawake wageni, vimekuwa vitendo mashuhuri, siku hizi. Mpaka wakati huu mambo haya hayakujulikana kila sehemu. Hayakujulikana katika Bara Arabu wala nchi zingine. India haikufahamu habari za Mungu Mmoja, lakini haikukumbwa na uzinzi. Iran ilikuwa nchi iliyopenda sana anasa, lakini haikutekwa na tamaa ya uzinzi. Warumi wa kwanza, waliokuwa sababu kubwa ya nguvu ya Ukristo, kwa tabia walikuwa washenzi, lakini hawakuwa na tabia ya uzinzi. Lakini ni nini tuonacho leo? Kama sura ya mambo ya kweli yaliyoko leo ingeoneshwa katika siku za kale, hakuna ambaye angeisadiki. Hakuna ambaye angeamini kuwa zinaa ingefanywa kwa kadiri hii katika jina la ustaarabu. Ngoma na starehe vilikuwako hata zamani, lakini hakuna ambaye alifikiri kuwa wanawake wa jamaa nzuri wangecheza densi kwa kadiri kama hii. Hakuna ambaye angedhani ya kuwa kucheza ngoma kungefanywa kuwa ndiyo madaha ya mwanamke, chanzo cha ufahari, na siyo tabia mbaya. Dhambi mbaya kuliko zote za kimwili - uasherati - leo inazidi kuongezeka. Imeenea kwa kadiri kubwa, (na zaidi katika nchi za Ukristo), hivi kwamba ni shida kufikiriwa kuwa dhambi. Inafikiriwa kuwa kazi ya umbile tu. Naam, kulikuwako wazinzi hata kabla. Lakini hakuna aliyeweza kufikiri kuwa wazinzi watakuja ajiriwa kwa mishahara mikubwa na kuwekwa katika makambi ya maaskari na kuwatumikia askari wakiwakidhia tamaa zao za mwili. Hakuna ambaye alifikiri kuwa uhusiano baina ya mwanamume na mwanamke ungekuwa kiasi kama hiki hivi kwamba mwanamume na mwanamke wasiojuana hawatajiona wageni kila mmoja kwa mwenzake. Na ya kwamba utaanza kufikiriwa kama sehemu ya maana sana ya uhuru wa mwanadamu. Kwa upande mwingine ndoa itaanza kuelezwa kama utumwa. Mamia ya maelfu ya watu katika Ulaya na Amerika

wanaonekana wakiwa na fikara hii. Mpaka leo, nani aliweza hata kufikiri kwamba wakati utafika ambao watu wangejadiliana vikali wakipinga kuwa ndoa si desturi ya kibinadamu? Mwanamke amekuwa chombo cha kumzalia watoto mwanamume yeyote ampendaye. Ni nani aliweza kufikiri kuwa watoto, ama wazaliwe ndani au nje ya ndoa ni shauri bora? Bali katika nchi za wasoshalisti, hususa nchi za wakomunisti, wanawake wanahimizwa kuzaa watoto ovyo ili kuongeza idadi ya wananchi.

Hii kuwa ndiyo hali za tamaa ya kimwili, mtu anaweza kupima ni kubwa kiasi gani lazima iwe idadi ya watoto wa haramu. Mahali ambapo uhusiano wa tamaa za kimwili nje ya ndoa unafikiriwa kuwa ni dhambi, watu hawapendi kuacha nyuma yao watoto wa haramu. Lakini zama jamia imeghafilika na madhambi, zama ndoa inafikiriwa kama jambo lisiloeleweka kwa upande wa dini, hakuwezi kuwa na soni kuzaa watoto wowote wa haramu. Kwa kweli, zama mambo yanakuwa kama hivi, halali inakuwa jambo lililotengwa kuliko kuwa sheria. Wale wasiojali dhambi za uzinzi, hawachelei kuzaa watoto kwa njia hiyo. Watoto wa halali wanapatikana wachache katika nchi zenye mawazo kama hayo!

Kwa hali yoyote, sauti nyingi zinatolewa kwa kuunga mkono uhusiano wa ndoa. Lakini pia kuna tabia ya kupendelea watoto wa haramu. Mafilosofa na wataalamu wanaandika kwa niaba yao na kueleza kuwa ni sehemu ya utajiri wa kila nchi na ni njia ya kuilinda. Au wanajaribu kushawishi kila serikali kuwafikiria watoto wa haramu kama watoto wao. Katika kipimo hiki cha dhambi ya zinaa, mtu anaweza kuona ni kubwa kiasi gani budi iwe idadi ya watoto wa haramu duniani. Hatuwezi kuona mfano wake katika taarikh ya kale. Hakuna ambaye aliweza kufikiria hali kama hii.

Badiliko la tabia juu ya wakati wa kufika Masihi Aliyeahidiwa lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni mwongezeko katika kutumia pombe. Kwa maelezo ya Anas bin Malik (Muslim), mojawapo ya alama za Akhir zaman ni utumiaji uliopita kiasi wa pombe. Hivyohivyo Abu Naim amesimulia, kwa upokezi wa Huzaifa bin Al-Yamaan, ya kwamba moja wapo ya alama ya Saa, kwa usemi wa Mtume s.a.w., ni unywaji wa pombe barabarani (Hilya). Kiasi

ambacho pombe inatumiwa leo hakuna haja ya uhakikisho zaidi. Katika nchi za Ulaya pombe inanywewa zaidi kuliko maji. Pombe ilitumiwa hapo zamani lakini kama tu chanzo cha kujiburudisha au kama dawa. Lakini sasa katika sehemu kubwa ya dunia inatumiwa kama kinywaji cha kawaida wakati wa chakula au wakati mwingine. Ishara iliyotiliwa mkazo na Mtukufu Mtume s.a.w. ya kwamba pombe itakuja nywewa barabarani inaupambanua wakati huu na nyakati nyingine zote. Katika nyakati nyingine pombe ilikuwa ni kiburudisho kwa watu wachache, siyo kwa kila mtu. Ilikuwa ikitolewa mahali maalum. Lakini sasa imekuwa kinywaji kikubwa. Hivyo, inatolewa mwahala mwote na kwa wingi sana kwa ajili ya wote. Katika nchi za Ulaya vilabu vya pombe viko hatua chache kimoja baada ya kingine ili kwamba watu wasiwe na haja ya kwenda masafa marefu wakitafuta mahala wanapoweza kununua pombe wakanywa. Katika magari ya moshi vyumba vya kulia chakula vimejaza pombe tele. Katika sehemu kama London pombe na maji pengine huuzwa kwa bei moja. Hakuna anayehitaji maji kwa ajili ya kunywa. Maji yanahitajiwa kwa matumizi mengine tu. Hapa ninakumbuka aliyoyaona mmoja wa Wabashiri wetu katika nchi za Ulaya. Mbashiri huyu alimvuta sana mwenyeji wake kwa tabia yake njema na ubashashi. Siku moja mwenyeji wake akamwambia "Kumbuka shauri langu - litakusaidia kukuweka katika afya njema. Usinywe maji hata kidogo ukiwa katika nchi hii. Baba yangu alijaribu kunywa maji mara moja tu katika maisha yake na hakukawia kufariki. Mimi nimeng'amka. Sijagusa maji mpaka leo." Mwenyeji huyu alipojibiwa na Mbashiri wetu kuwa hakupata kunywa pombe bali maji tu, alishtuka na akaona vigumu kusadiki!

Badiliko lingine kubwa linalohusu wakati wa Saa lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni mwongezeko wa kamari. Imepokelewa na Hadhrat Ali na ikasimuliwa na Dailami ya kwamba mojawapo ya ishara za Siku ya Kiyama ni mwongezeko wa kamari. Badiliko hili kubwa pia liko wazi. Katika nchi za Ulaya na Amerika kamari siyo tu ni mchezo. Bali ni sehemu na bahasha ya maisha ya miji mikubwa. Katika kila hatua ya maisha kamari inayo nafasi. Ni kawaida hasa kuchezea fedha kwa kamari baada ya karamu za chakula, lakini hii siyo basi. Mifuto ya *bahati nasibu* (kamari)

imeenea sana hivi kwamba inaweza kuwa karibu robo moja ya mali ambayo ingetumiwa katika biashara inatumiwa katika kamari. Watu wa daraja zote, maskini na matajiri, wanaingia katika hiyo, na wanafanya hivyo si kwa siku fulani bali karibu kila siku. Vilabu vyenye kufanikiwa zaidi ni vile ambavyo ndani yake kamari inaendeshwa. Katika Monte Carlo, markaz (kituo) ya kamari katika Italia, pengine milioni nyingi za pauni zinatoka mikononi mwa watu na kuingia mikononi mwa wengine kwa usiku mmoja tu. Dhambi ya kamari imeenea mno hivi kwamba ni shida kuutambua ustaarabu wa kisasa bila ya kitendo hicho. Naam, kamari ilipatikana hata katika siku za kale, lakini hakuna kulingana kati ya zamani na sasa. Pengine mwaka mzima wa kamari hapo zamani unaweza kuwa mdogo sana sana ukilinganishwa na siku moja ya kamari kwa sasa. Sura nyingi za bima ya maisha, ya moto, ya kuibiwa na kadha wa kadha, zimevumbuliwa. Hapo zamani watu hawakujua hata majina ya bima hizi, lakini leo zimekuwa ndiyo lazima.

Badiliko lingine kubwa lililotabiriwa na Mtume s.a.w. kuhusu hali ya tabia wakati wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni kutoweka kwa 'Nafs Zukiyyah', kama ilivyosimuliwa na Naim bin Hammaad kutoka kwa Ammaar bin Yaasir (Hujajul-Karaamah). Ni msiba, lakini ni kweli. Watu wamejaribu kuyaeleza kwa namna nyingi. Bali inabakia kama ishara ya maana sana ya Saa. Ina maana kwamba wakati wa Masihi Aliyeahidiwa watu wema, wale ambao wako tayari kumtii Mola wao, watakuwa ghali sana. Tunaweza hasa kuona badiliko hili tayari. Nje ya wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. watu watawa, watu wanaofuata mwongozo wa mbingu, wamekuwa wachache sana. Kulikuwako wakati ambao jamia za Kiislamu zilikuwa na mamia ya maelfu ya watu walioweza kusemwa kama wacha-Mungu. Lakini kama tuwatafute leo, zama haja yetu ya watu hao ni kubwa sana, ni taabu kumpata hata mmoja. Hapana shaka tunao wanazuoni wa urithi maimamu na masufi. Wafuasi wao wamo katika mamilioni, lakini hakuna hata mmoja wao mwenye maungano hasa na Mwenyezi Mungu. Wanatumia saa nyingi wakisoma uradi na dhikri za hadharani. Lakini kusoma soma uradi na dhikri hizi zio usafi wa roho. Alama ya usafi wa ndani ni kuzama katika mapenzi ya Mwenyezi Mungu, mbizi itakayoleta ishara mpya za mapenzi

kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tumwone Mwenyezi Mungu akija kuwasaidia anaowapenda. Tumwone akiwasimamia kwa ushindi wao, akiwafunulia siri za Kitabu Kitukufu na kuwazawadia lundo la elimu za kiroho. Wale, wanaompenda Mwenyezi Mungu na wanaopendwa naye, wangepigana vita ya Islam, na kuondoa taabu zinazowakabili Waislamu, na kuwaponya maradhi yao. Lakini kundi lote la Maulamaa, Madarweshi, Masheikh na wataabadi, haliwezi kutoa hata mmoja wa sifa hizi. Kwa ufupi, wema wa kibinadamu umekufa kabisa. Badala yake, tunao ufalme wa matamanio mabaya. Masheikh na wanazuoni wanafukuzia matamanio yao zaidi kuliko ucha-Mungu.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni kutoweka kwa uadilifu. Hadhrat Ali (kwa usemi wa Dailami) anapokelewa kusimulia ya kuwa ishara moja ya Siku ya Kiyama ni kutoweka kwa uadilifu (Hujajul Karaamah). Hali hii ya kutoweka uadilifu leo iko wazi kila mahali. Haina haja ya kazi kubwa wala ushuhuda zaidi. Leo, kila mtaa, kila mji, na kila nyumba, inaweza kushuhudia mfano wa kutokuwa na uadilifu.

Badiliko lingine la tabia lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni kwamba heshima kwa wazazi itapunguwa na heshima kwa marafiki itaongezeka, (imesimuliwa na Abu Naim katika Hilya, kwa upokezi wa Huzaif bin Al-Yamaan). Wakati ambao bishara inasema kwao, ulikuwa uoneshwe kwa wazazi kutotiiwa na watoto wao. Na heshima kwa marafiki ilikuwa iongezeke. Badiliko hili liko wazi kwa nguvu sana hivi kwamba watu wote wastahiki wanasumbuliwa na yale wayaonayo. Wapenzi wa tabia za kimagharibi na walioelimishwa elimu za Kimagharibi, vijana wa leo, wanawaona wazazi wao na ndugu zao kama washenzi na wajinga. Wanachukia kujumuika nao na badala yake wanapenda kutumia wakati wao wakiwa na rafiki zao wanaofuata mwendo wa Kimagharibi. Wanatumia wakati wao katika mazungumzo ya ufasiki na wakifanyiana mambo machafu. Vijana wanawapokea na wako tayari kuzungumza na rafiki zao na kusahau shida za wazazi wao maskini. Katika nchi yetu wanaweza kuonwa maelfu ya wazazi wanaoishi kwa taabu sana. Walifanya kazi kwa ajili ya kumaliza elimu ya watoto wao. Lakini watoto walipokuwa na kuanza kuchuma,

wakaanza kuwadharau wazazi wao, wakifikiri ni aibu kuwafanya kama ni sawa nao, na kuwafanya kama kwamba walikuwa watumishi wao. Mifano ya tabia hii ya dharau ya watoto kwa wazazi wao inaweza kuonwa kwa maelfu. Hapo kale ilikuwa hakuna.

## HALI YA ELIMU YA DINI

Vilevile Mtume s.a.w. alieleza hali ya elimu katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Inasimuliwa katika Tirmidh kwa upokezi wa Anas bin Maalik), ya kwamba Mtume s.a.w. alisema ya kuwa mojawapo ya ishara za Saa ni kutoweka elimu na kukithiri ujinga. Bila ya kubadilika sana, upokezi huu umo katika Bukhari pia. Badiliko hili - kutoweka elimu (ya dini) leo liko wazi kabisa. Kulikuwako wakati ambao hata wanawake waliweza kuwa na elimu kubwa ya fik'ha. Safari moja Hadhrat Umar alisema ya kwamba wanawake wa Madina walimpita yeye katika elimu ya Quran Tukufu. Wanawake na watoto walijua Quran Tukufu vizuri sana hivi kwamba waliweza kutoa makosa hukumu za Masheikh. Walitoa makosa fatwa zao, siyo kwa ujinga, au utovu wa adabu, bali kwa msingi wa elimu na kwa manufaa ya watu wote. Bibi Aisha alikuwa mmoja wa wanazuoni wakubwa waliopata kuishi. Elimu yake na uamuzi wake ulikuwa wa juu. Ukweli huu haujapata kuhojiwa. Lakini leo elimu ya dini inachukuliwa na wale ambao kwa kukosa njia au akili, hawawezi kupata elimu ya kidunia. Elimu ya dini leo inachukuliwa na wale wasioweza kupata elimu ya desturi, ambao wanaipata kwa sababu kupatikana kwake kwa uchache kunawawezesha wao kuwa Masheikh, na kupata riziki kwa urahisi. Elimu ya namna hii ina faida kidogo tu na wale wanaoifuata hawafai kwa walimwengu.

Hadithi inayotabiri kutoweka kwa elimu inaungwa mkono na Hadithi nyingine. "Elimu" katika Hadithi hizi maana yake ni elimu ya dini. Elimu ya aina nyingine ni jambo jingine. Katika vitabu vya

Hadithi, tunazo bishara juu ya kuongezeka kwa elimu kama hizo. Tirmidhi amesimulia, kwa upokezi wa Abu Huraira, ya kwamba katika Akhir zaman watu watapta sana elimu hata watapata taklifu kwa kuipata. Hivi ndivyo hasa ilivyo leo. Elimu na maarifa ya kidunia yameendelea sana hivi kwamba kila mtu amejawa mshangao. Kwa upande mwingine elimu na maarifa ya dini yamepungua sana hivi kwamba wajinga wanajisingizia kuwa wanazuoni na waalimu.

## HALI YA UJAMAA

Matukufu Mtyum s.a.w. alieleza hali ya ujamaa pia katika wakati wa Masihi. Ametaja ishara ambazo zikikusanywa pamoja zinatupa sura halisi ya hali za ujamaa katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Mojawapo ya mabadiliko ya ujamaa yaliyoelezwa na Mtume s.a.w. ni badiliko la njia ya kuamkiana iliyofundishwa kwa Waislamu. Kwa upokezi wa Imam Ahmad kutoka Mu'aaz bin Anas, ishara moja ya maana juu ya mwanguko na uoza wa Waislamu ni kutoweka amkizi la Kiislamu "Assalaamu Alaikum" na kudhihiri aina za maamkizi zinazotumiwa na Waislamu kama sura ya kulaaniana. Mufasirina wamedhani ya kuwa badiliko hili linawahusu watu wa daraja za chini kati ya Waislamu. Kwa Hadithi hiyo, Waislamu wa aina hii - wanapokutana - watajilaani wenyewe kwa wenyewe wala hawatatumia amkizi la Kiislamu, "Salaam." Lakini badiliko hili halionekani kwa watu wa daraja fulani tu. Kwa kweli, badiliko hili limeathiri watu mashuhuri kati ya Waislamu, waziwazi kuliko watu wengine. Waislamu mashuhuri katika sehemu nyingi za India wanasema Bandagi, au Taslim au Adab badala ya Salaam (kama shikamoo katika Waswahili. *Mfasiri*). Wanaona udhia kutumia amkizi la Kiislamu. Sasa, Bandagi ni amkizi la Kibaniani ambalo maana yake ni kujiweka chini kama mtumwa. Hii ni kinyume na heshima ya mwanadamu, na hasa ni kinyume na tamko na kiini cha amkizi la Kiilsamu - Salaam. Amkizi hili la Kibaniani lililoigwa na Waislamu linawafanya wanadamu kama washirika wa Mungu na kutumia laqabu ambazo zingetumiwa kwa ajili ya Mungu.

Wanaendelea kujilaani kwa kupeana sifa ya kiungu wenyewe kwa wenyewe. Amkizi la Adab, lionekanavyo kijuu juu kama la upole, lina tofauti kidogo. Amkizi hili linakwepa tu lile amkizi hasa la Kibaniani la Bandagi au Taslim. Kazi yake ni kupunguza kosa linalotokea kwa kutumia amkizi lisilo la Kiislamu.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni kwamba wakati huo heshima itapewa wale tu wenye hali za juu katika utajiri au katika siasa, siyo katika elimu au ucha-Mungu. Ibn Mardwaih amesimulia, kwa upokezi wa Ibn Abbas, ya kwamba Mtume s.a.w. alisema ya kuwa mojawapo ya ishara za Kiyama itakuwa heshima zaidi itakayoneshwa matajiri. Badiliko hili liko dhahiri. Wakati ulikuwako ambao heshima ilitolewa kwa mkubwa wa ukoo. Sasa heshima kwa ukubwa huo imepita. Laqabu za heshima zinatolewa kwa sababu moja tu: "tajiri kiasi gani?" wakati ulikuwako ambao matajiri waliona ni heshima kutoka na kuonana na wanazuoni wa dini. Sasa wakati umefika ambao wanazuoni wa dini - Masheikh - wanafikiri ni heshima wao kuwaendea matajiri, kujilundika katika sebule za matajiri, kwao kunaonekana jambo la fahari sana.

Vilevile Huzaifa bin Al-Yamaan amesimulia kwamba watu watasifiwa kwa sifa za kidunia (Tirmidh). Mtu atasifiwa kuwa mjasiri au mwenye busara pasipokuwa na imani moyoni mwake hata kidogo. Hali hii iko dhahiri shahiri. Mtu wa dunia kwelikweli anaweza kuwa kiongozi wa Waislamu siku hizi, mradi tu akiweza kutoa maneno ya kuvutia.

Hakuna aulizaye kama mtu huyo ana ucha-Mungu wowote. Sasa, bila ya kuwa na ucha-Mungu anawezaje kuwa kiongozi wa Waislamu? Kama anaweza kuhutubia mkutano wa hadhara, kama ana uwezo wa kulaghai au kushinda wapinzani wake wa siasa, basi inatosha.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. kwamba waaminio wataondokewa na heshima yao na watajaribu kujificha kwa watu. Kwa upokezi mwingine, Mtume s.a.w. alisema ya kuwa waaminio watakuja dhalilika kuliko mjakazi. Mjakazi anaweza kutazamia mahaba na ndoa, lakini mwumini hataweza kufikiri hata hizi. Kwa upokezi wa Dailami, Hadhrat Ali amesimulia ya kuwa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa watu wema watakuwa hawaonekani.

Badiliko hili limekuwa dhahiri hasa tangu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Wanaofuata Quran na Mtukufu Mtume s.a.w. wanachukiwa zaidi na kuepwa kuliko wanawake malaya na wanaume wasiosali Sala tano na waongo na mahaini na wanaotoa matusi kwa Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. Wale wanaochagua kuitika wito wa Mwenyezi Mungu wanadharauliwa na kufukuzwa!

Bado, badiliko lingine lililoelezwa na Mtume s.a.w.nalo ni kupungua matumizi ya lugha ya Kiarabu miongoni mwa Waislamu. Kwa upokezi wa ibn Mardwaih, Ibn Abbas amesimulia ya kuwa katika wakati huo mistari ya wataabadi itakuwa mirefu lakini lugha zitakuwa mbalimbali sana. Badiliko hili linaweza kuonwa katika siku za Haj. Kusudi moja la amri ya Haj ni kwamba Waislamu kutoka sehemu mbalimbali za dunia wakutane na kufikiria matatizo yao. Lakini hili limekuwa haliwezekani kwa sababu Waislamu walio nje ya Bara Arabu wameacha kutumia lugha ya Kiarabu; hivyo kwa kukosa lugha moja, hawawezi kupeana mawazo katika Haj. Hawawezi kutumia mkutano huo mkubwa kwa kuzidisha maendeleo ya dini, ujamaa na utamaduni. Laiti Waislamu wangehifadhi elimu yao ya Kiarabu, ingesaidia kuwa nguvu ya kisakafu baina ya Waislamu wa sehemu mbalimbali za dunia. Ingewafungamanisha pamoja - umoja ambao mwenye nguvu kiasi gani hangeweza kuuvunja.

Badiliko lingine lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni juu ya mavazi ya wanawake. Wanawake, kwa tabiri hiyo, ilikuwa waje kuonekana wa uchi licha ya kuwa wawe wamevaa (Masnad Ahmad bin Hamble, simulizi la Ibn Umar). Badiliko hili limetokea katika njia mbili. Kwanza, hariri na nguo nyingine nyepesi nyepesi zinatengenezwa kwa wingi sana. Nguo za aina hii zinapatikana kwa watu wowote. Hapo zamani zilivaliwa na matajiri tu. Nguo zenyewe zimetengenezwa kwa ulaini na wepesi sana. Zinaweza kutosheleza wazo la uzuri wa mwanamke. Ili ziweze kuondoa haya na staha. Pili, badiliko limetokea kwa njia ya mitindo iliyoenea katika Ulaya na Amerika. Katika nchi hizi wanawake wanaelekea zaidi na zaidi kuonesha sehemu za miili yao, jambo ambalo hapo zamani lilifikiriwa ni uchafu. Vifua vinaoneshwa nje. Mikono inaachwa wazi mpaka makwapani. Maelezo ya bishara juu ya mavazi ya

wanawake ni ya kweli - wanawake leo wanaonekana wako uchi ijapokuwa wawe wamevaa. Badiliko hili limeingia kwa Waislamu kwa kutumia hariri na nguo nyepesinyepesi na miongoni mwa Wakristo kwa njia ya mitindo ya kuonesha kifua, kichwa, mikono na kadhalika.

Badiliko lingine kuhusu wanawake ni jinsi ya kusuka nywele zao. Kwa maelezo ya Mtukufu Mtume s.a.w. wanawake ilikuwa wasuke nywele zao kwa kuweka makonga vichwani mwao na vichwa vyao kuonekana kama nundu za ngamia. Katika Ulaya wanawake hawasuki nywele zao kama walivyofanya hapo zamani. Leo wanaziweka nywele zao kwa vidonge zikivutia kama kitu chororo kichwani. Kwa kuwaiga wanawake wa Ulaya, wanawake katika sehemu zingine za dunia pia wanazisuka nywele zao namna hii. Kuigana siku hizi kumekuwa kawaida. Mtindo wa Ulaya unaheshimiwa zaidi kuliko ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu. Kuwaiga wazungu kunaonekana kama maendeleo.

Bado, badiliko lingine lililoelezwa na Mtukufu Mtume s.a.w. na kusimuliwa na Ibn Abbas ni wanawake kuingia katika biashara kama washirika wa waume zao au ndugu zao (Hujajul-Karaamah, kwa kunukuu Ibn Mardwaih). Badiliko hili limekuwa dhahiri pia; kwa kweli, limekuwa dhahiri hivi kwamba mwahala mwa biashara hamwezi kusemwa mmefanikiwa mpaka mmekuwa na wanawake. Wanawake warembo wanaajiriwa madukani ili kuwavutia wanunuzi na kuchonganisha biashara.

Bado, badiliko lingine lililoelezwa na Mtukufu Mtume s.a.w. linalohusu kuongezeka kwa uhuru wa wanawake. Wanawake ilikuwa waje kuwa huru zaidi na zaidi. Ilikuwa waje kuvaa kama wanaume, waendeshe farasi na kadhalika. Vilevile, wanawake ilikuwa wawatawale wanaume (Ibn Mardwaih, simulizi la Ibn Abbas). Badiliko hili tayari limekwisha tokea. Katika Amerika na nchi zinginezo za Kikristo wazo la kupita fikara juu ya uhuru wa wanawake limetokea. Kwa kuiga Magharibi ya Ukristo, wazo hilihili limeenea nchi zingine. Wazo hili la uhuru limebadilisha kabisa sura ya ujamaa. Wanawake zaidi na zaidi wanashirikiana na wanaume katika michezo wakiwinda juu ya farasi na michezo ya mbio. Wanawake zaidi na zaidi leo wanaonekana katika michezo ya

kuigiza na wanafanya kazi za kutumbuiza watu kwa ngoma na nyimbo katika miji. Mtindo wa mavazi ya kiume kwa wanawake umeenea sana katika nchi za Kikristo. Badiliko hili lilikuwa wazi zaidi baada ya vita Kuu ya kwanza ya dunia. Mamia ya maelfu ya wanawake wakaanza kuvaa kama wanaume, wanawake wengi wanavaa chupi tu na shumizi. Kuvaa nguo za kiume kwa wanawake kumekuwa mtindo sasa.

Utawala wa ujumla wa wanawake juu ya wanaume uliotajwa katika bishara ni wa ajabu upande wake. Kwa badiliko hili hali ya maisha katika nchi za Ulaya na zilizo chini ya nguvu yao, taratibu za maisha zimepata mabadiliko ya ajabu. Taratibu hizi zina hatari kubwa saba mpaka Mwenyezi Mungu awahurumie. Udhaifu huu katika kazi za wanaume na wanawake unaweza kuleta maangamizi makubwa. Kunaweza kutokea mageuzi makubwa ya ujamaa au desturi ya ndoa inaweza kupata mashaka makubwa na maendeleo ya ujamaa wa kibinadamu yakapata hasara isiyoweza kurekebishwa.

Badiliko lingine lililoelezwa na Mtume s.a.w. ni kwamba wanaume watachukua taklifu kwa kujipodoa hata waonekane "Kama wanawake." (Hilya Abu Na'im, simulizi la Huzaifa). Kunyoa ndevu videvuni na mashavuni leo kumekuwa mtindo na mtindo huu umewafanya wanaume waonekane kama wanawake. Wakati ulikuwako ambao ndevu zilifikiriwa kama pambo kwa wanaume. Kwa Waislamu kilikuwa kitu cha thawabu, kwa sababu ilikuwa ni sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w., alama ya kutii tabia yake. Ndevu zimetoweka kati ya Waislamu. Wanazuoni wa Kiislamu na masufi wanaheshimika sana katika ulimwengu wa Kiislamu wanapendelea kunyoa ndevu zao. Ushahidi zaidi kwa badiliko hili unaweza kuonwa katika tafrija ambazo wanaume huvaa kama wanawake na wanawake huvaa kama wanaume. Wanaume katika Ulaya na Amerika wanajikalifu kupita kiasi kwa kusafisha na kutinda nywele zao. Bidii inayofanywa na wanaume kwa kutinda nywele zao si zaidi kuliko inayofanywa na wanawake. Lakini kwa hakika ni zaidi kuliko bidii iliyofanywa na wanawake hapo zamani.

# HALI YA AFYA

Mtukufu Mtume s.a.w. ameeleza pia hali za kimwili za watu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Mathalan, kwa upokezi wa Tirmidh, Anas amesimulia ya kuwa atakapotokea Dajjal na keelekea Madina, ugonjwa wa tauni utatokea duniani. Kwa hali yoyote, Mwenyezi Mungu atailinda Madina katika mashambulio ya Dajjal na tauni. Bishara hii imetimia. Kwa miaka mingi ugonjwa wa tauni umeangamiza duniani. Umeangamiza mamia ya maelfu ya watu, na kuteketeza mamia ya vijiji. Lakini sehemu takatifu za Islam zilihifadhiwa na mashambulio haya. Hatua zilivumbuliwa zilizosaidia kulinda sehemu takatifu. Mojawapo ni kutengwa kwa watu ambako kulizuia tauni kuingia sehemu takatifu za Islam. Kudhihiri kwa tauni kulitabiriwa na Mtukufu Mtume s.a.w. katika njia mbili. Pengine aliueleza kama Daabba (mdudu) wa ardhi. Maelezo haya ni kweli kwa sababu tauni inaletwa na kuumwa na kiroboto. Hiki kiroboto hutoka chini na kuuma mwili wa mwanadamu. Quran Tukufu imetumia jina hilihili. Huu siyo ugonjwa wa kawaida. Ni ugonjwa wa dunia ambao umeleta vifo na maangamizi sehemu nyingi sana. Katika Bara Hindi ulienea kwa miaka mingi.

Kutokea kwa Daabba, kama ilivyoelezwa katika bishara, hakuoneshi kutokea kwa tauni tu. Bali kunaonesha kutokea kwa maradhi mengi ya kuambukiza yaletwayo na *bacteria*, vile vijidudu visivyoonekana kwa macho. Naam, siku hizi tuna magonjwa ya *micro-organisms (* vidudu vidogo visivyoonekna kwa macho matupu) ambayo hayakujulikana zamani. Hapo zamani magonjwa kama haya ama hayakujulikana au hayakuenea na kuleta vifo kwa kadiri yanavyoleta siku hizi. Bishara kuhusu tauni na magonjwa ya aina hiyo iliyotolewa na Quran tukufu na Mtume s.a.w. inatabiri kwa kudokeza kuvumbuliwa darubini na kugunduliwa *bacteria* kuwa sababu na vienezaji vya ugonjwa. Wakati wa Mtume s.a.w. hakuna kilichojulikana juu ya *bacteria*. Wakati huo, elimu ya utabibu bado ikisemwa kwa maneno kama nyongo, nyongo nyeusi, damu na kikohozi.

Mtume s.a.w. ametaja alama nyingine kuhusu afya na maradhi.

Mojawapo ni mwongezeko wa idadi ya vifo vya ghafla kwa kusimama kwa moyo n.k. (Hujajul-Karaamh, simulizi la ibne Abi Shaibah). Mojawapo ya sababu za vifo kama hivyo ni ulevi uliopita kiasi. Na nyingine ni maumivu ya ubongo na idadi ya wagonjwa wa ubongo. Pombe inadhoofisha moyo na ubongo. Na kujisomea kwingi na kufanya kazi nyingi kunaleta madhara katika mishipa ya akili. Sababu zote mbili hizi zinazidi siku hizi. Matokeo yake ni mwongezeko wa vifo vya ghafla. Katika yote yaletwayo na vileo, vifo vya ghafla ndiyo mno. Mtu mara kwa mara anagwaya. Maelfu ya watu hufa kila mwaka kwa ugonjwa wa moyo. Wanakufa wakiwa wamesimama au wakifanya kazi, vitini mwao au vitandani. Jambo hili halikujulikana zamani.

Miongoni mwa maradhi ambayo Mtume s.a.w. ametaja, ni maradhi yanayoungana na pua ambayo huleta idadi kubwa sana ya vifo. Maradhi haya yalitokea baada ya Vita Kuu ya kwanza. Tangu hapo yakaanza kuitwa *influenza* (mafua). Katika mwaka 1918 maradhi haya yakaleta vifo vya watu milioni ishirini, ambapo vita ilileta milioni sita. Hivyo *influenza* iliangamiza khumusi moja katika kila mia moja ya watu wa ulimwengu mzima. Zama *influenza* ilipooenea ulimwenguni, ilileta hofu ya Mwenyezi Mungu katika mioyo mingi. Kila mmoja aliona ya kuwa uhai na salama vi mikononi mwa Mwenyezi Mungu.

## WANAWAKE WATAWAZIDI WANAUME KWA WINGI

Mtume s.a.w. alitaja pia uwiano wa idadi ya wanawake na wanaume kama alama ya maana sana ya Kiyama. Bishara inaeleza kuwa wakati huo wanawake watakuwa wengi kuliko wanaume, hivi kwamba wanawake hamsini wataangaliwa na mwanamume mmoja. Bishara hii imetimia. Kuna wanawake wengi zaidi ulimwenguni leo kuliko wanaume. Katika nchi za Ulaya, idadi ya wanaume imepunguzwa kwa vita. Kwa kweli, hali hii ni ya masikitiko makubwa hivi kwamba wataalamu wa ujamaa wamefanywa wafikirie amri ya Islam ya kuruhusu kuoa wake wengi kuwa ndiyo dawa ya tukio hili. Wale waliokuwa wakilaumu Islam kwa ruhusa

hii, wanashurutishwa kufikiri sana juu yake. Hapana shaka kwamba ruhusa ya Islam ya kuoa wake zaidi ya mmoja ndiyo tu dawa ya mwongezeko huu wa idadi ya wanawake. Wataalamu wengi wa ujamaa wanaonekana wakikubali kwamba njia ya kuondoa machafuko ni kuruhusu kuoa wake wengi. Njia nyingine waonayo ni zinaa kama kosa la lazima kwa ujamaa. Ndio sababu, siku hizi kuweka wanawake wawili kumekuwa rahisi huko Ulaya. Hawapendelei sana sasa kuwaburura mahakamani wale wawekao wanawake wawili wawili. Hali hii ni mpya na imeletwa na kuzidi kwa wanawake katika mataifa ya Ulaya. Kwani si zamani sana jambo hili lilifanywa kuwa ni dhambi katika Ulaya. Hakukuwa na Mkristo au Mzungu yeyote aliyeweza kulieleza kwa utulivu. Ilikuwa kubwa sana hofu ya Wazungu juu yake hivi kwamba kwa kuwaiga Wazungu, Waislamu walioelimika wakaanza kusumbuliwa sana juu ya ruhusa ya Islam ya kuoa wake zaidi ya mmoja na wakaanza kuitakia radhi.

## NJIA MPYA ZA USAFIRI NA USHIRIKA

Mtume s.a.w. alitoa sura ya hali ya jumla juu ya njia za usafiri na ushirika katika wakati ulioahidiwa. Alisema ya kwamba njia za usafiri za zamani zitatoweka na mahala pake patashikwa na magari yaendayo mbio sana. Yatatumiwa magari hayo sehemu zote barani na baharini. Hadithi inasema:

> "Na kwa yakini wataachwa ngamia wala hawatatumiwa kwa kusafiria" (Sahih Muslim, Kitaabul Iman).

Badiliko hili limejieneza zimazima. Njia zote za zamani za usafiri zimetoweka katika nchi nyingi. Kwanza tulikuwa na reli. Wale ambao hawakusafiri kwa njia za reli, walisafiri kwa njia zingine. Walipanda ngamia au wanyama wengine. Lakini tangu kuvumbuliwa motokaa safari za barabara pia zimekuwa za magari. Kadiri mashine mpya za kusafiria zinavyoendelea, utumiaji wa

wanyama kwa kusafiria unatoweka.

Mtume s.a.w. alitabiri kutokea kwa meli mbali na kutokea kwa njia ya reli. Alisema:

> "Punda wa Dajjal atasafiri baharini kama atavyosafiri barani. Na atakaposafiri atakuwa na mawingu mbele na nyuma" (Kanzul Ummal, Kitabu cha 7. uk. 267).

Ni dhahiri kwamba hizi ni hali za gari moshi na mashua. Magari yanayoendeshwa kwa nguvu za mvuke yanaweza kusafiri majini na nchi kavu. Na kama ilivyo, njia hizi mpya za usafiri zimo mikononi mwa Dajjal. Bishara inadokeza juu ya wahubiri wa Kikristo watakavyotumia zaidi njia mpya za usafiri. Kwa sababu ya magari ya moshi na mashua, wahubiri wa Kikristo wamesafiri sehemu mbalimbali za dunia na kueneza elimu ya Biblia. Mafundisho yao ni mafundisho ya Dajjal. Mawingu yaliyotajwa kwenye bishara ni mawingu ya moshi unaoonekana mbele ya magari yaendayo kwa mvuke na nyuma yake. Moshi na mvuke vinaonekana lazima kwa magari haya. Kuni zake ni makaa. Hiki ndicho chakula cha punda wa Dajjal kilichotajwa vitabuni mwa Hadithi. Hivyo njia mpya za usafiri zimeleta uhusiano na ushirika wa namna nyingine kabisa baina ya mataifa mbalimbali ya dunia.

## HALI YA UCHUMI

Juu ya hali ya uchumi, Mtume s.a.w. (kwa upokezi wa Huzaifa bin Al-Yamaan), alisema ya kwamba wakati wa Masihi Aliyeahidiwa dhahabu na fedha zitakuwa nyingi sana (Hilya cha Abu Na'im). Hali hii ni ya kweli. Kuna dhahabu na fedha nyingi leo duniani hivi kwamba hata sehemu moja ya kumi haikupatikana zamani. Kila mji una watu tele wanaoshughulika na dhahabu na fedha. Njia mpya za kuchimbua dhahabu na fedha zimevumbuliwa. Hizi zimefanya madini hizi ziwe kwa wingi sana. Uingereza peke yake ina dhahabu nyingi leo kuliko iliyopatikana katika dunia nzima hapo zamani. Matokeo ni kwamba biashara imekuwa nyepesi, kwani biashara inaendelea kwa msaada wa dhahabu na fedha. Hapo kale vitu vya kubadilishana vilikuwa vipande vya shaba na kauri. Leo

kauri imetoweka na hata vipande vya shaba havitumiwi sana. Katika Uingereza sarafu ndogo sana ni penny, na katika Amerika ni cent. Sehemu kubwa ya biashara katika nchi hizi inaendeshwa kwa sarafu za dhahabu.

Miongoni mwa hali za uchumi zilizotajwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni kuchukua na kutoa riba. Hadhrat Ali, kwa upokezi wa Dailami, amesimulia ya kuwa mojawapo ya ishara za Kiyama, ni mwongezeko wa utumiaji wa riba. Hii ni kweli. Riba leo imeongezeka kwa kadri ambayo hapo kale hapakuwa na hata sehemu yake ya milioni moja. Riba imekuwa ya muhimu sana kwa watu wengi hivi kwamba inasemwa kwamba biashara haiwezi kuendelea bila ya hiyo. Benki za biashara zimezidi sana kwa kadiri ambayo maelfu zinaonekana hata katika nchi ndogondogo. Serikali zinatoa na kupokea riba. Wafanyi biashara wanatoa na kupokea riba. Mafundi na wenye viwanda wanafanya kadhalika. Matajiri wanafanya kadhalika. Mataifa yote yanaendesha riba. Inaonekana hivi ya kwamba kila mtu ameona aazimishe mali yake kwa wengine kwa riba na kuazima kutoka kwao kwa riba vilevile. Kati ya labda milioni kumi, ni elfu chache tu za mali ya biashara inaweza kuwa si riba. Waislamu wameambiwa katika Kitabu chao Kitakatifu kuacha kutumia riba. Kama wapuuze amri hii wanaonywa kuwa:

"Basi fahamuni mtakuwa na vita kutoka kwa Mwenyezi Mungu" (2:280).

Lakini ni nini wafanyacho Waislamu leo? Wanachukua "riba" na kuiita "faida". Wengi wao wanakubali kuwa riba imekatazwa, lakini wanachukua tu. Maulamaa wa Kiislamu wamevumbua tafsiri ngeni kabisa za "riba" na faida, na wakatoa fatwa kuhalalisha kupokea riba itolewayo na benki hizo. Wamehalalisha riba katika nchi zinazotawaliwa na wasio Waislamu, hivi kwamba hata Waislamu hawajiepushi na kuchukua riba, wanasahau kuwa sharia ya Islam ni ya mwisho kwa mwanadamu. Kwa hakika, wamevumbua sheria mpya. Haya yote yanaonesha kuwa kuongezeka kwa riba kumeruka mipaka. Hakuna awezaye kuikwepa mpaka kwa rehema na msaada maalum wa Mwenyezi Mungu.

Miongoni mwa ishara za uchumi wakati wa Masihi Aliyeahidiwa, ishara ya maana iliyotajwa na Mtukufu Mtume s.a.w. ni kwamba Wakristo watakuwa daraja ya kwanza kabisa ya utajiri duniani. Wengine wote watahesabika kama maskini. Katika Tirmidh, Nawas bin Sam'aan amesimulia ya kuwa Mtume s.a.w. alisema kuwa Dajjal atawambia watu, "Nikubalini mimi na uongozi wangu." Wale watakaokataa watakuwa maskini na watakaokubali watafaulu na kupata utajiri. Dajjal atachukua taklifu ya kuwashushia bidhaa kutoka juu na kuwatolea zingine kutoka ardhini. Hali hii ni kweli. Mataifa ya Kikristo yameendelea sana katika utajiri, na wengine wameendelea kuwa maskini. Mnamo karne moja iliyopita badiliko hili limejisogeza mbele na mbele.

## HALI YA SIASA

Miongoni mwa hali za siasa zilizotajwa na Mtume s.a.w. ni hali ambazo zikichukuliwa pamoja zinaonekana kutoa sura kamili ya wakari tulionao. Mojawapo ni kuanguka kwa Waislamu katika hali ya siasa (kwa upokezi wa Huzaifa bin Al-Yamaan). Maelezo yenyewe ya Mtume s.a.w. yamo katika maneno - Waislamu watakuwa kama Mayahudi. Mfano huu wa Mayahudi unahusu hasara ya haiba na maarifa ya siasa. Kama Mayahudi; watapungua nguvu yao ya siasa na wataishi kwa kuwategemea wengine. Tazama jinsi ilivyo ni kweli hali hii! Haiba ya Waislamu imepungua kabisa katika siasa. Wakati ulikuwako ambao bendera za Kiislamu zilipepea katika sehemu zote za dunia. Lakini leo tunaweza kuona nchi chache tu ambako bendera za Kiislamu zinaweza kuonekana zikipepea. Waislamu wanafurahia madaraka hapa na pale, lakini wanaona shida sana kuendesha madaraka yao pasipo msaada wa nguvu ya Ukristo. Ee Mwenyezi Mungu Tusaidie! "Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea."

Alama nyingine ya siasa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa, kwa usemi wa Mtukufu Mtume s.a.w., ni kwamba Sham, Iraq na Misri zitaasi Wafalme wa Kiislamu, na Waarabu watagawanyika katika falme

mbalimbali.Katika Muslim, Abu Huraira amesimulia ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alisema:

"Iraq itakataa kufanya shirika mali yake na nafaka zake. Halkadhalika Sham na Misri. Nanyi (yaani Waarabu), mtagawanyika na kutengana kama mlivyokuwa kwanza" (Sahihi Muslim - Kitabul Fitan na Ashraat-us-Saa'at).

Bishara hii imetimia. Iraq, Sham na Misri ni nchi zinazojitegemea, hazitii tena Uturuki na zinakataa kushirikiana mazao yao na mali yao pamoja na uongozi wenye nguvu wa Kiislamu. Waarabu wamerudia tena kujigawa. Naam, Hijaz ina serikali ya Kiarabu. Lakini ina maadui wengi na pia si tajiri sana. Sehemu zingine za Bara Arabu hazina taratibu nzuri. Serikali zao haziwezi kulingana na serikali zingine za leo.

Badiliko lingine la siasa lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni kwamba mataifa mawili yaliyotajwa katika bishara za zamani, Yaajuja na Maajuja, yatakuwa na nguvu ya ajabu hivi kwamba mataifa mengine ya dunia yatakuwa si chochote mbele yao. Muslim na Tirmidh, vinaeleza kuwa Nawas bin Sam'aan amesimulia, kwa usemi wa Mtume s.a.w. ya kuwa Mwenyezi Mungu atamwamuru Masihi Aliyeahidiwa:

Waongoze watumishi wangu kwenye mlima. Nimeleta watu fulani duniani ambao hakuna anayeweza kuwashinda kwa vita". Mtume s.a.w. alisema pia ya kuwa Mwenyezi Mungu atainua Yajuja na Maajuja duniani. Alama hizi zimetimia. Yaajuja na Maajuja wamedhihiri tayari. Nao ni mataifa ya Mashariki na Magharibi ambayo hakuna taifa liwezalo kuyashinda katika vita. Mataifa ya

Mashariki ni Warusi, na ya Magharibi ni Waingereza na Waamerika. Tunasoma habari zao katika Biblia:

"Gogu, mkuu wa Roshi, Mesheki na Tubali; .... na juu ya watu wote wakaao salama katika visiwa" (Ezekieli 39).

Mataifa haya yote mawili (na wasaidizi wao) yamefikia upeo wa nguvu yao. Kama ilivyotabiriwa katika Hadithi, kuinuka kwa mataifa haya ilikuwa kuwe baada ya kudhihiri Masihi Aliyeahidiwa. Kwahiyo kutokea kwa Yaajuja na Maajuja kunaonesha kuwa Masihi Aliyeahidiwa amekwishafika.

Badiliko la siasa lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni kuinuka kwa mataifa ya chini. Kama ilivyosimuliwa na Huzaifa bin Al-Yamaan, ishara ya maana ya kufika kwa Masihi ni kuinuka kwa watu maskini walio uchi na kuwa watawala. Neno lililotumiwa katika hadithi ni "uchi" nalo lieleweke kwa hali ya uhusiano. Kwa uhusiano mbele ya matajiri, maskini wako uchi. Kwa kuhitaji vitu mbalimbali ambavyo matajiri wanaweza kuvipata, maskini kila mara wamesimuliwa kama wako uchi. Alama hii imetimia. Kwa vile serikali za niaba zimekuwa na matawi zaidi na zaidi katika nchi zingine, nguvu ya siasa imechukuliwa na maskini. Kwahiyo maskini wamekuwa wafalme. Wafanyakazi na vibarua wamekuwa na nguvu sana leo, hivi kwamba wafalme wa dunia wanatetemeka mbele yao. Vyama vingine vya siasa pia vinaona ni lazima kuishi kwa amani na wafanyakazi. Katika nchi kama urusi na Switzerland, viongozi wa wafanyakazi ndio watawala. Sehemu za Australia wanazidi kupata ufaulu. Kadhalika nchi nyinginezo pia.

Ishara nyingine ya wakati wa Masihi Aliyeahidiwa, kwa upokezi wa Huzaifa bin Al-Yamaan, ni kuongezeka idadi ya watawala. Neno lililotumiwa katika Hadithi ni *shurt*, na *shurt* maana yake ni wasaidizi au manaibu wa watawala. Alama hii imetimia. Katika taratibu za Serikali hapo kabla, hatukuwa na manaibu makatibu wasaidizi kama tulio nao leo. Kila nchi ilikuwa na mtawala na alifanya kazi mwenyewe. Lakini leo taratibu za utawala zimekuwa nyingi, hivi kwamba idadi ya wasaidizi na manaibu inakuwa kubwa sana. Kuna orodha ndefu ya wizara na idara ambazo kwazo serikali imejigawa - polisi, afya, usajilishaji, ujenzi, posta, reli, uhusiano, bandari, kodi, uchunguzi wa vileo, maji n.k. Idadi hasa ya wizara na idara ni kubwa

zaidi kuliko hii. Kila serikali inabidi iteue wataalamu kwa ajili ya taratibu za wizara na idara mbalimbali. Kila mmoja wa wataalamu inabidi awe na wasaidizi wengi. Hivyo leo kila serikali ina kazi nyingi sana na idadi kubwa sana ya manaibu na makatibu.

Badiliko lingine kuhusu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa lililotabiriwa na Mtume s.a.w. ni kutanguka kwa adhabu zilizoelezwa na Sharia ya Kiislamu juu ya makosa ya jinai. Kwa upokezi wa Dailami, Hadhrat Ali anasimulia ya kuwa alama moja ya Akhir Zaman ni kutanguliwa kwa adhabu zilizoruhusiwa na Islam (Hujajul-Karaamah). Alama hii imetimia. Katika serikali zote za Kiislamu siku hizi, adhabu za Kiislamu zimetoweka. Katika Uturuki, Bara Arabu, Misri, Iran na hata Afghanistan, "kupiga mawe kwa uzinifu" na kukata kiganja cha mkono kwa wizi" hazitambuliwi tena kuwa adhabu. Serikali zingine za Kiislamu zimekubali kubatilishwa kwake chini ya mikataba na serikali zingine. Hii ni ya wazi sana katika ishara. Zama serikali za Kiislamu zilipokuwa na nguvu na maoni ya Islam yametawala, hakuna yeyote aliyeweza kufikiri ya kuwa adhabu za Kiislamu zingekuja achiliwa mbali. Hakuna aliyeweza kudhani kwamba kungetokea kuchukiwa kwa adhabu za Kiislamu hivi kwamba hata serikali za Kiislamu zipendazo kuhifadhi adhabu hizi zingekuja shindwa kufanya hivyo.

Hali na ishara nilizoeleza mpaka hapa zinahusu dini, tabia, elimu, afya, siasa na utamaduni. Zinahusu hali za ujamaa na uhusiano wa wanawake na wanaume kwa ujumla. Lakini zaidi ya hayo, ishara zingine zilisimuliwa na Mtume s.a.w. kuhusu hali ya kiulimwengu. Ishara zinazohusu ardhi na zinazohusu mbingu.

## ISHARA ZA ARDHI

Juu ya ardhi, Huzaifa bin Al-Yamaan anasimulia kuwa Mtume s.a.w. aliwaeleza Masahaba zake ishara za maana sana za wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Akiwasimulia alisema:

"Zama ishara hizi zimetimia, muwe tayari kupambana na misiba."

Msiba mmoja ni *Khasf*. Na *Khasf* maana yake ni mafuriko ya maji. Elimu ya tabii inatueleza kuwa kutokea kwa mafuriko kunafungamana na tetemeko la nchi. Hivyo Mtume s.a.w. alipotaja *Khasf* alikuwa na maana ya matetemeko ya nchi; ambayo yalikuwa yaashirie kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa. Ishara hii imekwishatimia. Zama hizi matetemeko mengi yametokea hivi kwamba idadi yote ya matetemeko yaliyotokea katika karne 3 zilizopita ni ndogo sana. Maelfu ya watu wamekufa kwa matetemeko ya nchi katika miaka yetu michache hivi kwamba idadi ya watu waliokufa kwa matetemeko hayo katika karne zilizopita ni ndogo sana.

## ISHARA ZA MBINGU

Mbali na mabadiliko ya ardhi, Mtume s.a.w. alitaja matukio ya kimbinguni ambayo yalikuwa yaashirie kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa. Mathalan, Mtume s.a.w. alisema ya kuwa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa, Jua na Mwezi vitapatwa mnamo tarehe fulani za Mwezi wa Ramadhani. Mtume s.a.w. alizihesabu ishara hizi kama zenye maana sana. Kwa kweli, alisema kuwa tangu kuumbwa mbingu na ardhi, ishara hizi mbili - kupatwa kwa Jua na Mwezi katika Mwezi wa Ramadhani - hazijapata kuoneshwa kama ishara kwa madai ya Mtume yeyote. Maneno ya Hadithi yanaeleza:

"Kwa yakini kutakuwa na ishara mbili za maana kwa ajili ya Mahdi wetu. Ishara hizo hazijapata kutokea tangu kuumbwa mbingu na ardhi. Moja ni kupatwa kwa Mwezi mnamo usiku wa kwanza wa Ramadhani, na nyingine ni kupatwa kwa Jua kati ya Ramadhani, na alama hizi mbili hazijapata kutokea tangu kuumbwa mbingu na ardhi."

Ishara hii iliyosimuliwa na Muhammad bin Ali ina maana sana. Hadithi imebainisha kuwa ishara hii haijapata kutokea kama ishara ya kudhihiri kwa nabii yeyote wa Mwenyezi Mungu. Ishara hii inakubaliwa kama ya kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa na Sunni na Shia wote na imetajwa ndani ya vitabu vyao. Sunni na Shia katika mkusanyiko wa Hadithi zao, mmetajwa ishara hizi. Kwahiyo haiwezi kusemwa kuwa imepokelewa na hawa na kukataliwa na wale. Tena ishara hii ni ya maana sana, kwani imetajwa hata katika vitabu vya zamani kama ishara ya kufika Yesu mara ya pili. Katika Agano Jipya. Yesu akisimulia alama za kufika kwake mara ya pili alisema:

"Lakini mara baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza na mwezi hautatoa mwanga wake" (Mathayo 24:29).

Ni dhahiri alama hii inahusu kupatwa kwa Jua na Mwezi.

Ingawa ninahusika hapa na kueleza ishara zilizotajwa katika Hadithi, haionekani kuwa ni nje ya shabaha kusema kuwa hata katika Quran Tukufu kupatwa kwa Jua na Mwezi kumetajwa kama ishara kubwa ya Akhir Zaman. Katika Sura Qiyaama tunasoma:

Anauliza: itakuwa lini siku ya Kiyama? Basi jicho litakapofanya kiwi, na mwezi utakapopatwa, na jua na mwezi vitakapokutanishwa (katika kupatwa)" (75:7-10).

Aya hizi zinatoa hali hasa ya wakati huu. Swali linatolewa - Itakuwa lini siku ya Kiyama? Jawabu ni - Zama ishara fulani zitakapotokea. Miongoni mwazo ni jicho kufanya kiwi, yaani kutokea kwa matukio ya ajabu ajabu na mabadiliko, pia kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua na kutokea kwa kupatwa kwa vyote katika mwezi mmoja. Kufika kwa Masihi Aliyeahidiwa kunaashiria siku za mwisho wa dunia. Kwa hivi Quran Tukufu inaunga mkono hali zilizoelezwa katika Hadithi.

Ishara hii ilitimia mnamo mwaka 1894 (1311: A.H.). Mnamo mwezi wa Ramadhani wa mwaka huu, mwezi ulipatwa tarehe ya kwanza ya tarehe tatu (yaani tarehe 13) ambazo mwezi uliweza kutazamiwa kupatwa. Jua likapatwa tarehe ya kati, yaani tarehe 28.

Kukutana huku kwa kupatwa kwa mwezi na jua katika mwezi wa Ramadhani kulifanyika katika uhai wa mtu aliyedai kuwa Mahdi Aliyeahidiwa katika bishara, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Kwahiyo njia mbili zinaonekana wazi kwa Waislamu wenye fikara. Ama (1) wakubali kuwa bishara za Mtume s.a.w. ni za kweli, pia za Quran Tukufu na vitabu vya zamani ambavyo vyote vinanadi kuwa wakati wa Mjumbe wa Akhir Zaman utaashiriwa kwa kupatwa kwa mwezi na jua. Kama bishara hizi zikubaliwe kuwa ni za kweli, na kama pia zimetimia katika uhai wa mdai yeyote, basi madai ya mdai huyo pia hayana budi yakubaliwe. Bishara imesema kuwa kukutana kwa kupatwa kwa jua na mwezi hakutafanyika ila katika wakati wa Mahdi. Au (2) kama hawako tayari kukubali bishara hizi wala Mahdi - anayehusika nazo, basi ni lazima wakubali kuwa bishara hizi haziashirii kwenye tukio lolote ambalo linaweza kusaidia kumpambanua mdai wa unabii.

Baadhi ya watu wanahoji na kusema bishara hii inasema juu ya kupatwa kwa mwezi mnamo tarehe mosi na kupatwa kwa jua mnamo tarehe ya kati ya Ramadhani. Lakini kupatwa tunakosema sisi kumefanyika hasa mnamo tarehe 13 na 28 za Ramadhan. Tusisahau kuwa kupatwa kwa mwezi na jua kumesemwa ni budi kufanyike katika tarehe fulani. Si kosa katika haya mpaka desturi yote ya ulimwengu, kanuni ya mzunguko wa vitu vya angani ichunguzwe na ipangwe katika msingi mwingine. Taratibu mpya ya ulimwengu inaweza kuwa na hilaki ya ulimwengu mzima. Hivyo, kama maneno ya bishara yashikwe, bishara hii inaweza kuashiria kwenye siku ya Kiyama, alama zake au wakati wa Mahdi.

Wale wanaotoa hoja hii, bila shaka wanachoma itikadi yao kwenye tarehe mosi na tarehe ya kati zilizotajwa katika bishara, lakini wanasahahu kuwa neno lililotumiwa katika bishara kwa ajili ya mwezi ni *Qamar*. Kama bishara hii ingekusudia hasa tarehe mosi mwezi wa Ramadhan wa kupatwa kwa mwezi, basi neno la Kiarabu *Hilaal* lingetumiwa na sio *Qamar.* Mwezi huitwa Qamar wakati umefikia usiku wa nne. Katika kamusi ya Kiarabu tunasoma:

"Nao huitwa *Qamar* baada ya siku tatu za mwanzo mpaka mwisho wa mwezi. Amma katika siku tatu za mwanzo mwezi unaitwa Hilaal" (Aqrab-ul-Mawarid, kitabu cha pili).

Kwa hiyo tuna mambo mawili ya maana sana kufikiria. Mosi, Hadithi imetumia neno Qamar ambalo kwa vyovyote haliwezi kuwa na maana ya mwezi wa tarehe mosi, pili na tatu; pili, kupatwa kwa mwezi kwa kufuata kanuni ijulikanayo sana ya taratibu ya ulimwengu, kunaweza kufanyika mnamo tarehe 13, 14 au 15 za mwezi wa kupatwa kwake, sio katika tarehe mosi. Kwahiyo, mwanzo wa Ramadhani, uliotajwa katika bishara, maana yake ni tarehe ya mwanzo ya tarehe tatu ambazo kupatwa kwake kunawezekana, yaani tarehe 13. Hivyo kushikilia ya kuwa kupatwa kwa mwezi kungetokea usiku wa kwanza wa Ramadhani haipatani kabisa. Ni wale tu wanaopenda kupuuza Neno la Mwenyezi Mungu na bishara ya Mtume s.a.w. ndio wanaweza kufanya hivyo.

## BISHARA NYINGINE

Kwa ufupi, Mtume s.a.w. alieleza idadi kubwa ya ishara kwa kumtambulisha Masihi Aliyeahidiwa. Baadhi yao ni za maana sana hata kama zichukuliwe mojamoja. Kwa hali yoyote, Mtume s.a.w. alikusudia kwamba ishara hizi zichukuliwe pamoja na kufanywa sura nzima ya wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Zama ishara chungu mzima zinadhihiri pamoja, ni lazima ziashirie tukio la maana sana. Pamoja na sura hii iliyo wazi hakuna anayeweza kuona shida kuutambua wakati ulioahidiwa unapodhihiri. Naam, kulikuwa ugonjwa wa tauni hata zamani, vilevile matetemeko ya nchi, na pia mchezo wa kamari. Bila shaka watu walipotoka mara kwa mara. Kadhalika Wakristo walikuwa na siku zao za utukufu na nguvu yao ya dunia. Lakini swali ni hili, je, haya yote aliyosema Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa ni ishara za Masihi Aliyeahidiwa, yalipata kutokea pamoja hapo zamani, au yanaelekea hata kutokea baadaye? Jawabu ni laa. Ishara chungu mzima namna hii haziwezi kutokea pamoja mara kwa mara. Hebu tubuni akilini mtu mmoja ambaye hajui hali mbalimbali juu ya ujamaa, tabia, dini n.k., ambazo zimo katika wakati huu. Tumsimulie ishara za wakati wa Masihi

Aliyeahidiwa kama zilivyoelezwa na Mtume s.a.w. Halafu tumwombe asome taarikh ya ulimwengu na atuambie ni wakati gani katika taarikh angeweza kufika Masihi Aliyeahidiwa. Mtu huyu wa kubuni atasoma wakati wa Adam, halafu wakati wa nabii mwingine, halafu wa mwingine n.k. Hakuna hata mmoja wa nyakati hizo atakaoweza kupambanua kuwa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Lakini mara atakapofika wakati wetu huu na kuanza kusoma juu ya hali za kweli zilizopo, atatangaza kuwa kama Mtume s.a.w. alikuwa mkweli, kama kweli alitabiri haya anayosemwa kuwa alitabiri, basi si mwingine bali huu ndio wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Mtu wetu huyu atafahamu juu ya kuachwa kwa amri za dini ambako kuko dhahiri. Ataona maendeleo makubwa ambayo sayansi imefanya. Ataona ni udhaifu wa namna gani umewapata Waislamu baada ya siku zao za utukufu. Ataona Ukristo ukiendelea mbele katika utawala baada ya kupona katika siku zake za maanguko. Ataona mataifa ya Kikristo yakiwa na sehemu kubwa ya mali ya dunia. Ataona mataifa mengine yakidhalilika kwa umaskini. Vilevile ataona ugonjwa wa tauni na magonjwa mengine kama mafua yakihilikisha maelfu ya watu ulimwenguni, maendeleo ya utabibu na sayansi. Ataona kuwa inavumbuliwa siku hizi ya kuwa magonjwa yanaletwa na *bacteria.* Ataona pia ushirikina mkubwa wa toka zamani na mila vikitia kiharusi akili za wanadamu. Ataona magari moshi na meli na chungu ya majumba ya kuwekea akiba. Ataona matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara, kutokea kwa Yajuja na Maajuja na kutawala kwao katika dunia nzima. Atasoma juu ya kupatwa kwa jua na mwezi. Ataona kuongezeka kwa mali na utajiri. Kadhalika ataona watu wa chini wakiinuka na kuwa wafalme ulimwenguni. Kwa ufupi, hali yote ya ulimwengu itamfahamisha kuwa huu ndio wakati wa kufika Masihi Aliyeahidiwa. Mchunguzi wetu huyu hataona ishara hizi mojamoja bali ataziona zote katika sura moja. Mara baada ya kuona sura hii yote, atajiona mwili mzima ukimtetemeka na moyo wake ukimdunda. Atafunga kitabu cha ishara zote, atakiweka chini na kutangaza kuwa uchunguzi wake umekwisha na ya kwamba uchunguzi zaidi ya huo ni bure. Kwa mujibu wa ishara hizi Masihi Aliyeahidiwa amekwishafika. Kama hajaja bado, basi hatakuja kamwe.

# HABARI YA DAJJAL

Mara nyingi mgogoro unapatikana juu ya bishara inayomhusu Dajjal. Inasemekana kwamba Dajjal ilikuwa adhihiri kabla ya Masihi Aliyeahidiwa. Na kwa kuwa Dajjal hajadhihiri, basi wakati wa Masihi bado haujafika.

Hapana budi ikumbukwe kuwa bishara kuhusu Dajjal, kama bishara zingine zote, ni maneno yanayotakiwa kufasiriwa. Tunasoma katika Quran Tukufu:

"Na jua na mwezi, nimeviona vikinisujudia (12:5).

"Nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja" (37:103).

Aya hizi ni juu ya ndoto za Nabii Yusuf na Nabii Ibrahimu. Ndoto hizi zote zinajulikana sana. Zote ni mifano ya matukio ziliyoyatabiri.

Bishara kuhusu Dajjal haziwezi kueleweka ila katika nuru ya Hadithi zingine na katika nuru ya kanuni za jumla za Mwenyezi Mungu. Kama ni kweli kama zisemavyo Hadithi ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa atatanguliwa na Dajjal, na kama ni kweli ya kwamba kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa kutatokea wakati wa utawala wa Ukristo, je, sio sawa na shabaha ya kwamba bishara juu ya Dajjal inaashiria kwenye nguvu na kuenea kwa utawala wa Ukristo zama hizi? Bishara zinaelekea kueleza kuwa Dajjal na Ukristo zitakuwa ni jamia zenye nguvu sana na ya kwamba zote zitatokea wakati fulani kabla ya Masihi Aliyeahidiwa. Jamia mbili zenye nguvu nyingi, na zenye kutokea wakati mmoja, ni lazima iwe kitu kimoja. Hivyo taabu inaweza kuondolewa kwa kusema kuwa majina haya mawili sio ila ni majina ya kitu kimoja.

Fikara ya maana sana inayoongoza kwa shauri hili ni kwamba Mtume s.a.w. aliwaamuru wafuasi wake kusoma aya kumi za mwanzo za Sura Kahf, wanapopambana na matisho ya Dajjal. Aya hizo kumi za Sura hiyo ndani yake mna maonyo kwa Ukristo. Aya moja inasema:

"Na kiwaonye wale wanaosema Mwenyezi Mungu Amepanga mwana" (18:5).

Makusudio ya ufunuo wa Quran ni kuonya wanadamu. Miongoni mwa makusudio mengine ni kuwaonya wale wanaompangia Mwenyezi Mungu mwana. Aya hizo, kwa maoni ya Mtukufu Mtume s.a.w. zinatoa mwongozo kwa Waislamu kupambana na matisho ya Dajjal. Bali aya hizo zina maonyo juu ya Ukristo. Je, hii haioneshi wazi kuwa Dajjal na Ukristo ni kitu kimoja? Dawa ya maradhi ni lazima ihusiane na maradhi yenyewe. Kama Dajjal na Ukristo vilikuwa vitu viwili mbalimbali, Mtume s.a.w. asingeashiria kusomwa kwa aya za Kitabu Kitukufu ambazo zinaeleza sio juu ya Dajjal bali juu ya Ukristo. Kusomwa kwa aya hizi kungekuwa upuuzi kama zisingemhusu Dajjal. Hivyo basi, inaonekana kuwa hata kwa maoni ya Mtume s.a.w., kudhihiri kwa Dajjal ni kudhihiri kwa waenezi wa Ukristo.

Shida kubwa sana iliyoko katika kuelewa maana hasa ya Dajjal ni wazo ambalo kwalo watu wengi wameangukia kufikiri kwamba Dajjal ni mtu mmoja mwenye nguvu sana, namna fulani ya mtu wa kiajabu ajabu. Na hivi sivyo hata kidogo. Hata kamusi za Kiarabu zinapinga wazo hilo. Zinaeleza:

"Dajjal ni jina la jamia kubwa ya watu ambao kwa wingi wa nguvu zao, wataenea dunia nzima, na kwa mujibu wa tafsiri zingine, ni jina la kundi la watu ambao wanaendelea kutembeza bidhaa zao sehemu fulani ya dunia mpaka sehemu nyingine" (Taj).

"Dajjal ni kundi kubwa" (Aqrab).

Hali hizi zinapatikana kwa waenezi wa Ukristo leo. Wanasafirisha vitabu vyao toka sehemu moja ya dunia mpaka sehemu nyingine, na pia njia zingine kwa ajili ya kukaribishia watu; kadhalika wanakuza kazi za biashara za namna mbalimbali popote waendapo. Maana moja ya Dajjal ni mwongo. Ni kwa wepi inaweza

kupatikana zaidi sifa hii zaidi kuliko kwa waenezi wa Ukristo wa zama hizi? Wanamweka mtu Yesu aonekane kuwa mungu.

Naam, Dajjal ana alama zingine pia. Ilikuwa awe na jicho moja na ilikuwa awe na punda mkubwa sana. Mawingu ya moshi ilikuwa yaonekane mbele ya punda huyo na nyuma yake. Sifa hizi ni za mfano. Dajjal mwenye jicho moja ni kundi la watu ambao hawaoni mambo ya kiroho. Upande wa kulia katika mfano wa kiroho maana yake ni dini na utawa. Kama Dajjal hana jicho la kulia, ni mfano wa watu wasioweza kuelewa habari na mambo ya kiroho. Punda wa Dajjal ni mfano wa gari moshi. Njia mpya kabisa katika njia za kisasa za uchukuzi. Ilivumbuliwa na Wakristo katika nchi za Ukristo. Zama gari moshi linapiga honi, mlio wake unafanana na mlio wa punda. Linatumia moto na maji, na mawingu ya moshi yanaonekana mbele yake na nyuma yake. Waenezi wa Ukristo hulitumia kwa kujisafirishia sehemu mbalimbali za dunia.

Tunasoma katika Hadithi kuwa safari moja Mtume s.a.w. alikwenda kumtazama Ibn Sayyad, mtu aliyekuwa na ujuzi wa mambo ya ajabu. Alikuwa naye kwa muda fulani na akamwuliza maswali. Kutokana na majibu ya maswali ilionekana kwamba Ibn Sayyad alikuwa na ujuzi wa kizingaombwe na ujuzi wa ghafla unaomjia mtu. Umar ambaye alifuatana na Mtume s.a.w. alinyanyua upanga wake na kusema kwa kiapo kuwa Ibn Sayyad alikuwa Dajjal wa bishara. Mtume s.a.w. alimnyamazisha Umar na kusema:

> "Kama huyu siye Dajjal, si haki kumwua. Na kama ndiye , si juu yako bali ni juu ya Masihi kumwua"
> (Mishkaat, chini ya Ibn Sayyad).

Tukio hili linaonesha wazi kuwa alama za Dajjal zilizotajwa katika bishara za zamani ni za mfano na ni zenye kufasiriwa. Zama Umar alipomtangaza Ibn Sayyad kuwa Dajjal, Mtume s.a.w. hakumpinga. Angeweza kutaja alama ambazo yeye mwenyewe alizisimulia juu ya Dajjal; ya kwamba Dajjal atakuwa na KFR

zimeandikwa usoni pake, ya kwamba atakuwa na jicho moja, ya kwamba atashindwa kufika Madina n.k. (Tirmidh). Alama hizi hazikupatikana kwa Ibn Sayyad. Hakuwa na jicho moja, wala hakuwa na KFR usoni pake. Sifa hizi za maana sana hazikuonwa na Mtume s.a.w. mwenyewe, wachilia mbali watu wengine. Pamoja na hayo Ibn Sayyad alikuwa Madina. Swali ni hili, kama alama kuhusu Dajjal siyo mfano, kwa nini Mtume s.a.w. hakumpinga Umar moja kwa moja? Kwa nini alisita? Kwa nini hakumwambia Umar mara moja kuwa Dajjal ilikuwa awe na jicho moja; awe na KFR usoni pake na ya kwamba ilikuwa asifike Madina? Hivyo ilikuwa ni bure kumwita ibn Sayyad kuwa Dajjal wa bishara. Mtume s.a.w. kutokumpinga Umar moja kwa moja vile hivi kwamba kidogo alifikiri inawezekana ibn Sayyad kuwa Dajjal, kunaonesha kuwa kwa maoni ya Mtume s.a.w., alama kuhusu Dajjal ni za kufasiriwa. Ikiwa hata kwa maoni ya Mtume s.a.w. alama za Dajjal ni za kufasiriwa, hapana mtu mwenye haki kugeuza ukweli huu.

## HOJA YA TATU
## UTAKATIFU WA MTU

Nimeonesha kuwa huu ndio wakati wa kufika Masihi Aliyeahidiwa. Vilevile nimeonesha kuwa kwa ushuhuda wa Mtume s.a.w. Mujaddid, kwa ajili ya karne hii, si mwingine ghairi ya Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa. mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni mdai pekee aliyedai ujumbe huu. Kumkana yeye ni kuikana sheria ya kale ya Mwenyezi Mungu na kupuuza bishara za Mtume s.a.w.

Sasa ninaendelea kueleza hoja zinazohakikisha (mbali na haja ya wakati na bishara za zamani), ya kwamba Mirza Ghulam Ahmad ni mkweli katika madai yake kuwa yeye ndiye mjumbe aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wakati wetu.

Utakatifu unakubaliwa na watu wote kuwa ni mojawapo ya dalili zenye nguvu kabisa juu ya ukweli wa wadai unabii. Katika sehemu hii ninapenda kueleza hoja juu ya tabia ya mdai kama ilivyotajwa ndani ya Quran Tukufu. Imeandikwa:

> "Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale wasiotumai mkutano Wetu husema: Lete Quran isiyokuwa hii, au ibadilishe. Sema: Siwezi kuibadilisha kwa hiari ya nafsi yangu: sifuati ila ninayofunuliwa kwangu. Hakika mimi naogopa nikimwasi Mola wangu, adhabu ya Siku iliyo kuu. Sema: kama Mwenyezi Mungu Angalitaka nisingaliwasomeeni hiyo, wala Asingaliwajulisheni hiyo. Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mwingi kabla ya hayo, je hamfahamu" (10:16-17).

Aya hizi zinaeleza mabishano kati ya Mtume s.a.w. na wapinzani wake. Zinaishia na wito unaosema kuwa Mtume s.a.w. amekuwa na tabia safi kabisa isiyo na ila mpaka hapo. Kwa kuwa na hali hiyo hangeweza mara kubadilika.

Hoja hii ya maana iliyowekwa na Quran kwa ajili ya ukweli wa Mtume s.a.w. inaweza kutumiwa kuwa mizani ya kupimia ukweli au uongo wa kila mdai wa Unabii. Ushuhuda wa kuwapo kwa jua uko juu ya jua lenyewe, kwa mwangaza na joto linaloleta kwetu. Hivyohivyo ushuhuda juu ya ukweli wa mdai wa Unabii uko juu ya utakatifu na usafi wa tabia yake. Utakatifu ambao unasema kwa marafiki, maadui, wageni na wenyeji, walio karibu na walio mbali. Unawaambia - "Fikirini mara mbili tatu kabla hamjaniita mwongo. Kwani mmenifahamu mimi kuwa mtu mkweli hata mkaniita Mwaminifu. Kama sasa mniite mwongo, hamtakuwa na njia yoyote ya kupambanua mkweli na mwongo. Hamtabakiwa na mizani ya kupima mtu mmoja kati ya mwingine." Kila kitu hukua kwa hatua. Hakiwezi kuruka kutoka hatua mpaka hatua nyingine bila ya kupitia kwenye hatua zinazofuata katikati. Mtu mwema anakuwa mwema

na anaufikia wema kwa kupitia kwenye ngazi fulani. Hivyohivyo mtu mbaya anakuwa mbaya kwa kupitia kwenye ngazi fulani. Mtu aliyekuwa anakimbilia upande wa magharibi, hawezi ghafla kujiona yuko upande wa mashariki. Mtu aliyekuwa akikimbilia upande wa kusini, hawezi kujiona mara yuko upande wa kaskazini. Kwa wote walioamua kumkana na kumkadhibisha, Mtume s.a.w. anaonekana akisema:

Nimekaa kati yenu umri mrefu. Nilikuwa mtoto na nikakua kati yenu. Nimekuwa kijana nikiwa pamoja nanyi. Hata nimefikia utu uzima nimo miongoni mwenu. Mmeniona nje na hata nyumbani. Chochote nilichopata kusema au kutenda kinajulikana kwenu. Hakuna yeyote miongoni mwenu aliyeniona kuwa nimepata kusema uongo kabla ya haya, au ufisadi, fitina, uzushi, uasi au hata kujaribu lolote kutaka mamlaka au utawala kwa watu. Mmenichungua kwa njia nyingi na mmenijaribu. Katika kila hali mmeniona mimi imara kabisa kwa ukweli na uamininifu. Mmeniona sina dhambi yoyote wala uchafu. Rafiki zangu na hata wapinzani wangu mliopo mmenijua hata mkaniita "Al-Amin." Nimekuwa nikiaminiwa kwa ukweli wangu na uaminifu mpaka jana. Sikuweza kuongopa juu ya kitu chochote. Niliweza kujitoa kwa ajili ya ukweli. Kwa kweli maisha yangu yamekuwa pambo na heshima kwa ukweli. Mliniamini kwa mambo yote makubwa na madogo. Mlikubali chochote nilichowaambia. Lakini sasa ghafla mnanigeuka na kuniita mbaya kuliko watu wote, mwongo mkubwa na kadha wa kadha. Sikuweza kuongopa juu ya wanadamu, lakini sasa ghafla ninaweza kuongopa juu ya Mwenyezi Mungu? Badiliko la ghafla namna hii katika tabia ya mtu, kweli linawezekana? Je, tunaweza kupata mfano wowote katika taarikh ya wanadamu? Kama nimekuwa mkweli na mwaminifu kwa siku mbili tatu tu, au hata kwa mwaka mmoja, mngeweza kusema kuwa nimejivika ganda tu la uaminifu wala sio kiini, ili kwamba niwaghilibu watu. Lakini sikupata kuwa na hali kama hiyo tangu mwanzo wa maisha yangu. Mmeniona nikiwa mtoto na mpaka mtu mzima. Je, mtoto anaweza kujivika ganda tu la tabia njema? Miaka ya utoto ni miaka isiyo na dhambi. Hakuna mtoto awezaye kujivika ganda la tabia fulani ambayo siyo ya asili kwake. Basi katika muda wa ujana ambao mtu anakuwa na nguvu na tamaa

sana, ningewezaje kuficha tabia yangu hasa nyuma ya ganda la nje? Hamna budi kufikiri na kuniambia ni kwa vipi niliweza kujivika tabia ambayo haikuwa yangu. Ikiwa ninyi kwa kufikiri mtaona maisha yangu yote ya utoto yalikuwa safi kabisa, ya unyofu na uaminifu, hamna haki kuniita mwongo na mzandiki leo. Kwa kuliona jua hamwezi kusema kuwa ni usiku. Kwa kuona mwangaza hamwezi kunung'unika kwa giza. Je, mna haja ya ushuhuda wa ukweli wangu? Maisha yangu mpaka leo yako dhahiri mbele yenu. Ni ushuhuda gani zaidi mnataka? Tabia yangu ni shahidi yangu. Maisha yangu ni ushuhuda wangu. Ziulizeni akili zenu. Mtazisikia zikisema kuwa maisha yangu ni ushahidi wa ukweli wangu. Mimi ni kweli na ukweli ni mimi. Ninauheshimu ukweli nao unaniheshimu mimi. Kwa kuthibitisha ukweli wangu sina haja ya hoja, kwa sababu mimi mwenyewe ni hoja. Kama mkitaka ushuhuda wa jua ni lazima mlitazame jua lenyewe. Ushuhuda wa jua ni jua.

## WAAMINIO WA KWANZA WALIVUTWA

Hii ndiyo dalili ambayo kwayo Abu Bakar r.a. mwaminio wa kwanza aliingia katika Dini ya Islam. Ndiyo dalili ambayo kwayo watu wengi waliotafuta ukweli waliamini madai ya Mtume s.a.w. Inajulikana sana kwamba zama Mtume s.a.w. alipotangaza madai yake, Abu Bakar, rafiki yake mpenzi alikuwa nyumbani kwa jamaa yake mmoja. Mjakazi wake mmoja alimkuta kule na kumhadithia madai ya Mtume s.a.w. - "Mke wa rafiki yako Muhammad anawaambia shoga zake kuwa mumewe amekuwa Nabii kama vile Musa." Abu Bakar hakusema neno lolote aligutuka na kwenda mara ile kwa Mtume s.a.w. Akamwambia kama ni kweli kuwa amedai kuwa Nabii. Mtume s.a.w. akasema; "Naam" na hapohapo Abu Bakar akasilimu. Mtume s.a.w. alisema, "Sikumwita mtu yeyote kwenye Uislamu bila ya kuwa alisita kwanza na kufikiri juu yake. Lakini nilipotamka madai hayo kwa Abu Bakar, hakusita hata dakika moja na mara moja alisilimu."(Zurqaani, jalada 1, uk. 240). Abu Bakar hakuomba apate ishara au ushuhuda wowote. Alijiona anashurutishwa kuamini mara baada ya kusikia madai ya Mtume

s.a.w. Yalikuwaje haya kwa Abu Bakar? Alithibitishiwa na tabia safi ya maisha yake yote Mtume s.a.w. Tabia ya mtu ndio ushuhuda wake.

Bi Khadija, mke wa kwanza wa Mtume s.a.w., Ali, binamu yake, Zaid bin Harith, mtumwa aliyeachwa huru na Mtume s.a.w., wote hawa waliamini madai ya Mtume s.a.w. kwa dalili hii. Bi Khadija amesimulia kisa cha kusilimu kwake. Zama Mtume s.a.w. alipomwona Jibril katika Jabal Hira na kupokea ufunuo wa kwanza wa kumwamuru atangaze Utume wake, alikuja nyumbani kwake na kumpasha habari Bi Khadija: "Ninaogopa juu ya nafsi yangu", alisema kumwambia Bi Khadija. Bi Khadija akimjibu alimfariji Mtume s.a.w. "La, la, Mwenyezi Mungu hatakufedhehesha. U mwema kwa jamaa zako. Unawasaidia wasiojiweza. Unazo tabia njema zilizoadimika kwa wengine. Unawakirimu wageni wako na kuwasaidia wenye taabu."

Ushuhuda kama huu leo umetolewa na Mwenyezi Mungu kuthibitisha madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Hadhrat Ahmad aliishi Qadian, mji ambao wakazi wake ni Mabaniani, Masingasinga na Waislamu. Hivyo alikuwa mbele ya macho ya jamia tatu kubwa za dini. Uhusiano wa ukoo wake na jamia hizi tatu haukuwa wa furaha kama ilivyotakiwa. Alipozaliwa Hadhrat Ahmad Waingereza walikuwa wamechukua sehemu yote ya Punjab. Kabla ya wakati huo, wakazi wa Qadian na pembezoni mwake waliishi kama wapangaji na raia wa ukoo wake. Kwa kuingia Waingereza kukatokea badiliko kubwa. Wakazi wa zamani wa Qadian waliazimia kufanya makubwa katika badiliko hilo. Wakaanza kufanya kazi ya kujikomboa na mapatano ya zamani. Matokeo yake yakawa hivi ya kwamba karibu Qadian nzima ikaingia katika mabishano na baba wa Hadhrat Ahmad.

Kwa amri ya baba yake, Seyidna Ahmad ilimbidi awe akifika mahakamani kwa ajili ya mashauri baina ya wakazi hao na baba yake. Alipokuwa peke yake alikaa akisoma faraghani, lakini hali iliyokuwako wakati mwingine ilimlazimu awe akifika mahakamani kama mtu mmoja akipingana na watu wengi.

Hususa Masingasinga, wenyeji wa Qadian, walikuwa maadui wakubwa wa ukoo wake. Hii ilikuwa ni kwa sababu wakati fulani

kabla, Masingasinga waliutoa nje ukoo wa Hadhrat Ahmad na kuchukua ardhi yote. Ushindi uliporudi mikononi mwa Bwana Mirza, Masingasinga wakawa washindani wake.

Tangu siku za utoto wake Hadhrat Ahmad alipenda sana kusoma na kuutumikia Uislamu. Mara kwa mara alipambana na Wakristo. Mabaniani na Masingasinga katika majadiliano ya hadhara na kuwatoa kwa hotuba zake na maandishi. Hii ilifanya jamia zote za dini ziwe na udhia juu yake.

Hadhrat Ahmad alijulikana sana na viongozi wa jamia zote za dini. Aliishi na kutembea miongoni mwa washindani wake. Lakini wote hao, Mabaniani, Masingasinga, Wakristo na Waislamu walikubali kuwa Mirza Ghulam Ahmad aliishi maisha yasiyo na doa, alionesha kwa kadiri kubwa huruma na dhana njema kwa wengine, na kwa kudumu, amekuwa mkweli na mwaminifu katika matendo yake yote. Aliweza kuaminiwa na wote. Katika mabishano na ukoo wake, hawa washindani kila mara walikubali uamuzi wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Kwa ufupi, wote waliomjua walimfahamu kuwa mtu mstahiki na mwaminifu sana. Wakristo, Mabaniani na Masingasinga, licha ya tofauti kali kabisa ya dini na yeye, walishuhudia utakatifu na tabia yake safi.

## USHUHUDA WA SHEIKH MUHAMMAD HUSSAIN WA BATALA

Utukufu na heshima ya Hadhrat Ahmad kwa wale waliomjua inaweza kupimwa katika maneno ya kiongozi na mwanachuoni mmoja ya Kiislamu, ambaye baadaye alikuja kuwa mmoja wa maadui zake wakubwa; ambaye kwa hakika, aliongoza uadui ambao ulikuwa mkubwa juu ya Seyidna Ahmad na madai yake, wa kwanza kutoa fatwa ya ukafiri kwa Seyidna Ahmad. Kiongozi huyu hakuwa mtu tu wa kawaida. Alikuwa ni Sheikh Muhammad Hussain wa Batala, mkuu aliyekubaliwa katika Madhehebu ya Ahli Hadith. Aliandika maoni yake juu ya *Baraahin Ahmadiyya*, kitabu cha kwanza kikubwa cha Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Katika gazeti

lake Ishaa'at-us-Sunnah, Sheikh huyu aliandika akithibitisha utakatifu na usafi wa tabia ya Seyidna Ahmad:

"Mtungaji wa *Baraahin Ahmadiyya* anajulikana sana kwetu. Kwa kweli, wachache tu wanajua zaidi juu ya fikara zake, juhudi yake n.k. kama tujuavyo sisi. Yeye ni mtu wa wilaya yetu, na alipokuwa mdogo alihudhuria mafunzo ya namna moja pamoja nasi. (Tulisoma Qutbi na Sharah Mulla pamoja). Tangu siku zile tumekuwa tukiandikiana barua na kuzungumza mara kwa mara. Hivyo hakuna mtu awezaye kufikiri kuwa tunatia chumvi kama tukisema kuwa tunamfahamu mtungaji wa kitabu hiki vizuri sana (Ishaa'at-us-Sunnah, 6:7).

Mpaka hapa, Sheikh huyu amethibitisha kuwa ushuhuda wake ni wa kuona sio wa kusikiasikia, bali wa urafiki hasa na mtungaji wa *Baraahin Ahmadiyya.* Sasa soma ushuhuda wenyewe:

"Kwa maoni yetu, kitabu hiki *Baraahin Ahmadiyya - Mfasiri*), hakina mfano wake katika zama hizi, na kwa sababu ya haja za zama hizi zetu hakujapata kuwa na chochote kilicho mfano wa hiki katika taarikh nzima ya Uislamu. Juu ya baadaye hakuna awezaye kusema. "Mwenyezi Mungu huenda akafunua jambo baada ya wakati huu." Ama juu ya mtungaji, tunaweza kusema ya kuwa kumekuwa na Waislamu wachache, kama kulikuwa na wowote, ambao wameendelea kwa kudumu katika kazi ya Islam, kazi kwa mali na kalamu, kwa tabia njema na kwa maneno ya mdomo. Kama tunalaumiwa ati tunatia chumvi, hebu basi tuambiwe, kwa uchache, kitabu kimoja tu kilichoandikwa zama hizi, ambacho kinajibu upinzani wa maadui wa Uislamu, kama Maarya na jamaa wa Brahmu, kwa nguvu ileile na juhudi. Kadhalika tuambiwe juu ya masahibu wawili watatu tu ambao wameazimia kuutumikia Uislamu

kwa njia kama hiihii, kwa mali na kalamu na kwa maneno na nafsi; ambao maisha yao pia ni wakfu, ambao wanaweza kusimama kiume kuwaita maadui wa Uislamu waje kushuhudia kazi hizo na kuondolewa na mashaka juu ya ufunuo kupatikana na ambao wamewafanya wasio Waislamu waonje ukweli wa Uislamu" (Ishaa'at-us-Sunnah, jalada 6, namba 7).

## ALIMPINGA BAADA YA MADAI

Mwandishi wa makala hiyo, Sheikh Muhammad Husain wa Batala, baadaye alianzisha upinzani kwa madai ya Seyidna Ahmad a.s. na kutumia maisha yake yote kwa kumwita kafiri na mwongo. Kama makafiri wa Makka ambao kabla ya madai ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. walimwita mkweli na mwaminifu, na baadaye walipitisha maisha yao katika kumkadhibisha. Amma uadui na upinzani baada ya madai ya mtu hauwezi kuwa na maana sana. Tunafahamishwa na Quran Tukufu kwamba haiwezekani mtu awe ameonekana, baada ya kujaribiwa sana, kuwa mwema na mkweli kwa rafiki na hata maadui, na ghafla ageuke na kuanza kuongopa juu ya Mwenyezi Mungu. Mungu si mdhalimu. Kama maisha ya mtu yamejulikana kuwa safi kabisa hata na maadui zake, Mwenyezi Mungu hatambadilisha mara moja kuwa mbaya wa wanadamu. Mtu anayesimama imara kabisa katika majaribio makubwa, na ambaye haachani na haki hata aone hatari kubwa mno, hawezi ghafla kuanza kuzua juu ya Mwenyezi Mungu. Haiwezekani mtu kulipiwa maovu kwa mema. Wala Mwenyezi Mungu haufuti moyo wa mtu mwema na mkweli na kumjaza uongo na udanganyifu!

Mtume s.a.w. aliwaita maadui zake mara kwa mara na kuwataka wataje hata kosa kidogo katika mwendo wa kibinadamu ambalo alipata kulifanya tangu hapo kabla. Je, hawakumhesabu kama mbora wa wanadamu? Hakuna hata mmoja aliyekubali wito huu. Hivyo hivyo, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitangaza kwamba alihakikishiwa kwamba maadui zake hawataweza kutaja hata dhambi moja katika mwendo wake mzima (Nuzuul-ul-Masih, uk. 212). Kwa kusaidiwa

na uhakikisho huu aliwaita maadui zake mara kwa mara na kuwataka wataje hata dhambi ndogo tu aliyopata kufanya kabla ya madai yake. Walimwona akiwa mtoto hata mtu mzima. Walimtambua kuwa mfano mwema kwa wema wake na utawa. Basi aliwaita mara nyingi katika mas'ala hii. Wale ambao walimjua tangu utoto wake walikuwako. Waliweza kuwa wapinzani wake wakubwa, lakini hawakuweza kuficha ukweli juu ya tabia yake njema tangu zamani. Seyidna Ahmad a.s. kwa mujibu wa ushuhuda wa ulimwengu, alikuwa mtu bora sana. Alikuwa mtawa sana kwa maoni ya wale waliomjua tangu siku za utoto wake, wengi wao wakiwa Mabaniani, Masingasinga na Waislamu. Wengine wao wahai hata sasa, lakini hawathubutu kumtolea kosa maisha yake safi ingawa hawakuamini madai yake.

Kwa ufupi utakatifu wa tabia ya mtu ni hoja yenye nguvu sana juu ya ukweli wa mdai yeyote wa Unabii. Hoja hii imetolewa na Quran juu ya Mtume s.a.w. Inaweza kutolewa pia kwa ajili ya madai ya Masihi Aliyeahidiwa. Ukweli wa madai yake unakubaliwa na utakatifu wa maisha yake kabla ya madai yake. Jambo hili halikanwi na maadui zake. Hivyo basi, tabia ya Seyidna Ahmad a.s.ni ushuhuda juu ya ukweli wa madai yake.

## HOJA YA NNE
### USHINDI WA ISLAM JUU YA DINI ZINGINE

Hoja ya nne inahusu bishara iliyomo ndani ya Quran ambayo inampa Masihi Aliyeahidiwa kazi kubwa ya kuongoza Uislamu mara nyingine ili uzishinde dini zote. Seyidna Ahmad a.s. alifanya kazi hii kwa kuuthibitisha Uislamu kuwa na fadhili juu ya dini zingine. Aliweza kufanya yote haya kwa msaada na rehema za Mwenyezi Mungu, na ukweli huu unayo hoja madhubuti kabisa kusaidia madai yake. Mwenyezi Mungu anasema katika Quran:

"Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote: (9:33; 61:10).

Katika Hadithi za Mtume s.a.w. imebainishwa ya kwamba ushindi wa Dini ya Islam juu ya dini zingine ulioahidiwa katika aya hizo ulikuwa upatikane wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Kuanguka kwa Dajjal, kuangamia kwa Yajuja na Maajuja na kushindwa kwa Ukristo ni kazi kubwa mno ambayo iliwekewa Masihi Aliyeahidiwa kuifanya. Hatari hizi zote zimeelezwa kuwa ni hatari kubwa sana katika taarikh nzima ya Dini ya Kiislamu. Tunaambiwa pia kuwa Dajjal au Uhubiri wa Ukristo utafaulu kuenea ulimwenguni na kushinda dini zingine. Kushindwa kwa Ukristo basi, maana yake ni kushindwa kwa dini zingine zote.

Maneno "kuifanya (Islam) ishinde dini zote," yanahusu wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Katika jambo hili Mufasirina wote wa Kiislamu wanaonekana kuwa wamekubaliana. Mathalan, katika *Jaami 'ul Bayan,* kitabu cha 29, chini ya aya hiyo mmeandikwa:-

*"Wadhaalika 'inda nuzuuli 'isa bin Maryam,"* yaani "Huo ushindi utapatikana zama za kufika Isa bin Mariamu".

Akili pia inakubali jambo hili. Lundo la dini zilizopo leo, halikupatikana hapo zamani. Uhusiano kati ya dini na dini, watu na watu, umeongezeka kinyume na matamanio. Kuvumbuliwa kwa mitambo ya kupiga chapa kumerahisisha, kinyume na kipimo, kazi ya kuandika na kueneza vitabu. Kadhalika kuna juhudi kubwa ya mashindano baina ya dini mbalimbali. Idadi ya mashindano ya makundi ya dini mbalimbali imeongezeka mno. Wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. kulikuwa na dini nne tu zilizoinuka kinyume cha Uislamu. Na wafuasi wao walikuwa waabuduo masanamu wa Makka, Wakristo, Mayahudi na Wamajusi. Chungu ya dini zingine ambazo zimetokea ulimwenguni hazikujulikana wakati ule. Kwa hiyo, katika zama zile ushindi wa Islam juu ya dini zingine zote usingeweza kudhaniwa kuwa mradi hasa wa aya hiyo. Jambo hili linawezekana tu leo. Leo dini zote zimedhihirika nje. Njia mpya za usafiri na ushirika zimekithirisha juhudi baina ya dini mbalimbali.

Hivyo inaonekana kuwa kwa mujibu wa Quran, Hadithi za

Mtume s.a.w. na akili, ushindi wa Islam juu ya dini zingine zote ulichaguliwa kupatikana wakati wa Masihi Aliyeahidiwa, na hili ndilo kusudi la maana sana katika makusudio ya kufika kwake. Kama mdai wa Umasihi anaweza kutimiza kazi hii kubwa, hapana shaka itakayobaki kwamba madai yake ni ya kweli. Dalili ambazo ninaendelea kuzitaja sasa zitaonesha kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ametimiza hasa ushindi uliochaguliwa wa Islam. Na kwa hiyo yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa

Kabla Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. hajatangaza madai yake, haiba ya Islam ilikuwa imepungua hivi kwamba Waislamu wenyewe walianza kukata tamaa. Baadhi yao hawakusita kutangaza maafa ya Islam. Wahubiri wa Kikristo walikuwa shughulini wakiukokota Uislamu nje ya mizizi yake. Ilidhaniwa ya kwamba chini ya karne moja Uislamu utatoweka kabisa duniani. Waislamu waliogofywa na mashambulio ya ukristo hivi kwamba hata wazao wa Mtume s.a.w. Masharifu, waliuacha Uislamu na kuingia Ukristo kwa maelfu, wachilia mbali Waislamu wengine. Hawa hawakuwa wakristo wa jina tu. Bali walifanya kazi kubwa katika kutayarisha na kuchapisha vitabu vya matusi juu ya Uislamu na Mtume s.a.w. Waliweza kuhubiri katika hafla za watu wakitoa mashutumu juu ya Mtume s.a.w. Baadhi ya mashutumu haya hadi yalikuwa yanavunja mioyo. Waislamu walivunjwa mioyo hivi kwamba hata Mabaniani tu ambao walikuwa kama waliokufa na dini yao, ambao hawakupata kuthubutu katika kazi za kuhubiri, ambao walikuwa wakijisumbua bure ati wailinde dini yao, nao pia waliazimia kutoka uwanjani kuushambulia Uislamu, na hata wakapata wafuasi kutoka katika Islam. Madhehebu moja maarufu sana ya Mabaniani, Arya, ilifanya juhudi kubwa kuwaingiza Waislamu katika Ubaniani. Kwa kazi hii walifanya kikundi maalumu cha watu. Tendo hili lilikuwa la kusikitisha sana. Kwa Dini ya Islam ilikuwa kana kwamba mtu mmoja mwindaji hodari sana ambaye alikuwa akiogopwa na ndege na wanyama wa porini alipokuwa hai, sasa amelala maiti akizungukwa na mbesi na tai. Mtu huyo alipokuwa hai, tai hawa hawakuthubutu hata kumsogelea. Lakini sasa wamekuwa wanachana nyama yake wakikalia mifupa yake. Waislamu ambao waliweza kuandika maandishi yoyote kwa kuulinda Uislamu walifanya hivyo

kwa kuomba radhi na nasaha. Mathalan waliweza kusema kuwa sheria za Islam zilikusudiwa kwa wakati wa ujinga; hazihusiani na wakati huu. Na kwa hivi si haki kuzipinga katika wakati huu wa mwangaza na ustaarabu. Katika wakati huu wa kukata tamaa na maangamio, alifika Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. na kuanza kuulinda Uislamu. Shambulio lake la kwanza katika kuulinda Uislamu liliwatia kiwewe maadui za Islam. Aliandika kitabu chake maarufu sana, *Baraahin Ahmadiyya,* ambacho kina maelezo ya misingi ya Islam. Ndani ya kitabu hiki alitoa pia wito kwa wauumbuao Uislamu watoe majibu kwa niaba ya dini zao walau khumsi moja tu ya hoja zilizomo ndani ya *Baraahin Ahmadiyya.* Kama yeyote angeweza kufanya hivyo angepata zawadi ya rupia 10,000/-. Wengi walijaribu kujibu hoja zilizomo katika kitabu hicho lakini hakuna hata mmoja aliyefaulu. Nchi nzima ilivuma kwa kelele za kitabu hicho. Maadui wa Islam wakawa kimya kama mabubu. Mpaka wakati huo Islam ambayo ilikuwa haina nguvu yoyote ya kujilinda, kwa sababu ya Shujaa huyu wa vita ikaanza kushambulia dini za maadui zake. Upanga wa Islam ukawaangukia na wote wakawa mbioni.

Madai ya Umasihi yalikuwa bado kutangazwa. Chuki iliyoletwa baada ya kutangazwa kwa madai bado haijatokea. *Barahiin Ahmadiyya* na wito wake kilipokelewa vizuri na Waislamu. Maelfu yao walitangaza waziwazi kuwa mwandishi wa *Barahiin Ahmadiyya* alikuwa ndiye Mujaddid wa karne hii. Walii mmoja na mwanachuoni wa Ludhiana aliandika:

"Sisi wagonjwa tunakutazamia wewe tu; kwa ajili ya Mwenyezi Mungu uje uwe Masihi wetu."

Kuenea kwa *Barahiin Ahmadiyya* kukaanzisha mwendeleo kwa ajili ya kuulinda Uislamu. Hatimaye maadui wa Islam iliwabidi wakubali kuwa Islam bado iko hai kabisa kama kwanza. Mashaka mashaka yakaanza kuwaelemea. Wakaanza kuhofia hatima yao. Dini yenye nguvu sana miongoni mwa dini adui za Islam, ambayo ilijaa kiburi na majivuno kwa mafanikio yake ya dunia, na ambayo iliifikiria Islam kama mateka yake, ikaanza kutahayari tangu hapo,

hivi kwamba wafuasi wake walikimbia mara walipomwona mfuasi wa Seyidna Mirza Ghulam Ahmad a.s. kama punda milia anavyokimbia akimwona simba akija. Mhubiri wa Kikristo hakuweza kusimama mbele ya Ahmadiyya. Kwa juhudi na kazi ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Islam imeenea tena na kushinda dini zingine zote. Hoja kali ndiyo silaha ya Islam; na hoja zinaweza kuwa pole katika athari yake, lakini athari yake inadumu.

Naam, hapana shaka Ukristo bado una nguvu sana duniani kwa ujumla. Dini zingine zinaendelea kama zamani. Lakini kengele ya mauti yao imekwisha lia, na mgongo wao umevunjika. Mila na ujamaa vinazuia idadi kubwa ya watu wa dini zingine kuingia Uislamu waziwazi. Kwa hiyo, mbele ya wachunguzi wa juu juu tu, ushindi wa Islam si dhahiri sana, Lakini dalili za ndani zipo.

Mchunguzi hodari anaweza kutabiri hatima ya jambo kutokana na mianzo midogo tu. Mti unaweza kuonwa ndani ya mbegu. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ameshambulia dini zingine vikali kabisa hivi sasa hawawezi tena kuyakwepa maafa yao. Hivi karibuni watalala maiti chini ya nyayo za Islam.

Sasa tuendelee kueleza kwa urefu kidogo namna gani Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alizishambulia dini zilizo adui za Islam.

## USHINDI JUU YA UKRISTO

Tukianza na Ukristo, mafanikio yaliyoletwa na Ukristo miaka mingi iliyopita yako juu ya msingi wa itikadi ya Kikristo kwamba Yesu Kristo alikuwa msalabani kuwa kafara kwa ajili ya dhambi za wafuasi wake. Baada ya kufufuka katika umauti sasa amekaa juu mbinguni mkono wa kulia wa Mungu. Hadithi hii imeleta athari kubwa sana katika vizazi vingi vya wanadamu. Kifo cha Yesu "kwa ajili ya wengine" kikaleta furaha kwa wale waliokipokea. Kufufuka kwake na kupaa kwake mbinguni na kukaa mkono wa kulia wa Mungu kukaleta hofu; na hivyo kukawafanya watu wamheshimu kama Mungu. Itikadi mbili hizi, kufa msalabani na kufufuka, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alizikadhibisha kwa msaada wa Agano jipya

lenyewe. Alihakikisha kuwa Yesu asingeweza kufa msalabani. Ilijulikana kwamba hata kama mtu alitundikwa msalabani na kubakia hapo kwa siku tatu, haikuwa lazima afe. Yesu alikuwa msalabani kwa saa tatu nne tu. Kadhalika imeandikwa katika Agano Jipya kuwa zama aliposhushwa chini, mkuki uliochomwa ubavuni mwake ulitoa nje damu yenye joto (Yohana 19:13-34). Hatuwezi kutoa damu ya joto katika mwili wa maiti. Pamoja na hayo, Yesu alitabiri, na bishara hii bado imo ndani ya Agano Jipya, ya kwamba atashuka chini hali yu hai kutoka msalabani. Alisema:

Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara, wala hakitapewa ishara ila ishara ya Yona. Maana kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi" (Mathayo 12:39-40).

Inajulikana kwamba Nabii Yunus alimezwa na nyangumi akiwa yu hai, lakini pia alitoka nje ya nyangumi akiwa hai vilevile. Yesu alikuwa aoneshe ishara ya namna hii. Hivyo ilikuwa aingie kaburini yu hai na atoke nje yu hai baada ya kutwa tatu na kucha tatu. Hoja zilizotolewa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. zilisimamishwa katika misingi ya Agano Jipya. Hapo Wakristo wakawa kama mabubu. Hawakuthubutu kupambana naye. na hawawezi mpaka leo pia. Hadithi nzima ya kifo cha Yesu msalabani kuwa kafara kwa ajili ya dhambi za wanadamu wengine ikaanguka chini. Mvuto mkubwa wa Ukristo kwa Wakristo ukatoweka. Ukristo hapo ukapoteza mguu wake mmoja.

## YESU ALIZIKWA KASHMIR

Mguu mwingine ambao kwao Ukristo umesimama ulikuwa ni itikadi ya kufufuka kwa Yesu na kupaa kwake mbinguni na kukaa mkono wa kulia wa Mungu. Kwa hoja zilizotolewa ndani ya Agano Jipya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. aliuvunja mguu wa pili pia, kama alivyouvunja wa kwanza. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alihakikisha kuwa kwa ushuhuda wa Agano Jipya baada ya tukio

la msalaba, Yesu hakupaa mbinguni bali alikimbilia upande wa Mashariki, akisafiri mpaka Iran, Afghanistan na India akiyaendea makabila yaliyopotea ya wana wa Israeli. Tunajua kutokana na Agano Jipya ya kwamba mara kwa mara aliwakumbusha wanafunzi wake kuwa alikuja kuwakusanya kondoo wa nyumba ya Israeli. Tunasoma:

"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili, na hao nao imenipasa kuwaleta" (Yohana 10:16).

Katika taarikh inajulikana ya kwamba Nebuchadnezzar mfalme wa Babeli, aliyachukua mateka makabila 10 kati ya makabila 12 ya Waisraeli. Na akayahamishia sehemu za mbali za Afghanistan. kwa kuwa Yesu ilikuwa ayakusanye makabila yaliyopotea, ilikuwa lazima kwake kusafiri mpaka Afghanistan na Kashmir ili makabila haya yaupokee ujumbe wake. Kama hakusafiri mpaka sehemu hii ya dunia, basi makusudio ya kuja kwake hayakutimizwa.

Mbali na Agano Jipya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alitoa dalili zinazopatikana katika taarikh na jiografia kusaidia hoja zake. Alieleza habari zilizomo katika vitabu vya taarikh vya zamani kuhakikisha kuwa wafuasi wa zamani wa Yesu walifika Bara Hindi. Katika Tibet kumeonekana kitabu chenye maneno kama yale yaliyomo ndani ya Agano Jipya. Kitabi hicho kina taarikh ya maisha ya Yesu. Ushuhuda kama huu unaonesha kuwa Yesu alisafiri mpaka sehemu hizi. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akatoa pia dalili zingine zinazopatikana leo katika Afghanistan na Kashmir kwa majina ya miji, vijiji, mito, na makabila, kuonesha kuwa sehemu hizi zilikaliwa na Mayahudi. Dalili kubwa kabisa ni jina la Kashmir yenyewe. Ni ugeuzi tu wa Kashir. Wakazi wa zamani sana wa Kashmir huita nchi yao Kashir, yaani Kama Shir, au kama Syria. Neno Shir likasimama badala ya neno Syria. Kadhalika jina Kabul na majina mengine ya Afghanistan ni miigo ya majina katika Syria. Sura, alama za usoni, umbo la kichwa n.k. vya watu wa Afghanistan na Kashmir vinafanana na watu wa Israeli. Kwa hali yoyote ushindi wake ulikuwa katika kugundua kaburi la Yesu. Alilifahamu kuwa liko katika mtaa wa Khanyar, Srinagar. Katika taarikh ya zamani sana ya Kashmir inaonekana kuwa kaburi hili tangu kale limeelezwa kama ni kaburi la "Mfalme nabii" aliyefika huko tangu mika 1900 iliyopita.

Wenyeji wa zamani wa Kashmir hueleza juu ya kaburi hili kuwa ni kaburi la Isa Sahib (yaani, Bwana Yesu).

Kwa ufupi, juu ya ushuhuda uliotolewa kutoka pande mbalimbali Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alihakikisha kuwa Yesu alikufa kifo cha asili na alizikwa Kashmir, na ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyomo ndani ya Quran:

"Na Tukawapa makimbilio mahali palipoinuka penye starehe na chemchem" (23:51), ilitimia barabara. Hali iliyoelezwa katika aya hiyo ni hali hasa ya Kashmir. Habari hii ya maisha na kifo cha Yesu, pamoja na kugunduliwa kaburi hili, ilifanya kuamini kuwa Yesu alikuwa Mungu iwe vigumu. Mungu Yesu akafa. Imani hii haitaishi tena.

## MASIHI ALIYEAHIDIWA NDIYE ALIYEAHIDIWA WA DINI ZOTE

Zama hizi Ukristo una fursa ya kutosha sana kwa sababu ya nguvu yake ya utawala, wingi wa nchi zake, kazi zake za kuhubiri, na maendeleo ya elimu mbalimbali yaliyoletwa na wafuasi wake. Kwa hiyo, ili kuonesha fadhili ya Islam juu ya dini hii, Mwenyezi Mungu alimpa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. silaha maalumu. Kwa ajili ya dini zingine alipewa silaha nyingine moja kubwa. Hii silaha nyingine ilitosha kuzishinda zote. Silaha yenyewe ni bishara zilizomo katika vitabu zinazotabiri kufika kwa Mujaddid mkubwa katika Akhir Zaman. Katika matazamio ya kutimia kwa bishara hizi, wafuasiwa dini zote walingojea kufika kwa Mujaddid fulani. Pamoja na kufika kwa Mujaddid huyo kuna matumaini ya kuamshwa na kutiwa nguvu dini yaliyomo mioyoni mwa wafuasi wa dini mbalimbali. Bishara hizi zimo ndani ya vitabu vya Masingasinga na Mabaniani. Makundi mengine ya dini, makubwa na madogo, pia yanazo bishara ndani ya vitabu vyao vitakatifu. Katika hivyo vyote mna maelezo ya Aliyeahidiwa na wakati wake. Ishara za wakati

ulioahidiwa zilizoelezwa humo karibu zote ni za namna moja. Kama sehemu fulani mmeelezwa ishara nyingi zaidi, basi sehemu zingine ishara zinazoelezwa zinaashiria kwenye wakati huohuo. hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alieleza kuwa bishara za dini zote ambazo zinatabiri kufika kwa Mujaddid katika Akhir Zaman zinahusu wakati mmoja.

Bishara zinazotabiri matukio ya miaka elfu nyingi kabla ya kutokea kwake, ni lazima ziwe zimetoka kwa Mwenyezi Mungu. Haziwezi kuwa zimechanganyika na mawazo ya mtu wala Shetani. Tunalo fundisho la wazi wazi la Quran juu ya madhumuni hii:

"Wala Hamdhihirishii yeyote siri Yake, isipokuwa Mtume Wake Aliyemridhia" (72:27-28).

Elimu ya mambo ya ghaibu au mambo ya baadaye inafunuliwa tu kwa Mitume wakweli wa Mwenyezi Mungu. Hapohapo inaonekana kuwa kinyume na akili kwamba katika wakati mmoja kila jamia ya dini, kila kundi liwe na Rasul, Nabii au Avatar, aliyetumwa kwao kuinua nguvu ya dini yao na kuifanya ishinde dini zingine zote. Hii itakuwa na maana kwa Mitume wa Mwenyezi Mungu kuhitilafiana na kushindana wao kwa wao. Inaonekana upuuzi pia kufikiri kuwa katika wakati mmoja kila jamia ya dini itaishinda kila jamia ya dini nyingine. Kwa ufupi, kwa kuwa bishara hizi zote ni za kweli na za Kiungu, haziwezi kuwahusu watu mbalimbali. Kama zingewahusu watu mbalimbali, ingekuwa tu maana ya ugomvi na fujo. Ingekuwa kinyume na mpango wote wa akili. Hivyo, shauri tunaloweza kushika ni hili tu ya kwamba bishara hizi zilizoandikwa katika vitabu vya dini na zikashikwa mpaka wakti huu na jamia mbalimbali za dini, kwa hakika zinamhusu mtu mmoja. Makusudio ya Mwenyezi Mungu katika kupeleka bishara hizi kwa watu wa kila dini yalikuwa hivi ya kwamba jamia ya kila dini duniani itazamie kufika kwa mwalimu huyo Aliyeahidiwa afike katika wakati hasa, atangaze ukweli wa Islam, na kuwaita wafuasi wa dini zote kwenye boma la dini moja ya kweli. Kwa njia hii alete ushindi wa Islam juu ya dini zingine. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa Mahdi siye ila ni Masihi, Krishna siye ila ni Masihi, Aliyeahidiwa

wa Masingasinga na Mabaniani hawa wote sio ila ni Krishna, Mahdi au Masihi wa bishara za zamani. Hivyo jamia mbalimbali za dini hazina budi kumtazamia mtu mmoja. Kuja kwa mtu huyu mmoja kulitabiriwa katika majina mbalimbali. Kila jina lilijulikana na jamia nyingine. Kwa hiyo kila jamia ilitazamia kudhihiri kwa mtu fulani. Hii ilikuwa kwamba jamia mbalimbali za dunia zilifikiri kwamba Aliyeahidiwa huyo ni Aliyeahidiwa wa bishara zilizomo ndani ya vitabu vyao wenyewe, na katika lugha yao wenyewe. Awe kwao kama mmoja wao, na sio kama mgeni. Hatimaye anapodhihiri na ishara za wakati wake na ukweli wa madai yake unadhihirika, waukubali Uislamu na kuwa Waislamu kwa ushuhuda na wito wake.

Mpango wa Mwenyezi Mungu unaonekana umejaa hekima. Ili kuondoa ugomvi baina ya makundi mbalimbali na kuleta mapatano miongoni mwao walipewa shauri kuwa watu wa kila kundi wachagune hakimu. Baada ya kila kundi kuchagua hakimu wao ikaonekana ya kwamab wote wamemchagua mtu huyohuyo mmoja ila tu kila kundi lilimpa jina lililopendelea . Kwa namna hii amani ikapatikana.

Hivyo basi Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.alisema ya kuwa bishara zote zilizomo katika dini mbalimbali kuhusu kuja kwa Mujaddid zinahusu wakati huu, na haikuwa na maana kutazamia Mitume wa Mwenyezi Mungu zaidi ya mmoja katika wakati mmoja, kila mmoja ajaribu kueneza habari zake za ukweli na kuvuta watu upande wa dini yake duniani. Ilikuwa dhahiri kwamba dini hizi mbalimbali zenye majina mbalimbali zilitazamia kufika kwa mtu mmoja. Aliyeahidiwa huyo hakuwa mwingine zaidi ya Masihi Aliyeahidiwa wa Islam. Nabii si wa jamia yoyote moja. Ni wa Mwenyezi Mungu. Yeyote aliyeamua kuungana naye kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, anaweza kumfanya kuwa nabii wake. Kwa hiyo Masihi Aliyeahidiwa ni wa wote. Wafuasi wa kila dini wanaweza kudai kuwa ni wa kwao. na kwa hivi maendeleo yao ya kiroho yako pamoja naye. Wanaweza kumkubali kuwa kiongozi wao. Wanaweza kufanya hivyo kwa kukubali Islam na kuwa Waislamu. Na hapo watatimiza bishara kubwa inayotabiri ushindi wa Islam juu ya dini zote.

Kuendewa kwa dini zingine kulikuwa lazima na kwenye athari

sana hivi kwamba dini zingine hazikuweza kukaidi. Kila dini inazo bishara kuhusu Mujaddid katika Akhir Zaman. Ishara zinazomhusu huyo Mujaddid zinapatana na wakati huu. Ishara hizo zote zimetimia. Kuna mdai mmoja tu wa unabii naye ni Masihi Aliyeahidiwa, Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Wafuasi wa dini zinazofundisha bishara hizo wanaweza kuchagua mojawapo ya njia mbili. Ama wanaweza kuzikana bishara hizo. Au, ni lazima wakubali kuwa Aliyeahidiwa wa Islam pia ni Aliyeahidiwa wa bishara zao wenyewe. Hivyo ni lazima wamkubali na kukubali Islam. hakuna njia ya tatu. Kila moja ya njia mbili hizi zilizo wazi inaweza kuongoza kwenye ushindi wa Islam. Kama wafuasi wa dini zingine wakanushe bishara zilizomo katika vitabu vyao, wanakanusha ukweli wa dini yao. huu utakuwa ushindi dhahiri wa Islam. Na kama wakubali hizi na kumkubali mdai pekee wa unabii ambaye bishara zenyewe zinamtimilia, wanaingia katika boma la Islam. Tena itakuwa ni ushindi kwa ajili ya Islam.

hatua hii yenye nguvu ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ni budi ilete matokeo makubwa. Kadiri wakati unavyosonga mbele wafuasi wa dini zingine ni lazima wageuke zaidi na zaidi kwenye Uislamu ili kwamba wakati ufike ambao dini ya dunia nzima itakuwa Islam. Masihi Aliyeahidiwa amepanda mbegu. Hivi ndivyo wafanyavyo manabii wa Mwenyezi Mungu. Mti unakua na kutoa matunda kutokana na mbegu, lakini katika wakati wake. Watu wa dunia wanaonja matunda na kufaidi ladha yake na kupumzika chini ya kivuli chake, lakini ni hapo tu wakati ufikapo.

## KIONGOZI WA MASINGASINGA ALIKUWA MWISLAMU

Kundi moja la dini linajaribu kuukwepa wito usiokwepeka wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Kundi hilo ni la Masingasinga. Kiongozi wa Masingasinga, Guru Nanak, alifika muda mrefu baada ya Mtume Muhammad s.a.w. Kwa vyovyote, hata kitabu kitukufu cha Masingasinga kina bishara kuhusu kufika kwa nabii katika Akhir

Zaman. Imeandikwa waziwazi ndani ya vitabu vya Masingasinga ya kwamba nabii Aliyeahidiwa atadhihiri katika sehemu ya Batala (sehemu ambayo uko mji wa Qadian); kwa hiyo bishara ya Masingasinga imetimia barabara katika nafsi ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Taabu ya dini hii ya Masingasinga ni hii ya kwamba Mtume s.a.w. alikuwa Khaataman-Nabiyyin, Muhuri wa Manabii, chanzo na kibali cha Manabii wote. Ni namna gani kikundi kidogo kama cha Masingasinga kinaweza kutokea baada ya Mtume s.a.w.? Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alipokea mwongozo maalum kwa ajili ya dini hii ya Masingasinga. Aliona katika njozi ya kwamba Guru Nanak r.a. hakuwa mwanzilishi wa dini yoyote ile. Alikuwa mfuasi wa Dini ya Islam na alikuwa Mwislamu wa kweli. Ufunuo huu umeleta badiliko kubwa miongoni mwa wafuasi wa dini hii nao wakaanza kujitenga na Mabaniani na kutupa masanamu nje ya nyumba zao za ibada. Walikataa kabisa kuwa Wahindu!

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akaanza kuchungua. Akaona ya kwamba Granth Sahib, Kitabu cha Masingasinga, na mkusanyiko wa hotuba za Bawa Guru Nanak r.a. ndani yake mna mawaidha juu ya Sala tano, Saumu ya Ramadhani, Zaka na Kuhiji. Wale wasiosimamisha nguzo hizi wanaonywa vikali sana. Katika vitabu vingine vya Masingasinga mmeonekana kwamba Bawa Guru Nanak alikuwa akiishi miongoni mwa Mawalii wa Kiislamu. Alizuru makaburi ya mawalii wa Kiislamu. Aliungana nao katika Sala za jamaa.Alikwenda Hijaz kuhiji, na alizuru Baghdad na miji mingine mitukufu ya Kiilsamu. Seyidna Ahmad a.s. aligundua shati moja ambayo Masingasinga wameihifadhi na kuisujudia kama kumbukumbu. Kwenye shati hiyo mmeandikwa aya za Quran, Sura ya 112, mathalan, aya mashuhuri ya "Qursi." (2:256) na aya isemayo: Innaddina 'indallahil-Islam (3:20). Na Kalima ya Islam, *Laa ilaaha illallahu Muhammadur-Rasuulullah*, imeandikwa. Kwa vile watawa wa Kisingasinga hawakujua Kiarabu, waliziheshimu aya hizi kama mafumbo ya Kiungu. Hawakutambua kama maandishi hayo yalikuwa ni tangazo la Uislamu la Bawa Guru Nanak. Kwa hoja zenye msingi katika vitabu vya Masingasinga na kuhusiana na kumbukumbu zilizoheshimiwa sana nao, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alianza kuwaambia Masingasinga kuwa Kiongozi wao

mkubwa alikuwa Muislamu. Kukaanza kuwa na mpambano mkali na Masingasinga. Kuelekea kwao kwenye kupenda Uislamu kuko dhahiri sasa. Kadiri maana ya kweli ya ugunduzi huu itavyowafikia akilini mwao, watatambua kuwa wamepotea mbali kabisa na imani ya Kiongozi wao. Dini ya Masingasinga wa kwanza ilikuwa Islam. Polepole walianza kutengana kwa sababu ya magomvi ya kidini. Magomvi haya, kama yanavyothibitishwa na uchunguzi wa taarikh, yalikuwa kwa sababu ya Mabaniani, na sio Waislamu. Walifanya uhasama baina ya mwafaka uliokuwako wa Masingasinga na Waislamu. Lakini Masingasinga ni watu mahodari. Mtu anaweza kutumai, wanaweza kutanguliza ukweli juu ya siasa, wakasahau yaliyopita, na kuingia Uislamu, wakipiga ukelele wao maalum wa kidini wa Sat Sri Akaal (Mwenyezi Mungu Mmoja ndiye wa Kweli). Mujaddid Aliyeahidiwa ndani ya vitabu vyao, amekwisha fika sawa na ahadi iliyotolewa katika sehemu ya Batala. Ni juu yao kumkubalia na kujiunga naye na kujiunga katika jihadi ile aliyoianzisha kwa niaba ya Islam, na kujitenga kabisa na mambo ya uzushi na ukafiri.

## WAZO LA MAANA

Njia ya tatu ya kushambulia ambayo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. aliitumia kwa kuleta ushindi wa Islam juu ya dini zingine ilikuwa ni ufafanuzi wake wa wazo la maana sana lililofundishwa na Islam. Wazo hili linahusu nia ya kila dini juu ya dini zingine. Kabla ya wakati wa Hadhrat Ahmad, ilikuwa ni desturi, kwa kweli, ilifikiriwa kuwa ni sawa na ni haki kwa kila dini kuzifahamu dini zingine kuwa ni za uongo. Kuacha baadhi ya watu na baadhi ya fikra, Mayahudi wote waliamini kuwa Yesu alikuwa mwongo, Wakristo wote waliamini hivyohivyo juu ya Mtume s.a.w. wazartashti waliwatambua manabii wa dini zingine kwa namna hiihii. kwa kurudi, dini zingine zilimfahamu nabii wa Wazartashti namna hiihii. Wafuasi wa dini tatu hizi waliwafahamu waalimu wa dini zingine kama waongo na namna hiihii wafuasi wa dini hizo walifahamu kuwa Waanzilishi wa dini hizo nne walikuwa waongo

n.k. Mabishano kati ya dini na dini yakawa makali sana. Kila kundi la dini lilikuwa vitani na kila kundi jingine, na pamoja na hayo watu wenye akili waliweza kutambua ukweli katika dini zote. Kwa vyovyote ilionekana ni ukatili kuwafamu Waanzilishi wa dini zote kuwa waongo. Mtu hakuweza kumshawishi mwingine kufikiri hivyo. Lakini je, kulikuwa na tatizo lolote?

Matokeo ya mashindano haya yalikuwa ni mwongezeko wa chuki na uadui wa kidini. Mabaniani walisoma juu ya Waalimu wa dini yao na waliathirika na tabia zao njema na utawa. na kisha wakawasikia watu wengine wakisema kuwa Waalimu hao walikuwa waongo na wahadaa. Hii iliwashangaza sana na kuwakasirisha. Kwa hakika walifikiri kuwa hawa watu wengine walichochea hivyo kwa kijicho na kutopenda kuelewa. Kwa namna hii, wafuasi wa dini zingine walisoma juu ya Waanzilishi wa dini zao, na walivutwa na utawa wao, lakini waliposikia wakitukanwa na watu wengine walighadhibika. Taabu kubwa ikatokea. Ni kwa namna gani heshima ya waalimu wa dini ingepatikana? Wale waliochungua suala hili bila ya upendeleo na mawazo ya mbele, hawakuweza kufikiri kwamba Mwenyezi Mungu aliweza kuwateua watu wa taifa moja kwa fadhili zake na kuwasahau wengine wote. Kwa hali yoyote hakuna aliyethubutu kusema hivyo. Kila firka ya dini ilifikiri kuwa kuwakubali Waanzilishi wa dini zingine kulileta ukanaji wa dini yao wenyewe.

Mabaniani wakajaribu kubuni tatuzi moja. Wakaanza kufundisha kuwa dini zinatoka kwa Mwenyezi Mungu. Dini mbalimbali ni kama njia mbalimbali zinazoongoza kwenye jumba moja. Dini ya Mabaniani ilikuwa ndio bora ya njia hizi zote. Tatuzi hili la kijanja lilifungua hoja kali mbili zilizoonekana hazijibiki. Hoja ya kwanza ilikuwa hii, ya kwamba kama dini zote, kama tuzionavyo leo, zimetoka kwa Mwenyezi Mungu na zinaongoza Kwake, basi kwa nini zinafundisha mambo mbalimbali katika mambo ya lazima na maana sana? Kungekuwa tofauti katika maelezo, lakini sio katika misingi. Barabara nyingi zinaweza kuongoza kwenye mji fulani, lakini itakuwa si akili kufikiri kuwa barabara zinazotokea mashariki ziufikie mji huo kupitia Magharibi au Kaskazini, au kupitia Kusini. Zinaweza kukosana kidogo, lakini

welekea wao uwe mmoja. Katika misingi na mambo ya kweli hakuwezi kuwa na tofauti au hitilafu. Kunaweza kuwa hitilafu, mathalan, katika namna ya ibada, katika maelezo ya wajibu wa dini na kadhalika. Lakini ni vigumu kudhania ya kwamba kwa watu fulani (Mayahudi na Waislamu) Mwenyezi Mungu alisema: "Mimi ni Mmoja," na kwa wengine (Wakristo) "Mimi ni watatu," na kwa wengine (Mabaniani) "Mimi ni wengi," na kwa wengine (Wachina) "Mimi ni kila mahala na kila kitu." Wala haiwezekani kuwa kwa watu fulani (Waislamu) Mwenyezi Mungu aseme kuwa yu juu kuliko vitu vyote na Yu mbali na kujimithilisha katika umbo la mwanadamu." na bado kwa wengine (Mabaniani) "Hata katika maumbo ya wanyama kama nguruwe na kadhalika". Wala haiwezekani kwamba kwa watu fulani (Waislamu) afundishe kuwa maisha baada ya kufa hayana budi," na kwa wengine (Mayahudi) afundishe kuwa "La siyo." Wala hawezi kusema kwa watu fulani (Waislamu) kuwa "Wafu hawarudi duniani," na kwa wengine (Mabaniani) aseme kuwa wafu wanaweza kurudi duniani na baada ya kufa wanadamu hupita katika mwandamo wa maisha mengi. Kwa ufupi, inawezekana kwamba mafundisho yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yaoneshe mabadiliko madogo kutegemea watu wanaoyapelekewa (wakati wao, mazingira n.k.); lakini hakuwezi kuwa na hitilafu kubwa, wala tofauti katika hali ya matukio ya taarikh, mathalan, au katika mambo ya msingi. Mafundisho ya dini tuyaonayo leo yanahitilafiana sio katika maelezo tu, bali katika misingi vilevile. Hitilafu za misingi hasa haziwezi kusemwa zimesababishwa na Mwenyezi Mungu, na mafundisho ya dini ambayo ni tofauti sana kila moja kwa jingine hawawezi yote kuongoza kwa Mwenyezi Mungu.

Hoja ya pili kuhusu tatuzi hili la ukarimu la Mabaniani ni kwamba kwa maana fulani Mabaniani wanaifahamu dini yao kuwa na fadhili juu ya dini zingine (licha ya kuwa zingine zinaweza kuongoza kwa Mwenyezi Mungu). Dini ya Mabaniani ni bora, ya kale n.k. Hali hii ni ya taabu sana. Ikiwa Mwenyezi Mungu alifunua dini bora sana tangu azali, kulikuwa na haja gani kufunua baada yake dini duni kuliko bora? Kama wanadamu waliweza kupokea na kunufaishwa na dini kamilifu tangu hapo mwanzo, kulikuwa hakuna

shabaha yoyote katika kuleta dini pungufu moja baada ya nyingine. Inaonekana ni kinyume na akili kufikiri kuwa dini kamilifu na bora kabisa ingekuja mwanzo wa mwendo wa wanadamu, lakini baadaye zama maarifa ya wanadamu na ufundi yameendelea sana, tuwe na dini duni kuliko bora. Ni sawa na akili kufikiri kwamba dini za baadaye ziwe kamilifu zaidi, zenye maendeleo zaidi kuliko za kwanza. Kama sio zaidi, ziwe walau kamilifu na nzuri.

Hoja hizi mbili zilikuwa kavu sana. Kwa wale wanaochagua kuwakilisha dini kwa njia hii, swali la maana sana lilikuwa, - "Ni gani ulikuwa hasa mpango wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu tokea azali mpaka leo?

Wakristo nao wakatoa tatuzi.Walisema kwamba Mwenyezi Mungu aliwaita wanadamu wote katika mwongozo wake. Alifanya hivi kwa njia ya Yesu Kristo. Mwenyezi hana vipenzi vyake. Kwake makundi yote ya wanadamu yalistahiki kwa usawa kupata msaada wake na mwongozo. Lakini hata tatuzi hili halikutatua tata yenyewe. Swali likabaki palepale, "Ni nini alichofanya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu kabla ya kumleta Yesu?" Katika Biblia tunasoma ya kuwa Yesu Kristo alikusudiwa kwa Waisraeli, sio kwa wengine. Kwa vyovyote, hata kama iwe ni kweli kwamba Waalimu wa Kikrsto baadaye walifundisha Ujumbe wa Kristo kwa watu wote wa duniani, swali linabaki. "Ni nini alichofanya Mwenyezi Mungu kwa milioni nyingi za wanadamu waliopita kabla ya Yesu? Je, walipita bila ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu? Ujumbe wa Yesu haukuweza kuwafikia wale walioishi na kufa kabla yake.

## HALI YA DINI ZINGINE

Hivyo, swali likawa bila ya jawabu la kutosha. hali ya maelezo ya Risala za dini mbalimbali ilikuwa hapana budi iainishwe. Bila ya kutosha, dini hizi mbalimbali zilijiona zenyewe zimejitoma katika vita isiyokoma. hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akageukia kwenye Quran Tukufu kwa ajili ya jawabu la swali hili na akatoa taswira mpya na shabaha mpya. Quran Tukufu inasema:-

"Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Mwonyaji" (35:25).

Kwa mujibu wa fundisho hili hakukuwa na taifa lolote ambalo halikupata Mwonyaji kutoka kwa Mwenyezi Mungu wakati wowote na mahala popote ulimwenguni. Kwa mujibu wa Quran Tukufu manabii wamekuwako kila zama na kila nchi. Bara Hindi, China, Urusi, Afghanistan, sehemuza Afrika, Ulaya, Amerika, wote walikuwa na manabii sawa na fundisho la Quran Tukufu kuhusu mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, zama Waislamu wanaposikia juu ya manabii wa watu wengine au nchi zingine, hawawakani. Hawawaaibishi kama waongo. Waislamu wanaamini kuwa watu wengine walikuwa na manabii wao. Kama wengine walikuwa na Manabii, vitabu na sheria, hawaleti mgogoro wowote kwa Islam. Bali wanathibitisha fundisho la islam. Ila tu Islam inafundisha kwamba mafundisho ya zamani yalipimwa sawa na haja na uwezo wa watu wa zamani. Fundisho kamilifu ambalo Mwenyezi Mungu amelileta kwa Mtume s.a.w., limekuja katika wakati ambao wanadamu wameendelea vya kutosha kupokea na kunufaishwa nalo. Mtume wa Islam alitumwa kwa wanadamu wote. Wazo hili la fundisho la Mungu ni rahisi zaidi kueleweka. Hakuna watu wowote waachwao nje ya mpango wa uongozi wa mbingu. Leo Islam tu ndio njia ya mwongozo, kwa sababu ndiyo ya mwisho na kamilifu. Kwa kuwasili fundisho kamilifu zaidi, mafundisho ya zamani hayana budi yabatilike. Kubatilika kwake ni yumkini sio tu kwa mujibu wa Islam. Bali ni ukweli ulio dhahiri wa taarikh. Vitabu vya dini za zamani havikuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu. Viliingiliwa na mageuzi na maongezi ya wanadamu. Vimekuwa batili. Ni vya kweli kwa sababu usuli zao zimetoka kwa Mwenyezi Mungu. Ni vya uongo kwa sababu ya kuingiliwa na mageuzi ya wanadamu. Wazo hili la mwongozo wa mbingu katika kila zama ambalo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alilieleza toka ndani y Quran lilionesha ushindi. Kama yeyote achague kukana wazo hili, itakuwa akubali kuwa Mwenyezi Mungu anatoa mwongozo kwa watu fulani na sio kwa wengine, tokeo ambalo hakuna yeyote mwenye akili barabara anayeweza kukubali. Kwa hali yoyote, kama ikubaliwe kwamba

mwongozo wa Mwenyezi Mungu umekuwa ukipokelewa kila mahala nyakati zote, basi ukweli wa Islam hauwezi kuhojiwa. Hii ni kwa sababu Islam ni dini ya mwisho na kwa kuwa ni Islam tu ndio inayofundisha jinsi mwongozo wa Mwenyezi Mungu ulivyowafikia watu mbalimbali katika nyakati mbalimbali.

Habari hii ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu ina mvuto wa pekee. Watu wenye elimu, hata wawe wanafuata dini gani, wakiwa wenye mawazo mapana, wanaathirika na kushawishika nayo. Wanaona kwamba wazo hili si rahisi kulikana. Kukanwa kwake ni kukanwa kwa Mwenyezi Mungu. Kama hawawezi kumkana Mwenyezi Mungu, wala wazo la Islam juu ya mwongozo wa Mungu, hawana budi kuukubali Uislamu. Hawana njia nyingine. fikara nyembamba na ovyo iliyoenea zamani ikageuka kuwa ukarimu halisi, iliyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa. Jambo hili, miongoni mwa mambo mengine, lilifanya lilete ushindi wa Islam zama hizi.

## SURA MPYA YA MAJADILIANO YA DINI

Njia ya nne ambayo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad aliitumia kwa kuonesha fadhili ya Islam juu ya dini zingine ilikuwa na fikara mpya ya majadiliano ya dini. Wazo hili pia lilionesha ushindi na likawa lisilojibika; na tena, lilielezwa sawa na mwongozo wa mbingu. Maelezo yake yalibadili mawazo yote na njia za majadiliano ya dini. Hadhrat Ahmad alileta njia za haki na zenye akili kwa kupima madai ya dini. Maadui za Islam hawakuweza kuona makosa yoyote ndani yake, wala hawakuweza kuleta hoja za maana kwa kupinga Islam. Kama walikataa mizani hii, walishindwa. Kama waliikubali, pia walishindwa. Maadui za Islam hawakuwa na ujanja wa kuepuka mpambano huo.

Ni lipi lilikuwa wazo jipya la majadiliano ya dini? kabla ya wakati wa Hadhrat Ahmad a.s., majadiliano ya dini hayakuwa na upeo. Upande mmoja uliweza kutoa hoja zozote kinyume cha mwingine. Na hapo hapo uliweza kudai madai yoyote uliopenda kwa niaba yake mwenyewe. Kwa namna hii, kulikuwa hakuna

mwisho katika majadiliano ya dini wala mwisho wa uhasama ulileta nayo, na kwa haya yote, kulikuwa hakuna faida yoyote katika safari ya watafutao ukweli. Kama majadiliano fulani yawe na mwendo maalumu ni lazima yaendeshwe sawa na masharti fulani. pasipo masharti hatuwezi kupambanua mshindi. Ndivyo ilivyokuwa kwa wasemaji wa dini. Kabla ya Hadhrat Ahmad, msemaji wa dini aliweza kusema lolote alilopenda juu ya dini yake. Wazo hilo liliweza kuchukuliwa kutoka kitabu au fundisho jingine. Lakini msemaji huyu aliweza kusema kuwa wazo hilo ni la dini yake na kitabu chake. Majadiliano yaliyofuata hayakuwa majadiliano kuhusu wazo la dini yoyote iliyokuwako bali juu ya mawazo ya kubuni ya watetezi wake; hasa, mawazo yaliyoletwa na washindani wenyewe binafsi, sio ya dini walizokuwa wakishindania. Watafutao ukweli wakawa hawana msaada. Baada ya majadiliano makali walisimama pale waliposimama kwanza. Hadhrat Ahmad a.s. akaonesha upuuzi wa majadiliano ya namna hii. Akaweka sharti kwamba kama kitabu fulani kimetoka kwa Mwenyezi Mungu na kilikusudiwa kuwaongoza wanadamu, ni lazima kijisemee chenyewe. Hakina budi kutoa mafundisho yake katika maneno yake chenyewe waziwazi. Kadhalika kiweke hoja kinachotaka kuweka juu ya mafundisho yake. kama kitabu kishindwe kueleza madai yake na hoja kwa fundisho hilo ni za kuelezwa na wafuasi wake, kina maana gani basi kuwa kitabu cha Mungu? Je, inawezekana kweli dini inayofundishwa na kitabu hicho kuwa ya Mungu? La, ni lazima iwe dini iliyoundwa na watu. Kwa ajili ya dini hiyo hatudaiwi chochote kwa Mwenyezi Mungu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye anayedaiwa nasi kitu fulani, maana tunaeleza madai na hoja kwa niaba Yake. Hadhrat Ahmad akafundisha kwamba kwa kupata hatima njema ya majadiliano, ni lazima kwamba wasemaji wa vitabu hivyo vya Mungu wasitoe jambo lolote kuhusu vitabu hivyo mpaka wataje fundisho hilo ndani ya vitabu hivyo; vilevile, mpaka wataje kutoka vitabuni humo hoja za fundisho lenyewe. Kanuni hii ya majadiliano ya dini ikawa na nguvu sana. Maulamaa wa dini zingine hawakuweza kuipinga. Kuipinga kanuni hii kungekuwa na maana ya kwamba mafundisho yanayodhaniwa kuwa ya vitabu hivyo hayamo vitabuni humo. Kama yamo, basi ni lazima yaonekane na kusomwa. Pamoja na hayo kama

mafundisho yoyote yanaweza kurejewa katika vitabu fulani, ni lazima hoja za mafundisho hayo zichukuliwe kutokana na vitabu vyenyewe. Kwa hakika, haikuwa lazima sana kuuliza hivi. Ubongo wa mwanadamu ulivyoumbwa na Mwenyezi Mungu una akili. Ulikataa kukubali jambo lisilokuwa na ithbati yake au lisilopatana na akili. Ilikuwa vigumu kwamba Mwenyezi Mungu awatake watu kukubali mambo fulani lakini asitaje dalili za kusaidia mambo hayo. Kwa hiyo, Maulamaa wa vitabu vya dini hawakupinga kanuni hii. La, si hivyo, ingehakikisha udhaifu wa dini yao. Lakini hata hivyo hawakuona rahisi kukubali kanuni hii. Bila shaka itawashangaza watu wengi, lakini ni kweli ya kwamba zama madai ya dini zingine yalipopimwa kwa nuru ya kanuni hii, ilionekana kwamba tisa ya kila kumi ya madai yaliyotolewa kwa niaba ya dini hizo hayakusaidiwa na vitabu vya dini hizo. Zama mafundisho ya vitabu fulani yanaweza kurejewa kutoka katika vitabu hivyo, mara chache au pengine kabisa hayakusaidiwa na hoja zilizotolewa na vitabu hivyo vyenyewe. Kama kwamba Mwenyezi Mungu alisema neno moja na akawataka watu walithibitishe kwa hoja yao.

Kwa njia hii Hadhrat Ahmad alionesha kuwa Maulamaa wa dini mbalimbali walibuni misingi au kuazima fikara nzuri kutoka kwa wengine na kuzisema ni za dini zao. ndipo wakapambana na Maulamaa washindani wao na uzushi huo. Kukafuata majadiliano ya kipuuzi. Kama mambo hayo yangeonekana bora na yenye nguvu, yangeonesha tu ubora wa fikara na akili za Maulamaa wao; wala yasingeonesha ubora wa dini zao. Maana mambo yaliyoonekana bora na yenye nguvu hayakuonekana ndani ya vitabu vya dini ambazo mambo hayo yanadhaniwa kuwa yake. Kinyume cha haya yote, Hadhrat Ahmad alionesha kwamba mafundisho yote na madai yanayowekwa na Islam yanaweza kutolewa ndani ya kitabu chake, Quran Tukufu. Kadhalika hoja za mafundisho hayo zinaweza kutolewa kitabuni humo. Hadhrat Ahmad alionesha haya katika njia nyingi mbalimbali na katika hafla mbalimbali. Maadui za Islam wakajiona wameshindwa. Waliona vigumu kupambana na wito huo au kukwepa maafa ya matokeo yake. Wito huo ukabakia na utabakia bila jawabu. Unawaita washindani wa dini kwenye kanuni ambayo ni vigumu kuikataa, na ambayo kama ikubaliwe, inafanya iwe

vigumu kuenea kwa madai ya uongo au kujivika vilemba vya ukoka katika majadiliano ya dini. Zaidi watakavyosisitiza Waislamu juu ya kanuni hii, ndivyo zaidi Maulamaa wa dini za uongo watakavyotoweka kwenye uwanja wa majadiliano. Udhaifu wa hali yao utakuwa dhahiri zaidi na zaidi kwa wafuasi wao na ushindi wa Islam juu ya dini zingine utadhihirika zaidi na zaidi.

## UKARIBU NA MWENYEZI MUNGU NDIYO MIZANI YA UKWELI WA DINI

Njia ya tano aliyoitumia Hadhrat Ahmad a.s. katika mashindano yake na dini zingine, ilionesha kabisa msiba kwa ajili yao. Iliuletea Uislamu ushindi usiozuilika. Hadhrat Ahmad aliwakumbusha maadui za Islam kwamba makusudio ya dini hasa ni kumwezesha mwanadamu kupata maungano na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, mizani ya maana ya ukweli baina ya dini na dini ni daraja na kadiri ya maungano ambayo kila dini imefaulu kuleta baina ya Mungu na mwanadamu. Maungano hayo yanahusika na daraja ya ukweli wa kila dini. Kwayo tunaweza kupima ni kwa kadiri gani dini fulani inakubaliwa na Mwenyezi Mungu. Maungano kati ya mtu na Mwenyezi Mungu yawe na ishara za dhahiri. Tunafahamu kwamba zama vitu viwili vinapoungana, kila kimoja kinakuwa na athari kwa kingine. Tuendapo karibu na moto, tunachomwa au kwa kadiri fulani tunapata joto lake, na tunapokunywa maji tunazima kiu yetu na tunachangamka na kuburudika. Chakula kizuri kinaongeza uzito wetu. Mazoezi hugeuza misuli yetu na kuleta uzuri mwilini. Namna hii, dawa pia zina athari zake. Zinasaidia au kuzidhuru kazi za kawaida za mwili. Litakuwa jambo la ajabu sana kama maungano na Mwenyezi Mungu yaonekane kuwa hayana athari yoyote ile; kama tusujudu katika sala kwa muda mrefu ajabu, tufunge saumu mpaka kufa, tutoe sadaka karibu mali yetu yote, na bado tusipate mabadiliko yoyote katika nafsi zetu au katika hali ya maisha yetu. Kama kazi zetu zote za dini, toba yetu, na sadaka zetu, zijiishie hivihivi tu, kwa nini tutafute ukaribu wowote na Mwenyezi Mungu?

Una faida gani ukaribu huo kwetu? Tunapokuwa na ukaribu na mfalme wa kidunia na kustahiki kupata msaada wake na fadhili, tunaona matokeo ya ukaribu huo. Tunapata heshima. Maombi yetu yanakubaliwa, taabu zetu zinaondolewa. Wengine wanaotuona toka mbali wanaona kwamba tunapokea fadhili na msaada wa mfalme. Lakini hakuna chochote kinachoweza kujulikana au kuonwa cha matokeo ya maungano ya mtu na Mwenyezi Mungu? Hakuna athari yoyote inayoweza kuonwa katika maendeleo yetu au katika uhusiano wetu na watu wengine?

## DINI ILIYO HAI

Kwa hiyo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alisisitiza kwamba dini inayodai kuwa ya ukweli, hutoa matokeo ya dhahiri kwa wale wanaotenda sawa na mafundisho yake. Mfuasi wa kweli wa dini hiyo amwone Mwenyezi Mungu na kufaidi fadhili Zake. Ukaribu wa Mungu na mwanadamu lazima uwe na ishara waziwazi. Kwa hivi, Maulamaa wa dini mbalimbali hawana budi waache kushambuliana, waache kutoa madai makubwa kwa niaba ya dini zao, na kuumbua dini zingine. Badala ya hayo, walete istishhada ya uzima wa kiroho na nguvu waliyoipata kwa kufuata dini zao. Waoneshe ni daraja gani ya ukaribu na Mwenyezi Mungu wameipata kutokana na dini zao. Watoe mifano ya watu waliofuata dini zao wakavuna neema za kiroho ambazo dini hizo zimeahidi kutoa. Dini inayoonesha ukweli wake kwa mizani ya namna hii, ni budi ikubaliwe kama dini iliyo hai na ya kweli. Lakini dini kinyume na hivi, ni budi ikataliwe kama iliyokufa na ya uongo. Inawatweza wafuasi wake badala ya yenyewe kubeba mizigo yao. Kushiriki katika dini kama hiyo kunaleta mkosi katika dunia hii na pia adhabu katika Akhera. Kanuni hii ya kupimia dini iliyo hai haikuweza kupingwa. Mara ilipotolewa tu, ilianguka kama vile umeme juu ya dini zingine. Watu wa dini hizo wakaanza kutafuta njia za kujiokoa katika balaa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akatangaza kwamba istishhada ya uhai inaweza kupatikana katika Dini ya Islam tu. Dini

zingine zote hazinayo. Kuna aliyetaka kuhoji? Kama yeyote alitaka, basi ilikuwa tu auingie mtihani wa nguvu na Masihi Aliyeahidiwa. Hakuna aliyethubutu. Hakuna dini nyingine iliyobakiwa na uhai. Makelele na mahubiri ya kubwata ya dini ya mtu ni rahisi. Lakini kutoa istishhada ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na ukaribu naye ni kugumu.

## ASKOFU ALIITWA

Wito wa Masihi Aliyeahidiwa ulifikishwa kwa Mabaniani, Wakristo, Mayahudi na kila jamii ya dini. Lakini hata mmoja hakujitokeza. Kwa njia mbalimbali na katika hafla mbalimbali, aliwaita viongozi wa dini zingine waupime ubora wa maungano na Mwenyezi Mungu. Wakaona haina maana. Akamwita Askofu wa Lahore, mkuu wa jimbo kubwa la India ya Kaskazini, apime pamoja naye athari ya dua. Si Agano Jipya limeahidi kama Wakristo wawe na imani hata sawa na chembe ya haredali, wataweza kuhamisha milima? Hivihivi Waislamu wameahidiwa katika vitabu vyao kwamba waaminio wa kweli watategemea msaada wa Mwenyezi Mungu na juu ya matokeo ya dua zao. Kwa hiyo ilimstahili Askofu huyu kujiunga katika dua na kuona ni dua ya nani ingekubaliwa zaidi wakati wa mashindano - ya Mkristo au ya Mwislamu? Askofu akaziba masikio. Aliona ni salama kama ajitie hamnazo. Ukimya wa Askofu huyu ukaumua hasira. Baadhi ya magazeti ya Kiingereza yakamshambulia Askofu huyu. Maaskofu walikuwa wakila mishahara minene minene na kupiga makelele mengi, magazeti hayo yalisema, lakini zama walipoitwa kwenye majaribio au mashindano wakaondoka uwanjani. Askofu huyu hata halikumgonga. Licha ya mashutumu yote hayo, aliendelea kujikurupusha tu.

Masihi Aliyeahidiwa alirudia wito huo tena na tena. Lakini hakuna aliyethubutu. Hatua hii pia, kama hatua zingine kwa niaba ya Islam, ilikuwa isiyojibika. Kila mtu mwenye akili timamu hana budi akubali ubora wake. Matokeo yake yalikuwa ushindi wa Islam. Wasio Waislamu ni lazima wafahamu zaidi na zaidi umauti wa dini zao. Kwa wakati huohuo ni lazima watambue alama za

uhai wa Islam. Fadhila ya Islam ni lazima idhihirike zaidi na zaidi. Katika majadiliano ya maneno mtu anaweza kujiona asiyeshindika mpaka mwisho, lakini zama mashindano ni ya matendo, ukweli lazima uonekane upande mmoja. Hatua hii iliyotolewa na ikatumiwa Na Masihi Aliyeahidiwa ni lazima ioneshe athari yake kadiri wakati unavyoendelea mbele. Machoni pa watu wenye akili Islam imekwisha shinda. Hakuna dini nyingine inayoweza kudai kuwa hai. ushindi wa Islam umekwisha dhihirika.

Aina hizi tano za mashambulio alizozitumia Masihi Aliyeahidiwa kwa niaba ya Islam, ziliuongoza Uislamu kwenye ushindi juu ya dini zingine. Hivyo basi, kazi ya Masihi Aliyeahidiwa imekwisha fanywa: Kama Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad siye Masihi Aliyeahidiwa, basi swali linazuka hivi, ni kipi zaidi atakachofanya Masihi wa kweli atakapofika? Je, atawasilimisha watu kwa upanga? Kutakuwa na faida gani kwa ajili ya Islam au kwa Waislamu hao kuwasilimisha kwa nguvu? Hebu fikiri kidogo - kama Wakristo waanze kuwatanasarisha Waislamu kwa nguvu, tungesemaje sisi wote na wote wenye akili juu yao na tungewafikiriaje? Je, tusingesema kwamba jambo hilo ni kosa na upumbavu? Je, hatutamshutumu Masihi wa kweli kwa njia hii kwa kufanya kama haya? Lazima astahili lawama! Kusilimu kwa nguvu kutatisha sana. Kutaudhuru Uislamu na kugeuza watu wote waungwana wenye murua wauchukie Uislamu. Hivyo, Masihi "Aliyeahidiwa," hangekuwa na haja ya upanga. Njia yake ni lazima iwe njia ya hoja na dalili. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. amekwisha onesha kuwa Uislamu ni mshindi. Kwa hiyo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ndiye Masihi Aliyeahidiwa. Amefanya vile ilivyokuwa afanye Masihi Aliyeahidiwa.

Pengine inasemwa kuwa hoja alizotumia Hadhrat Ahmad hazikuwa zake. Zilikuwako tangu zamani. Viweje ushindi wa Islam ulioletwa na hoja hizo usemwe umeletwa naye? Upinzani huu ni wa kipuuzi. Upanga unaweza kukata bila mkataji? Unaweza kufanya kazi yake hapo tu atakapopatikana wa kuushika. Hali ya Islam wakati wa Masihi Aliyeahidiwa ilikuwa kwamba upanga wa hoja uliotumiwa na Islam tangu zamani ulikuwako, lakini Waislamu sio kwamba hawakuweza kuutumia tu, bali hawakuwa hata na

habari ya kuwako kwake. Masihi Aliyeahidiwa akapokea undani mpya wa maana ya Quran Tukufu. Akaeleza upya ukweli wa Islam na kuzitaja tena hoja ambazo kwazo ukweli huo umesimamishwa. Ndipo akatumia hoja hizo katika kuulinda Uislamu na katika vita ya Islam na dini zingine. Akafundisha matumizi ya hoja hizo kwa wafuasi wake na wengine. Hivyo, ushindi wa Islam umesababishwa na yeye. Quran Tukufu badala ya kuwasaidia Waislamu na Islam ilikuwa kizuizi na tatizo kwa ajili yao. Ila kwa Masihi Aliyeahidiwa tu, mambo yangejibakilia hivyo. Bunduki bila ya mfyatuaji huwa ni tisho, sio kwa adui, bali kwa mwenye bunduki mwenyewe. Quran Tukufu kwa kutoeleweka imekuwa mzigo mzito. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akatangaza madai yake, akaumba imani mpya na tumaini jipya. Baraka na neema za Quran Tukufu zikaanza kuonekana. Akapambana na maadui za Islam kwa hoja ambazo maadui hawakufaulu. Kwanza walijiona wakijilinda, baadaye wakaona hata kujilinda ni kugumu. Baadhi yao wakaandika maombi serikalini kuiomba isimamishe kazi ya Hadhrat Ahmad a.s. kwa nguvu. Hu ulikuwa ushindi dhahiri. ushindi wa Islam ukahakiki.

## HOJA YA TANO
## KUHUISHWA UISLAMU

Hoja ya tano ya ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ni kwamba ameuhuisha Uislamu. Ameuhisha Uislamu na kuujadidisha kuwa msafi na wenye nguvu. kwa kuwa hii ndiyo iliyokuwa kazi ya Masihi Aliyeahidiwa, bila shaka yeye ndiye Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa.

## WAISLAMU WAKO KINYUME NA UISLAMU

Watu wote wenye akili wanakubali kuwa Uislamu wa leo sio Uislamu alioufundisha Mtume s.a.w. kwa Masahaba zake. Wasiokubali ni Masheikh tu ambao wamekuwa hawana uwezo wa

kuutambua ukweli kwa sababu ya ulalamishi wao usiokwisha. Kuna mashaka kwamba jambo fulani limekosekana katika Uislamu wa leo. Juu ya Uislamu wa wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. tunaambiwa katika Quran Tukufu:

"Mara nyingi wale waliokufuru wanapenda wangalikuwa Waislamu (15:3).

Je, ndiyo fikara na maelekeo ya wasio Waislamu siku hizi? La, bali upande mwingine ni kitu cha mzaha na mashaka. Wachilia mbali wasio Waislamu, Waislamu wenyewe wameingiza mashaka juu ya mafundisho mengi ya Uislamu. Wengine wanaona makosa katika baadhi ya kanuni zake, wengine juu ya mafundisho yake ya tabia, bado wengine wanaona makosa juu ya amri zake katika maisha ya kila siku. Uhakika ulioletwa na Uislamu katika akili za wafuasi wake hauko tena siku hizi. Waislamu leo hawako tayari kutoa sadaka na kufanya jihadi walivyoweza kufanya hapo zamani. hali kuwa kama hii, yatupasa kukubali mojawapo ya mambo matatu. Ama tukubali kwamba nguvu ile ya Uislamu tunayosoma katika taarikh ni uongo mtupu na ni chumvi iliyoungwa na vizazi vilivyokuja nyuma. Au tukubali kwamba hakuna mtu yeyote anayejaribu kutenda sawa na mafundisho ya Quran. Au tukubali kwamba Uislamu tunaoufuata sio Uislamu wa kweli, kwa sababu hii Uislamu hautoi tena matunda ambayo ulitakiwa kutoa. Kwa kweli jambo hili la tatu ndilo linaloonekana la dhahiri. Nguvu ya utakaso ya Uislamu na athari ya matokeo yake imethibitishwa na sio taarikh tu bali pia ushuhuda unaoweza kuonekana katika sehemu zote za dunia. Zama Waislamu walipoelewa na kuufuata Uislamu sawasawa, walifaulu na kutawala. Wala haiwezi kusemwa ya kwamba hakuna anayefuata uislamu siku hizi. Waislamu wa madhehebu mbalimbali wanafuata Uislamu wanaouamini. Kuna Waislamu wanaojichagulia kanuni ngumu kwelikweli na hawasiti hata kutoa maisha yao; na bado hawafanikiwi lolote kwa ajili yao wala kwa ajili ya Uislamu. Uamuzi basi ni kwamba wazo la Uislamu lililomo akilini mwa Waislamu leo sio la kweli. Mtume s.a.w. alisema:

"Hakutabakia katika Uislamu isipokuwa jina lake"
(Mishkaat, Kitabul 'Ilm).

Inaonekana kwamba wakati umefika. hakuna kilichobakia katika Uislamu isipokuwa jina lake, yaani Uislamu wa nje lakini wa ndani umekwenda. Aina ya Uislamu unaoaminiwa na kufuatwa leo haiwezi kutoa yale matunda iliyotoa hapo zamani. Wala Uislamu huu hauwezi kuwavuta wafuasi wa dini zingine jinsi ulivyowavuta hapo zamani. hapana shaka, baadhi ya watu wa dini zingine wanavutwa na utukufu wake uliochujuka. Lakini ni wachache, ni lazima watu hao wawe wazuri mioyoni mwao kwa namna isiyo ya kawaida. Kwa neno zima, Uislamu hauna mvuto ule hasa uliokuwa nao hapo kabla. Maneno ya Mtume s.a.w. yanaashiria kwenye shauri hilihili. safari moja alisema Mtume s.a.w.

"Watu wa Umati wangu watafarikiana katika firka sabini na tatu. Zote zitastahili moto isipokuwa moja."

Baadhi ya Masahaba wakauliza ni Waislamu wepi hao ambao watakuwa upande wa Uislamu wa kweli. Mtume s.a.w. akajibu:

"Wale watakaofuata mfano wangu na mfano wa Masahaba zangu" (Tirmidh).

Safari nyingine akasema:

"Enyi watu, ishikeni elimu kabla haijatoweka"

Waliomsikia wakauliza:

Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, itatowekaje elimu na hali tunayo Quran Tukufu?"

Mtume s.a.w. akajibu:

"Kama vile ilivyotokea zamani. Mama zenu wakuhurumieni, je, hamwoni kwamba Mayahudi na Wakristo wana vitabu vyao? Lakini hawayajali mafundisho ya vitabuni mwao waliyoletewa na Manabii wao kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Elimu inatoweka ardhini zama wale wenye elimu wanapotoweka ardhini" (Mishkaat, Kitabul I'tisaam bissunnah).

Fungu la mwisho la maneno hayo Mtume s.a.w. alilirudia mara tatu. Kutokana na Hadithi hii inaonekana kwamba wakati wa hatari kubwa ulikuwa uufikie Umati wa Mtume s.a.w. Wakati wa hatari ulikuwa wakati elimu itatoweka ardhini. Hapohapo inaonekana kwamba zama wakati huo utakapofika, kundi moja miongoni mwa Waislamu litaonekana likifuata Uislamu wa kweli. Kundi hilo lilikuwa liwe kundi litakaloiga mfano wa Mtume s.a.w. na Masahaba zake. Kundi hilo si jingine ghairi ya kundi la Masihi Aliyeahidiwa. Kwani Mtume s.a.w. alisema pia:

> "Umati wangu ni kama mvua. Sijui kama sehemu ya mwanzo wake ndiyo bora zaidi au ya mwisho" (Mishkaat, Sura: Thawaabu Haadhihil Ummah).

Hivyo, maneno ya Mtume s.a.w. "Wale watakaofuata mfano wangu na mfano wa Masahaba zangu" yanahusu wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa. Kwa kweli, hakuna firka au kundi jingine lolote linaloweza kutoa sifa hii. Hakuna firka ya Kiislamu inayoweza kuiga mfano wa Masahaba wa Mtume s.a.w. mpaka wawe wamemwona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika hali ya kimwili, mpaka wawe wameingia chini ya mvuto wake wa kiroho.

## KUHUISHWA UISLAMU NI AHADI YA MUNGU.

Tokana na Hadithi niliyotaja hapo juu inafuata kwamba kuhuishwa Uislamu na kujadidishwa, baada ya kutoweka elimu na dini ya kweli miongoni mwa wafuasi wake, ni ahadi ya Mwenyezi Mungu . Kwahiyo ni lazima kwamba yule anayedai kuwa Masihi

Aliyeahidiwa, ayaweke tena mafundisho ya kweli ya Uislam na kuupa ulimwengu maana ya kweli ya Quran Tukufu. Kama ashindwe, hawezi kuwa Masihi Aliyeahidiwa. Kama , kwa upande mwingine, katika siku za hatari ambazo Mtume (s.a.w.) ametuonya juu yake, aweze kuulinda Uislamu katika upotovu ulioletwa na wafuasi wa Uislamu wajinga, basi yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa. Yeye na wafuasi wake wanatoa sifa iliyomo ndani ya bishara ya Mtume (s.a.w.) - wale watakaofuata mfano wangu na mfano wa Masahaba zangu. Inafuata kwamba katika Ujadidishaji wa Uislamu tunayo mizani ya maana sana ya kupima ukweli wa yeyote anayedai kuwa Masihi Aliyaahidiwa. Ni lazima tuone kama Uislamu, kama unavyojulikana na kufuatwa leo, kweli umepoteza sura yake halisi.Na baada ya kufanya hivi itatupasa tuone kama mdai yeyote wa Umasihi kwa hakika amehuisha ile sura yake ya kweli.

Kusema kwamba Uislamu wa leo umepotea mbali na Uislamu wa kweli, inakubaliwa kwa mikono miwili. Watu wote wenye fikara wanakubali, Kitendo cha Mwenyezi Mungu chenyewe kinajulisha kwamba Waislamu wamepoteza usafi wa imani yao. Uislamu unaojulikana siku hizi wajishuhudia wenywewe kwamba Uislamu umeharibika. Mambo haya yanaonesha kwamba Uislamu wa leo ni hitilafu kabisa na ule Uislamu uliokuwako hapo kabla. Suala linabakia ni hili tu, "Je, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ameleta au hakuleta ulimwenguni mafundisho safi ya Kiislamu, ambayo kwa uzuri na mvuto wake, yanaweza kuwasogeza watu wote karibu nayo? Je, hakuondoa doa katika dhahabu ambalo watu wasiyo na ucha Mungu na Masheikh wenye ubinafsi walichanganya pamoja nayo?" Kwa kuyajibu maswali haya ninaendelea kutoa mifano mmoja baada ya mwingine ya jinsi Uislamu ulivyopotelewa na jinsi Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.w.) alivyohuisha uzuri wake mara nyingine.

## MAONI KINYUME NA TAUHID:

Fundisho kubwa kabisa la dini ni itikadi juu ya Mwenyezi Mungu. katika Uislamu imani hii inafanya kazi kama mzizi ambao kwao imani zingine na wajibu zinatokeza nje kama matawi na

majani. Imani juu ya Mwenyezi Mungu ni msingi. Imani zingine zimo katika hali ya maongezo au madoido ya imani hii kubwa. Shina la imani juu ya Mwenyezi Mungu ni Tauhid (Umoja wa Mwenyezi Mungu). Mtume (s.a.w.) tangu kutangaza madai yake ya Utume mpaka kufariki kwake, aliendelea kufundisha jambo hili la maana sana *"Laa ilaaha illallah."* Alitaabishwa sana sana kwa hali zote, lakini hakuacha kufundisha ukweli huu. Alipokuwa akifariki fikara moja tu ilikuwa akilini mwake. Ilikuwa fikara ya "Umoja wa Mwenyezi Mungu" Aliogopa isije fundisho hili la maana sana likaanguka baada yake; alipata taabu sana kwa fundisho hili.Waislamu wanaosoma katika vitabu vya Hadithi na taarikh juu ya sehemu ya mwisho wa maisha ya Mtume (s.a.w.) akilala kitandani hali yu mgonjwa sana. Ugonjwa ulizidi kuwa wa taabu kwa ajili yake. Fikara za yale yanayoweza kutokea nyuma yake kinyume cha fundisho lake la Tauhid zilimsumbua sana roho yake. Je, Waislamu watasahu kabisa aliyowafundisha kwa muda mrefu? Je, wataanza kumshirikisha Mwenyezi Mungu na vitu au watu wengine? Mashaka haya hayakuwa juu yake au ahli zake. Bali yalikuwa juu ya wafuasi wake, Ummati wake. Akitaabishwa na fikara hizi, aligeuka kitandani mwake tena na tena , na alipokuwa akigeuka alisema:

"Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya Mayahudi na Wakristo! Wamefanya makaburi ya manabii wao kuwa misikiti" (Bukhari, Sura Maradhi -un-Nabii).

Kwa kusema hivi ni dhahiri alikuwa na maana ya kuwaonya wafuasi wake kinyume cha maelekeo ya kuwasifu Maimamu wao mpaka kuwapa sifa ya Mwenyezi Mungu ambaye ni Mmoja tu. Manabii ni wanadamu tu. Katika sehemu ya mwisho ya maisha yake, Mtume (s.a.w.) hakutaabishwa na fikara nyingine yoyote. Alitaka wafuasi wake wakumbuke kumwabudu Mwenyezi Mungu peke Yake. Maneno yenye kuvuta haya ambayo yamejaa huruma, yaliwafanya walioyasikia ambao walijaaliwa mapenzi ya Mtume (s.a.w.) mioyoni mwao waone wasifikirie kabisa jambo hili la *shirk.* Walipenda kukanusha hata maelekeo kidogo sana ya kuweza

kushirikisha chochote na Mwenyezi Mungu. Lakini Oh! msomaji mpenzi, unajua fika kwamba Waislamu leo - wengi wao - wanakana waziwazi fundisho ambalo Mtukufu Mtume (s.a.w.) aliona ni la lazima sana kuwaonya wafuasi wake alipokuwa kitandani katika hali ya gharighari. Nani angedhani ya kuwa Waislamu ambao zaidi ya miaka 1,300 iliyopita walitoa maisha yao yote kwa ajili ya kulinda fundisho la Tauhid, wangeanza kuwabudu mawalii wao na kuelekea makaburini kwao hata kwa Sala tano; ya kwamba wangeanza kuwasifu wanadamu kwa sifa ya elimu ya mambo ya ghaibu; ya kwamba wangewajaalia watakatifu wao sifa za Mwenyezi Mungu; ya kwamba wangeomba dua zao kwa wafu na kuchinja dhabihu juu ya makaburi yao; ya kwamba wangewadhani Masheikh wao kuwa na nguvu ya kumshawishi Mwenyezi Mungu afanye wapendavyo wao; ya kwambva wangewadhania kuwa na uwezo wa kuwako kwa kimwujiza mahala popote na wakati wowote; na ya kwamba wangechinja wanyama kwa majina ya watu hao ghairi ya jina la Mwenyezi Mungu? Na lililo baya kupita yote, nani angedhani kuwa wangeyafanya yote haya na kusema ni mafundisho ya Quran Tukufu na Mtukufu Mtume s.a.w.? Lakini, Alhamdu lillah, zama fundisho la Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu likipotolewa hivi na Waislamu kila sehemu, zama idadi yao kubwa inafurahia itikadi na matendo kinyume na Uislamu, kaburi la Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe limehifadhika na shirki hii. Kwa kufahamu fikara ya Mtukufu Mtume s.a.w. Wake aliyokuwa nayo wakati akikata roho, Mwenyezi Mungu amelisalimisha kaburi lake na matumizi haya ya shirki. Lakini makaburi ya watakatifu wa Kiislamu hayako salama kama hivi. Yamekuwa mahala pa ibada za kishirikina hata ni shida kuwa tofauti na ibada za Mabaniani katika mahekalu yao. Kama Mtume s.a.w. angekuja na kuwaona wafuasi wake leo, asingefikiri ni Waislamu. Labda, wafuasi wa dini fulani ya kipagani.

Inaweza kusemwa ya kwamba itikadi na ibada hizo za kishirikina ni kwa wale tu wasiojua kusoma na walio maamuma, na ya kwamba watu wenye elimu wanachukia sana mambo hayo. Lakini hali ya jumla ya watu hupimwa katika daraja yao ya mwandamano. Kama idadi kubwa ya mwandamano yaWaislamu imeangukia kwenye

fikara hizo na matendo, hatuna budi kusadiki ya kuwa Waislamu wameachilia mbali Tauhid iliyofundishwa na Mtukufu Mtume s.a.w. Fundisho la *Laa ilaaha illallah,* ndiyo roho ya Uislam. Roho hii Waislamu wa kawaida tu ndiyo wanaoshika itikadi hizi. Viongozi wa dini na Masheikh pia wanazishika na wako pamoja na wafuassi wao. Kama mioyoni hawasadiki itikadi hizi, kwa nini hawazikanushi kwa maneno ya vinywa vyao? Ni dhahiri kwamba hawako imara. Wanaogopa kuwafarikisha wafuasi wao. Hii yote ni istishhada ya uoza wa imani ya Waislamu juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu.

Naam, kuna fikara safi miongoni mwa Waislamu ambazo zinafikiri hazina hata chembe ya mwelekeo wa shirki. Wanajitenga Waislamu wa firka zingine na wanaona kwamba hao wanaubomoa Uislam kwa kuingiza ushirikina. Tofauti yao ni hii tu, ya kwamba Waislamu wengine wakiwa wanamshirikisha Mwenyezi Mungu na mawalii wengi, wao wanamweka nabii Isa yuko hai mbinguni. Mtume s.a.w. mbora wa Manabii wote na Mkuu wao, amezikwa ndani ya ardhi; lakini nabii Isa yuko huko mbinguni sasa yapata zaidi ya miaka 2,000. Saa ya kifo chake bado haijaja. Waziwazi wanasoma ndani ya Quran Tukufu kwamba mawalii na watakatifu wote wanaoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu ni wafu wote si wazima. Hakuna hata mmoja ajuaye ni lini atafufuliwa. Inasema Quran Tukufu:

"Ni wafu, si wazima, na hawajui watafufuliwa lini"(16::22).

Kadhalika wanajua ya kuwa Wakristo wanamwabudu nabii Isa badala ya Mwenyezi Mungu. Kwa kusoma aya hii ndani ya Quran Tukufu na kujua kwamba Wakristo wanamwabudu nabii Isa badala ya Mwenyezi Mungu, hata hivyo hawawezi kuacha itikadi yao hii ya kuwa nabii Isa yuko hai mbinguni. Na kwa kushika itikadi hii bado wanafikiri, wanaamini Umoja wa Mwenyezi Mungu.

Vile vile wakiwalaumu watu wengine kwa shirki, wao wenyewe wanaamini kuwa nabii Isa aliweza kufufua wafu. Wanasoma ndani ya Quran Tukufu:

"Na ni haramu kwa mji Tulioangamiza ya kwamba wao hawatarejea: (21:96).

Hii ndiyo kanuni isiyobadilika ya Mwenyezi Mungu. Wafu hawarudi duniani. Mahala pengine tunasoma:

"Na nyuma yao iko kinga mpaka siku watakapofufuliwa: (23:101).

Ni wazi kuwa wafu wamo nyuma ya kinga fulani. Watakaa humo mpaka siku ya Kiyama.

Firka hii ya Kiislamu ni Ahli Hadithi, lakini wanasahau aliyoyasema Mtume s.a.w. juu ya kurudi kwa wafu duniani. Zama baba ya Jabir, Abdallah, alipokuwa anakufa. Mwenyezi Mungu aliuliza, "Unataka jambo lolote?" Abdallah alisema anataka aishi ili ajiunge na Mtume Mtukufu s.a.w. katika Jihadi na afe katika njia ya Mwenyezi Mungu, halafu aishi tena na afe tena katika njia ya Mwenyezi Mungu na kadhalika. Hapo Mwenyezi Mungu akasema:

"Laiti nisingelijifanyia ahadi kutorudisha wafu duniani, ningefanya hivyo" (Tirmidhi, Kitabu Tafsir, Sura Ali-Imrani; Ibn Maaja, Babu fiima ankaratil Jahmiyyatu; na Mishkaat, Abwabu Jami'ul Manaaqib).

Inaonekana kwamba haikumbukwi ya kuwa kufufuliwa kwa wafu na kurudi duniani hakuruhusiwi na Mwenyezi Mungu. Ni kanuni Yake isiyobadilika. Angewezaje Yesu kufanya kinyume na hayo? Naam, Quran Tukufu ilitumia maneno:

"Nitahuisha wafu" (3:50),

na maneno hayo yanahusu nabii Isa, lakini maneno hayo hayo yametumiwa kwa ajili ya Mtukufu Mtume s.a.w. lakini hakuna Sheikh yeyote anayetoa sifa kwa Mtume s.a.w. ya kufufua wafu. Quran Tukufu inasema:

"Enyi mlioamini, Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapokuiteni kwenye yale yatakayowapeni uzima" (8:25)

Zama tamko la *Ihyaa* linatumiwa kumhusu Mtume s.a.w. lina maana ya kutoa uhai wa kiroho kwa wafu wa kiroho. Mwenyezi Mungu Ikiwa maana hii ya Ihyaa inawezekana na tujuapo kwamba Mwenyezi Mungu peke Yake ndiye awezaye kufufua wafu, na tujuapo pia kwamba wafu hawarudi duniani, tena kwa nini hatuwezi kutia tafsiri ya kiroho juu ya neno *Ihyaa* linapotumiwa kumhusu nabii Isa? Kwa nini tuzijaalie aya hizi za Quran Tukufu tafsiri isiyopatana na aya zingine za Quran nzima; tafsiri ambayo waziwazi inatutua kwenye shirki?

Jamaa hawa wanaamini kwa ithibati kabisa kwamba nabii Isa aliweza kuumba ndege. Na bado wanasoma ndani ya Quran Tukufu ya kuwa Mwenyezi Mungu tu ndiye Mwumbaji. Quran Tukufu inasema:

"Na wale ambao wanawaita badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochote, bali wao wameumbwa" (16:21)

Tena inasema:

"Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika ambao wameumba sawa na kuumba Kwake, kwahiyo viumbe(vya pande mbili) vimeshabihiyana kwao? Sema: Mwenyezi Mungu ndiye Mwumbaji wa kila kitu, naye ni Mmoja, Mwenye nguvu" (13:17).

Na tena inasema :

"Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawawezi kuumba nzi wajapokusanyika kwa jambo hili""(22:74).

Wanasoma aya hizi ndani ya Quran Tukufu na bado wanampa nabii Isa sifa ya uumbaji na hali yeye mmoja wa hao wanaoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu.

Kwa ufupi, Quran Tukufu inafundisha waziwazi kuwa Mwenyezi Mungu tu ndiye Aumbaye. Kama mtu yeyote aweze

kuumba, basi yeye pia atastahiki kuabudiwa. Na bado wanapofikia aya kama "Nawaumbieni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege" (3:50), wanadhani inaonesha kuwa nabii Isa aliweza kuumba ndege tokana na udongo. Hawakumbuki ya kuwa neno fulani linaweza kuwa na maana nyingi. Huu ndiyo upotovu wa hatari sana juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu ambao Waislamu, Wanazuoni na maamuma, wafuasi wa Maimamu wanne na wasiokuwa wafuasi wao, Masunni au Mashia, wa firka hii au ile, wameuingia. Mbele ya upotovu huu hakuna awezaye kusema kwamba Waislamu bado wanaamini *"Laa ilaaha illallah."* Hapana shaka Waislamu bado wanayo itikadi hii na wanatamka Kalima hii. Lakini pia wanaamini itikadi kinyume na Tauhid; hivyoWaislamu wamehama kwenye mafundisho ya kweli ya Mwenyezi Mungu kama vile mataifa na watu wengine walivyoshika itikadi za kipagani. Ili kusahihisha makosa haya na kuwarudiha Waislamu kwenye fundisho hasa la Tauhid, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.w. akaeleza na kufundisha tena fundisho hasa la Uislamu juu ya Tauhid. Ufafanuzi wake wa fundisho hili ni wa kweli katika roho ya Uislamu na pia unavutia sana, hivi kwamba anayeukubali, anaona upya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na chuki ya shirki ambayo ndiyo yaliyowapambanua Waislamu na mataifa mengine. Ufafanuzi huo unahuisha imani juu ya Mungu Mmoja na kutuokoa katika hatari ya mashaka juu ya imani hii. Mtu anapata imani ile ile iliyoshikwa na Masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu. Hadhrat Ahmad alipinga imani hizi za kishirikina kwa hoja zenye nguvu. Aliuthibitisha tena Umoja wa Mwenyezi Mungu. Mungu ni Mmoja tu. Kumwomba mtu ye yote aliyekufa, kuchinja dhabihu juu ya makaburi ya wafu, kukiabudu cho chote kilicho hai au kilichokufa, kutoa sifa za kiungu hata kwa manabii wa Mungu, kuchinja wanyama kwa majina ya wengine ghairi ya Mwenyezi Mungu, kutoa chochote kile ili kupata radhi ya huyu,-kufikiri kwamba mtu ye yote,awe mtakatifu namna gani, anaweza kumshawishi Mwenyezi Mungu kutoa kitu chochote, imani hizi au kuelekea kwazo,ni kupotoa fundisho la kweli la Uislam juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akathibitisha kwamba Yesu Kristo alikufa kifo cha kawaida kama manabii wengine na alizikwa hapa hapa ardhini. Alihuisha wafu wa kiroho na siyo wa kimwili. Aliumba kama awezavyo kuumba mwanadamu yeyote. Lakini kuhuisha wafu wa kimwili haikuwa kazi yake. Hakuweza kuumba uhai katika umauti, bila ya idhini au kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ni mwivu kwa sifa Zake. Hashirikiani na yeyote katika hizo. Fundisho la Quran Tukufu linapinga fikara hii . Nguvu za Kiungu ni kwa Mwenyezi Mungu. Haziwezi kushirikishwa na Yesu Kristo au mwanadamu yeyote.

Hadhrat Ahmad akaeleza tena fundisho la Uislam linalokubaliana na akili ya mwanadamu. Akaondoa giza la itikadi za kipagani zilizowaingia Waislamu na kuonesha tena njia ya kweli iliyokuwa imesahauliwa. Kwa hakika , alifanya yale ambayo Masihi wa bishara alitakiwa afanye.

## MAONI MAGENI JUU YA MALAIKA

Imani juu ya Malaika ni nguzo ya pili baada ya imani juu ya Mwenyezi Mungu. Imani hii pia imepotelewa katika njia mbalimbali. Wengine wanaamini kuwa Malaika waliweza kufanya dhambi. Waliweza kumlaumu Mwenyezi Mungu. Juu ya Adamu , Malaika wanasemwa walimpinga Mwenyezi Mungu,waliweza kuhoji juu ya kuumba kwa Mungu. Inasahauliwa ya kuwa habari za Adam, zilivyoelezwa katika Quran Tukufu zinaweka sifa kubwa za Mwenyezi Mungu vinywani mwa Malaika:

"Sisi twakutukuza kwa sifa Zako na kukutaja utakatifu Wako?" (2:31)

Malaika wanathibitisha kwamba wao wanamsifu Mwenyezi Mungu wala hawampingi kwa jambo lolote. Hadithi ya Harut na Marut, uzushi kamili, umeingia katika elimu ya dini ya Waislamu. Inasemwa ya kuwa Mwenyezi Mungu aliwatuma Malaika wawili

waliomithilika kibinadamu. Wakaingiwa na mapenzi na mwanamke mmoja. Wakaadhibiwa kwa kutundikwa kisimani, vichwa chini (Mungu apishe mbali). Kadhalika inasemwa ya kuwa Iblis au Shetani (Mungu apishe mbali) alikuwa mwalimu wa Malaika. Itikadi nyingine ya jamaa hawa juu ya Malaika ni kwama Malaika ni viumbe vya kimwili wanaoshughulika na kazi ndogo, wakikimbia kimbia huko na kule kwa amri mbalimbali. Malaika Izraili hukimbia huko na huko. Alivyo ni Malaika wa mauti, humbidi sasa achukue maisha ya huyu na mara ya yule.

Kinyume na mawazo haya ya kijinga, tunao ukanaji hasa juu ya kuwako kwa Malaika. Kwa maoni ya wengine, Malaika ni majina ya viumbe vya kubuni tu. Fundisho la Quran Tukufu juu ya Malaika kwao linafasiriwa kwa namna ya umbile. Malaika inasemwa, ni majina ya nguvu mbali mbali za kimwili. Baadhi yao wanakataa moja kwa moja fundisho la Quran Tukufu na Hadithi. Hawafikiri kuwa ufunuo wa Quran ulileetwa na Jibrili. Wanatoa hoja zingine vile vile juu ya fundisho la Quran Tukufu juu ya Malaika. Kuamini Malaika, wanasema ni aibu kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akasahihisha makosa haya, akafundisha fundisho hasa la Islam juu ya Malaika, na akaondoa mashaka yote na upinzani ulioletwa na baadhi ya Waislamu juu ya madhumuni hii. Alithibitisha kwamba Malaika hawafanyi dhambi wala kuasi amri na mipango ya Mungu. Tunalo fundisho dhahiri la Mwenyezi Mungu ndani ya Quran.

> "Hawamwasi Mwenyezi Mungu Aliyowaamuru, na hutenda wanayoamriwshwa" (66:7).

Malaika ni namna maalumu ya viumbe. Wamewekwa kufanya mambo fulani fulani katika njia maalumu.Tabia yao ni utii kamili, bila ya hiari ya kufanya wapendavyo. Je, viumbe wa namna hii wanaweza kuasi?

Tabia yao ya asili waliyopewa na Mwenyezi Mungu inapinga fikara hii. Kufanya mapenzi nawanawake haiwezekani kwao. Hawawezi kumsahau Mungu na kujitoma katika adhabu ya Mungu.

Kama Malaika wanaweza kufanya dhambi kwa nini tumetakiwa kuwaamini? Imani zinafundishwa pale utii unapooneshwa. Mwenyezi Mungu hawezi kutuamuru kutii viumbe vyenye kuweza kufanya dhambi na kuasi. Si sawa na akili kutii viumbe vyenye kuasi.

Kadhalika Hadhrat Ahmad akafundisha kuwa Malaika ni viumbe vya kiroho. Hawana haja ya kutoka sehemu fulani mpaka nyingine. Uwezo wao na kazi zao zinafanyika toka pale pale walipo. Wako kama jua linaloangaza nuru yake na kutoa joto lake toka pale pale lilipo,nawao kama hivyo wanapeleka amri za Mwenyezi Mungu. Katika kufanya kazi wanazoamriwa wanatumia nguvu zile walizojaaliwa. Wanafanya yale wanayoambiwa.

Vile vile Hadhrat Ahmad (A.S) alikanusha fikara kwamba Shetani alikuwa mmoja wa Malaika au kiongozi mwao. Kwa mujibu wa Islam, Shetani alikuwa ni roho mbaya. Mwenyezi Mungu anasema juu yake;

Na alikuwa miongoni mwa makafiri" (2:35), yaani kafiri kwa hali yake ya asili. Moyo wake ulimkana Mwenyezi Mungu.

Kadhalika akasahihisha itikadi iliyowaingia baadhi ya Waislamu wa siku hizi kwamba Malaika ni majina tu ya viumbe vya kubuni au nguvu fulani za kidunia. Akatoa istishhada yake mwenyewe juu ya itikadi ya Malaika. Alikazana sana kupinga wale wanaosema kuwa kuamini Malaika ni idhilali kwa Uwezo wa Mungu. Mwenyezi Mungu ametupa masikio. Lakini pia ameumba hewa ili tuweze kusikia. Kuamini anga na hewa siyo idhilali kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu. Itakuwaje kaumini Malaika kuwe idhilali kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu. Inaonekana Mwenyezi Mungu anafanya kazi kwa njia fulani fulani; hizi ni sehamu ya hekima yake. Anazitumia katika uumbaji wake wa kiroho. Kwa njia hizo analeta mabadiliko ya kidunia na ya kiroho pia. Hadhrat Ahmad a.s. akathibitisha kwamba njia na sababu hazileti upungufu katika uwezo wa Mwenyezi Mungu. Zinatolewa njia ili kwamba mwanadamu ambaye ana upeo maalumu wa fahamu aweze kupata maendeleo hatua baada ya hatua. Malaika wakiwa viumbe vya kiroho wamekusudiwa kusaidia fahamu za mwanadamu. Kwa njia hii, Hadhrat Ahmad a.s. alieleza maana ya kweli ya imani juu ya Malaika.

# MAONI YA KOSA JUU YA QURAN

Nguzo ya tatu ya Islam ni kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu. Imani hii pia imebadilika kiajabu. Waislamu wameingiza fikara ngeni juu ya vitabu vya Mwenyezi Mungu, hasa juu ya Quran Tukufu . Hatuna haja sana na vitabu vingine. Tunahusika zaidi na Quran Tukufu. Kwetu sisi, kuamini vitabu vingine ni kwa pili. Vitabu vingine haviko katika sura ile ya asili. Wala hatuna lazima ya kutenda sawa na mafundisho yake yaliyopotolewa.

Mawazo ambayo Waislamu wameyashika juu ya Quran Tukufu ni ya ajabu kwelikweli. Kwangu mimi yanaonekana ya ajabu zaidi kwa sababu nimejifunza ukweli wa Kitabu hiki Kitukufu kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Kwa kweli, kama si yeye, ningekubali uzushi fulani juu ya Quran Tukufu. Jambo la ajabu zaidi lilifundishwa na kuaminiwa juu ya Quran ni kwamba eti maneno ya Kitabu hiki Kitukufu yalitoweka baada ya kufariki Mtume s.a.w. Kama siyo yote, basi yalitoweka mengi sana. Kwa maoni ya baadhi ya Maulamaa wa Kiislamu, hata maandishi haya yaliyoko ya Quran yana ushahidi wa kuingiliwa na watu. Wengine wanakadhibisha wazo hili. Hata wanawaita Makafiri. Lakini wanafundisha mambo mengine juu ya kuwa baadhi ya aya za QURANTukufu zimekua mansukh. Msingi wa kutanguka huko ni kutopatana baina ya sehumu moja na nyingine. Kama aya au sehemu fulani inaonekana inapingana na nyingine, ni lazima ifikiriwe kuwa imetanguka. Kwa kusukumwa na mawazo haya, Waislamu wengine wakiashiria kwenye "kutopatana" kwingine katika Quran Tukufu, wameanza kutoa maelezo ya kutopatana juu ya sehemu zingine za Quran. Aya zinazosemwa zimebatilika ni nyingi mno.Kwa kufuata inavyokubaliwa, sehemu kubwa ya Quran imebatilika, na Waislamu hawana tena lazima ya kufuata sehemu hiyo. (Mungu atulinde na mawazo haya mabaya).

Matokeo ya kutanguka aya za Quran yameendelea mbali sana. Kwa maoni ya jamaa wengine siyo tu kwamba baadhi ya sehemu za Quran zimetanguliwa; bali itikadi na tumaini walilokuwa nalo Waislamu wa kwanza juu ya kila aya ya Quran Tukufu imepotea sana. Waislamu wenye kufikiri wanasumbuliwa sana na hali hii.

Aya zingine zibatilike, na zingine zisibatilike, lakini hakuna uhakika ni zipi zilizobatilika na hazikubatilika. Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawakutuambia jambo hili. Waislamu wanawezaje kukitegemea kitabu hicho? Waislamu wanaweza kukifanya kitabu chao kitukufu kama wapendavyo. Aya wasizozipendelea, wanaweza kuziachilia mbali kuwa zimetanguka. Zile wanazozipendelea wanaweza kuzikubali kuwa hazikutanguka.

Wazo la kosa juu ya vitabu vya Mwenyezi Mungu , na hasa Quran Tukufu, ni kwamba hakuna kitabu chochote kisichokuwa na mvuto mbaya wa Shetani. Inasemwa ya kuwa Shetani huchanganya meneno yake na maneno ya Mungu zama yanapofunuliwa kwa wanadamu. Ili kusaidia itikadi hii ya kigeni aya ya Quran Tukufu inatajwa. Aya 53 ya Sura ya 22 ndiyo inafikiriwa kuwa inasaidia:

"Na Hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii ila alipotamani, Shetani alitia (fitina) katika tamanio lake."

Neno la maana linaloshikwa katika Aya hii ni Ummiyyah. Katika maneno ya mwanzo ya aya hii tafsiri ya neno hili ni nia badala ya ujumbe. Lugha ya Kiarabu inaruhusu maana zote mbili, lakini mufasirina wa Kiislamu walipendelea maana ya kosa. Umniyyah likifasiriwa kama nia linafanya aya iwe na maana kamili. Hivyo aya itakuwa na maana kwamba kila mara Manabii wanapotaka kufikisha nia yao, Shetani hutia vizuizi njiani. Mufasirina wa Kiislamu hawakuishia hapo tu. Wametaja na mifano ya aya za Quran zilizopokelewa na Mtume s.a.w. ambazo ati Shetani alichanganya maneno yake mwenyewe. Inasemwa kuwa Mtume s.a.w. alikuwa akisoma aya za Sura Najm. Alipofika maneno, "Je, umewaona Lat na Uzza, na Manat, mwingine wa tatu?" (53:20-22), Shetani alichanganya hayo na maneno yake mwenyewe: "miungu hii yenye mashingo marefu ya sanaa inaweza kuwa waombezi!" Maneno, haya, inasemwa, yaliyokuja kutoka kwa Shetani, vilevile yalisemwa na Mtume s.a.w. kama sehemu ya Quran. Miongoni mwa waliokuwapo

walikuwa baadhi ya makafiri. Waliposikia sifa hii isiyotazamiwa ya miungu yao, wakasujudu. Mtume s.a.w. alishangaa. Baadaye akatambua maneno ya kuisifu miungu ya kipagani yaliingizwa na Shetani. (Mungu apishe mbali). Hapo Mtume s.a.w. akasumbuliwa sana na tukio hili.

Yote haya ni uzushi mtupu lakini Waislamu waliwezaje kwa urahisi kukubali wazo hili?

Mufasirina wengine wameleta jambo jingine. Kwa kuona kuwa tafsiri yake ya kawaida haileti maana, wamefikiri kwamba maneno yanayosemwa ni ya Shetani hayakutiwa na Shetani alipokuwa anayatamka Mtume s.a.w. bali yaliongezwa naye kwa sauti yake mwenyewe iliyofanana na ya Mtume s.a.w. Waliokuwapo walidhani maneno yale yalitoka kinywani mwa Mtume s.a.w. Jambo hili nalo ni la kipumbavu kama la kwanza. Kwa mawazo yote mawili, Quran Tukufu haiwezi tena kutegemewa kuwa ufunuo halisi wa Mwenyezi Mungu kama inavyoaminiwa na Waislamu. Kama Shetani anao uwezo wa kuchanganya maneno yake na maneno ya ufunuo, hakuna ufunuo wowote wa unabii unaoweza kufikiriwa kuwa ufunuo halisi wa Mwenyezi Mungu. Kwa hali yoyote, mufasirina wa Quran wameashiria kwenye aya ifuatayo kuwa ndiyo tatuzi la tatizo hili. Ni aya isemayo:

> "Lakini Mwenyezi Mungu Huondoa anayoyatia Shetani, kisha Mwenyezi Mungu Huziimarisha ishara Zake; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima" (22:53).

Hii sio tatuzi la tatizo hili. Inapokubaliwa tu ya kwamba Shetani anaweza kuchanganya maneno yake na ya Mwenyezi Mungu, hatuwezi kusema maneno fulani hayana mchanganyiko huo au yanao. Kama isemwe ya kwamba aya inayoahidi kutakasa mchanganyiko wa Shetani, yenyewe ni maneno ya Shetani, basi jibu lake litakuwa nini? Mashaka makubwa yatapatikana juu ya Quran! Hivyo basi ni lazima tudhamini kuwa Quran ni ufunuo halisi wa Mwenyezi Mungu.

# UAMUZI WA QURAN NA HADITHI

Wengi wamepunguza hukumu ya Quran na kuelekea Hadithi dhaifu na hata Hadithi za uzushi zimeinuliwa kwenye hatua ya juu kuliko Quran Tukufu. Kwa jina la Mtume s.a.w. maneno ya Mungu yamedharaulika na hao Masheikh wapungufu wa akili. Quran inaweza kukana kitu waziwazi. Lakini kama Hadithi dhaifu inaweza kupatikana inayoeleza mas'ala hayohayo, itawekwa juu kinyume cha Quran. Vilevile Quran inaweza kuthibitisha kitu waziwazi, lakini kama Hadithi dhaifu ipo inayopinga jambo hilo, Hadithi itatangulizwa juu ya Quran.

Waislamu wengine wanafikiri kuwa Quran Tukufu siyo maneno ya Mwenyezi Mungu bali ya Mtume s.a.w. mwenyewe. Naam, wanaeleza Kitabu Kitukufu hiki kama cha kiungu, hata kama Neno la Mungu. Lakini maoni yao ni kwamba mawazo safi yaliyomwingia Mtune s.a.w. yalichangamshwa na kukubaliwa na Mwenyezi Mungu. Na kwa njia hii maneno ya Quran Tukufu yanakuwa maneno ya Mungu. Zaidi wanasema fikara na maoni yalikuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini maneno yake yalitoka kwa Mtume s.a.w. Mwenyezi Mungu haleti maneno. Kuleta maneno kunakuwa kuwe na kitu cha sauti (kama midomo na ulimi) ambacho hakidhaniwi kwa Mwenyezi Mungu! Kwa hiyo mawazo yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, maneno kwa Mtume s.a.w.!

Waislamu wengine wanafikiri kuwa Quran haiwezi kutafsiriwa. Lakini Waislamu wa kawaida waliweza kuielewa tafsiri. Hivyo uharamu huu wa kutafsiriwa Quran umewazuia Waislamu wengi wasiielewe Quran Tukufu. Ni nini matokeo yake kama sio ujinga na kurudia mila za zamani.

Wengine wanafikiri kuwa Quran ni kitabu chenye misingi mikubwa ya falsafa. Ni kweli mambo fulani yameelezwa humo lakini hakuna mas'ala inayothibitika ndani yake.

Wengine wanafikiri kuwa maneno ya Quran siku zote hayana haja ya kusomwa kwa mpango kama yalivyoandikwa, ati yanaweza kufanywa kama wanachokiita *taqdim* na *ta'khiri* kwa sababu hii mpango wa maneno unaweza kubadilishwa kupatana na maana. Pasi na kuelewa namna ya kufanya ya mbele iwe nyuma na ya nyuma iwe mbele, tutapotea.

Wengine walikusanya hadithi zote za uzushi walizozipata ziwe na maana au la, zichukize au la, hata zinaweza kuwa kinyume na fundisho la Quran Tukufu, lakini zimekubaliwa na mufasirina kama hadithi za Waisraeli. Hadithi kama hizo zinasemwa ni za mawalii na watu watakatifu walioishi zamani sana na zimefikiriwa kuwa maelezo safi ya Quran.

Wengine wanakana kwamba hakuna katika Quran mpango wa maana za maneno kati ya aya na aya nyingine, sura na sura nyingine. Wazi wanasema kuwa maneno ya Quran hayakuungana, ni kama vile maneno ya mtu ambaye amezimia wala hajui kile anachozungumzia. Madhumuni yake kabisa yameachana moja na nyingine, hayako kwa mfuatano. Hakuna mpango hasa.

Maoni yaliyoenea sana kwa jumla miongoni mwa Waislamu ni kwamba Mwenyezi Mungu hazungumzi tena na wanadamu. Sifa ya Mwenyezi Mungu ya Takallum (Kusema) imesimamishwa. Mungu sasa anaona na kusikia lakini hasemi.

Kwa ufupi, fikra mbalimbali za Kiislamu zimebuni maoni mbalimbali juu ya Quran Tukufu. Uzuri, utukufu na mvuto wa Kitabu hiki Kitakatifu umeharibiwa, yote haya kwa jina la kuitumikia! Kwa kweli huu sio utumishi bali dharau. Athari yake imekuwa kuwazuia watu na kuwafanya wasikifuate Kitabu Kitukufu hiki.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akaondoa mawazo yote haya ya kosa. Kwa hoja kali kabisa alithibitisha ya kuwa Quran Tukufu ni Sheria ya mwisho ya Mwenyezi Mungu kwa wanadamu. Hakuna hata sehemu yake moja iliyobatilika. Kila fundisho lake linawezekana kufuatwa na mwanadamu. Hakuna sehemu yake yoyote inayoipinga sehemu nyingine. Hivi kwamba hakuna sehemu yoyote inayohitaji kubatilishwa. Wale wanaotoa makosa yoyote ni wajinga au wachache wa elimu. Wanaleta ukosefu wao wenyewe wa kuelewa katika Quran. Quran, Hadhrat Ahmad alifundisha, haijabatilika hata sehemu kidogo tangu ilipofunuliwa. Kila neno, kila herufi, iko vilevile kama ilivyofunuliwa. Sio tu kwamba Quran haijabatilika sehemu yoyote, bali pia haiwezekani kuibatilisha. Sio herufi zake wala maana yake, haviwezi kupata mabadiliko yoyote. Hakuwezi kuwa na maongezo wala mapunguzi yoyote katika Quran.

Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye Mhifadhi wake. Ametoa njia za kuhifadhi Kitabu hiki Kitukufu kwa kimwili na kwa kiroho pia. Wanadamu hawawezi kubadili chochote katika Quran, sio maneno yake wala mafundisho yake. Hivyo, ni kosa kufikiri kuwa aya ziwazo zote zile za Quran zimekuwa mansukh; au kwamba kumebadilika chochote ndani yake. Quran leo imesalimika kwa kila nama. Kusema ya kuwa sehemu yoyote ya Quran ilitoweka ni kumtusi Mwenyezi Mungu. Ina maana kwamba Mwenyezi Mungu alileta mwongozo kamili kwa wanadamu, lakini kitabu cha mwongozo huo hakikuweza kubakia kikamilifu. Kilishindwa kutimiliza makusudio yake hata kwa siku moja. Kufikiri kuwa Kitabu Kitukufu hiki kinaweza kubatilika ni kukifanya kuwa kitabu kisichotegemewa. Kama Quran inaweza kubatilika, ni lazima kwamba nabi mpya na kitabu kipya atumwe kuwaongoza wanadamu. Ni kinyume na akili kufikiri kuwa wanadamu wanaweza kuishi bila ya mwongozo wa Mungu hata kwa siku moja.

Hadhrat Ahmad alithibitisha pia ya kuwa Quran Tukufu, kwa kweli, kila namna ya ufunuo ni salama na machnganyiko wa Shetani. Haiwezekani kwamba Shetani achanganye maneno yake na maneno ya Mwenyezi Mungu aishinde sauti ya Mtukufu Mtume s.a.w. au akatoe sauti yake kama sauti ya Mtume s.a.w. Seyidna Ahmad a.s. akatoa ushuhuda wake mwenyewe juu ya jambo hili. Mfuasi mnyenyekevu wa Mtukufu Mtume s.a.w., mtumishi tu, hata ufunuo aliopokea wowote ule haukuwa wa kutiliwa shaka. Viweje tena ufunuo uliopokelewa na bwana unaweza kutiliwa shaka? Hivyo, hakuna shaka inayowezekana kwa Quran Tukufu. Quran ni mwongozo kwa nyakati zote. Kufikiri hata kwa dakika moja kuwa ufunuo huu uliweza kuingiliwa na mchanganyiko wa Shetani ni maamngamio.

Hivyo Hadhrat Ahmad a.s. akasisitiza heshima ya Quran. Akaeleza kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuihifadhi Quran ilitimia katika njia za ajabu sana. Hata maadui za Uislamu wamekubali ya kuwa Quran imebakia vilevile kama ilivyofunuliwa. Kujaribu na kuendesha Hadithi za Quran pamoja ni tusi kwa Quran. Hata inamfikisha mtu kwenye kuikana Quran. Kama kuna Hadithi zinazokadhibisha Quran, haziwezi kuwa za kweli. Mtume s.a.w.

hawezi kwenda kinyume na Neno la Mungu. Wala Hadithi mbalimbali hazikukusanywa kwa uangalifu kama ilivyokusanywa Quran. Hivyo Hadithi ziko chini ya Quran. Kama pingamizi lolote lionekane kati ya Hadithi za sehemu yoyote ile ya Quran, hatuna budi tuiache hadithi. Hadithi inayopingana na Quran ni uzushi tu, sio kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w.

Ilijulikana sana ya kwamba maelezo ya mafundisho ya dini yametufikia kwa njia ya Hadithi. Hadhrat Ahmad akafundisha kuwa kuna chanzo kingine cha elimu ya Kiislamu, na chanzo hicho ni Sunna. Sunna ni matendo ya dhahiri ya Mtukufu Mtume s.a.w. Chochote alichofanya Mtume s.a.w. na alichoonwa na Masahaba zakeakikifanya ndiyo Sunna. Mamilioni ya Waislamu waliwaona Waislamu wengine wakifanya mamabo fulani fulani kwa njia fulani fulani na wakajifunza nao kufanya hivyo katika njia hizo. Hivyo, matendo yao yakawa ni mwigo kwa Waislamu wengine. Matendo ya namna hii yaliyokaa sana, yakashikwa na vizazi mbalimbali vya Kiislamu, hayawezi kukadhibisha Quran Tukufu. Hadithi ni matamshi ya Mtume s.a.w. Katika njia ya kusimulia, maneno hayo yanaweza kupotolewa, hivi kwamba yanaweza kukadhibisha Quran. Hivyo, kutegema Hadithi ni budi kuhojiwe. Kama Hadithi inakadhibisha sehemu yoyote ya Quran, haina haja ya kufuatwa. Na kama inapatana nayo, inastahiki kukubaliwa. Hapo inakuwa sehemu ya taarikh, na ushuhuda wa taarikh hauwezi kuachwa bila sababu. Kwani matukio ya maana sana yangepotea kama ushuhuda wa taarikh ungeachiliwa mbali.

Kadhalika, alionesha Hadhrat Ahmad, hatari ya maoni kwamba maneno ya Quran siyo ya kiungu; ya kwamba yanaweza kusemwa ni ya Mtume s.a.w. Alithibitisha ya kuwa maneno, herufi, irabu, na nukta zote za Quran ni za Mwenyezi Mungu. Mtume s.a.w. mwenyewe alikuwa Mjumbe, mfikishaji wa Neno la Mwenyezi Mungu, sio mwenye Neno. Ni kosa kufikiri kuwa kama vile tamko la mwanadamu linavyohitaji ulimi na mdomo na chombo cha kutolea sauti, na kwa vile Mungu hawezi kusemwa anavyo viungo kama hivi, basi ni vigumu ati kufikiri kuwa Mwenyezi Mungu anasema na mwanadamu kama vile mwanadamu anavyosema na mwenzake. Mawazo haya ni ya mbali sana. Mwenyezi Mungu ni wa pekee.

Hakuna kinachofanana naye. Uwezo wa Mungu na sifa zake haziwezi kuonwa na mwanadamu. Kama kusema hakuwezekani bila ulimi na mdomo, basi vilevile haiwezekani kutengeneza kitu bila mikono. Ni ujinga kufikiri kuwa Mungu ana mikono kama ya wanadamu. Je, tukane kwamba Mungu siye Mwumba wetu? Hivyo basi, inaonekana ya kuwa Mungu anaweza kusema na mwanadamu bila kutumia viungo avitumiavyo mwanadamu, kama vile anavyoweza kuumba bila mikono ya kibinadamu. Pia alieleza ushuhuda wake mwenyewe na kusema ya kuwa mgogoro huu umezuka kwa sababu ya ujinga. Wale wasio wageni wa ufunuo wa Mungu, wanajua ufunuo unaweza kuwa wa namna gani. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alisema ya kwamba ufunuo aliopata yeye ulimjia kwa maneno. Ikiwa yeye aliweza kupokea ufunuo wa maneno, kwa nini asipokee Mtukufu Mtume s.a.w., Kiongozi wa wanadamu, Mteule, Mpenzi wa Mwenyezi Mungu? Wale amabao hawajapata namna fulani ya ufunuo hawana haja ya kuchungua asili yake. Ujinga ni mbaya sana, lakini kutoa maoni juu ya mambo tusiyoyajua, ni vibaya zaidi. Ilikuwa upuuzi, alisema Hadhrat Ahmad, kwa wageni wa Mungu kukisia njia za Mungu.

Kadhalika, Hadhrat Ahmad, alikanusha maoni ya kusema kwamba Neno la Mungu haliwezi kutafsirika. Ni kwa namna gani maana ya Quran, uzuri wake na undani wake ungewafikia wale wasiojua Kiarabu? Naam, ni kosa kuandika tafsiri tu peke yake. Kwani kama tafsiri tu ndiyo ipigwe chapa, kidogo kidogo watu watasahau maneno ya ufunuo. Hata ingewezekana kwamba tafsiri za tafsiri zifute kabisa maneno ya asili ya Quran. Hivyo ilikuwa bora zaidi kuchapisha tafsiri na maneno ya asili pamoja. Ilikuwa lazima pia kuzidisha elimu kidogo ya lugha ya Kiarabu. Waislamu wajue Kiarabu ili waweze kusoma Kiarabu cha Quran Tukufu na kupokea manufaa na baraka ambazo hawawezi kuzipata kwa njia nyingine. Vilevile ilikuwa lazima wafahamu, kwa uchache, baadhi ya sehemu za Quran kwa Kiarabu kwa kutumiwa katika Sala tano za kila siku.

Vilevile alieleza kuwa Quran ina mafundisho yaliyo waziwazi kabisa. Imefundisha kila haja inayohitajiwa na mwanadamu kwa ajili ya maendeleo yake ya kiroho. Na kwa haya haina mfano. Lakini

Waislamu wameacha kujifunza maana za Quran; na kwa hivi, wao wanakuwa wanastahili lawama endapo maana fulani ya Quran hawaielewi. Quran Tukufu inatufundisha:

"Hapana atakayeigusa ila waliotakaswa" (56:80).

Ili kuelewa maana za ndani za Quran Tukufu, ni lazima mtu awe safi. Wale wanaoielewa Quran kijuu juu wanaleta maoni na fikara zao ndani ya Quran. Hivyo, Hadhrat Ahmad alionesha ni kwa namna gani wajibu na usuli za dini zinaweza kupatikana ndani ya Quran yenyewe. Alijibu hoja mbalimbali za maadui wa Uislamu na akaonesha kwamba dawa safi na nyepesi zaidi ya tabia, dini, na taabu za kiroho za mwandamu, haziwezi kupatikana. Quran Tukufu imefupisha maneno, lakini chini ya maneno kuna habari ya maana zake. Neno moja linaweza kutoa matawi ya maana za namna mbalimbali. Maneno ya Quran Tukufu ni ya kimwujiza kwa sababu maneno hayohayo yanaweza kukidhi haja mbalimbali za mwanadamu. Haja za wanadamu zinabadilika badilika kwa sababu mbalimbali na nyakati mbalimbali.

Akapinga vilevile fundisho la Taqdim na Ta'khir. Alifundisha ya kuwa maneno ya Quran Tukufu yamepangwa sawa. Mwahala yalimopangwa hayawezi kubadilishwa ila yataharibu maana. Ni wajinga tu ndio wanaofikiri kuwa maneno ya Quran yanweza kupanguliwa. Maneno ya Quran lazima yasomwe vile yalivyopangwa. Mahala pa kila neno ni pa lazima kwa maana yake. Uzuri wa mkusanyiko wa maana unategemea vile maneno yalivyopangwa katika Quran. Kwa mifano mbalimbali, alionesha kwamba mpango wa maneno ni sehemu ya maandiko ya Quran. Ujinga na kutojua undani kunawapotosha watu vibaya sana juu ya suala hili.

## HADITHI ZA MAYAHUDI

Alipinga pia, Hadhrat Ahmad a.s. kwamba hadithi za Mayahudi zimejaa tele ndani ya Quran tukufu. Kufanana kidogo kwa

mafundisho ya Quran Tukufu na yale ya vitabu vya Mayahudi hakuoneshi ya kuwa ni kitu kimoja. Zama fundisho la Quran ni tofauti, ni kwa sababu Quran haikubali tafsiri ya Kiyahudi. Quran sio kitabu cha visa au hadithi. Hakina haja katika masimulizi juu ya matukio ya zamani ila kwa ajili ya ubora wake wa kiroho au kama ni bishara za matukio ya baadaye. Marudio ya taarikh za zamani ni onyo kwamba matukio ya namna ileile yatatokea katika wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. au katika taarikh ya baadaye ya Waislamu. Ikiwa habari zinazotolewa na Quran juu ya matukio ya amani, zifasiriwe kwa namna ambayo zifanywe kuwa sawa na fasiri za madoido za matukio hayo hayo zilizomo ndani ya vitabu vya Mayahudi, tutakuwa tunaangamiza tu maana iliyotaka kufikishwa na Quran Tukufu. Quran ni shahidi juu ya vitabu vya zamani. Vitabu vya zamani si shahidi juu ya Quran Tukufu. Ili kuelewa maana ya Quran hatuna haja ya kuchukua ushuhuda katika vitabu vya zamani. Kwa kuelewa maana yake inatulazimu tushuhudiwe na Quran yenyewe. Maana ya Quran imo ndani ya Quran. Hakuna haja ya msaada wa nje.

Kadhalika, Hadhrat Ahmad alionesha kuwa Quran ni kamili katika taratibu yake - mpango baina ya sura moja na sura nyingine, aya moja na aya nyingine na baina ya neno moja na neno jingine - ilivyo kama katika fikara yake na lugha. Viini vya Quran Tukufu vimeungana. Havipishani bali vinajitokeza vyenyewe kwa lazima kimoja baada ya kingine. Mpango kamili kabisa umepangwa. Tokeo neno la mwanzo la sura ya kwanza mpaka neno la mwisho la sura ya mwisho mpango wa akili sana umepangwa. Quran inayo kazi iliyokamilika ndani yake. Sura zake, aya na maneno yake, yanafuata mpango mkamilifu. Wale wanaojua kazi hii wanajwa na furaha ya ajabu. Wanapolinganisha uzuri wa mpango wa Quran na uzuri wa mpango uliomo ndani ya vitabu vya wanadamu, wanaona dunia nyingine kabisa. Wale wasio na elimu ya ndani ya Quran, wanadhania kwamba Quran imejaa habari zisizopatana au masimulizi yasiyo na maana. Wazo hili ni matokeo ya ujinga, nao wameutegemea na kuuonea fahari ujinga huo. Hadhrat Ahmad akaonesha kwa mifano mbalimbali jinsi Quran Tukufu ilivyo na mpango mkamilifu na akawashangaza watu wa dunia nzima.

Hadhrat Ahmad a.s. alipinga vilevile usemi kwamba Mwenyezi Mungu hasemi sasa na wanadamu. Akaeleza ushuhuda wake na mazoea wake mwenyewe na akasema ya kuwa sifa za Mwenyezi Mungu hazina kikomo. Ikiwa Mungu bado anasikia na kuona kama alivyokuwa zamani, ni lazima pia aseme. Na Mungu hafikishi tu sheria na amri. Anafikisha pia yakini na ushuhuda. Yakini ya furaha yake mathalan. Kama ushuhuda wa namna hii ukome, hatutakuwa na njia ya kuona kama Mwenyezi Mungu anapendezwa nasi au la. Hivyo, ni lazima Mwenyezi Mungu aendelee kusema. Ambapo wamo wanadamu ulimwenguni na ambapo wako wale wanaojitahidi kwa shauku na mahaba kwa ajili ya kuipata radhi yake na wanafuata mafundisho ya Islam, ni lazima aendelee kuwapa yakini kwa maneno Yake. Kwa namna hii Hadhrat Ahmad a.s. aliondoa mawazo mengi ya kosa yaliyoenea vitabuni juu ya ufunuo. Mawazo haya ya kosa yakikusanywa pamoja yanaleta mashaka makubwa juu ya manufaa ya vitabu vya Mungu, pamoja na Quran. Hadhrat Ahmad kajenga tena sehemu hii ya imani ya Kiislamu kwa misingi madhubuti. Alibainisha asili hasa ya ufunuo na utukufu wake na kuwashawishi waamini na kutambua tena. Aliondoa makosa yaliyoenea miongoni mwa Waislamu na wengine juu ya ufunuo. Waislamu na wasio Waislamu wakaona nuru yenye kung'aa ya Quran Tukufu. Hawakuweza kuinua macho yao kuikodolea.

## MAONI YA KOSA JUU YA MANABII

Nguzo ya nne ya Islam ni kuamini manabii. Imani hii pia imeoza. Kwa kukosa fikara na elimu ya kiroho, Waislamu wamechafua imani yao juu ya manabii katika njia za ajabu nyingi. Sio tu kwamba imani imebadilika, bali imekuwa haina mvuto kwa Waislamu na kwa wengine inachukiza. Mashambulio mabaya yaliyofanywa dhidi ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni matokeo ya fikara za kijinga zilizoshikwa na Waislamu wa leo juu ya manabii kwa ujumla na hususa kwa Mtume s.a.w. Wakristo na washutumi wengine wa Uislamu wanashika zaidi hadithi za uongo zilizomo ndani ya vitabu vya Waislamu kuliko ushuhuda walioubuni wenyewe. Hadithi hizi za

uongo wanazisimulia katika mazungumzo yao ya kila siku na katika hotuba zao juu ya mimbari. Ni sikitiko kwa hawa Waislamu. Maadui wa Islam wanaonekana wakishambulia tabia za Mtukufu Mtume s.a.w. kwa silaha zilizotungwa kwa ujinga wa Waislamu wenyewe. Mashambulizi haya yanadhihirisha unafiki wa wale waliozitunga hadithi hizo na kuzieneza kati ya Waisalmu. Lakini pia wanawapa nafasi wasio Waislamu kushambulia tabia ya Mtume s.a.w.

Manabii hutumwa ili kukuza wema na utakatifu miongoni mwa wanadamu na kuwaongoza tena kwenye makusudio yaliyoachwa na kusahauliwa. Waislamu zama za maanguko yao walianza kuwasifu Manabii wa Mwenyezi Mungu kwa sifa za uchafu ambazo mtu anaweza kusita kuwadhania hata watu wa kawaida. Hakuna hata nabii mmoja aliyeepukana na lawama zao. Masimulizi yake yanasikitisha mno. Tokea Adam mpaka Mtume s.a.w. wote wamesemwa walipata kuasi amri za Mungu. Adama anasemwa alivunja amri iliyo wazi ya Mungu. Nuhu anasemwa alimwombea mwanawe kwa Mwenyezi Mungu ambapo alikatazwa kufanya hivyo. Ibrahimu anasemwa alipata kusema uongo mara tatu. Yakubu anasemwa alimdanganya baba yake aliyekuwa kufani na akapata baraka zake kwa kujifanya kama kaka ayake mkubwa. Yusufu anasemwa alitaka kuzini na mke wa mfalme wa Misri. Inasemwa ya kuwa Yusuf hakuweza kujizuia na dhambi hiyo. Halafu akaona mfano wa baba yake Yakubu, akaona haya na akajizuia. Inasemwa pia ya kuwa alipokuwa mtoto alipata kuiba, na ya kwamba alipata kufanya hila ili akae na nduguye. Musa anasemwa alimwua mtu mmoja bila sababu na kwa hivi akawa amefanya dhambi kubwa. Inasemwa tena kwamba Musa alichukua mali ya watu pasina idhini yao. Daudi anasemwa alimwulisha mtu kwa kutaka kuwa na mke wa mtu huyo. Akalaumiwa na Mungu kwa kumwoa mjane wa aliyemwua. Suleimani anasemwa aliingiwa na mapenzi na mwanamke mmoja wa kipagani; vilevile alitekwa na Shetani na hivyo Shetani akaanza kutawala mahala pake. Kwa kuathiriwa na mapenzi ya mali, alisahau wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kukagua farasi, alisahau wakati wa Sala na hakukubmuka mpaka baada ya jua kutua.

Kwa hali yoyote, mashutumu mabaya zaidi yanasemwa juu ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hili ni chukizo kubwa mno. Sisi wanadamu tunawiwa sana na Mtume s.a.w. hivi kwamba kumshukuru, tunalazimika kuinamisha vichwa vyetu mbele yake. Ni ukatili kwamba yule ambaye anatuwia sana amepata mashutumu mabaya sana kupita kiasi. Hakuna hatua ya maisha yake ambayo haikuguswa. Inasemwa, mathalan, ya kwamba alitaka Ali awe Khalifa wake, lakini hakumteua kwa sababu aliwaogopa watu. Kadhalika inasemwa (Mungu apishe mbali) ya kwamba alipumbazwa na pendo la Zainab, binamu yake. Inasemwa ya kuwa hatimaye Mwenyezi Mungu alimruhusu amwoe Zainab baada ya kuwa kuachika Zainab kwa Zaid kulikuwa kwa amri ya Mungu. inasemwa pia ya kuwa alikuwa na uhusiano wa siri na msichana mtumwa aliyekuwa akimwangalia mmoja wa wake zake. Mkewe aliwafumania na hapo Mtume s.a.w. akajuta sana na kuahidi kwa kiapo kuwa hatafanya vile tena. Pia alimwambia mke huyu aahidi kwamba hatafichua siri hii kwa mtu yeyote. Kadhalika inasemwa ya kwamba alipenda mafundisho ya Islam yarahisishwe kwa ajili ya wapagani wa Kiarabu wapate kuyaamini. Fikara zao na mawazo yao yaangaliwe.

Fikara hizi za Waislamu wa siku hizi zimeenea sana juu ya Manabii. Kwa maoni yao haya Manabii walikuwa si zaidi kuliko wasuluhishi tu wa mataifa yao. Waliwapenda watu wao na wakataka kuwainua katika hali ya tabia yao na siasa. Bali waliona kwamba fundisho lolote la tabia au la siasa haliwezi kufanikiwa mpaka liunganishwe na imani juu ya Akhera, Kiyama, Pepo na Jahannam n.k. Fundisho la mafumbo haya ni la lazima siyo kwa sababu ni ya kweli, bali kwa sababu bila ya hayo - hakuna watu ambao wangefuata mipaka ile ya ustaarabu. Madai ya kupata ufunuo hayakuwa ya kweli. Hakuna nabii yeyote aliyepata elimu yoyote ya ufunuo na mwongozo. Walidai hivyo tu kwa kutaka kuwavuta watu. Maazimio yao yalikuwa safi kabisa. Itikadi hizi haziwezi kuwa sehemu ya Islam, lakini zimeshikwa na Waislamu siku hizi.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alikanusha mawazo haya yote kati ya mawazo mengine ya kosa aliyoyapinga. Alieleza fundisho hasa la Islam juu ya mambo haya kwa faida ya Waislamu na wasio Waislamu. Alifundisha, mathalan, ya kwamba makusudio

ya kwanza kabisa ya kufika Manabii ni kukuza maisha ya utawa. Huja na kufanya kazi kama mifano kwa ajili ya wengine. Ikiwa hii sio moja wapo ya kazi zao za maana, basi hujia nini? Ikiwa kinachotakiwa ni mafundisho, kitabu cha itikadi na sheria, kwa nini tusiwe na vitabu tu kutoka kwa Mungu? Bali tumekuwa na manabii na vitabu pia; jambo ambalo kwalo inaonekana kwamba makusudio makubwa ya kufika kwa manabii ni kwamba matendo yao yaigwe, na ya kwamba watu wajaribu kudumisha yanayofundishwa na ufunuo, na ili wajue ufunuo hasa una maana gani na wachangamke na kutiwa moyo kwa kuona mifano ya wanadamu juu ya wema na utawa, na washinde udhaifu wao kwa kuimarika na nguvu zenye kutakasa za Manabii hao.

Hadhrat Ahmad alifundisha ya kwamba makosa mengi yaliyoenea miongoni mwa Waislamu yalikuwa kwa sababu ya kutoelewana. Uangalifu uliohitajika katika kuelewa Neno la Mwenyezi Mungu haukushikwa, hukumu zimekuwa zikikatwa kwa uzembe kabisa tokea kizazi mpaka kizazi. Manabii wa Mungu ni safi, hawana dhambi, na ni mifano ya ukweli, upendo na utii. Katika tabia yao imo taswira ya sifa tukufu za Mwenyezi Mungu. Maisha yao matakatifu na ya kupendeza yanaashiria kwenye utakatifu wa Mwenyezi Mungu. Wanakuwa kama kioo kwa ajili ya wengine waone mfano wao wenyewe katika wao. Kwahiyo, watu wabaya mara kwa mara huona asili ya uovu katika manabii. Wanayowadhania manabii kwa hakika ni mambo ya watu waovu. Adam hakuwa mwasi wala Nuhu hakuwa mfanya dhambi. Ibrahimu hakupata kusema uongo wala Yakubu hakupata kudanganya. Yusufu hakufikiri kufanya tendo lolote baya wala hakuiba wala kufanya hila mbaya. Musa hakumwua yeyote bila haki. Daudi hakumchukua mke wa yeyote. Sueliman hakusahau wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya mwanamke wa kipagani au kwa sababu ya farasi zake. Wala Mtume s.a.w. hakufanya dhambi yoyote, kubwa wala ndogo. Alikuwa mtakatifu, hakuweza kuasi kabisa. Yeyote anayetoa dosari katika maisha ya Mtume s.a.w. anatoa dosari zake mwenyewe. Hadithi zinazoelezwa juu yake ni uzushi tu wa wanafiki. Haziwezi kuthibitishwa na taarikh au habari za maisha. Hazipatani kabisa na maisha yake yote, fikara na nia yake. Masingizio juu yake

au manabii wengine ni masalia ya uongo wa makusudi uliotungwa na wanafiki walioishi miongoni mwa waminio. Au ni matokeo ya kutoelwa Quran Tukufu.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alithibitisha toka ndani ya Quran kuwa fikara zote hizi ni za kikafiri. Zimeingia katika maandishi ya Waislamu kutokana na mvuto wa Wakristo. Katika vitabu vya Wakristo imekuwa ni makusudio kueleza makosa ya manabii kwa ujumla. Walifanya hivi ili wathibitishe uungu wa Yesu. Mpaka Yesu amekuwa hana dhambi kabisa na manabii wengine wawe na madhambi kwa kadiri fulani fulani, Yesu asingeweza kuthibitishwa kuwa mwana wa Mungu. Hii inaonekana kuwa sababu kwa nini hata miongoni mwa Waislamu, mashutumu yametolewa juu ya manabii hata juu ya Mtukufu Mtume s.a.w., lakini Yesu hana dhambi kabisa. Sio Yesu tu bali na Mariamu pia, mama yake, anafikiriwa kuwa mfano mwema wa utakatifu. Tofauti hii baina ya dhana juu ya Yesu na manabii wengine, inaonesha kwamba hadithi hizi za uongo na masingizio zimepata njia kuingia kwa Waislamu toka kwa Wakristo. Jinsi mvuto mbaya huu wa Wakristo ulivyoingia katika Islam ni suala jingine. Inawezekana kuwa Waislamu walivutika, bila kujua, kwa sababu ya mchanganyiko wao wa kila siku na Wakristo. Pia inawezekana kwamba baadhi ya Wakristo wabaya walikubali Uislamu kinje nje na halafu wakaeneza hadithi hizi za uongo za Wakristo miongoni mwa Waislamu. Hapo mwanzoni waandishi wa taarikh wa Kiislamu na wakusanyaji wa Hadithi walichanganya uzushi huu na Hadithi zingine miongoni mwa Waislamu. Uaminifu wao juu ya uchunguzi wa taarikh haukutaka kitu kingine zaidi. Upambanuzi baina ya hadithi za kweli na za uongo ulishikwa kwa muda. Halafu masafa kutoka katika mfano na mvuto wa Mtume s.a.w. yakaongezeka. Waandishi waliokuja baadaye hawakuweza kupambanua ukweli katika uongo. Walikubali hadithi zilizo kinyume na daraja ya Islam, lakini walikataa Hadithi zinazoashiria ukweli wa manabii. Laiti Hadithi hizi zingebakia katika maandiko haya, zingetatua migogoro na mashaka yote.

Lakini, Alhamdu lillah, Hadharat Mirza Ghulam Ahmad alitenga mbali dhahabu kutoka kwenye takataka. heshima ya kweli ya manabii ikathibitishwa na kuimarishwa tena, hususa heshima ya

Mtukufu Mtume s.a.w., Mtume wa Islam. Utakatifu wa maisha na tabia aliokuwa nao Mtume s.a.w. sio tu ulithibitishwa, bali ulianishwa kwa hoja zisizokwepeka. Maadui wakubwa wakafumba midomo yao.

Juu ya utakatifu wa Mitume Seyidna Ahmad a.s. alisema katika ushairi wake wa Kiajemi:-

Kila Mtume alikuwa jua la ukweli;
kila Mtume alikuwa jua ling'aalo.
Kila Mtume alikuwa kivuli kilindacho dini;
kila Mtume alikuwa bustani lenye matunda.
Katika dunia kama kundi hili takatifu lisingefika;
kazi ya dini ingebaki pungufu kabisa.
Yeyote asiye na shukurani juu ya ufikaji wao;
yeye kwa hakika ni mkanaji wa neema za Mungu
Hao Mitume ni kama malulu waliotoka nyumba moja;
katika dhati na asili na johari ni kitu kimoja.
Wa kwanza wao Adamu, na wa mwisho Ahmad;
mwenye bahati ni yule amtambuaye wa mwisho.
Mitume ni majohari yenye kumetameta;
lakini Ahmad amewapita wote katika uzuri.
Kila mmoja wao alikuwa chimbuko la maarifa;
kila mmoja alipasha habari ya njia ya Mola.
Yeyote aliye na elimu ya umoja wa Mungu;
mzizi wa elimu yake ni Mtume fulani.
Amefikia ujuzi huu kwa mafundisho yake;
ingawa sasa anakataa kwa sababu ya kiburi.
Ni watu wapotofu na wenye maoni machafu;
ambao wanakataa kutii watakatifu hao.
Tazama bahati mbaya ya watu hao;
wanajivunia macho na wanalichukia jua.
Jicho lisingekuwa na haja ya jua;
bundi wangelikuwa ndio wenye kutazama mbali sana.
Mwanzoni Mungu alipowagawia watu heri na shari;
Mitume walipata ukweli na wengine uongo.
Ukweli juu yao ndio huu; watu wengine

wasiofuata Mitume ni waongo na wenye hila mbaya.
Almasi ing'aayo iwapo unaisema haina nuru;
usemi wako unapunguza nini katika nuru yake?
Lawama juu ya watakatifu haiwi juu yao hasa;
unajithibitishia mwenyewe kwamba umwovu.

## HAWANA IMANI JUU YA AKHERA

Nguzo ya tano ya Kiislamu ni kuamini Siku ya Kiyama, Pepo na Jahannam. Imani hii pia imetoweka. Kwa haika imetoweka kabisa mioyoni. Kwani kama ingekuwako hasa, Waislamu wasingetupilia mbali mafundisho ya Islam namna walivyofanya leo. Mawazo ya Waislamu na mijengo yao juu ya suala hili la maisha ya Akhera, Pepo na Jahannam, yanaonekana na uhusiano kidogo tu na lile fundisho la kweli la Islam. Ni gani lilikuwa wazo la Waislamu juu ya Jannah? Mahala pa starehe na anasa zisizopungua. Ikiwa hii ndiyo Jannah iliyoahidiwa kwa watu wema na wacha-Mungu, basi makusudio ya wanadamu ni anasa, mvinyo, wanawake na mimbo! Kulikuwa hakuna zaidi ya hayo! Lakini makusudio ya kuwako kwa wanadamu, kwa mujibu wa Quran, ni tofauti na hivi. Ni kwamba mwanadamu ajifunze kumpenda Mwenyezi Mungu (51:57). Kupenda utii. Kutii ni kuiga. Kuiga ni kuyeyuka kabisa, na kuyeyuka ni kujipatia sifa za Mwenyezi Mungu. Kwahiyo, makusudio ya kuwako wanadamu ni kuendeleza maisha ya kiungu. Maisha ya kiungu ni maisha mazuri. Kwahiyo, haiwezekani kufikiri kuwa mwanadamu katika maisha haya kwa miaka sabini hivi ajitahidi kujifunza na kuishi maisha ya kiungu, lakini katika Akhera aingie maisha ya furaha na anasa. Wazo hili la maisha ya Akhera halina uhusiano hata wa thamani ya maisha ya dunia hii. Namna hii, Jahannam ilifikiriwa kuwa maskani ya milele ya watu wabaya. Wale watakaohukumiwa kuishi motoni wataishi humo milele. Ukatili usiokoma. Mwenyezi Mungu asiwasamehe wenye dhambi milele!

Hadhrat Ahmad alikanusha mawazo haya yote. Alitoa hoja na akaonesha miujiza kuhuisha wazo la kweli la aimani ya Islam juu

ya kila suala. Aalionesha ulegevu wa maisha katika dunia hii, uzuri na thamani ya maisha ya Akhera. Aliumba katika nyoyo za watu yakini juu ya maisha ya Akhera  na tamaa ya kuishi na kufanya kazi na kuyangojea. Fikara za upuuzi na mifano ya starehe ambayo Waislamu wameiingiza juu ya Pepo, yote hii iliondolewa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Pepo haikuwa mfano tu. Wala hapakuwa mahala pa starehe za kimwili, kubwa zaidi kuliko za dunia hii. Baraka za Peponi ni za pekee kabisa. Starehe za Akhera ni kama furaha anayopata mtu katika kazi nzuri za maisha haya. Kilicho kiini na roho katika maisha haya, kinakuwa mwili katika Akhera. Kinachokuwa kiini na roho katika Akhera kinakuwa imara zaidi na chenye maendeleo zaidi kuliko roho ya mwanadamu katika maisha haya. Nguvu za roho katika Akhera ni za juu zaidi kuliko nguvu za roho tuijuavyo katika maisha haya. manii ya mwandamu yana sehemu ya kimwili na ya kiroho pia. Yana mwili na roho. Lakini mwandamu ambaye anaendelea toka katika manii ana roho bora zaidi kuliko roho katika manii.

Vilevile, Hadhrat Ahmad alithibitisha kuwa adhabu ya Jahannam sio adhabu isiyokuwa na mwisho. Inaweza kuchukua muda mrefu lakini siyo milele na milele. Jahannam ya milele ni kinyume na heshima ya Mwenyezi Mungu Mrehemevu. "Rehema yangu hukienea kila kitu" (7:157). Hii ndiyo tabia ya Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa Quran Tukufu. Kila kitu kinatawaliwa na rehema ya Mungu.

Quran inaeleza malipo ya Peponi kuwa ni malipo yasiyokoma (11:109; na 95:7).  Maneno haya hayakutumiwa juu ya Jahannam. Ni tofauti sana basi! Hali iliyoelezwa kwa Pepo na Jahannam inathibitisha kuwa ni vya kuchukua muda mrefu lakini katika njia mabalimbali kabisa.

Mtume s.a.w. mwenyewe alisema katika kueleza fundisho la Quran juu ya Pepo na Jahannam:

> "Utaifikia Jahannam wakati ambao hata mtu mmoja hatabaki ndani yake. Milango na madirisha yatalia kwa mvumo ya pepo"
> (Kanzul Ummal, uk. 270).

## WAISLAMU WAKO MASHAKANI

Mbali na nguzo za imani, mabadiliko makubwa yametokea katika maisha ya kila siku ya Waislamu. Waislamu wengine wamekuwa walafi kupita kiasi. Baadhi yao wameomba kuachwa kwa mafundisho ya Kiislamu. Walidhani ya kuwa ilitosha kabisa ya kwamba mtu aamini Kalima *Laa ilaha illallahu Muhammadur-Rasulullah.* Baada ya Kalima hii mtu yuko huru kufanya na kuishi atakavyo. Mtume s.a.w. ndiye mwombezi wao. Ati kama hakuna wafanyao madhambi, ni kwa ajili ya kina nani basi Mtume s.a.w. atakuwa mwombezi?

Wengine wakafikiri kuwa amri za dini zilikuwa na mwisho. kama jahazi linalompeleka mtu pwani. Wale ambao wamemwona Mungu, hawana haja na amri za dini. Ati hizi zinawafaa wale ambao hawajamaliza safari.

Wengine walifikiri kuwa amri za dini zimeamriwa kama mifano ya nje ya hali za ndani. Zama Mtume s.a.w. alipodhihiri katika Bara Arabu, Waarabu walikuwa washenzi. Akili zao vilevile zilikuwa za kishenzi na changa. Kwa hiyo, kukatiwa mkazo sana juu ya matendo ya nje, kama udhu, maombi, kusujudu, saumu n.k. Sasa wanadamu wameendelea vya kutosha. Akili zao pia zimeendelea. Sasa matendo hayo ya nje si lazima tena. Ikiwa mtu ni safi, kama anamkumbuka Mola wake, anakidhi haja za jamaa zake, anawatumikia masikini, anakula ana kunywa kwa kiasi, anajiunga katika kazi za taifa n.k., anafanya vile anavyotakiwa afanye akiwa Mwislamu. Sala zake, saumu, zaka na haji sasa ndiyo hizo kazi njema azifanyazo.

Waislamu wengine wao wakarukia kwingine. Wakafikiri kuwa ili kupata wokovu, ni lazima mtu amwige Mtume s.a.w. katika mambo madogo. Mathalan, kama Mtume s.a.w. alitumia mshono fulani wa nguo, ni wajibu wa Mwislamu kuvaa nguo ya namna ileile. Kama Mtume s.a.w. alikuwa na nywele ndefu, basi nywele ndefu lazima zifugwe na kila Mwislamu n.k.

Waislamu wengine walifikiri kuwa Mtume s.a.w. hakuwa na haki kufundisha chochote kwa njia ya kazi za dini. Quran tukufu ina kila kitu alichotaka Mwenyezi Mungu kifanywe na mwandamu. Chochote ghairi ya hiki ni uongo. Mtume s.a.w. hali ya kuwa

mwanadamu hakuweza kufundisha lolote zaidi ya lile alilofundisha Mungu.

Bado, wengine wanaweka mategemeo yao yote kwa wanazuoni na Masheikh fulani. Hawa, wanadhani, wamesema neno la mwisho juu ya suala la itikadi na matendo. Wajibu wetu ati ni kutii bila kuuliza uliza.

Hizi ndizo itikadi pana na kazi ambazo kwazo Waislamu wametoka nje ya Uislamu wa kweli. Tukielekea yaliyo madogo zaidi, tutakuta njia hata zaidi kuliko hizi zenye kumkufurisha mtu. Waislamu wengine wametoa fatwa ati ni kufuru kujifunza lugha zingine, Kiingereza mathalan. Wengine akafikiri kuwa kujifunza elimu za kisasa ni madhara kwa imani ya kweli. Kwa upande mwingine, baadhi ya Waislamu wanakana baadhi ya mafundisho ya waziwazi ya Quran. Kula riba ni kama kupigana vita na Mungu (2:280). Na bado kula riba kunasemwa na jama hao kuwa halali.

Katika maelezo ya Sala, Saumu na Zaka, kanuni za urithi na mambo mengine, kuna hitilafu kubwa baina ya chuo na chuo. Mafundisho ya Islam yamechafuliwa kabisa. Pengine, mambo madogo madogo yanafanywa kuwa ya msingi hasa. Wale wanaoamua kufikiria maelezo fulani kwa namna nyingine wanalaumiwa. Kama Mwislamu anyooshe kidole chake cha shahada zama za kutoa shahada, atapoteza kidole hicho. Kama Waislamu waseme Amin kwa sauti kubwa katika Sala ya jamaa, watajazwa uchafu vinywani mwao. Maisha hasa ya Kiislamu, kama maisha ya imani, yamepotea kwa kupotoka kwa Waislamu na kutopatana kwao.

Hadhrat Ahmad akahuisha maisha hasa ya Kiislamu. Akaeleza jinsi jinsi ilivyo ni kosa na hilaki kuacha mafundisho ya Kiislamu. Mtu asifanye dhambi makusudi, na halafu atazamie ati Mtume s.a.w. atamwombea Siku ya Kiyama. Uombezi wa Mtume s.a.w. ni kwa wale waliojitahidi kujiepusha na madhambi. Uombezi utakaowasaidia juu ya udhaifu wao na mwanguko uliowafikia katika juhudi yao kubwa ya kujiepusha na madhambi. Uombezi sio kwa watu wenye nia hasa ya kutenda madhambi. Haki hii ya uombezi amepewa Mtume s.a.w. ili kuteremsha dhambi, sio kuipandisha.

# MAKUSUDIO YA KUUMBWA MWANADAMU

Kwa namna hii Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alionesha kuwa makusudio ya kuwako kwa mwanadamu ni 'Ubuudiyyah; kuzama katika sifa za Mwenyezi Mungu au kuiga tabia yake. Makusudio sio Shariah, kutekeleza amri na sheria. Naam, alichoamuru Mwenyezi Mungu ni lazima kutekeleza na kwa muda uleule aliosema Mwenyezi Mungu. Lakini maungano na Mwenyezi Mungu ni mnyororo usio na mwisho. Tunaweza kuwa karibu naye sana, na bado tuwe hatujamfikia kabisa; hivi kwamba hatutaweza kufikiri kuwa ukaribu na Mungu umeshapatikana, na ya kwamba sasa hakuna kingine zaidi cha kufanya wala ibada haina haja. Dua iliyofundishwa katika Sura ya Alhamdu - "Wewe tu twakuabudu" na "Wewe tu tunakuomba mwongozo katika njia iliyonyoka" hapana budi isomwe mara kwa mara kila siku na Waislamu. Dua hii ilisomwa hata na Mtume s.a.w. ambaye aliendela kuisoma mapaka kufariki. Kadhalika alisoma mara kwa mara dua zingine zilizomo ndani ya Quran kama "Ee, Mola wangu, nizidishie elimu" (20:115). Ikiwa Mtume s.a.w. hakufikiri kuwa kuomba kumekwisha, ni nani mwingine awezaye kudai ya kuwa amemaliza safari yake ya kiroho? Wale wanaofikiri hivyo, hawawezi kuwa na wazo juu ya wasaa wa Mwenyezi Mungu. Mungu ni kama bahari isiyo na kikomo. Mtu hawezi kutumai kuivuka. Kufikiri hivyo ni kumkosea Mwenyezi Mungu.

Vilevile Hadhrat Ahmad a.s. akaeleza kuwa makusudio ya kuwako kwa wanadamu yamo katika kufuata mafundisho ya Kiislamu. Mafundisho haya yanakidhi haja za nyakati zote na hali zote za utamaduni na ustaarabu. Maendeleo ya kiroho ya mwanadamu yanalazimu kufuatwa sawasawa kwa mafundisho na itikadi za Kiislamu. Ni kosa kufikiri kuwa yalikusudiwa kwa watu wa zamani.

Akafundisha pia ya kuwa kazi za mwanadamu ni za namna mbili. Namna moja ni ya hukumu za ibada na jinsi ya kufanya mambo. Na namna nyingine ni tabia, njia na desturi zinazopendelewa na jamii au taifa. Mtume s.a.w. alionesha katika maisha yake namna zote za kazi. Alionesha namna mbalimbali za ibada ambazo zilikuwa zije kuwa sehemu ya maisha ya Mwislamu. Kadhalika alionesha

njia za kufanya mambo, ambazo alipendelea zaidi kuliko zingine. Lakini pia alifanya mambo fulani kama desturi za wakati wake, jamii yake au taifa. Haya hayakuwa sehemu ya Islam. Islam ni ya kuonwa sio kwa njia ya jamaa fulani au taifa. Ni ya kuonwa katika hali ya kiulimwengu mzima. Kuwalazimisha Waislamu kufuata njia na sesturi alizokuwa nazo Mtume s.a.w. hali ya kuwa Mwarabu au Mkuraishi ni ukatili na sio Uislamu. Katika mambo kama hayo, hata Masahaba wa Mtume s.a.w.hawakupatana. Walifanya njia zao wenyewe, lakini hawakulaumiana.

Hadhrat Ahmad akakanusha wazo la kusema kuwa kwa kuwa Mtume s.a.w. alikuwa mwanadamu tu kama wanadamu wengine, Waislamu wana haki kumtii Mungu na sio Mtume s.a.w. Kinyume na hivi, Hadhrat Ahmad alifundisha kuwa manabii wamejaaliwa kipaji maalum cha kuelewa Neno la Mwenyezi Mungu. Elimu ya kiungu waliyonayo manabii, haiwezi kuwa na mtu mwingine yeyote. Fasiri ya Maneno ya kiungu ni haki ya kila nabii. Asiyetaka kufuata maelezo ya Mtume s.a.w. amepoteza imani ya kweli.

Hadhrat Ahmad akasahihisha pia itikadi ya kuwa mtu mwema yeyote anaweza kushikwa kama mwenye uamuzi na neno la mwisho juu ya itikadi ya dini na mafundisho yake. Naam, kuna watu ambao hawawezi hata kujihukumu wenyewe. Kwa ajili yao inaonekana ni yumkini wasamehewe na hata ni lazima kwamba wamteue kiongozi wao, mtu ambaye hali yake ya utawa, utakatifu na elimu ya dini imewazidi. Lakini hili haliwasameheshi Waislamu kadhaa wanaokata hukumu ya maswali yote wao wenyewe na kupata majawabu yao wenyewe juu ya maswali hayo. Waislamu waliopata elimu hawawezi kumtii yeyote kama vipofu na bila kuuliza. Wenye elimu inawawajibikia kutenda sawa na elimu yao na kufutu (kufafanua) kila mas'ala sawa na ilivyosema Quran na Hadithi.

Akaeleza Hadhrat Ahmad upuuzi wa kupanua fundisho la Islam bila maana. Dini inahusiana na maendeleo ya kiroho na tabia ya mwandamu. Makatazo yake na amri hayaendi nje ya shabaha. Elimu ya lugha, mathalan, ni kitu chenye manufaa sana. Lugha zote zimeumbwa na Mwenyezi Mungu. Lugha fulani inaweza kutumiwa au isitumiwe, kutegemea ni vipi inasaidia au haisaidii madhumuni fulani. Sio tu kwamba si dhambi kupata ujuzi wa lugha zenye

manufaa, bali ni lazima. Lugha zingine zina faida katika kueneza dini. Kujifunza lugha za namna hii ni jambo la thawabu.

Hadhrat Ahmad a.s. akasimama imara kabisa kupinga ulaji wa riba. Akafundisha kwamba katazo hili lina hekima nyingi. Waislamu wasilirahisi fundisho hili kwa ajili ya manufaa kidogo ya kidunia.

Akafundisha pia ya kuwa mafundisho ya dini yamo katika namna mbili za mambo. Ni usuli au matawi ya usuli. Usuli zimefundishwa katika Quran na kwa ajili yake haiwezekani kupingana. Kwa hali yoyote, ni nafasi kwa kila mtu kujaribu kuelewa maana na mafundisho yake. Matawi ya usuli, kwa upande mwingine ni ya namna mbili: (1) Maelezo yaliyotolewa na Mtume s.a.w. mwenyewe; inawezekana aliamuru mambo fulani yafanywe kwa njia fulani na akakataza njia zingine za kufanya mambo hayo. Katika matawi kama hayo, Waislamu wanatakiwa wafanye vile alivyoamuru Mtume s.a.w. Au (2) Matawi ambayo yanaweza kueleweka katika njia mbalimbali. Pengine tuna zaidi ya tafsiri moja za jinsi Mtume s.a.w. alivyofanya jambo fulani. Inawezekana pia ya kwamba katika maelezo kama hayo Waislamu tangu mwanzo walifanya kwa njia mbalimbali. Katika mambo kama hayo wajibu wa Waislamu ni kustahamiliana. Wanaweza kuchanga njia za kufanya mambo hayo zao wenyewe lakini ni lazima wavumilie njia zilizo tofauti na zao. Njia zingine vilevile zimeshikwa na watu kuwa njia wanazozipendelea wao. Njia mbalimbali hizo ni lazima zifahamiwe kuwa za sawa. Kama njia hizi mbalimbali hazikuwekwa na Mtume s.a.w. ni kwa vipi Masahaba wa Mtume s.a.w. waliweza kushika njia fulani ya kufanya jambo fulani na kundi jingine la Masahaba likashika njia nyingine ya kufanya jambo hilohilo moja? Ukweli wa jambo hili ni kwamba wanadamu wameumbwa tofauti. kwa hiyo, wanatenda mambo kwa njia mbalimbali. Akifahamu asili hii ya mwanadamu, Mtume s.a.w. aliruhusu njia mbalimbali katika kutekeleza kazi fulani. Yeye mwenyewe aliweza kushika njia mbalimbali katika kufanya jambo la namna moja. Alifanya hivi ili kuonesha kuwa tabia ya mwanadamu ina mabadiliko, na kuwa sio tu kwamba watu mbalimbali walifanya jambo moja kwa njia mbalimbali, bali watu haohao walifanya jambo hilohilo kwa njia mbalimbali katika mwahala mbalimbali. Kuinua mikono miwili

wakati wa kusema *Takbir* katika sala kulitekelezwa kwa namna hii ya tabia ya wanadamu. Bila shaka, inajulikana ya kuwa Mtume s.a.w. mwenyewe pengine aliinua na pengine hakuinua mikono miwili wakati wa *Takbir*. Vilevile kusema *Amin* mwisho wa kusomwa Sura ya Alhamdu na Imam katika sala ya jamaa. Jamaa wengine walisema *Amin* kwa sauti kubwa na wengine hawakusema kwa sauti kubwa. Mtume s.a.w. alikubali yote mawili. Kukunja mikono miwili katika Sala vilevile kulifanywa kwa njia mbalimbali. Inaonekana kwamba Mtume s.a.w. au Masahaba walikunja mikono, pengine karibu na kitovu, na pengine juu zaidi. Hapo pia badiliko limeruhusiwa. Ndani ya mipaka mtu aliweza kuchagua kufanya alivyopenda. Lakini anayechagua kufanya jambo fulani kwa njia fulani hana haja kumlaumu mwingine kwa kufanya jambo hilohiloo kwa njia nyingine. Mtu mwingine vilevile ana hiari kufanya jambo hilohilo kwa njia yake. Kwa kuweka na kueleza amri zote za hekima za Islam, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alitatua migogoro yote baina ya firka (kundi) na firka nyingine na kumaliza mabishano kati yao. Mabishano hayo yanahusu maelezo ya jinsi ya kufanya mambo fulani. Kutolewa kwa mgogoro huu, Waislamu wa zama hizi wanaweza kufanya kazi zao za dini kwa heshima na uhuru wa Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w.

## BADO TUMNGOJE NANI?

Hili linaweza kukupa, msomaji mpenzi, mawazo fulani juu ya islahi aliyoileta hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian a.s. katika itikadi za Waislamu. Kama islahi hii isimuliwe yote kabisa kama ilivyo, itahitaji kitabu cha pekee. Kwa hiyo, nimeona nieleze yale mambo muhimu. Unaweza kuamua hata kutokana na haya machache kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad aliondoa makosa yaliyoingia katika itikadi za Waislamu na matendo yao. Ameiweka islam katika nuru yake ya kweli mara nyingine, hivi kwamba uzuri wake wa zamani umeanza tena kuwavutia wafuasi wake na wengine pia. Nguvu ya Islam ya kutakasisha imeumuka tena.

Sasa, msomaji mpenzi, nimeeleza makosa ya itikadi na matendo ambayo kwayo Waislamu wameanza kudhalilika zama hizi. Makosa haya yamewaingia Waislamu, licha ya kuwa wanayo Quran Tukufu ambayo kila neno, herufi na irabu zake zimo katika hali ya usafi tangu mwanzo wa kufunuliwa kwake. Watu wenye maandiko matakatifu yaliyohifadhiwa kama Quran Tukufu wasingeweza kupotoka katika makosa mabaya zaidi kuliko haya. Makosa mabaya zaidi ya itikadi na matendo yangetokea kama, Mungu apishe mbali, Quran Tukufu ipate mabadiliko. Lakini kwa kuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu, Quran haiwezi kubadilika. Kwa hiyo Waislamu wasingeweza kuanguka kwenye makosa mabaya zaidi ya haya yaliyo hivi sasa.

Sasa, hebu tufikiri kidogo. Makosa waliyoangukia Waislamu yamefikia mipaka ya mwisho ya ubaya. Je, bado tu haujafikia wakati wa Masihi Aliyeahidiwa? Kwa upande mwingine, sio kwamba Hadhrat Ahmad amekuja tu, bali amesahihisha pia makosa ya Waislamu na kuondoa hatari zote zilizoufikia Uislamu. Je, tumsubiri mtu mwingine aje afanye kazi hii hii? kazi iliyochaguliwa kwa Masihi Aliyeahidiwa imefanywa barabara na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Kwa hiyo ni lazima awe Masihi Aliyeahidiwa. Jua linapokuwa wakati wa adhuhuri, ni upumbavu kusema kuwa haliko. Mbele ya hoja na dalili za waziwazi, ni ujinga kusema kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad siye Masihi Aliyeahidiwa.

## HOJA YA SITA
## MSAADA WA MWENYEZI MUNGU

Hoja hii pia kama hoja zingine, ina idadi kubwa ya hoja ndogondogo. Ni hoja ya msaada wa mbingu. Bila ya huo Mjumbe wa Mungu hawezi kuthibitisha maungano yake na Mungu. Kila Mjumbe wa Mungu au kiongozi anapendwa na Mwenyezi Mungu. Uhusiano wake mahususi na Mungu hauwezi kuthibitika mpaka mkono wa Mwenyezi Mungu uonekane ukifanya kazi nyuma yake. Mungu amsimamie kwa sababu yeye anasimama kwa ajili ya wale anaowapenda Mungu. Mjumbe anaweza kujidai kazi maalum kwa

niaba ya Mwenyezi Mungu, lakini kama hapokei kutoka kwa Mwenyezi Mungu msaada ambao mpenzi wa Mungu anastahili kuupata, ni lazima akataliwe mbali kuwa mhadaa na mwongo. Haiwezekani kwamba Mwenyezi Mungu amteue Mjumbe, lakini asioneshe ulinzi maalum au mahaba kwa ajili yake; ya kwamba asimsaidie, zama ambazo msaada anauhitaji. Wafalme wa kidunia wanawasaidia wajumbe wao. Wanawaangalia na kuwapa kila msaada wa lazima. Hazina ya Mungu haina idadi. Ana elimu ya ghaibu. Ni lazima awasaidie wajumbe wake na watumishi. Mdai wa unabii wa Mungu ambaye anapata msaada na ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni Mjumbe wa kweli. Kwani, haiyumkiniki Mwenyezi Mungu asahau watumishi wake wa kweli. Na ni vigumu pia ya kuwa Mungu amsaidie mwongo na asimkamate kwa uongo wake akienda huko na huko kuwapoteza viumbe wa Mungu na kupata mafanikio. Na zaidi haikubaliani na akili ya kwamba Mungu amsaidie sana mwongo kama huyo na mhadaa. Amesema Mwenyezi Mungu katika Quran:

"Mwenyezi Mungu amekwisha andika: bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu! Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye heshima" (58:22).

Mwenyezi Mungu amehukumu hivi mwenyewe ya kwamba Yeye na Mitume Wake watashinda siku zote. Huu ni ushuhuda wa Uwezo Wake juu ya vitu vyote. Wale wanaoleta Ujumbe kutoka kwa Mungu ni lazima wafaulu. Mungu ni Mdhamini wa ufaulu wao. Kama si hivyo, watu wataanza kutia shaka juu ya Uwezo Wake na ufalme. Tunasoma katika Quran:

"Bila shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi" (40:52).

Na tena:

"Lakini Mwenyezi Mungu Huwapa mamlaka Mitume Wake juu ya yeyote Amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu" (59:7).

## MANABII WA UONGO HUADHIBIWA

Ni dhahiri kutokana na aya hizi kwamba kwa mujibu wa Quran Tukufu Mwenyezi Mungu Hujaalia ushindi na ufaulu kwa Wajumbe wake. Anawapa ushindi juu ya wengine. pengine kwa kimwili na kiroho pia, au kwa kiroho peke yake.

Kadhalika tunasoma katika Quran jinsi Mwenyezi Mungu alivyowafanyia manabii wa uwongo. Tunasoma kwamba waongo hawezi kupata ufaulu. Ni lazima waipate adhabu ya Mungu:

"Na kama (Mtume) angelizua juu Yetu baadhi ya maneno, bila shaka Tungalimshika kwa mkono wa kuume. Kisha kwa hakika Tungalimkata mshipa mkubwa (wa moyo)" (69:45-47).

Aya hizi ziko wazi kabisa. Kama nabii aongope makusudi juu ya Mungu, adai kwamba amepokea Ujumbe kutoka Kwake, basi Mungu anamkata mshipa wake wa shingo. Msaada wa Mungu na Ulinzi unaondolewa kwa ajili yake - badala yake anakutana na mkosi.

Tena tunasoma ndani ya Quran:

"Na nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uongo Mwenyezi Mungu au azikadhibishaye Ishara Zake? Hakika wadhalimu hawatafaulu" (6:22).

Aya hii inatoa mashaka yote kwamba mwongo hawezi kufaulu kwa mujibu wa kanuni ya Mungu. Itawezekanaje kwa mtu amtungiaye Mungu uongo, mtu ambaye ni maluuni, afaulu katika kutunga madai ya uongo? Yeye ni mdhalimu mkubwa kuliko wadhalimu wote, kwani anadhulumu roho za watu!

Kwa hiyo inaonekana kuwa Mwenyezi Mungu anafanya kazi kwa njia mbili: Kwanza anawapa nguvu na ufaulu Mitume wake. Pili, kama mtu, makusudi, anatunga ujumbe na kusema ni wa Mungu, sio tu kwamba ananyimwa msaada wa Mungu, bali anafedheheshwa na kuhilikishwa na Mungu. Niliyoyasema kwa njia ya akili hapa yanasaidiwa na aya za Quran. Kwa mujibu wa Quran Tukufu, hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowafanyia manabii wa uongo. Hizi ni kanuni mbili za Mungu.

Kama tukichunguza madai ya Hadhrat Ahmad a.s., kwa nuru ya kanuni za Mwenyezi Mungu, ukweli wake utaonekana wazi kama mchana. Atathibitika kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

kabla sijaendelea kuonesha ni kwa njia gani mbalimbali Mwenyezi Mungu alimsaidia, inaonekana ni lazima nieleza hali aliyokuwa nayo alipozaliwa, hali ambazo zingemsaidia, na hali zilizokinga njia yake, na kama madai yake yaalielekea kufaulu au la kwa hali aliyokuwa nayo na hali ya wakati wake.

## HAKUWA NA NJIA ZA KUMSAIDIA

Ni njia gani zingemsaidia Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.? Alikuwa wa ukoo maarufu. Hii imekuwa ni bahati ya manabii wote wa Mwenyezi Mungu. Wamekuwa wakitolewa katika nasaba maarufu. Hii ni kurahisisha kukubaliwa kwao na watu. Ukoo wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ambao kwanza ulikuwa maarufu, lakini wakati huo haukuwa hivyo tena. Ulikuwa ukoo wa kimaskini ukilinganisha na mafanikio na mvuto wake wa mwanza. Ardhi yao yote na nguvu ya utawala iliondoka. Nguvu ya utawala ilikuwa imenyang'anywa na Masingasinga, ardhi yote ilitolewa kwa Waingereza ambao walishika mahala pa Masingasinga kuitawala

Punjab. Kwa hiyo, nguvu na mali havikuwako. Haikuweza kusemwa ya kwamba nguvu ya utawala na heshima ya ujamaa ndiyo imezaa kundi kubwa la wafuasi kama hili.

Wala hakuwa na cheo chochote cha jadi au usufi au usheikh. Elimu yake ilikuwa imepangwa na walimu wa majumbani, hivi kwamba ilikuwa ndogo au pengine si chochote ukilinganisha na elimu iliyopatikana katika vyuo vya dini vya zamani katika nchi hiyo. Wala katika wilaya yake au mkoa, wala nje yake, hakuhesabiwa miongoni mwa masheikh au Maulamaa wa Kiislamu. Watu hawakumfuata kwa sababu ya kuwa na hati yoyote ya Uanachuoni. Ukoo wake haukuwa ukoo wa Masheikh wa urithi au masufi. Wala hakupata kuwa na cheo hicho. Heshima kama hizi wanazipata viongozi wengi wa dini, hivi kwamba baada ya kufariki kiongozi huyo, wa nyuma yake anarithi kiti chake na kujitangaza kuwa khalifa wake. Hadhrat Ahmad hakuwa na heshima ya namna hii wala daraja.

Hakushika kazi yoyote wakati huo katika serikali. Kwa hiyo hakuweza kumvuta mtu yeyote kwa ajili ya haiba ya cheo kikubwa serikalini.

Akiwa mtu mwenye tabia ya kukaa peke yake, alipenda kukaa faraghani kwa ajili ya ibada, hivi kwamba hata wale walioishi jirani naye hawakuweza kumjua. Alifikiwa na wageni lakini wengi wao walikuwa mayatima na wenye haja. Kila siku alikuwa akila chakula pamoja nao. Mara kwa mara alijiacha na njaa akiwaachia wao chakula chote. Baadhi ya wageni wake walipenda sana dini. Hakukuwa na wengine. Hakukutana na watu mbalimbali na wala watu hawakuwa na haja ya kukutana naye.

Kwa hali na njia, ambazo zilikuwa kizingitini kwa ajili yake, ni lazima tukumbuke kuwa hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Alidai kuwa Masih na Mahdi Aliyeahidiwa katika Hadithi. Kundi la kwanza kubwa lililoanza kupinga madai yake ilikuwa kundi la Maulamaa. Kukubali madai yake kulikuwa na maana kumaliza heshima yao waliyoipata kwa Waislamu kwa miaka mamia na mamia. Inastaajabisha kidogo kuwa Maulamaa hawa walijiona wanashambuliwa vibaya na Hadhrat Ahmad. Mafanikio ya madai yake yakaleta kushindwa na kuanguka kwao. Kama watu kwa ujumla wamwendee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na wamwone mkweli,

nani angewatazama Maulamaa kwa ajili ya mwongozo?

Masufi wa urithi pia wakawa maadui zake. Pamoja na mwongezeko wa mvuto wa Hadhrat Ahmad a.s., masufi hawa walikuwa na hakika ya kuwakosa wafuasi wao. Hawakuweza tena kujifanya kuwa Masheikh wa viongozi. Iliwabidi kumkubali mtu mmoja kuwa Sheikh wao na kiongozi wao. Mafanikio ya Masihi Aliyeahidiwa hali ya kuwa kiongozi na mhuishaji yalikuwa pia yakomeshe uhuru wa matendo uliotumiwa na Masheikh hao wa urithi kama haki yao.

Matajiri pia walikuwa maadui zake. Kwani Hadhrat Ahmad aliwahimiza kutekeleza amri za Islam. Matajiri hawakuzoea hivi. Wajibu wa Uislamu kwao ulikuwa kero. Wakati huohuo alifundisha kutoa sadaka, usawa na huruma; usawa baina ya watu wote, msaada na huruma kwa ajili ya maskini na wanyonge. Hili, matajiri hawakulipenda. Waliweza kuona ya kuwa kwa mvuto wa Hadhrat Ahmad, utumwa wa watu maskini utatoweka; na fadhila waliyokuwa nayo juu ya watu maskini pia itapotea.

Wafuasi wa dini zingine walikuwa na chuki. Dini zote zingine zisizo Islam zilionekana zina woga wa kushindwa. Kama vile mwana kondoo amwogopavyo chui. Hivihivi wasio Waislamu wote walimwogopa. Walifanya vyote walivyoweza kutaka kumhilikisha yeye na Mwendeleo wake.

Watawala pia walikuwa maadui zake. Siku zote wamekuwa na woga kwa Masihi na Mahdi. hadithi za zamani ziliunganisha majina haya na machafuko na uasi. Kwa kweli, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alifundisha utii kwa serikali yoyote. Lakini hili halikuwatosheleza. Maelezo ya utii waliyadhania kuwa sehemu ya matayarisho ya vita. Walifikiri kuwa mara tu Hadhrat Ahmad akipata nguvu, atautupilia mbali utii wake na kuanza vita.

Watu wa kawaida vilevile walimjia juu. Kwanza, watu raia wako chini ya viongozi wao, Masheikh, masufi, matajiri, makuhani na Mapadre. Pili, ni maamuma na wanaongozwa na mila zao. Wanalichukia wazo lolote jipya, na badiliko lolote la imani. Madai ya Masihi Aliyeahidiwa yalikuwa mapya kwao. Kwa hiyi, upande mmoja wakiwa chini ya mvuto wa viongozi wao, na upande mwingine wakiwa wajinga, wao pia walimchukia.

Ilimradi, katika njia mbalimbali, kwa nia mbalimbali, watu wa aina zote walikuwa maadui zake. Walifanya chini juu kumhilikisha. Maulamaa wakatayarisha fatwa za ukafiri kinyume chake. Walikwenda Makka na Madina kupata sahihi juu ya fatwa hizo. Kwa kweli kwa desturi yao, walibuni sababu mbalimbali za kumtangaza Hadhrat Ahmad kuwa kafiri na kuwachochea watu wafanye kila namna ya chuki ili kumshinda.

Masufi vilevile waliwachochea wafuasi wao kumchukia. Walieleza mafundisho yake ya dini kuwa ni kinyume na Islam. Kwa wakati huohuo walifanya madai yaliyotiwa chumvi ya kwamba wana nguvu ya kiroho na wana maungano na Mwenyezi Mungu. Wakiwatisha wafuasi wao na kuwachochea wamchukie Hadhrat Ahmad, hawakusita kubuni hadithi juu ya nguvu zao za kimwujiza na kuwadanganya watu kwa kazi zao za ulaghai. Baadhi yao waliwaambia wafuasi wao kuwa kama Mirza Ghulam Ahmad ni mkweli, dhambi ya kumkadhibisha wataibeba wao. Wafuasi hawakuwa na haja zaidi. Kwa njia za namna hii wakasimamisha kundi kubwa la upinzani.

Matajiri walijivuna kumfanyia uadui kwa mali yao na nguvu. Viongozi wa dini zingine wakajiunga na maadui zake wa Kiislamu. Watawala wakatumia madaraka yao katika kuwafanya watu wamwadui. Wale waliotaka kumwamini na kuungana naye, walijiletea ghadhabu. Watu wa kawaida wakajitia kugoma, kufanya ghasia, na kuwashawishi viongozi wao wazidi kumwaduia.

kwa ufupi, kila namna ya njia iliyowezekana ilifanywa kwa kumwadui. Akipingwa na jamaa zote, na wafuasi wa dini zote, Waislamu na wengine, alijiona mtu mmoja khilafu ya watu wote.

Sasa, ni kwa vipi mafundisho yake yalihusiana na maelekeo yaliyokuwako? Kama tu yalizidisha itikadi ziliokuwako na desturi, ingeweza kusemwa ya kuwa mafanikio hayakuwa kwa sababu ya msaada wowote wa mbingu, bali ni kwa sababu ya maelekeo ya wakati. Ya kwamba maelekeo haya pengine yasingeelezwa waziwazi na mtu yeyote. Pia ingeweza kusemwa ya kuwa aliyofundisha Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad na aliyoyahubiri yalikuwa sawa na maelekeo; kwa hiyo, watu akakusanyika pembezoni mwake. Ya kwamba walimwona akisema mambo

yaleyale na kuzidisha makusudio yaleyale. Maeleko katika wakati wowote yanaweza kuwa ya namna mbili. Ama yale yanayokubaliwa na watu wengi, au kama sio yanakubaliwa na wengi, basi yanayokubaliwa na elimu mpya iliyoenea wakati huo. Fikara na itikadi zinazokubaliwa na wengi zinaenezwa kwa urahisi. Fikara na itikadi zinazokubaliwa na wachache tu wenye elimu nyingi pia zinaenezwa kwa urahisi. Fikara na itikadi za wachache kama hao hukutana na upinzani mwanzoni, lakini baada ya uchunguzi wa akili na mazoea ya kila siku, zinakubaliwa na kuenea. Kuenea kwake kunangojea kuenea kwa elimu.

## MAFUNDISHO KINYUME NA MAELEKEO

Fikara na itikadi alizofundisha Hadhrat Ahmad a.s. hazikuwa za aina yoyote ya aina hizi mbili. Aliwaita watu kwenye mawazo ambayo wengi hawakupenda kuyakubali. Wala itikadi zake na fikara hazikuwa zenye kuchukuana na elimu iliyokuwa inaenezwa wakati ule. Kwa hiyo, mafundisho yake yalipingwa na watu wa aina zote mbili. Ilimbidi ashindane na wote. Ilimbidi apigane na mawazo ya kimila na ya wataalamu wa ustaarabu. Wale walioshiriki katika itikadi za kimila, walimsema kuwa mkanaji aliyejitenga., kafiri. Wale walioshiriki katika elimu za kisasa, walimsema kuwa mtu asiyekuwa na fikara pana, wa nyuma, mwenye kushikilia mambo ya kizamani. Alipofundisha kutoamini kuwa Yesu yu hai, mazingaombwe ya kishirikina, makosa juu ya malaika, kutanguliwa kwa sehemu fulani za Quran, makosa juu ya Pepo na Jahannam, na maana za kosa juu ya amri za dini, aliwaudhi watu wa kawaida. Aliposisitiza juu ya faida ya kutekelza amri za dini kama kukataza kula riba, kuamini malaika, athari ya dua, ukweli juu ya Pepo na Jahannam, uthabiti wa miujiza, aliumua hasira za wataalamu. Hakuwa na wengi wa kawaida wala wachache wataalamu. Hivyo basi, hawezi kusemwa ya kwamba alifaulu kwa sababu aliogelea pamoja na maelekeo ya wakati. Alikuwa kinyume na maelekeo yaliyokuwako na pia maelekeo ambayo yalitazamiwa kutokea baadaye.

Kwa hiyo, hakukuwa na hali za asili wala njia ambazo zingemsaidia katika madai yake. Kwa upande mwingine, njia za kila aina na hali zilimpinga yeye. Hali yake mwenyewe ya maisha haikuweza kusaidia madai yake. hakuwa na mali wala nguvu yoyote, hakuwa na fahari yoyote ile, yake wala ya ukoo wake. Wala hakuweza kutumaini kufanikiwa kwa sababu ya hali za wakati wake. Aliyofundisha hayakufuatana na amelekeo ya watu. Kama alifaulu licha ya kukosa kabisa kabisa faida yoyote ya asili, ufaulu wa madai yake ni lazima usemwe ni msaada maalumu wa Mwenyezi Mungu, sio kwa sababu za kawaida.

## ALIFAULU KWA MSAADA WA MBINGU.

Sasa ninaendelea kueleza ni kwa namna gani, licha ya uadui wa watu wa aina zote na kukosekana kwa njia za kawaida, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alifaulu katika madai yake. Nimekwisha eleza ya kuwa ni kanuni ya Mwenyezi Mungu kwamba hawaachi wakae muda mrefu duniani watu wanaomzulia uongo. lakini tunaona kuwa Hadhrat Ahmad alitangaza ufunuo alioupata kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ambao ulimwita kwa jina la Mhuishaji. Na bado, aliishi miaka arobaini baada ya kutangazwa. ufunuo huo na mnamo muda huu mrefu aliendelea kupaata msaada na rehema za Mwenyezi Mungu, katika njia ndogo na kubwa. Kama mwongo anaweza kuishi muda mrefu namna hii, na kufanikiwa sana baada ya kutangaza ufunuo wa uongo, basi, Mungu apishe mbali, itatulazimu tukubali kwamba fundisho la Quran katika sura 69 aya 45 niliyoitaja hapo mbele ni la uongo na ya kwamba hata Mtume s.a.w. hawezi kutaja mizani hii kuthibitisha madai yake. Lakini mizani iliyoelezwa na Quran haiwezi kuwa ya uongo, basi ni lazima pia iwekwe kwa ajili ya madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Kama alitangaza ufunuo aliopata, na akaishi umri mrefu baada yake, na Mungu sio kwamba alimwacha tu, bali alimsaidia pia, basi yatupasa tukubali ya kuwa alikuwa mkweli.

Zama alipotangaza ufunuo huo, hakujulikana na wengi, kwa hakika hakujulikana na ulimwengu mzima kwa mapana. Baada ya kutangazwa kwake, licha ya uadui wa watu wa aina zote, alifaulu kupata kundi kubwa la wafuasi, hivi kwamba hata maadui zake walilazimika kumheshimu. Akaanza kuitwa kiongozi wa maana sana wa Kiislamu. Serikali ya siku hizo ambayo kwanza ilimshuku, ikaanza kumheshimu na kumwamini kuwa kama mvuto wa amani na upendo. Jina lake likaenea sehemu nyingi za dunia na miongoni mwa wafuasi wake wanapatikana wengi walio na mahaba naye sana ambao wako tayari kutoa sadaka roho zao kwa ajili yake. Hata katika nchi za Ulaya ambako watu kwa kawaida ni maadui za Uislamu, alipata wafuasi waliokubali Islam kwa kusikia Ujumbe wake. Walimpenda kikweli kweli. Mmoja wao aliniandikia barua akisema kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad amemwia deni kubwa. Alipata baraka ya Islam kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Kwa hiyo, aliandika, kila asiku alipokwenda kulala aliomba kwa ajili ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad na aliongeza dua hii baada ya kumsalia Mtume s.a.w. Sadaka, heshima na mapenzi aliyokuja kuyapata Hadhrat Ahmad, licha ya uadui wa pande zote hapo mwanzoni, yasingepatikana kamwe kama angekuwa mwongo.

Zama Hadhrat Ahmad alipotangaza madai yake, alikuwa peke yake. Uadui wa aina mbaya sana wa Masheikh, Mapandit na Mapadre, wa matajiri na maskini, (na hasa mwanzoni kabisa) wa watawala, uliusalimu ujumbe wake. Dhamiri ya hao wote ilikuwa kumfanya hata mmoja asikubali wala kusikiliza madai yake. Licha ya hayo, watu walianza kujiunga naye kwa wawili wawili mpaka watatu watatu. Akapata wafuasi miongoni mwa matajiri na maskini, miongoni mwa Masheikh na Masufi. Waislamu walijiunga naye kama walivyojiunga naye Mabaniani na Wakristo, kutoka nchini mwake hata nchi za mbali. Jumuiya yake ikaongezeka katika Afghanistan, wafusi wake waliweza kupatikana kila wilaya na hivi hata baada ya kupigwa mawe Waahmadiyya kadha kwa amri ya watawala wa Afghanistan, wakichochewa na Mashiekh. Waahmadiyya wakapatikana katika Bara Arabu, Uajemi, Urusi, Afrika ya Magharibi, Kaskazini na Kusini, Australia, Amerika na Ulaya. Hadhrat Ahmad alikuwa na watu waliotawaliwa, na bado alipata wafuasi miongoni mwa

mataifa yaliyokuwa huru. Alipata wafuasi miongoni a wafuasi wa dini ambazo kwa muda mrefu sana wamekuwa maadui wakubwa wa Islam. Ufaulu wa namna hii na wa kadiri hii hauwezi kupatikana minghairi ya msaada wa Mwenyezi Mungu.

Kadhalika walijaribu kumlisha sumu na kumfungisha gerezani. Alifikishwa mahakamani. Lawama za uongo zililetwa khilafu yake. Wakristo, Waislamu, Mabaniani, wote walikuwa wameungana kumwangamiza. Kwa kweli walikuwa wamtie msalabani Masihi wa pili kama walivyomfanya wa kwanza. Lakini mashambulio yalishindwa alibakia salama. Msaada wa Mungu ulizidi kumteremkia.

Makusudio ya kufika kwake, tukumbuke, yalikuwa ni kuhuisha na kuutangaza Uislamu. Kwa makusudio wakuu haya mawili Mwenyezi Mungu alimjaalia wafusi wenye mapenzi na vilevile fedha za kutosha, hivi kwamba sasa Jumuiya inafanya kazi kwa kiasi cha rupia laki tano kwa mwaka. Magazeti yanachapishwa kueneza Uislamu katika Panjab, Bengali, Sri Lanka. Misri na Amerika. Vitabu mamia na mamia vimeandikwa kutangaza madai yake. Mwenyezi Mungu anawafunulia nyoyo zao watu wakubali ujumbe wake, hivi kwamba wanamgeukia kwa utii na msaada. Maelfu ya watu walijiunga naye kwa sababu walipata njozi au ufunuo wa namna fulani ambao kwao ukweli wa Hadhrat Ahmad ulifikishwa kwao na Mwenyezi Mungu. Walimchukia, lakini Mungu akatia mapenzi katika nyoyo zao kwa ajili yake.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alifaulu licha ya uadui mkubwa uliokuwako na kukosekana njia za kumsaidia. Ametayarisha Jumuiya iliyo na jazba motomoto ya kuueneza Uislamu nayo inaongezeka katika heshima, utajiri, nguvu na heba. Jumuiya hiyo imeenea dunia nzima!

Kanuni ya Mwenyezi Mungu ni kwamba mdai wa kweli anapata msaada wa Mwenyezi Mungu, na mwongo anashindwa, anafedheheka na anakufa mara moja. Hii kuwa ndio kanuni na hakuna kanuni nzuri zaidi kuliko hii, basi hakuna shaka inayobaki juu ya ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Kama madai yake bado yana shaka, swali ni hili: Kuna istishhada gani basi ya ukweli wa manabii waliofika ulimwenguni?

## ALAMA ZIPAMBANUAZO

Hebu nifafanue hapa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. yalikuwa ya kweli; sio tu kwamba alianzia na njia dhaifu na halafu akafikia ufaulu. Heshima na ufaulu mara nyingi huwafikia wale waliokuwa dhaifu mwanzoni. Nadir Shah alikuwa mtu mnyonge na baadaye akawa mtu maarufu na mshuhuri. Na Poleon alikuwa mtu wa kawaida tu, lakini alikuja kuwa mshindi duniani. Licha ya ushindi huo, hawawezi kudai kuwa waliteuliwa na Mwenyezi Mungu kufanya waliyoyafanya. Hawawezi kusemwa walipokea baraka zake na mapenzi yake. Lakini Hadhrat Ahmad anaweza kudai aliteuliwa na Mungu na kupata heshima kwa rehema na msaada wa Mwenyezi Mungu - kwa sababu:

(1) Hadhrat Ahmad alidai tangu mwanzo ya kuwa alitumwa na Mwenyezi Mungu kwa kazi ya unabii. Kama dai hili lilikuwa uzushi, uongo wa makusudi, angepambana na mkosi na hata kifo. Kwani kwa mujibu wa kanuni ya Mungu, huu ndio mwisho wa watungao uongo.

(2) Kulikuwa hakuna njia ambazo zingesaidia katika madai yake.

(3) Sio kwamba kulikuwa hakuna njia tu; zaidi ya hayo, alikutana na uadui wa kila namna, kwa watu wote. Hakuwa na marafiki wala wafuasi ambao wangeweza kuipa Jumuiya chanzo.

(4) Alifundisha na kutangaza kwa watu mambo yaliyokuwa kinyume na maelekeo ya watu wote.

(5) Licha ya taabu hizi alifanikiwa na akaanzisha Jumuiya. Itikadi na mambo ambayo watu waliyachukia, yakaanza kukubaliwa. Alibakia salama katika mashambulio ya maadui zake. Msaada wa Mwenyezi Mungu ulimshukia kwa njia nyingi mbalimbali.

Alama hizi tano zenye maana zinampambanua mdai wa uongo wa unabii. Pamoja haziwezi kupatikana kwa mdai wa uongo. Kama zipo pamoja kwa mdai yeyote, ni kweli ametoka kwa Mwenyezi Mungu. Kama hata mizani hii inashikwa kwa shaka. hakuna tena mizani ya kupambanua wakweli na waongo.

Mizani hii haihusiani na watu wasiodai unabii. Haihusiani, mathalan, na Nadir Shah wala Napoleon. Wala haihusiani na wale wanaodai kuwa na miungu au kushiriki katika sifa za Mungu. Wala mizani hii haihusiani na wenda wazimu, wala wale wanaodhania maneno yao kuwa maneno ya Mungu. Firka ya *Shaikhiyya* ilishika

itikadi za namna hii. Walifikiri kuwa kila zama duniani kulikuwa na watu walioweza kusemwa waliwakilisha matakwa ya Mahdi. Kama ilivyo matakwa ya Mahdi ni matakwa ya Mwenyezi Mungu, basi kila kinachotokea kusemwa na watu hao au kutokea mioyoni mwao kinatoka kwa Mwenyezi Mungu. Ali Muhammad Bab, na Bahaullah, mwanzishaji wa Bahai, walikuwa wa firka hii. Kama inavyoamini firka hii kwamba watu fulani ni mifano wa Mungu, na ya kwamba maneno yao ni maneno ya Mungu, fikara zao ni fikara za Mungu, hawapati adhabu iliyotajwa ndani ya Sura 69:45 ya Quran. Aya hii inwahusu wale tu wanaotunga uongo juu ya Mwenyezi Mungu.

Mtu anayefikia mafanikio ya muda tu katika madai yake hawezi kudai kuwa hayo ni alama ya ukweli wake, kama mafanikio yake yanaweza kusemwa ni kwa sababu fulani za asili, tuseme umashuhuri, kukubaliwa na kundi la watu, mafundisho yanayofuata maelekeo; au kama unawaita watu kwenye uvumbuzi wa elimu za kisasa ambao una hakika kutokea, elimu inayokubaliwa na wengi; au kama mafanaikio yake yanaweza kuwa kwa sababu ya kukosa upinzani.

## HOJA YA SABA
## KUSHINDWA KWA MAADUI

Hoja ya saba, ambayo pia ina hoja zingine nyingi ndani yake, inaeleza kwamba wale wanaochagua njia za uadui kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, walishindwa, walifedheheshwa, wakabutaika na hata kufa kabisa.

Hoja hii inatokea katika asili ya kiungu na kibinadamu. Kama tukiwaona wapenzi wetu wanasumbuliwa, tunamkasirikia msumbuaji, tunashindana naye, na hata, kama ni lazima, tunamwadhibu kwa njia yoyote tuiwezayo. Kama tukiona mipango yetu inazuiwa, tunajaribu kuondoa kizuizi njiani. Hivihivi, hatuna budi kumtazamia Mwenyezi Mungu aondoe kizuizi katika mipango Yake mwenyewe, aoneshe uangalizi maalum kwa Wajumbe Wake, awafedheheshe maadui zao na kuwashinda wale wanaochagua kushindana na Wajumbe hao. Kama Mwenyezi Mungu hakufanya hivi, basi mapenzi Yake juu ya Wajumbe Wake hayataoneshwa na

hayatathibitishwa. Madai ya wajumbe hao yatabakia katika shaka daima. Wafalme na watawala wa kidunia, ambao wana nguvu ndogo sana, wanawasimamia watumishi wao. Wale wanaojaribu kuwawekea vizuizi watumishi hao na kuwachukia wanaadhibiwa na wafalme hao.

## QURAN INAVYOELEZA JUU YA MAADUI ZA MANABII

Inaonekana kutokana na Quran ya kuwa kile ambacho kimeoneshwa na akili ya kibinadamu, kiko sawa na fundisho la Mwenyezi Mungu. Maadui wa Wajumbe wa Mungu ni lazima waadhibiwe kwa uovu wao. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Quran:

"Na nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uongo Mwenyezi Mungu au azikadhibishaye Ishara Zake? Hakika wadhalimu hawatafaulu" (6:22).

Kutunga uongo juu ya Mungu ni maangamizi; na maangamizi ya namna hii yanapatikana kwa kuwaadui Wajumbe wa Mwenyezi Mungu. Watungaji ya uongo juu ya Allah, kwa mujibu wa Quran Tukufu, hawawezi kufaulu, Vilevile wale wanaochagua kuwapinga na kuwashinda manabii wa Mungu.

"Na hakika wamefanyiwa mzaha Mitume wa kabla yako. lakini yakawazinga wale waliofanya mzaha miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha. Sema: Safirini katika nchi, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wakadhibishaji" (6:11-12).

Wale wanaowakadhibisha manabii wa Mungu wanazungukwa na dhihaka yao wenyewe. Watu wamwogopao Mwenyezi Mungu yawapasa kukumbuka ni nini kilichotokea kwa wale waliowakadhibisha Mitume.

Aya za namna hii ziko nyingi. Alama hii haina haja ya kusisitizwa zaidi. Tukubali hii kuwa ndiyo kanuni ya Mwenyezi Mungu ya kwamba maadui za Wajumbe Wake hukutana na adhabu na wanakuwa fundisho kwa ajili ya wengine.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alipata istishhada ya namna hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mojawapo ya funuo zake inasema:

"Nitamfedhehesha kila atakayetaka kukufedhehesha."

Ahadi hii iliyofunuliwa kwa Hadhrat Ahmad ni sawa na kanuni ya Mungu. Maadui za Hadhrat Ahmad walishindwa na kufedheheka, fedheha iliyotosha kumtanabahisha kila mtu.

## MAADUI ZA MASIHI ALIYEAHIDIWA

Nimemtaja mwanzo Sheikh mkubwa, Kiongozi wa Madhehebu ya Ahli Hadith, na rafiki wa Hadhrat Ahmad tangu utoto, ambaye aliandika maoni juu ya kitabu kikubwa cha kwanza cha Hadhrat Ahmad *"Baraahiin Ahmadiyya."* Sheikh huyu alieleza kazi hii ya Seyidna Ahmad kuwa ni kazi isiyo kifani katika taarikh nzima ya Kiislamu.

Sheikh huyu huyu baadaye alikuja chukizwa na akawa adui mkubwa, wakati Hadhrat Ahmad a.s. alipotangaza madai yake kuwa Masihi Aliyeahidiwa. Sheikh akaanza kufikiri kuwa umaarufu wowote na umashuhuri alioupata Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ulikuwa ni kwa sababu ya 'maoni' yake aliyoandika juu ya *Baraahiin Ahmadiyya*. Mirza Ghulam Ahmad, alifikiri Sheikh huyu, alipata heshima yake kwa "maoni" yale. ya kwamba sifa alizosifia Sheikh huyu ndizo zimemfanya Mirza Ghulam Ahmad ajione sana! Hivyo, Sheikh huyu alitangaza, atamkana Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kwa kumkadhibisha na kumwumbua kama alivyompandisha kwa

sifa zake za mwanzo.

Pamoja na makusudio haya, Sheikh huyu akaazimia kuitembelea India yote. Aliwashawishi Maulamaa watie sahihi zao kwenye Fatwa ya ukafiri aliyoitayarisha. Sio tu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alikuwa kafiri, bali wafuasi wake pia. Wale ambao hawakuwafahamu kuwa ni makafiri, wao pia walikuwa makafiri. Fatwa hii ilipigishwa chapa na kutangazwa katika nchi nzima. Sheikh huyu akaona amefanya vya kutosha kumfedhehesha Seyidna Mirza Ghulam Ahmad a.s. Maskini, hakujua kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa ameazimia kupanga mpango wa Sheikh huyu katika njia yake Mwenyewe. Malaika mbinguni walikuwa wamekwisha jiweka tayari juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyomo ndani ya Sura ya 6:11.

"Lakini yakawazinga wale waliofanya mzaha miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha."

Vilevile walijiweka tayari juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyotolewa na Seyidna Ahmad mwenyewe:

"Nitamfedhehesha kila atakayetaka kukufedhehesha."

Ilitokea hivi, msomaji mpenzi, ya kwamba muda mrefu haukupita tangu tangazo la fatwa ya sheikh huyu kutangazwa ila umaarufu wa Sheikh huyu ukaanza kupungua. Mpaka wakati huo, hakupita mtaa wowote mjini lahore, mji mkuu wa Panjab, ila watu walisimama kwa kumheshimu. Hata wasio Waislam. Mabaniani na wengine, walimheshimu sana wakiwaiga Waislamu. Kila alipokwenda alipokewa kwa heshima kuu. Kwa kuona heshima yake kwa watu, watu wakubwa katika nchi, watawala na hata Gavana Mkuu, walimpokea kwa taadhima. Baada ya kutangazwa fatwa hii kwa hali yoyote, bila ya sababu inayojulikana, heshima kubwa aliyoipata miongoni mwa watu wa kila daraja ikaanza kupungua. Upungufu huu uliendelea mpaka wafuasi wa madhehebu yake mwenyewe wakakata shuri kumwachilia mbali. hakuwa tena kiongozi kama alivyokuwa. Binafsi yangu nimepata kumwona katika

kituo cha gari moshi akibeba mzigo mzito akiwa na sanduku mikononi na nyingine mgongoni akipita katikati ya watu akisukumwa huku na huko. Watu wengine hawakujua alikuwa nani. Wafanya biashara na wenye maduka wote wakakataa kumwuzia chochote. Alipata mahitaji yake kwa wengine. Maisha yake ya myumbani pia yakawa machungu. Uhusiano na ukoo wake ukapungua. Mke wake akajitenga naye; baadhi ya watoto zake na wake zao wakakataa kumwona. Mmoja wao akaachilia mbali Uislamu. Siku zake zikawa za huzuni tupu. Alipoteza heshima yake yote na umaarufu, na akafa mwenye kudharauliwa, asiyekumbukwa. Mwisho wake ulikuwa ni thibitisho la aya:

"Sema: Safirini katika nchi, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wakadhibishaji" (6:12).

Mfano wa pili wa mwisho mbaya, uliowafikia maadui, ni ule wa Chirag Din wa Jammu. Mtu huyu mwanzoni alijihesabu kuwa mfuasi wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, lakini baadaye alidai kuwa ametumwa na Mungu. Alitangaza kwamba ameamriwa na Mwenyezi Mungu kuhuisha ulimwengu. Akapigisha chapa vijitabu na makala kumpinga Hadhrat Ahmad. Hakutosheka na haya, akaona afadhali aombe dua. Dua hiyo ikapigwa chapa na kutangazwa. Inasema:

"Ee, Mwenyezi Mungu, mtu huyu (yaani Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad), ni sababu ya machafuko mabaya sana katika Dini Yako. Anawatisha watu kwaba tauni imetokea kwa sababu yake na ya kwamba matetemeko ya ardhi ni matokeo ya kukadhibishwa kwake.

"Ee, Mwenyezi Mungu thibitisha uongo wake. Uondoe ugonjwa

watauni, ili kwamba uongo udhihirike na ukweli upate kupambanuka' (Kitabu cha Chiragh Din, kilichotajwa katika *Haqiqatul Wahyi*).

Dua hii ilipelekwa kwenye mtambo. Lakini jinsi mkono wa Mwenyezi Mungu ulivyomua ni vya mastaajabu. Dua hii ilikuwa imekwisha nakiliwa tu na mwandishi na ilikuwa bado haijafikishwa kwenye chumba cha kuchapia, hapo ugonjwa wa tauni ambao aliufahamu kuwa ulisemwa na Hadhrat Ahmad kuwa ni Ishara ya Mwenyezi Mungu, na ambao Sheikh huyu aliomba dua Mungu utoweke, uliwaangamiza yeye na jamaa yake nzima. Kwanza, wanawe wawili, ambao walikuwa ni haohao tu, walikufa. Halafu mkewe alimtoroka akiwa na bwana mwingine. Na mwisho yeye mwenyewe akashikwa na tauni na kuiaga dunia. Alipokuwa anakufa alisema, "Ee Mungu, hata mimi umeniacha."

Kifo cha Chiragh Din kilikuwa ni ushuhuda halisi kwamba uadui kwa watu wa Mwenyezi Mungu si jambo la kawaida. Mara tu uadui wa namna hii humwingiza mtu kwenye adhabu ya Mungu.

Wengine, mbali na Chiragh Din, waliomba dua ya mubahala (dua ya kuombea laana juu ya mwongo), nao pia wakaondolewa na Mwenyezi Mungu. Mmoja wao alikuwa ni Sheikh Ghulam Dastgir wa Kasur, Mwanachuoni wa chuo cha Hanafi na ambaye alikuwa mashuhuri sana katika Madhehebu yake. Yeye pia aliomba dua kuita adhabu ya Mungu juu ya mwongo. Mnamo miezi michache tu Sheikh huyu alikufa kwa ugonjwa wa tauni. Mwingine alikuwa Fakir Mirza wa Dulmiyal, Wilaya ya jehlum, ambaye alianza kutangaza kila mahala ya kwamba ameambiwa na Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. atakufa mnamo mwezi wa Ramadhani tarehe 27 mwaka 1321 A.H. Aliandika kwenye karatasi moja bishara hiyo na akaikabidhi wanachama wa Jumuiya yetu wa kijiji hicho. Ilikuwa na habari ya njozi na kudai kwamba kama Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad au Jumuiya yake haikukoma mnamo tarehe 27 Ramadhan mwaka 1321 A.H. atakuwa radhi kukubali adhabu yoyote ile. Dai hili lilishuhudiwa na idadi kubwa ya sahihi. Baada ya kusahihishwa ilionekana kwamba iliandikwa tarehe 7 ya Ramadhan. Tarehe 27 ya Ramadhan ikapita. Hakukutokea lolote. Wakweli hawakuogopa kujitapa kwa waongo. Lakini mwaka uliofuata mnamo mwezi wa Ramadhan, ugonjwa wa tauni uliingia Dulmiyal na kumwua mkewe.

Halafu yeye mwenyewe akaupata na ilikuwa mwaka mmoja kamili baada ya kutia sahihi, yaani tarehe 7 ya Ramadhan, mwaka 1322 A.H., alikufa kwa mateso mabaya sana. Baada ya siku chache binti yake pia akafa.

Mifano ya vifo vilivyoletwa na uadui hali ya kuwa Hukumu ya Mwenyezi Mungu ni mingi. Inafikia kwenye mamia na hata maelfu. Maelfu ya watu walishindwa katika majadiliano na kuchukia sana, waliomba dua Hadhrat Ahmad afe au afedheheke. Matokeo yalikuwa vifo vyao wenyewe na fedheha yao wenyewe. Sehemu ya ajabu katika jambo hili ni kwamba Mwenyezi Mungu alionesha ishara hii ya majonzi katika njia mbalimbali. Wale walioomba kifo kwa "mwongo" katika uhai wao walikuwa wenyewe katika uhai wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Wale waliosema kwamba umri mrefu haukuwa ishara ya mtu kuwa mkweli; ya kwamba kwa kweli, waongo waliishi umri mrefu, ya kwamba Musailama mwongo, aliishi umri mrefu baada ya Mtume s.a.w. na kadhalika, wao waliishi umri mrefu na walithibitishwa kuwa mifano ya kiroho ya huyo Musailama Mwongo.

Ishara ya aina hii ya pili ilioneshwa kwa Sheikh Sanaullah wa Amritsar, mhariri wa gazeti la Ahli Hadith. Sheikh huyu alikiuka mipaka yote. hadhrat Ahmad akifuata fundisho la Quran, alimwita Sheikh huyu kwenye mubahala. Aya ya Quran ikieleza njia hii ya kuomba hukumu ya Mwenyezi Mungu inasema:

> "Lakini atakayekuhoji katika hayo baada ya kukufikia elimu, basi sema: Njooni tuwaite watoto wetu, na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na watu wetu na watu wenu; kisha tuombe kwa unyenyekevu na kuiweka laana ya Mwenyezi Mungu juu ya waongo." (3:62)

Wito huu ulimwogofya Sheikh huyu. Njia zote zilishindwa kumshawishi akubali kuomba hukumu ya Mungu kwa namna hii. Hakukubali wito huu, lakini hakuacha uadui wake. Hapo Hadhrat

Mirza Ghulam Ahmad aliandika dua fulani na akamtaka Sheikh huyu kuinakili na kuitia katika gazeti lake la Ahali Hadith. Dua hii ilimwomba Mwenyezi Mungu kuhukumu baina yake na Sheikh juu ya mizani kwamba mwongo mwongo afe katika uhai wa mkweli. Hata hii haikumfanya Sheikh huyu akubali. Mara nyingi Sheikh huyu aliandika kwamba: "Hii sio mizani, na wala hawezi kuikubali." "Quran Tukufu," alisema, "ilifundisha mwongo aliishi umri mrefu." Kanuni ya Mungu ikathibitisha kauli hii hi. Musailama aliishi umri mrefu kuliko Mtukufu Mtume s.a.w." Basi Mwenyezi Mungu akamkamta Sheikh huyu kwa mizani yake mwenyewe. Akampa umri mrefu na kuishi baada ya kufariki Hadhrat Ahmad. Hivyo Sheikh huyu akathibitisha kuwa ishara ya Mwenyezi Mungu.

## MWISHO MBAYA

Katika njia mbalimbali maadui wa Masihi Aliyeahidiwa walikutana na mwisho mbaya sana. Wale waliosema kuwa mizani ni "umri mfupi kwa mwongo," walikufa katika uhai wake. Waliosema kwa la, bali mizani ni "umri mrefu kwa mwongo," wakaishi baada yake umri mrefu. Abu Jahal na Musailama, mifano hasa ya umri mfupi n umri mrefu kuhusu Mtume s.a.w., walioneshwa tena katika taarikh ya Masihi Aliyeahidiwa, ambaye alithibitishwa kuwa mkweli kama Bwana wake, mtume s.a.w. Shughuli ya Mwenyezi Mungu juu ya maadui wa Masihi Aliyeahidiwa ilichukuana na itikadi zao wenyewe. Sio tukio la ghafla, bali hukumu ya Mungu ilionekana imehakiki mwisho wa kila moja. Maadui za Masihi Masihi Aliyeahidiwa walifanyiwa njia mbalimbali. Walishuhudia adhabu za kila namna. Taabu walizoziona hazina kifani katika taarikh ya zamani. Kuelezea habari hizo kutachukua muda mrefu na sina nafasi ya kueleza zote. Mifano yake imeshuhudiwa na karibu watu wa kila nchi. Ugonjwa wa tauni, matetemeko ya ardhi, mafua makali, hofu ya vita, njaa, vita mbalimbali, zimetembelea sehemu mbalimbali za ulimwengu na kueneza maangamizi.

Maadui wengine mmoja mmoja wametaabika kwa njia nyingi za pekee kabisa. Kila mara adui aliupata mwisho wake kwa maradhi au msiba alioutaka umfikie Masihi Aliyeahidiwa. Kama mtu fulani alisema kuwa alikuwa anaumwa ukoma, basi ukoma ulimwua mwenyewe. Kama mtu alisema kuwa Masihi Aliyeahidiwa atakufa kwa ugonjwa wa tauni, basi tauni ilimwua mwenyewe mtakaji. Dr. Abdul hakim Khan wa Patiala akatabiri kwamba Hadhrat Ahmad atakufa kwa ugonjwa wa mapafu. Bwana tabibu huyu mwenyewe alikufa kwa ugonjwa huu. Inaweza kutajwa mifano mingi mamia kwa mamia. Uongo wowote uliotungwa juu ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ulimshika mtungaji mwenyewe Ishara za kutisha sana zilizooneshwa na Mwenyezi Mungu kwa kumthibitisha, ni lazima sana kuzifikiri kwa akili kunjufu. Uwezo na kiasi cha Mungu vikadhihirika katika ishara hizo; Ishara zilizooneshwa waziwazi kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s alikuwa mtumishi mkweli wa Mwenyezi Mungu. Msaada wa ajabu aliompa Mwenyezi Mungu na ambao bado anaendelea kumpa hauwezi kuwa na maana nyingine.

## HOJA YA NANE
## UTII WA MALAIKA

Tunafahamu kutoka katika Quran Tukufu kwamba Mwenyezi Mungu alimwumba Adam, na kuwaamuru Malaika kumtii. Njia ya kawaida ya kuonesha utii ni kusujudu. Lakini kusujudu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Kusujudia wengine, wawe wa juu vipi na wawe na nguvu namna gani, ni marufuku. Mtu hawezi kuwasujudia manabii, wala Mkuu wa Manabii, Muhammad Mustafa s.a.w. Sio tu kwamba ni marufuku kukisujudia chochote ghairi ya Mwenyezi Mungu, bali ni mojawapo ya madhambi makuu. Yeyote anayefanya hivi anapoteza radhi na rehema za Mwenyezi Mungu kwa ajili yake. Kwa hali yoyote, mtu anaweza kusujudu kwa maana nyingine; katika maana hii kusujudu si tendo la ibada.

Haiwezi kusemwa kwamba kusujudu mbele ya vitu ghairi ya Mwenyezi Mungu kuliruhusiwa zamani zama taifa la wanadamu lilikuwa bado changa, na ya kwamba kukaa kutangzwa zama lilipopea. Jambo la maana hii ni kosa. Sijda ya namna hii ni namna fulani ya shirk. Matendo ya shirk hayakuweza kuruhusiwa wakati wowote: Mwenyezi Mungu ni Mmoja na Umoja Wake ni msingi wa imani. Kama ikisemwa kwamba kusujudia watu wengine ghairi ya Mwenyezi Mungu kuliruhusiwa hapo kwanza, lakini kulikatazwa baadaye, kwa kuwa ni aina ya shirk, basi Shetani atakuwa na sababu upande wake. Shetani alikataa kumsujudia Adam. Hii inaweza kuwa kumkosea Mungu wakati ule, lakini baadaye hata Mungu mwenyewe alikataza kusujidiwa mwanadamu, au viumbe vyovyote ghairi ya Mwenyezi Mungu.

## MALAIKA WAMSUJUDIAPO MWANADAMU

Sijda kwa viumbe haiwezi kuwa ni sawa. malaika walipoamriwa na Mwenyezi Mungu kumsujudia mwanadamu, sijda haikuwa tendo la ibada. Sijda hii ina maana nyingine. katika lugha ya Kirabu sijda maana yake ni utii kamili. Sijda inaweza kuwa ibada au utii. Katika *Lisanul-Arab,* Kitabu cha nne, chini ya Sajada mmeandikwa:

"Anayeonesha utii kamili na kusalimu amri anaweza kusemwa kuwa amesujudu."

Amri iliyotolewa kwa Malaika kumsujudia Adam haikuwa amri ya kumwabudu Adam, bali amri ya kumtii. Kumtii mtu ilikuwa kumsaidia katika mipango yake na juhudi yake. Amri kwa Malaika kumsaidia Adam inarudiwa katika wakati wa kila nabii na mtu anayedai unabi, ni lazima atazamie na apate msaada wa Malaika. Ni lazima apate msaada huo kwa sababu ameamriwa na Mwenyezi Mungu kufanya kazi hiyo.

Katika maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w. mnaweza kutajwa matukio yanayoonesha jinsi Mtume s.a.w. alivyopata msaada wa

Malaika katika mipango yake na maazimio. Mfano mmoja ni katika vita ya Badri. Katika vita hii Malaika waliwaogofya sana maadui kwa hofu isiyo na kiasi. Mtume s.a.w. alizoa gao moja la mchanga kuwatupia maadui, na hapo ukavuma upepo mkali sana. Mfano mwingine ulishuhudiwa katika vita ya Khandak. Waislamu walizungukwa na maadui kila upande. Maadui ilikuwa washinde lakini kwa sababu ya moto uliowashwa na mkuu wa mmoja ulizimwa na upepo, madui waliona hofu sana katika kambi yao. Bado mfano mwingine ni kuiepuka kwake kimwujiza sumu ambayo mwanamke mmoja Myahudi alitaka kumpa Mtume s.a.w.

Kwa kawaida msaada wa Malaika huja katika matukio ya asili. Sharti za kwanza na sababu za matukio yote ya asili ni Malaika. Zama nabii anapokutana na maadui na taabu inatokea, Malaika wanashughulika kugeuza mambo ya asili kumsaidia Nabii. Licha ya kukosekana njia za kawaida lakini Mtume s.a.w. alipata ushindi juu ya maadui zake. Ushindi unaokuja hivi ni ushuhuda wa ukweli wa nabii.

Halkadhalika msaada wa Malaika ulimfikia Masihi Aliyeahidiwa. Alishuhudia msaada wao. Malaika walimsaidia katika kila aina ya taabu; waliongoza kanuni ya asili kumpendelea. Hapa nitataja mfano maarufu sana. Safari moja Masihi Aliyeahidiwa pamoja na jamaa wengine, miongoni mwao wakiwa Mabaniani, Waislamu na watu wa dini zingine, walikuwa wamelala chini ya dari moja. Kwa ghafla aliamka na akaona dari ile ilikuwa karibu kuporomoka. Kulikuwa hakuma alama zozote za nje kuonesha kuwa dari ingenguka. Bali kijisauti kidogo, labda kijisauti cha mchwa, ndicho kilichoweza kusikilia. Masihi Aliyeahidiwa aliwaamsha wenzake na kuwaambia watoke nje. Jamaa hao hawakujali shauri lake na wakarudia kulala. Walisema kuwa Hadhrat Ahmad alikosea kwani kulikuwa hakuna hatari yoyote. Baada ya muda kidogo, tena Hadhrat Ahmad aliona kuwa dari litaanguka. Akawaamsha tena jamaa; safari hii alisisitiza kabisa kuwa watoke nje. Jamaa walikubali, lakini sio bila ya kunung'unika. Walisema kuwa Hadhrat Ahmad alitaka watoke nje vile kwa sababu ya mawazo tu. Kwa upande mwingine Hadhrat Ahmad aliona ya kuwa kuanguka kwa dari kulimngoja yeye atoke. Alimwacha kila mmoja atoke nje

kwanza. Baada ya kutoka kila mtu, alitoa mguu wa kwanza nje na alipomaliza wa pili tu dari likaporomoka chini. Wote walijawa na mshangao na wakamshukuru sana Hadhrat Ahmad kwa kuokoa maisha yao.

## ALIPOUGUA SANA

Mara nyingi ilitokea hivi ya kwamba alipokuwa mgonjwa sana, aliambiwa njia za matibabu. Dawa iliweza kutokea katika ndoto, pengine katika *Kashaf*. Kudhihirika kwake ni katika tendo la Malaika. Safari moja Masihi Aliyeahidiwa aliugua sana. Alitumia dawa fulani lakini hazikumfaa kitu halafu kitu kilijionesha mbele yake na kusema "mimi peremende" Peremende ikawa ndiyo dawa na ugonjwa ukakoma. Pengine ilitokea hivi ya kwamba mtu fulani alikuja kumwua. Mara nyingi kuja kwa mtu namna hii alikufahamu mbele kwa njia ya ufunuo. Au, Malaika walimwogofya mtu huyo, kama katika vita ya Badr. Wauaji waligeuka kuwa wafuasi. Jiha ya Masihi Aliyeahidiwa iliwavuta; na wakaamua kujiunga naye badala ya kumwua - Matukio yanayotukumbusha kusilimu kwa Hadhrat Umar aliyesilimu wakati wa jitihada ya kumwua Mtume s.a.w.

## ALISAIDIWA NA MALAIKA

Ishara kubwa kabisa ya kusaidiwa na Malaika ilitokea wakati wa kutokea kwa ugonjwa watauni ambao ulianzia sehemu ileile aliyoishi Masihi Aliyeahidiwa. Ninayo mengi zaidi ya kueleza juu ya madhumuni hii. Hapa ninapenda kusema kwamba ugonjwa wa tauni alioneshwa katika ndoto kwa sura ya tembo anayeshambulia huko na huko ardhini. Katika hali hii, mnyama huyu alionekana katika ndoto yenye kuonya kuwa tauni itatokea akiwa mpole na mwenye adabu sana mbele ya Masihi Aliyeahidiwa. Ndoto hii

ilionesha kuwa tauni haitamdhuru Masihi Aliyeahidiwa. Malaika wa Mwenyezi Mungu ilikuwa waangalie jambo hili. Kwa ahadi hii ya msaada wa Malaika, Masihi Aliyeahidiwa alipata ufunuo mwingine. Mmoja unasema: "Moto ni mtumwa wetu, la, bali mtumwa wa watumwa." Baada ya kupokea ufunuo wa namna hii alitangaza kuwa yeye na wafuasi wake watasalimika katika maangamizi ya tauni. Mtu mmoja mmoja anaweza kuupata lakini hilo halitabatilisha ukweli wa ahadi hii; hata zama za Mtume s.a.w. Waislamu walikufa katika mapambano na maadui, lakini maadui walikufa wengi zaidi.

Kadhalika alitangaza ya kuwa mji wa Qadian hautashambuliwa na tauni kama itakavyoshambuliwa miji mingine na sehemu zingine; ya kwamba katika Qadian ugonjwa hautatisha zaidi kama katika miji na sehemu zingine na ya kwamba nyumba yake itasalimika kabisa bila kuguswa hata kidogo na ugonjwa wa tauni. Hakuna hata mmoja wa nyumbani mwake atakayeshikwa na tauni. Bada ya matangazo haya ugonjwa wa tauni ukadhihiri katika Bara Hindi na ukashambulia kikweli. Kila mwaka mamia ya maelfu ya watu wakafa kwa ugonjwa wa tauni, wafuasi wake walisalimika katika hilaki ya ugonjwa huu. Hili liliendelea kwa miaka kadhaa. Watu wengi walivutwa. Maelfu wakaingia ndani ya Jumuiya. Kwa kweli idadi kubwa ya wafuasi wake wakati ule ilikuwa ni matokeo ya ishara hii.

Zama tauni iliposhambulia nchi hii, iliua maadui zake wengi. Namna maadui mashuhuri walivyoshikwa na tauni imeisha elezwa tayari. Wafuasi wake walisalimika; isipokuwa athari ya kupita tu ya tauni iliwapata wachache kati yao. Ulinzi alioupata yeye na wafuasi wake katika hilaki ya tauni ni ishara waziwazi ya Mwenyezi Mungu. Hilaki ya namna hii ilikuwa haijatokea hapo kabla Ilitokea baada ya kutangaza njozi zake za taabiri ya ugonjwa wa hilaki hiyo. Ugonjwa huu ulimwacha yeye na wafuasi wake. Usalama huu wake yeye na wafuasi wake ulithibitisha ukweli wa ufunuo wake, "Moto ni mtumwa wetu, la, bali mtumwa wa watumwa." Malaika walitimiza ahadi hii. Wadudu wa tauni walimpendelea na kuonesha utii ambao ndio wajibu wao kwa kila Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Tauni ilifika Qadian kama ilivyofika mahala pengine. Lakini haikukaa Qadian kwa muda mrefu. Iliondoka baada ya miaka mitatu.

Katika sehemu zingine ilikaa muda mrefu mpaka kufikia miaka kumi hata zaidi.

## WATU WA NYUMBANI MWAKE WALIHIFADHIWA

Jinsi watu wa nyumbani mwa Masihi Aliyeahidiwa walivyosalimika katika ugonjwa wa tauni ni ushuhuda usiobishika wa utii wa Malaika. Maradhi na vifo vya tauni vilitokea nyumba ya pili. Ugonjwa uliendelea kukaa katika nyumba hiyo kwa miaka mitatu. Nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa ilijaa watu zaidi kuliko mia moja, na ilikuwa mahala penye bonde pasipo afya. Lakini hakukuwa na aliyekufa humo kwa ugonjwa wa tauni. Hata panya. Inajulikana kwamba ugonjwa huu unapoingia mahala, wa kwanza kabisa kuupata ni panya. Hii ni ishara ya ajabu ambayo inaweza kuwavuta wenye kufikiri. Kama hawakuwa Malaika walioshuhgulika kumsaidia, kilikuwa nini basi? Ni kipi kilicholeta tofauti hii ya ajabu? Wafalme na watawala na watu wenye nguvu hawakuweza kumiliki majeshi na nguvu zilizomsaidia. kanuni za asili zilionekana zimegeuza njia zake za kawaida na kujitolea kwa ajili yake. Matabibu ambao walikuwa na dawa za kujikinga, wakafa kwa tauni. Wale walioishi katika kambi zenye wasaa na afya, mbali, nje ya mji hawakuweza kuukwepa. Wale ambao walipiga sindano kuuzuia, wakahiliki. Nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa haikuwa ndogo. Ilikuwa kubwa kama ilivyokuwa, lakini ilikuwa kubwa vile kwa sababu ya wageni wengi waliokuja kujihifadhi wasishambuliwe na tauni.

Kama tauni haikuwa imefika Qadian; au kama baada ya kufika Qadian haikushambulia nyumba za jirani, ingeweza kusemwa kwamba huu, ambao yeye, ahli zake, na watu wa nyumbani mwake waliupata ulikuwa ni bahati tu. Lakini alitangaza jambo hili kabla, alivyopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Baada ya kutangazwa kwake Malaika walishughulikia bishara hii. Tauni ikafika Qadian, lakini ilikuja kama mtumwa. Ilifanya kazi yake, lakini katika mipaka

maalum, kama kwamba ilikuwa chini ya uangalizi wa mtu fulani. Ilifika mjini, ikawashika jirani zake wa karibu kabisa, lakini haikumgusa yeyote wa nyumbani mwake. Hata panya! Huu ni ushuhuda wa utii wa Malaika juu yake. Waliambiwa wamtii na wakatekeleze kazi yao hii kwa uaminifu. Waliteuliwa kumlinda. Nguvu za asili zilitiwa utumwani kwa ajili yake.

Kujitolea kwa nguvu za tabia kwa ajili yake kunathibitishwa na matukio mengine mengi. Lakini ninatumaini mifano niliyoitaja itatosha, na ya kwamba itatoa fununu fulani juu ya ulinzi wa kimwujiza alioupata Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Masimulizi ya mifano hii yanafaa kufafanua kwamba msaada wa ulinzi wa namna hii hangeweza kupata mdanganyifu na mwongo.

## HOJA YA TISA
## ZAWADI YA ELIMU MAALUM

Hoja ya tisa, ambayo pia ina hoja nyimgi ndogondogo, inahusu kipawa cha elimu maalum. Kuja kwa manabii kunatimiza haja moja kubwa, nayo ni kuwaongoza wanadamu katika misingi ambayo minghairi ya hiyo hawawezi kuwa na maisha ya kiroho. manabii huja na kuwaongoza wanadamu kwenye chemchem ya elimu ya kiroho; ili waweze kuizima kiu yao ya kiroho. Sasa basi, asili ya maisha yote ya kiroho ni Mungu Mmoja, Mwenye Enzi. Manabii huja na kuweka maungano baina ya mwanadamu na Mola wao. Na matokeo yake yanakuja katika elimu ya mambo ya kiroho. Elimu hii inaleta ukaribu na Mwenyezi Mungu na kujua Dhati Yake na Sifa Zake. Yule ambaye anaweza kuigawanya elimu hii kwa wanadamu wote, ni lazima yeye mwenyewe awe na nyingi zaidi.

## MANABII WALIJAALIWA ELIMU MAALUMU

Anayedai unabii, hawezi kuyathibitisha madai yake mpaka yeye mwenyewe awe na elimu nyingi sana ya kiroho, na Mwenyezi Mungu awe ndiye ampaye elimu hii na kumwongoza. Kwa hiyo ili kupima madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, tunaweza kushika mizani ya elimu maalumu. Tunaweza kuona ni nyingi kiasi gani elimu aliyozawadiwa na Mwenyezi Mungu. Anasema Mwenyezi Mungu katika Quran:

"Na Akamfundisha Adam Majina (Yake) yote, kisha Akawaweka (wanaoyadhihirisha) mbele ya Malaika, ana Akasema: Niambieni majina ya hawa ikiwa mnasema kweli" (2:32).

Majina hapa maana yake ni sifa za Mwenyezi Mungu. Elimu ya sifa hizi na elimu ya mambo yote. Elimu ya Mungu ni elimu ya sifa za kiungu, ambayo inakuja kwa mazoea na ushuhuda. Lakini anayechaguliwa na Mwenyezi Mungu hujaaliwa elimu hii na Mungu Mwenyewe. Tunasoma juu ya Nabii Lut a.s.

"Na Luti Tukampa hukumu na elimu" (21:75)

Na juu ya Daudi na Sueliman tunasoma:

"Na bila shaka Tuliwapa Daudi na Suleiman elimu" (27:16)

Na juu ya Yusuf:

"Na (Yusufu) alipofika balehe yake Tukampa hukumu na elimu (12:23).

Na Juu ya Musa:

Na (Musa) alipofika balehe yake na akastawi, Tukampa hukumu na elimu na hivi ndivyo Tuwalipavyo wafanyao mema" (28:15).

Juu ya Mtume s.a.w. tunasoma:

"Na Amekufundisha yale uliyokuwa huyajui; na fadhila za Mwenyezi
Mungu zilizo juu yako ni kuwa"(4:114).

Manabii wote, na wote wanaopewa kazi na Mwenyezi Mungu, hubarikiwa kwa zawadi ya elimu maalumu. Mtume s.a.w. sio tu kwamba alizawadiwa elimu hii; bali aliahidiwa elimu zaidi na zaidi. Akafundishwa dua hii:

"Na uombe: Mola wangu, nizidishie elimu" (20:115).

Hivyo basi, mojawapo ya zawadi maalumu ambazo kila Mjumbe wa Mungu hupokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni zawadi ya elimu maalumu. Elimu hii aligawiwa Masihi Aliyeahidiwa. Tofauti kati Ya Masihi Aliyeahidiwa na Wajumbe wengine ni kwamba Masihi Aliyeahidiwa alipata baraka maalumu kufikia kwenye kilele cha elimu. Hii ni kwa sababu ya mapenzi yake kwa Bwana wake, Mtume wa Islam s.a.w. Alipata zawadi hii kwa kumwiga Mtume s.a.w. Baraka maalumu ilimjaalia Masihi Aliyeahidiwa kima (kiwango) maalumu cha elimu ya nje na ndani pia. Sio tu kwamba alizawadiwa elimu ya kiroho, bali alijaaliwa pia kipaji cha kuieleza. Aliwaita maadui zake kwenye mashindano. Elimu na kipaji cha kueleza mambo ilikuwa ni zawadi yake ya kiungu.

## QURAN TUKUFU NI MWUJIZA WA AJABU

Katika mawili, ninaendelea kulieleza la pili, kipaji cha kueleza elimu. Kwa kutoa mfano wake nitataja mwujiza wa lugha, urithi wa kiroho aliomrithi Bwana wake, Mtume Muhammad s.a.w. Mwujiza huu haukupewa manabii wa zamani. Ulikuwa ni Quran Tukufu ambayo kwayo dai lake la pekee lilitolewa mwanzoni:

"Na ikiwa mna shaka kwa hayo Tuliyomteremshia Mtumishi Wetu, basi leteni sura iliyo mfano wa hii, na mwaite wasaidizi wenu ghairi ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli" (2:24).

Wito huu wa Quran unadai thamani ya pekee ya lugha na maneno ya Quran Tukufu. Wito huu umefuatana na onyo kwamba wakadhibishao Quran hawataweza asilan kuleta chochote mfano wake. Thamani ya Quran ambayo kwayo wito huu unatolewa ina vyote, mafundisho yake na mtindo, kwa ufupi wito huu umetolewa kwa wote. Hebu wote walinganishe maandiko yao na Quran Tukufu. Sehemu moja tunasoma:

"Kitabu ambacho Aya Zake zinalindwa, kisha zinaelezwa kimetoka kwa Mwenye hekima, Mwenye habari" (11:2).

Madokezi mawili mapana yamo katika sifa za hekima na utambuzi. Mungu Mwenye hekima anaweza kufunua kitabu chenye hekima nyingi. Mwenyezi Mungu Mtambuzi sana alitambua kwamba dunia ilikuwa ikiingia katika duara la maendeleo makubwa ya akili. Kwa hiyo, miujiza ya akili ilikuwa lazima ioneshwe ili kuuhakikishia ulimwengu juu ya Hekima na Elimu ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivi, Mwenyezi Mungu akaifanya Quran Tukufu kwa mwujiza wa elimu kamilifu na maneno kamilifu. Quran haitoi madai tu, bali inajieleza pia. Ni shahidi ya yenyewe.

Masihi Aliyeahidiwa alikuwa mwanafunzi na kivuli cha Mtume s.a.w. Kwa hiyo, zawadi za masihi Aliyeahidiwa zilikuwa ni kivuli cha zawadi za Bwana wake. Nuru yake ilikuwa iliyozimwa. Kwa hiyo, Masihi Aliyeahidiwa aliweza kuonesha mwujiza wa ufasaha wa lugha. Hakufika chuoni. Alikuwa na waalimu wa nyumbani wenye ujuzi haba tu wa kawaida. Alijifunza sehemu chache tu za maandiko kutoka kwao. Hakupata kufika nchi za Bara Arabu. Wala hakuishi katika miji ambamo Kiarabu kilisemwa. Aliishi kijijini na

mapato yake yalikuwa haba. Masomo yake hayakuzidi kawaida ya watu wengine.

## ALIANDIKA VITABU KWA KIARABU

Alipotangaza madai yake na kuanza kazi ya islahi, maadui zake kwanza walishambulia kukosa kwake elimu. Walimweleza kuwa ni Munshi, yaani mtu mwenye elimu haba ya lugha ya Kiarabu. Wakasema likuwa amesoma kidogo, hivyo aliweza kuandika. Ya kwamba baadhi ya maandiko yake yalikuwa ya kuvutia; ndiyo sababu akadhani amekuwa na sifa. hakuwa mwanachuoni, hakujua lugha ya Kiarabu, wala hakuwa na haki ya kufutu mas'ala za dini. Shutuma hizi zilitolewa katika kila mazungumzo na maandiko ya uadui. Kwa hali yoyote haikuwa kweli kusema kwamba hakujua Kiarabu. Alikuwa amesoma vitabu vya Kiarabu. Lakini kwa kweli hakunufaika na uongozi wa mwanachuoni mkubwa yeyote. Hakupata hati yoyote katika chuo maalumu cha zamani. Hakuwa miongoni mwa viongozi, Maulamaa wala Masheikh wa daraja yoyote. Zama shutuma hizi zilipoenea sana, na Masheikh wakaanza kuzibwata nje na ndani ya kila majira, Mwenyezi Mungu alimjaalia elimu maalumu ya lugha ya Kiarabu. Alisema ya kuwa Mwenyezi Mungu alimfundisha maneno 40,000 mnamo usiku mmoja. Alijaaliwa ustadi kamili wa lugha ya Kiarabu, aliamriwa kuandika vitabu vya Kiarabu na kuahidiwa msaada maalumu. Kazi yake ya kwanza ya Kiarabu ilikuwa ni wito aliouandika ndani ya Kitabu chake *Ainai-Kamaalaati Islam*. Wito huu aliwaita wale waliomshutumu kwa kutojua kwake Kiarabu. Aliwataka walete kilicho bora. Hakuna aliyekubali wito huu. Halafu akaandika kitabu baada ya kitabu katika lugha ya Kiarabu. Idadi ya vitabu vyake vya Kiarabu ni zaidi ya ishirini. Baadhi yao vilikuwa na tangazo la zawadi ya rupia 10,000. Zawadi hii hata sasa anaweza kuipata yeyote atakayeleta kitabu chenye ufasaha wa lugha ya Kiarabu zaidi ya Kitabu cha Masihi Aliyeahidiwa. Hakuna aliyepokea wito huu. Hakuna aliyetoa lolote kujibu. Baadhi ya vitabu vyake vilikuwa na

wito kwa Waarabu. Hata wao walishindwa kuandika chochote; hivyo waliukwepa wito. Mojawapo ya vitabu vyake alikiandika kwa Seyyid Rashid Riza, mhariri maarufu wa gazeti la *Al Manaar.* Seyyid huyo aliombwa kutoa jawabu lakini hakutoa lolote. Waarabu wengine vilevile waliombwa hata wao hawakuthubutu.

Masheikh katika Bara Hindi walionesha kushindwa aliposema ya kuwa vitabu vya Kiarabu vinavyosemwa viliandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kwa kweli viliandikwa na Waarabu aliowaficha kwa kazi hii. Shutuma hizi zilionesha waziwazi kuwa thamani ya vitabu vyake ilikuwa ya juu sana. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alipambana na shutuma hizo kwa kusema washindani wake wanaweza kusaidiwa na waandishi wa Bara Arab na Shamu wengi kadiri wawezavyo kuwapata. Jitihada hii na hii ilifanywa kuwashawishi waingie shindano hili lakini hakuna aliyekuja mbele. Mapaka leo hivi hakuna jawabu lililotolewa.

## HOTUBA YA UFUNUO

Mbali na vitabu vyake vya Kiarabu, alitoa hotuba ya ghafla katika lugha ya Kiarabu. Aliamriwa katika ufunuo kujaribu, ingawa alikuwa hajapata kutoa hotuba katika lugha ya Kiarabu. Id-ul-Adh'ha ilikuwa siku ya pili yake. Kwa kutekeleza amri ya ufunuo alitoa hotba ndefu kwa Kiarabu baada ya sala ya Idi. Hotuba hii baadaye ilipigishwa chapa kwa anuani *Khutba ilhamiyya* (Hotuba ya ufunuo). Hotuba hii ina Kiarabu kikavu sana. Inawaathiri waandishi wa Kiarabu na wasi Waarabu na ndani yake yameelezwa maajabu ya lugha na mambo ya siri ya kiroho yanayokuza thamani yake.

Mwujiza huu wa elimu ni mojawapo ya miujiza yake mikubwa. Baadhi ya miujiza inavutia sana lakini kwa muda ule tu wa kushuhudiwa kwao. Mingine ina mvuto unaoishi kwa muda mrefu sana. Ukweli wa mwujiza huu umeshuhudiwa na kukubaliwa na hata maadui. Mwujiza huu unaiga mwujiza wa Quran Tukufu. Quran Tukufu inabakia bila kifani. na ndivyo itakavyokuwa kwa vitabu vya Kiarabu vya Masihi Aliyehidiwa. Ishara hii ya ukweli wake

itakuwa hoja juu ya maadui na itabakia yenye kung'aa milele.

Wengine ambao wanashangazwa na mwujiza huu, wanatoa hoja kwamba dai la kuonesha mwujiza wa lugha ni tusi kwa Quran Tukufu; ati kwani ni Quran ilidai kwanza kuwa na thamani isiyo kifani. Na kwamba kusema kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alizawadiwa milki ya lugha kimwujiza, ati ni kudaia maandiko yake kuwa sawa na Quran Tukufu. Hoja hii ni ya husuda. Kufikiri kidogo tu kutamfahamisha mtu yeyote kwamba thamani ya maandiko ya kimwujiza ya Masihi Aliyeahidiwa haipunguzi chochote katika thamani ya kimwujiza ya Quran Tukufu. Bali kwa maandiko hayo thamani ya Quran Tukufu inazidi.

Thamani ni za namna mbili, ya pekee na ya uhusiano. Thamani ya pekee inajitegemea yenyewe. haina hoja ya malinganisho na mifano mingine ya thamani. Thamani ya uhusiano ni thamani ya kulinganishwa na zingine. Wazo hili la thamani ya pekee na uhusiano inaweza kuoneshwa kutokana na Quran Tukufu. Inasema (kuwaambia wana wa Israeli):

"Na Nikawapa heshima kuliko viumbe wengine" (2;48).

Kuwaambia Waislamu Quran imetumia mtindo huohuo wa maneno:

"Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu" (3:111).

Quran Tukufu inawaeleza Waisraeli na Waislamu kuwa wabora wa walimwengu wote. Kwa nje, kuna upingamizi lakini tukichunguza kwa makini tutaona hakuna upinzani wowote. Hali iliyoelezwa kwa ajili ya Waisraeli inahusu wakati fulani maalumu tu; yaani wakati ambao hali ile ilitumiwa. Hali iliyotumiwa kwa ajili ya Waislamu inahusu wakati wote, uliopita, uliopo na ujao. Vilevile upekee na thamani ya kimwujiza ya maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa ni lazima ieleweke katika hali ya uhusiano, uhusiano na maandiko mengine ya wanadamu. Lakini thamani ya Quran Tukufu ni ya pekee. Imepita maandiko yoyote yale ya wanadamu

na vitabu vingine vilivyofunuliwa na Mungu. Maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa pamoja na Hotuba yake ya ufunuo, yana thamani ya uhusiano tu ambapo thamani ya Quran ni ya upekee halisi. Kwa hiyo, mwujiza wa lugha aliouonesha Masihi Aliyeahidiwa a.s., haupunguzi na hauwezi kupunguza chochote katika thamani ya kimwujiza ya Quran Tukufu.

## KIARABU CHA MASIHI KILITHIBITISHA UPEKEE WA QURAN

Kwa hali yoyote, nilisema kuwa maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa yamezidisha thamani ya mwujiza wa Quran Tukufu. Hili linaweza kuelezwa ifuatavyo. Upekee peke yake ni wa namna mbalimbali. Aina moja ya upekee ni duni. Mandiko yanaweza kuwa ya pekee miongoni mwa maandiko yote maarufu lakini tofauti ya thamani kati ya hayo na mengine yanaweza kuwa si kubwa sana. Maandiko mengine yanaweza kuwa duni, lakini yasiwe duni sana kwayo. Katika mashindano ya mbio mtu wa kwanza anaweza kushinda hata kama tofauti baina yake na wa pili ni inchi chache tu. Tofauti ingeweza kuwa kubwa. Ingeweza kuwa tofauti ta dhiraa moja au kadhaa. Namna hii maandiko ya pekee yanaweza kuwa na fadhila juu ya maandiko mengine kwa daraja ndogo au kwa daraja kubwa sana. Maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa ni kati ya Quran na maandiko mengine. Kama yanapatikana maandiko yaliyo na fadhila juu ya maandiko ya wanadamu, lakini ni duni kwa Quran Tukufu, yataonesha tu ni fadhila iliyoje ya thamani ya Quran Tukufu. kwa hiyo, maandiko ya Hadhrat Ahmad a.s. yameongeza thamani ya Quran Tukufu. Maandiko yaliyofanywa ni sawa na Quran, sasa yameonekana duni hata kwa maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa. Na hili linapandisha zaidi thamani ya Quran Tukufu. Mwujiza wa Masihi Aliyeahidiwa ni duni ya mwujiza wa asili. Unasaidia tu kudhihirisha upekee wa mwujiza wa asili. Unathibitisha zaidi kuliko kwanza kuwa ni marefu kiasi gani masafa baina ya Quran na vitabu vingine.

# KIARABU NDIO MAMA YA LUGHA ZOTE

Mbali na zawadi ya kumiliki lugha ya Kiarabu ambayo Masihi Aliyeahidiwa alijaaliwa na Mwenyezi Mungu, alifunuliwa pia undani wa hali ya pekee ya lugha ya Kiarabu. Undani huo ni kwamba Kiarabu ni mama ya lugha zote. Huu ulikuwa uvumbuzi mkubwa na wa kustaajabisha. Wanazuoni wa kimagharibi, baada ya uchunguzi wa bidii saba, waliona kuwa ama *Sankrit* au *Pahlavi,* ndiyo mama ya lugha zote. Baadhi yao walifikiri kuwa lugha ya asili ilitoweka kabisa na ya kwamba lugha zilizojulikana mwanzoni, *Sankrit* na *Pahlavi,* zilikuwa ni matawi tu ya lugha hiyo. Hii ndiyo ilikuwa hali ya wachunguzi wa Kimagharibi. Wanazuoni wa Kiarabu hawakutambua upekee wa lugha yao. Hata wao, kama wanazuoni wa Magharibi, walitafuta lugha ya asili hasa miongoni mwa lugha isiyokuwa yao. Zama wanazuoni wakitafuta lugha ya asili ya mwanadamu, Masihi Aliyeahidiwa alipata ufunuo juu ya jambo hili. Aliambiwa kuwa lugha ya Kiarabu ndiyo mama ya lugha zote. Ulikuwa uvumbuzi wa ajabu. Kwa hali yoyote, kwa kuifikiria Quran Tukufu, mara ilibainika kuwa uvumbuzi huu ulihusiana na fundisho la Quran Tukufu; na hii ni kwa sababu moja nzuri. Quran ni ufunuo kwa ajili ya ulimwengu mzima. Ilivyopasa ni kwamba lugha ya ufunuo huu ingekuwa iwe lugha ya watu wote. Ni lugha ya kwanza tu, asili ya lugha ndogo ndogo zote zilizojitokeza kutokana nayo, ingeweza kusemwa kuwa lugha ya wanadamu wote. Quran inafundisha kwamba nabii anaambiwa maneno na Mungu kwa lugha ya wale waliotumwa afikishe maneno hayo:

"Na Hatukumtuma Mtume yeyote isipokuwa kwa lugha ya watu wake" (14:5).

Mtume s.a.w. alikuwa Nabii kwa wanadamu wote. Hivyo ilistahili mwongozo aliofunuliwa na Mungu uwe katika lugha ya kiulimwengu mazima. Ni lugha ya kwanza tu aliyozungumza mwanadamu ndiyo inaweza kusemwa kuwa lugha ya wanadamu. Na kwa kuwa ufunuo ulimshukia Mtume s.a.w. kwa lugha ya

Kiarabu, basi Kiarabu ni lazima kiwe ndiyo lugha ya kwanza ya wanadamu, mama ya lugha zote.

Kwa kuthibitisha uvumbuzi huu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kwa fadhili maalumu ya Mwenyezi Mungu, alieleza misingi ambayo kwayo lugha ya asili inaweza kupambanuka katika lugha za matawi. Kwa misingi hii aliweza kusema kwamba Kiarabu ndiyo lugha iliyo mama ya lugha zote, lugha iliyofunuliwa na Mwenyezi Mungu kwa wanadamu, lugha ambayo kwayo lugha zote za duniani zilikua kama matawi kwenye shina. Hakuna lugha nyingine inayoweza kutoa sifa za kuwa lugha ya asili. Hadhrat Ahmad akaazimia kuandika kitabu juu ya madhumni hii. Kitabu hiki hakikuwahi kuisha. Hata hivyo, kina maelezo ya masingi ambayo inaweza kuandikwa kwa urefu na madhumuni yote ikaelezwa kwa njia nzuri. Nimeazimia, Inshallah, kuandika kwa misingi mikubwa na madokezi ambayo Masihi Aliyeahidiwa hakuyamaliza, na kuandika kwa taratibu nzuri asili za lugha mbalimbali. Katika maelezo yangu nitapenda kutoa ushuhuda mpana wa Masihi Aliyeahidiwa. Vilevile nitapenda kutumia, baada ya kuisahihisha, misingi iliyotumiwa na wanazuoni wa Magharibi juu ya elimu ya lugha. "Na hakuna msaada ila utokao kwa Mwenyezi Mungu" Hata hivyo, uvumbuzi huu utabakia usio kifani katika taarikh ya elimu za Kiarabu na utaacha athari katika sura mpya ya Islam ambayo dunia inaelekea kuishika katika siku zijazo. Uvumbuzi huu utaongeza nguvu ya Islam.

Mbali na zawadi hizi za kielimu ambazo Masihi Aliyeahidiwa alizipokea kwa wingi kutoka kwa Mwenyezi, vilevile alipata zawadi za kiroho ambazo ni haki maalum ya Manabii. Aliwaita watu wapime nguvu zao za akili na nguvu zake alizopewa na Mungu. Lakini hakuna yeyote aliyekubali wito huo. Kama nilivyokwisha sema Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad hakuwa mwalimu wa dini yoyote mpya wala sheria mpya. Kwa kutimiza bishara za zamani amkuja kuitumikia tu na kuitangaza Dini ya Mtume Muhammad s.a.w. Kufafanua na kueneza duniani elimu ya Quran Tukufu ndiyo ilikuwa kazi yake. Baada ya Quran Tukufu hakuna elimu nyingine ya kiroho inayoweza kushuka kutoka mbinguni. Elimu zote ambazo mwanadamu anazihitaji kwa ajili ya maendeleo yake ya tabia na roho zimo katika hiki, Kitabu cha Mwisho cha Mwenyezi Mungu.

Baada ya Mtume s.a.w. hakuwezi kuwa na mwalimu yeyote wala mwongozi kwa wanadamu. Yeyote atakayeinuka kufundisha na kuongoza, ni lazima afundishe elimu ileile iliyokwisha gawiwa na Mtume s.a.w. Mwalimu kama huyo anaweza kuwa mhuishaji wa hazina zilizosahauliwa. Hakuna zaidi. Kazi yake ni kujadidisha, sio kuunda. Ufunuo mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa unasema:

"Kila baraka zinatoka kwa Muhammad, rehema na amani iwe juu yake. Basi, amebarikiwa afundishaye na anayefundishwa."

Ufunuo huu unaeleza uhusiano baina ya Mtume s.a.w. na Masihi Aliyeahidiwa, Bwana na Mtumishi.

## ALIGUNDUA SIRI ZA QURAN

Kwa kuwa neno la mwisho juu ya maendeleo ya kiroho limesemwa ndani ya Quran Tukufu, wale ambao wanateuliwa kwa kazi yoyote ya kiroho, wanaweza tu kupata zawadi wa elimu maalumu ya Quran yenyewe. Hawawezi kupata elimu mpya ya aina yoyote. Ukweli wa maungano yao na Mwenyezi Mungu utapimwa kwa kadiri ya elimu yao ya Quran Tukufu. Elimu kama hiyo iwe na sifa ya kiungu, sio tu elimu ya akili ya masufi. Tunaona ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa alipata lundo la elimu hii. Elimu hii ilikuwa nyingi hivi kwamba tunaweza kusema kwa uaminifu kuwa kwa Masihi Aliyeahidiwa, Quran Tukufu imefunuliwa tena wakati huu. Kusema hivi itakuwa sawa na Hadithi ya Mtume s.a.w. mwenyewe. Alisema Mtume s.a.w.:

> "Lau kama Quran ikirudi mawinguni, mtu mmoja wa asili ya Waajemi atairudisha tena."

Hadithi hii inamhusu Masihi Aliyeahidiwa, Mwajemi kwa asili.

Sasa nitaendelea kuleza juu ya elimu malumu ya Quran Tukufu ambayo Masihi Aliyeahidiwa aliitoa kwa wanadamu. Kwanza nitaanza na msingi wa elimu hii; ambayo ilithibitika kuwa ya maana sana katika vita yake na dini zingine. Kwa hiyo washindi wakawa washindwa na washindwa wakawa washindi. Quran Tukufu ambayo ilifikiriwa kuwa kitabu kilichokufa, kwa uvumbuzi nitakaoeleza, kikawa kitabu hai mara nyingine. Maadui wa Kitabu Kitukufu hiki wakawa hawajuani.

Kabla ya kudhihiri Masihi Aliyeahidiwa, Waislamu kwa ujumla waliamini kuwa elimu ya Quran ilikwisha elezwa na Wanazuoni wa Islam na Mufasirina wa Quran. Hakuna kipya cha kuongeza. Kujaribu kuongeza chochote kwenye elimu hii ni upuuzi na hata ni kuihatarisha imani. Juu ya hayo, Masihi Aliyeahidiwa alihakikishiwa na Mwenyezi Mungu kuwa Quran Tukufu ni ulimwengu wa elimu ya kiroho. Haina upepo kama ulivyo ulimwengu wa kimwili. Quran Tukufu haina upeo wa maana yake kama umbile lilivyo katika jinsi yake. Elimu ya kisasa imeonesha mipaka isiyokadirika ambayo maarifa ya umbile la kimwili inayo. Nyuki ni kiumbe duni, lakini huendelea kutoka jinsi zaidi na zaidi. Siri zilizomo ndani ya sehemu mbalimbali za mwili wake na kazi za sehemu hizo zinaonekana hazina mwisho. Jani dogo sana linaonekana limeficha ndani yake sehemu nyingi sana za kazi. Hatuoni kwa nini Neno la Mungu liwe na mwisho katika maana. Je, litoe maana yake kwa vizazi viwili tu au vitatu lakini lisitoe chochote kwa vizazi kadhaa baadaye? La, neno la Mwenyezi Mungu ni lazima liendelee kuinufaisha dunia. Lisiwe kama mgodi, ambao ukisha chimbwa mara moja, hauwezi kuchimbwa tena. Kwa kweli Neno la Mwenyezi Mungu linatakiwa liwe na umbali sana usiokoma katika maana yake kuliko ulimwengu wa jinsi ya kimwili ulivyo katika umbile lake. Dunia ionekane ina ukomo ikilinganishwa na maana isiyokoma ya Neno la Mungu. Ikiwa jinsi ya asili inaweza kuchipiusha elimu mpya kila siku baada ya siku, kama elimu ya sayansi na falsafa inaweza kuendelea, kama elimu ya tabaka za ardhi na elimu ya vyombo vya zamani na elimu ya maungo ya mwanadamu na elimu ya mimea na elimu ya wanyama na falaki na iktisadi na matendo na nafsi na roho na tabia na elimu zingine za asili zinaweza kuongezeka siku baada ya siku, je,

Neno la Mungu lisichipushe elimu zaidi na zaidi kadiri tuendeleavyo toka muda fulani wa taarikh hata muda mwingine? kwa nini tufikiri ya kuwa Neno la Mungu lina ukomo au limekufa hivi kwamba lilikusudiwa kuonesha nguvu yake katika wakati fulani, ambalo baada yake ilikuwa lisiwe zaidi kuliko kitu kilichokufa? Je, tufikiri kuwa kwa miaka mamia kadhaa sasa Quran Tukufu haikuchipusha elimu yoyote mpya?

Kutoweka kwa mapenzi ya dini na kukosekana maungano na Mwenyezi Mungu na mafundisho Yake tunakoona leo kunahusiana - kwa namna hii au ile - na maendeleo yaliyoletwa na sayansi na falsafa wakati huu. Ikiwa Quran Tukufu ni Neno la Mungu, Kauli Yake hasa, ilipasa tupate ndani yake elimu mpya zaidi na zaidi ili kwamba elimu ya kiroho ifuatane na elimu ya asili. Makosa ya elimu ya kisasa, kupotoka kwake au chumvi yake, ingesahihishwa, kila ambapo ingelazimu, kwa elimu mpya ya Quran Tukufu, ikaelekea kutilia shaka ukweli, tupate uhakika wa Quran Tukufu ya kwamba fundisho ka Kitabu Kitukufu ni la akili na la kweli, na ya kwamba shaka inayotolewa na elimu ya asili ni matokeo tu ya kukosa kufikiri.

## QURAN IMETABIRI ISHARA ZA WAKATI WETU

Kwa kuweka msingi huu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kwa hoja, alionesha kuwa Quran Tukufu ni bishara kuhusu wakati wetu huu. haitoi tu maelezo ya maendeleo ya kawaida tuyaonayo leo bali pia maelezo ya sehemu fulani fulani maalum ya maendeleo yaliyofanyika siku hizi. Mufasirina wa zamani hawakuwa na elimu juu ya mabadiliko yaliyokuwa yatokee zama hizi. Kwa hiyo, hawakuweza kuelewa madokezi ya bishara za Quran Tukufu ambazo zimetimia leo. Moja kwa moja walifasiri madokezi hayo kwa hali ya Siku ya Kiyama. Bila kuiona rahisi sana mara kwa mara walipotoa maana ya Quran Tukufu.

Ninataja hapa ishara kumi na mbili za wakati huu zilizomo ndani ya Sura mashuhuri. Al-Takwiir, (81:2-13), ya Quran Tukufu:

" Jua litakapofunikwa, Na nyota zitakapotiwa giza, Na milima itakapotembezwa, Na ngamia watakapoachwa, Na wanyama wa mwitu watakapo-kusanywa, Na mito itakapopasuliwa, Na nafsi zitakapounganishwa, Na msichana aliyezikwa hai atakapoulizwa: Kwa kosa gani aliuawa? Na sahifa zitakapoenezwa, Na utando wa mbingu utakapota-nduliwa, Na Jahanamu itakapokokwa, Na Pepo itakaposogezwa,

Aya hizi zi sura ya wakati wetu huu. Mufasirina walipotea kwa aya mbili za mwanzo, "Jua litakapofunikwa, na nyota zitakapotiwa giza" - kwa kawaida ishara hizi mbili zinaungana na Siku ya Kiyama. Kwa hiyo Mufasirina walifikiri kuwa aya zingine zote za Sura hii zinaungana na Siku ya Kiyama. Kwa hali yoyote hii si kweli, kwa sababu aya zingine hizo ni wazi zinaeleza hali na matukio ya wakati huu. Kusogea kwa milima, mathalan, kuachwa kwa ngamia kutumiwa kama wanyama wa mizigo na usafiri, na kurudi nyuma watu wastaarabu mpaka kwenye unyama, na kutengwa mbali au kuangamizwa makabila ya kishenzi (kama Australia, Amerika, n.k.), kupasuliwa mito kwa makusudi ya kunyweshelezea mashamba, kukusanyika kwa watu toka sehemu za mbali za dunia, mwongezeko wa ujamaa, marufuku ya kuua watoto wachanga, mwongezeko wa ajabu wa kuchapishwa vitabu na magazeti, mwongezeko usio wa kawaida wa maarifa wa mambo ya kimbinguni na (kwa lugha ya mfano) mambo ya kiroho, na mwongezeko wa kueneza maelezo na tafsiri ya Quran Tukufu na Uislamu, na maendeleo ya ajabu ya elimu za aina mbalimbali na matokeo ya kutomjali Mwenyezi Mungu, na mwongezeko wa kutafuta ladha za kidunia, na mwisho kusogezwa kwa Pepo au Rehema ya Mwenyezi Mungu kurudisha ucha Mungu

dunaini (kuamka imani, kuongezeka matendo ya kiungu, watu kuweza kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu na kupata kwa wingi Pepo Yake). Je, hizi sio ishara za wakati wetu huu?

Kusema kwamba "Jua litakapofunikwa, na nyota zitakapotiwa giza" ni ishara za Siku ya Kiyama; kwa hiyo sura hii inahusu siku hiyo, si kweli. Hii ni kwa sababu sura hii inaendelea waziwazi kusema kwamba Saa itaashiriwa kwa kuachwa kwa ngamia kwa kutumiwa kuwa wanyama wa kusafiria na kusafirishia bidhaa. Je, hii inaweza kuwa ishara maalum ya Siku ya Kiyama? La, kwa sababu siku hiyo siyo ngamia tu bali kila kitu, wanyama, wanadamu, ndugu, baba, mama, wana, mabinti, mke, dada, wataachwa. Juu ya hili tunayo maelezo maalum ndani ya Quran yenyewe. Zama mfarakano wa mambo yote haya unatokea hakutakuwa na dalili ya kusema maalumu juu ya ngamia. Kutaja hili kuwa ishara ya maana sana itakuwa kichekesho, zama hali ni ya mfarakano wa vitu vyote vya ulimwengu. Sasa swali ni hili, kunaweza kuwa na maana gani ya kukusanywa kwa wanyama kuwa ishara ya Siku ya Kiyama? Ni ipi inaweza kuwa maana ya kupasuliwa kwa maji, kukutana kwa bahari, kuulizwa juu ya mtoto mchanga wa kike? Hizi haziwezi kuwa ishara za Siku ya Kiyama. Kuulizwa juu ya watoto wachanga kunaweza kuwa baada ya kufufuliwa na sio wakati wa mafarakano wa viumbe vyote na fujo. Aya zinazofuatia aya nilizozitaja, pia zinaonesha kuwa matukio yaliyoelezwa ndani ya sura hiyo si matukio ya Siku ya Kiyama, bali ya maisha hayahaya na ulimwengu huuhuu. Sura inaendelea kusema:

"Na kwa usiku uondokapo, Na kwa asubuhi inapopambazuka."

Haya ni maelezo ya mabadiliko ya usiku na mchana. Mabadiliko kama haya yanawezekana tu katika ulimwengu mtulivu ambao jua na nyota zinaendesha kazi zao za kawaida katika njia zao maalumu. Kama jua likifunikwa, kama itakavyokuwa Siku ya Kiyama, tunawezaje kupata mabadiliko ya usiku na machana? Kwa hiyo, aya hizi hazihusu Siku ya Kiyama kama Mufasirina wengi wanavyoonekana kudhania. Bali hasa zinahusu wakati huu wetu.

Zinaeleza juu ya mwongezeko wa madhambi, utamaduni wa sanaa, zinaa, na kufika kwa Rehema ya Mwenyezi Mungu, na pia mwongezeko wa imani na kuondolewa kwa shaka.

Huu ni mfano tu wa bishara zilizomo ndani ya Quran juu ya mabadiliko na matukio ambayo ilikuwa yatokee zama hizi. Mfano huu ulitajwa na Hadhrat Ahmad mwenyewe; bali madhumuni ya bishara za Quran yameelezwa zaidi na wafuasi wake kwa kufuata misingi ilyowekwa naye. Katika Kitabu cha Mungu maelezo zaidi juu ya uharibifu wa watu uliotokea katika wakati wetu huu yametolewa na njia zingine za kushughulika na maelekeo hayo mabaya zimeandikwa waziwazi. Kwa kusoma maelezo hayo, mkanaji mkubwa namna gani atahakikishiwa kuwa Quran Tukufu ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kina maelezo ya matukio makuu ya ulimwengu, yaliyopita, yaliyoko na yajayo. Ningeendelea kutoa mifano mingine, lakini hii itakuwa kwenda mbali na madhumuni.

Uvumbuzi wa pili juu ya Quran Tukufu aliofanya Masihi Aliyeahidiwa ni uvumbuzi wa maana sana kwamba Quran haidai jambo lolote mpaka pia inaashiria sababu ya dai hilo. uvumbuzi huu wa maana sana kama ulivyo ni wa kweli. Unaweka mikononi mwa wafuasi wa Kitabu ufunguo ambao kwao wanaweza kufungua wa Masihi Aliyeahidiwa walipoendelea kusoma Quran Tukufu, wakiwa na fundisho hili la pekee la Kitabu Kitukufu hiki akilini, waliona kwamba maelfu ya mambo yaliyofikiriwa kuwa madai matupu yasiyo na dalili zake ambayo Wanazuoni wa katika hiki waliamini tu ati kwa sababu ni madai ya Mwenyezi Mungu, yalionekana yamechukua pamoja nayo misingi yake pia ya akili. Huu ulikuwa ufunuo wa maana sana. Hatua ya elimu za kisasa na jinsi mbalimbali za maendeleo imezalisha siku hizi tabia ya kuacha kukubali chochote bila ya hoja.

Kwa sababu ya tabia hii, ilikuwa vigumu kwa watu wa zama hii kukubali maneno ya Quran Tukufu mpaka yawe yamefuatana na dalili na kuwa sawa na akili. Pamoja na mkazo wa Masihi Aliyeahidiwa wa kutumia njia ya Quran na kutoa hoja na madai pamoja, wapenzi wa Quran waliona wametoshelezwa kabisa.

Walistaajabishwa na mahala ambamo Quran Tukufu imepanga madai na hoja kamili. Watu waliotaka kuitupilia mbali Quran wakaikumbatia kwa pendo kubwa. Wasomaji hawakuona tena taabu katika mafundisho yake. Quran Haikuwataka wasomaji wake wakubali chochote bila ya akili. Bali imewataka wakubali itikadi na amri ambazo zinakubaliana na akili yao. Quran haikukusudia kutia utumwani bali kunawirisha kama kiongozi hodari. Masihi Aliyeahidiwa pia alipata hoja ndani yake juu ya kuwako kwa Mwenyezi Mungu. Hoja hizi haziwezi kukanwa na elimu za kisasa. Athari yake kwa jamia zilizoelimika ni kubwa mno. Wengi, ambao wangemkana Mwenyezi Mungu, wanarudishwa kwa Mwenyezi Mungu na njia za kiungu.

Hivihivi, hoja zilizotolewa juu ya Malaika zilijibiwa pia na Masihi Aliyeahidiwa, kutokana na Quran Tukufu. Haja ya unabii, mizani ya ukweli wa Manabii, ithbati ya Siku ya Kiyama, haja ya matendo mema na faida yake, hatari ya kuvunja makatazo na njia za kuiepa hizi na madhumuni mengine ya maana yalielezwa na Masihi Aliyeahidiwa kutokana na Quran Tukufu. Madai na dalili zake zilitolewa kwa msaada wa Quran. Masihi Aliyeahidiwa alithibitisha kuwa elimu za kisasa na falsafa haziiwezi Quran Tukufu. Haziwezi kuonesha baina ya Quran na akili. Sayansi inahusika na mambo ya asili, kazi ya Mwenyezi Mungu. Quran ni Neno la Mungu. Vyote, kazi na Neno, ni Vyake. Hakuwezi kuwa na hitilafu baina ya hivi viwili. Inapoonekana Neno la Mungu linapingana na mambo ya asili, ni lazima iwe ya kwamba neno hilo linalosemwa ni la Mungu si neno Lake hasa. Kama ndilo, basi ni lazima iwe kwamba halikueleweka sawa. Neno hasa la Mwenyezi Mungu haliwezi kufundisha chochote kinyume na mambo ya asili.

Kutangazwa kwa uvumbuzi huu juu ya Quran kukaleta yakini mpya, tegemeo jipya juu ya Quran Tukufu. Wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa leo wanashughulika kujipatia elimu za kisasa kama wengine. Lakini wakati huohuo yakini yao juu ya itikadi na amri za Quran Tukufu inakuwa na nguvu zaidi kama ilivyokuwa wakati wowote katika taarikh ya Uislamu. Yakini hii haitokei kwa kupenda mila za zamani, bali kwa kufikiri na kwa hoja. Wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa wako tayari kutoa ushuhuda juu ya chochote

wanachoamini. Waislamu wengine wanajoina wamo katika mashaka ya ajabu. Ili kusalimisha imani yao wanaona ama wasijifunze kabisa elimu za kisasa na falsafa, au kinyume na akili yao, wanaona heri wakane na kulaumu kuwa ni kufuru chochote kinachofundishwa na elimu za kisasa. Itikadi zao za dini zinastawi katika ulimwengu wa mawazo. Au akili yao na hukumu zinashindwa na elimu mpya na wanakuwa na imani ndogo au kabisa hawana imani mioyoni mwao. Ni Waislamu kwa woga tu lakini wana mashaka akilini mwao.

Uvumbuzi wa tatu alioufanya Hadhrat Ahmad juu ya Quran ni kwamba endapo akili inatilia shaka sehemu yoyote ya Quran, basi tatuzi la shaka hiyo linapatikana ndani ya Quran yenyewe.
Hadhrat Ahmad alitilia mkazo sana madhumuni hii ya Kitabu hiki Kitukufu. Sio tu kwamba alidai hivyo, bali alithibitisha kwa mfano wa wazi. Kadiri ya alivyofanya juu ya suala hili inastaajabisha. Alipata matatuzi yote ndani ya Quran yenyewe. Hakupata kueleza fikra fulani kuwa ya kuchukiza sana kwa sababu ya kuwa kinyume na Quran. Alifafanua vilivyo kila jambo na kwa hoja za Quran zinazokubalika akilini, akaonesha hatari ya mashaka hayo. Ni wachache tu ambao kwa sababu ya kupendelea hawakuyakini juu yake na kuathirika.

Uvumbuzi wa nne ulikuwa ni uvumbuzi wa sifa zinazofanya Quran kuwa na fadhila juu ya vitabu vya dini zingine. Kabla ya wakati wa masihi Aliyeahidiwa, mtu aliweza kusikia tu dai pana sana ya kwamba Quran Tukufu ina fadhila juu ya kitabu cha dini nyingine yoyote ile. Quran ilisemwa ni ya pekee, lakini hakuna aliyeweza kusema ni kwa vipi. Hadhrat Ahmad alitoa jawabu, tena kutokana na Quran yenyewe. Alikariri suala hili mara nyingi. Wale ambao walijali kufuata maandiko yake, hawatashindwa kutekwa na mvuto wa hoja alizozitoa. Kwa kweli mtu atapenda kujitoa kabisa kabisa kwa ajili ya Quran na Mtume s.a.w. ambaye kwake wanadamu wamepokea zawadi hii yenye thamani ya mwongozo.

Uvumbuzi wa tano ulikuwa ni wingi wa maana za manenoMatukufu. Aya fulani inaweza kuwa na maana kadha wa

kadha, zingine karibu na uso, zingine chini sana, zingine chini zaidi. Yoyote itakayokuwa hatua ya fahamu ya msomaji, mazoea yake au vingie, ataona ndani ya aya hiyo tafsiri ambayo itafaa fahamu yake, na ambayo itakuwa ya kweli na inayoihusu. Maneno hayohayo yanaweza kufanya kazi kwa makusudio mbalimbali na kwa watu wa namna mbalimbali. Mtu wa fahamu ya kawaida ataona katika maneno hayo fundisho rahisi ambalo haoni shida kulielewa na kuamini. Mtu mwingine, aliyejaaliwa fahamu zaidi kidogo, ataona ndani ya maneno hayohayo, tafsiri sawa na fahamu yake na ujuzi. Mtu wa fahamu ya juu sana ataona tafsiri ya juu vilevile. Ilmuradi Quran Tukufu inatoa kwa watu wa kila namna ya fahamu jambo fulani la maana sana. Wale wa fahamu kidogo hawataiona Quran inashinda fahamu yao; wale wa fahamu ya juu hawataiona Quran chini ya fahamu yao. Watu wa daraja zote wataiona Quran Quran inaweza kuathiri fahamu yao na maendeleo ya tabia yao.

Uvumbuzi wa sita ulikuwa kwamba Quran Tukufu inatoa elimu juu ya matukio ya asili ambayo ni ya lazima na ya kutosheleza maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Si kitabu cha mambo ya kiroho tu. Bali ni Kitabu chenye mambo mengine ya maana. Kuelewa mambo haya mengine kunafuatana na wakati. Kwa hiyo, wakati wowote katika taarikh, watu wanaweza kuigeukia Quran na kuhuisha imani yao juu ya Mwenyezi Mungu.

Uvumbuzi wa saba ni uvumbuzi wa misingi ya tafsiri ambayo kwayo tunaweza kujikinga na makosa katika juhudi ya kuielewa Quran Tukufu na kuinasibisha na migogoro inayotukabili. Kwa kuchungua misingi hii ya tafsiri, msomaji anaweza pia kujua mambo ya kweli, ambayo hapo kabla hakuwa na habari nayo. Kwa kusaidiwa na misingi hii, msomaji wa Quran Tukufu anaweza kupata furaha mpya kila wakati anapoisoma.

Uvumbuzi wa nane ambao Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad aliufanya ni kwamba Quran Tukufu ina maelezo kamili juu ya hatua za maendeleo ya kiroho ambayo wanadamu wanaweza kuzifikia. Suala hili limekwisha zungumzwa mwanzoni, bali kwa msingi wa

ushuhuda wa hoja. makosa yalifanywa mara kwa mara katika tafsiri za kiakili. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alikuta suala hili lote ndani ya Quran yenyewe. Kwa rehema za Mwenyezi Mungu alieleza hatua za kiroho za mwanadamu, (toka ya chini mpaka ya juu sana), zilizoelezwa kwa taratibu nzuri sana na Quran Tukufu. Kwa kufuata maelezo hayo, mtafutaji ukweli na maendeleo ya kiroho anaweza kumfikia Mwenyezi Mungu na kufaidi matunda ya pekee ya imani katika kila hatua. Elimu ya hatua za kiroho katika hali hii haikuwako hapo kabla. Watu walisoma Quran, lakini waliweza kuashiria tu kwenye sehemu zinazoeleza nusu ya suala hili. Hakuna aliyeweza kuzikusanya sehemu zote pamoja na kuweka suala la maendeleo ya kiroho katika taratibu maalumu.

Uvumbuzi wa tisa ni uvumbuzi wa utaratibu kamili wa Quran Tukufu. Aya za kila sura zenyewe zina utaratibu wa akili sana. Kila sura,, kila aya katika kila sura, na kila neno katika kila aya, liko mahala pake hasa. Ni mkamilifu kabisa mpango baina ya neno na neno, baina ya aya na aya na baina ya sura na sura nyingine, hivi kwamba mpango uliomo ndani ya vitabu vingine unaonekana si chochote mbele ya mpango wa Quran. Mpango katika vitabu vingine ni wa namna moja. Hauwi sawa zikifuatwa tafsiri nyingi za maneno. Mpango wa Quran Tukufu ni wa juu sana na wa namna nyingi. Sio tu kwamba maneno na aya zinafuata taratibu ya namna moja, bali namna nyingi zingine. Ikifuatwa misingi safi ya kuieleza Quran kila sehemu ya Quran ina maana kadha wa kadha, na kila maana inapatana na kuungana na makusudio au shabaha maalumu. Mpango wa maneno na aya katika kila sehemu unaonekana unafuatana na kila namna ya makusudio ya kweli na shabaha. Mpango wa namna hii ni wa kimwujiza. Unakidhi haja za fundisho la jumla la sehemu na pia mafunsidho maalumu ambayo mtu anaweza kuyaona chini ya uso. Uzuri wa sehemu ya Quran unabakia, tuwe tumeifikiria sehemu fulani katika shabaha hii au ile. Mpango kama huu hauwezi kupatikana ndani ya kitabu chochote cha kibinadamu.

Uvumbuzi wa kumi ni kwamba Quran ina maelezo kamili juu ya hatua mbalimbali za tabia njema na mbaya za mwanadamu. Quran inatuambia ni mambo gani mema yanayongoza kwenye mambo

fulani mengine mema, na ni gani mabaya yanayoongoza kwenye mengine mabaya. Elimu ya namna hii ina msaada usiokoma katika kukuza maisha mema. Maisha mema yanakua kwa hatua fulani na kila hatua inaweza kufafanuliwa. Hii inafanya iwezekane kuendelea katika wema ambao bila ya hii isingewezekana Elimu kama hii inamwezesha mwenye kujitahidi katika njia ya tabia njema kufanya hatua moja mbele kama matayarisho kwa ajili ya nyingine. Anaweza pia kujisalimisha na kurudi nyuma kokote. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alieleza mambo haya kutoka ndani ya Quran Tukufu. Quran inaashiria kwenye chemchem ya mema ambayo kwayo wenye kiu ya kiroho wanaweza kutuliza kiu yao, pia inaonesha mahandaki na njia za giza ambazo wasafiri wa kiroho wangependa kuzikwepa.

## SURA YA ALHAMDU NI MUHTASARI WA QURAN NZIMA

Uvumbuzi wa kumi na moja ambao Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. aliufanya ni kwamba Sura ya Alhamdu, sura ya mwanzo ya Quran, ni muhtasari halisi wa Quran Tukufu. Sura hiyo ni kama matini na sura zingine zote zikiwa kama maelezo yake. Kila kitu, kiwe imani, vitendo au kingine, kilichoelezwa kwa urefu ndani ya Quran Tukufu, kina shina lake ndani ya Sura ya Alhamdu. Alitunga vitabu vingi akiandika maelezo ya sura hii fupi. Katika maelezo hayo aliweka mafundisho mazuri sana ya kuvutia ambayo yote yalitoka ndani ya sura hii moja. Tafisiri ya Uislamu kwa manufaa ya Waislamu na wengine, imerahishishwa kinyume na kipimo kwa uvumbuzi huu. Watu wengi wanapendelea muhtasari juu ya maelezo marafu. Maelezo marefu sana ni magumu kufuatwa, lakini muhtasari ni rahisi. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alionesha kwamba karibu kila suala linaweza kuelezwa kutokana na sura hii moja. kwa hivi, mtu anaweza kushinda dini zote kwa msaada wa sura Alhamdu na kuona ndani yake daraja zote za maendeleo ya kiroho.

Hiyo ni mifano michache ya elimu ya misingi. Ni uvumbuzi wa kanuni ambazo zimeonekana kuwa ni za lazima katika tafsiri ya

Uislamu siku hizi. Bali kuna uvumbuzi wa kumi na mbili ambao tunauwia kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kuhusu Quran Tukufu. Ni maana ya sehemu na aya za Quran Tukufu wa mradi wake maalumu unaohusiana na haja za wakati huu. Kazi zake zilizojaa mifano ya uzuri wa maelezo na tafsiri zinaweza kukusanywa katika lundo la vitabu. Lundo kubwa la elimu kama hili, linashiria tu kwenye chemchem ya baraka nyingi. Si mwingine bali Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Seyidna Ahmad a.s. aliungana naye kikweli kweli. Juu Yake Quran Tukufu inafundisha:

"Wala hawazunguki chochote katika elimu Yake ila Apendavyo." (2:256).

Si juu ya mtu kuvumbua elimu zaidi kuliko mipaka yake. Elimu kama hii inaweza kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu. Ndiyo sababu katika Quran tunaona habari za maana, tusomapo kwa msaada wa misingi ya mwongozo iliyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alisisitiza sana mizani ya ukweli na utakatifu iliyoelezwa na Quran:

"Hapana atakayeigusa ila waliotakswa." (56:80).

Kuigusa Quran Tukufu maana yake ni kujua maana yake na mbinu zake. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad aliwaita maadui zake na kuwauliza:

"Kama mimi niwe mwongo, kwa nini nijaaliwe elimu mpya kabisa ya Quran Tukufu?

Aliwaita Masheikh na Maulamaa wa wakati wake wajitokeze na kulinganisha ujuzi wao wa Quran na wake. Mwamuzi atoe sehemu fulani ya Quran halafu ampe yeye na yeyote ambaye angejitoa kushindana naye katika jitihada ya kuona maana mpya kutoka sehemu hiyo ya Quran. Kisha basi, ingebainika ni yupi anayepata baraka ya mbingu katika jitihada ya kuielewa Quran Tukufu. Wito huu ulirudiwa mara nyingi. Hakuna aliyekuja mbele. Na si ajabu, kwa sababu katika kuelewa Quran, watu wengine

hawawezi kushindana hata na wafuasi wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Ninapenda kuifunga hoja hii pamoja na kipande kidogo cha shairi la Kiajemi la Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akiusifu uzuri wa Quran Tukufu:

Tokana na nuru safi ya Quran, kumekucha mchana wenye baraka,
Na juu ya mboni za mioyo ulivuma upepo mwanana.
Jua la adhuhuri halina nuru hii, hata mwezi hauoneshi uzuri huu.
Nabii Yusuf alibaki peke yake kama mahabusu kisimani, lakini Yusuf huyu (Quran) ametutoa nje ya kisima.
Yeye (Quran) ametoa mamia za kweli zenye maana toka mashariki ya maana.
Mviringo wa mwezi umekuwa zaidi kwa sababu ya wororo wake.
Je, unajua utukufu wa elimu za Quran Takatifu?
Asali ya mbinguni inatiririka chini na upuzio wa kiungu.
Jua lile la ukweli lilipoielekea dunia hii, kila bundi mpenda usiku alijitenga na kujificha pembeni katika giza.
Hakuna yeyote katika dunia hii, anayepata kuona uso wa yakini,
Isipokuwa yule anayepata utulivu katika uso wake.
Yule aliyefikia kuijua, akawa hazina ya mambo ya maarifa,
Yule aliyekuwa hana habari nayo, alibakia mjinga wa kila kitu.
Mvua ya fadhili za Mwenyezi Mungu Mfadhili amenyesha kwa ufikaji wake,
Ole wake anayepiga kisogo na kuelekea upande mwingine.
hakuna kishawishi cha kufanya dhambi, isipokuwa shetani aliyomo ndani ya mtu.
Kwangu mimi mtu ni yule tu aliyeepukana na kila shari.
Ee chimbuo la uzuri ninajua umetoka wapi;
Wewe ni Nuru ya Bwaba aliyeumba dunia na vyote.
Simpendi mwingine yeyote, Wewe peke yako ndiwe mpenzi wangu.
Ni kwa sababu ya mapenzi haya ndio Nuru hii yako ilinijia.

# HOJA YA KUMI
# BISHARA ZA MASIHI ALIYEAHIDIWA

Hoja ya kumi ambayo ndani yake mna maelfu ya hoja ndogondogo, ni kwamba Mwenyezi Mungu alimjaalia Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad elimu nyingi za siri zake, na elimu hizi ni dalili ya ukweli wake. Inasema Quran Tukufu:

"Wala Hamdhihirishii yeyote siri Yake, isipokuwa Mtume Wake Aliyemridhia" (72:27-28).

Wingi wa elimu ya kiroho juu ya mambo yasiyokuwa katika uwezo wa wanadamu ni ishara ambayo kwayo Manabii wa Mwenyezi Mungu wanaweza kupambanuka katika watu wengine. Manabii hao hupokea wahyi ung'aao usio na mchanganyiko. Husaidiwa kwa ishara za bayana na kupaswa habari za matukio ya baadaye kabla hayajatukia. Hutumwa na Mwenyezi Mungu. Kuwakadhibisha wao ni kuikadhibisha Quran Tukufu. Quran Tukufu inafundisha kuwa elimu ya siri za Mwenyezi Mungu inapewa Manabii tu. Kukadhibisha hili ni kuwakadhibisha manabii wote. Manabii daima wametoa elimu ya siri za Mwenyezi Mungu kama dalili ya ukweli wao. Biblia inafundisha kwamba alama ya nabii wa uongo ni hii kwamba anaweza kusema jambo fulani kwa jina la Mwenyezi Mungu na jambo lile lisitimie. Kwa mizani hii tunapochunguza madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Masihi Aliyeahidiwa, ukweli wake unaanza kung'aa kama jua la adhuhuri. Alijaaliwa na Mwenyezi Mungu elimu nyingi za siri za Mwenyezi Mungu hivi kwamba isipokuwa Mtume Mtukufu wa Islam s.a.w., bishara za Manabii wengine hazitoi kifano cha bishara zake. Kwa kweli, kama bishara zilizotolewa kwa Masihi Aliyeahidiwa zingegawanywa kwa manabii, zingetosha kuthibitisha unabii wa wengi.

Miongoni mwa bishara hizo nitaeleza hapa chini bishara kumi kuwa mifano:

Bishara za Masihi ALiyeahidiwa zilikuwa za namna mbalimbali. Baadhi yake zilihusu mabadiliko ya siasa, zingine zilihusu

maendeleo ya ujamaa, zingine zilihusu matukio ya anga, zingine juu ya mambo ya dini, zingine juu ya kazi za akili, zingine kuhusu kuzaliwa watoto, zingine juu ya kutozaliwa watoto, baadhi yake zilihusu mabadiliko ya dunia baadhi juu ya uhusiano baina ya mataifa, zingine kuhusu mafanikio ya kazi yake, zingine kuhusu sura ya baadaye ya mambo. Kwa ufupi, bishara zake ni nyingi mno na orodha yake inaweza kuwa ndefu.

Bishara kumi na mbili ninazopenda kuzieleza zimekwisha timia tayari. Ya kwanza kabisa inahusu nchi ya Afghanistan.

## BISHARA YA KWANZA KUUAWA KWA MASHAHIDI WAWILI

Mauti ya Sahibzada Seyyid Abdul Latif na Maulvi Abdul Rahman wa Afghanistan na matukio yaliyofuata.

Mwenyezi Mungu awape watawala ulinzi Wake maalumu na awaokoe na matokeo ya makosa katika kazi ambayo hawakuhusiana nayo! Miaka 40 iliyopita Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alipokea ufunuo:

"Mbuzi wawili watachinjwa, na kila aliyomo katika nchi hiyo atakufa."

Mbuzi wawili katika lugha ya mfano maana yake ni wanawake au raia watii. Hivi ndivyo inavyokubaliwa na taabiri za ndoto. Kama tuchukue mbuzi kwa maana ya wanawake, basi fungu lote la maneno haliwezi kutoa maana nzuri. Wanawake hawachinjwi kwa akwaida; ni wanaume ndio wanachinjwa. Hivyo, mbuzi wawili, maana yake ni watu wawili wanaume walio ni watii na wakunjufu wa kazi. ufunuo unasema kuwa watumishi wawili sana kwa mfalme, wasio na makosa ya uasi wowote kwa serikali na hasa wasiostahili adhabu ya kifo, watauawa. Sehemu ya pili ya ufunuo "na kila aliyomo katika nchi atakufa" inaashiria vifo na hilaki itakayofuata kuuawa kwa watu wema wawili.

Ufunuo hautaji nchi inayohusikana na tukio hili, lakini maneno yaliyotumiwa yanabainisha kuwa:

(1) Tukio hili linahusikana na sio nchi ya amani iliyoko chini ya Waingereza bali nchi ambayo raia watii wanaweza kuuawa ili kuridhisha hasira ya watu;
(2) Watu wa kuuawa ni wafuasi wake mwenyewe nabii; kinyume na hivi, kutajwa kwa watu wawili tu ndani ya bishara kutakuwa na shabaha ndogo;
(3) Mauaji hayo ilikuwa yawe yasiyo ya halali, bali ilikuwa yawe sio kwa sababu ya kosa lolote la kisiasa; na
(4) Matokeo ya mauaji haya yasiyo ya halali, ni kutokea kwa hilaki ya ujumla katika nchi ambayo mauaji hayo ilikuwa yatokee.

Shabaha hizi nne zinapambanua bishara hii katika bishara za kawaida. Kama jina la nchi limeachwa, haipunguzi uwazi wa bishara hii. Shabaha hizi nne zinathibitisha ubora wa bishara hii. Haziwezi kutokea ghafla.

Karibu miaka 20 ilipita baada ya kutangazwa kwa bishara hii, hakukutokea chochote. Baada ya miaka 20 mfuatano wa matukio ukaanza na hii ilileta kutimia kwa bishara hii kiajabu. Ilitokea hivi ya kwamba vitabu vya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad viliingia Afghanistan na Mwanachuoni, Sahibzada Seyyid Abdul Latif wa Khost, aliyeheshimiwa sana katika Afghanistan kwa sababu ya wema wake na utawa na marafiki zake na wafuasi, alisoma vitabu hivyo na akaamua kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ni mkweli. Alimtuma mmoja wa wafuasi wake kwenda Qadian kuulizia zaidi, na kumwamuru afanye Baiat kwa niaba yake kama atahakikisha kuwa ni mkweli. Mfuasi huyu alikuwa Maulvi Abdul-Rahman. Maulvi huyu alikwenda Qadian na akafanya Baiat yeye mwenyewe na kwa niaba ya kiongozi wake Sahibzada Seyiid Abdul Latif vilevile. Alirejea Afghanistan na vitabu zaidi vya Seyyidan Mirza Ghulam Ahmad. Akaamua kwenda kwanza Kabul ili akampashe mfalme habari ya uvumbuzi huu mpya.

Mara tu baada ya Maulvi Aabdul-Rahman kufika Kabul, watu fulani wachochezi wakamchochea Amir Habibullah Khan kinyume chake. Walisema kuwa mtu huyu amekuwa kafiri. Ametoka nje ya

Uislamu na adhabu yake ni kifo. Amir alibembelezwa atie sahihi Fatwa ya kifo. Basi Maulvi Abdul-Rahaman akauawa kikatili sana. Alikuwa hajafika kijijini kwake. Alikuwa ameamua kwenda kwanza kwa mfalme wake kumwambia kwamba Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa amekwisha fika. Alifanya hivi kwa sababu ya mapenzi na mfalme wake. Lakini akazawadiwa kifo. Alifungwa shingoni kikweli na kufariki dunia. Mkono wa Mwenyezi Mungu ulikuwa unafanya kazi. Miaka ishirini kabla, Mwenyezi Mungu aliarifu juu ya kuuawa kwa raia wawili wema wa Amir. Mmoja wao akawa ameuawa tayari.

Kupata miaka miwili hivi baadaye, Sahibzada Abdul latif aliondoka Afghanistan kwena Haj. Baada ya kufanya Baiat na kujiunga na Hadhrat Ahmad, aliona atembelee Qadian na baada ya hapo ndipo aende Makka. Katika Qadian alionana na Hadhrat Ahmad. Mvuto alioupata katika vitabu vyake uliongezeka; moyo wake safi ulijazwa Nuru ya Mwenyezi Mungu. Aliathirika sana hivi kwamba aliamua kuhiji baadaye na kutumia muda mrefu Qadian. Baada ya miezi michache alirudi Afghanistan. Yeye pia alipitia Kabul kumpasha habari mfalme juu ya aliyoyaona. Alipofika Khost, aliandika barua nne kwa wazee wa baraza la mfalme. Wao wakajua ni nini kimetokea na wakaamua kumchochea Amir Habibullah Khan kinyume chake, baba wa mfalme Amanullah. Walieleza mambo mengi ya uongo na kumshawishi Amir aamuru Sahibzada Abdul latif akamatwe na kupelekwa Kabul. Amri ilipelekwa Khost na sahibzada akapelekwa Kabul. Huko Kabul, Sahibzada alitolewa kwa Masheikh. Masheikh hawakuweza kuthibitisha chochote kinyume chake. Ndipo baadhi ya watu, wabaya zaidi kuliko wachochezi, wakamchochea Amir habibullah Khan na kumwambia kwamba kama Sahibzada ataachiliwa na mvuto wake uruhusiwe kuenea, watu hawatakuwa na bidii ya Jihad na hii itaidhuru serikali ya Afghanistan. sahibzada alizawadiwa zawadi ya kupigwa mawe. Amir Habibullah Khan kwa fikara yake juu ya Sahibzada alimwomba aachilie mbali imani yake na akaahidiwa kupata msamaha. Sahibzada alijibu kuwa ameuona Uislamu wa kweli. Je, artadi na kuwa kafiri? Hakuwa tayari kuacha ukweli alioukubali baada ya kufikiri sana. Ilipobainika kuwa sahibzada hataacha imani yake, alitolewa mjini

na kupigwa mawe mbele ya kundi kubwa la watu.

Maskini raia huyu mwema mwenye mapenzi na nchi yake akauawa kwa sababu ya hila ya wachochezi hawa. Walimdanganya Amir walipomwambia kuwa kama Sahibzada angeishi angeleta hatari nchini. Ukweli ni kwamba watu kama Sahibzada ni ngao kwa ajili ya nchi yao. Kwa ajili yao, Mwenyezi Mungu anakawiza maangamizi mengi yanayoikabili nchi. Washauri hawa wakatili walimwabia Amir ya kuwa mvuto wa sahibzada ungepunguza bidii ya watu juu ya Jihad. Lakini hawakumwambia Amir ya kwamba sehemu ya itikadi alizokubali Sahibzada ilikuwa kuitii serikali ya nchi alimoishi mtu.

Fundisho hili laiti lingeruhusiwa kuenea, lingekomesha magomvi ya kuuana katika Afghanistan, na kuifanya nchi iwe yenye utii na mapenzi, ikiwa tayari kutii amri na kupambana na shida zote. Wala hawakumwambia Amir ya kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alikataza uchochezi, rushwa, uongo na unafiki. hawakumwabia Amir kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad sio tu alifundisha bali alitilia mkazo sana juu ya kutekeleza kazi za nchi. Kama mvuto wa Sahibzada ungeruhusiwa uenee, ungewafaidisha watu maendeleo na amani. Wala hawakumwabia Amir ya kuwa Jihad ambayo Sahibzada Abdul Latif aliikana ilikuwa ni Jihad inayotaka kusilimisha watu kwa vita. Jihad ya namna hii haikuwa sehemu ya Uislamu. Kinyume na hayo, ilikuwa ni kosa kwa Uislamu. Shibzada alipinga Jihad hii, sio Jihad aliyofundisha Mtume Muhammad s.a.w. Jihad ya Mtukufu Mtume s.a.w. ilikuwa ya kujilinda na makafiri waliowashambulia Waislamu kutaka waukane Uislamu. Wala Sahibzada hakuwa kinyume na vita halali ya siasa ambayo watu wa nchi fulani wanaweza kupigana na wengine kwa ajili ya kuhifadhi siasa na uhuru wa nchi yao. Alichofahamu Sahibzada kutoka kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kilikuwa hiki tu ya kwamba Islam inakataza kufanywa vita kwa jina la Jihad au jina la Islam, endapo watu wanaopigwa hawakuingilia Dini ya Islam na chochote. Kufanya hivi ni kuudhuru Uislamu na mafundisho yake. Mambo ya siasa ya nchi ni jambo jingine. Juu ya mambo kama haya kila nchi ni hakimu wa wenyewe. Kama mambo ya nchi yalilazimu vita, basi vita ilifaa. Lakini vita kama hii haiwezi kusemwa ni Jihad. Ushindi unaoharibu

jina la Islam au mafundisho yake, ni mbaya kuliko kushindwa ambako jina la Islam lilihifadhiwa.

Kwa kifupi, Sahibzada Abdul latif alikufa akiwa shahidi, mwisho ulioletwa na uongo wa kikatili, Ufunuo "Mbuzi wawili watachinjwa" ukawa umetimia: Wafuasi wawili wa Masihi Aliyeahidiwa, raia watii wa mfalme wao, walichinjwa. Kukabakia sehemu ya pili ya bishara iliyotabiri maangamizi. Haukupiata mwezi mmoja, Kabul ikaingiwa na hilaki ya ugonjwa wa kuhara sana na kutapika. Watu wengi sana walikufa hivi kwamba wengine wote waliobaki wakaingiwa na hofu. Kila mmoja akafikiri kuwa ugonjwa huu ulikuja kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kuuawa kwa Seyyid bila ya kosa. Mchunguzi mmoja, A. Frank martin, ambaye kwa miaka mingi alikuwa bwana fundi mkuu katika serikali ya Afghanistan, aliandika katika kitabu chake "Under the Absolute Amir" ya kuwa ugonjwa haukutazamiwa kabisa. Kwa kufikiri magonjwa ya kuangamiza yaliyopata kuingia Afghanistan na muda wa mmoja baada ya mwingine, ugonjwa mwingine ungetokea baada ya miaka minne. Hivyo basi, kutokea ghafla kwa ugonjwa huu, kulikuwa ni ishara ya Mwenyezi Mungu. Tukio ambalo alimfunulia Mjumbe wake miaka ishirini na nane kabla. Ajabu yake ni kwamba ili kusaidia kutimia kwa bishara, kama ilivyokuwa, Sahibzada Seyyida Abdul Latif naye alipata kutabiri. Alitangaza ya kuwa aliona siku za vifo zinakuja baada ya kuuawa kwake. Ugonjwa huu ulishambulia kila nyumba ya Kabul. Haukuwacha maskini wala tajiri. Wala haukuwaacha wale waliokuwa wakichungua njia za kuzuia ugonjwa huu kwa elimu ya utabibu. Lakini waliokufa husuan ni wale wote walioshiriki katika kumtupia mawe marehemu Seyyid. Wengine walikufa; na wengine walifiwa na ndugu zao wote.

Ufunuo ulitimia sawasawa. Ishara za kutisha zilitokea. Mwenyezi Mungu alitangaza ukweli na ubora wa Mjumbe Wake. Walioona kwa jicho la insaaf, waliielewa kuwa ishara ya mbinguni na waliamini. Bishara kama hii haiwezi kutungwa na mwanadamu yeyote. Nini! je, anaweza mwanadamu kutabiri kuwa karibuni atapata idadi kubwa ya wafuasi? je, anawaza kusema kuwa wakati utafika ambao watu wengi sana watajiunga naye? Ya kwamba

mafundisho yake yatasafiri toka nchini kwake mpaka nchi zingine? Na halafu katika nchi fulani wafuasi wake wawili watauawa, sio kwa sababu ya kuasi serikali bali kwa sababu ya kumwamini kiongozi wao? Je, anaweza kusema hayo ya kuwa zama wafuasi hao wawili wamekwisha uawa, Mungu atapeleka adhabu katika nchi hiyo na ya kwamba adhabu hiyo italeta hilaki kubwa mno hivi kwamba itawakumbusha watujuu ya Siku ya Kiyama na ya kwamba wengi wao watakufa? Ufunuo wa waziwazi kama huu hauwezi kutungwa na mtu yeyote. Ama sivyo, kusingekuwa na tofauti baina ya Neno la Mungu na neno la mwanadamu.

Kuna kosa moja ambalo napenda kuliondoa. Maneno katika bishara ni "Na kila aliyomo katika nchi atakufa." Inaweza kusemwa kuwa watu wote katika Afghanistan hawakufa. Wengine walikufa na wengi wakasalimika. Napenda kueleza kuwa neno "kullu" (kila) likitumiwa katika bishara katika Kiarabu linaweza kuwa na maana ya wote au fulani. Hapa maana yake ni fulani. Katika Quran Tukufu tunasoma juu ya Mwenyezi Mungu akiwafunulia nyuki:

"Halafu kuleni kila namna ya matunda" (16:70).

Kila mtu anajua kuwa kila nyuki hali kila namna ya matunda. Kwa hiyo, "kul" katika bishara hasa ina maana ya fulani wengi. Vilevile tunasoma juu ya Malkia wa Sheba katika Quran:

"Na alipewa kila kitu" (27:24).

Maelezo hayo ni ya Malkia aliyekuwa matawala wa nchi fulani ndogo. Aya hi ina maana kwamba Malikia alipata hisa kubwa katika fadhila za dunia. Ina maana hii tu kwamba neno kul alinapotumiwa lina maana ya wingi. Ugonjwa wa kipindupindu uliotokea Kabul mara baada ya kuuawa Sahibzada unaonesha hali hizi mbili za maana sana. Uliwaogofya watu wengi kwa ujumla na wengi wao walikufa kwa ugonjwa huu; hivi kwamba mwandishi wa Kimagharibi, akiwa asiyejua habari zozote juu ya aufunuo wowote aliutaja katika kitabu chake.

Kuelewa kwingine kwa kosa kunaweza kuzuka kuhusu bishara hii nako ni kwamba maneno ya bishara ni Tudhbahaani, yaani "Watachinjwa." Lakini hali hii haipatani na hawa mashahidi wawili. Mmoja aliuawa kwa kunyongwa, na mwingine aliuawa kwa kupigwa mawe. kwa hiyo, maelezo ya ufunuo hayapatani na vifo hivi. Kosa hili linazuka kwa ukosefu wa kufikiri. Neno la Kiarabu *Dhab'h* (kuchinja) lina maana mbili (1) kunchinja na (2) kumaliza, njia ya kufanya haya haikuainishwa. Katika Quran Tukufu tunayo mifano mingi ya matumizi ya neno *Dhab'h*. Katika masimulizi ya Nabii Musa, tunambiwa ya kuwa Wamisri "waliwaua wana wenu na kuwacha hai mabinti zenu" (2:50) Neno lilitumiwa ni *yudhabbihuuna* ambali limetokana na *Dhab'h* na hasa kama lingekuwa na maana ya kwamba njia ya kuua wana iliyoshikwa na Wamisri ilikuwa ya kuchinja tu ama kukata koo. Hii si kweli. Inajulikana katika taarikh ya kuwa Wamisri walitumia njia nyingi mbalimbali za kuulia wavulana wa Waisraeli. Kwanza wakunga waliamriwa kuua watoto wa kiume walioazaliwa na Waisreli. Zama wakunga hawa waliposita, Firauni aliamuru wakunga hao watoswe motoni (Kutoka 1:22 na Matendo 7:19 na Talmud). Kadhalika kamus ya Kiarabu Taj-ul-Urus (sehemu ya pili), uk. 141) inasema kuwa mojawapo ya maana za *Dhab'h* ni kuharibu. Kwa hiyo ni kosa kusema kwamba neno *Dhab'h* lina maana ya kuchinja tu, (kwa vile neno hili linaweza kutumiwa kwa namna nyingine za kuua), na ni kosa kuitoa makosa bishara hii kusema ya kuwa Shibzada aliuawa kwa mawe na sio kwa kuchinjwa.

## BISHARA YA PILI MAPINDUZI YA IRAN

Bishara ya pili ambayo, miongoni mwa maelfu ya bishara, ninapenda kueleza, inahusu Iran, nchi iliyo jirani ya Afghanistan. Mnamo tarehe 15 Januri 1906. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa, alipokea ufunuo:

"Matetemeko yametokea katika jumba la Kisraa."

Kama kawaida, ufunuo huu ulitangazwa katika magazeti yote ya Kiurdu na Kiingereza ya Jumuiya. Zama za kutangazwa kwake, mfalme wa Iran wa wakati huo alikuwa amestarehe katika kiti cha enzi yake (Encyclopaedia Britanica). Katika mwaka 1905 alikuwa amekubali maazimio ya kupanua ujumbe wa serikali. Serikali ya Halmashauri iliahidiwa na kutangazwa. Wananchi walifurahia sana jambo hili na mfalme Muzaffar-ud-Din Shah alikuwa mfalme maarufu wa taifa kubwa. Watu walitoshelezwa kwa sababu mabadiliko ya utawala yametokea bila ya kumwaga damu.
Sehemu zingine za duni ziliitumainia Iran kwa sababu jaribio hili katika serikali ya watu wengi lilikuwa geni katika Bara zima la Asia, isipokuwa Japan. Lakini hawakujua migogoro yake. Watu hawakuwa na elimu ya kutosha wala ujuzi wa kutosha juu ya serikali ya uwakala. katika wakati huo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alitangaza ufunuo "Matetemeko yametokea katika jumba la Kisra." Ufunuo huu ulionekana mgeni. Hakuna aliyefahamu matokeo yaliyoashiriwa katika ufunuo. Iran ilikuwa ikifurahia uhuru wake mpya. Mfalme Muzaffar-ud-Din Shah, alikuwa na furaha kwa kundi kubwa la watu alilolijenga.

Mnamo mwaka 1907, mfalme huyu alikufa akiwa na miaka 55. Mwanawe, Mirza Muhammad Ali akashika mahala pake. Mfalme huyu mpya akathibitisha katiba ya serikali iliyoanzishwa na baba yake. Baraza Kuu la Iran lililoitwa Majlis ilikuwa liendelee. Wajumbe mbalimbali walikaa. Lakini baada ya siku chache ishara za kutisha zikaanza kudhihirika ambazo ziliashiria matukio yaliyotabiriwa katika ufunuo wa Masihi Aliyeahidiwa. Mwaka mmoja tu ulipita baada ya kutangazwa kwa ufunuo na maasi na vita ikatokea. Hitilafu ikaanza baina ya mfalme na Baraza kuu. Majlis ilitoa maombi ambayo mfalme hakuyakubali. Hatimaye, kwa masisitizo ya Majlis, mfalme alikubali kuwatoa watu fulani; viongozi wa uasi, kama walivyoitwa na Majlis. Hapohapo mfalme akaamua aondoke Tehran, mji mkuu wa Iran. Wasiwasi mkubwa ukazuka baina ya watu wa kitaifa na watu wa dini. Hawa wenye mawazo ya kidini wakawa upande wa mfalme. Ufunuo wa Masihi Aliyeahidiwa ukatimia sehemu moja. Majlis ya Iran iliharibika. Mfalme akaivunja. Mapigano yakaanza katika sehemu nyingi za Iran. Laristan,

Labadjan, Akbarabad, Busher, Shiraza na kwa jumla Iran ya Kusini yote ikaingia vitani. Watawala na maafisa wa serikali ya zamani waliondolewa na utawala ulioshikwa na watu wa kitaifa. Iran yote ikawa katika vita ya kutisha sana. Mfalme akaona hali hii mbaya ya nchi. Akaanza kuhamisha hazina na vitu vingine Urusi, yeye mwenyewe akabaki ili atumie busara yake kumaliza uasi ule. Lakini uasi uliendela tu. Mnamo mwezi wa Januari, 1909, ulikuwa umeenea mpaka Isphahan. Viongozi wa Bakhtiari pia wakajiunga na watu wa kitaifa. Majeshi ya mfalme yakashindwa vibaya sana. Mfalme akalazimika kutangaza kuwa amekubali serikali ya uwakala. Akawaambia watu mara nyingi ya kuwa serikali ya kizamani haitawekwa tena. Lakini Mwenyezi Mungu alikuwa amepanga vingine. Katika jumba la mfalme la Iran mashaka yalizidi siku baada ya siku. Hatimaye hata watu wa dini, washauri wa mfalme, walijiunga na watu wa kitaifa. Mfalme na ahli zake wakaliacha jumba lao na kukimbilia kwa Balozi wa Urusi. Hii ilikuwa mnamo mwezi wa Julai tarehe 15 mwaka 1909, miaka miwili na nusu baada ya kutangazwa kwa ufunuo "Matetemeko yametokea katika jumba la Kisraa." Ufunuo ulitimia sawasawa . Ufalme wa mtu mmoja ukatoweka kabisa Iran. na utawala wa Jamhuri ukasimamishwa. Miezi ya Juni na Julai ilipita katika mashaka makubwa. Wale tu waliopata kupitia hali hii wanaweza kuyafahamu mashaka, mahangaiko na kutokwa na matumaini kulikolifikia jumba la mfalme wa Iran katika miezi hiyo miwili. Inahitaji fikara sana kufahamu ni nini kilichotokea. Kwa hali yoyote, ni wazi kuwa bishara ya Masihi Aliyeahidiwa ilitimia. Ilikuwa ni ishara ijapokuwa ni wachache wanaonufaika kwa ishara kama hizi.

## BISHARA YA TATU:
## KIFO CHA ABDULLAH ATHAM

Bishara hii inayomhusu Abdallah Atham ni ishara kwa Wakristo kwa ujumla ma hususa Wakristo wa Bara Hindi. Sijui, msomaji mpenzi, kama unafahamu mashambulio mabaya sana yaliyofanywa

na wahubiri wa Kikristo siku hizo kinyume cha tabia ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mashambulio haya yalitumia zile itikadi zilizotiwa na Waislamu katika Islam, kadhalika baadhi ya hadithi za uongo zilizoingizwa katika vitabu vya Kiislamu. Wakati huo mashambulio haya yalifikia hadi ya ubaya wake. Sasa hayako hivi tena. Kwa kuchukizwa sana na upana wa mashambulio haya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akaazimia kulipa kisasi. Matokeo yalikuwa hivi ya kwamba Wakristo walijiona wanashindwa kusimama naye. Waliachilia mbali njia zao za kushambulia. Njia wanayoitumia sasa katika kuandika kuishambulia Islam ni tofauti. Miongoni mwa watukanaji mstari wa mbele kabisa alikuwa Abdallah Atham, aliyekuwa kwanza mtumishi serikalini, Ilitokea hivi ya kwamba munadhara kwa kuandika ulipangwa baina ya Hadhrat Ahmad na Abdallah Atham. Muhadhara huu ulifanyika Amritsar. Katika mnadhara Abdallah Atham alishindwa vibaya sana. ALidhalilika miongoni mwa Wakristo na wengine. katika munadhara huu likazuka suala la miujiza. Kwa suala hili, ilionekana ya kuwa Mwenyezi Mungu hakuuacha Muhadhara huu uende bila ya mwujiza. Hadhrat Ahmad akapokea ufunuo:

"Katika muhadhara huu upande wa mwongo, ambao umemwacha Mungu hasa na amabo, unatafuta kumfanya mtu kuwa Mungu utaangukia Motoni. Hili litatokea mnamo miezi 15, yaaani mnamo muda unaohesabika kwa kadiri ya mwezi mmoja kwa kila siku moja ya muhadhara huu, kwa sharti kwamba upande wa mwongo usielekee haki."

Katika karatasi yake ya mwisho ya majadiliano, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alitia bishara hii na akatangaza ya kuwa bishara hii itathibitisha kuwa Mtukufu Mtume s.a.w., ambaye Abdallah Atham alimtaja (Mungu apishe mbali) kuwa ni Dajjal katika kitabu chake Andruna-i-Bible, (yaani Hali ya Ndani ya Biblia), alikuwa Mtume wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

Bishara hii ilikuwa na sehemu mbili za maana sana:-

(1) Ni kwamba Abdallah Atham (aliyetafuta kuthibitisha kuwa Yesu ni Mungu), atakwenda Motoni kwa sababu ya chuki na matusi

yake; (2) kwamba kama atatubia na kutamka kosa lake, atasalimika ma adhabu hii. Au kama hakubadili fikara zake na kudumu katika uadui wake na matusi, na kisha asalimike na adhabu hii, bishara hii itakuwa ya uongo; kwa upande mwingie, kama akijibadilisha na bado afe tu mnamo miezi 15 kuanzia siku ya mwisho ya majadiliano, hata hivyo bishara itakuwa ni ya uongo. Maneno ya bishara yameainisha kuwa kwa elimu ya Mwenyezi Mungu, Abdallah Atham ilikuwa aishi umri mrefu zaidi ya miezi 15, lakini ilikuwa afe mnamo miezi 15 kama angeendelea na uadui wake. Kwa kufikiri kidogo maneno hayo yanaonesha kuwa hatua za pili zina adhama zaidi kuliko mbili za kwanza. Hatua mbili za kwanza ni kwamba kama Abdallah Atham ataendelea na uadui, basi atakufa mnamo miezi 15. Kwani Atham kuendelea na uadui lilikuwa jambo la kawaida kwake na jepesi. Alikuwa mwandishi wa Kikristo aliyeandika vitabu kuusaidia Ukristo katika kushambulia Uislamu. Alikuwa maarufu sana hata miongoni mwa Waingereza.

Kwa majadiliano baina ya Wakristo na Waislamu, alichaguliwa yeye kusimamia Ukristo badala ya Mapadre wengine na wahubiri. Wahubiri mashuhuri wa Kikristo walikuwa kama wasaidizi wake. Mtu huyu alitazamiwa kuendelea kushikilia itikadi zake za Ukristo. Kwa kufanya yote haya kwa kuueneza Ukristo na kuwa msemaji mkubwa wa Kikristo katika mjadiliano, mtu asingeweza kufikiri kuwa hata mara moja angerudisha nyuma itikadi yake juu ya uungu wa Yesu na kuathirika na nguvu ya kimwujiza ya Uislamu. Kusema kwamba katika hali ile angekufa mnamo miezi 15 inaonekana ni bishara kubwa sana. Lakini Atham alikuwa na umri wa miaka 65 na mtu mzee kama huyu anaweza kusemwa ametumia maisha marefu. Kama angekufa, isingeonekana kuwa ni ajabu. Bali fikiria sehemu nyingine. Kama Atham angeacha uadui wake, angesalimika na kifo mnamo miezi kumi na tano. Ilikuwa ni vigumu sana kwa Atham kutubia na kuacha mwendo wake kuuadui Uislamu. Na kwa kuwa kifo kinaweza kuletwa hata na mikono ya wanadamu, dhamana ya maisha kwa miezi kumim na tano haiwezi kutolewa na yeyote. Hatua ya sehemu ya pili ni wazi ilikuwa ngumu sana. Hatua hii iliweza kuifanya bishara iwe kubwa zaidi na ya kuvutia. Inaonekana ya kuwa Mwenyezi Mungu alichagua sehemu iliyo ngumu sana.

Atham, licha ya umaarufu wake na uhodari, aliogofywa na bishara hii. Alama yake ya kwanza ilitokea wakati Atham katika majadiliano aliweka vidole masikioni na kusema ya kuwa hakumwita Mtume s.a.w. Dajjal.

Baada ya kutangazwa bishara hii kila mtu akawa anatazamia matokeo yake. lakini Mwenyezi Mungu hakuacha miezi kumi na tano ipite bila ya alama zingine za kutubia kwa Atham. Atham aliacha kazi zake zote za kuusaidia Ukristo. Aliacha kusema na kuandika. Mhubiri mashuhuri na mwandishi hawezi mara moja kuwa kimya kabisa. Hivyo, Atham kufanya hivi, inaonesha kuwa Islam ilimvutia Atham kwa namna fulani akilini mwake, ya kwamba kwa kadiri fulani alifikiri kuwa ni kosa kushambulia, labda hata kupinga Dini Ya Islam. Lakini hakuonesha hivi kwa kunyamaza tu. Alipata maumivu makali sana ya ubongo, namna fulani ya moto. Mawazo ya uadui kwa Islam yakahama. Alianza kuona ndoto za ajabu na kuzisimulia kwa ndugu na rafiki zake. Aliota juu ya mijoka, mijibwa yenye wazimu, na mijitu yenye silaha tayari kumshambulia. Mambo haya hayawezi kuoneshwa kwa mtu kwa njia ya wanadamu. Mijoka na mijibwa haiwezi kutembezwa kwa ajili hii, na katika Bara Hindi kwa sababu ya marufuku ya kutumia silaha, mijitu yenye silaha isingeweza kuonwa katika safu namna ile. Ndoto hizi zilifanya namna fulani ya moto kwa Atham. Ilikuwa ni matokeo ya mawazo ya toba juu ya kusaidia Ukristo katika kuuadui Uislamu. Moto huu wa ubongo ulikuwa badala ya Moto wa kimwili ambao angeuingia, laiti angeendelea na uadui wake. Kama imani yake juu ya Ukristo ilibakia kama ilivyokuwa kwanza, kama angeendelea kuufahamu Uislamu kama dini ya uongo kama alivyoufahamu hapo kabla, asingetaabika kwa fikara na ndoto za namna ile. Kama aliendelea kuona kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja naye, kwa nini wanyama na wadudu hawa walionekana kwake vya kutisha sana? Kwa nini aliacha kuandika kote na kuhubiri kwa niaba ya Ukristo? Kwa nini alikuwa akienda toka mji mpaka mji kwa hofu?

Kwa ufupi, Mwenyezi Mungu alichagua kutimia kwa sehemu ya pili ya bishara, sehemu iliyotabiri toba ya Atham. Sehemu hii haikuwa na welekea wa kutimia. Atham akaanza kutia shaka juu ya

Yesu kuwa Mungu. Ukweli wa Uislamu ukaanza kuingia akilini mwake. kwa toba yake Mwenyezi Mungu alitimiza sehemu ya pili ya bishara hii. Atham alisalimika na kifo ijapokuwa woga na matisho yalimpeleka karibu yake. Ahadi ya Mungu ikawa ya kweli. Alisalimika kwa sababu alitubu.

Hii ilikuwa bishara kubwa sana ya kufaa kufumbua mamcho ya kila mtu. Lakini kama kusingefanywa chochote baada ya muda uliotajwa maadui wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wangeendelea kusema ya kuwa Atham hakufanya toba yoyote. Ilikuwa ni matengenezo ya Hadhrat Ahmad na wafuasi wake. Ili kuufanya ukweli wa bishara hii uwe zaidi hata kuliko kwanza, Mwenyezi Mungu akainua kikundi cha Wakristo na Waislamu kusema ya kuwa bishara ile imethibitika kuwa si ya kweli na ya kwamba Atham hakufa mnamo muda uliotajwa. Kwa kusema hivi wakaambiwa kuwa bishara hii ilikuwa itimizwe katika mojawapo ya njia mbili. Imetimia katika njia ya pili. Lakini maadui hawakukubali na wakaendelea kusema ya kuwa Atham hakutubia. Hadhrat Ahmad akamwita Atham atangaze kwa kiapo kwamba hao Wakristo na Waislamu walikuwa wakweli na ya kwamba katika muda wote huu hakuingiwa na hata chembe ya fikara juu ya ukweli wa Islam na ya uongo wa Ukristo. Atham akakataa kutangaza hivi kwa kiapo. Alitoa matamshi bila ya kiapo ya kuwa bado aliufahamu Ukristo kuwa ni kweli. Lakini, Alhamdu lillah, palepale akatangaza kwamba imani yake juu ya uungu wa Yesu ni tofauti na imani ya Wakristo wengine. Tangazo hili lilitimiza tu bishara. Kwani bishara ilisema kuwa upande uliotafuta kumfanya mtu kuwa Mungu utakwenda Motoni. Atham alikubali ya kuwa hakumfikiri Yesu Kristo kuwa Mungu. Licha ya tangazo hili, Atham aliulizwa kama atatangaza kwa kiapo ya kuwa hakuingiwa na mashaka yoyote juu ya ukweli wa itikadi za dini yake na ya kwamba ukweli wa Islam haukumwingia hata chembe na ya kwamba katika muda wote ule aliendelea kuamini yote aliyokuwa akiamini hapo kabla. Akimtaka Atham atoe tangazo hili kwa kiapo, Hadhrat Ahmad mwenyewe alitangaza kwamba kama Atham akitangaza vile kwa kiapo kisha asipate adhabu ya Mungu, basi yeye ni mwongo. Akaahidi pia hapo ya kuwa kama Atham akitangaza vile kwa kiapo atampa zawadi ya

rupia 1,000/- taslimu. Atham akatoa jawabu kwamba kuapa hakuruhusiwi katika dini yake. Hii ilikuwa ni ajabu kwa sababu katika Agano Jipya wanafunzi wa Yesu wanasemwa walifanya viapo vya namna mbalimbali. Katika serikali za Kikristo mtu hateuliwi kwa kazi kubwa ya madaraka mpaka awe ameapishwa. Hata mfalme ni lazima aape. Mahakimu, Wabunge, maafisa wakubwa wa serikali, wote wanalazimika kuapa. Mashahidi katika mahakama inawalazimu kuapa. Kwa weli, mahakama za Kikristo zinasisitiza kufanya kiapo kwa mashahidi wa Kikristo. Mashahidi wasio Wakristo husema tu, "Ninatamka mbele ya Mungu wa milele na mwonaji wa milele" n.k. Kwa hiyo, kama kupa, kwa mujibu wa Wakristo, ni haki maalumu ya Wakristo, Atham hangeweza kusema si halali katika dini yake. Hivyo kukataa kwake hakukuwa kwa uaminifu. Bali ilikuwa hila ya kukwepa kiapo na adhabu zake. Kwani aliona ishara za kutisha hata akafahamu kwa yakini kuwa angekula kiapo, lazima angekufa. Hivyo Atham kukataa kuapa vile kunadhihirisha zaidi kwa ukweli ya kwamba miongoni mwa Wakristo hakuna kazi yoyote ya maana inayopewa mtu yeyote mpaka ale kiapo cha utii. Wakristo wa Kilutheri, na Atham alikuwa Mlutheri, wao huwalazimu kuapa viapo viwili, kimoja cha utii kwa Kanisa na kingine cha utii kwa serikali. Mambo haya yalipoelezwa kwa Atham alinyamaza kimya kabisa. Zawadi aliyowekewa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kupewa kama angeweza kula kiapo ilipanda kutoka kwenye rupia 1,000/- mpaka rupia 4,000/- Aliwekewa muda wa mwaka mmoja. Atham angejichukulia zawadi ile kama angeapa. Lakini alijua ya kuwa kwa kuwaogopa watu wa dini yake alikuwa anajaribu kuficha hali ya akili yake aliyoitaabikia sana kwa miezi kumi na tano. Kwa kufahamu haya yote hakuthubutu kula kiapo. Akatumia siku zake zote zilizobaki akiwa kimya kabisa. Kuandika kwake kote na kuhutubu kushambulia Uislamu kukakoma. Kuhubiri Ukristo vilevile kukakoma. Ukweli wa bishara ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ukawa wazi kuliko kwanza. Kuacha kwa Atham imani yake juu ya uungu wa Yesu, kwa namna fulani, kumethibitishwa na Atham mwenyewe. Ya kwamba fikara zake za kwanza juu ya Islam zilibadilika ilithibitishwa kwa kukataa kwake kuapa na kwa jawabu lake alipoitwa aape; (Kwani katika moja wapo ya karatasi zake katika

majadiliano mwishoni ambako kwao bishara hii ilitolewa, Atham alijaribu kuthibitisha kuwa Kristo alikuwa Mungu na ya kwamba alikuwa na sifa zote za Mwenyezi Mungu).

Adham ya bishara hii inahuisha imani ya kila mtu mwaminifu. Katika hii mtu anaweza kuona kazi ya Mkono wa Mwenyezi Mungu. Alikuwa adui mkubwa wa Islam, kiongozi wa jamia mashuhuri, msemaji katika majadiliano. Alitumia maisha yake marefu katika kuhubiri dini moja na kuitukana nyingine. Mtu huyu akaingiwa na shaka juu ya dini yake mwenyewe na kuipendelea nyingine. Hasimu mgumu huyu alipata ndoto za kutisha vilevile. Kwa kufikiria badiliko hili la fikara akasalimika na kifo kwa miezi kumi na tano kamili. Mambo haya ni kinyume na uwezo na mpango wa mwanadamu.

## BISHARA YA NNE: MWONGO WA AMERIKA

Hii inahusu kifo cha Dowie, mwongo wa Amerika. Ni ishara kwa Wakristo kwa ujumla na hususa kwa Waamerika.

Sasa nitaendelea kueleza bishara iliyokuwa ni ishara kwa Wakristo kwa ujumla. Pamoja na kuwa ishara kwa Wakristo, pia ni ishara kwa watu wa Magharibi. Alexander Dowie alijulikana sana Amerika. Alizaliwa Australia na kuwa raia wa Amerika. Mnamo mwaka 1892 akaanza kuhubiri. Alijidaia uwezo wa kuponya maradhi, na watu walikuwa wakimkusanyikia. Mnamo mwaka 1901, alidai kuwa mtangulizi wa kufika mara ya pili kwa Kristo, kama alivyokuwa Eliya mtangulizi wa kufika kwake mara ya kwanza. Hapo kufika kwa Kristo mara ya pili kukawa suala la kufikiriwa sana. Ishara zilizoandikwa zimedhihiri na watu wenye hamu ya dini wakakungoja kwa shauku. Tangazo la madai yake likamletea Dowie wafuasi zaidi. Alinunua sehemu fulani ya ardhi na kuanzisha mji ulioitwa Zion. Akatangaza ya kuwa Kristo atashukia katika mji ule. Matajiri wengi, kwa shauku ya kuona kuja kwa Kristo, walilipa

fedha nyingi kwa ardhi ile ili wajenge majumba katika mji ule. Dowie akaanza kutawala mji ule mzima kama mfalme asiyetawazishwa. Si muda mrefu wafuasi wake wakafikia 100,000. Alituma wahubiri katika nchi mbalimbali za Kikristo. Akiuchukia sana Uislamu alianza kuutukana vibaya sana. Mnamo mwaka 1902, alitangaza bishara kwamba Waislamu wote wa duniani kama hawatakuwa Wakristo basi watapata mahilikisho. Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa, akasikia na kuandika kijitabu cha jawabu. katika kijitabu hiki Hadhrat Ahmad alieleza fadhili za Islam na kusema kwamba haikuwa na maana kwa Dowie kutabiri hilaki ya Waislamu. Kwani yeye (Hadhrat Ahmad) ametumwa na Mwenyezi Mungu kuwa Masihi Aliyeahidiwa. Kwa hiyo Dowie aingie katika mashindano ya dua pamoja naye. Matokeo ya dua yatawawezesha watu wote wa duniani kufahamu ukweli. Kijitabu hiki kilitangazwa mnamo mwezi Septemba mwaka 1902, kwa wingi sana katika Amerika na Ulaya. Tokea mwezi wa Desemba mwaka 1902 mpaka mwishoni mwa mwaka 1903, magazeti ya Amerika na Ulaya yaliendela kufafanua maneno ya kijitabu cha Masihi Aliyeahidiwa. Karibu waandishi arobaini walipeleka nakala za magazeti yao Qadian yaliyokuwa na maelezo yao juu ya kijitabu cha Masihi Aliyeahidiwa. Kwa kutazama jinsi tangazo hili lilivyozagazwa magazetini, inaweza kusemwa ya kuwa karibu watu milioni mbili na nusu walijua juu ya shindano hili la dua.

Dowie hakuandika jawabu la kijitabu hiki; bali aliendela kuomba dua ya kuanguka na kuhiliki kwa Dini ya Islam. Kadhalika alijadidisha mashambulio yake. Mnamo mwezi wa Februari tarehe 14 mwaka 1903, akaandika katika gazeti lake: "Ninamwomba Mwenyezi Mungu kwamba Islam itoweke haraka duniani. Ee Mola, nikubalie dua yangu hii. Ee Mola, iangamize Islam."

Tena, mnamo mwezi wa Agosti tarehe 5 mwaka 1903, akaandika gazetini mwake: "Doa jeusi kwenye nguo ya mwanadamu (Islam) litaukuta mwisho wake katika mikono ya Zion."

Hadhrat Ahmad akaona kwamba Dowie hakuelekea kulegeza uadui; kwa hivi akaandika kijitabu kingine wakati fulani katika mwaka 1903. Kijitabu hiki kiliitwa Bishara juu ya Dowie na Piggot. Piggot alikuwa mwongo pia katika Uingereza. Hadhrat Ahmad

aliandika katika kijitabu hiki ya kuwa alitumwa na Mwenyezi Mungu ili kuimarisha tena imani juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu, kukomesha kila namna ya shirki; ya kwamba alipewa ishara fulani kuonesha katika Amerika. Ishara yenyewe ni hii ya kuwa Dowie aingie katika mashindano ya dua pamoja naye na kwamba kama akiamua, kwa njia hii au ile, kukubali wito huu, basi Dowie ataiaga dunia kwa maumivu makali na udhalilifu kabla ya Masihi Aliyeahidiwa. Akaendelea kusema ya kuwa Dowie aliitwa kwenye shindano hili kabla, lakini hakutoa jawabu. sasa anapewa muda wa miezi saba zaidi. Katika muda huu wote anaweza kutoa jawabu lake. Akamaliza kwa kusema ya kuwa "Muwe na hakika ya kuwa msiba hauna budi kuiangukia Zion Ya Dowie."

Hatimaye, bila ya kungojea jawabu la Dowie aliomba: "Ee Mola. Amuru ya kuwa uongo wa Piggot na Dowie uwadhihirikie watu haraka."

Kijitabu hiki pia kilienezwa katika Ulaya na Amerika kwa wingi mno. Magazeti ya huko yakatoa maelezo juu yake. Glasgow Herald la Uingereza na New York Commercial Advertiser la Amerika yalitoa maelezo juu ya kijitabu hiki. Watu mamilioni wakawa na habari hii.

Zama kijitabu hiki kilipotangazwa, nyota ya Dowie ilikuwa imestawi barabara. Idadi ya wafuasi wake ilikuwa ikiongezeka. Walikuwa matajiri sana hivi kwamba Dowie kila mwaka mpya walimpelekea zawadi zenye thamani ya dola elfu mia moja. Dowie mwenyewe alikuwa na viwanda vingi. Akiba yake katika benki ilifikia dola karibu milioni ishirini. Watumishi wake walikuwa wengi kuliko watumishi wa tajiri yeyote yule. Alikuwa mwenye afya ya kutosha sana. Afya, alisema, ilikuwa mwujiza wake maalumu. Alidai mwujiza wa kuponya maradhi kwa kugusa tu kwa mkono wake. Dowie alikuwa na mali, afya, wafuasi, mvuto, na kila kitu kwa wingi sana.

Baada ya kutangazwa kijitabu cha Hadhrat Ahmad, watu walimwuliza Dowie mbona hukumjibu Masihi wa Kihindi? Dowie akasema kwa dharau sana:

"Kuna Masihi Muhammadiyya katika Bara Hindi ambaye mara nyingi ameniandikia kuwa Yesu Kristo amezikwa Kashmir na watu

wananiuliza kwa nini simjibu. Mnadhani ya kuwa nitawajibu wadudu na nzi hao? Kama niweke kisigino changu juu yao naweza kupoteza mara moja maisha yao. ninawapa fursa waruke na kuishi."

Kijinga kabisa, Dowie huyu, ambaye alikataa kutoa jawabu la mashindano na Hadhrat Ahmad, sasa kaliingia shindano hilo, ijapokuwa aliendelea kusema kwamba hakuliingia. Alisahau kwamba Hadhrat Ahmad aliandika waziwazi ya kuwa hata kama Dowie aingie shindano hili kwa njia hii au ile, ataiaga tu dunia kwa maumivu makali sana na udhalilifu, katika uhai wa Hadhrat Ahmad. Dowie alimwita Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad kuwa mdudu na kwamba angeweza kumwua kwa kisigino chake. Kwa namna hii Dowie akawa ameliingia shindano na kuiita adhabu ya Mwenyezi Mungu.

Kiburi na majivuno ya Dowie yakaongezeka. Baadaye tena akamsema Hadhrat Ahmad kuwa "Masihi Muhammadiyya mpumbavu." pia akaandika: "Kama mimi si mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika ardhi hii, basi hakuna ambaye ni mjumbe." Mnamo mwezi wa Desemba mwaka 1903, akaingia kinaganga katika mashindano. Alitangaza ya kuwa malaika walimwambia ya kuwa atakuwa mshindi juu ya maadui zake. Tangazo hili lilikuwa bishara ya kifo cha Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Shindano la kiroho lililokuwa likiendelea polepole, sasa likawa dhahiri kabisa. Baada ya tangazo hili la mwisho, Masihi Aliyeahidiwa hakuandika chochote kama ilivyofundishwa na Quran Tukufu ya kuwa "Na subiri kama wanavyosubiri wao," akingojea hukumu ya Mwenyezi Mungu. Mungu ni mwenye subira lakini madhubuti katika mkamato Wake. Basi naam, mshiko wa Mwenyezi Mungu ukamshika miguu Dowie, aliyetaka kumsagia nayo Masihi Aliyeahidiwa wa Mwenyezi Mungu. Miguu ya Dowie ikadhoofika. Wachilia mbali kumsagia nayo Masihi Aliyeahidiwa, haikuweza hata kuikanyaga ardhi. alikuwa amepata ugonjwa wa kupooza. Baadaye kidogo alipata ahueni. Lakini baada ya miezi miwili tena, yaani, Desemaba 19, akapata ugonjwa tena. Aliumwa sana hivi kwamba kazi yake alimwachia mwandishi wake, na yeye mwenyewe akaenda kwenye kisiwa fulani kilichodhaniwa kuwa kina hewa nzuri ya kuweza kuponya ugonjwa wa kupooza. Lakini ghadhabu ya Mwenyezi

Mungu ilimwandama. Dowie alisema Masihi wa kweli alikuwa mdudu. Nguvu ya kimwujiza aliyokuwa akijigamba nayo ikaaza kumtupa. Alipokwisha ondoka nyumbani kwake, huku nyuma wafuasi wake wakaanza kustaajabu mbona huyu aliyekuwa na uwezo wa kuponyesha hakuweza kujiponya mwenyewe? Naye hakuhitaji hata kuomba dua bali kugusa tu. Kwa nini anaumwa tena? Wakaanza kupekuapekua vyumbani mwake ambamo mlikuwa hamwingiliki. Wakakuta chupa za pombe. Mke wake na wanawe wakasema ya kuwa Dowie alikuwa akinywa sana pombe ijapokuwa alikuwa akiwakataza wafuasi wake wasinywe pombe kabisa. Alikuwa amekataza hata tumbaku. Mkewe huyu akaeleza kuwa alikuwa akimtii sana Dowie hata katika siku zake za umaskini, lakini alifadhaika sana kufahamu kuwa Dowie kwa kumwoa mwanamke mzee tajiri vile, ameanza kusema kuwa halali kuoa zaidi ya mke mmoja. Kwa kutangaza sheria hii aliona udhuru katika kosa la kuoa zaidi ya mke mmoja. Mke huyu akaonesha barua ambazo huyo mwanamke mwingine alikuwa akimwandikia Dowie kuwa majibu ya barua zake. Wafuasi wake wakaghadhibika sana. Wakaamua kuchungua hesabu ya fedha za Jumuiya ya Dowie. Ilionekana kwamba Dowie alichukua karibu dola milioni moja na nusu. Kadhalika ikabainika ya kuwa alitoa zawadi kiasi cha rupia 100,000/- kwa wasichana wa mji huo. kwa ufichuzi huu wafuasiw ake maarufu wakaamua kumtoa uongozini. Wakampelekea simu iliyosema: "Kwa umoja Jumuiya inapinga kwa nguvu desturi yako ya ubadhirifu, unafiki, uongo, maneno ya chumvi, dhulma, unyang'anyi na ukorofi wako. Kwa hiyo, hivi sasa unatolewa katika kazi yako."

Dowie hakuweza kupinga maneno haya. hatimaye wafuasi wake wote wakamkataa. Akataka kuwahutubia ili wamrudie tena. Lakini alipoteremka katika kituo cha gari moshi, ni watu wachache sana walikuja kumpokea. Hakuna aliyejali kumsikiliza. Akaenda mahakamani, lakini mahakama haikumsaidia kupata fedha zozote katika fedha za Jumuiya. Hivyo akapata zawadi ya huzuni kubwa. Kwa upande mwingine, ugonjwa wake wa kupooza ulikuwa umemzidi vya kutosha. Watumishi wake wa Kinegro walikuwa wakimbeba toka chumba mpaka chumba. Aliishi peke yake na

maumivu makali sana. Katika muda huu ni marafiki zake wachache sana ndio walikuwa wakimkaguakagua. Walimshauri kupata matibabu sawasawa, lakini hakukubali. Alijua ya kuwa yeye mwenyewe alikuwa akiwakataza watu kutumia dawa. Angewezaje yeye tena kutumia dawa? Baadaye miongoni mwa wafuasi 100,000, akabakiwa na wafuasi 200 tu. Alishindwa katika mahakama. Ugonjwa wake uliendelea. Hakuweza kukomesha tabu zake hizo. Alipoteza kabisa akili yake na akawa mwenda wazimu kamili. Katika hali walipomwendea baadhi ya wafuasi wake ili kusikiliza wa'dhi wake walimkuta amefungasha lundo la mavitambaa mwilini pake. Dowie akasema jina lake ni Jerry! Ya kwamba usiku uliopita alikuwa amepigana na Shetani! Ya kwamba katika vita generali wake mmoja aliuawa! Ya kwamba yeye mwenyewe alipata majeraha kidogo! Waliposikia haya wakajua ya kwamba Dowie amekuwa mwehu. Wafuasi wake waliokuwa amebakia nao pia wakatoka. Hapo maneno ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad yakatimia. Yeye alisema kabla ya kuwa Dowie ataiaga dunia kabla yake "Kwa maumivu makali na udhalilifu." Katika mwaka 1904 mwezi wa Machi tarehe 8, Dowie akaiaga dunia, akiwa aliyeachwa na kufedheheka. Alipokuwa alikuwa na watu wanne tu pamoja naye na rasilimali yake ilikuwa rupia 30 tu!

Taswira mbaya sana ya maumivu na udhalilifu isiyoweza kudhaniwa. Kifo cha Dowie kilikuwa somo na ishara kwa ajili ya watu wa Magharibi. Magazeti mengi yakatangaza ya kuwa bishara ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad imetimia. Yakaandika:

"Ahmad na wafuasi wake wanaweza kusamehewa ikiwa watajivunia bishara ambayo imetimia sawasawa miezi michache iliyopita" (Dunville Gazette, June 7, 1904).

"Mtu wa Qadian alitabiri ya kuwa kama Dowie akikubali wito wa mashindano "ataiaga dunia mbele yangu kwa huzuni na maumivu." La, akikataa, Mirza alisema: "Hatima haitageuka; kifo kitamngoja polepole, na msiba utauingia mji wa Zion hivi karibuni." Hii ilikuwa bishara kubwa: Zion kuanguka na Dowie kufa kabla ya Ahmad. Ilionekana ni hatua ya kujihatarisha kwa Masihi Aliyeahidiwa kumtaka Eliya aliyefufuka kushindana juu ya uhai, kwani Ahmad alikuwa miaka 15 zaidi kuliko Dowie na kulikuwa

hakuna matumaini ya kuishi zaidi kwa vile aliishi nchi ya tauni, lakini alishinda" (Trurh Seeker, June, 15, 1904).

"Dowie alikuwa hali ya kuwa marafiki zake walimkimbia na bahati yake ilipungua. Aliugua ugonjwa wa kupooza na wenda wazimu. Alikufa kifo cha huzuni, hali ya kuwa mji wa Zion umechanwa na kuvunjwa kwa mafarakano ya watu. Mirza anatokea uwanjani mkunjufu na kusema ya kuwa amefaulu katika wito wake wa mashindano" (Herald of Boston, June 23, 1904).

Maneno haya kutoka katika magazeti ya Amerika yanaonesha ya kuwa bishara hi haikuwavutia Wakristo tu bali pia wahariri wa magazeti ya Amerika. Walivutiwa na adhma ya bishara hii hivi kwamba waliona wanashurutishwa kuandika juu yake. Hawakuwa na uwezo wa kupinga ukweli wake au ubora wake. Kila inaposimuliwa ishara ya kifo cha dowie mbele ya watu wa Magharibi, watapata ushahidi wa magazeti mengi, yaliyoandikwa na watu wa nchi zao na imani yao. Watu wa magharibi kwa kusikia juu ya Ishara za namna hii, watalazimika kukubali ya kuwa Islam ni dini ya kweli. Ya kwamba wokofu haupatikani nje ya Islam. Kwa kuhakikishiwa hivi watatupilia mbali imani zao za kizamani. Wataingia Islam na kutangaza imani yao juu ya Mtukufu Mtume wa Islam s.a.w., na mtumishi wake, Masihi Aliyeahidiwa a.s. Matukio ya mbele huonesha vivuli vyake kabla. Katika Amerika, watu mia mbili wamekwisha jiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya.

## BISHARA YA TANO
### KIFO CHA LEKHRAM ISHARA KWA WAHINDI

Sasa ninaelekea bishara nyingine; moja miongoni mwa nyingi zilizothibitisha ukweli wa Islam kwa watu wa Bara Hindi. Kutimia kwake kuliwastaajabisha malaki ya watu na kuwahakikishia ukweli wa Islam na kuwashawishi wengi wao kutangaza kinaganaga ya kuwa Islam ni Dini ya kweli. Athari ya bishara hii imeendelea tangu wakati huo mpaka sasa.

Sababu zenyewe za bishara ni kwamba mwishoni mwa karne iliyopita kulianzishwa firka moja ya Wahindu iitwayo Arya Samaj. Kwa kuona udhaifu wa Islam siku hizo, firka hii ilipanga mpango mkubwa wa kuwaingiza Waislamu kwenye Uhindu. Wakati huo waandishi wa Arya Samaj wakaanza kuandika mashambulio ya matusi hadi ya matusi juu ya Islam. Mkubwa kabisa wa waandishi hao alikuwa Lekh Ram. Kwa njia ya kuandikiana mara kwa mara, Hadhrat Ahmad alijaribu kumweleza kiongozi huyu wa Kiarya ukweli wa Islam. Lakini hakuathirika. Lekh Ram alishikilia uzi wake uleule wa kuutukana Uislamu. Akatoa tafsiri mbaya kweli kweli za sehemu fulani za Quran. Watu wa kawaida waliweza kuzisoma tafsiri hizo. Alishika maoni machafu mno juu ya Mtukufu Mtume s.a.w. na Quran Tukufu. Mbora wa wanadamu, alimfikiri kuwa mbaya wa wanadamu. Kitabu bora kabisa alikifikiri kibaya sana katika vyote. Jicho linaloumwa haliwezi kustahamili mwangaza. Hii ndiyo ilikuwa hali ya Lekh Ram. Kubishana naye kukaanza kupanda. Lekh Ram akaendelea mbele na mbele kumtukana Mtume s.a.w. na kumdhihaki Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Basi kiongozi huyu akadhihiri kuwa ishara. Hadhrat Ahmad akamwomba Mwenyezi Mungu na akafunuliwa ya kuwa kifo cha Lekh Ram kiko karibu. Kabla ya kutangaza bishara hii Hadhrat Ahmad aliahidi kuacha kutangaza bishara hii ikiwa Lekh Ram alikuwa na hoja yoyote. Lakini Lekh Ram alisema ya kuwa hakuwa na cha kuogopa katika bishara kama hizi. Kwa hali yoyote, ufunuo aliokuwa akipata kwanza juu ya bishara hii haukuwa umetaja wakati wowote wa kufa kwa Lekh Ram akasisitiza kutaka uelezwe wakati. Kwa hivi Hadhrat Ahmad akaacha kwanza kutangaza bishara hii akingojea kupata elimu zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mara akafunuliwa ya kuwa Lekh Ram atakufa miaka sita tokea tarehe 20 mwezi wa Februari mwaka 1893. Baada ya kupata ufunuo huu Hadhrat Ahmad akatangaza bishara hii. Akaiongezea ufunuo mmoja wa Kiarabu kuhusu Lekh Ram.

"Maskini ndama aliye ni nusu mfu anabwata; hakuna kimngojeacho isipokuwa huzuni na adhabu." Yaani, ni ng'ombe tu asiye na uhai wa kiroho, wala hana maneno ya maana ila kupiga kelele za bure.

Akitangza bishara hii Hadhrat Ahmad aliandika (kwa firka za dini zote): "Kama katika miaka sita tokea Februari tarehe 20, mwaka 1893, mtu huyu hakukutana na adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ambayo si ya kawaida katika uchungu wake na huzuni na ambayo itawajaza watu hofu ya Mwenyezi Mungu, basi kila mtu afikiri kuwa sitoki kwa Mwenyezi Mungu."

Baadaye kidogo, Hadhrat Ahmad aliiongezea bishara hii ufunuo mwingine. Aliandika:

Na Mwenyezi Mungu alinipa habari ya kuwa nitashuhudia siku ya 'Id, na siku hii itakuwa karibu sana na 'Id."

Aliendela:

"Na miongoni mwa fadhiliza Mwenyezi Mungu, ambazo nimepata, ni kwamba amekubali maombi yangu kuhusu Lekh Ram wa Peshwar na kwamba ameniarifu ya kuwa hivi karibuni atakutana na kifo chake. Mtu huyu alikuwa mbaya sana kwa kumtukana Mtukufu Mtume s.a.w. na alikuwa adui wa Mungu na Mtumewe. Niliomba juu yake. Hivyo Mola wangu akaniarifu ya kuwa mtu huyu atakufa mnamo miaka sita ijayo. Katika haya mna ishara kwa watafutao ukweli."

Tena, Hadhrat Ahmad akaongeza maelezo mengine. Haya yalichapishwa kama habari ndani ya kitabu chake Barakaat-ud-Duwaa. Yalitiliwa kichwa cha maneno "Bishara nyingine juu ya Lekh Ram wa Peshwar." Ndani yake aliandika:

"Leo Aprili tarehe 2 mwaka 1893 A.D. (Ramadhani tarehe 14 mwaka 1310), asubuhi mapema siku ya Jumapili, usingizini, nilijiona

nimekaa katika nyumba kubwa, nikiwa na baadhi ya marafiki. Kwa ghafla mbele yangu nilimwona mtu mmoja mwenye kutisha sana akiwa na macho yaliyomwiva. Nilivyomwona, alionekana kuwa kiumbe wa ajabu, wa aina ngeni kabisa. Nilifikiri sio mwanadamu, bali malaika mkali mwenye kutisha sana. Aliwaogopesha waliomwona. Nilipomtazama, aliuliza, "Yuko wapi Lekh Ram?" Halafu akamtaja mtu mwingine na kuniuliza pia yuko wapi. Halafu nikafahamu ya kuwa mtu huyu ameteuliwa ili kumwadhibu Lekh Ram na huyu mtu mwingine."

Hadhrat Ahmad aliandika pia katika kitabu chake Ainai-Kamaalaati-Islam kwa ushairi:

"Ee adui mpumbavu na uliyepotea, Uogope upanga mkali wa Muhammad.

Mkanaji wa utukufu wa Muhammad, na wa nuru ing'aayo ya Muhammad.

Mwujiza unaweza kuonekana ni hadithi, hebu basi njoo uone mwujiza mmoja kwa mtumishi wa Muhammad."

Bishara kuhusu Lekh Ram zikikusanywa pamoja zilitabiri:

(1) kwamba Lekh Ram atapata msiba mkubwa na mwishowe atakufa;
(2) kwamba msiba huu utatokea mnamo miaka sita;
(3) kwamba utatokea siku ya karibu na 'Id, kabla au baada yake;
(4) kwamba atapata msiba wa Ndama wa Samiri; yaani, kuchanwachanwa na kufa na kuchomwa moto na majivu kutupwa mtoni;
(5) kwamba msiba huu utaletwa na mtu mmoja mwenye kutisha na macho mekundu;
(6) kwamba Lekh Ram atauawa kwa upanga wa Muhammad.

Maelezo haya yako dhahiri hivi kwamba hakuna anayeweza kuwa na shaka yoyote juu ya maana yake. Miaka mitano baada ya kutangazwa kwa bishara hizi, watu wakaanza kumcheka Masihi Aliyeahidiwa. Wakati wa kutimia bishara hizi, walisema, ulikuwa unapita na hakuna kilichotokea! Je, Mirza Ghulam Ahmad anaweza kuwa mkweli? "Id-ul-Fitri ya pili ilitokea siku ya Ijumaa. Mnamo

siku ya pili baada ya siku ya 'Id, yaani Jumamosi, mchana mtu mmoja asiyejulikana alimchoma tumboni Lekh Ram kwa kisu kikali. Baada ya kuchomwa Jumamosi akafa Jumapili. Neno la Mwenyezi Mungu likatimia sawasawa. Bishara iliweka miaka sita. Lekh Ram akafa mnamo miaka sita. Bishara ilisema siku hiyo ya msiba itakuwa karibu sana na 'Id, na ya kwamba siku hii itaonesha kuwa furaha ya Waislamu. Ikatokea vilevile. Lekh Ram akachomwa kisu siku iliyofuata siku ya 'Id. Bishara ilisema ya kuwa Lekh Ram atakufa kwa mikono ya mtu mwenye macho mekundu. Hivi hasa ndivyo ilivyotokea. Lekh Ram ilikuwa auawe kwa upanga wa Muhammad; hivyo akafa kwa kuchomwa. Bishara ilisema Lekh rama atapata msiba kama ule wa Ndama wa samiri. Ndama huyu alitumbuliwa Jumamosi, alichomwa mpaka kuwa majivu, na majivu yakamwagwa mtoni. Hivi ndivyo ilivyotokea kwa Lekh Ram. Kwa kuwa alikuwa Mhindu alichomwa moto na majivu yake yakatupwa mtoni.

Hadithi ya kifo cha Lekh Ram, kama inavyosimuliwa, ni kwamba wakati fulani kabla, mtu fulani mwenye macho mekundu alifika kwa Lekh Ram, akitaka aingizwe katika Uhindu toka kwenye Uislamu. Watu walijaribu kumzuia asimkaribishe mtu huyu. Lakini Lekh Ram hakukubali. Mtu huyu akawa mfuasi mwaminifu sana kwa Lekh Ram. Lekh Ram alikuwa amechagua siku ya Jumamosi iwe ndiyo siku ya kumwingiza katika dini yake. Lekh Ram alikuwa akiandika. Akaomba kitabu fulani. Mtu huyu akijifanya mwenye kumpa Lekh Ram kile kitabu, alimchana tumboni kwa kisu, na akakizungusha mara nyingi humo tumboni ili kuyakatakta amtumbo vizuri. halafu akatoweka. Haya ndiyo waliyosema ahali zake Lekh Ram mwenyewe. Lekh Ram alikuwa katika ghorofa ya juu ya nyumba. Karibu ya gati, nyumba ya chini kulikuwa na watu wengi; lakini hakuna aliyemwona muaji akishuka na kukimbia. Mama na mke wa Lekh Ram walikuwa na hakika kuwa mwuaji alikuwa bado yumo ndani ya jumba lile. Wakapekuapekua bila ya kumwona. Alikimbilia wapi? Mbinguni au ardhini? Lekh Ram akafa kwa maumivu makali siku ya Jumapili. Siku moja ya Jumapili Masihi Aliyeahidiwa alimwona katika njozi mtu yule aliyemwuliza Lekh Ram. Kifo cha Lekh Ram kilikuwa ni ishara ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa, onyo la mbingu kwa wale ambao wangemtuka Mtume s.a.w.

# BISHARA YA SITA
## MWANA MFALME DALIP SING
## ISHARA KWA MASINGASINGA

Sasa nitaeleza bishara nyingine ambayo ilidhihiri kuwa ishara kwa ajili ya Masingasinga na iliyowaonesha ukweli wa Islam na Masihi ALiyeahidiwa.

Ilitokea hivi ya kwamba Waingereza walipoitwaa Panjab, walishauri kumhamisha mwanae Mfalme Dalip Singh, aliyekuwa mwenye kurithi utawala huo, na kumpeleka Uingereza angali mtoto. Ilikuwa akae huko mpaka dola ya Waingereza ilipokomaa katika Panjab. Baada ya maasi ya mwaka 1857, masalia ya dola ya Kimughali yalitoweka kabisa katika Delhi na hapo kila kitu kikawa salama kwa Waingereza. Raja Dalip Singh akaomba arudishwe Panjab na hata uvumi ulienea kwamba kijana Dalip atarudi. Wakati huo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akapata ufunuo kwamba mwana wa kifalme Dalip hatarudi. Aliwahadithia watu wengi habari hii na hasa Mabaniani. Katika mojawapo ya vijitabu vyake alieleza ya kuwa mtawala huyo atapata msukosuko. Wakati wa kutangazwa bishara hii hakuna aliyedhani ya kuwa Dalip angezuiwa kurudi kwao. Kwa kweli, ilifahamika kuwa si muda mrefu angekanyaga ardhi ya kwao. Lakini wakati huohuo Waingereza wakabadili mawazo yao. Waliona ya kuwa kurudi kwa Raja Dalip nyumbani kwao kutaleta hatari kwa serikali. Kadiri habari za kurudi kwake zilivyoenea, Masingasinga walichekelea zaidi na zaidi. Mawazo yao yakarudi kwenye mambo yao ya zamani na kutaka kuleta mapinduzi. Watawala wa Kiingereza wakaanza kuogopa ghasia. Meli iliyompeleka mwana wa kifalme ilifka Aden. Akasimamishwa palepale na kurudishwa Uingereza. habari za badiliko hili zilifika wakati ambao kila mtu alikuwa akimtazamia Raja dalip kuwasili nyumbani. Masingasinga wakahuzunika sana. Uwezo wa Mwenyezi Mungu ukajidhihirisha. Mwenyezi Mungu alijua mawazo ya Waingereza kabla wao hawajujua wangewaza nini.

# BISHARA YA SABA
## UGONJWA WA TAUNI

Nimeeleza bishara za Masihi Aliyeahidiwa kuhusu Afghanistan na jirani yake Iran. kadhalika bishara nne zinazoweza kusemwa zimemaliza hoja ya Islam juu ya jamia tatu mashuhuri za Bara Hindi (Wakristo, Wahindu na Masingasinga). Sasa nitaelekea bishara iliyokamailisha hoja yake juu ya jamia zote za Bara Hindi, na pengine dunia nzima. Bishara hi ilithibitisha ya kuwa Mwenyezi Mungu anao uwezo juu ya kila kitu. Anapopenda anaweza kugeuza vitu fulani kumtumikia Mjumbe wake. Bishara nyingi za Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad zilikwisha timia. Nyingi zingine zinangojea kutimia. Kwa kutoa mfano wa bishara hizi nitaeleza bishara yake kuhusu ugonjwa wa tauni. Katika bishara hii kuna shabaha moja zaidi. Nayo ni kwamba ugonjwa huu umetajwa katika bishara za Mtume s.a.w. aliyetabiri ya kuwa ugonjwa wenye kuangamiza utadhihiri wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. Zama, kwa mujibu wa bishara ya Mtume s.a.w., mwezi ulipatwa mnamo tarehe 13 ya mwezi wa ramadhani na jua likapatwa tarehe 28 ya Mwezi huo, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alijulishwa ya kuwa kama watu hawatatanabahi kwa ishara hii ya maana sana na hawatamkubali, watapata adhabu ya mbingu isiyo kifani.

Akaandika:

"Kupatwa kwa jua na mwezi kulikuwa ni ishara mbili zenye kutisha. Kupatwa kwao katika mwezi mmoja ni onyo kali la Mwenyezi Mungu na linaashiria ya kuwa adhabu imewekwa tayari watakayoipata wale watakaoendelea na uadui."

(*Nur-ul-Haq,* sehemu ya pili).

Alilazimika kuomba kutokea kwa ugonjwa huu. Katika mojawapo ya mashairi yake ya Kiarabu ameandika (1894).

"Zama ufasiki uangamizao ulipofikia hadi ya ubaya wake,
kama vile mfuriko unapofikia upeo wa kufurika,
Nilipenda laiti tauni ingekuja kuangamiza; Kwani,
mbele ya watu wenye akili, ni aula zaidi watu kuhiliki,
kuliko kuingia katika upotevu wenye kutia hasara.

Kadhalika katika kitabu chake *Siraaj Muniir,* aliandika ufunuo wake:

"Ee Masihi wa wanadamu, tuokoe katika magonjwa yetu.

Akielezea juu ya ufunuo huu aliandika:

"Ngojeni na mwone, ni kwa vipi na ni lini maonyo haya yatatimia. Kuna nyakati ambapo dua huleta kifo, na nyakati ambapo dua huleta uhai."

Wakati bishara hii ya mwisho ilipotangazwa, tauni ilikuwa imekwisha dhihiri tayari katika Bombay. Ilikaa huko kwa mwaka mmoja kisha ikatoweka. Kulikuwa na wazo la utulivu ya kwamba kuenea kwake kulikuwa kumeharibiwa na matibabu. Lakini onyo la Mwenyezi Mungu liliashiria kwingine. Wakati watu wote walipotulizwa kwa kuamini kwamba tauni ilikuwa imekuja na kuondoka, zama Panjab, isipokuwa kijiji kimoja au viwili, ilipoonekana isalama, zama katika Bombay madhara yake yalikuwa yamekoma. Masihi Aliyeahidiwa aliandika tangazao:

"Ninalazimika kuandika juu ya jambo la maana sana na hii ni kwa sababu ya huruma nyingi niliyo nayo. Ninafahamu ya kuwa wale wasio na macho ya kiroho wataelekea kudhihaki maneno yangu. Lakini hata hivyo kwa sababu ya kuwahurumia, ni wajibu wangu kuwaonya watu. Onyo lenyewe ni hili: Leo tarehe 6 mwezi wa Februari mwaka 1898, Jumapili, niliona katika ndoto ya kuwa Malaika wa Mwenyezi Mungu walikuwa wakipanda miche myeusi katika sehemu mbalimbali za Panjab. Miche hiyo ilionekana kuwa mibaya sana, inatisha kwa kuitazama, nayo ina urefu kiasi. Nikamwuliza mmoja wa malaika wapandao miche hiyo juu ya miche yenyewe. Akaniambia ya kuwa ile ilikuwa miche ya ugonjwa

utakaoenea chini muda si mrefu. Haikunidhihirikia kama huu utatokea wakati wa kipupwe  kijacho au cha baada yake. lakini onesho lenyewe lilikuwa la kutisha sana. Ninakumbuka pia ufunuo wangu mmoja kuhusu tauni. Ulisema "hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wao wenyewe wabadili yaliyomo nafsini mwao. Hakika yeye ataulinda mji huu." Inaonekana kwamba tauni haitatoweka mpaka madhambi n auasi wa kupita kiasi utoweke kwanza."

Mwishoni mwa onyo hili masihi Aliyeahidiwa aliongeza mashairi yake ya Kiajemi:

"Lau kama rafiki zangu wangeona ninayoyaona, Wangetokwa
na machozi ya damu na kuiambia dunia kwaheri!
Jua ling'aalo limefifia kwa sababu ya madhambi ya wanadamu,
Ardhi imetoa tauni ili kuogofya na kuonya.
Laiti mngelijua, mtafananisha msiba huu na msiba wa Siku ya
Kiyama.
Hakuna dawa ya msiba huu, isipokuwa dawa ya vitendo vizuri.
Yote haya ninayasema kwa sababu ya kuwahurumieni; ni juu
yenu kufikiri, Tumieni busara yenu leo enyi wenye akili!

Kutokana na bishara hizi inaonekana ya kuwa kabla ya mwaka 1894 Masihi Aliyeahidiwa alitabiri msiba mkubwa sana. Aliueleza msiba huo kuwa ni wa maradhi. Halafu tauni ilipodhihiri kwa mara ya kwanza katika Bara Hindi, akatoa onyo maalumu kwa watu wa Panjab kuhusu hilaki inayowanyemelea. Aliueleza msiba huu kuwa hilaki ya Siku ya Kiyama na kwamba  hakungekuwa na kuukwepa msiba huu isipokuwa kwa kubadili mioyo.

Kilichotokea baada ya muda mfupi tu ni cha kutisha zaidi kuliko maneno. Tauni ilianzia Bombay kana kwamba athari yake kubwa sana ilikuwa iwe pale. Lakini baadaye Bombay ilipona na tauni ikapiga hema lake nchini Panjab. Tauni ilitisha na kuenea sana, hivi kwamba pengine watu karibu 30,000 walikuwa wakifa kila juma, na mamia ya maelfu ya watu walikufa katika mwaka mmoja. Mamia ya matabibu waliteuliwa. Namna nyingi mbalimbali za matibabu zilivumbuliwa. Lakini hazikufaa kitu. Kila mwaka  tauni ikazidisha nguvu yake ya kuambukiza. Serikali ikawa haijiwezi.

Watu wakaanza kufikiri kuwa haya yalikuwa matokeo ya kumkadhibisha Masihi Aliyeahidiwa. Hapo si maelfu bali malaki ya watu wakamwamini. Hilaki hii iliendelea mpaka Masihi Aliyeahidiwa alipoambiwa na Mwenyezi Mungu ya kuwa "tauni imekwisha, imebakia homa tu." Baada ya tangazo hili tauni ikaanza kupungua polepole. Kwa hali yoyote, kutokana na ufunuo mwingine inaonekana kuwa tauni inaweza kushambulia baadaye nchini mwetu na nchi zingine. Mwenyezi Mungu alinde watu wake wanyonge na dhaifu!

Bishara hii ya wazi wazi inakubaliwa na waaminio na wakadhibishaji pia. Kama kulikuwako walioendelea kukadhibisha, basi tunawasikitikia sana. Wale wanaofikiri kwa moyo safi, ni lazima wakubali kwamba:

(1) Onyo kuhusu ugonjwa wa tauni lilitolewa kabla ya kutokea kwake tena wakati mrefu kabla matabibu hawajatabiri kutokea kwake katika sehemu yoyote.

(2) Tauni ilipotokea kwa mara ya kwanza watu walionywa kwamba shambulio hili litaendelea toka mwaka mpaka mwaka.

(3) Watu walionywa pia ya kuwa katika Punjab shambulio litakuwa kali zaidi. Na ilikuwa katika Panjab kwamba ugonjwa huu ulishambulia sana zaidi, na kulikokufa watu wengi zaidi.

(4) Matabibu waliwahakikishia watu ya kuwa tauni ilikuwa imemilikiwa, lakini Masihi Aliyeahidiwa akatangaza kwamba tauni haitapungua mpaka Mwenyezi Mungu atake. Kama inavyojulikana maangamizi yaliendelea kwa miaka tisa mfululizo.

(5) Mwishowe Mwenyezi Mungu mwenyewe kwa huruma zake, aliahidi kupunguza mashambulio yake. Masihi Aliyeahidiwa aliambiwa kuwa tauni imekwisha, imebakia homa tu. Baada ya ufunuo huu shambulio kali kabisa lilikoma. kwa hali yoyote, mfuatano wa homa ya malaria uliendelea kushambulia katika Panjab. Hakukuwa na hata nyumba moja iliyosalimika. Idara ya utabibu imeeleza kwamba ugonjwa wa malaria huwa haushambulii kiasi kile.

# BISHARA YA NANE
## MATETEMEKO MAKUBWA

Bishara ninayoendela kuieleza sasa inahakikisha Uwezo na Ufalme wa Mwenyezi Mungu chini kabisa ya ardhi kama ilivyo katika uso wake. Bishara yenyewe inahusu tetemeko kubwa la ardhi lililotokea Panjab mnamo tarehe 4 April; mwaka 1905. Tetemeko hilo lilitimiza tabiri ya bishara hii na kutimia kwake kulikuwa, kwa ajili ya dini zote, kama ushuhuda wa ukweli wa Dini ya Islam na Masihi Aliyeahidiwa. Ufunuo ulio na bishara hii ulisema:

"Msukumo wa mtetemeko wa ardhi." Mwingine: "Nyumba za kukaliwa kwa muda na zenye kukaliwa siku nyingi zitaangamia."

Ufunuo huu mara ulitangazwa katika magazeti ya Jumuiya ya Ahmadiya. Kutimia kwake kwa uhalisi kulikuwa mbali sana. Wengi walifikiri kuwa ufunuo huu ulitaja tu habari za hilaki ya tauni. Kumbe Mwenyezi Mungu alikuwa na maana nyingine. Mwenyezi Mungu alikuwa na maana ya kuchemka kwa mlima Kangra. Mlima huu ulifikiriwa kuwa mfu usio na harakati. Uliwekewa juu yake sanamu ya mungu na kwa hiyo Wahindu walikuwa wakitoa sadaka. Wataalamu wa mambo ya ardhi walifikiri ya kuwa mlima huu ulikuwa umeishiwa nguvu yote ya madhara; ya kwamba kulikuwa hakuna hofu yoyote ile. Nyumba za ibada zilikuwa zimejengwa kuuzunguka. Zilijengwa kwa gharama kubwa sana na zilikuwako kwa miaka mamia na mamia. Madarweshi wa Kihindu waliishi katika majumba hayo. Maelfu ya mahaji walikuwa wakizuru huko kila mwaka. Mwenyezi Mungu akaamuru mlima ule wa moto ufufuke uanze kazi yake na uwe shahidi wa ukweli wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Maneno ya ufunuo uliotabiri matetemeko yanahusu zaidi pale ambapo pana nyumba nyingi zenye kukaliwa kwa muda. Nyumba hizi ama ni mahoteli au makambi ya maaskari vita. Wageni na maaskari wanakuja kukaa makao hayo kwa muda na kuondoka. Watu hawakai miaka na miaka ndani ya mahoteli na makambi. Haiwezi kusemwa kwamba katika ufunuo "Nyumba za kukaliwa kwa muda" zilitanguliwa bila sababu juu ya "Nyumba zenye kukaliwa siku nyingi." Ingawa maneno ya ufunuo ni ubeti ulitungwa

na mshairi wa Kiarabu, bwana Labid bin Rabi'ah wa kabila la 'Aamiri; lakini hii si sababu ya mpango wa ubeti kubakia vilevile. Hakuna anayeweza kumshurutisha Mwenyezi Mungu asiondowe neno hapa na kuliweka kule. Wala Mwenyezi Mungu asingeshindwa kuchagua maneno mengine mbali na haya yaliyofunuliwa. Bali kwa hakika Mwenyezi Mungu alichagua haya maneno kwa vile ndiyo yaliyofaa kuhusu utabiri huu. Maneno haya yanadhihirisha kwamba mahali patakapoathirika zaidi na mtetemeko ni pale panapokaliwa kwa muda. Na mahali hapo ni mahoteli na makambi ya maaskari na panapotembelewa na watu.

Muda kidogo baada ya kutangazwa kwa ufunuo huu, ghafla mlima wa mto huu wa Kangra ukachemka. Ilikuwa mapema tarehe 4 Aprili; mwaka 1905. Sala ya Alfajiri ilikuwa imekwisha saliwa tayari. Kwa masafa marefu kuzunguka mlima Kangra, ardhi ilipata mtetemeko mkali. Kangra, mahekalu yake, viliharibiwa kabisa kabisa. Maili nane nje kulikuwako kambi ya askari. Nyumba zote za askari wa vita zikabomoka. Vijumba vilivyojengwa na Waingereza kwa kutumiwa nyakati za likizo na kukaliwa kwa muda viliteketea vibaya. Majumba ya dalhozi na Bakloh ambayo hukaliwa siku za Kiangazi tu yakaanguka vibaya. Ilimradi mji na vijiji vyote viliteketea. Karibu watu 20,000 wakafariki dunia. Wataalamu wa ardhi wakastaajabu kwa nini matetemeko haya yalitokea. Hawakujua kwamba matetemeko haya yalikuwa ni matokeo ya kukadhibishwa na kudhihakiwa Masihi Aliyeahidiwa. Yalikuja ili kuwajulisha watu ubora wa madai yake. Wataalamu hao wakatafuta sababu chini ya ardhi. Kumbe sababu ilikuwa nje. Mlima mfu wa moto wa Kangra ulikuwa umetii amri ya Bwana wake Mwumba wake ya kuangamiza penye kukaliwa kwa muda na penye kukaliwa siku zote. Masihi Aliyeahidiwa alitabiri matetemeko mengine, na yote yakatimia katika wakati wake. Na mengine mengi ambayo hayajaja bado.

# BISHARA YA TISA
## VITA KUU YA DUNIA

Bishara ya tisa ya Masihi Aliyeahidiwa, ambayo ninaendelea kuisimulia, ni mojawapo ya nyingi zilizouthibitishia ulimwengu mzima ya kuwa Ufalme wa Mwenyezi Mungu umeenea juu ya mioyo na akili za watawala na viongozi, kama unavyoenea juu ya watu wa kawaida, na ya kwamba mwanadamu juu ya kiburi chaka na nguvu, anashurutishwa kumtii Mwenyezi Mungu kama viumbe vyovyote vingine. Bishara hii ilitangazwa mnamo mwaka 1905. Bishara hii ilitabiri kutokea kwa vita kuu ya mwaka 1914 mpaka mwaka 1918 ambayo iliitikisa Ulaya na kuwafadhaisha watu wote duniani. Ilifagia watu wa kawaida, wake kwa waume, na athari yake iko mpaka leo. Mwako wake haujafa bado.

Bishara yenyewe kwa nje inasema juu ya tetemeko lakini hali ya tetemeko hili inaonesha ya kuwa lilikuwa liwe msiba wa dunia nzima, mfano wa tetemeko. Ufunuo mwingine kuhusu tukio hili pia unaashiria kwenye msiba usio tetemeko la ardhi hasa.
Ninataja hapa ufunuo wa bishara hii:

"Ishara mpya. Shindo la ishara mpya."

"Tetemeko mfano wa Siku ya Kiyama. Jiokoeni maisha yenu. Nilishuka kwa ajili yako. Tutaonesha ishara nyingi kwa ajili yako. Tutaangamiza chochote wanachojenga. Sema, " Nina ushahidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, je, mtamini?" Nimeokoa wana wa Israeli. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao yamo katika hatia."

"Ushindi unaong'aa. Ushindi wetu."

"Ninakuja kwako na majeshi tena ghafla." (Ufunuo huu ulirudiwa mara nyingi).

"Mlima ulianguka; na tetemeko likaja! Mlima wa moto!"

"Njia za manufaa kwa Waarabu. Waarabu watatoka majumbani mwao."

"Majumba yatatoweka kama vile kulivyotoweka humo kukumbukwa Kwangu. Nitakuonesha tetemeko la siku maalumu. Mwenyezi Mungu atakuonesha tetemeko la siku maalumu. Ufalme siku hiyo utakuwa wa nani? Kwa Allah aliye Mmoja, Mkali."

Tetemeko lililotajwa katika bishara hi lilielezwa pia na Masihi Aliyeahidiwa kwa urefu katika shairi la Kiurdu. Kwa maelezo ya shairi hilo:

"Tetemeko hilo ilikuwa lilete maangamizi kwa wadhalimu, vijiji na mashamba. Mtu aliyekuwa uchi hatapata fursa ya kuvaa. Tetemeko hilo litawataabisha sana wasafiri. Wengi watangatanga mbali sana wakijaribu kukimbia misukosuko ya tetemeko. Mashimo yatafanyika katika ardhi. Mito ya damu itatirirka. Mito ya maji inayotiririka toka milimani itakuwa myekundu kwa damu. Masiba huo utaifikia dunia nzima. Watu wote, wakubwa kwa wadogo, na serikali zote zitadhoofika kwa mshindo wake. Hususa mfalme wa urusi atapata mashaka makubwa sana. Hata ndege wataumia. Watapoteza akili zao na kusahau nyimbo zao."

Masihi Aliyeahidiwa alipata ufunuo mwingine juu ya jambo hili usemao: "Mashua zinasafiri ili kuwe na mapigano," na mwingine, "Nyanyua nanga." Hadhrat Ahmad aliandika pia ya kuwa yote haya yatatokea mnamo muda wa miaka kumi na sita. Ufunuo wa kwanza ulitaja msiba kutokea katika uhai wake. Halafu alifundishwa dua hii, "Ee Mola wangu usinifanye nishuhudie tetemeko hili."

Hivyo, vita Kuu ikatokea mnamo muda wa miaka kumi na sita baada ya kutangazwa bishara hii, lakini sio katika uhai wake.

Bishara inasema "tetemeko" katika maana ya msiba wa dunia wa namna fulani, yaanivita ya dunia. Kwa wale ambao hawawezi kutambua hivi mara moja nitaeleza sababu nyingine hapa chini:

(1) Neno "tetemeko" mara kwa mara hutumiwa kwa maana ya Vita, msiba mkubwa. Tunao mfano katika Quran Tukufu:

"Walipowajieni (kuwashambulieni) kutoka juu yenu na kutoka chini yenu; na macho yaliponywea na mioyo ikapanda kooni, nanyi mkaanza kumdhania Mwenyezi Mungu dhana mbalimbali. Hapo waaminio walijaribiwa na wakatetemeshwa kwa tetemesho kali" (33:11-12).

"Tetemeko" katika aya hizi, katika Kiarabu *"Zilzaala",* limetumika kwa kila msiba mkubwa na hapa lina maana ya vita. Neno hili lina uwezo wa maana hii na Quran imelitumia kwa maana hii hii. Kwa hiyo tukiruhusiwa na neno la mbele tunaweza kushika neno "tetemeko" kwa maana ya msiba wa namna fulani.

(2) Zama Masihi Aliyeahidiwa alipotangaza hii, aliiongezea maelezo yaliyosema:

"Inawezekana, hali hii ikahusu sio tetemeko la kawaida bali msiba mwingine wa kutisha sana hata utukumbushe Siku ya Kiyama na uwe sio wa kawaida ambao haukujulikana kabla. Msiba huu unaweza kuangamiza vibaya maisha na majengo pia." (*Baraahiin Ahmadiyy,* Sehemu ya 5, uk. 120).

Hii inaonesha wazi ya kuwa hata Masihi Aliyeahidiwa fikara yake ilielekea kutafsiri neno hili vinginewala sio lazima liwe jinsi ya tetemeko la ardhi. Inaweza kuwa ni jinsi ya msiba tofauti na tetemeko la desturi. Alipotangaza bishara hii wapinzani wake walisistiza kushika "tetemeko" la bishara kuwa na maana ya tetemeko la desturi. Wakamtaka Hadhrat Ahmad asilete maana nyingine juu ya "tetemeko". Lakini Hadhrat Ahmad alisema tena na tena ya kuwa katika ufunuo mifano kadha wa kadha imetumiwa. kwa hiyo hakuweza kushika maelezo hayo kuwa na maana ya kitu chochote maalumu. Adhma ya bishara hii imo ndani ya ishara nyingi

iliyozitabiri, kutabiri ambako hakumo katika uwezo wa mwanadamu. Bishara ilieleza upeo wa wakati. Kadhalika ilieleza kuwa, matukio iliyoyabashiri hayajapata kuonwa kabla katika taarikh ya mwanadamu.

(3) Maneno yaliyotumiwa katika bishara yenyewe yanaainisha kuwa kusingemaanishwa tetemeko la ardhi hasa; bali, labda msiba wa namna nyingine:

(a) Bishara inasema ya kuwa tetemeko hili litatokea katika dunia nzima. Lakini kila mtu anajua ya kuwa matetemeko ya ardhi huwa hayatokei dunia nzima. Bali hutokea katika sehemu sehemu za dunia.

(b) Bishara inasema ya kuwa msiba utawataabisha sana wasafiri ambao wataacha njia zao na kutangatanga. Lakini matetemeko ya ardhi huwa hayawasumbui wasafiri. Bali huwataabisha wale wanaokaa majumbani, katika miji mikubwa. msiba uwezao kuwataabisha wasafiri unaweza tu kuwa vita. Vita inapoanza wasafiri hawawezi kufuata njia zao za kawaida. Badala yake huziwacha na kushika njia za taabu sana.

(c) Bishara inaashiria kwenye madhara yatakayoletwa na msiba huo makondeni na mabustanini, n.k. lakini matetemeko ya ardhi huwa hayadhuru mashamba ambayo huharibiwa na vita tu. Makombora yatokayo kila upande, huangamiza mashamba. Waakati mwingine mpango wa "ardhi iliyounguzwa" huyaharibu.

(d) Bishara inaashiria madhara ya msiba huu kuwaathiri ndege; ndege ilikuwa wapoteze "akili" zao na "nyimbo" zao. Tetemeko la ardhi la desturi haliwezi kuleta msukosuko huu. Msukosuko wake ni wa muda mfupi tu. Kama ndege wakaao mitini au juu ya nyumba wakiruka angani, huwa hawapati taabu yoyote ile. Vita ya kisasa, kwa hali yoyote, ni mbaya sana kwa ndege. Makombora ya usiku na mchana na kuangamizwa miti kunafanya ndege wasiweze kuishi. Ama wanakufa au wanapata wakati wa mahangaiko.

(e) Bishara ina ufunuo: "Nimeokoa wana wa Israeli". Hii inaonesha kuwa msiba huu ni wa kutokea na faida ya namna fulani kwa Mayahudi. Jambo kama hili haliwezi kuwa na uhusiano wowote na tetemeko la desturi. (baadaye nitaeleza maana ya sehemu ya bishara hii; na nitaonesha kuwa bishara hii imo katika Quran pia).

(f) Bishara inasema juu ya vita, kwa sababu kwa nje ikisema juu

ya tetemeko la ardhi inendelea kusema kuwa Firauni na Haman na majeshi yao wamo hatiani. Hii ni dhahiri inaeleza juu ya Kaisar wa Ujerumani aliyejifikiria kuwa mungu au makamu wa mungu, kama vilevile Firauni wa Musa alivyofikiri kuwa alikuwa "Mungu Mwenye enzi kwa watu wake." Haman katika ufunuo maana yake ni rafiki wa Kaisar, mfalme wa Austria, ambaye hakuwa na fahari sana na ambaye alimtii sana jemedari wa vita wa Ujerumani. Kama bishara ilikusudia tetemeko la desturi, maneno "Hakika Firauni na Haman na majeshi yao wamo hatiani" yasingekuwa na maana.

(g) Ufunuo unataja ahadi ya mara kwa mara "Nitakuja ghafla na majeshi Yangu." Hii pia inaashiria kwenye vita na sio tetemeko la ardhi.

(h) Ufunuo unasema juu ya mlima wa moto, ambao kupasuka kwake kutawafaidia Waarabu ambao watatoka majumbani mwao. Jinsi hii haipatani na tetemeko la desturi. Mlima wa moto unaweza tu kuwa na maana ya mhimizo wa machafuko ya siasa ambao unatokea kwa sababu ya matukio yaliyopita. Baadhi ya matukio kama haya ilikuwa yawachangamshe Waarabu katika tendo moja kubwa ambalo wangepindua tukio hilo upande wao.

(i) Ufunuo unasema kwamba siku hiyo Mwenyezi Mungu atakuwa ndiye Mfalme wa Ulimwengu. Jinsi hii pia ni ya kivita ambayo serikali zenye nguvu sana zitainuka kupigana. Nguvu kubwa kubwa, kwa mujibu wa bishara, ilikuwa zije kuwa dhaifu. na hivyo Ufalme wa Mwenyezi Mungu uthibitike kwa ishara zenye nguvu.

(j) Ufunuo mmoja unasema, "Mlima ulianguka na tetemeko la ardhi likaja." Hata watoto wa shule wanajua kuwa tetemeko la ardhi halisababishwi na kuanguka kwa mlima. Kwa kweli ni kinyume chake. Milima inaweza kuanguka kwa sababu ya mtetemeko wa ardhi. Hii pia inaonesha kuwa bishara hii haihusu mtikisiko wa desturi, bali ni maneno ya mfano ya msiba mwingine mkubwa utakaowaingiza wanadamu katika vita.

(4) Sababu ya nne, kwa nini tetemeko lililotajwa katika bishara halina maana ya tetemeko la desturi, bali msiba mwinge ni kwamba ufunuo mwingine aliopokea Masihi Aliyeahidiwa katika muda uleule unaashiria kwenye vita kubwa. Ufunuo mmoja unasema: "Nyanyua nanga." Hii inaashiria kwenye mwingio wa mataifa mbalimbali

katika vita ya manowari kila moja kwa nyingine. Amri "Nyanua nanga" inaashira magomvi ya manowari. Ufunuo mwingine unasema: "Mashua zinasafiri ili kuwe na mapigano." Hii ni taswira ya manowari zikienda toka upande mmoja hadi mwingine.

Bada ya kuonesha kwamba tetemeko lililotajwa katika bishara hasa maana yake ni Vita Kuu ya mwaka 1914 mpaka 1918, ninapenda kueleza kwa urefu sana ni kwa namna gani sehemu mbalimbali za bishara zilipata kutimia katika matukio ya Vita Kuu.

Jambo la kwanza linalotupasa kukumbuka ni kwamba kwa mujibu wa bishara hii vita ilikuwa isababishwe na tukio fulani. kwa mujibu wa bishara hii, tukio la mkosi lilikuwa lifuatwe na "tetemeko la dunia nzima." Vita kuu ya Ulaya ilianza hasa kwa njia hii. Marithi wa Austria - Hungry na mkewe waliuawa kwa siri. Mauaji haya yakaleta vita. Hii ilikuwa ni tofauti na vile vita vinavyoanza kwa kawaida. Vita huletwa kwa hitilafu na kutokupatana baina ya nguvu mbili kubwa. Lakini vita ilisababishwa na kuawa kwa siri kwa mwana mflame na mkewe.

Jinsi ya pili ya msiba huu iliyotabiriwa ni hali yake ya kiulimwengu. Jinsi hii pia ilitimia barabara. Kabla ya vita kuu, misiba ya kiulimwengu haikujulikana. Vita hii ilikuwa ya kwanza kuwa msiba wa kiulimwengu. nchi za Ulaya ziliingia vitani kwanza, baadaye Asia na halafu china, Japan, na Bara Hindi zilikuwamo. Meli ya vita ya Kijerumani ilishambulia forodha za Bara Hindi toka katika bahari ya Hindi. Iran ilikuwa mahala pa mapigano baina ya majeshi ya Ulaya na Uturuki. Wairan walikuwa na mgogoro na ubalozi wa Ujerumani. mapigano makali yakafanyika Iran, Sham, Falastini na Siberia. Yalifanyika pia katika sehemu nne mashuhuri za Afrika. Afrika ya kusini ilishambulia Afrika ya Magharibi ya Wajerumani. Katika Afrika ya kusini penyewe palikuwa na machafuko. Walowezi wa Kijerumani wakashambuliwa katika Afrika ya Mashariki. Huko pwani ya magharibi mapigano yalifanyika Cameroons. Yakafanyika mapigano katika Suez na mpakani mwa Misri na Tripoli. Meli ya Kijerumani ikashambulia katika New Guinea. Mabaharia wa Kiingereza na wa Kijerumani wakambana karibu na pwani ya Amerika. Canada na Amerika zikaingia. Serikali za Amerika ya Kusini zikatangaza vita kwa

Wajerumani. Ilmuradi hakuna sehemu yoyote ya dunia ambayo ilisalimika na madhara ya vita hii.

Hali nyingine ya vita iliyotajwa katika bishara ni kuvunjika kwa milima na kuanguka kwa miji na mashamba na hivi ndivyo ilivyokuwa. Milima mingi ilitoweka kwa sababu ya makombora au machimbo yaliyopasuliwa kwenye milima hiyo. Miji mingi iliangamizwa. Ujerumani ilipaswa kutumia fedha nyingi kwa kuitengeneza miji yake. Bado inaibidi kulipa fedha nyingi kwa matengenezo hayo. Uharibifu uliofanyika mashambani na mabustanini hauwezi kukadiriwa. Popote yalipotokea mapigano, maanganizi ya mashamba pia yalifuata. Miji iliangamizwa na hakuna kilichobakia mashambani. Maaskari wenye silaha walipangwa kwa maili maelfu kwa maelfu. Maangamizi yaliyotokea yalikuwa hayana idadi.

Hali nyingine ya vita ilikuwa ndege kupotewa na akili. Hivi ndivyo ilivyotokea. Katika uwanja wa mapigano ndege walipoteza maisha yao.

Ishara nyingine ya vita ilikuwa ni ardhi kutiwa mashimo na kuharibiwa kwa ujumla. Katika Ufaransa, Servia na Urusi, kupigwa kwa makombora mengi sana kulifanya ardhi iwe na mabonde mabonde marefu. Sehemu zingine mabonde haya yalitoka maji. Mapigano yalilazimisha watu kuchimba mahandaki. Nchi iliyoona mapigano ilikuwa na mhandaki tele. Hakuna aliyeziona akafikiri kuwa zilikuwa nchi zilizokaliwa na watu wengi. Sehemu zote zilionekana mapango au mashimo ya kuchomea matofali.

Ishara nyingine ya vita hii ilikuwa ya kwamba mito ya maji ilikuwa igeuke kuwa mito ya damu ya wanadamu. Hivi ndivyo ilivyotokea. Damu nyingi ilimwagika hivi kwamba kwa maili nyingi mito iliweza kugeuka kuwa myekundu. Kulikuwa na mapigano mengi kwenye kila mpaka hivi kwamba mito ya damu ilitiririka hasa.

Ishara nyingine ilikuwa wasafiri wapate taabu sana. Wengi wao ilikuwa waache njia zao. Hivi ndivyo ilivyotokea. Katika nchi, kwa sababu ya majeshi ya vita na safari zao, njia za kawaida zilifungwa. Baharini, kwa sababu ya mapigano ya merikebu, mashua zilizokuwa zikichukua wasafiri zilikuwa hatarini siku zote. Vita ilipoanza mamia ya maelfu  kadha ya watu waliachwa katika nchi za maadui. Wengi

wao iliwabidi kushika njia za mzunguko ili kufikia nchini kwao. Majeshi ya nchi mbalimbali pia yalipaswa kusafiri katika njia za mzunguko, njia za mkato zilikuwa mikononi mwa maadui. Askari wa Kiingereza waliopigana Ufaransa pia walipoteza njia zao. Matukio ya huzuni mengi yalitokea, ambayo ili kuyaepuka, askari wa Kiingereza waliamriwa kuvaa kwa Kifaransa majina ya vikosi vyao na vituo vyao mashingoni mwao.

Alama nyingine ilikuwa "vitu" ambavyo dunia inajaribu kujenga ilikuwa vibomolewe. Hivi ndivyo ilivyotokea kwa kimwili na kwa mfano. Majumba mengi maarufu katika ulaya yaliteketezwa. Hilaki ilifanyika katika utamaduni wa watu wa Ulaya. Amani na tumaini la zamani likaondoka. Mataifa ya Ulaya yakajaribu kujenga tena usuli hizo, lakini wapi, jitihada haishindani na Kudra. Ilionekana hapana budi kwa watu wa magharibi kutafuta njia za kujenga tena utamaduni wao. Usuli za zamani ziliangamizwa, tena milele, Usuli mpya zitakuwa lazima ziwe za akili na za ukaribu sana na mafundisho ya Islam. Hili ni jambo lililokwisha kadiriwa na Mwenyezi Mungu.

Hali ya maana sana ya vita ilikuwa ni utulivu kwa Waisraeli. Hali hii ya bishara ilitimia kinaganaga. Vita ilikuwa haijaisha, kama matokeo ya vita, Lord Balfour alitangaza ya kuwa watu wa Israeli waliokuwa bila ya "ardhi yao" watawekwa katika "ardhi yao," Falastini. mataifa yaliyopigana yakaahidi kuwalipa fidia watu wa israeli kwa dhuluma waliofanyiwa zamani. Kwa kufuata matangazo haya, Falastini ikatolewa kwa Waturuki na kutangazwa kuwa ardhi ya Wayahudi. Taratibu ya utawala wa Falastini inafanywa kwa namna ambayo Wayahudi wanaweza kukaa vizuri ardhini kwao. Mayahudi toka nchi mbalimbali wanatumainishwa kukaa Falastini. Ombi la zamani sana la Mayahudi kwamba kufanywe kanuni za kuinua mwungano wa taifa lao likawa limetimizwa.

Jambo la ajabu sana juu ya sehemu hii ya bishara ni kwamba Quran pia imeeleza juu ya tukio hili. Katika Sura Bani Israaiil tunasoma:

"Na Tukawaambia baada yake wana wa Israeli, kaeni katika nchi; na itakapofika ahadi ya mwisho, Tutawaleteni pamoja" (17:105).

Mufasirina wengine wa Quran wanachukua ardhi kuwa Misri na "ahadi ya siku za mwisho" kuwa Siku ya Kiyama. Lakini tafsiri hizi ni za kosa kwa sababu Waisraeli hawakuamriwa kabisa kuishi katika nchi ya Misri. Bali waliamriwa kuishi katika ardhi Takatifu, yaani Falastini, na huko ndiko walikoishi. Vilevile "ahadi ya siku za mwisho" haiwezi kuwa na maana ya Siku ya Kiyama kwa sababu Siku ya Kiyama haina uhusiano na Waisraeli kuishi katika Ardhi Takatifu. Kwa hiyo kinachomaaniwa na ahadi ya siku za mwisho ni kwamba wakati fulani ilikuwa ufike Mayahudi kuiacha Ardhi Takatifu, bali wakusanywe mara nyingine katika ardhi hiyo, katika wakati wa "ahadi ya siku za mwisho." Ahadi ya siku za mwisho inahusiana na wakati wa Masihi Aliyeahidiwa. kwa hiyo kukusanywa kwa mara ya tena kwa Waisreli kulikuwa kufanyike wakati wa Masihi Aliyeahidiwa.

Katika maelezo ya *Fathul Bayaan* tunaambiwa ya kuwa "wakati wa ahadi ya siku za mwisho unaashiria kushuka kwa nabii Isa kutoka mbinguni." Kadhalika Sura ya Quran Takatifu niliyoitaja hapo inagawa taarikh ya Mayahudi katika zama mbili kubwa (17:5). Kuhusu zama za pili Sura hii inaendelea kusema:

"Na ilipofika ahadi ya mwisho, (Tukawapelekeeni watu) ili wawafanye vibaya wakubwa wenu, na wauingie Msikiti kama walivyouingia mara ya kwanza, na wayaangamize kabisa waliyoyashinda" (17:8).

Kutokana na aya hizi inadhihirika ya kuwa onyo la siku za mwisho linahusu wakati katika taarikh ya Mayahudi unaofuata kufika kwa mara ya kwanza kwa Nabii Isa. Kwa hali yoyote, baada ya onyo hili, tunajua kutokana na taarikh, ya kuwa Mayahudi hawakukusanywa; bali walitawanywa. Kwa hiyo, katika Sura 17:105

onyo la siku za mwisho linahusu zama baada ya kufika mara ya pili Nabii Isa. Maneno "Tutawakusanyeni pamoja" yanaeleza juu ya majilio yaliyopo ya Mayahudi katika Falastini. Mayahudi wa toka nchi mbalimbali wanapatiwa misaada ya safari na matengenezo ya maskani. Ufunuo wa Masihi Aliyeahidiwa ulisema: "Nimeokoa wana wa Israeli." Huu uliashiria badiliko kubwa katika mawazo ya mataifa mbalimbali juu ya makao ya Mayahudi. Alama ya maana sana ya vita hii ilikuwa muda usiozidi miaka kumi na sita. Ilitokea barabara kama ilivyotabiriwa. Funuo kuhusu vita zilipokelewa katika mwaka 1905; vita ilianza mwaka 1914, yaani mnamo miaka kumi na sita toka tarehe ya bishara.

Alama nyingine ya vita ilikuwa ya kwamba majeshi ya manowari ya mataifa mbalimbali ilikuwa yawekwe tayari. Sawasawa, tunaona kwamba sio mataifa mapigani tu, bali mataifa mengine pia iliwabidi kuweka tayari majeshi yao ya manowari. Kila taifa liliona kwamba hakuna taifa jingine lolote la kuharibu maji yake. Vita ziliweza kuwatukia wakati wowote. Hivyo majeshi ya manowari yalikuwa tayari tayari, hata kwa ajili ya kujilinda wale wasiokuwamo vitani.

Alama nyingine ya maana sana ya vita ilikuwa safari za meli kwa ajili ya vita ya baharini. Bishara haikuashiria matayarisho tu kwa wapiganaji bali pia safari za meli. Sawasawa, katika vita hii meli nyingi zilitumiwa kuliko hapo kabla. meli ndogo, meli za kuteketeza, meli zinazoweza kuzama chini ya bahari, zilitumiwa kwa kadiri ambayo haikujulikana hapo kabla. Neno lililotumiwa katika bishara ni "mashua" ambalo linaashiria upendeleo wa mapigano ya vyombo vya baharini vya kadiri ndogondogo na huu ni ukweli wa Vita Kuu ya 1914-1918.

Alama moja iliyoambiwa ya vita kutokea kwake kwa ghafla. Jinsi vita hii ilivyotokea ghafla inajulikana sana. Wakuu wa serikali baadaye walikubali ya kuwa ijapokuwa walitazamia vita wakati fulani, lakini hawakuwa na habari ughafla uliojia vita hii. Kifo cha mwana mfalme wa Austria na mkewe ndicho kilicholeta vita. Moto wa dunia nzima ukawaka.

Alama moja ya vita ilikuwa ni manufaa ambayo vita ilikuwa iyalete kwa ajili ya Waarabu na njia ambayo Waarabu ilikuwa wazitumie fursa walizopata kutokana na vita. Kwa muda mrefu,

Waarabu walileta fikara ya uhuru wa Bara Arabu. Waliposikia ya kuwa Waturuki wakiingia vitani, walifikiri ya kuwa wakati wa uhuru wao ulikuwa amefika. Mara moja walitangaza vita na Waturuki na wakaingia kupigana nao. Waarabu wakapata shabaha ya uhuru wao.

Alama moja ilikuwa ni maangamizi ya miji na mwahala mwa ibada zao za kishirikina. Ufunuo ulisema, "Majumba yatatoweka kama vile kulivyotoweka humu kukumbukwa kwangu." Inakubaliwa ya kuwa Ufaransa ya Mashariki ilikuwa ni sehemu mbaya sana ya Ulaya katika mapenzi ya anasa za kimwili. Kutoka sehemu hii ilipelekwa pombe iliyonywewa katika nchi mbalimbali za Ulaya. Palikuwa na mahala pa kukutania wapenda anasa kutoka nchi za Magharibi. Sawasawa na bishara, sehemu hii iliteketezwa zaidi. majumba ya sehemu hii yalivunjika vunjika na kufikinyika, na yalifutiliwa mbali kama vile jina la Mwenyezi Mungu lilivyofutwa mioyoni mwao.

Alama moja iliyotajwa katika ufunuo ilikuwa "Ushindi wetu." Hii waziwazi ilionesha wa kuwa ushindi ulikuwa uende upande uliokuwa na mapenzi na wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa. Hivi ndivyo ilivyotokea. Masihi Aliyeahidiwa aliwaombea Waingereza katika msiba mkubwa huu. Wakuu wa serikali ya Uingereza wanaweza kunasibisha ushindi wao kwa mipango yao, lakini uchunguzi wa makini wa hali ya kweli iliyokuwako ya vita unaonesha ya kuwa majeshi ya Uingereza yalipata msaada wa kimwujiza kila mara. Mara kwa mara matukio ya ghafla yalikuwa upande wao. Hii inaonesha ya kuwa ushindi wa Uingereza ulisababishwa na msaada maalumu wa mbingu. Haukusababishwa na mipango ya kibinadamu tu.

Alama moja katika bishara ilikuwa ya maana sana. Kwa sababu hii alama moja ilijaa chungu ya alama zingine. Alama hii ilikuwa kwamba vita hii ilikuwa imdhalilishe Czar wa Urusi kwenye hali ya kusikitisha sana. Hali zilizokuwako zama za kutangazwa bishara hii hazikuwa na ishara hii. Kwa kweli, kulikuwa na ishara za kinyume. Lakini bishara ilitimia, na kutimia kwake kulimshangaza kila mtu.

Maelezo ya bishara juu ya kilichokuwa kitokee kwa Czar (tamka 'Zaar') yana chungu ya bishara zingine. Moja ilikuwa kwamba mpaka

"msiba' utokee, kulikuwa hakuna yoyote ya kumfikia Czar. Madhara kwa Czar ilikuwa yafike wakati wa matokeo ya "msiba", yaani, vita hii. Ya pili, bishara ilidokeza kwamba madhara yaliyowekewa Czar yalikuwa sio kifo au mwisho wa ghafla. Kifo au mwisho wa ghafla hauoneshi hali mbaya ya kusikitisha. Kwa hiyo maelezo ya bishara hayaoneshi kifo cha ghafla kwa ajili ya Czar. Badala yake yanaonesha hali ya kumalizika baada ya muda fulani na iliyojaa machungu na taabu za namna mbalimbali. Kadhalika maelezo hayo yanadokeza mwisho wa Czar kuwa wa nasaba ya mfalme. Maelezo ya bishara yanasema juu ya lakabu ya Czar. Yanaashiria nasaba ya Kifalme ya urusi, sio kwa matawala fulani wa Kirusi. Hebu basi tazama jinsi bishara hii ilivyotimia sawasawa! Kabla ya vita Kuu juhudi zilifanywa kumwondoa Czar na kufuta kabisa Ufalme wa kinasaba wa Czar, lakini hakuna kilichotokea. Halafu vita ikaja na wakati uliochaguliwa kwa mwisho wa Czar. Mwisho huu ulikuja na ughafla uliomstaajabisha kila mtu. Inaonekana kwamba mapinduzi yalipoanza katika mwaka 1917, Czar hakuwako mjini pake, bali alikwenda mbele ya vita akikagua maaskari na mwahala mwao. Alipoondoka kutembelea sehemu ya mapigano, hakukuwa na dalili za mapinduzi ya serikali. Halafu, kwa sababu ya makosa fulani upande wa Gavana watu walikasirika sana. Lakini makasiriko ya namna hii ni ya kawaida katika serikali zenye taratibu maalumu. Mara chache au pengine kabisa hayaelekezi kwenye mwanguko wa serikali. Kwa hali yoyote, hapa Mkono wa Mwenyezi Mungu ulikuwa kazini. Czar, kwa kusikia haya, alipeleka maagizo kwa gavana ayamalize kwa mkono wenye nguvu. Lakini mkono wenye nguvu wakati huo ulileta athari ya kinyume. Ulileta makasiriko zaidi, Czar akamwakilisha Gavana na yeye mwenyewe akarudi mjini. Lakini njiani alisikia maelezo zaidi juu ya hali iliyokuwako. Alishauriwa kwamba maasi yalizidi na ya kwamba asingeingia mjini. Lakini Czar hakujali. Akiamini kwamba kuwako kwake kungewatuliza watu, aliendelea na safari yake ya kurudi. Alikuwa hajaenda mbali sana kwa gari la moshi mara akasikia kwamba mapinduzi ya serikali yamefanyika; ya kwamba wapinduzi hao wamechukua ofisi zote za mawaziri wa serikali; na ya kwamba serikali nyingine imeundwa. Mnamo mwezi Machi tarehe 12, mwaka

1917, katika mchana mmoja, mfalme mkubwa kabisa na mwenye nguvu sana, Czar, (yaani mtu anayetawala watu na asiyetawaliwa na yeyote), aliondolewa kitini na kurudishwa kwenye daraja ya uraia wa watu wake mwenyewe. Mnamo tare 15 Machi akatia sahihi tangazo kwa kushurutishwa ya kuwa yeye na nasabu yake hawatadai tena ufalme wa Urusi. Hii ilitimia sawasawa na bishara. Nasabu ya Czar haikuwa tena nasabu ya kifalme. Lakini kulikuwa na sehemu nyingine za bishara. Czar, Nicholas II, alidhania ya kuwa kwa kukiacha kiti cha ufalme angesalimisha maisha yake mwenyewe na Malika wake na watoto wao na ya kwamba wangeweza kuishi kama raia wa pekee akitumia mapato ya mali yake. Lakini haikuwa ije kuwa hivi. Aliacha kiti mnamo tarehe 15 machi. Kupata tarehe 21 Machi, akakamatwa na kuwa mfungwa na akapelekwa Skosilo. Tarehe 23 Amerika ikatangaza kuwa imeitambua serikali ya mapinduzi. Tarehe 24, Uingereza, Ufaransa na Italia zikatambua serikali mpya. Hii ikaua matumaini ya mwisho. Kiti kilikuwa kimekwenda. Hata salama ya mwili ilikuwa ya mashaka. Aliweza kuona kwamba nguvu alizotegemea msaada wake na ambazo kwazo majeshi yake yalikuwa vitani yakipigana na Wajerumani hazikuchukua zaidi ya juma moja kutambua mapinduzi haya ya uasi. Hizi nguvu rafiki za zamani hazikuinua hata sauti ndogo tu kusaidia. Bali kulikuwa na maumivu mengine ya kuendelea kwa ajili yake. Ili kutimiza bishara, hali ilikuwa ije kuwa ya kusikitisha sana. Czar alikuwa mfungwa, lakini utawala ulikuwa bado umo mikononi mwa mtu wa nasabu yake, Prince Dilvao. Utawala wa Prince huyu ulihakikisha ukarimu wake kwa Czar gerezani. Kwa kweli, Czar na jamaa yake walikuwa wanafanya kazi bustanini, na kazi zinazomstahili hasa mtu aliyeacha ufalme. Lakini mnamo mwezi Julai, huyu Prince ilimbidi pia aache kiti. Mamlaka ya serikali yakawa mikononi mwa Kerensky. Maisha ya wafungwa wa kifalme sasa yakawa magumu zaidi lakini ya kuvumilika. Hasa tarehe 7 Novemba uasi wa Bolshevik ukaiondoa serikali ya Kerensky, na hali ya Czar ikawa ya kusikitisha sana hivi kwamba moyo wenye ithbati kama ule ukanywea. Czar akaondolewa kwenye kambi ya wafungwa wa Kifalme ya Skosilo na kupelekwa toka mahala mpaka mahala pengine, hatimaye mpaka Ekaterinsberg. hapa ilimbidi apate

mwonjo wa adhabu alizokuwa akiwapa maskini wafungwa katika Siberia. Mji huu mdogo uko Mashariki ya Urals, maili 1440 kutoka Moscow. Hapa ndipo mahala palipokuwa panatengenezwa mashine za kutumiwa kwenye machimbo ya Siberia. Wafungwa wa Kirusi iliwabidi kufanya kazi katika machimbo haya. Taswira iliyozunguka mahala hapo papya ilimkumbusha Czar ukatili aliokuwa akiwafanyia wengine.

Kwa hali yoyote hali ya kusikitisha sana ya Czar haikuwa ya kupimwa kwa adhabu hizi tu. Serikali ya Bolshevik (wafanya kazi wa Kirusi) ilipunguza posho yake na starehe ya kawaida. Mtoto wake mgonjwa alipigwa na walinzi wakali sana. Wazazi iliwabidi waone na kustahamili. Mabinti zake walifanyiwa vibaya sana. Hata adhabu hizi hazikuwatosheleza wapinduzi wa serikali. Walivumbua adhabu mpya na maumivu  mapya. Siku moja ya mwisho Czarina (mkewe Czar) alipokuwa akitazama, mabinti zake waliobalehe walibikiriwa na maaskari. Kama Czarina akiwa hawezi kuvumilia kutazama, aligeuza uso wake kwingine, maaskari walimshurutisha kutazama tendo lile la kinyama. Akishuhudia ukatili huu na kuvumilia maumivu zaidi machungu kuliko yanayoweza kuvumiliwa na mtu yeyote, hatimaye Czar alifariki dunia. Aliuawa kwa risasi mnamo tarehe 16 Julai, 1919; pamoja na jamaa ya kifalme yote. Bishara, "hata Czar wakati huo atakuwa katika hali ya kusikitisha sana," ikawa imetimia barabara.

Vita ilikwisha. Czar alikufa kifo cha kusikitisha sana. Watawala wa Ujerumani na Austria walikuwa wameacha viti vyao vya kifalme. Miji ilikuwa kama majangwa. Milima ilikuwa imeondoka. Mamilioni ya wanadamu walikuwa wamekufa. Mito ya damu ilikuwa imetiririka na mateketezo yalikuwa yamepanua ardhi. Lakini lo! dunia bado ilitaka hoja na dalili kuthibitisha ukweli wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. hazina za Mwenyezi Mungu hazina mwisho. Adhabu Yake tayari kuja kama ulivyo msamaha Wake. Lakini waliobarikiwa ni wale wanaopenda kuelewa; ambao wangeharakia kufanya suluhu na Mola wao kuliko kuendelea kufanya naye vita. Ambao wanaangalia Ishara Zake na hawaziepi kana kwamba hawakuziona. Wanajitakia Huruma ya Mwenyezi Mungu; wanapokea baraka Zake na kuonekana wabarikiwa duniani.

# BISHARA YA KUMI
# KUPANUKA KWA QADIANI

Mpaka hapa nimesimulia bishara zenye maonyo, au vyote viwili, maonyo na ahadi. Sasa ninapenda kusimulia bishara tatu zenye ahadi za mafanikio, mpanuko, na maendeleo ya ujumla.

Bishara hizi tatu, kama zingine zote, zilitangazwa kwa ukamilifu wakati mrefu kabla ya kutimia kwake. Marafiki na maadui walizijua. Watu wa dini zote wanaweza kuonwa ambao wangesema, walijua kuwako kwa bishara hizi. Zilikuwa zimetolewa mara kwa mara katika magazeti na vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa. Ya Kwanza ya bishara hizi tatu inahusu mpanuko wa Qadian, kitovu na markaz ya Mwendeleo wa Ahmadiyya, kitakua toka mwaka  mpaka mwaka na baadaye kije kuwa mji mpana sana, hata kiwe kama vile Bombay na Karachi, pamoja na watu milioni au zaidi. Upande wa Mashariki kilikuwa kipanuke mpaka mto Beas, maili tisa kutoka Qadian. Tangazo hili lilipotolewa watu wa Qadian walikuwa karibu elfu mbili tu. Isipokuwa nyumba chache zilizojengwa kwa matofali ya kuchoma, mji wote ulikuwa na nyumba zilizojengwa kwa udongo. Kodi za nyumba zilikuwa chini sana, hata si vya kusimulia. Mtu aliweza kupata nyumba kwa pesa nane kwa mwezi. Ardhi kwa kujenga nyumba iliweza kupatikana kwa bei rahisi sana. Ardhi iliweza kupatikana kwa Rupia kumi au kumi na tano. Maduka ilikuwa ni shida kuwapo. Unga wa ngano wa rupia mbili au tatu haukuweza kununuliwa mara moja. Watu waliishi kama vijijini. Walisaga unga wao wenyewe kufanya mikate yao. Kulikuwa na shule moja tu, shule ndogo; ikiwa na mwalimu mmoja, kwa wadhifa mdogo ambaye pia alifanya kazi ya ukarani wa posta ya kijiji hicho. Barua kutoka nje ziliwasili mara mbili kwa juma! Nyumba zilijengwa zikizungukwa na ukuta wa kijiji. Hakukuwa na hali za asili ambazo zingesaidia bishara hii kutimia. Qadian ilikuwa umbali wa maili kumi na moja tokea kituo cha gari moshi . Barabara iliyoiunganisha na kituo cha gari moshi ilikuwa ya mavumbi matupu. Miji hupanuka kwa njia ya relii au zingine, lakini Qadian haikuwa kwenye njia zozote. hakukuwa na viwanda ili kuwavutia wafanya

kazi, wala kazi za ukarani, sio wizara wala idara. Qadian haikuwa markaz ya Wilaya kubwa wala ndogo. Haikuwa hata na kituo cha polisi. Haikuwa gulio la namna yoyote ile ya mazao au bidhaa. Wafuasi wa Hadhrat Ahmad wakati huo hawakuwa zaidi kuliko mia chache. Mji usingeundwa kwa kuwaita wafuasi wake waje na kuishi Qadian.

Naam, inaweza kusemwa ya kuwa dai la Unabii lilikuwa limefanywa. Kwa hiyo Mirza Ghulam Ahmad aliweza kutazamia kupata wafuasi wa kadiri fulani na ufuasi huu ungeweza kuja Qadian na kuifanya mji mkubwa. Lakini ni nani aliyeweza kusema ya kuwa Hadhrat Ahmad angepata ufuasi mkubwa wa kutosha? Na mara ngapi wafuasi wa nabii huacha kazi zao na maskani yao ili wakae karibu na kiongozi wao? Yesu alizaliwa Nazareti na Nazareti ingali kijiji tu. Mawalii wakubwa kama Shahabud-Din Suhrawardy, Sheikh Ahmad Sirhindi na Bahaaud-Din Naqshabandi, (radhi ya Mwenyezi Mungu iwe juu yao), walizaliwa vijijini. Au, walikwenda kuishi vijijini. Lakini vijiji hivyo vilibaki vijiji tu. Havikukua kufikia kadiri nyingine yoyote zaidi. Kama vilifanya hivi vilikuwa katika mipaka ya uchumi. Kuanzisha miji midogo au mikubwa si rahisi. Wafalme, ambao wanapanga na kuanzisha miji bila kufikiria hali za uchumi, huwa hawafanikiwa. Miji kama hiyo huachiliwa mbali baada ya muda mfupi. Kwa uchumi, Qadian ilikuwa katika hali ya umaskini sana. Haikuwa kwenye njia ya reli wala hata karibu yake. Wala haikuwa mbali sana na njia ya reli hivi kwamba wakazi wake wangeukuza kuwa kama kituo cha utamaduni wao. Wala haikuwa karibu na mto au mfereji. Mito na mifereji huchangamsha biashara na kusaidia makuzi ya miji, lakini Qadian haikuwa na hata njia hii.

Kinyume cha hali zote za asili na kawaida, Qadian ilikuwa ya kukua toka zaidi hata zaidi. Baada ya kutangazwa bishara hii, Mwenyezi Mungu akaanza kuisaidia Jumuiya kwa kuongezeka idadi. Wanachama wa Jumuiuya wakaanza kuelekea Qadian kuwa maskani yao. Waahmadiyya waliokuja kukaa waliwavuta wengine. Kutimia kamili kutachukua muda lakini sehemu yake moja ya kutimia inastaajabisha. wakazi wa Qadian sasa ni kiasi cha 4,500, tayari zaidi kuliko mara mbili ya idadi ya wakazi wa zamani. Ukuta wa zamani wa kijiji umetoweka na mji umepita mipaka yake. Wakati

huu nyumba zinaweza kuonwa kwa masafa ya maili moja nje ya kijiji cha zamani Majumba mengine makubwa ya matofali na barabra pana pana zimeongezwa, hivi kwamba kilichokuwa kijiji zamani sasa ni mji. Maduka vilevile yameongezeka. Manunuzi ya maelfu yanaweza kufanywa kwa wakati mmoja. Badala ya shule ndogo ya zamani, kuna shule kubwa tatu, (miongoni mwazo iko moja ya Wahindu na nyingine ya wasichana), na Chuo Kikuu kwa ajili ya masomo ya dini. Ofisi ya Posta iliyokuwa ikipokea barua mara mbili kwa juma, na ambayo ilikuwa ikitumikiwa na mwalimu wa shule, sasa ina maafisa saba au wanane. Kazi za siku zinaongezwa. Magazeti kadha wa kadha yanatolewa; hivi sasa yanatolewa magazeti haya; moja la kila juma mara mbili; mawili ya Kiurdu yenye kutoka kila juma na jingine la Kiingerza, moja la mwezi mara mbili na mawili ya kila mwezi. Kuna mitambo ya kupigia chapa, mmojawapo ni wa mashine. Vitabu vingi hutolewa kila mwaka. Jina Qadian limekuwa imara katika ramani ya posta. Miji mikubwa inaweza kupoteza barua zao lakini sio Qadian. Kwa ufupi, katika hali za kinyume, Qadian imepanuka kwa namna isiyo kifani. Upanuzi wake ni kinyume na kanuni za uchumi. Kupanuka kwake kusiko kwa kawaida ni dalili ya ukweli wa maungano na Mwenyezi Mungu. Wale walioijua Qadian na mahala ilipo, (wawe wa dini gani), wanakubali ya kuwa Qadian imepanuka na inapanuka. Wanaweza kuufikira kuwa tukio lisilo la kawaida. Lakini ole wao ambao hawaulizi kwa nini matukio haya yatukia kwa ajili ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. tu!

## BISHARA YA KUMI NA MOJA: MSAADA WA FEDHA

Mfano wa pili wa bishara zinazoahidi maendelo na ufaulu ni bishara kuhusu mwongezeko wa msaada wa fedha. Bishara hii ilitumikiwa na njia za ajabu sana. Kwa hakika, ilikuwa bishara katika

bishara kubwa kubwa za kwanza kabisa za Masihi Aliyeahidiwa. Ilitokea hivi ya kwamba baba yake Hadhrat Ahmad alikuwa mgonjwa. Mpaka wakati huo Hadhrat Ahmad a.s. hakuwa na mazoea ya kupata ufunuo. Siku moja ilionekana kwamba baba yake alikuwa hajambo. Ilibakia tumbo kuendesha kidogo. Hadhrat Ahmad akapata ufunuo:

"Naapa kwa mbingu na kwa ajaye usiku."

Ajaye usiku (kwa Kiarabu, Taariq), maana yake ni kile kinachokuja usiku. Hadhrat Ahmad akaelewa ya kuwa ufunuo huu ulitabiri wakati wa kifo cha baba yake na ya kwamba ulikuja kama rambi rambi juu ya msiba uliokaribia - huruma ya Mwenyezi Mungu katika huzuni hiyo. Mitaji mingi ya mapato ya jamaa hii iliungana na baba yake, kama ujira wa uzeeni na bahashishi, na sehemu ya mali. Hivi vyote ilikuwa viende. Lakini ukaja ufunuo wa pili na huu ulikuwa na bishara kubwa ndani yake. Ulisema:

"Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi Wake?"

Ufunuo ulifikisha kwa Hadhrat Ahmad a.s. ahadi ya kwamba Mwenyezi Mungu atamwangalia na kukidhi haja zake zote. Akisimulia ufunuo huukwa rafiki zake Mabaniani na Waislamu. Mmoja wa Wahindu ambaye bado yu hai, alipelekwa Amritsar apate kutengenezesha pete iliyochorwa manneo ya ufunuo huu. Elimu ya ufunuo huu ikaenea. ubora wake ulithibitika zaidi wakati, kwa majaliwa, sheria juu ya mali ya jamaa ilipoanza katika jamaa yake. Hata vile vilivyoelekea kusalia na Hadhrat Ahmad a.s. tokana na mali ya jamaa ilionekana vikiponyoka. Kaka yake akaangalia mambo ya jamaa. Migogoro ikatokea baina ya kaka huyu na ndugu wengine. Hadhrat Ahmad a.s. akatoa shauri ya kuwa wawafanyie ndugu wengine zaidi kuliko kawaida. Kaka hakukubali. Mashauri

yakafikishwa mahakamani. Kaka huyu akamwomba Hadhrat Ahmad aombe dua na akaomba, lakini alionywa ya kuwa kaka huyu atakosa na ndugu wengine watashinda. Onyo likathibitika kuwa la kweli. Zaidi kuliko theluthi mbili ya mali ya jamaa ilikwenda kwa wengine, kidogo sana ilibakiwa nao. Ya kutosha kwa matumizi, lakini haikuwa ya kutosha kwa kazi kubwa ambayo Hadhrat Ahmad a.s. alikaribia kuichukua. Alikuwa akitayarisha kitabu chake Baraahin Ahmadiyya, kazi iliyokusudiwa kuleta badiliko katika ulimwengu wa dini. Kuchapishwa kwa kitabu hiki kulihitaji fedha. Kupatikana kwa fedha kulionekana hakuwezekani. Kukawezekana kwa njia za kimwujiza. Watu wasiokuwa na mapenzi ya dini walivutwa kusaidia na kutoa fedha za kukipigisha chapa. Sehemu nne za kitabu hiki zikapigwa chapa. Lakini ilikuwa wazi kwamba fedha zaidi na zaidi sasa zilihitajiwa. Sehemu zilizopigwa chapa ziliwafadhaisha waumbuzi wa Islam. Waliacha kushambulia Uislamu, bali walianza kumshambulia Hadhrat Ahmad. Chuki kubwa ikatokea. Waalimu wa Kibaniani, wa Kikristo na Kisingasinga, walijiunga. Hadhrat Ahmad akabezwa kwa funuo zake. Makusudio ya propaganda yao yalikuwa ni kuwafarakisha watu kwa maandiko yake juu ya Islam na kuwasalimisha waumbuzi wa Uislamu katika kushindwa kulikoonekana hakuna budi. Waislamu wengine, kwa wivu, wakajiunga nao. Kushambuliwa kwa Hadhrat Ahmad kukaja tokea katika pande nne. Ili kuondoa mashambulio haya fedha zaidi zilihitajiwa. Mashambulio ya Waislamu na ya wasio Waislamu ililazimu yakabiliwe ili kulinda utukufu wa Dini ya Islam. Alhamdu lillah, njia hazikubaki nyuma.

Na sasa Hadhrat Ahmad aliendelea kweye sehemu ya tatu ya maisha yake. Akaanza kupata funuo kwamba yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa katika bishara za zamani. Ya kwamba Masihi wa kwanza si mzima mbinguni, bali alikufa kama wanadamu wengine. Kwa kutangazwa madai haya, wengi waliokuwa wameungana naye wakamwondoka. Watu arobaini tu walikubali madai haya na kufanya Bai'at. Sasa Hadhrat Ahmad a.s. akawa katika vita na dunia nzima. Rafiki wengi wa tangu zamani wakajiunga na maadui na kuanza kufanya uovu wao. Fedha zilizohitajiwa zikaanza kupita makadirio yote. Majibu kwa maadui, kutangazwa kwa madai na dalili za madai,

pia kupigisha chapa vijigazeti kwa kuwaongoza wafuasi, yalikuwa madaraka mazito. Wakati huohuo uwezo wa Mwenyezi Mungu ukawa ujidhihirishe katika njia mpya. Bado madaraka makubwa yalikuwa yaletwe na Hadhrat Ahmad. Mwenyezi Mungu alimwamrisha kuanzisha nyumba ya wageni katika Qadian na kuwakaribisha watu wote kuja na kukaa wakiwa wageni wake; wapate mwongozo wa moja kwa moja katika dini; na waondolewe mashaka na taabu zao kwa fungamano maalum pamoja naye. Kuondokewa na marafiki wa zamani na wasaidizi, mwongezeko wa mahitaji ya kuchapisha na kutangaza, na sasa kujenga nyumba ya wageni na kuangalia msururu wa wageni, kulileta mzigo mkubwa. Ingeweza kuvunja Mwendeleo tokea mwanzo kabisa, kama Mwenyezi Mungu asingekuwa tayari kwa msaada wake. Watu wachache waliokuwa wamejiunga naye (na bila hata tajiri mmoja miongoni mwao; wengi wao kwa kweli maskini sana), walionesha kuwa sawa na shida. Mwenyezi Mungu akajaza shauku ya ajabu katika akili za hawa watu maskini. Wakastahamili taabu na maumivu, lakini hawakuacha imani ipotee. Kijuu juu, mapenzi yao na sadaka yao, lakini hasa Ahadi ya Mwenyezi Mungu katika ufunuo, "Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi Wake"? ilikuwa kazini.

Jamaa ya Ahmadiyya sasa ikapambana na dhulma kubwa. Masheikh walitoa Fatwa ya kwamba adhabu ya Waahamdiyya ni kifo. Kuteka majumba yao na kunyang'anya mali zao na kuoa wake zao pasipo kawaida ya talaka kulikuwa sio halali tu bali tendo la thawabu. Watu wenye nia mbaya na mawazo ya uhalifu wakiona udhuru wa kuonesha tamaa zao walianza kufanya sawa na Fatwa hii. Waahmadiyya walitolewa majumbani mwao na kutolewa kazini kwao. Vile vile walinyang'anywa chochote walichokuwa nacho. Wokofu katika taabu hizi zote ulikuwa tu kuhamia Qadian. Msururu madhubuti wa wahamiaji Qadian uliongeza matumizi ya malazi na chakula cha kuwalisha. Jumuiya sasa ikawa na watu toka elfu mpaka elfu mbili, lakini kila mmoja wao alikuwa ametolewa kwa sababu ya uadui na chuki. Waliishi katika wasiwasi wa kuendelea; wasiwasi juu ya maisha yao, heshima, vitu vyao na mali zao. Vilevile walikuwa na majadiliano ya kila siku kuhusu hitilafu. Na bado

walipata fedha zilizohitajiwa kwa kueneza Uislamu, kwa kuwalisha na kuwaweka wageni, na kwa ajili ya idaidi iliyooongezeka ya wahamiaji. Mamia ya watu walipata chakula chao mara mbili kwa siku katika jumba la wageni lililoimarishwa na Hadhrat Ahmad a.s. Waliokuwa maskini sana miongoni mwao walikidhiwa haja zao mbili. Wakazi wengine vilevile waliwakaribisha wageni na wahamiaji. Kila nyumba katika Qadian ilikuwa wazi kwa makusudio haya. Nyumba ya Masihi Aliyeahidiwa mwenyewe daima ilikuwa imejaa. Kila chumba katika nyumba hiyo kilisitiri wageni, pengine jamaa nzima. Mzigo wa matumizi uliokuwa mzito tayari ukawa mzito zaidi na zaidi. Shida mpya na madaraka mapya yaliongezeka kila siku. Lakini wasiwasi haukukaa. Uliondolewa na ahadi ya mbingu - "Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi Wake?" Sababu ambazo zilionekana kuogofya kuwako kwa Jumuiya, zikageuka kuwa mali; mianzo ya udhaifu ikageuka kuwa ya nguvu. Radi zikageuka kuwa mwangaza zikikaribisha mvua. Kila tone likaitika mwito wa ahadi ya msaada wa mbingu - "Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi wake?" Shida za siku hizo zinaweza kudhaniwa vyema. Watu wa Afghanistan, wakati mmoja, iliwabidi wapokee msururu wa wahamiaji kutoka India. Afghanistan ilikuwa na serikali iliyokuwa tayari kuwapokea. Wahamiaji wengi waliangalia matumizi wao wenyewe. Idadi ya wenyeji ilikuwa kubwa zaidi ya wageni. Waafghanistan milioni kumi waliwakaribisha mia au mia mbili elfu ya wahamiaji. Na bado shida zilitokea. Taabu ya mapato ya Jumuiya, ya maskini elfu moja au mbili kuwalisha mamia kadha ya wahamiaji, na ya kutoa fedha kwa ajili ya kueneza Uislamu inaweza kufikiriwa vyema. Na tusisahau, ya kuwa kundi dogo lililobeba yote haya halikuwa limeishi katika amani, bali mashaka makubwa.

Haja na madaraka ya Mwendeleo hayakuwa ya kwisha mnamo siku kadha ua miezi, au hata miaka. Yaliongezeka toka mwaka hata mwaka. Lakini kila mwaka msaada wa Mwenyezi Mungu ulifika na kutoa njia zilizohitajiwa. Katika mwaka 1889, Hadhrat Ahmad a.s alifungua Shule Kubwa moja kwa ajili ya elimu ya vijana wa Jumuiya. Shule hii ilikuwa na upande maalumu wa dini. Madaraka ya fedha yakasonga mbele. Baadaye kidogo magazeti ya kila mwezi

mawili, moja la Kiingereza moja la Kiurdu, yakaanzishwa kwa ajili ya kueneza Uislamu. Shughuli za Jumuiya zikapanuka. Njia zilizotolewa na Mwenyezi Mungu. Hivi sasa Jumuiya inaendesha Shule ya wasichana katika Qadian, shule ndogo na za kati katika mahala pengine. Vilevile ina wahubiri wengi wa kufanya kazi katika Bara Hindi. Jumuiya kwa ajili ya kueneza Uislamu zinaangaliwa katika kisiwa cha Mrisi, Sri Lanka, Uingereza na Amerika. Vilevile kuna jumla ya watu katika markazi kusimamia na kuongoza kazi ya Jumuiya. Kuna idara za waandishi na watungaji, idara ya kuongoza na elimu, idara ya taratibu za Jumuiya, idara ya usuluhishi wa mabishano, idara ya Fatwa za sheria za dini, na kadhalika. Matumizi ya fedha za Jumuiya yalifikia rupia laki tatu au nne. Kupanda huku kwa madaraka ya matumizi ya Jumuiya kunakidhiwa na rehema maalumu ya Mwenyezi Mungu iliyoandikwa katika ufunuo "Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi wake?"

Jumuiya inabakia maskini. Ni katika kufuatana na kanuni ya Mwenyezi Mungu inayoruhusu maskini tu kujumuika kwa nabii wa Mwenyezi Mungu mwanzoni. Watu huwadharau wafuasi wa mwanzo. Quran inasimulia usemi wao:

"Hatuoni ila wamekufuata wale waonekanao dhaifu wetu" (11:28).

Hekima ya kanuni hii ni kwamba mafanikio ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hayawezi kunasibishwa na msaada wa wanadamu. Hakuna rafiki wala adui awezaye kusema hivi. Jambo hili ya kwamba jamaa ndogo na maskini inaweza kuangalia mzigo mkubwa wa matumizi linawezekana tu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Wanachama wa Jumuiya wanalipa kodi ileile inayolipwa na raia wengine. Wanalipa ushuru uliokadiriwa kwa radhi zao. Wanalipa barabra, hospitali, shule na kadhalika. Wana wajibu wao mwingine wa kawaida wanaoutimiza kwa fedha; lakini pamoja na hayo, wana madaraka ya kujitolea kwa ajili ya kueneza Uislamu ambayo pia wanayatimiza. Wamefanya hivi sasa kwa miaka thelathini na tano. Naam, katika muda huu baadhi ya wenye hali nzuri na matajiri wameingia katika Jumuiya, lakini tena hapo

madaraka ya Jumuiya yameongezeka. Ingeonekana ni ajabu kwamba wakati watu wengine, ambao ni matajiri na waliofanikiwa sana, wananung'unikia matumizi yao wenyewe, Waahamdiya kila mwaka sio tu kwamba hawanung'unikii matumizi yao bali wanatoa malaki ya rupia kwa aliji ya Mwenyezi Mungu. Wengi wanaategemea rehema ya Mungu sana hivi kwamba kama haja itokee wangetoa mali yao yote katika njia ya Mwenyezi Mungu. Je, imani hii na roho hii ilitoka wapi? Ilitoka kwa Mwenyezi Mungu tu. Mwenyezi Mungu tu ndiye anayeweza kutoa mvuto. Alikuwa Mwenyezi Mungu aliyemuhakikishia Masihi Aliyeahidiwa tokea mwanzo kuwa - "Je, Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa Mtumishi Wake?" Hakuna nguvu nyingine ambayo ingeweza kutoa ahadi ya namna hii tena mapema sana kabla. Wakati wa ufunuo huu Masihi Aliyeahidiwa alihofia maisha tu. Basi angewezaje kutumaini kupata fedha nyingi zilizohitajiwa kwa ajili ya madaraka yaliyoongezeka mara kwa mara kwa ajili ya kuenezea Uislamu? Ni nguvu gani ingeweza kuahidi jambo la namna hii na halafu kutimiza ahadi hiyo? Kuna Waislamu wengi duniani. Ni fedha ngapi wanazozitoa kwa ajili ya kueneza Uislamu? Kama Waislamu wengine wa Bara Hindi watoe michango yao sawa na watoavyo wanachama wa Jamia ya Ahmadiyya kwa ajili ya kueneza uislamu, wangeweza kutoa milioni 80 kila mwaka katika makusudio haya. Hii ni kama hatua yao ya uchumi iwe sawa na Waahmadiyya. Lakini Waislamu wa Bara Hindi wana matajiri wengi zaidi kati yao, watawala wa serilaki za kienyeji na wafanya biashara wakubwa. Kama tufikirie mapato ya Waislamu matajri zaidi, Waislamu wa Bara Hindi peke yao wangeweza kutoa rupia milioni 160 kila mwaka kwa ajili ya kueneza Uislamu. Lakini hawatoi hata sehemu kidogo tu ya vile wanavyoweza kutoa watu wa Jumuiya hii maskini kwa ajili ya kueneza Uislamu. Mbona imekuwa tofauti hivi? Ni kwa sababu Waahmadiyya wanasaidiwa na ahadi ya mbingu - "Je Mwenyezi Mungu Hatoshi kwa mtumishi Wake?"

## BISHARA YA KUMI NA MBILI
## MPANUKO WA JUMUIYA

Bishara hii inahusu ahadi ya Mwenyezi Mungu juu ya kuenea kwa mawazo, mafundisho na roho ambayo Hadhrat Ahmad a.s. aliamriwa kugawanya. Haya yalikuwa ni maoni ya mafundisho ya Quran Tukufu, lakini yalisahauliwa na Waislamu na wengine. Bishara hii ilienezwa sana. Ilitangazwa zama ambazo hakukuwa na hata njia ndogo sana za kuelekea kutimia kwa bishara hii duniani. Maneno hasa ya ufunuo ni haya"

"Nitaueneza ujumbe wako mpaka pembe za dunia."

"Nitawaongeza rafiki zako wapenzi na watiifu. Nitaongeza kizazi chao na mali yao na kuwafanya wengi zaidi."

"Yeye, Mwenyezi Mungu ataifanya (Jamaa ya Ahmadiyya) ikue, hivi kwamba ukubwa wake na wingi wake utaanza kuonekana wa ajabu."

"Watakujia (wageni katika Qadian) kwa wingi - kutoka kila nchi ya mbali."

"Hakika Sisi Tutakuongezea kila kitu."

Funuo zingine zilikuja kwa Kiingereza. Mmoja ulisema:

"I will give you a large party of Islam", yaani "Nitakupa kundi kubwa la Islam."

Ufunuo mmoja ulisema:

"Kundi miongoni mwa wa kwanza na kundi miongoni mwa (watu) wa mwisho."

Hii inaweza kuwa maana ya kuwa wanachama wa Jamaa ya Ahmadiyya watatolewa tokana na wafuasi wa manabii wa zamani na kutokana na Waislamu pia.

Mwingine unasema:

"Ewe nabii wa Mungu, nilikuwa sikujui."

Kauli hii ni ya ardhi, kwa maana ya kuwa watu wote wakaao ardhini kwa ujumla watajuta sana kwa kushindwa kumwamini Masihi Aliyeahidiwa.

Ufunuo mwingine unasema:

"Ardhi ni urithi Wetu. Tutaimeza tokeo pande zote."

Baadhi ya funuo hizi ni za siku za mwanzo. Zilipokelewa na kutangazwa zama ambazo Hadhrat Ahmad a.s. hakuwa na hata mfuasi mmoja. Funuo zingine zilipokelewa baadaye wakati ambao Jumuiya haikuwa na kimo chochote. Halikuwa jambo la kawaida kwa Hadhrat Ahmad kutangaza ya kuwa wakati utakuja ambao atakuwa na kundi kubwa la wafuasi; ambao wanachama wa Jumuiya yake hawataonekana katika Bara Hindi tu bali pia katika nchi zingine; ya kwamba watatokea tokana na dini na madhehebu zote; na idadi yao itaongezeka na hakutakuwa nchi itakayokosa kupata ujumbe wake. Kusema jambo la namna hii si rahisi. Mawazo ya wanadamu hayawezi kutoa tabiri za kadiri hii, wala kwa elimu ya kawaida.

Siku hizi ni za elimu. Imani katika dini zote imo katika kupungua. Itikadi zilizoshikwa tokea utoto zinaachwa. Wakristo leo sio Wakristo tena, Wahindu sio Wahindu tena, Mayahudi sio Mayahudi tena, Waparisi sio Waparisi tena. Mahala pa itikadi za zamani pamechukuliwa na maoni ya akili ambayo yanaelekea kuja kuwa itikadi za kidini. Sura za nje zinabakia tofauti. katika uso wa welekea huu, ilikuwa ni upuuzi kutazamia watu kugeukia kwenye mafundisho ya Hadhrat Ahmad a.s. na kushika itikadi alizozifundisha. Wafuasi wa manabii wa zamani, ambao walikuwa wakiwakengeuka manabii wao wenyewe na ambao polepole walikubali namna fulani ya dini ya mawazo, wasingekubali kwa urahisi madai ya Hadhrat Ahmad a.s. Kwa wakati huo huo nguvu

ya Hadhrat Ahmad a.s. kuwafikia watu wote wa dunia ilikuwa ndogo. Alijua lugha ya Kiurdu, Kiarabu na Kiajemi peke yake. Alizaliwa katika India, na Wahindu mpaka miaka 30 iliyopita walikuwa wakichukiwa katika Bara Arabu na Iran. Hakuna aliyeweza kufikiri ya kuwa wenyeji wa Bara Arabu, Iran, Afghanistan, Sham na Misri wangeamini madai ya Unabii yaliyotolewa na Mhindi. wahindi walioelimishwa Kiingereza walianza kufikiri ya kuwa ufunuo ni uongo tu, ya kwamba Quran sio Neno la Mwenyezi Mungu, bali ni la Muhammad Mtume wa Mungu. Waliwezaje kuamini ya kuwa ufunuo ni kweli na ya kwamba Mwenyezi Mungu kwa kweli anazungumza na watumishi Wake? Hata kwa wale wasiojua Kiingereza? Kutokujua Kiingereza ni kama dhambi mbele ya Wahindi walioelimishwa Kiingereza. Hadhrat Ahmad hakujua kabisa lugha za watu wa Magharibi, elimu za Kimagharibi wala desturi na taratibu zao. hakupata kwenda nje ya mkoa wake mwenyewe. Mara moja tu alipata kwenda Aligarh. Mtu wa namna hii, hakuna aliyeweza kudhania ya kuwa angefikisha ujumbe wake nchi za Magharibi na kupata wafuasi. Hakuna aliyeweza kufikiri ya kuwa Wazungu walioelimika kikweli waliojaa dharau kwa Wahindi, wangesikiliza kwa vyovyote mafundisho ya Mhindi, wachilia mbali kuyakubali. Hakuna aliyewaza kufikiri ya kuwa watu katika sehemu mbaliambali za Afrika wangekubali mafundisho ya mtu kama huyu. Hakukuwa na mtu katika Bara Hindi aliyeweza kutumia lugha ya Kiafrika. Taabu hizi kubwa sana ziliondolewa na neno la Mwenyezi Mungu likawa kweli. Mtu mmoja aliyetembea peke yake nyumbani mwake na kuandika funuo za Mwenyezi Mungu kama alivyozipokea; na funuo zikatabiri kukubaliwa kwa mafundisho yake na dunia; hivi katika zama ambazo kijiji chake mwenyewe hakikumjua vizuri. Katika hali ya taabu zote, alitokeza na kunguruma kama radi. Macho ya husuda na uadui yakatazama. Lakini radi ikachoma maini yao na kuwafadhaisha. Ikaenea mawinguni kote na mvua ikanyesha. Ikanyesha Bara Hindi, Afghanistan, Bara Arabu, Misri, Ceylon, Bukhara, Afrika ya Mashariki, Mrisi, Afrika ya Kusini, sehemu za Afrika ya Magharibi, (Nigeria, Ghana na Sierra Leone), Australia, Uingereza, Ujerumani, sehemu za Urusi na Amerika.

Katika kila Bara la dunia, mahali fulani au pengine, wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa wanaweza kupatikana. Hakuna Jumuiya yoyote isiyoingiza bado wafuasi ndani ya Jumuiya yake. Wanachama wa Jumuiya ya Ahmadiyya wametokana na Wakristo, Wahindu, Waparisi, masingasinaga na Mayahudi, pia wametokana na Wazungu, Waafrika na Waasia.

Kama aliyotabiri Masihi Aliyeahidiwa hayakutabiriwa kwa Jina la Mwenyezi Mungu, basi kwa nini yalitimia? Kwa nini yakawa kweli? Ni ajabu kwamba Ulaya na Amerika mpaka leo ziliufanya Uislamu kuwa mateka yao. Lakini sasa, ahsante kwa Masihi Aaliyeahidiwa, Uislamu unaweza kuzifanya ulaya na Amerika kuwa mateka yake. Watu kadha wa kadha katika Uingereza na Amerika wameingia Uislamu tayari. Kadhalika, baadhi wa watu katika urusi, ujerumani na Italy, wamejiunga na Jumuiya. Uislamu uliokuwa ukipata kushindwa mikononi mwa dini zingine sasa unazishinda dini hizo. Hali sasa imepinduliwa chini juu kwa dua na nguvu ya kiroho ya Masihi Aliyeahidiwa. Uislamu unasonga mbele na adui yuko mbioni anarudi. na Mwenye kusifiwa ni Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.

## HOJA YA KUMI NA MOJA: MAPENZI YA MASIHI ALIYEAHIDIWA KWA MUNGU NA MTUME WAKE

Baada ya kutaja baadhi ya bishara za Masihi Aliyeahidiwa a.s., ninaendela na hoja ya kumi na moja kwa ajili ya madai yake.

Hoja hii imesimamishwa kwenye aya maarufu sana ya Quran Tukufu:

"Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu" (29:70).

Na aya nyingine isemayo:

> "Sema: Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni" (3:32).

Aya hizi zinafundisha kwamba mwako wa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. unaleta makutano baina ya mwanadamu na Mwenyezi Mungu. Anayempenda Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. anakuwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu. kwa hiyo mapenzi ya kweli ya Mwenyezi Mungu ni alama ya ukweli na unyofu. Zama ukweli na unyofu wa mtu unafikiriwa, tunatakiwa kuuliza, "je anampenda Mwenyezi Mungu? Je, anampenda na kumtii Mtukufu Mtume s.a.w.?"

Suala la mapenzi ni maarufu sana. Washairi wa nchi zote wanapanua jambo hili. Dini mbalimbali zinashika suala hili kuwa mizani hasa ya imani na ukaribu na Mwenyezi Mungu. Kwa hali yoyote, kipande hiki cha Quran Tukufu:

> "Sema: Kama baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mlizochuma, na biashara mnazoogopa kusimama, na majumba mnayoyapenda ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya juhudi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu Alete amri Yake, na Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu waasi" (9;24).

Kwa mujibu wa kipande hiki, mapenzi kamili ya Mwenyezi Mungu ni kuwa tayari kutoa kila kitu sadaka kwa ajili Yake. Kama mtu fulani hayuko tayari kutoa sadaka kila kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi madai yake ya mapenzi ni bure, madai ya

kinywa tu. Wengi wangesema ya kuwa wanampenda Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume s.a.w. Kwa hakika hakuna Mwislamu ambaye angesema ya kuwa hampendi Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume s.a.w. Bali ni suala la kwamba je, mapenzi anayojidaia yana dalili yoyote ile ya kidhahiri? Je, yanavuta maisha yake ya kila siku, maneno yake, tabia yake na maendeleo yake ya kila siku? Wengi wanaojidaia mapenzi makubwa kwa Mtukufu Mtume s.a.w., ambao wanatunga au kusikiliza kwa shauku sana maneno ya kumsifu, hawajali hata kidogo mambo aliyofundisha na kuyathamini. Mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamo vinywani mwao, lakini hawafanyi lolote kabisa kumpendeza na kupata ukaribu naye. mtu anayependwa sana nasi anapotutembela, tunaweka pembeni kwanza kazi zote za muhimu kwa ajili yake. Panapopatikana nafasi ya kuonana na marafiki, tunafurahi kupita kiasi. Tunapokutana na mfalme, tunaona fahari na furaha sana. Lakini tunafanyaje kwa Mwenyezi Mungu. Tunadai mapenzi kwa ajili Yake, lakini hatujali kujumuika katika Sala tano za kila siku, au tunafanya hivi kwa bahati nasibu zana. Kama tusimamishe Sala tano sawasawa; tunasali kwa haraka ya ajabu; rukuu, sijda na mengine yanaingiana, kwa haraka isiyoonwa. Hakuna kuogopa wala kunyenyekea. Hivihivi katika saumu. Ujira wa saumu, Hadithi sahihi inasema, ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe; na bado wale wanaodai kumpenda Mungu hawatafuti ukaribu naye kwa saumu wa Ramadhan na kupata mapenzi yake; wanadhulumu vya watu, wanatangaza uongo juu yao; na kusengenya. Wanampenda Mwenyezi Mungu, lakini hawajali kukifunua Kitabu Kitakatifu ili kufahamu maana yake. Wanavyokifanyia Kitabu Kitakatifu siyo wanavyozifanyia barua zitokazo kwa rafiki zao. Ni nani ambaye asingeifungua barua ya kutoka kwa rafiki yake? Ni nani ambaye asingeisoma barua kama hiyo kwa makini ili afahamu ujumbe na maana yake kwa hiyo dai la mapenzi ni jambo moja, lakini kufanya sawa na mapenzi ni jambo jingine. Mapenzi ya kweli ni lazima yatafute vitendo. Ni lazima yajioneshe katika sadaka, mathalan. Ishara hii ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na nia ya kujitoa kwa ajili Yake, inapatikana leo kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad na wafuasi wake.

## HAKUPENDA KUFANYA KAZI ZA KIDUNIA

Ushuhuda wa jambo hili unaweza kuonekana katika maisha ya Hadhrat Ahmad a.s. Tokea ujana wake, Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. ndio walikuwa makusudio ya mapenzi yake. Kila sehemu ya mwili wake ililoweshwa katika mapenzi haya. Alisimamisha sheria za Kiislamu tokea utoto wake. Alipenda sana kukaa faraghani kwa ajili ya ibada. Baada ya elimu yake ya mwanzo, baba yake alimtaka kukubali kazi fulani, lakini alikataa kabisa kukubali kazi yoyote licha ya kuwa baba yake alisisitiza. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu faraghani alikupendelea zaiadi kuliko shughuli zingine zozote. Ukoo wake ulikuwa maarufu sana. Kama angejali, angeweza kupata kazi fulani maalumu serikalini. Kaka yake alikuwa na kazi fulani ya heshima serikalini, lakini Hadhrat Ahmad a.s aliepuka haya yote. Sio kwamba hakupenda kazi ngumu. Maisha yake ya baadaye yanaonesha ya kuwa watu wachache tu wanaweza kufanya kazi ngumu zaidi. Mzee mmoja wa Kisingasinga ambaye jamaa yake wameijua jamaa ya Hadhrat Ahmad a.s alikuwa akisimulia tukio moja; hivi licha ya tofauti kubwa kabisa ya dini, na tena akitokwa na machozi: "Safari moja baba yake Mirza Sahib alinituma kumshawishi aonane na maafisa fulani kwa ajili ya kazi kama karani wa kodi. Tulimkuta Mirza Sahib katika faragha yake, akijisomea. Tulimhadithia madhumuni hii. Je, baba yake, aliuliza, alimtaka afanye kazi serikalini? Kama ni hivyo, jawabu lake lilikuwa - "amekubali kumtumikia Mmoja Mwingine; kwa hiyo, ilifaa aachwe peke yake."

Siku hizo alikuwa ameshughulika katika kusoma Quran Takatifu, Hadithi za Mathnawi Rumi. Alipata wageni wake lakini walikuwa ni maskini na mayatima aliowalisha chakula chake mwenyewe cha kila siku. Mara nyingi, kwa ajili yao alikosa chakula na kutosheka. Mtu wa faraghani aliweza kusahauliwa kwa urahisi; mara nyingi jamaa ya kaka yake walisahau kumpelekea chakula.

Safari moja aliamua kuondoka Qadian na kukwepa wasiwasi ulioendelea kumsumbua baba yake kwa ajili yake. Alikwenda Sialkot na huko akakubali kazi katika mahakama ya Wilaya. Alitumia wakati wote aliopata baada ya kazi ya mahakamani katika

kusoma na ibada. Alipokaa Sialkot, alitambua kwa mara ya kwanza kwamba Uislamu ulikuwa mashakani na ya kwamba Ukristo na dini zingine zilifikiria kuzima kabisa. Sialkot ilikuwa markazi ya kazi za Ukristo. Mapadre waliweza kuonwa wakihubiri Ukristo waziwazi mitaani na viwanjani. Waliushambulia Uislamu na kuzidisha chuki juu yake. Hadhrat Ahmad a.s. alistaajabu kuona kwamba hata mtu mmoja hakujitokeza kuto majibu. Ukristo ulikuwa ni dini ya watawala; kwa hiyo watu waliogopa kupambana na wahubiri wa Kikrsto waziwazi. Masheikh walikwepa kuwajibu Mapadre. Baadhi yao walithubutu walishindwa. Walikuwa na elimu ndogo ya Quran Tukufu, na walikuwa wakishindwa katika majadiliano. Kwa kuona haya, Hadhrat Ahmad a.s. akaazimia kukutana na mapadre waziwazi, na halafu maadui wengine wa Uislamu kama vile Maarya. Punde kidogo, baba yake akamtaka arudi Qadian. Pengine alifikiri ya kuwa mwanaye amesuluhika kukubali kazi serikalini. Kwa hiyo, akaanza mashawishi yake tena na kumtaka akubali kazi fulani ya heshima sana serikalini. Mwana akamwomba baba mtu aache majaribio haya. Lakini aliona baba yake akijitia katika taabu za namna nyingi; mbaya kabisa ni juu ya madai ya jamaa yake. Hadhrat Ahmad akakubali kumfariji baba yake kwa kuhudhuria mahakamani. Alipokuwa akifika mahakamani, shughuli yake ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu ilidhihirika zaidi. Ilikuwa imekuwa sehemu ya maumbile yake. Safari moja alifika mahakamani, lakini mashauri yalikuwa hayajaanzwa. Wakati wa Sala ulifika. Wengine hapo mahakamani walisisitiza akae kwani mashauri yangeweza kuanzwa wakati wowote. Lakini Hadhrat Ahmad a.s. hakukaa. Shauri alilofuata lilianzwa alipokuwa hayupo. Alikwenda kuitwa lakini hakuja mpaka alipomaliza kusali. Kwa haki, katika mashauri haya, angeshindwa. Hakimu akapuuza kutokuwako kwa Hadhrat Ahmad a.s. na kukata shauri kwa kumpa haki yeye; kwa kumpa haki baba yake kuwa mwaminifu. Tukio jingine linaloonesha shughuli yake katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu linasimuliwa na rafiki yake wa zamani sana aliyeishi Lahore. Rufani ambayo kama ingeshindwa ingemtia hasara kubwa baba yake na jamaa yote, ilifikishwa katika mahakama kuu ya Mkoa. Hadhrat Ahmad alirudi kutoka mahakamani akiwa mwenye kutosheka na

furaha. Rafiki yake alifikiri kuwa rufani ile imefaulu. Hivyo alikwenda kumpa pongezi. "Lakini", alisema Mirza Sahib, "si kweli kwamba ameshinda. Alijisikia mwenye kutosheka, kwa sababu sasa kwa wakati fulani atapata wakati wa faragha kwa ajili ya kufanya ibada." Hatimaye aliona kwamba asingeweza kushughulishwa vile. Baada ya kufikiri alimwomba mzee wake amtoe katika kazi zinazohusu madai ya jamaa. Barua hii ifuatayo inaonesha kutopenda dunia kwa Hadhrat Ahmad a.s. hata tangu ujana wake. Alitaka wakati wake wote uwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Sawa na desturi barua iliandikwa kwa Kiajemi:

"Bwana wangu na baba yangu, Salaam!

Kwa utii na unyenyekevu mwingi, ninaomba kukusihi ya kwamba ninaweza kuona kwa macho wazi kabisa ya kuwa kila mwaka msiba fulani unahujumu nchi na miji ambao unawatenganisha rafiki na rafiki na ndugu na nduguye. Misiba hii na maonesho haya ya huzuni, yanaleta maombolezo na majuto makubwa kila mwaka. Kwa kuona hivi vyote, moyo wangu umegeuka kuwa baridi kwa dunia, na uso wangu umefifia kwa woga. Mara kwa mara ninakumbuka mistari miwili kutoka kwa Sheikh Muslih-ud-Din Saad wa Shiraz na machozi hunitoka ninapokumbuka:

"Usitegemee maisha haya mafupi; usifikiri ya kuwa u salama katika mchezo wa dunia."

Mistari miwili tokana na ubeti wa Farrukh wa Qadian (Seyidna Ahmad mwenyewe) pia inafanya kama chumvi kwa ajili ya moyo wangu ulioumia:

"Ewe kijana, usiweke moyo wako juu ya dunia hii hafifu;
Wakati wa mauti unaweza kuja ghafla."

Kwa hiyo, ninatamani kutumia maisha yangu yote yaliyobaki katika faragha, kuepuka kuchanganyika na watu na kubakia mashghuli katika ibada ya Mwenyezi Mungu, huenda iwe fidia kwa uzembe uliopita na kujikinga na maangamizi.

"Maisha yamepita na hakuna kilichobaki isipokuwa hatua chache. Kwahiyo, ni afadhali niwe macho kwa mausiku machache katika kumkumbuka fulani Mmoja."

"Dunia hii haina msingi imara na maisha hapa si ya kutegemewa."

"Mwenye busara ni yule anayejifunza tokana na mfano wa wengine."

Wassalaam."

Baba yake alipokufa, alijiepusha na kila kitu cha kidunia, akashika maisha ya kujisomea, kusali, kufunga saumu, na kuabudu usiku. Mara kwa mara aliandika magazetini majibu ya mashambulio ya maadui wa Uislamu. Kinyume na desturi, Hadhrat Ahmad alimpa kaka yake mali yake. Alipata chakula chake kutoka kwake, nguo zake pia alipata kutoka kwake. Hakuchukua chochote katika mali ya jamaa wala hakutoa wakati wake wowote kwa kuiangalia. Alitumia wakati wake wote katika kufasiri uzuri wa Uislamu na kuwahimiza watu kusali na kufunga saumu. Aliwaitika maskini na wenye haja. Akiwa na kidogo cha kutoa alishirikiana katika chakula chake, yeye mwenyewe akiishi kwa wakia chache tu za chakula kila siku au pengine bila ya chochote kabisa. Sehemu yake ya mali haikuwa ndogo hivi kwamba aliweza kuipuuza kwa kukosa riziki. Alichangia kijiji chote na kaka yake na mapato yaliyotoka katika mali nyingine yaliongezeka.

## ALIFADHAISHWA NA HALI YA UISLAMU

Katika wakati huo alifadhaishwa na hali ya Uislamu. Akaamua kujitoa kwa ajili ya ibada, kuomba ghofira na kuwa mnyenyekevu. Kwa kufuata dokezi kutoka kwa Mwenyezi Mungu alianza kuandika kitabu chake kikubwa *Baraahiin Ahmadiyya.* Katika kitabu hiki aliahidi kueleza dalili 300 kuthibitisha ukweli wa Dini ya Islam. Kitabu hiki, alisema, kitakuwa silaha kali katika kulinda fundisho la Islam. Sehemu nne tu ndizo zilitoka. Hata hivyo, kitabu kilipata sifa kubwa kwa marafiki na maadui kadhalika. Masheikh wakubwa wakubwa wa wakati huo walisema ya kuwa kitabu hiki hakikupata mfano wake tokea miaka 1300 iliyopita. Uislamu ulikuwa na waandishi wake na watungaji vitabu; kwa hiyo, tukichungua msatri huu uliopambanuka, sifa iliyotolewa kwa ajili ya *Baraahiin Ahmadiyya* inajisemea yenyewe. Hadhrat Ahmad a.s akatafuta

nafasi zingine kuandika na kutangaza Uislamu. Kama kulikuwa na gazeti lolote ambalo angeweza kuandika ndani yake ubora wa Uislamu, aliharakia kuandika na kujibu maadui za Islam. Kadiri alivyoanza kujulikana, chuki juu yake pia iliongezeka. Lakini alidumu katika kazi ya Uislamu bila kujali uadui wa watu.

Kwenye hatua hii mashambulio mabaya yalifanywa juu ya maisha na tabia ya Mtukufu Mtume s.a.w. Waandishi wa Kikristo na Maarya walikuwa mbele katika genge hili na kutukana. Lakini Masheikh wa Hindustan walikuwa mashughuli wakitoleana fatwa za ukafiri. Uislamu ulisonga karibu na maangamizi na Masheikh walikuwa wakicheza cheza. Walijadiliana juu ya maswali ya kijinga: "je, halali kuinua mikono miwili pamoja na takbira wakati mtaabadi anapokwenda toka sehemu moja hata nyingine ya Sala? Je, maamuma waseme *Amin* kimya kimya au kwa sauti kubwa? Haya na maswali mengine ya namna hii ndiyo yaliyokuwa shughuli yao kubwa. Ni Masihi Aliyeahidiwa tu ndiye aliyehusika na kuulinda Uislamu katika mashambulio ya maadui zake. Ni yeye tu aliyepinga mabishano ya Kimadhehebu waziwazi. jambo la maana halikuwa ni nani aliyekuwa mkweli, Wahanafi au Ahli hadith. Bali jambo la maana lilikuwa ni utumishi wa shauku uliosimamishwa na itikadi zilizoshikwa na upendo. Walichohitaji kilikuwa ni kujiepusha na njia zisizo za dini na uzembe; badala yake, mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Sheria Zake. Miongoni mwa Maarya alioshindana nao Hadhrat Ahmad a.s., alikuwa Pandit Dayanand, pia Lekh Ram, Jiwan Das Murli Dhar, na Indar Man. Akishindana na hao wote pamoja, Hadhrat Ahmad aliingia katika majadiliano ya hadhara. Aliwashika mpaka walitoka uwanjani au kuangamia. Miongoni mwa wahubiri wa Kikritsto alioshindana nao Hadhrat Ahmad alikuwa Fateh masih, Atham, Martin Clark, Howell, Wright, Talib Masih. Kuandika hakukumtosheleza. Aliweza kuandika na kuyatoa maandiko yake yafasiriwe kwa Kiingereza na kupigishwa chapa nakala mamia ya maelfu na kuyazagaza Ulaya na Amerika. Kama alimsikia yeyote mwenye hamu ya Uislamu, alimuandikia na kumkaribisha akubali ukweli. Msilimu maarufu sana wa Kiamerika Alexander Russel Webb, alikuwa ni tunda la juhudi zake. webb alikuwa Mwamerika

aliyeheshimika sana. Aliitumikia nchi yake akiwa Balozi wake. Hadhrat Ahmad a.s. alimwandikia. Hatimaye Alexander Webb alikubali Uislamu, akaacha kazi yake na kuwa Mbashiri wa Kiislamu. Hadhra Ahmad alitawaliwa na hamu kubwa mbili: Umoja wa Mwenyezi Mungu na ukweli wa Mtukufu Mtume s.a.w. Kila siku alikuwa tayari kuthibitisha na kueleza mafundisho haya mawili ya islam. Akili yake haikushughulikia jambo lingine lolote. Baadaye, baada ya kutangaza madai yake, alikuwa mashughuli zaidi na zaidi katika mafundisho haya. je, kulikuwa na adui wa Uislamu popote pale? Kama alikuwako, Hadhrat Ahmad alikuwa tayari kupigana. Kama mtu yeyote alifikiri kuushambulia Uislamu, Hadhrat Ahmad alikuwa tayari kupambana na mashambulio hayo. Dowie, mwongo wa Amerika, amekwisha tajwa. Mara alipomsikia tu, Hadhrat Ahmad aliamua kupambana naye haidhuru ng'ambo ya bahari. Hivihivi alimwita Piggot, nabii wa uongo wa Uingereza aliyejidaia uungu. Kama kulikuwa adui wa Islam popote duniani, ilimbidi kupambana na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Halafu mapigano yangeendelea mpaka adui alikimbia au alikufa. Aliishi miaka sabini na nane. Usiku na mchana mnamo maisha yake haya marefu alishughulika na utumishi wa Uislamu. Mara nyingi alijitia kwa miezi katika kutunga vitabu na kuwa mashughuli sana hivi kwamba hakuna aliyeweza kusema kama alikuwa akipata usingizi saa ngapi. Shughuli yake kwa Mwenyezi Mungu na mtume s.a.w. ilikuwa kubwa. Kuutumikia Uislamu kulionekana kama kujitumikia mwenyewe na wapenzi wake. Kama alipata msaada wowote kwa kazi hii, alishukuru sana. Usiku baada ya usiku aliweza kuupitisha bila usingizi wa kawaida kwa kufanya kazi. Kama mtu yeyote alimsaidia, tuseme, katika kulinganisha au kusahihisha nakala au kusoma *proof*, au kukaa naye kwa usiku mmoja au mausiku mawili, alimshukuru kama vile alimtendea jambo kwa manufaa yake mwenyewe. hakujali kama kazi ya Uislamu ilikuwa ni ya watu wengine. Kuutumikia Uislamu alifikiri ni kumtumikia yeye mwenyewe binafsi. Licha ya kuumwa umwa kwa mara kwa mara, aliandika zaidi ya vitabu themanini na vijigazeti mamia kadha na pia alitoa hotuba mamia na mamia. Pamoja na hayo, alipata wageni wa kila siku ambao alikuwa akiwahutubia juu ya Uislamu, kuhusu

uzuri na mafundisho yake. Matabibu wangemshauri apumzike, lakini kupumzika mbele yake, angesema, kulikuwa ni kuendelea kueleza maana na makusudio ya Uislamu na kupigana na maadui zake. Hata siku aliyofariki alikuwa mashughuli kwa kazi hii, shauku ya maisha yake. Alifariki mnamo asubuhi moja. Jioni ya kabla yake alikuwa mashughulini alimaliza kitabu cha kuwakaribisha Wahindu kwenye kuuelewa Uislamu. Tokana na haya, mtu anaweza kupima kiasi cha shauku yake na kina cha mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume s.a.w. Alikuwa na hamu moja nayo ni kuwadhihirishia watu wote uwezo wa Mwenyezi Mungu na ukweli wa Mtukufu Mtume s.a.w.

## ALIMSIFU SANA MWENYEZI MUNGU

Kiasi cha mapenzi kama nilivyosema hakipimwi kwa mbwato wa maneno. Hapa alikuwako mtu aliyethibitisha mapenzi yake kikweli. Aliyethibitisha katika matendo yake madogo madogo sana na hata hatua zake ndogo sana. Madai ya mtu huyu yana mpango tofauti. Ni wakala wa kweli wa fikara zake za ndani sana. Mapenzi ya kweli hupimwa kwa matendo. Kadhalika hupimwa kwa mawazo na fikara za ndani sana ambazo zinatokea kuwa ishara njema za mapenzi ya mdomo. Kuwa vilio vya mtu mkweli yanatoboa mioyo ya wengine. Ninatoa hapa mashairi mawili ya Masihi Aliyeahidiwa, moja lililoandikwa kwa ajili ya mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu, na jingine juu ya Mtume s.a.w.

Bwana wangu Mkarimu, maisha ni dhabihu kwa ajili Yako,

Umebakisha nini kwa ajili yangu, ili nami nibakishe chochote kwa ajili yako?

Kila tamanio na kila ninayomwomba Asiyeonekana, Kila hamu ambayo moyo wangu unataka kuomba,

Imefanikiwa kwa Huruma Yako, Kwa kweli Umekiheshimu kibanda changu hiki kwa ziara Yako ya Rehema.

Sikujua chochote kuhusu mapenzi au utii. Ni Wewe uliyejaza kifua changu utajiri wa Mapenzi Yako.

Ee, Uliyegeuza udongo huu kuwa dhahabu, Ilikuwa ni Uzuri

Wako ulioniazima mimi uzuri wa rehema.

Mwangaza wa moyo wangu si kwa sababu ya utawa wangu wala toba yangu. Ni Wewe uliyeniangazia fadhila Zako na zawadi Zako.

Mamia ya fadhili Zako zimemiminika juu ya mwili huu wa udongo. Roho yangu na mwili wangu unawiwa shukrani nyingi kwa huruma Yako isiyokwisha.

Ni rahisi vilioje kuziacha dunia mbili, kama mapenzi Yako yanaweza kusikiwa nami, Ee, kimbilio langu, ngao yangu, amani yangu!

Haunifai musimu wa maua, hewa nzuri! Maana daima nimo bustanini nikiwazia Uso Wako.

Ninaweza kuwa na haja ya mtu anayeweza kunifundisha? Nimepata mafunzo kwa Bwana wangu Mlinzi.

Ukarimu wa milele umekuja karibu sana nami. Hivi kwamba sauti ya Bwana inanifikia toka kila sehemu na pembe za mbali.

Ee, Mola nifanye imara katika kila hatua. Ule mchana usiwepo ambao ndani yake ningevunja ahadi yako!

Kama wapenzi Wako wanauawa kwa ajili ya kukupenda Wewe,

Basi nitakuwa wa kwanza kutangaza mapenzi yangu kwa ajili yako.

## ALIMSIFU MTUME S.A.W.

Kuna nuru ya mwujiza ndani ya roho Muhammad, kuna kito cha jabu katika chimbuo la Muhammad.

Moyo hutolewa giza lote, kama ukiwa mmoja wa wapenzi wa Muhammad.

Ninastaajabia busara ya wapumbavu hao wanaoondoka katika karamu iliyoandaliwa na Muhammad.

Simjui yeyote katia dunia mbili, anayeshiriki katika ukubwa na utukufu wa Muhammad.

Mara mia Mwenyezi Mungu anachukizwa na kile kifua, ambacho kina uadui kwa ajili ya Muhammad.

Mwenyezi Mungu Mwenyewe humteketeza motoni, mdudu dhaifu anayechagua kuwa mmoja wa maadui za Muhammad.

Kama unataka kuuaga ulevi wa nafsi mbaya, basi njoo ukae miongoni mwa wapenzi wa Muhammad.

Kama unataka ya kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe aimbe sifa zako, basi imba kwa shauku sana sifa za Muhammad.

Je, unatazama ushuhuda wa ukweli wake?

Basi anza kumpenda, kwani Muhammad mwenyewe ni ushuhuda wa Muhammad.

Nina kichwa nitoe sadaka kwa ajili ya vumbi alilokanyaga Ahmad.

Na moyo ulio tayari kutolewa dhabihu kwa ajili ya Muhammad.

Ama niuawe au nichomwe moto katika njia hii, sitageuka kamwe kutoka barazani pa Muhammad.

Kwa ajili ya kazi ya dini, siogopi hata dunia nzima; kwani nimechukua rangi katika imani ya Muhammad.

Kila sehemu ndogo sana yangu imetolewa sadaka, katika njia yake kwani nimeona uzuri uliojificha wa Muhammad.

Sijui jina la mwalimu mwingine, kwani nimesoma katika shule ya Muhmmad.

Ninapenda kutazama lile jicho tu zuri, sitaki chochote isipokuwa bustani ya Muhammad.

Usitazame moyo wangu unaodundwa upande wangu, kwani nimeufunga kanzuni mwa Muhammad.

Mimi ni ndege mtamu niliyetoka katika kundi takatifu, ambalo lina kiota chake katika bustani ya Muhammad.

Umemulika roho yangu kwa mapenzi yako, niwe dhabihu kwa ajili yako, roho ya Muhammad.

Hata kama ingenilazimu kutoa maisha mia katika njia hii, bado ingeshindwa kufikia thamani ya Muhammad.

Ni kishindo kilioje anachotishia huyu kijana (Muhammad)?

Hata hakuna mtu anayeweza kupambana naye uwanjani pake!

Amka ewe adui mpumbavu uliyepotoka, uogope upanga mkali wa Muhammad.

Njia ya Mwenyezi Mungu ambayo watu wameipotea mbali, bado unaweza kuiona na wafuasi na rafiki za Muhammad.

Sikiliza ewe ukataaye ukuu wa Muhammad na nuru imulikayo ya Muhammad!

Ijapokuwa miujiza inaonekana kama jambo lililopita, hebu njoo uione kwa watumishi wa Muhmmad.

Huyu ndiye mtu aliyetumia hasa kila hatua ya maisha yake katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu, akieleza ujumbe wa Mtume s.a.w. na kueleza mapenzi yake kwa ajili yake na mafundisho yake. mtu huyu alitaabika mikononi mwa watu wa taifa lake mwenyewe na wengine, kwa sababu ya mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu, fikara yake kwa jina na heshima ya Mtume s.a.w. Kila sehemu ya mwili wake, akili na roho, ilitolewa kwa kumtumikia. Je, mtu kama huyu anaweza kupotoka, kuasi na kuwa Dajjal? Kama yote aliyofanya na kusema na kufikiri yanafanya uasi; kama mapenzi ya aina hii yanaonesha ukafiri; kama huba ya namna hii ni khilafu na dini; basi tunaweza kusema tu:

Upotevu wa namna hii, Mungu anijaalie mwingi mno!

Na kufuru hii anipe ya dunia nzima!

Na sasa, Mwenyezi Mungu, Kauli Yake, Mtume Wake s,a,w, na akili ya kiutu ni mashahidi ya kuwa mtu kama huyu hawezi kuwa mpotevu na mwongo. Kama mtu fulani anaweza kumpenda na kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake s.a.w. kwa kadiri hii, na kujitupa kabisa katika kazi ya kueneza kweli zilizofundishwa nao; kama anaweza kuonesha heshima zaidi kwa mambo haya kuliko mtu yeyote hai na mfu, na bado asemwe ni mwongo na Dajjal, basi ni lazima tuseme: hakujapata kuwako, na hakutakuwako kamwe, mtu wa kustahili kupata mwongozo wa Mwenyezi Mungu.

## HOJA YA KUMI NA MBILI:
## NGUVU YA KUHUISHA

Katika hoja yangu ya kumi na mbili ya ukweli wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ninataka kutaja nguvu zake za kuhuisha. Hoja hii pia, kama hoja zingine zilizopita, ina hoja elfu moja na moja. Leo Waislamu kama Wakristo wanaamini ya Kuwa Nabii Isa a.s. alikuwa na uwezo wa kufufua wafu. Itikadi hii, kama nilivyokwisha onesha, ni kinyume na mafundisho ya Quran Tukufu. Inaelekea kwenye *Shirk* au kumshirikisha Mwenyezi Mungu na vitu vingine.

Ni kuangamiza imani juu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu. Kwa maana nyingine, nabii Isa alihuisha wafu; na mwujiza huu manabii wote waliufanya katika zama zao. Kauli ya Mwenyezi Mungu inathibitisha jambo hili, na kukana jambo hili ni kuikana kauli ya Mwenyezi Mungu. Ni wa kiroho sio wa kimwili, wafu ambao manabii huwahuisha. Kwa kweli, kuhuisha wafu wa kiroho na kuponyesha magonjwa ya kiroho ndio sababu kubwa ya kufika kwa Manabii. Kwa hiyo, hakuna nabii aliyepata kuja ambaye hakuhuisha wafu kwa maana hii. Tokea Adam mpaka Mtume s.a.w. manabii wote walitumwa kwa makusudio haya. Mizani moja ambayo kwayo madai ya manabii wakubwa yanaweza kupimwa ni ama manabii hao wanaleta au la uhai kwa waliokufa kiroho. Kama mdai wa unabii hawezi kuonesha mwujiza huu, madai yake ni lazima yatiliwe shaka sana. Kama kwa upande mwingine, anaweza kuonesha nguvu zake za kuhuisha, ni lazima awe mtu wa Mwenyezi Mungu. Hakuna mtu anayeweza kuwa na nguvu za kuhuisha mpaka iwe kwa kazi na msaada wa Mwenyezi Mungu; na mtu anayepata sana msaada wa Mungu ni lazima awe mkweli.

## ZAMA ZA MAUTI YA KIROHO

Sasa, msomaji mpenzi, ishara kuhusu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ni ya dhahiri sana hivi kwamba kifano chake hakiwezi kupatikana katika nabii mwingine yeyote isipokuwa, na hasa, Nabii Mtukufu wa Islam s.a.w. Mwenyezi Mungu anajua vyema zaidi; lakini Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s alifika katika wakati ambao mauti ya kiroho yalikuwa yameufikia ulimwengu mzima. Sio kifo tu bali pia kufarakana na ubovu ulikuwa umeingia. Ni cha huzuni, ni cha hakika kabisa kifo hiki hivi kwamba tunaona manabii wote wa zamani wakituonya juu yake. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema:

"Kila Nabii baada ya Nuhu aliwaonya watu wake juu ya hatari ya Dajjal. Mimi pia ninawaonya juu yake" (Tirmidh, Abwabul Fitan).

Kifo na maangamizi katika zama hizi kilikuwa kienezwe na Dajjal. wanadamu wasingeweza kuwa wafu zaidi kuliko walivyo leo. Kuwahuisha, ilikuwa ni kazi ya taabu sana. Bado, kazi hii imefanywa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Amewahuisha mamia ya maelfu nyingi ya wanadamu waliokuwa wafu wa kiroho. Ameumba ufuasi usio kifano miongoni mwa manabii wengine isipokuwa Mtukufu Mtume wa Islam s.a.w. Musa alikuwa kiongozi wa siasa na dini pia. Walimkubali na kumfuata kwa sababu ya fikara za kisiasa, na wengine kwa sababu ya nia ya kiroho pia. Juu ya jambo hili tunao ushaidi wa Quran Tukufu:

"Lakini hawakumwamini Musa isipokuwa baadhi ya wazao wa kaumu yake" (10:84).

Hii ndiyo ilikuwa hali ya Misri. Baada ya Musa kuitoka Misri, wengi wa watu wake walikuwa hawajaungana naye moyoni. Kisiasa ndio walikuwa pamoja naye. Kwa ajili ya hili pia, tunao ushahidi wa Quran Tukufu. Wakati fulani baada ya kutoka Misri kikundi cha watu kilimwabia Musa:

"Ewe Musa, hatutakuamini kamwe mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi! Ndipo ikawashikeni ngurumo na hali mnaona!" (2:56).

Katika Quran Tukufu na Agano Jipya na katika taarikh inadhihirika ya kuwa watu wachache sana walimwamini Nabii Isa a.s. Kati ya idadi hii ndogo, wale waliokuwa na shauku na wakapata uhai hasa wa kiroho, walikuwa wachache zaidi. Lakini Hadhrat Ahmad a.s. alikuwa na wanafunzi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Alifika dunaini kuonesha rehema za kiroho za bwana wake na kueneza baraka za mvuto wa bwana wake na mfano wake. Alikuwa Masihi wa duara la Muhammad, sio wa duara la Musa. Kwa njia ya Hadhrat Ahmad a.s. Mwenyezi Mungu amehuisha wengi waliokufa kiroho, na wafu aliowahuisha walikuwa wafu sana hivi kwamba isipokuwa kwa maji ya uhai yaliyochukuliwa toka kwenye chemchem ya

Muhmmad, hakukuwa na matumaini ya kupatikana uhai ndani yao tena.

## TASWIRA YA NGUVU YA UTUME

Inastaajabisha, ni makubwa vilioje mabadiliko ya kiroho yaliyoletwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Aliona nini alipokuja? Utungo wa kibinadamu na mawazo yakigeuzwa kuwa dini ya Mungu; mapenzi ya haja za dunia na kuchukia kabisa maisha ya kiroho, chuki ya njia za kiungu, ya elimu ya ufunuo na sheria ya ufunuo; kutojali sifa ya tabia njema; kuacha Sala tano na utovu wa adabu kwa walimu wa dini. Hivi ndivyo alivyoona. Na alipata nini? Ufuasi wa watu walioelimika kama yeyote yule, ambao walimwamini Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w., Malaika, dua, miujiza, ufunuo, Akhera, Kiyama, Pepo na Jahannam: Ufuasi unaotekeleza wajibu za dini zilizolazimishwa na Dini ya Islam. Wachache sana miongoni mwa wafuasi wake wanaoweza kuonekana hawasali Sala tano na kutekeleza wajibu mwingine. Hata hao wanaoweza kuwa namna hiyo inawezekana kuwa ni sababu ya udhaifu wao wa tangu siku za mwanzo na unaweza kutoweka baada ya muda. Inajulikana sana kwamba vijana walioelimika katika vyuo vikuu na wale waliojipatia hati zozote za elimu za kisasa, wana chuki kubwa ya dini. Kama wanathamini dini ni kwa sababu ya manufaa yake ya kisiasa. Lakini Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ameumba ufuasi wa walioelimika kisasa, ufuasi unaoongezeka kwa imara, wenye watu ambao kwa wakati huo huo wanajitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na dini Yake. Machozi huwatiririka wanaposujudu katika Sala. Vifua vyao huchemka wanapomwomba Mola wao. Wanatanguliza kazi ya islam na kuueneza juu ya manufaa yao ya kidunia. Wanatoa sadaka wakati wao, mali, na fursa zingine kwa ajili ya Uislamu. Wanakerwa na shida iliyoingia Dini ya Mwenyezi Mungu leo. Wamevutwa na haja ya taratibu ya kufasiri Uislamu, Jihad ya akili, Jihad ya hoja. Wengi miongoni mwao wangeweza kupata ufaulu mkubwa katika kazi za kidunia, lakini wameacha kazi zao kwa sababu ya dini. Wanapendelea umaskini

na njaa. Midomoni mwao mna majina mawili tu: Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume s.a.w.; mioyoni mwao mmejaa mapenzi ya wote wawili. Vitendo vyao vinamtukuza Mwenyezi Mungu na Mtume s.a.w. na nyuso zao zimefunikwa na roho ya mapenzi. Wanakaa katika ulimwengu huu huu kama watu wengine. Wanajua mvuto wa maisha. wanajipenda nafsi zao. Wao pia wangependa maisha yao wenyewe. Wao pia wanasoma na kusikia yale ambayo watu wengine wanayasoma na kusikia. Lakini wamekata shauri kujiweka chini ya mafunzo na mwongozo kwa ajili ya Uislamu. Uislamu, wanaona, unahitaji taratibu zaidi kuliko uhuru. Madhara yaliyoletwa na Dajjal leo, yamefanywa kwa njia ya propaganda ya kiulimwengu mzima. Jihadi kwa ajili ya Uislamu leo, inahitaji taratibu ya namna ileile. Inahitaji Waislamu waje pamoja chini ya bendera moja. Inawahitaji wakubwa wao na wadogo wao, matajiri wao na maskini wao, waalimu wao na maamuma wao, wote wasogeze bidii zao na kujiweka katika taratibu moja chini ya kiongozi mmoja. Kujitenga na kutosikilizana kwa Waislamu kunarudisha nyuma Uislamu na kunawasaidia maadui zake. Ili kukuza taratibu yenye mwungano na yenye jihad kwa ajili ya Uislamu, wafuasi wa Hadhrat Ahmad a.s. wameamua kutanguliza haja za Islam juu ya haja zao za kidunia, Wito wa Mwenyezi Mungu juu ya shughuli zao wenyewe. Wamejitoa katika mivuto yote ya kisasa na kuingia katika utii wa hiyari kwa Imam wao. Ni juu ya Imam kutaja ni wapi na lini wanatakiwa kwenda kuutumikia Uislamu. Ni juu yao kutii, na tena kutii bila kusita, bila kunung'unika. Hakuna sadaka yoyote iliyo nzito sana kwao, wala shida iliyo kubwa kwa ajili yao. Wanafanya yale wanayoamini. Hivi sasa wengi wao wanaweza kuonwa nje ya majumbani kwao na ahali zao wakifanya kazi sio kwa ajili ya maslahi yao bali kwa ajili ya Uislamu. Licha ya upungufu wa mali na afya njema, chini ya amri ya kiongozi wao, Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa, wengi wao wako tayari kwenye medani, wengi wakingojea zamu yao. Hawajali sana maisha yao ya kidunia. Wameacha nyumba zao na ndugu zao kwa ajili ya Utukufu wa Mwenyezi Mungu. "Hivi baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanangojea" (33:24).

Wanaogofywa na kupigwa. Pengine wanatolewa majumbani

mwao. Kwa kudumu wanatukanwa na kudhihakiwa. Lakini wanavumilia yote haya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mboni zao za kiroho zimesafishwa. Wameona yale ambayo watu wengine hawaoni na hawawezi kuona. Wao wanapigwa, na wanawatakia heri wengine. Ingawa wanafedheheshwa, lakini wanawaombea heshima.

Kama kuna mtu yeyote ambaye hana mali wala njia ya maisha, ambaye anaweza kuonwa akifanya kazi kwa ajili ya uislamu, tuseme katika Amerika, basi ni mfuasi wa Hadhrat Ahmad. Anaweza kuwa kama tone katika bahari, lakini havunjiki moyo wala haogopi hatima. Alikuwa mtu mfu ambaye amehuishwa kwa mkono wa Masihi. Yu peke yake lakini anaweza kuthubutu kuliita Bara zima la Amerika likasome, likachungue na kuukubali Uislamu. Anaweza kufanya hivi kwa sababu anajua ya kuwa mtu mmoja aliye hai ni bora kuliko mamilioni waliokufa,.

Kama kuna watu wowote huko Ulaya ambao wanajaribu kutangaza Uislamu miongoni mwa Waingereza, tena ni lazima wawe wale wale wafu waliohuishwa na Masihi wa Muhammad. Kwa nguvu ya kidunia, Ulaya iliweza kuishinda Bara Hindi, lakini wafuasi wa Masihi wanajua kuwa kiroho, Ulaya imekufa na imepotea mbali na Mwenyezi Mungu. Wamepeleka maji huko Ulaya ya uhai ambayo walipewa na Masihi na ambayo yatawapa uhai sasa wafu wa nchi zingine. Nguvu na utajiri wa Ulaya hauwatishi wao kwani wanajua ya kuwa wao wako hai na Ulaya imekufa. Walio hai hawawaogopi wafu kwa chochote.

Sasa, tazama upande wa Pwani ya Afrika ya Magharibi. Wahubiri wa Kikristo walifika sehemu hii ya dunia zamani sana na walianza kufanya kazi kwa ajili ya Ukristo. Waafrika milioni nyingi wa Afrika ya Magharibi wakaingia Ukristo. Wakaanza kumwabudu mtu kama Mungu. Je, kulikuwa na yeyote aliyepata kwenda sehemu hii kuwaambia juu ya Mungu Mmoja? Je, kuna yeyote aliyekwenda kupambana na itikadi za kimawazo na kipagani na matendo ya watu hawa? Ndio, wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa, waliohuishwa kwa pumzi yake, walikwenda huko kueleza Uislamu zama ambazo Uislamu uliachiliwa mbali kama kitu kilichokufa, zama ambazo mwanguko wake ulikuwa wazi.

Je, kuna yeyote aliyekifikiria kisiwa cha Mrisi, kisiwa kilichosahauliwa? Au ni nani aliyewazindua wenyeji wa Ceylon ambako taarikh ndefu ilifanywa? Au ni nani aliyefika Urusi na Afghanistan? Ndio watu waliohuishwa na Masihi Aliyeahidiwa!

## ALAMA ZA UHAI

Nani anayeweza kuzikosea alama hizi za uhai? Miongoni mwa milioni mia nne au mia tano za Waislamu, hata mmoja wao hakuacha nyumba yake kwa nia ya kuwaambia wengine juu ya Uislamu, kuwabashiria ujumbe wa Mtukufu Mtume s.a.w. lakini mamia ya Waahmadiyya wanaweza kutajwa ambao wameondoka majumbani kwao na kuenda kuishi na kufanya kazi katika nchi zingine. idadi ya Waahmadiyya katika dunia nzima haiwezi kuwa kubwa sana. Hata hivyo wanawafanya kuwa Waislamu, watu ambao wangechukia hata kusikia juu ya Uislamu. Kama wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa hawana uhai, waliwezaje kuibadilisha ramani ya ulimwengu? Walithubutuje kupambana na bara mbalimbali na nchi mbalimbali? Walipata wapi moyo huu, na imani hii? Ni kipi kilichowashawishi kuacha nchi zao wenyewe na kwenda nchi ngeni, na kwa ajili gani? Wana jamaa zao na wapenzi wao, wana ndugu zao, ahali zao na rafiki zao. Wana maslahi yao na kazi zao. Ni kipi kinachowaongoza kuiacha dunia na kuelekea dini? Ni zawadi ya uhai waliopokea kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa. Wanaweza kuona tofauti baina ya mzima na mfu. Si taabu kwao kumwacha mfu na kumwelekea Mwenyezi Mungu, Chanzo cha uzima wote. Ameingia ndani yao, na wameingia ndani Yake. Mwenye Mibaraka ni Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbao.

Nguvu za kuhuisha za Masihi Aliyeahidiwa zimerithiwa na wafuasi wake. Uzima unaumba uzima zaidi. Huu hapa ni ushahidi wake mzuri sana. Hadhrat Ahmad hakutoa uhai tu kwa wafuasi wake. Amewapa pia nguvu ya kutoa uhai, nguvu ya kufufua wafu. Laitani Hadhrat Ahmad asingefanya hivi, nguvu yake mwenyewe ya kuhuisha kwa rehema ya Mwenyezi Mungu ingebaki katika shaka. Hapo ingesemwa kwamba nguvu zake, elimu yake maalum, maonyo

yake, na dua zake zilikuwa majaala ya kiasili, sifa maalumu za ubongo. Hazikuwa ushahidi wa rehema za Mwenyezi Mungu. Lakini shaka za namna hii haziwezi kushika. nguvu za kuhuisha ambazo Masihi Aliyeahidiwa alizionesha hazikubakia kwake tu, hazikuondoka pamoja naye. Zimerithiwa na wafuasi wake wa kweli. Kwa kadiri mbalimbali, wameonesha nguvu zilezile. Sawa na kujitolea kwao kwa ajili yake na daraja za maungano yao ya kiroho, wao pia wananyeshewa mvua ya elimu. Wengi wao wanaweza kufafanua uzuri wa Quran Tukufu na mbio yao katika jambo hili inashinda mbio za farasi aendaye kasi. Ufasaha wao ni wa ajabu. Hotuba zao zina athari na ni za kuvutia wanapoanza kusema juu ya jambo. Ni tatuzi la mashaka na shida. Quran Tukufu ambayo kwa wengine ilifungwa, kwetu sisi i wazi sana. Hakuna dini wala falsafa wala fikara inayochagua kuushambulia Uislamu, inaweza kutuogofya sisi. Tunaweza kushuhgulika nayo kwa msaada wa Quran Tukufu. Hakujapata kuzuka taabu yoyote au hoja juu ya aya hata moja ya Quran Tukufu, ambayo hatukufunuliwa jawabu lake kwa rehema maalumu ya Mwenyezi Mungu. Matunda ya kiroho, yaani kupata ufunuo wa Mwenyezi Mungu, kuona njozi za kweli pia yametoka kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. na kwenda kwa wafuasi wake, ambao kwa namna fulani wamezaliwa mara ya pili, kwa mfano wake na mvuto wake na wamepokea zawadi za mvuto wake na wamepokea zawadi za aliyoyapata kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wanapokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na njozi za kweli. Kutimia kwao kunaongeza imani na uhakika wa yakini kwao wao na kwa rafiki zao. Mungu aliye hai anazungumza nao na kuwafichulia Makusudio Yake. Wanagundua njia zinazoongoza kwenye radhi Yake. Wanazishika njia hizi na hili linawapa moyo na kuwapa nguvu katika akili na roho zao.

## MATUNDA YA KIROHO YANAPATIKANA

Kukubaliwa maombi na zawadi ya msaada wa mbingu pia zinaendelea; ahsante sana kwa mvuto wa ukarimu wa Hadhrat Mirza

Ghulam Ahmad a.s. Wale waliopata uhai kutoka kwake wanahisi ishara ya uhai wenyewe ndani yao. Dua zao zinakubaliwa zaidi kuliko dua za watu wengine. Wanapata msaada wa Mwenyezi Mungu zaidi kuliko wengine. Maadui zao wanafedheheka na kushindwa. Juhudi zao na sadaka zinalipwa mara nyingi. Hawaachwi peke yao. Mungu yuko pamoja nao na anaonesha ghera yake kwa ajili yao.

Kwa kifupi, Hadhrat Ahmad sio tu kwamba amehuisha wafu. Bali aliinua wafuasi ambao wanaweza kufanya kadhalika. Nguvu hii na mvuto huu ni haki maalumu ya manabii watukufu wateule na wapenzi wa Mungu. Zawadi maalum hii, anaiwia kwa bwana wake Mtukufu Mtume s.a.w. Masihi Aliyeahidiwa anaendeleza kazi ya Mtukufu Mtume s.a.w. Zawadi zake ni zawadi alizopokea kutoka kwa Bwana wake. Ufunuo mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa unasema:

"Kila baraka inatoka kwa Muhammad, amnai ya Mungu na rehema juu yake. Basi amebarikiwa aliyefundisha na aliyefundishwa."

## WITO
## MASIHI AMEKWISHA KUJA

Hoja kumi na mbili nilizoeleza zinatosha kuthibitisha ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Mtu yeyote aliye tayari kuzifikiri kwa makini kwa nia ya kutafuta ukweli, hataona ukweli tu bali atafikia yakini pia. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ndiye Masihi Aliyeahidiwa na ametumwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wakati wetu; ni Mjumbe Wake. Haina maana kumngojea mwingine. Anayefikia yakini hii hatasita kutangaza imani yake, kama vile mwenye kiu kukimbilia kwenye chemchemu. Hatataakhari hata kidogo, bali mara moja atajiunga na Jumuiya ya Masihi. Ataona ndio wokovu wake.

## USHUHUDA WA MUNGU NA MTUME

Ni nani anayeweza kumyakinishia Mwislamu zaidi kuliko Mungu na Mtume Wake s.a.w. Kwa ajili ya Hadhrat Ahmad a.s., tunao ushahidi wa Mungu na Mtume Wake s.a.w.; na zaidi ushahidi wa manabii wengine ambao vyuo vyao vinapatikana mpaka sasa. Uamuzi wetu wenyewe unaashiria kuwa wakati huu ndio wakati wa kufika Mujaddid. Alama alizoeleza Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa alama za kufika Masihi na Mahdi zimedhihirika. Utakatifu wa maisha yake unatangaza ukweli wa madai yake. Maadui za Islam ambao Masihi Aliyeahidiwa angewashinda wamepatikana na wamesimama washindwa mpaka hii leo. Hatari zilizowaingia Waislamu zimeruka mipaka yake. Pamoja na kuwako Quran Tukufu, hatari hizi zisingekuwa mbaya sana kadiri zilivyo. Masihi Aliyeahidiwa ameeleza itikadi za Islam kwa mara nyingine na kuondoa zile hatari zilizoupanda Uislamu. Kwa maisha yake yote alifaidi msaada wa Mwenyezi Mungu na mapenzi Yake, kama ambavyo kila siku manabii na wapendwa wa Mungu walivyokuwa wakifaidi. Alipewa ushindi katika kila uwanja. Alihifadhiwa katika kila shari na mashambulio. Maadui zake walifedheheka na kufa; kama walivyofedheheka maadui za manabii wa Mungu hapo kabla. Njia za kiasili zilifanya kazi kumtumikia na mbingu na ardhi zilitembea kumpendelea. Alifunguliwa milango ya elimu maalum ya Quran Tukufu; njia maalumu ya kuifafanua na kuieneza. Aliwaita watu wote, pamoja na wataalamu, ili waje kujaribu madai yake kwa zawadi za elimu za kimwujiza, lakini hakuna aliyethubutu. Kazi zake za kimwujiza za Kiarabu na elimu yake maalumu ya maana ya Quran Tukufu ilibakia bila wa kuitambia. Na kwa nini? Si ameahidi Mwenyezi Mungu Mwenyewe kwamba "Hakuna atakayeigusa ila waliotakaswa?" (56:80). Alijaaliwa vilevile elimu ya ghaibu. Maelfu kadha ya mifano ya elimu hii alionesha kwa msaada maalumu wa Mwenyezi Mungu. Bishara zake zilitimia na zilionesha waziwazi utukufu na jalali ya Mwenyezi Mungu. Hii ilifuatana na kanuni ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Kwani, wingi wa elimu kama hizi Mungu huwajaalia Wajumbe Wake tu. Maisha yake yote alikuwa aliyejitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake

Mtakatifu, na watumishi kama hawa hawafukuzwi katika Baraza la Mwenyezi Mungu. Nyuma yake ameacha wafuasi walio wema na imara katika maneno na matendo. Wengi wao wana maungano maalumu na Mwenyezi Mungu. Wanaweza kuhuisha wafu wa kiroho na kutatua migogoro ya kiroho. Wamejitolea kwa ajili ya dini na kuacha maslahi ya dunaia na maungano ya kidunia. Wanajitahidi kwa ajili ua utukufu na ushindi wa Uislamu na hawajali kitu kingine chochote. Kweli hizi zinashuhudia ukweli wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Hivyo kukataa kumwamini, hakuwezi kuwa ni sawasawa wala hakuwezi kuwa ni kumpendeza Mwenyezi Mungu. Waislamu wanaopenda Uislamu na Mtukufu Mtume s.a.w. walio tayari kutanguliza maslahi ya Islam juu ya maslahi yao, hawatasita kuukubali ukweli baada ya kuwadhihirikia. Kama hoja nilizozieleza zinashindwa kuthibitisha ukweli wa madai yake, basi swali ni hili, "Kulikuwa na hoja gani kuthibitisha ukweli wa manabii wazamani? Ni dalili gani zilizoleta imani katika ukweli wao?" Hoja za kusaidia madai ya Hadhrat Ahmad ni nyingi mno na za wazi zaidi kuliko hoja zilizosaidia madai ya manabii wa zamani, isipokuwa, kwa kweli, Mtume s.a.w. Basi kwa nini waaminiwe manabii wa zamani lakini asikubaliwe Masihi Aliyeahidiwa? Imani ya kweli siyo imani ya kurithi kutoka kwa wazazi au inayokubaliwa kama mila. Imani ya kweli inakuja baada ya kufikiri na dhamiri. Kama hii iwe siyo imani ya kweli, basi tukatae ukweli wa manabii wa zamani. Kama hatuwezi kukana ukweli wa manabii wa zamani, ni lazima tukubali ukweli wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mtu mwenye akili atashika njia hii. Atamkubali Masihi Aliyeahidiwa kuliko kuwakataa manabii wa zamani Hatasita kumkubali yule aliyakuja kutangaza ukweli wa Mtukufu Mtume wa Islam; aliyekuja kuuongoza Uislamu tena ili upate ushindi na kuwafanya Waislamu kuwa Waislamu safi na imara zaidi. Kukubali Nia ya Mwenyezi Mungu na kushiriki katika mpango Wake ni njia ya kujipatia baraka Zake. Kukataa mpango Wake na Nia Yake hakuleti baraka yoyote.

Hali ya Uislamu leo inaumua huruma yetu. hakuna mtu anayeupenda Uislamu anaweza kuutazama kwa utulivu. Kila anayeupenda Uislamu atafanya chini juu kuulinda Uislamu katika

hatari zinazoonekana za kutisha kuwako kwake. Atatamani auone ukiishi na kushinda mara nyingine. Maadui za Uislamu wamekuwa wagumu kweli, wanaweza kuona ndani yake ubaya tu lakini hawaoni uzuri wowote. Pengine wanaichukia, na pengine hawaishughulikii. Wanatamka tu utii kwa ajili yake. Lakini tamko lao halivuki midomo yao. Naam, wanajali ufaulu wa kisiasa wa Kiislamu. Kama nchi ya Kiislamu ipoteze uhuru wake, wanagongwa na wanaanzisha kitali. Lakini kama mamia ya maelfu ya Waislamu wanauacha Uislamu na kuwa Wakristo au Wahindu, hawashtuki hata kidogo. Wanao wengi wajitoleao kwa ajili ya mipango ya kisiasa, lakini hata mmoja hatoki nje kwa ajili ya kueleza na kueneza Uislamu. Kukataliwa kwa Sultani wa Kituruki kuwa Khalifa kunawaghadhibisha. Lakini sio kukataliwa kwa Mtume s.a.w. Hali hii sasa inaendela. Waislamu wa India ndio wameghafilika kabisa. Hawajali kazi ya kubashiri Uislamu. Hawataki hata kurejesha mashambulio yanayotolewa na maadui kushambuali Uislamu. Kufanya hivi wanaona sio adabu. Hawana kazi na Uislamu kabisa. Kuna njia moja tu ya kuuondoa Uislamu katika hali mbaya. Nayo ni kumkubali Masihi Aliyeahidiwa na kuingia katika Jumuiya yake. Uislamu hauwezi kuendelea sasa isipokuwa kwa uongozi wake. Jihadi ya upanga haiwezi kuusiadia Uislamu. Kinachotakiwa ni imani ya kweli juu ya Uislamu, fahamu ya kweli ya mafundisho yake, na umoja wenye nguvu. Bila ya hii Uislamu hauwezi kuinuka tena. Maadui za Uislamu wanasema ya kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. alitumia upanga kwa ajili ya kuueneza Uislamu. Isipokuwa kwa upanga, wanasema, uislamu usingeenea. Wanasema Uislamu haukuwa na hoja yoyote kuusaidia. Kwa kujua na kutojua, Waislamu wenyewe wamekubali shambulio hili. Mwenyezi Mungu leo ameamua kwamba shambulio hili kwa Mtume Wake Mpendwa, lifutwe na kuthibitisha kuwa ni la uongo. Hivyo amemtuma mmoja wa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. awashinde maadui za Uislamu na auongoze kwenye ushindi mara nyingine, sio kwa vita bali kwa hoja na dalili. Ni kwa hivi tu ndio dunia itajua kuwa kile ambacho mtumishi anaweza kupata, bwana aliweza kupata zaidi mno. Kwa ajili ya Waislamu leo, hii ndiyo njia peke yake. Mwenyezi Mungu anataka hata maadui za Mtukufu Mtume s.a.w. wajiunge naye na wawe wafuasi wake na watumishi. Ili kufanya

hili liwezekane, kuna njia moja tu. Nayo ni kueleza Uislamu wa kweli ulimwenguni, Uislamu ulivyoelezwa upya na Masihi Aliyeahidiwa, kwa njia alizofundisha na kwa imani aliyoumba. Hii ndiyo njia ya kuwarudisha wanadamu waliopotea, kwenye njia ya kweli. Kama Mwenyezi Mungu anajua njia zingine ambazo kwazo Uislamu ungeweza kufaidiwa, kwa nini hakutufungulia njia hizo? Kubakia nje ya Masihi Aliyeahidiwa ni kurudisha nyuma maendeleo ya Uislamu, na kuwapa kichwa maadui zake. Kuacha kuungana na Masihi Aliyeahidiwa ni kuwapa kichwa maadui za Uislamu, kutia nguvu mashambulio yao juu ya Mtukufu Mtume s.a.w., mafundisho yake, mfano wake na heshima yake. Mwislamu gani mwenye ari juu ya dini yake anaweza kuvumilia haya? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema:

"Unawezaje kuangamia umati ambao una mimi mwanzoni mwake na Masihi bin Mariamu mwishoni mwake" (Kitabu *Ibn Majah,* Babul I'tisam Bis Sunnah).

Katika haya inaonekana ya kuwa imani inahitaji ngome mbili ili kuisalimisha. Anayemkataa Masihi Aliyeahidiwa a.s. anakuwa nje ya usalama. Anayemzuia masihi Aliyeahidiwa ni adui wa Uislamu. Hafurahii maendeleo ya Islam. kama hivi sivyo, kwa nini apinge kuinuliwa kwa ukuta unaodhamini usalama wa Uislamu? Uadui wake unaita ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Ingalikuwa ni bora laiti asingezaliwa na kubakia vumbi tu. Laiti asingaliiona hii siku yenye nuksi!

## AHADI KUBWA KUBWA

Ahadi zote kubwa kubwa zilizofanywa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya wakati huu, zinafungamana na kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa. Uislamu ulikuwa upate muda mpya wa uhai kwa njia yake. Mti unaoanza kufa kwa kukauka, huwa hai tena kama mvua ikinyesha kwa wakati mzuri. Hivi ndivyo mti uliokauka na

kufa wa Uislamu una hakika ya kuchipusha tena kwa kufika Masihi Aliyeahidiwa. Wale wanaojiunga na Masihi Aliyeahidiwa watajaaliwa nguvu mpya na roho mpya. Kwa muda mrefu Mwenyezi Mungu amevumilia yale aliyoyaona. Amekuwa kimya muda mrefu, lakini sasa hatakuwa hivyo tena. Hataruhusu tena kwamba mtu tu, kiumbe Wake, afanywe mshirika Wake; ya kwamba wale wanaomfanya Yesu kuwa mwana wa Mungu au kuamini kuwa yuko hai mbinguni, au kwamba aliweza kufufua wafu wa kimwili, au kwamba aliweza kuumba, waendelee kufanya hivyo. Naam, Mwenyezi Mungu ni mwenye huruma, lakini pia ni mwivu katika Upekee Wake na Umoja Wake. Alingoja ya kwamba watu waelekee Kitabu Chake Kitukufu, lakini walikiacha tu. Wakapenda vitu vingine vya kipuuzi na kujali kidogo tu Kitabu Kitukufu. Wakasahau onyo lililomo ndani ya Kitabu Kitukufu:

"Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Quran hii kuwa kitu kilichoachwa" (25:31).

Waliacha Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kuelekea vitu vingine. Ndiyo sababu, Mwenyezi Mungu akawaacha kabisa. hatawaelekea sasa mpaka waweke mkono wao katika mkono wa Masihi Aliyeahidiwa, waache kutojali kwao na kutofuata Kitabu Kitukufu, na wasahihishe udhaifu wao wa zamani na makosa yao. Waliipenda dunia lakini hawakumpenda Mwenyezi Mungu. Ndipo Mwenyezi Mungu akaondoa kwao dunia na kuwafedhehesha. Walidai kuwa Waislamu, na bado wakamzika ardhini Mpendwa wa Mwenyezi Mungu wa mwisho, lakini wakampandisha Masihi wa Nazareti mzima mzima mbinguni. Mwenyezi Mungu pia akawafanya wao wawe chini katika ardhi na kuwafanya Wakristo wawatawale. Hali yao sasa haitabadilika mpaka wakubali kujisahihisha. Mipango ya kisiasa inaweza kufaa kidogo tu. Udhalilifu wa Waislamu ni matokeo ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Mpaka Waislamu wapatane na Mwenyezi Mungu, watakuwa chini tu. Basi mwenye kubarikiwa ni yule anayeharakia kupatana na Mwenyezi Mungu. Ataokolewa katika fedheha na mkosi. Msaada wa Mwenyezi Mungu

utakuwa pamoja naye na Mkono wa Mwenyezi Mungu utamtoa katika taabu.

## KUJA KWA MASIHI NI TUKIO KUBWA

Kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa sio tukio la kawaida. Ni tukio kubwa sana. Je, Mtume s.a.w. hakuwaonya wafuasi wake na kusema: Hawana budi waende kujiunga na Masihi Aliyeahidiwa hata kama kwa shida kubwa? Bishara kumhusu Masihi Aliyeahidiwa zimepatikana katika dini zote. Hakuna nabii ila alitabiri kufika kwa Masihi Aliyeahidiwa. Mtu anayejibu bishara za manabii wengi namna hii ni lazima awe mtu mkubwa sana; ambaye kuja kwake manabii wote waliwataka watu wao wakungojee. Wenye kubarikiwa ni wale wanaomshuhudia Masihi Aliyeahidiwa au wakati wake na kupokea matunda yaliyoahidiwa katika mikono yake. Manabii hawafiki mara kwa mara, hususan manabii wakubwa kama Masihi Aliyeahidiwa. Mtukufu Mtume s.a.w. alisisitiza kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa zaidi kuliko kuja kwa mwingine yeyote. Hakuna mtu mkuu zaidi atakayeinuka kati ya Waislamu. Yeye ni Muhuri wa Makhalifa (Khatamul Khulafaa) ambaye alitajwa kuwa atatokea miongoni mwa wafuasi wa Mtukufu Mtume s.a.w. Baada yake tunangojea tu Siku ya Kiyama. Kwa hiyo kila siku, katika wakati wetu huu, ni ya thamani sana, la, bali ya thamani zaidi kuliko chochote chenye thamani sana cha dunia hii. Mwenye bahati njema ni yule anayejua thamani ya wakati uliopo na kuamua kujiunga na Masihi Aliyeahidiwa, na kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu. Mtu kama huyo ataiona shabaha ya maisha yake, na kuiteka ile siri ya kuwa mwanadamu hasa.

## HALI YA BAADAYE YA UAHMADIYYA

Anapofika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kuinua Jumuiya wa kwanza kujiunga naye huwa watu maskini. Lakini Jumuiya haibaki maskini wakati wote. huanza kupata ufaulu na hatimaye

hata wafalme wanajiunga nayo. Inasimamisha mzizi wake katikati, halafu inatawala sehemu zile alizopelekwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo mtu asifikiri kuwa Jumuiya yetu ni maskini na itabakia maskini. Itakuwa kwa kila hali. Hebu nchi zenye nguvu sana zijiunge pamoja na kujaribu kusimamisha kukua kwake. Nasema, hazitafaulu kamwe. Siku itafika ambapo Jumuiya hii itayashinda makundi yote na jamii zote katika mashindano. Funuo za Hadhrat Mirza Gulam Ahmad a.s. zilimwahidi kwamba "Wafuasi wako watakuwa washindi juu ya maadui zao mpaka Siku ya Kiyama": na pia kwamba: "Idadi ya wale wasiojiunga na Jumuiya yako itaendelea kupungua; na mpaka wafalme watajiunga na Jumuiya hii."

Hivyo Jumuiya ya Ahmadiyya haitabakia ndogo na ya kupuuzwa kama inavyoonekana leo, bali itazidi idadi yake na mvuto wake na kuanza kuwashinda wote. Haitabakia dhaifu bali itakuja kuwa yenye nguvu sana na iliyoshinda. Ufunuo mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa unasema:

"Wafalme watatafuta baraka katika nguo zako."

Thamani ya matukio makubwa au kazi njema inategemea wakati wake vilevile. jambo linafanywa wakati fulani na linakuja kuwa la maana sana. Kwa wakati mwingine jambo hilohilo linakuwa halina maana sana. Wale waliokuwa wa kwanza kumwamini Mtukufu Mtume s.a.w. mpaka leo wanabakia kuwa viongozi wa dunia. Lakini wale waliomwamini zama ambazo Uislamu ulikuwa umepata nguvu duniani hawakufikia heshima hii. Kwa hiyo wale wanaojiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya sasa, ambapo inafikiriwa kuwa dhaifu, watafikia ile heshima ya waaminio wa kwanza. Watarithi zawadi na baraka maalumu. Wakati mrefu umekwisha pita, lakini mlango wa kupatia heshima bado uko wazi; kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu bado ni rahisi. Ninakuita, msomaji mpenzi, ufikirie thamani ya nafasi yako hii. Ni juu yako kusema walivyosema waaminio wa kwanza:

"Mola wetu, hakika tumesikia Mwitaji anayeita kwenye imani ya kwamba Mwaminini Mola wenu. Kwa hiyo tumeamini" (3:194).

Ni juu yako kusema 'Labeika' kwa yule anayelia katika jina la Mwenyezi Mungu. Inakupasa uwe mpendwa wa Mwenyezi Mungu.

Ninasema kwelikweli ya kuwa hapana yeyote awezaye kumwona Mwenyezi Mungu nje ya Jumuiya ya Ahmadiyya. Laiti kila mtu aliye nje ya Jumuiya hii, angejichungua moyoni mwake, angekubali ya kuwa hana ile yakini ya imani juu ya Mwenyezi Mungu na ahadi Zake ambayo mtu anatakiwa awe nayo. Kadhalika angeshindwa kuona moyoni mwake ile nuru ambayo kwayo angeuona Uso wa Mwenyezi Mungu. Yakini hii, nuru hii, hutaiona nje ya Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa. Mpango wa Mwenyezi Mungu ni kuwaunganisha tena wanadamu. Anayejua kwa yakini ya kuwa mauti ni ya hakika, hawezi kukubali maisha yaliyo mbali na Mwenyezi Mungu, maisha yasiyopata Nuru Yake. Basi harakia upesi upesi kwenye Nuru na yakini ambayo utaiona leo katika Jumuiya ya Ahmadiyya peke yake; na ambayo bila ya hiyo maisha hayawezi kuwa na mvuto wala uzuri wowote. Waongoze wengine kwa tangazo lako ili ukumbukwe kwa heshima, ili waaminio watakaokuja baada yako wakuombee mpaka mwisho wa dunia.

## SADAKA SIO MZIGO

Naam, wale wanaojiunga na Jumuiya ya Kimbinguni inawabidi wabebe mizigo mizito ya sadaka na madaraka lakini kila mzigo sio mzigo. Je, mkulima anayebeba mgongoni mwake mzigo wa mazao yake ya kazi ngumu, anaufikiria mzigo? Au mama anayemchukua mwanawe mikononi, je, anafikiri kuwa mwanawe ni mzigo? Kwa hiyo kuitumikia na kuitolea sadaka Jumuiya ya mbingu sio mzigo kwa waaminio. Wengine wanaweza kufikiri ni mzigo, lakini kwa waminio ni jambo la furaha na matumaini. Hivyo usiogope madaraka ambayo utayaingia kwa kukubali ukweli. Bali fikiri kuwa una deni la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake ambazo

wanadamu wamepokea kutoka kwa Muhammad, Mtume wa Mungu s.a.w. Usisite basi kuinamisha bega lako ili ubebe mzigo ambao ni wajibu wa kila Mwislamu kuubeba. Unaweza kuwa mtu mkubwa au mdogo, kiongozi au mtu wa kawaida. lakini mbele ya Mwenyezi Mungu ninyi nyote ni sawa. Kuutumikia Uislamu ni wajibu wako na wao pia. Kuwaamini Mitume wa Mwenyezi Mungu ni wajibu wako na wao pia. Basi hebu pokea amri ya Mwenyezi Mungu na mpango Wake wa kazi na thawabu. Ingia katika Jumuiya ya Mbingu na uchume thawabu zilizowekwa kwa ajili ya waiingiao. Malipo yaliyo duni sana yatokayo kwa Mwenyezi Mungu ni afadhali na yana thamani zaidi kuliko ufalme.

Mtukufu Mtume s.a.w. alisema:

Anayejitenga na Jumuiya (ya mbingu) walau kwa shubiri moja si wa kwetu."

Basi kukaa nje ya Jumuiya iliyoinuliwa na Mwenyezi Mungu ni jambo zito sana, hususa huwa zito mara mbili kwa wale ambao wana madaraka. Mosi, kwa ajili yao wenyewe na, pili, kwa ajili ya wale wanaofuata uongozi wao. Watu huwafuata viongozi wao hata katika mambo ya dini. Mbele ya Mwenyezi Mungu, makosa wanayoyafanya ni makosa ya viongozi wao. Mtukufu Mtume s.a.w. alieleza fikara hii alipomwandikia mfalme Kaisari, mfalme wa Urumi:

"Basi ukikataa, zi juu yako dhambi za raia zako."

Amini basi, msomaji mpenzi, ili kwamba rafiki zako au wafuasi wako, au wowote wale, wasione shida kuamini; ili kwamba usiwazuie wengine kuamini. Bali ushiriki katika thawabu ya kuamini kwao.

## MBELE YA MWENYEZI MUNGU

Maisha hapa duniani ni mafupi. Hakuna ajuaye kila mmoja wetu ataishi kwa muda gani. Leo au kesho watu watalazimika kwenda na kusimama Mbele ya Mungu Mwenyezi. Hapo hakuna kitakachofaa isipokuwa imani ya kweli na kazi njema. Wote sisi tuwe matajiri au maskini, tukitoka hapa, tunakwenda huko mikonomitupu. Si maskini wala tajiri, hakuna miongoni mwetu anayechukua chochote anapotoka hapa kwenda nacho Akhera. Sote tunachukua imani tu na vitendo. Basi mwamini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ili Mwenyezi Mungu akujaalie amani. Itika wito wa Uislamu ili ukubaliwe na Mungu. Ile kazi iliyokuwa niifanye nimekwisha ifanya. Nimekufikishia ujumbe. Ni shauri yako kukubali au kukataa. Ninachotumaini na kutazamia, kwa akali (uchache), ni kwamba utausoma ujumbe huu kwa makini sana, na kwamba kama ukiona ni wa kweli, hutasita kuuamini.

Mwenyezi Mungu akujaalie!
Na maneno yetu ya mwisho:

"Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote."

Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikia wachukie.
(Al-Quran, 61:10)

# MWITO KWA MFALME MWISLAMU


**KIMEANDIKWA NA:**
**AL-HAJ HADHRAT MIRZA BASHIR-UD-DIN MAHMUD AHMAD r.a.**
**Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.**

*Mfasiri:*
**HEMED FERUZI M'BYANA**



*KIMEENEZWA NA:*
**JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA TANZANIA.**

Chapa ya mara ya kwanza 1975. Nakala 5000
*Kilienezwa na:*
**KATIBU WA UENEZAJI WA UISLAMU.**
**TAHRIK JADID, RABWAH PAKISTAN.**

Chapa ya mara ya pili Februari, 2000. Nakala 3000
*Kimeenezwa na:*
**JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA**
**TANZANIA.**

Idhini ya kunakili: Islam International Publications Ltd.

*Kimechapwa na:*
Ahmadiyya Printing Press
S. L. P. 376
Dar us Salaam.
Tanzania.

## NENO LA MBELE

Kitabu hiki ni tafsiri ya *Da'wat-ul-Amir* kilichoandikwa na Khalifa wa Pili wa Seyidna Ahmad a.s. (Mwenyezi Mungu awe radhi naye), mnamo mwaka 1926 ili kumpelekea mfalme wa Afghanistan, Amir Amanullah Khan, apate kujua itikadi za Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya na hoja zake na pia kuelewa mpango wa Mwenyezi Mungu juu ya kuleta ushindi wa Uislamu zama hizi. Kiliandikwa maalumu kwa ajili ya mfalme huyo kwa sababu baadhi ya wafuasi wa Seyidna Mirza Ghulam Ahmad a.s. (amani ya Mwenyezi Mungu iwe kwake), waliuawa mfululizo kwa fat'wa za masheikh wa nchi hiyo waliodai kwamba wazee hao wametoka katika Uislamu kwa kujiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya na ya kuwa Dini ya Islam inataka watu wa namna hii wauawe. Ilionekana hatari kuwa nchi ile ya Kiislamu itapata adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kutesa wenye imani safi kwa ajili ya dini tu.

Masheikh hao waliandika fat'wa zao bila kupeleleza uhakika ni nini. Walifikiri Mwislamu anayejiunga na Jumuiya hii anatoka katika Uislamu na ya kuwa adhabu ya mtu kama huyo ni kifo. Maoni hayo yote mawili yalikuwa si sawa. Si kwamba Mwislamu, anayejiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya hatoki katika Uislamu tu, bali Uislamu wake unapigwa msasa na imani yake juu ya misingi yote ya Kiislamu inakuwa imara kabisa. Maneno yake na matendo yake yanachukua picha safi ya Uislamu na yeyote anayesuhubiana naye anaelewa ubora wa Uislamu na kuathirika na mafundisho yake. Vilevile si kweli ya kuwa mtu anayetoka katika Uislamu anastahili kuuawa. Hata si mafundisho ya Kiislamu. Dini yetu ni ya pekee inayotoa uhuru kamili katika

mambo ya kidini. Mtu hatakiwi kusilimu ila baada ya upelelezi wa kutosha na kuhakikisha kwamba dini ya Islam ni dini ya kweli. Wala hakatazwi kujitenga nayo ikiwa ametosheka moyoni mwake kwamba si dini ya haki.

Fat'wa hizo zilizotolewa na kufuatwa pasi na ujuzi mwingi hazikukawia kuleta matokeo mabaya nchini. Miaka michache tu baada ya wazee hao kuuawa bila kosa lolote, uasi ukatokea katika nchi ya Afghanistan. Serikali ya Amir Amanullah Khan ikapinduliwa naye akakimbia bila kurudi tena maisha yake yote. Alifungua hoteli huko nchi ya Italia na akafia kule miaka michache iliyopita. Nchi nzima ilipata msukosuko mkubwa na mbali na taabu nyingine maelfu ya watu walikufa kwa sababu ya maradhi.

Tangu mwanzo kitabu hiki kimeongoza watu wengi kwa vile kimechukua hazina ya hoja safi zilizotolewa ndani ya Quran Tukufu na Hadithi sahihi za Mtume Muhammad s.a.w. na kinaeleza kinaganaga ushindi wa Uislamu utakavyopatikana katika miaka ijayo. Kiliandikwa kwa Kiurdu na tafsiri yake ya Kiajemi akapelekewa Amir wa Afghanistan, maana ndiyo lugha aliyoifahamu vizuri, lakini mara nyingi kilipata kupigwa chapa kwa Kiurdu. Mnamo mwaka 1961 tafsiri ya Kiingereza ilitoka mara ya kwanza. Katika tafsiri hiyo, kwa idhini ya Khalifa wa Pili r.a., jina la Amir lilitolewa na mahala pake yakaandikwa maneno kama "msomaji mpenzi" ili yamhusu kila akisomaye. Tafsiri ya Kiingereza ilisambazwa dunia nzima na ilipofika Dar es Salaam, Tanzania, kijana wetu hodari Bwana Hemed Feruzi M'byana akavutika sana nayo, akapata shauku ya kukifasiri kwa Kiswahili ili kiwanufaishe wale wananchi wa Afrika ya Mashariki wasiojaaliwa elimu ya Kiingereza. Bwana huyo aliendelea kufanya kazi hii kwa juhudi na ujuzi mkubwa, wakati alipopata nafasi kazini kwake, mpaka kitabu kizima kikamalizika.

Kazi moja kubwa aliyopata kufanya Khalifa wa Tatu, Hadhrat

Hafidh Mirza Nasir Ahmad*, Mwenyezi Mungu amsaidie, tangu mwaka 1965 aliposhika uongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya ni kueneza kwa wingi vitabu vya Jumuiya na tafsiri zake kwa lugha mbalimbali. Alipopata habari kwamba tafsiri ya *Da'wat-ul-Amir* imeisha kuwa tayari kwa lugha fasaha ya Kiswahili akaiagiza iletwe Rabwah. Baadaye tafsiri ile ikachunguzwa na Mbashiri Mkuu wa Tanzania, Sheikh Muhammad Munawwar, na kulinganishwa na maneno ya asili ya Kiurdu. Ikiisha kusahihishwa na maneno yaliyoachwa kuongezwa ndani yake, tafsiri ikaenda mtamboni mnamo mwaka 1969 kwa kupigwa chapa.
Mwenye kufasiri na mwenye kusahihisha nawashukuru wote wawili kwa moyo mkunjufu na kumwomba Mwenyezi Mungu akifanye kitabu hiki kiwaongoze watu wote wakaao Afrika ya Mashariki na nje yake kunakosemwa Kiswahili. Amin.

Furaha yangu kuu ni kuona kuwa kwa fadhili za Mwenyezi Mungu wameanza kupatikana miongoni mwa Waahmadiyya wananchi wanazuoni wanaoufahamu Uahmadiyya na wako tayari kujitolea kwa kuitumikia Dini kwa ujuzi wao na kalamu yao. Mfasiri wa kitabu hiki anahusiana na ndugu mpenzi Sheikh Amri Abeidi. Mwenyezi Mungu amweke peponi milele, na pia ni mwanafunzi wake. Aliwahi kufanya kazi kama mbashiri wa Jumuiya huko Kenya na kusaidia kwa namna mbalimbali. Mwenyezi Mungu amtakabalie huduma yake hii na awajaalie wanafunzi wengine wa marehemu nao watumie kalamu yao kwa kuiinua Dini ya Mwenyezi Mungu - Uislamu.

Kitabu hiki ijapokuwa kiliandikwa kwa sababu ya kuwapatia Waislamu mwangaza zaidi juu ya Mwendeleo ya wa Ahmadiyya kinaweza kuwaongezea maarifa watu wowote wanaotaka kujua ushindi wa Uislamu utapatikanaje katika siku zijazo. Kwa kuona udhaifu fulani uliopatikana upande wa Uislamu labda baadhi ya watu wamekuwa na fikara zinazokwenda kinyume chake

---

* Ambaye sasa ni marehemu.

wakadhani Dini hii haiwezi kuinuka tena duniani; lakini watu hao hawawezi kukanusha kwamba Uislamu leo una nguvu zaidi kuliko ulivyokuwa nayo siku ya kwanza misingi yake ilipowekwa. Ikiwa Dini hii iliweza kushinda duniani katika zama zilizopita, hata sasa iko ahadi ya Mwenyezi Mungu na bishara za Mtume Mkweli Muhammad s.a.w. juu ya ushindi wake wa mara ya pili. Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inayo imani hii na inafanya kazi huku ikitazamia kwa yakini kwamba ushindi huu bila shaka utapatikana. Juhudi zilizopata kufanywa katika miaka 80 iliyopita zimeleta mafanikio makubwa na matokeo hayo yanatuhakikishia kwamba Uislamu waweza kuleta mapinduzi makuu ya kiroho na kuunganisha mataifa yote ulimwenguni. Ushindi huu lazima uonekane katika muda wa miaka 300. Karibuni wasomaji, mkajionee wenyewe njia zipi zitakazoleta ushindi wa Uislamu.

Mirza Mubarak Ahmad,
Vakilut Tabshir.

Rabwah, Pakistan.

## DIBAJI YA CHAPA YA PILI

Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad r.a., Khalifa wa Pili wa Seyidna Ahmad a.s., ndiye mwana Aliyeahidiwa na Muslihe Maud.

Katika wakati wa Ukhalifa wake Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya iliimarika namna yake, na kazi ya msingi ilifanyika na Jumuiya ilipata maendeleo mazuri. Kazi moja kubwa aliyofanya ni kuandika kitabu hiki. Mimi kuwa Mbashiri nashuhudia kwamba kitabu hiki ni cha pekee kuwaelezea Waislamu habari za Jumuiya.

Tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mara ya kwanza mwaka 1975. Nakala ya tafsiri iliisha mapema sana. Watu walikitamani lakini hakikuwepo. Sasa Mwenyezi Mungu ameisaidia Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania kukichapisha mara ya pili. Katika chapa ya mara ya pili tumejaribu kusahihisha kasoro za uchapaji zilizojitokeza katika chapa ya kwanza, na mwanzo wa kitabu tumeongeza faharisi ili msomaji aweze kutafuta kwa urahisi mada anayoipenda.

Mwenyezi Mungu awaongoze watu wengi kwenye njia yake iliyonyoka kwa kupitia mafundisho ya kitabu hiki, Amin.

Amir na Mbashiri Mkuu.
Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya
Tanzania.
20 Februari, 2000.

# FAHARISI


1. Uahmadiyya si Dini Mpya .................... 1
2. Itikadi za Waahmadiyya .................... 4
3. Nabii Isa a.s. alikufa kama kawaida ............... 11
4. Kuja kwa Masihi ni kuja kwa mfuasi wa Mtume s.a.w. . 25
5. Wahyi na Unabii Unaendelea .................... 39
6. Maana ya Khaatamunnabiyyiin .................... 44
7. Imani ya Waahmadiyya juu ya Jihadi .............. 54
8. Madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. .......... 60
9. Hoja ya Kwanza: Haja ya wakati .................. 62
10. Hoja ya Pili: Ushuhuda wa Mtukufu Mtume s.a.w. . 80
11. Hoja ya Tatu: Utakatifu wa mtu. ............... 121
12 Hoja ya Nne: Ushindi wa Islam juu ya dini zingine 129
13. Hoja ya Tano: Kuhuishwa Uislamu ............. 153
14. Hoja ya Sita: Msaada wa Mwenyezi Mungu ..... 191
15. Hoja ya Saba: Kushindwa kwa maadui .......... 203
16. Hoja ya Nane: Utii wa Malaika ................ 211
17. Hoja ya Tisa: Zawadi ya Elimu Maalum ........ 217
18. Hoja ya Kumi: Bishara za Masihi Aliyeahidiwa ... 240
19. Hoja ya Kumi na Moja: Mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa kwa Mungu na Mtume Wake ........ 299
20. Hoja ya Kumi na mbili: Nguvu za kuhuisha ....... 311
21. Wito: Masihi Ameshakuja .................... 319

**INVITATION TO AHMADIYYAT**
**Dawat-ul-Amir**
**(Swahili translation)**

Invitation to Ahmadiyyat was first published in Urdu in 1926, and then translated into Persian for presentation to the ruler of Afghanistan, Amanullah Khan. Two years or so before the book was compiled, three Afghan Ahmadis had been stoned to death by the orders of Amanullah Khan. These Tragic events made it necessary that the massage, aims and the rationale of the Ahmadiyya Movement should be expounded for the special attention of the king. The purpose of the book therefore was to convey to His Majesty an authentic account of the beliefs and doctrines of the Movement and the purpose of its establishment. It was also intended to refute the false charges that were made against the Movement by the orthodox divines and to contradict the baseless allegations made against the Movement. The events and the book now belong to history, but the book itself continues to grow in impact and influence.

It sets out the prophecies of the Holy Prophet (peace be on him) mentioned in the books of Tradition and examines their true import. It presents an exposition of the claims of the Founder of the Ahmadiyya Movement and details the reasons in their support. It goes on to establish, on the basis of the Holy Quran and the Traditions of the Holy Prophet (peace be on him) that the spiritual preceptor whose advent had been prophesied had already appeared in the person of the Founder of the Ahmadiyya Movement, and to emphasise that the salvation of mankind lies in accepting him and following him.

**AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA**